# Misingi

## Inayojenga katika Imani

*Kuweka Msingi juu ya Mwamba, Yesu Kristo*

**Luka 6:48**

**a publication of**

Village
Ministries
International

**VillageMinistries.org**

© 2001 na
Village Ministries International, Inc. (VMI)

VMI inatoa ruhusa kwa yeyote kunakili na kusambaza kitabu hiki kwa makusudi ya kuwafundisha wengine kuhusu Kristo na Neno la Mungu; hata hivyo, hairuhusiwi kubadilisha, kurekebisha au kufanya mabadiliko yoyote yale katika kitabu hiki( haijalishi kwa mapungufu gani yaliyomo katika kitabu hiki). Hairuhusiwi **kuuza kitabu** hiki kwa mtu au kundi la watu au kudai malipo kwa ajili ya matumizi ya kitabu hiki, ieleweke kwamba VMI ina neema ya pekee na hivyo huwa haidai malipo ya aina yoyote kwa ajili ya matumizi ya kitabu hiki.

Any copying, retransmission, distribution, printing, or other use of *FOUNDATIONS* must set forth the following credit line, in full, at the conclusion of the portion of *FOUNDATIONS* that is used:

Copyright © 2001 Village Ministries International, Inc. Reprinted with permission.
*Foundations* is a publication of Village Ministries International, Inc.
VillageMinistries.org

All Scripture quotations from the *New American Standard Bible*®, Copyright © 1960, 1962, 1963, 1968, 1971, 1972, 1973, 1975, 1977, 1994 by:

The Lockman Foundation
A Corporation Not for Profit
La Habra, CA

# ORODHA YA YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| **Shukrani** | | **8** |
| **Utangulizi** | | **8** |
| **Sura ya 1:** | **Jinsi ya Kuanza** | **9** |
| Sehemu ya 1 | Maandalizi Binafsi | 10 |
| Sehemu ya 2 | Biblia | 12 |
| Sehemu ya 3 | Mitazamo ya Kihistoria | 14 |
| Sehemu ya 4 | Mtazamo wa Kikalenda | 17 |
| Sehemu ya 5 | Maandalizi ya Kujifunza Neno la Mungu | 21 |
| **Sura ya 2:** | **Agano la Kale** | **25** |
| | Utangulizi | 26 |
| Sehemu ya 1 | Sheria: Vitabu Vitano vya Kwanza | 27 |
| | Mwanzo | 27 |
| | Kutoka | 28 |
| | Mambo ya Walawi | 30 |
| | Hesabu | 31 |
| | Kumbukumbu la Torati | 32 |
| Sehemu ya 2 | Vitabu vya Historia | 34 |
| | Yoshua | 34 |
| | Waamuzi | 35 |
| | Ruthu | 36 |
| | 1 Samweli | 37 |
| | 2 Samwelil | 39 |
| | 1 Wafalme | 40 |
| | 2 Wafalme | 41 |
| | 1 Mambo ya Nyakati | 43 |
| | 2 Mambo ya Nyakati | 44 |
| | Ezra | 46 |
| | Nehemia | 47 |
| | Esta | 48 |
| Sehemu ya 3 | Vitabu vya Mashairi | 50 |
| | Ayubu | 51 |
| | Zaburi | 54 |
| | Mithali | 58 |
| | Muhubiri | 59 |
| | Wimbo wa Sulemani | 61 |
| Sehemu ya 4 | Manabii Wakubwa | 62 |
| | Isaya | 63 |
| | Yeremia | 65 |
| | Maombolezo | 67 |
| | Ezekieli | 68 |
| | Danieli | 69 |
| Sehemu ya 5 | Manabii Wadogo | 71 |
| | Hosea | 72 |
| | Yoeli | 73 |
| | Amosi | 74 |
| | Obadia | 75 |
| | Yona | 76 |
| | Mika | 77 |
| | Nahumu | 78 |
| | Habakuki | 79 |
| | Sefania | 80 |

| | | |
|---|---|---|
| | Hagai …… | 80 |
| | Zekaria …… | 82 |
| | Malaki …… | 83 |
| **Sura ya 3:** | **Agano Jipya ……** | **85** |
| | Utangulizi…… | 86 |
| Sehemu ya 1 | Vitabu vya Historia …… | 90 |
| | Mathayo …… | 91 |
| | Marko …… | 93 |
| | Luka …… | 95 |
| | Yohana …… | 97 |
| | Matendo …… | 100 |
| Sehemu ya 2 | Nyaraka za Paulo …… | 102 |
| | Warumi …… | 104 |
| | 1 Wakorintho…… | 106 |
| | 2 Wakorintho …… | 108 |
| | Wagalatia …… | 110 |
| | Waefeso …… | 111 |
| | Wafilipi …… | 112 |
| | Wakolosai …… | 113 |
| | 1 Wathesalonike …… | 113 |
| | 2 Wathesalonike …… | 114 |
| | 1 Timotheo …… | 115 |
| | 2 Timotheo …… | 116 |
| | Tito …… | 117 |
| | Filemoni …… | 118 |
| Sehemu ya 3 | Nyaraka za Jumla…… | 119 |
| | Waebrania …… | 119 |
| | Yakobo …… | 121 |
| | 1 Petro …… | 122 |
| | 2 Petro …… | 123 |
| | 1 Yohana …… | 125 |
| | 2 Yohana …… | 126 |
| | 3 Yohana …… | 127 |
| | Yuda …… | 127 |
| Sehemu ya 4 | Kitabu cha Unabi …… | 129 |
| | Ufunuo …… | 129 |
| **Sura ya 4:** | **Kanuni Muhimu za Ufasili ……** | **133** |
| | Utangulizi…… | 134 |
| Sehemu ya 1 | Sheria ya Kwanza: …… | 135 |
| | Kanuni ya 1: Jifunze Asili ya Mungu …… | 135 |
| | Kanuni ya 2: Tafuta Njia Jinsi Yesu Anavyofunuliwa …… | 136 |
| Sehemu ya 2 | Sheria ya Pili: Tafuta Kuelewa …… | 139 |
| | Kanuni ya 3: Tambua Kwamba Ufunuo ni Kitu Kisicho na Mwisho . | 139 |
| | Kanuni ya 4: Fasiri kwa Njia ya Maandiko…… | 140 |
| | Kanuni ya 5: Chunguza Mambo Maalumu…… | 140 |
| | Kanuni ya 6: Soma Sura Muhimu …… | 141 |
| | Kanuni ya 7: Tambua Haki wa Mwanadamu …… | 142 |
| | Kanuni ya 8: Kumbuka Maagano …… | 143 |
| Sehemu ya 3 | Sheria ya Tatu : Kuwa Mwenye Hekima …… | 146 |
| | Kanuni ya 9: Tafuta Tofauti…… | 146 |
| | Kanuni ya 10: Chunguza Yaliyomo…… | 147 |
| | Kanuni ya 11: Fasili kwa Kulinganisha Maandiko…… | 149 |
| | Kanuni ya 12: Tafuta Mwafaka …… | 150 |

| | | |
|---|---|---|
| | Kanuni ya 13: Fikiria Mpango wa Mungu ……………………………. | 150 |
| | Kanuni ya 14: Kuwa Makini na Unabii ……………………………….. | 152 |
| Sehemu ya 4 | Sheria ya Nne: Tafuta Jinsi ya Kuishi …………………………….................... | 154 |
| | Kanuni ya 15: Matumizi Mazuri ………………………………………. | 154 |
| **Sura ya 5:** | **Mafundisho juu ya Nafsi ya Mungu ……………………..……………………..** | **159** |
| Sehemu ya 1 | Utatu …………………………………………………………………………….. | 160 |
| Sehemu ya 2 | Majina ya Mungu …………….……………………………………………….. | 164 |
| Sehemu ya 3 | Mungu Baba …………………………..………………………………………. | 167 |
| Sehemu ya 4 | Mungu Mwana ……………..……………………….....……………………. | 172 |
| Sehemu ya 5 | Mungu Roho Mtakatifu ………………...……………….…………………….. | 181 |
| **Sura ya 6:** | **Misingi ya Mazao ya Mungu ………….……………………………………..** | **189** |
| Sehemu ya 1 | Uumbaji……………..………………..………………………………………… | 190 |
| Sehemu ya 2 | Malaika……………….…………….……………………….. ………………. | 191 |
| Sehemu ya 3 | Mwanadamu……………..……………………..……..……………………….. | 197 |
| Sehemu ya 4 | Migogoro ya Malaika ……………………..……………………………………. | 207 |
| **Sura ya 7:** | **Mafundisho ya Mipango ya Mungu ……………………..…………………….** | **209** |
| Sehemu ya 1 | Ufunuo: Biblia…………..……..……………………………………………….. | 210 |
| Sehemu ya 2 | Tatizo: Dhambi……………………………………….………………………….. | 211 |
| Sehemu ya 3 | Ufumbuzi/Njia: Wokovu……………..……………………..……………………. | 214 |
| Sehemu ya 4 | Usalama: Ahadi ya Mungu………………………………………………………... | 217 |
| Sehemu ya 5 | Yajayo: Unabii……………..………………………………….………………. | 219 |
| **Sura ya 8:** | **Mafundisho ya Makusudi ya Mungu …………………………………………….** | **223** |
| Sehemu ya 1 | Maisha Binafsi ya Mkristo ……………..…..………………….................... | 224 |
| Sehemu ya 2 | Maisha ya Kikristo ya Kushirikiana ……………………...….……………………. | 233 |
| **Sura ya 9:** | **Utendaji ……………..……………………………………………………………….** | **237** |
| | Utangulizi…………………………………………………………..……………….. | 238 |
| Sehemu ya 1 | Kukielewa Kitabu ………..………………………………………………………. | 239 |
| Sehemu ya 2 | Kutengeneza Muhtasari wa Kitabu ……………………..………………………….. | 240 |
| Sehemu ya 3 | Kupunguza Uelewa Wako katika Kujifunza …………..……………………… | 242 |
| Sehemu ya 4 | Kuangalia Mahusiano …………..……………………………………………… | 244 |
| Sehemu ya 5 | Kuyatambua Yaliyo ndani Kabisa …………………….………………………… | 247 |
| Sehemu ya 6 | Kupanua Uelewa Wako katika Kujifunza ……………………..……………….. | 249 |
| Sehemu ya 7 | Kufanya Mchanganuo …………………….……………………………………. | 252 |
| **Barua ya Mwisho** | **……………………..…………………………………………..…………………….** | **253** |
| **Majibu** | **………………………………………………………………………………………..** | **254** |
| **Orodha ya Vitabu** | **………………………………………………………………………………………..** | **268** |
| **Ujumbe wa Mwisho** | **………………………………………………………………………………………..** | **269** |

# Shukrani

Kitabu cha *MISINGI* kimetayarishwa chini ya maelekezo ya huduma ya Village Ministries International, Inc. Tangu mwanzo, ujumbe wa Village Ministries umekuwa ni kufikia vijiji na maeneo ya ndani kabisa katika ulimwengu kwa kueneza injili ya Yesu Kristo. Mara zote nafasi za Wamisionari zimekuwa zikipatikana kwa kipindi kifupi. Maono ya huduma yetu imekuwa ni kupata watu walio tayari katika maeneo haya tunawafundisha ili waweze kuwafundisha watu wao maneno ya Mungu baada ya Wageni kuwa wameondoka, na hivyo " Kuwafanya wanafunzi" ili kutimiza utume mkuu tuliopewa na Bwana wetu Mwokozi.

Sura ya 2 na 3 imeandikwa kwa ruhusa kutoka kwa J. Hampton Keathley III's, ***The Concise Old and New Testament Survey***. Kazi kamili isiyohaririwa ya Bwana Mr. Keathley inapatikana kwa makubaliano na Biblical Studies Foundation, katika Tovuti ya:

**www.bible.org**

Village Ministries International inapenda kuwashukuru Mr. Keathley kwa ruhusa ya kutumia utafiti wake. Kwa kwelli utafiti huu ni muhimu sana katika kujifunza Biblia. Marekebisho machache yamefanyika katika utafiti wake hasa katika eneo la tarehe za Biblia.

VMI inatumaini kutoa mafundisho ya Biblia katika sehemu mbalimbali duniani ambako mafundisho ni machache, yanahitajika lakini hayapatikani. Kwa huduma hii, VMI inauwezo wa kusaidia na kutegemeza idadi ya wachungaji inayoongezeka kwa kutoa mafundisho na vitendea kazi.

Kuna watu wengi wa kuwashukuru kwa kujitoa kwao ili kuwezesha uandaaji wa kitabu hiki. Kwanza kabla ya yote tunamshukuru Bwana wetu Yesu Kristo ambaye kwa neema yake ametupa wokovu wake mkuu na ametukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa wa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe (2 Petro 1:3). Pili, Mchungaji Drue Freeman aliye na huruma na shauku ya neno la Mungu ambalo kwa kweli lina uvuvio. Nia yake ya kusoma neno la Mungu na ushawishi wake wa kutafasiri kwa usahihi kwa kweli unaonekana dhahiri katika kitabu hiki. Mwisho kwa namna yoyote ile kuna watu wengi binafsi ambao wametoa wakati wao,vipaji na karama zao ili kuwezesha kukamilika kwa kitabu hiki, nao hatuna budi kuwashukuru. Kwa kweli ni mashujaa wasioonekana.

# Utangulizi

Sehemu hii ya mafunzo ya VMI inaitwa "Misingi" imekusudiwa kuwasaidia wasomaji wa Biblia waweze ***"kukua katika neema na maarifa ya Bwana wetu Yesu Kristo"*** (2 Petro 3:18). Kwa hiyo mkazo wa kitabu kizima cha MISINGI si kuelewa umuhimu na kina cha neno la Mungu lakini pia na kumsaidia msomaji katika kuendelea katika maisha yake ya Kiroho.

*Kitabu cha Misingi kimekusudiwa kumjenga msomaji ili aweze kuwafundisha na wengine kwa sababu msomaji atakuwa amekwisha elewa na kuyameza mameno ya Mungu katika Roho yake*. Ni chombo cha thamani kwa "Kufanya wanafunzi" katika kutimiza utume mkuu (Mathayo 28:18-20).

Kitabu hiki kina habari ambazo msomaji wa neno la Mungu anahitaji kuzifahamu. Sura ya 1, "Jinsi ya kuanza," inakusudia kuona umuhimu wa maandalizi ya Kiroho na halafu inatoa mtazamo wa neno la Mungu.

Sura ya 2 na 3 zinaonyesha utafiti mfupi wa kila kitabu ili kumpa msomaji habari za mwandishi na nia ya kitabu hicho. Sura ya 4 inamwongoza msomaji katika kanuni za kufasiri ambazo zimeandikwa kwa nia ya kusoma na kuelewa maandiko.

Sura ya 5 hadi ya 8 inamwonyesha msomaji theologia inayofaa, kwa kutoa muhtasari wa maneno ya Biblia na mawazo yake na sura ya 9 imekusudiwa kumfundisha mwanafunzi jinsi ya kutekeleza kile alichosoma, kwa uandaaji halisi wa somo katika Biblia.

Ni maombi yetu kwamba kitabu cha Misingi kitakusaidia katika kumkumbatia Bwana wetu Yesu Kristo katika kutembea kwako kwa imani iliyodhihirishwa katika neno lake.

# Karibu kwenye furaha ya neno la Mungu!

## Sura ya 1

# Jinsi ya Kuanza

# Sehemu ya 1
# Maandalizi Binafsi

**A. Kanuni Sita za Maandalizi Binafsi ya Kusoma Neno la Mungu:**

**1. Mwamini Yesu Kristo**

Maandalizi binafsi ya kusoma neno la Mungu hayawezi kuelezeka. Msomaji ni lazima amwamini Yesu Kristo kama mwokozi wake "mwanadamu wa asili" (mtu asiye na Yesu)" hawezi kukubali wala kuamini mambo ya Mungu (1 Wakorintho 2:14). Kwa hiyo, Wokovu ni kwa njia ya Imani katika Kristo (Waefeso 2:8-9). Roho wa Mungu huwawezesha wasomaji wa neno wapate kuelewa vitu vya Rohoni.

**2. Kubali kwamba Biblia Ina Pumzi ya Mungu**

Neno la Mungu linajisema lenyewe kwamba lina pumzi ya Mungu (2 Timotheo 3:16-17). Kusoma neno la Mungu ni lazima uanze kwa kushukuru ukweli wa Neno. Haihitajiki imani kubwa sana bali ni kukubali ukweli kwamba Biblia ni kweli na haina mapungufu.

**3. Omba**

Maombi ni muhimu katika kuyaelewa maandiko. Neno la Mungu linatuelekeza kwamba ikiwa mmoja wenu atapungukiwa na hekima na aombe dua kwa Mungu awapaye wote kwa ukarimu wala hakemei naye atapewa (Yakobo 1:5). Katika Yohana inasema "Na huu ndio ujasiri tulionao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake atusikia" (1 Yohana 5:14) pia Mathayo 7:7-8).

**4. Jifunze Kwa Juhudi na Uvumilivu**

Kwa kuwa kurasa nyingi za maneno ya Mungu wakati mwingine ni ngumu kuzielewa unaposoma jitihada na uvumilivu vinahitajika katika kujifunza Neno la Mungu (2 Timotheo 2:15), Kwa kuwa sisi ni wanadamu wenye ufahamu mfupi, maandiko yanasema; Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari ukilitumia kwa halali Neno la Kweli.

**5. Ungama Dhambi Zako**

Ni vizuri kuungama dhambi zako kila wakati ili umruhusu Mungu asafishe maisha yako, ili kwamba ushirika wako na Mungu udumu (1 Yohana 1:6-10). Tunapotambua kukiri dhambi zetu na kuziungama inatufanya sisi kuwa waangalifu na kila namna ya dhambi katika kufikiri, kunena au katika kutenda na hivyo tunashinda.

**6. Ishi kwa Kufuata Mapenzi ya Mungu**

Bwana Yesu alisema ***"Mtu akipenda kuyatenda mapenzi ya Mungu yake atajua habari ya yale mafunzo kwamba yatoka kwa Mungu au kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu tu"*** (Yohana 7:17). Ikiwa lengo ni kudumisha uhusiano na Mungu aliye hai kwa hiyo ufahamu tunaoupata unasaidia katika kufafanua uhusiano huo. Ujuzi huleta majivuno bali upendo hujenga. (1 Wakorintho 8:1). Ikiwa ufahamu wako ni kuonekana kwa watu na kwa kudumisha mahusiano yako na Mungu aliye hai kwa hiyo ufahamu utakaokuwa umepata hautakusaidia chochote kile.

**B. Faida Tano Zinazopatikana katika Kujifunza Neno la Mungu Kibinafsi**

**1. Imani Hukua**

Mwana theologia wa kanisa Mtume Paulo alisema "***Maana twaenenda kwa Imani si kwa Kuona"*** (2 Wakorintho 5:7). Na pia tumeokolewa kwa Neema Kwa njia ya Imani (Waefeso 2:8-9), na hivyo basi Kwa Paulo tunaona kuwa jinsi tulivyoingia na tutembee hivyo hivyo (Wakolosai 2:6-7).

**2. Maarifa Mapya**

Kuna maarifa mapya tunayopata katika kujifunza neno la Mungu. ***"kueni katika neema na katika kumjua Bwana wetu na mwokozi Yesu Kristo"*** (2 Petro 3:14-18). Ufahamu huu unatufanya sisi tukue katika imani hasa tunaposikia neno la Mungu kupitia maandiko (Warumi 10:17). Hivyo mtumaini Mungu kwa kila jambo.

**3. Maisha Yetu Yanakuwa Safi**

Neno la Mungu ni muhimu sana katika maisha yetu kwa sababu neno la Mungu ni kweli (Yohana 17:17). Japo ni waumini tuna shida ya dhambi katika maisha yetu (1 Yohana 1:6-10). Hivyo tuna sababu kubwa ya kujifunza neno la Mungu katika maisha yetu. Tuombe utakaso na uponyaji (Zaburi 51). Tafadhali elewa kuwa watu wameongeza maneno yao katika maneno yao katika maneno ya Mungu na kulipotosh neno. Hii inaitwa Upotoshaji inayo maanisha kuwa mwanadamu amekwisha tengeneza maneno yake anayoona yanafaa ili kulinda. Yesu mwenyewe anatoa changamoto katika kazi yake (Marko 7:1-13). Hivyo tunapaswa kuwa waangalifu na makini katika Neno la Mungu ili tusilipotoshe.

4. **Nguvu katika Huduma**
   Kwa uweza wa Roho Mtakatifu kadri tunavyojifunza "***hekima ya Mungu"*** (1 Wakorintho 2:14-16), kunakuwa na nguvu katika huduma zetu (Waefeso 2:10). Tuko katika vita na Ibilisi pamoja na jeshi lake. Hivyo tunahitaji nguvu katika kuimarika kwetu (Waefeso 6:10-18). Nguvu inapatikana kadri tunavyojitoa mbele za Mungu kwa sababu ni Mungu ambaye yuko akishughulika nasi ***"kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi lake jema***" (Wafilipi 2:13).

5. **Chombo cha Huduma**
   Kwa huduma hii ya ufahamu wa neno la Mungu tunaweza tukaitenda Kweli katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo (Wakolosai 3:16-17), na kuitangaza kwa wasioamini wanaoangamia katika ulimwengu huu. Chombo muhimu cha mawasiliano katika neno la Mungu ni "***kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya huduma itendeke ili mwili wa Kristo ujengwe***" (Waefeso 4:11-13). Ili "kuwaimarisha" wengine inatupasa tuwe tumeimarishwa kwanza.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 1, Sehemu ya 1

1. **Neno " Asili" kwa kiyunani ni (PSUCHIKOS) linapatikana katika 1 Wakorintho 2:14 na Wakorintho 15:44, 46; Yakobo 3:15 na Yuda 1:19 (ambapo limetafasiliwa kama akili za mambo ya dunia). Soma sura hizzi halafu eleza neno " Asili."**

2. **Soma 2 Timotheo 3:16-17. Kuna aina ngapi za faida tunazozipata katika Neno la Mungu? Lengo ni nini?**

3. **Ni nini kinachoahidiwa katika Yakobo 1:5 kwa wale wanaopungukiwa na hekima?**

4. **Soma 2 Timotheo 2:15. Tunapaswa kudumu katika yapi kama watu tunaojifunza Neno la Mungu? Nini liwe lengo letu?**

5. **Soma 1 Yohana 1:6-10. Ni ahadi gani mbili zilizoahidiwa pale tunapoungama dhambi zetu?**

6. **Yohana 7:17 inaeleza masharti katika kuyatenda mapenzi ya Mungu. Nini sharti hilo?**

7. **Soma Wakolosai 2:6-7 na Waefeso 2:8-9. Ni vitu gani viwili vinapaswa kuwa sifa katika maisha yetu ya Kikristo?**

8. **Soma 2 Petro 3:14-18. Ni lengo gani la Kikristo lililoelezwa katika mstari wa 18 ambalo tunapaswa kukua katika hilo?**

9. **Rudi katika 1 Yohana 1:6-10. Ni mambo gani mawili yanayohitajika kwa Mkristo ili asafishwe katika udhalimu wake?**

10. **Soma Waefeso 6:10-18. Adui yetu hasa ni nani na tunapaswa kumshinda kwa namna gani?**

11. **Soma Waefeso 4:11-13. Nini malengo matatu yaliyoelezwa katika "kuujenga mwili wa Kristo"?**

# Sehemu ya 2
# Biblia

## A. Biblia ni Nini?

### 1. Ni Neno la Mungu Lililo Andikwa

Biblia si kitabu cha kawaida. kimeandikwa na zaidi ya watu arobaini ambao maisha yao yamekuwepo zaidi ya miaka 1500 iliyopita. Yesu Kristo aliita “Kitabu” (Waebrania 10:47). Bila Biblia mwanadamu asingetambua haki na neema iliyo katika maisha yake. Mungu aliamua neno lake liandikwe ili kwamba ukuu wake upate kueleweka vizuri. Neno hili lililoandikwa limekubalika kwa imani na linathibitika kwa njia ya historia. Mwanadamu anazungumza na Mungu kwa njia ya maombi na Mungu anazungumza na mwanadamu kwa njia ya Neno lake.

Makundi ya watu wanaofasiri Biblia hufasiri kutoka katika Biblia iliyoandikwa katika lugha ya kwanza kabisa. Kwa asilimia kubwa Agano la kale liliandikwa kwa lugha ya Kiebrania, na tunaona katika kitabu cha Danieli sura ya 2–7 na Ezra 4–7. Sura hizi ziliandikwa katika lugha ya karibu kabisa na ile ya kiebrania inayojulikana kama Aramaiki. Hii ilikuwa ni lugha iliyokuwa ikizungumzwa na Wayahudi wengi wakati vitabu hivi vikiandikwa. Lakini katika Agano Jipya lugha iliyotumika ni Koine au kwa kawaida inajulikana kama KIYUNANI.

Sura na mistari iliyofuata katika Biblia iliongezwa na watu kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu ili kwamba iwe rahisi kwa sisi kutafuta sura za Biblia. kwa hiyo sura si kwamba zina uvuvio wa Roho na pumzi ya Mungu bali hizi zimewekwa tu ili kutusaidia sisi kuelewa.

### 2. Ni Neno Lenye Pumzi ya Mungu

Kila sehemu ya Biblia inauvuvio wa pumzi Mungu (2 Timotheo 3:16-17) na hivyo inafaa. Neno Uvuvio ni neno lenye maana kuliko akili za mwanadamu kwa sababu kila neno lina pumzi ya Mungu na linamsaidia na kumjenga mwanadamu.

### 3. Ni Ufunuo wa Neno la Mungu Lililo Hai

Biblia ni ufunuo ulioandikwa wa neno la Mungu lililo hai la Bwana wetu Yesu Kristo. Ufunuo ina maana ya kutoa habari za yajayo. “Mwanga” hii hutukia wakati Roho Mtakatifu anapofanya kazi ndani yetu ya ufunuo ili neno lipate kueleweka kwa wanaojifunza. Neno lililo andikwa si andiko hai bali ni maelezo ya Mungu juu ya Yesu Kristo Bwana wetu (Waebrania 4:12 na Yohana 5:39-47).

Kuna tofauti za kufanya. Wino na karatasi hazina nguvu ya Mungu lakini nguvu nyuma ya karatasi na wino ni Roho ya Mungu inayofanya kazi muhimu katika maisha ya mwanadamu.

## B. Mpangilio wa Biblia

### 1. Migawanyo Miwili Mikubwa

Biblia imegawanyika katika sehemu mbili kubwa. Agano la Kale na Agano Jipya.

Kuna vitabu 66 katika Biblia, 39 katika Agano la Kale vilivyoandikwa na waandishi 30, na 27 katika Agano Jipya vilivyoandikwa na waandishi 10. Kuna sura 1,189 katika Biblia, Sura 929 katika Agano la Kale na sura 260 katika Agano Jipya. Agano la Kale lina mistari 23,214 na Jipya lina mistari 7,959, jumla mistari 31,173 katika Biblia nzima.

“Agano” ni mkataba ambao kitu cha thamani kinapewa mtu mwingine kwa makubaliano na anayekabidhiwa anakuwa radhi nacho. Kwa mfano mtu anaponunua kitu fulani muuzaji anaweza kumpa kitu kama zawadi kwa sababu amenunua au punguzo fulani na anayepewa au kupunguziwa anakuwa na hiari ya kukubali au kukataa. Kama atakubali mkataba unakuwa umeshaingia kati yao. Mkataba unamambo fulani ambayo yanamfunga mtu fulani kati yao walioingia mkataba huo. Mkataba mzuri tunauona katika utoaji wa mahari ili mtu aoe au kuolewa. Mahari hii ni mkataba kati ya Bibi harusi na Bwana harusi kama msingi wa ndoa yao.

Agano la Kale lina mkataba ambao Mungu aliufanya kati yake na mwanadamu ili kuwaletea Yesu Masihi. Katika masomo haya tutaona vizuri mkataba huu.

2. **Migawanyo Mitano ya Agano la Kale**
   Agano la Kale limegawanywa kama ifuatavyo:
   a. **Sheria au Torati** (Kiebrania), au "Pentateuch" (Kiyunani " vitabu vitano)), navyo ni Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati.
   b. **Vitabu vya Historia** (kumi na mbili): Yoshua, Waamuzi, Ruthu,1 Samweli, 2 Samweli,1 Wafalme, 2 Wafalme, 1 Nyakati, 2 Nyakati, Ezra, Nehemia na Esta.
   c. **Vitabu vya Mashairi** (vitano): Ayubu, Zaburi, Mithali, Muhubiri na Wimbo ulio Bora.
   d. **Manabii Wakubwa** (watano) Isaya, Yeremia, Maombolezo, Ezekieli na Danieli.
   e. **Manabii Wadogo** (kumi na mbili) Hosea, Yoeli, Amosi, Obadia, Yona, Mika, Nahumu, Habakuki, Zephania, Hagai, Zekaria na Malaki.

3. **Migawanyo Mitatu ya Agano Jipya**
   Agano Jipya linaeleza kuja kwa Masihi na lina Agano ambalo limewekwa tangu zamani.

   Kwa kweli kuna mambo mengi katika Biblia. Mfano kuna Unabii (Mathayo 24, Marko 13 na Luka 21) na pia katika kitabu cha unabii kina nyaraka (Ufunuo 2-3). Kila muundo wa kitabu una namna yake. Agano Jipya liko katika sehemu kama ifuatavyo:
   a. Vitabu vya Historia: Mathayo, Marko, Luka, Yohana na Matendo.
   b. Vitabu vya historia vimefuatiwa na Nyaraka 21 (barua): Warumi, 1 Wakorintho, 2 Wakorintho, Wagalatia, Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, 1 Wathesalonike, 2 Wathesalonke, 1 Timotheo, 2 Timotheo, Tito, Filemoni, 1 Yohana, 2 Yohana, 3 Yohana, 1 Petro, 2 Petro, Waebrania, Yakobo na Yuda.
   c. Na kuna kitabu kimoja cha unabii: Ufunuo.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 1, Sehemu ya 2

1. **Soma Waebrania 10:1-7. Ni jambo gani ambalo Neno lililoandikwa haliwezi kufanya?**
2. **Pia kutoka Webrania 10:1-7 iyo hiyo, ni nini Neno lililoandikwa likekusudiwa kufanya?**
3. **Soma 2 Timotheo 3:16-17. Ni nini faida za Neno lililovuviwa?**
4. **Kulingana na 2 Timotheo 3:17, Ni makusudi gani mawili ya maandiko matakatifu?**
5. **Soma Yohana 5:39-47. Ni nini Yesu anachokionya kwa wale wanaosoma maandiko matakatifu?**
6. **Nini lengo kuu la "agano" au "mkataba"?**
7. **Taja migawanyo mitano ya Agano la Kale?**
8. **Je inaruhusiwa kuwaita Manabii Wakubwa na Manabii wadogo kuwa wote ni " Manabii"?**
9. **Taja migawanyo mitatu ya Agano Jipya?**

# Sehemu ya 3
# Mitazamo ya Kihistoria

Uzuri wa neno uko katika sehemu kulingana na jinsi kitabu kilivyo. Biblia imeandikwa na watu wengi waliopita. Historia inaangalia katika mambo yaliyopita.

Mfululizo wa matukio uliopo hapa chini unaonyesha hisitoria muhimu sana jinsi Mungu alivyoifungua Historia ya mwanadamu na Jinsi atakavyoifunga. Kwa kuangalia katika matukio haya makubwa tunaweza kutoa utangulizi na hata hitimisho la historia hii ya mwanadamu. Pia tunaweza kupata mtazamo mzuri katika maswali mengi ya wanafalsafa wanaojiuliza juu ya mwanadamu kwamba “Kwa nini tuko hapa?”

Mtazamo ufuatao unafikiriwa kuwa kweli kwamba baadaye tutaishi maisha yetu sehemu fulani, lakini kwa sasa ngoja tujifunze kutoka kwenye yale matukio ya historia kubwa yaliyowekwa mbele yetu na Mungu mwenyewe, na baadaye katika somo hili tutaona mtazamo mzuri sana na mpango wa Mungu katika maisha yetu.

**A. Maelezo ya Matukio:**

1. **Uumbaji**
   Mwanzoni mwa Biblia kitabu cha Mwanzo kinaeleza asili ya uumbaji wa mbingu na nchi (Mwanzo 1:1; 2 Petro 3:6) na mwisho katika kitabu cha Ufunuo, asili ya uumbaji inapotea na inakuja historia ya “mbingu mpya na nchi mpya” (Ufunuo 21-22).

2. **Uasi wa Ibilisi**
   Kabla ya kuumbwa mwanadamu shetani alimuasi Mungu (Isaya 14:12-14; Ezekieli 28). Na kusudi la uasi huu limeelezwa katika Biblia yote. Wakati mwingine huwa haieleweki vizuri, kinachoeleweka ni kwamba kuna vita iliyotokea kati ya Mungu na Ibilisi kabla ya kuumbwa kwa mwanadamu (Ufunuo 12) na uasi wa Ibilisi utakoma baada ya miaka 1000 ya utawala wa Yesu Kristo katika dunia hii kabla ya uumbwaji wa mbingu mpya na nchi mpya (Ufunuo 20:7-10).

3. **Dunia na Mwanadamu**
   Mungu aliiandaa dunia hii ili mwanadamu apate kuishi. Mwanzo 1:2–2:3 Maneno iliyojengeka Kiebrania TOHU na kuepukika (Kiebrania BOHU) ina maana ya kwamba isiyoishi na watu. Tatizo ni kwamba kuna mvamizi shetani ambaye kwa kweli anamjaribu Mungu. Lakini Bwana atakapokuwa amemfunga Ibilisi kwa miaka elfu (Ufunuo 20:1-3) atarudi na kuijenga dunia kwa ajili ya mwanadamu (Isaya 60–66).

4. **Adamu wa Kwanza na wa Mwisho**
   Adamu wa kwanza alisadikika kuwa ndiye mkuu wa uumbaji katika kuumbwa (Mwanzo 1:28; 2:4-25). Aliwekwa katika bustani ya Edeni ailime na kuitunza. Adamu wa mwisho Yesu Kristo (1 Wakorintho 15: 45) ataweka utawala wa miaka elfu (Ufunuo 20: 4) yeye ni wa mwisho na hakuna mwingine atakaye kuja nyuma yake na kuishi kama mwanadamu kamili asiye na wa.

5. **Vita ya Mwanadamu na Ibilisi**
   Adamu alipoanguka katika bustani ya Edeni aliingia katika hali ya dhabi ya ibilisi wa dunia hii (Mwanzo 3; Yohana 12:31; 16:11). Lakini hata hivyo Mungu atamleta Ibilisi kwa Yesu kabla ya kipindi cha utawala wa ile miaka elfu kuanza (Ufunuo 20:1-3).

6. **Wanadamu Wote Wamekwisha Hukumiwa**
   Mwanadamu kapewa uchaguzi na Mungu lakini Mungu atahusika na kila mwanadamu. Mwanzo 4–10 tunaona habari zinazotupeleka katika gharika kuu kwa sababu ya kutotii na uchaguzi mbaya. Mwanzo 6:1-13, inasema Mungu atashughulika na kila mtu wakati Yesu atakaporudi mara ya pili, baada ya miaka saba ya dhiki kuu. Wakati huu atawatenga watakaokuwa wamebakia kama “kondoo” (Walioamini) na “Mbuzi” (wasioamini) (Mathayo 25:31-46).

7. **Babeli**
   Baada ya gharika watu waliongezeka na baada ya muda mfupi watu walianza kurudia dhambi zao, na kumwacha Mungu. Wakajenga mnara mkubwa wa Babeli (Mwanzo 11) kama kielelezo cha kuweza kujiokoa wao wenyewe, walifikiri kama wangeliweza kujenga mnara mrefu sana hivyo wangeweza kuepukana na ghadhabu ya Mungu kwani walifikiri wangeliweza kufika mbinguni. Msingi walioujenga ulijulikana kama “Humanism” yaani ubinadamu ambao ulimaanisha kuwa mwanadamu anaweza kujiokoa mwenyewe kwa njia ya dini na hata kiuchumu. Na imani kama hizi ndiyo msingi wa dini nyingi. Unajua ni Mkristo tu ndiye anayejua kuwa mtu hawezi kujiokoa bali anamhitaji Yesu ili amwokoe. Na mawazo ya Wakristo wengine yamepotoshwa na wale wanapopingana na wokovu wa Mungu na haya

tunayaona hapo Babeli (Isaya 47 na Ezekilei 26–27). Mawazo kama haya potofu yako nasi makanisani na katika dini zetu. Yanamwelekeza mwanadamu kuwa anaweza kujiokoa. Na kipindi cha dhiki kuu Mungu itabidi aharibu Babeli ambayo imejengeka katika watu (Ufunuo 17–18).

8. **Israeli**
Baada ya kuanguka kwa Babeli watu walichanganywa Lugha na wakasambaa huku na kule katika mataifa na Mungu alimwita Ibrahimu kuanzisha taifa Jipya Isareli (Mwanzo 12) kwa njia ya uzao wa kijana wake Isaka na uzao wa mjukuu wake, Yakobo. Ibrahimu alipewa ahadi Ahadi ya masihi kuendelea katika kizazi chake (Mwanzo 22:1-18; 28:14). Watu wa Israeli walihamishwa toka katika nchi yao na wakasambazwa katika ulimwengu kwa sababu ya kuabudu miungu. Lakini ahadi ya Bwana ilibaki palepale,na Israeli watakusanywa tena baada ya dhiki kuu na kupewa ufalme wao (Mathayo 24:29-31).

9. **Kurudi kwa Yesu Mara ya Pili**
Kurudi kwa Yesu mara ya kwanza kulifanyika kwa muda muafaka katika Historia ya Mungu (1 Timotheo 2:6). Injili ya Mathayo, Luka, Marko na Yohana zilieleza vizuri historia ya Yesu, huduma yake, kifo kuzikwa na kufufuka. Yesu alikuwa ni" mtumishi wa mateso" na imeelezwa vizuri katika kitabu cha Isaya 53. Kurudi kwa mara ya pili kutafanyika baada ya dhiki kuu, wakati Yesu atakapokuja katika dunia hii na kumtawala adui yake (Zekaria 14:1-8; Ufunuo 19:11-19), Wakati huu atarudi kama Mshindi."

10. **Kupingwa kwa Huduma**
Injili inaonesha vizuri huduma ya Bwana Yesu Kristo (Mathayo, Marko, Luka na Yohana). Huduma ya Yesu ilikuwa ni msaada (Mathayo 20:28). Huduma hii pia inafananishwa na mazingira ya huduma ya mpinga Kristo (mtu asiye na sheria) ambaye atakuja na huduma yake binafsi ambaye ataleta Ibada na taratibu zake na kila mtu atamwabudu (2 Wathesalonike 2:1-12; Ufunuo 6-16).

11. **Kanisa**
Baada ya ufufuko na kunyakuliwa kwa Yesu Kristo katika mkono wa kuume wa Mungu Baba kanisa "liliitwa" kuhubiri habari njema za msamaha wa dhambi kwa njia ya dhabihu ya Yesu Kristo (Matendo ya Mitume). Kwa hiyo kanisa lina jukumu la kuwafanya watu kuwa wanafunzi (Mathayo 28:18-20), hadi pale litakapoitwa na Bwana Harusi (1 Wathesalonike 4:13-18; 1 Wakorintho 15:50-58; Ufunuo 19:7-10).

**B. Muhitasari**
Tukiangalia mpangilio huu wa matukio uliozungumziwa hapo juu tunaona jinsi historia ya mwanadamu ilivyofunguliwa na jinsi itakavyofungwa. Imeonyeshwa katika jedwali hapa chini kwa kuoanisha namba ili uone mpango kamili wa Mungu.[1]

**1. Uumbwaji wa mbingu na nchi. Mwanzo 1:1; 2 Petro 3:6**
**2. Uasi wa Ibilisi. Isaya 14:12-14; Ezekieli 28**
**3. Dunia kwa ajili ya Mwanadamu. Mwanzo 1:2–2:3**
**4. Ukuu wa Adamu wa kwanza. Mwanzo 2:4-25**
**5. Mwanadamu ni wa Ibilisi. Mwanzo 3**
**6. Wanadamu wote wamehukumiwa. Mwanzo 4–10**
**7. Ujenzi wa Mnara wa Babeli. Mwanzo 11**
**8. Israeli yaitwa kama Taifa. Mwanzo 12**
**9. Kuja kwa Yesu mara ya kwanza. Mathayo, Marko, Luka, Yohana**
**10. Huduma ya Kristo. Mathayo, Marko, Luka, Yohana**
**11. Kanisa linaitwa. Matendo**
**11. Kanisa linaitwa. 1 Wathesalonike 4:13-18; 1 Wakorintho 15:50-58**
**10. Huduma ya Mpinga Kristo. 2 Wathesalonike 2:1-12; Ufunuo 6–16**
**9. Kurudi kwa Yesu mara ya pili. Ufunuo 19:11-19**
**8. Kukusanywa kwa Israeli kama Taifa. Mathayo 24:29-31**
**7. Kuharibiwa kwa utawala wa Wababeli. Ufunuo 17–18**
**6. Wanadamu wote wamekwisha hukumiwa. Mathayo 25:31-46**
**5. Shetani kapewa Kristo. Ufunuo 20:1-3**
**4. Utawala wa Adamu wa mwisho. Ufunuo 20:4**
**3. Dunia ni Kwa ajili ya Mwanadamu. Isaya 60–66**
**2. Uasi wa mwisho wa Ibilisi. Ufunuo 20: 7-10**
**1. Uumbwaji wa mbingu na nchi mpya. Ufunuo 21–22**

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 1, Sehemu 3

1. **Soma Mwanzo 1–2 na Ufunuo 21–22. Zinaonesha nini?**

2. **Soma Isaya 14:12-14 na Ufunuo 20:7-10. Nini iliyokua dhambi halisi ya shetani na nini hatima yake?**

3. **Mwanzo 1:2–2:3 tena na Isaya 60–66. Katika Mwanzo dunia iliumbwa ikiwa kamili lakini kutokana na anguko la Adamu ikawa si kamili tena. Sasa sura ya Isaya inatueleza nini?**

4. **Soma Mwanzo 3, 1 Wakorintho 15:45 na 1 Petro 2:22-24. Ni nini tofauti ya mwanadamu wa Kwanza, Adam, na mwanadamu wa Mwisho "Adamu wa mwisho" ambaye ndiye Yesu Kristo?**

5. **Soma Waefeso 6:10-18. Adui zetu hasa ni nani na tunapambana nao vipi?**

6. **Soma Mwanzo 6:1-13 na Mathayo 25:31-46. Nini nia ya sura hizo?**

7. **Soma Ufunuo 17–18. Dini ya Babeli ilikuwa na lengo la kujiokoa, ikiwa na maana kwamba mwanadamu anaweza kujiokoa mwenyewe. Bila kujaribu kufuata alama katika sura hizo, jaribu kutafuta njia mbili kuu zinazojidhihilisha zenyewe. (Mwongozo: Sura ya 17 ni njia moja, Sura ya 18 ni njia ile nyingine.)**

8. **Soma Mwanzo 12:1-3, Waebrania 11:8-12 na Ufunuo 21:10-27. Ni lini ahadi ya Ibrahimu itakamilika kabisa?**

9. **Soma Isaya 53, Zakaria 14:1-8 na Ufunuo 19:11-19. Kwa ufupi Eleza tofauti kati ya Kuja kwa Yesu mara ya Kwanza na kuja kwa Yesu mara ya Pili.**

10. **Soma 2 Wathesalonike 2:1-12 na Mathayo 20:28. Ni nini tofauti kubwa kati ya huduma ya Yesu na huduma ya "Mpinga Kristo"?**

11. **Soma Mathayo 28:18-20, Matendo 1:8 na 1 Wathesalonike 4:13-18. Nini kazi kubwa ya kanisa hadi pale litakapochukuliwa kukutana na Bwan?**

# Sehemu ya 4
# Mtazamo wa Kikalenda

Wasomaji wa Neno la Mungu ni lazima wafahamu tarehe, nyakati na mahusiano ya muhimu katika matukio ya Historia. Sura hii inaonesha nyakati tatu. Orodha ya kwanza inaonesha matukio kumi makubwa yaliyo katika Biblia na tarehe zake na inatoa muhtasari kwa kila jambo muhimu. Na tarehe zingine zimetazama katika matukio ya Agano la Kale, na mwisho ni tarehe za vitabu vya Agano Jipya.

Tarehe zilizo na K.K. mwishoni zinamaanisha ni miaka kabla ya Kristo na zilizo na B.K. (zimechukuliwa katika kilatini zikimaanisha mwaka wa Bwana) hivyo zinamaanisha Baada ya Kristo.

Tarehe zilizotolewa ziko katika maandiko ya ufasiri wa neno la Mungu. Watu wengi waliosoma Neno la Mungu wameshawahi kufika katika tarehe tofauti tofauti. Kwa hiyo tarehe zilizomo humu zisikusumbue bali kujifunza matukio yaliyomo humu ni muhimu zaidi.

Kitabu cha Misingi kilichopita hakikuonesha miaka 60 ambayo haikutajwa katika kitabu cha Mwanzo 11:26–12:5, lakini imeoneshwa katika kitabu cha Matendo 7:4. Sura za matendo zinaeleza kwamba Abrahamu aliondoka Harani baada ya kifo cha Tera. Tera alifariki huko Harani katika miaka ya 205 (Mwanzo 11:32), na Abrahamu aliondoka Harani katika Umri wa miaka 75 baada ya kifo cha Tera (Matendo 7:4). Hii inamaanisa kwamba Tera alikuwa na umri wa miaka 130 kipindi Abrahamu alipozaliwa. Miaka 70 iliyotajwa katika Mwanzo 11:26 yumkini inahusika eidha na uzazi wa Nahori au Harani, na Yumkini (Mwanzo 11:28). Ni matumaini kwamba hii changa moto itamsaidia mwanafunzi anayejifunza katika kulinganisha andiko kwa andiko ili yajitafsiri.

**A. Matukio Kumi Makubwa na Tarehe Zake**

1. **Kuanguka kwa Adamu (3958 K.K.)**
   Ufasiri huu wa asili (mfululizo wa vizazi) ambao umetolewa katika Neno la Mungu unatufanya tufike katika tarehe kati ya miaka 3958 kabla ya Kristo katika anguko la Adamu. Kalenda hizi za Kibiblia zinatupa mwanga ili tupate kuanza kujifunza tangu kwa Adamu na pia tupate picha halisi ya miaka ya nyuma katika karne ya $4^{th}$ ya Sulemani (1 Wafalme 6:1). Biblia inatupa habari inayohusiana na matukio katika miaka na nyakati hizi. Hivyo tunapo unganisha matukio ya Kibiblia katika mfumo wa kalenda za historia za kidunia tunaweza kupata historia nzuri ya Biblia na Ulimwengu pia.

2. **Gharika la Nuhu (2302 K.K.)**
   Tunapoangalia kwa undani katika Mwanzo 5 tunaona kwamba maisha ya miaka 1,656 iliishia tangu anguko la Adamu hadi Gharika ya Nuhu. Hii inatupa tarehe za 2302 K.K.

3. **Ahadi ya Ibrahimu (1875 (K.K.)**
   Tunachojifunza katika Mwanzo 11:10-26 ni kwamba, Ibrahimu alizaliwa miaka ya 352 baada ya gharika au miaka 2008 baada ya Adamu. Na hii inaonesha kuwa alizaliwa miaka ya 1950 K.K. Tunajifunza toka kitabu cha Mwanzo 12:4 kwamba Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka 75 alipo pokea Ahadi kutoka kwa Mungu na ikawa Agano la Ibrahimu. Hii inaweza kumaanisha kuwa ahadi ilifanyika miaka ya 1875 K.K.

4. **Kutoka kwa Wana wa Israeli (1445) K.K.**
   Mwanzo 12–50 Inaonyesha habari za ukoo wa Ibrahimu. Watoto wa Yakobo (Wajukuu wa Ibrahimu) walihamia Misri ambako walifanywa kuwa watumwa na Wamisri (Kutoka 1). Mungu aliwaokoa kutoka katika utumwa huo kwa kumtumia Musa. Mtume Paulo anatueleza kwamba kizazi cha miaka 430 kimekwisha pita tangu ahadi ya Ibrahim kwa kupewa sheria (Wagalatia 3:17) tarehe hizi za Kutoka ni 1445 K.K. au miaka 2378 K.K. baada ya Adamu.

5. **Mwaka wa Nne wa Sulemani (965 K.K.)**
   Mfalme Sulemani alikuwa mfalme wa tatu wa Israel akimfuata baba yake, Daudi, na Mfalme Sauli. Katika 1 Wafalme 6-1 tunaelezwa kwamba miaka ya 480 iliishia kipindi cha kutoka kwa Waisraeli hadi utawala wa mwaka wa nne wa mfalme Sulemani alipoanza kujenga hekalu. Hivyo inatupa tarehe hizi za 965 K.K. au 2,918 baada ya Adamu.

   Tuna uwezo wa kuweka mwaka huu wa nne wa Sulemani katika historia nyingine ya kumbukumbu. Hii inatufanya tuwe na tarehe zilizowazi ambazo zinaweza kutufanya tujenge historia nyingine za nyuma kutoka kwa wana wa Israeli hadi ahadi ya Ibrahimu, gharika ya Nuhu na Adamu. Mwanadamu ingizwa katika uvumbuzi mkubwa uliofanywa miaka 100 iliyopita na wavumbuzi kwa kusogeza sogeza tarehe

za K.K. katika historia ya ulimwengu. Na hii ndio sababu zilizotofautiana katika mfumo mbalimbali wa kupata mfumo wa kalenda.

6. **Kuanguka kwa Ufalme wa Kaskazini (721 K.K.)**
   Baada ya kifo cha Sulemani Waisraeli waligawanyika katika falme mbili tofauti ambazo baadaye zilijulikana kama Ufalme wa kaskazini au Israeli na Ufalme wa kusini au Yuda. Na ufame wa kaskazini ulianguka katika Ufalme wa Waashuru mwaka 721 K.K. na ikalaaniwa kabisa na kuondoshwa kuwa ufalme.

7. **Kuanguka kwa Ngome ya Kusini (586 K.K.)**
   Ufalme wa kusini uliangukia katika Ngome ya Wababeli 586 K.K. na wakachukuliwa kuishi miaka 70 uhamishoni kabla ya Waisraeli kuruhusiwa kurudi katika nchi yao mwaka 516 K.K..

8. **Kuzaliwa kwa Yesu (1 K.K.)**
   Mfumo wa K.K. na B.K ulikuwa haujaanza kutumika hadi katika karne ya sita baada ya Kuja kwa Bwana wetu. Ilifanywa ili ipate kuweka kumbukumbu nzuri ya historia ya Uzazi wake. Wakati kanisa limeanzisha mfumo huu ilionekana kutoeleweka hasa kipindi Herode mfalme alipokuwa bado hai (aliyetajwa katika Biblia kuwa alikuwa mtawala wakati Yesu anazaliwa Luka 1:5). Lakini baadaye iligundulika kuwa mfumo unamakosa kati ya mwaka wa 1 na wa 2. Kwa kuwa tarehe tayali zilikuwa zimekwisha wekwa na zinafanya kazi hakukuhitajika marekebisho tena isipokuwa badala yake ikalazimika kusema kuwa Yesu alizaliwa kati ya mwaka 1 na 2 K.K.

   Kuna tofauti kati ya kalenda ya Juliana inayoanza tarehe 1 Januari na ile ya Wayahudi inayoanza Septemba. Na hii ndiyo sababu unaweza kuona kuwa imeandikwa “1-2 K.K”. au “966-965 B.K”.

9. **Kifo, Kuzikwa na Kufufuka kwa Yesu Kristo (32–33 B.K.)**
   Wasomi wa Biblia wanaliweka tarehe hizi za: kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu Kristo: kuwa ni (32-33 B.K.)

10. **Kitabu cha Mwisho katika Biblia (96 B.K.)**
    Hii ni tarehe inayohusishwa kipindi mtume Yohana akiwa uhamishoni kisiwani Patimo (Ufunuo 1:9) kipindi cha utawala wa Mrumi Domitian ambapo Biblia ilikamilika (Ufunuo 22:18-19).

**B. Kalenda ya Vitabu vya Agano la Kale**

1. **Adamu hadi Kwenye Gharika (3898–2242 K.K.)**
   Mwanzo 1–5

2. **Gharika hadi Ahadi ya Ibrahimu (2242–1875 K.K.)**
   Mwanzo 6–12

3. **Ahadi ya Ibrahimu hadi Kutoka kwa Wana wa Israeli (1875–1445 K.K.)**
   Mwanzo 12–50; Kitabu cha Ayubu

4. **Kutoka kwa Wana wa Israeli hadi Mwaka wa Nne wa Sulemani (1445–965 K.K.)**
   a. Kutoka
   b. Mambo ya Walawi
   c. Hesabu
   d. Kumbukumbu la Torati
   e. Yoshua
   f. Waamuzi
   g. Ruthu
   h. 1 Samweli
   i. 2 Samweli
   j. 1 Wafalme 1–5
   k. Zaburi
   l. 1 Mambo ya Nyakati

5. **Mwaka wa Nne wa Sulemani hadi Kuanguka kwa Yuda (965–586 K.K.)**
   a. 1 Wafalme 6-22
   b. 2 Wafalme
   c. 2 Mambo ya Nyakati
   d. Methali
   e. Muhubiri
   f. Wimbo Ulio Bora
   g. Obadia
   h. Yoeli
   i. Yona
   j. Amosi
   k. Hosea
   l. Mika
   m. Isaya
   n. Nahumu
   o. Zefania
   p. Habakuki

6. **Uhamishoni Babeli (586–516 K.K.)**
   a. Yeremia
   b. Maombolezo
   c. Ezekieli
   d. Danieli

7. **Uhamishoni Babeli na Agano La Kale (516–400 K.K.)**
   a. Ezra
   b. Nehemia
   c. Zekaria
   d. Hagai
   e. Malaki
   f. Esta

C. **Kalenda ya Vitabu vya Agano Jipya**
Ni mfululizo wa waandishi walioandika vitabu vyenye uvuvio wa pumzi ya Mungu katika Agano Jipya, na vinatazamwa kama ifuatavyo.

1. **Historia ya Maisha ya Kristo na Kanisa la Kwanza (B.K. 55–85)**
   a. Mathayo
   b. Luka
   c. Marko
   d. Yohana
   e. Matendo

2. **Nyaraka za Kanisa (B.K. 46–85)**
   a. Yakobo
   b. Wagalatia
   c. 1 Wathesalonike
   d. 2 Wathesalonike
   e. 1 Wakorintho
   f. 2 Wakorinto
   g. Warumi
   h. Philimoni
   i. Waefeso
   j. Wakolosai
   k. Wafilipi
   l. 1 Timotheo
   m. Tito
   n. 2 Timotheo
   o. Waebrania
   p. 1 Petro
   q. 2 Petro
   r. Yuda
   s. 1 Yohana
   t. 2 Yohana
   u. 3 Yohana

3. **Unabii (B.K. 96)**
   Ufunuo

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 1, Sehemu ya 4

1. **Panga matukio yafuatayo katika mpangilio sahihi:**
   Kuanguka kwa ufalme wa kaskazini
   Gharika la Nuhu
   Kuanguka wa ufalme wa Kusini
   Ahadi ya Ibrahimu
   Kufa, Kuzikwa na kufufuka kwa Yesu Kristo
   Kutoka kwa Wana waisrael
   Mwaka wa nne wa Sulemani
   Kuzaliwa kwa Yesu
   Anguko la Adamu
   Kitabu cha mwisho katika Biblia
   Kuzaliwa kwa Yesu
   Anguko la Adamu
   Kitabu cha mwisho katika Biblia

2. **Ni vitabu gani viwili vya Agano la Kale vinaeleza habari tangu uumbaji hadi kutoka kwa wana wa Misri?**

3. **Weka vitabu hivi katika mpangilio ulio sahihi:**
   1 Samwel
   1 Wafalme 1-5
   Hesabu
   Waamuzi
   Yoshua
   Kumbukumbu la
   Torati
   Ruthu
   1 Nyakati
   2 Samweli
   Mambo ya walawi
   Zaburi
   Kutoka

4. **Weka sehemu hizi za Agano la Kale katika mpangilio sahihi:**
   2 Nyakati
   1 Wafalme 6-22
   2 Wafalme
   Methali
   Muhubiri
   Wimbo wa Sulemani
   Isaya
   Nahumu
   Amosi
   Mika
   Yona
   Obadia
   Hosea
   Yoel
   Zephania
   Habakuki

5. **Pangavitabu hivi vya Agano la Kale katika mpangilio sahihi:**
   Nehemia
   Danieli
   Yeremia
   Ezekieli
   Malaki
   Ezra
   Zakaria
   Maombolezo
   Haga
   Esta

6. **Panga vitabu hivi vya Agano Jipya katika mpangilio sahihi:**

| | | |
|---|---|---|
| Mathayo | Luka | Matendo |
| Marko | Yohana | |

7. **Pangilia vitabu hivi vya Agano Jipya katika mpangilio ulio sahihi:**

| | | |
|---|---|---|
| Warumi | 2 Wathesalonike | 2 Petro |
| 1 Wakorintho | 1 Timotheo | 1 Yohana |
| 2 Wakorintho | 2 Timotheo | 2 Yohana |
| Wagalatia | Tito | 3 Yohana |
| Waefeso | Philimoni | Yuda |
| Wafilipi | Waebrania | Ufunuo |
| Wakolosai | Yakobo | |
| 1 Wathesalonike | 1 Petro | |

# Sehemu ya 5
# Maandalizi ya Kujifunza Neno la Mungu

Katika sehemu mbili za mwisho tulikuwa tukizungumzia umuhimu wa kusoma matukio muhimu yaliyotokea hapo zamani (Sehemu ya 3) na mlolongo wake jinsi yalivyotokea (Sehemu ya 4). Tunaweka msingi wa kusaidia kujibu maswali ambayo mtu anaweza kuwa nayo wakati akisoma Neno la Mungu: “Lini?” tunapokuwa tukitamani kuielewa Biblia. Tunapaswa kuwa na jibu la maana na muhimu kwani neno linasema ***“mkilitumia kwa uhalali neno la kweli”*** (2 Timotheo 2:15). Mungu anatuambia tumpelekee yeye maswali yetu yote (Mathayo 7:7-8).

Maswali tunayopaswa kujiuliza kwa kila mstari ni rahisi: **nani, nini, lini, wapi, kwa nini** na **kwa jinsi gani**? Jibu linapaswa kutokana na mambo mawili muhimu yanayokuwa katika maisha yetu ya Kikristo: Haya yanatusaidia nini katika uhusiano wetu na Kristo (Wafilipi 3:10), na tunapaswa kuishi namna gani (Yohana 7:17)?

**A. Maswali Sita kwa Kila Mstari:**

1. **“Nani?”**
   Tunapojiuliza swali la “nani” tunataka kujua nani anazungumza na nani anaambiwa. Mfano mmoja unaonekana katika kitabu cha Mwanzo 22:2 wakati Mungu alipomwambia Ibrahimu kumtoa mwana wake Isaka, mwana wa pekee. Katika hili Mungu anazungumza moja kwa moja na Ibrahimu na sio mtu mwingine. Kwa hiyo sisi kama wasikiaji wa Neno hatulazimishwi kutunza amri hii.

2. **“Nini?”**
   “Nini” inahusika na vitu halisi ilivyosemwa. Yesu Kristo anasemwa katika Ufunuo 5 kama “Mwanakondoo.” Hii haina maana ya kwamba yeye ni kondoo mwenye miguu minne, lakini inahusika na jinsi atakavyojitoa kwa ajili ya dhambi (Yohana 1:29) kitu ambacho ni “kweli halisi.”

3. **“Lini?”**
   “Lini” inaonyesha wakati wa ujumbe ulipotoka. Kwa mfano: Ibrahimu alipomuoa dada yake wa karibu, Sara, hii inaonekana kama kitu ambacho si kizuri kimaadili, hivyo msomaji anapaswa kujua ni lini ndoa hii ilifanyika . Hii ilifanyika kabla ya sheria za Musa hazijatoka ambazo zilikuja kukomesha tabia hizi. Kwa kuwa dhambi ya mtu si sababu wala kitu cha hatari kama hakuna sheria (Warumi 4:15), tunahitimisha kwamba kwa swala la Ibrahimu baba yetu ndoa hii haikuwa dhambi. Jibu sahihi la swali la “Lini”.

4. **“Wapi?”**
   “Wapi” inahusika na mazingira na tamaduni kipindi sura ile ilipoandikwa. Katika Biblia, tunaona neno “hadi Yerusalemu” katika mila nyingi neno mpaka lilimaanisha kaskazini. Hata hivyo kusudi la Biblia linahusika na mwinuko na si uelekeo. Wakati Yesu alipokuwa akitoka Galilaya alikuwa akipanda juu Yerusalemu lakini alikuwa akienda kusini japo alionekana kupanda juu.

5. **“Kwa Nini?”**
   “Kwa nini” ni swali gumu sana kulijibu. Jibu lake hupatikana kwa kusoma sura zingine. Kama utasoma katika Isaya 7:14 inasema, ***“Tazama Bikra atachukua mimba atazaa mtoto mwanamume naye atamwita jina lake Emanueli,”*** swali litakuwa ni kwa nini azaliwe na Bikra? Na tunaweza kujibu kwamba ni njia ambayo Mungu alipenda aitumie, jibu hili ni kweli lakini si kamili.

   Tunapotafuta jibu tutaangalia aya katika Warumi 5 inayoeleza madhara ya dhambi ya Adamu. Tunaona kwamba kwa mtu mmoja wanadamu wote wamefanya dhambi na wamepata dhambi ya asili. Kama Yesu angelikuwa na baba wa dunia hii angelikuwa na dhambi. Jibu la kwa nini lilikuwa ni kwamba ili Yesu alipe gharama ya dhambi zetu.

6. **“Kwa Jinsi Gani?”**
   Swali la “Kwa jinsi gani” nalo vilevile ni gumu kulijibu. Tunapaswa kujiuliza “Ni kwa jinsi gani Yesu alitembea juu ya maji?” jibu ni rahisi kwamba alitegemea Roho Mtakatifu (Luka 4:18). Tunapaswa kujiuliza “Ni kwa jinsi gani Mungu atafanya historia yake irudi wakati mwanadamu anao uhuru wa kuchagua?” Jibu halikujibiwa vizuri lakini tutaliona katika masomo yetu.

**B. Maswali Mawili Muhimu ya Kibinafsi:**

**1. Sura Hii Inanisaidia Nini katika Kuendeleza Uhusiano Wangu na Bwana Wetu Yesu Kristo?**

Hili ni moja ya maswali muhimu ya kujiuliza. Ufahamu tunaoupata kwa njia ya kusoma neno la Mungu ni lazima uunganishwe na imani (Waebrania 11:6), ili kwamba uhusiano wetu na Yesu ukue. Tunapaswa kuliamini neno la Mungu kuwa ni sahihi na halina upungufu. Matokeo yatakuwa ni uhusiano uliojengwa katika upendo wake na mbele ya ufahamu wa mwanadamu. Mtume Paulo amesema vizuri katika Waefeso 3:14-19:

> ***Kwa hiyo nampigia Baba magoti ambaye kwa jina lake Ubaba wote wa mbinguni na duniani unaitwa. Awajalieni kwa kadri ya utajiri wa utukufu wake kufanyika imara kwa nguvu kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo na urefu wa kimo na kina na kuujua upendo wake Kristo upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.***

Kama tutakuwa tunasoma neno la Mungu kwa kutafuta sababu zetu na si kukuwa katika upendo wetu na Mungu na wengine (Marko 12:29-31), tunapoteza Muda (1 Wakorintho 8:1). Mtume Paulo aliyekuwa anajua theologia kuliko mtu yeyote duniani (2 Wakorintho 12:1-4), alieleza shauku yake kwa kusema ***"Kwamba nitamjua"*** (Wafilipi 3:10). Paulo kama mfarisayo alikuwa ni mtu wa safari nyingi lakini kama Mkristo alianza kutafuta uhusiano wake wa karibu na Mungu aliye hai.

Tafuta ahadi za Mungu, ziamini ili kwamba upate ***"kukua katika neema na maarifa ya Bwana wetu Yesu Kristo"*** (2 Petro 3:18).

**2. Tuishi Namna Gani?**

Tunapoelewa maana ya Mistari tunayoisoma tunapaswa kutafuta jinsi ya kuutumia katika maisha yetu ya kila siku. Tumepewa mfano mzuri wa wazo lake katika Waebrania 12:1-3. Mstari wa 1 na 2 unasema:

> ***Basi na sisi pia kwa kuwa tunazungukwa na wimbi kubwa la mashahidi namna hii na tuweke kando kila namna ya mzigo wa dhambi ile ituzingayo kwa upesi na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu Kristo mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yetu. Aliustahimili msalaba na kuidharau aibu naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.***

Maelezo aliyoyatumia mwandishi wa Waebrania katika mistari hii miwili ni ya aina yake. Watu wakiwa wamesimama wanaangalia (shujaa wa Sura ya 11). Mashindano ni ya riadha na ya umbali mrefu, na mshindi atakaa katika kiti cha heshima. Yaliyomo yanaondoa uzito wa ziada utakaomfanya awe mzito kukimbia, au upinzani wowote utakaomfanya ashindwe. Macho yake yako katika mstari wa mwisho ambapo Yesu Kristo ambaye amekwisha shinda amesimama. Furaha ya kushindana ni nzuri sana kuliko ile ya kushindwa. Kwa sababu mkimbiaji huvumilia.

Halafu katika mstari wa 3 mwandishi anachukua mistari miwili na kuiweka katika maisha yetu:

> ***Kwa maana mtafakarini sana Yeye aliyestahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao msije mkachoka mkazimia mioyo yenu.***

Tunapokabiliana na shida,upinzani, maumivu na huzuni, aibu na kutokukubalika kwa sababu ya Kristo tunapaswa kumwangalia kiongozi wetu na tutiwe moyo naye. Kumbuka kwamba, ***"Kwa kuwa hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu bali yeye aliyejaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yetu bila kufanya dhambi"*** (Waebrania 4:15).

**C. Nini kama Hatutajibu Maswali Yote?**

Maswali na majibu yake ni Muhimu. Tunapaswa kukumbuka kwamba uhusiano wetu na Mungu aliye hai uko katika Imani (Waefeso 2:8-9; Wakolosai 2:6), hatutapata majibu yote tunayoyatafuta katika maisha yetu. Hata hivyo Mungu ametuahidi kwamba maswali yetu yote yatajibiwa (1 Wakorintho 13:12). Maandiko yana habari nyingi za kutuongoza katika maisha yetu yote.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 1, Sehemu ya 5

1. **Soma Yeremia 39:1-2 na ujibu maswali sita muhimu tunayopaswa kujiuliza kwa kila mstari.**

   Nani? =

   Nini? =

   Lini? =

   Wapi? =

   Kwa nini? =

   Kwa jinsi gani? =

2. **Soma Marko 12:29-31. Kwa mambo gani manne tunapaswa kumpenda Bwana ?**

3. **Soma Waebrania 11:6 na 1 Yohana 2:7-11. Ni mambo gani manne yanahitajika katika maisha ya Kikristo?**

## Sura ya 2

# Agano la Kale

# Utangulizi

Huu ni Utafiti mfupi wa vitabu vya Agano la Kale. Kusudi ni kumpa msomaji, mwandishi na tarehe za kitabu, watu muhimu, nia na makusudi na pia kwa ufupi ni kwa jinsi gani Yesu alivyooneshwa katika kitabu hicho. Kila kitabu kina mambo yake.

Utafiti wa kila kitabu ni muhimu kwa msomaji wa neno la Mungu ili kwamba msomaji apate kufikia uelewa wa matukio makubwa na sura ya kitabu. Ni dhahiri kwamba muda mwingi tunaposoma neno la Mungu ndivyo tunavyolijua. Lakini katika kitabu hiki tunataka tupate picha kwanza ili kwamba mengine tutayatafuta baadaye. Sura ya 1 ina mtazamo mzima wa Biblia yote. Sura hii inaanza kupunguza kusoma kwetu kwa kutazama vitabu vya kila mtu.

## Ulinganifu wa Agano la Kale na Jipya

Kristo ni tumaini na kusudi la vitabu vyote katika Biblia. Kwa matukio mbalimbali Yesu mwenyewe alisema yeye ni msingi wa kila andiko:

1. Katika Mathayo 5:17 alisema, ***"Sikuja kutangua (maandiko) bali kuyatimiliza."***
2. Akiwa na wanafunzi katika barabara ya Emau, Luka anatuambia 24:27 kwamba, ***"… tangu Musa na mitume wote waliopita walieleza mambo yote yanipasayo mimi katika maandiko."***
3. Baadaye jioni ile Yesu aliwaambia wanafunzi kumi katika Luka 24:44-47, ***"Haya ndiyo maneno yangu niliyowaambia nikali nipo pamoja nanyi ya kuwa ni lazima yatimizwe yote yaliyoandikwa katika kitabu cha Manabii na Torati ya Musa na Zaburi, ndivyo ilivyoandikwa kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi kuanzia Yerusalemu."***
4. Katika Yohana 5:39 na 40, kipindi anazungumza na wayahudi, Yesu alisema, ***"Mwayachunguza maandiko kwa sababu mwadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake na hayo ndiyo mnayonishuhudia wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima.."***

Kwa nyongeza katika Ufunuo 19:10, tunaambiwa kwamba ***"Ushuhuda wa Yesu (kuhusu Yesu) ni roho wa Unabii."*** Kwa maneno mengine asili ya unabii na mambo yote yaliyo katika Maandiko ni kumwonesha Yesu. Kwa sababu ya anguko la mwanadamu Kristo ni kusudi la Agano Jipya na Agano la Kale kwa sababu kwa yeye tuna uzima wa milele na maisha ya milele (Yohana 10:10).

| **Agano la Kale** | | |
|---|---|---|
| Sheria-Msingi wa historia ya Yesu<br>Historia-maandalizi ya Yesu<br>Mashairi-Uvuvio wa Yesu<br>Unabii-mategemeo ya kuja kwa Yesu | Maandalizi<br>&<br>Msingi | Agano la kale linaweka msingi wa kuja kwa Masihi Mwokozi na linamwonesha kama nabii,Kuhani,Mfalme na kama Mwokozi atakayeteseka ambaye atakufa kwa ajili ya dhambi za mwanadamu kabla hajatawala. |

| **Agano Jipya** | | |
|---|---|---|
| Injili | Mwonekano | Inaeleza habari za kuja kwa aliyetabiliwa Masihi na kazi zake. |
| Matendo | Kupanuka | Kwa njia ya Roho, matendo inaeleza ujumbe wa Mwokozi aliyekuja. |
| Nyaraka | Maelezo na Matendo | Zinaendeleza umuhimu wa utu na kazi ya Yesu na jinsi inavyoweza kuathiri mwenendo wa Mkristo kama balozi wa Yesu katika ulimwengu. |
| Ufunuo | Kumaliza | Inaonyesha matukio ya wakati wa mwisho na kurudi kwa Bwana,utawala wake na umilele wake. |

**Tafadhali elewa kwamba katika maelezo ya vitabu vya kila mtu vichwa vya habari hajijatolewa kwa sehemu mbalimbali za mistari ya Biblia. Soma kila sehemu na ipatie kichwa chake cha habari.**

# Sehemu ya 1
# Sheria: Vitabu Vitano vya Kwanza

Vitabu vitano vya kwanza katika Biblia huitwa “Pentateuch” inayomaanisha “vitabu vitano.” Pia vinajulikana kama vitabu vya sheria kwa sababu vinasheria na maelekezo yaliyotolewa na Bwana kupitia Musa kwenda kwa watu wa Waisraeli. Vitabu hivi viliandikwa na Musa, isipokuwa sehemu ya mwisho ya kitabu cha Kumbukumbu la Torati kwa sababu kinaeleza kifo chake. Vitabu hivi vinaweka msingi wa kuja kwa Kristo kwa namna hii kwamba Mungu aliwachagua na kuwarudisha taifa la Israeli. Kama wateule wa Mungu waisraeli walikuwa ni watunzaji wa Agano la Kale, wapokeaji wa Agano la Ahadi na watu wa ukoo wa Masihi (Warumi 3:2; 9:1-5).

## Mwanzo
### (Kitabu cha Kuanzia)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Musa ndiye mwandishi wa kitabu. Jina Mwanzo lina maana ya “Kuanza” na limechukuliwa katika Septuagin ( LXX) ambayo ni tafasiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania.

**Tarehe na Muda wa Kuandikwa: 1450-1410 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Japo katika kusoma tunaona makusudi makubwa ya Baraka na Imani, baraka katika bustani ya Edeni lakini kutotii kuna laana. Kitabu kizima kinakusudi hili la baraka na laana. Kusudi jingine ni kuteuliwa kwa Taifa kupitia Agano la Ibrahimu. Kupitia Ibrahimu Mungu aliahidi kubariki mataifa yote (12:1-3; 15:1-21).

Mwanzo haina maana ya kuanza lakini ni kitabu cha mwanzo katika Biblia. Kitabu cha Mwanzo kinatupa Historia ya ufunuo wa Mungu ulivyoendelea. Katika Kitabu cha Mwanzo kila kusudi lina mwanzo wake. Ni kitabu cha mambo mengi yalivyoanza; katika kitabu hiki tunaona jinsi ulimwengu ulivyoanza, mtu mme na mke, dhambi ya mwanadamu,na ukoo wa mwanadamu, mwanzo wa ahadi ya Mungu ya wokovu, na mwanzo wa taifa la Israeli kama watu walioteuliwa na Mungu kwa makusudi maalumu kwa ajili ya maandalio ya Masihi wetu. Katika Mwanzo tunajifunza juu ya Eva, Adamu, Shetani, Nuhu, Gharika, Ibrahimu, Isaka, Yakobo na Yusufu na ndugu zake. Tunaona mwanzo wa ndoa, familia, kazi, dhambi, uuaji, adhabu, dhabihu, ukoo, lugha, ustaarabu, majaribu ya serikali ya ulimwengu na Babeli (mkoa ulioanzishwa katika mnara wa Babeli). Biblia ni ufunuo wa kihistoria. Ni mwonesho wa kazi za Mungu katika Historia.

Neno lililo katika Mwanzo linasema: “Hivi ni vizazi vya.” limetumika mara 11 kumwonesha msomaji katika sehemu zinazofuatia zitoazo habari za yale yaliyotokea kwa kuunganishwa na matukio muhimu na watu, tangu uumbwaji wa dunia na mbingu hadi kwa Waisreli.

**Watu Muhimu:** Adamu, Eva, Nuhu, Ibrahimu, Sara, Isaka, Rebeka, Esau, Yakobo, Raheli, Yusufu

**Mwonekano wa Yesu Katika Kitabu cha Mwanzo–Kiunabii:** Baada ya anguko tu, ahadi ya wokovu ilitolewa katika mbegu ya mwanamke (3:15), lakini mahusiano ya kimasihi yameonekana katika kitabu chote cha Mwanzo: ukoo wa Sethi (4:25), watoto wa Shem (9:26), jamaa ya Ibrahimu (12:3), mbegu ya Yakobo (26:3), mwana wa Yakobo (46:3), na kabila la Yuda (49:10).

Kuna aina mbalimbali zinazomwonesha Yesu katika Mwanzo. **Adamu** ni aina ya Yesu (Warumi 5:14).

Adamu ni mkuu wa Uumbaji na Yesu ni mkuu wa uumbaji mpya wa kiroho.

Sadaka ya **Habili** ya damu inaonyesha Kristo atakaye kufa kwa ajiri yetu. Uuaji wa Habili wa ndugu yake Kaini inaonesha kifo cha Kristo.

Mfalme **Melkizedeki** na kuhani ni mfano wa Kristo (Waebrania 7:3).

**Yusufu**, aliyekuwa akipendwa na baba yake akasalitiwa na ndugu zake na halafu akawaokoa ndugu zake ni mfano wa Kristo.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

**Toa kichwa cha habari katika sehemu ambazo hazikupewa visa vyake. Katika vichwa vya habari vyako jaribu kuonesha mahusiano yaliyopo kati ka kifungu kimoja na kingine. Kwa mfano katika sehemu "C" mtu anaweza kueleza kama ifuatavyo:**

***1) Maandalizi ya Ibrahimu kwa ajili ya Gharika***
***2) Nuhu katika Gharika***
***3) Gharika***
***4) Agano na Nuhu***
***5) Familia ya Nuhu***

1. **Matukio Manne (1:1–11:32)**

a. Uumbaji wa Ulimwengu na Mwanadamu (1:1–2:25)

| | | |
|---|---|---|
| 1:1–2:3 | 2:4-25 | |

b. Anguko la Mwanadamu (3:1–5:32)

| | | |
|---|---|---|
| 3:1-24 | 4:1-24 | 4:25–5:32 |

c. Kuharibiwa kwa Mwanadamu, Gharika (6:1–9:29)

| | | |
|---|---|---|
| 6:1-22 | 8:1-22 | 9:18-29 |
| 7:1-24 | 9:1-17 | |

d. Utawanyika kwa Mwanadamu, Mataifa (10:1–11:32)

| | | |
|---|---|---|
| 10:1-32 | 11:1-9 | 11:10-31 |

2. **Watu Wanne: Kuteuliwa kwa Taifa na Maandalizi ya Mwokozi (12:1–50:26)**

a. Ibraham (Baba wa Imani na Taifa la Israel) (12:1–23:20)

| | | |
|---|---|---|
| 12:1-20 | 16:1-16 | 20:1-18 |
| 13:1-18 | 17:1-27 | 21:1-34 |
| 14:1-16 | 18:1-33 | 22:1-24 |
| 14:17-24 | 19:1-29 | 23:1-20 |
| 15:1-21 | 19:30-38 | |

b. Isaka (Mwana Mpendwa wa Ahadi) (24:1–26:35)

| | | |
|---|---|---|
| 24:1-67 | 25:19-34 | 26:26-35 |
| 25:1-11 | 26:1-17 | |
| 25:12-18 | 26:18-25 | |

c. Yakobo (Njamna na Adabu) (27:1–36:43)

| | | |
|---|---|---|
| 27:1-46 | 31:1-55 | 34:1-31 |
| 28:1-22 | 32:1-23 | 35:1-8 |
| 29:1-35 | 32:24-32 | 35:9-29 |
| 30:1-43 | 33:1-20 | 36:1-43 |

d. Yusufu (Mateso na Utukufu) (37:1–50:26)

| | | |
|---|---|---|
| 37:1-36 | 40:1–41:57 | 49:1–50:21 |
| 38:1-30 | 42:1–45:28 | 50:22-26 |
| 39:1-23 | 46:1–48:22 | |

# Kutoka
### (Kitabu cha Wokovu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Musa aliandika kitabu hiki. "Kutoka" ni neno la Kilatini lililotoka katika Lugha ya Kiyunani *EXODOS*, jina lilipewa kwa kitabu na wale waliotafasiri kwa kiyunani (LXX). Neno lina maana ya Kutoka.

**Muda wa Kitabu: 1450–1410 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Kuna makusudi mawili: (1) Wokovu kama ilivyoonyeshwa katika Pasaka, na (2) Ukombozi toka katika vifungo vya Wamisri kama ilivyoonekana.

Baada ya miaka zaidi ya miwili ya kuwa katika nchi ya Misri, Kutoka inaendeleza historia ya wateule wa Mungu, taifa la Israeli na inaeleza ukombozi wao kutoka Misri na kupewa sheria. Inaeleza kuzaliwa, historia, na kuitwakwa Musa na Mungu kuwaongoza watu kutoka Misri kwenda katika nchi yao ya ahadi Kanani. Kwa njia ya pasaka ya mwanakondoo ya mzaliwa wa kwanza pamoja na miujiza ya mapigo kumi na kupita katika bahari nyekundu, Mungu aliwaonesha watu wake kwamba hakuwa mwenye nguvu tu kama Farao wa Misri bali alikuwa ni mwenye mamlaka Bwana,Yahwe Mungu wa wokovu na ufunuo.

Watu walipotoka katika bahari nyekundu walifika katika jangwa na Mungu aliwapa sheria zake za haki na akasema kwamba walikuwa ni hazina yake na watakuwa makuhani wa ufalme,taifa takatifu kama ushuhuda kwa taifa (Kutoka 19:4-7). Sheria hii takatifu pamoja na amri kumi zilieleza utakatifu wa Mungu zikiwafundisha jinsi ya kumpenda Mungu na wengine, lakini si hivyo tu, lakini pia zilieleza ni kwa jinsi gani kila mtu amepungukiwa na utakatifu wa Mungu na anahitaji njia ya Mungu ili apate kusamehewa. Hizi zilitolewa katika Hekalu, Dhabihu na katika Makuhani wa Kilawi.

**Watu Muhimu:** Musa, Haruni, Miriamu, Farao

**Mwonekano wa Yesu Katika Kitabu cha Kutoka:** Japo kitabu cha Kutoka hakina unabii wowote wa Yesu lakini kuna mambo mazuri yanayo mwonyesha Kristo. Katika njia nyingi Musa ni mfano wa Kristo. Kumbukumbu la Torati 18:15 inaonesha kwamba Musa kama nabii anamwakilisha Kristo.

**Pasaka** ni mfano wa Kristo kama mwanakondoo asiye na hatia wa Mungu (Yohana 1:29, 36; 1 Wakorintho 5:7).

**Karamu saba** zinamwakilisha Kristo.

**Kutoka yenyewe** ambayo Paulo anaiunganisha na ubatizo inatuonyesha picha yetu ya kufa pamoja na Kristo, Kuzikwa na kufufuka (1 Wakorintho 10:1-2; Warumi 6:2-3).

**Mana na Maji** ni picha za Kristo (Yohana 6:31-35, 48-63; 1 Wakorintho 10:3-4).

Hekalu linamwakilisha Yesu katika vifaa vyake, rangi, vitu vya samani, mpango na hata dhabihu zilizofanyika (Waebrania 9:1–10:18).

**Kuhani mkuu** anamwakilisha Kristo na Huduma yake (Waebrania 4:14-16; 9:11-12, 24-28).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Ukombozi kutoka Misri (1:1–18:27)**
   a. Katika Vifungo (Lengo) (1:1–12:32)

| | | |
|---|---|---|
| 1:1-7 | 5:1-23 | 9:8-17 |
| 1:8-14 | 6:1-13 | 9:18-35 |
| 1:15-22 | 6:14-30 | 10:1-20 |
| 2:1-14 | 7:1-7 | 10:21-29 |
| 2:15-25 | 7:8-13 | 11:1-10 |
| 3:1-9 | 7:14-25 | 12:1-13 |
| 3:10-22 | 8:1-15 | 12:14-22 |
| 4:1-13 | 8:16-32 | 12:23-32 |
| 4:14-31 | 9:1-7 | |

   b. Kutoka katika Vifungo (Ukombozi kwa Njia ya Dani na Nguvu) (12:33–14:31)

| | | |
|---|---|---|
| 12:33-41 | 13:1-16 | 14:1-12 |
| 12:42-51 | 13:17-22 | 14:13-31 |

   c. Safari ya Kwenda Sinai (Elimu) (15:1–18:27)

| | | |
|---|---|---|
| 15:1-21 | 16:8-21 | 17:8-16 |
| 15:22-27 | 16:22-36 | 18:1-16 |
| 16:1-7 | 17:1-7 | 18:17-27 |

2. **Ufunuo Kutoka kwa Mungu (19:1–40:38)**
   a. Kupewa Sheria (19:1–24:18)

| | | |
|---|---|---|
| 19:1-17 | 22:1-15 | 23:20-33 |
| 19:18-25 | 22:16-31 | 24:1-18 |
| 20:1-26 | 23:1-9 | |
| 21:1-36 | 23:10-19 | |

   b. Utendaji Kazi katika Hema (25:1–31:18)

| | | |
|---|---|---|
| 25:1-9 | 26:31-37 | 29:31-46 |
| 25:10-22 | 27:1-8 | 30:1-21 |
| 25:23-30 | 27:9-21 | 30:22-33 |
| 25:31-40 | 28:1-43 | 30:34-38 |
| 26:1-14 | 29:1-9 | 31:1-11 |
| 26:15-30 | 29:10-30 | 31:12-18 |


c. Kuvunjwa Sheria (32:1–34:35)

| | | |
|---|---|---|
| 32:1-10 | 33:1-11 | 34:10-28 |
| 32:11-18 | 33:12-23 | 34:29-35 |
| 32:19-35 | 34:1-9 | |

d. Ujenzi wa Hema (35:1–40:38)

| | | |
|---|---|---|
| 35:1-9 | 36:8-38 | 39:1-43 |
| 35:10-19 | 37:1-29 | 40:1-33 |
| 35:20-35 | 38:1-20 | 40:34-38 |
| 36:1-7 | 38:21-31 | |

**Ramani ya Hekalu**
(haikuwa katika vipimo)




# Mambo ya Walawi
## (Kitabu cha Utakatifu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Musa ndiye mwandishi. Kitabu cha Mambo ya Walawi kilipata jina lake kutoka Septuagint na lina maana ya "Mahusiano na walawi". Walawi walikuwa ni makuhani waliokuwa wamechaguliwa na Mungu kutumika katika Taifa. Kitabu hiki kinasheria nyingi zilizotolewa na Mungu katika kazi zao kama makuhani katika kumwabudu Mungu.

**Muda wa Kuandikwa: 1450–1410 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Mambo ya Walawi 11:45 inasema, ***"Muwe watakatifu kama Mimi nilivyo mtakatifu."*** Maelezo yaliyotolewa katika Kitabu hiki yaliwaonesha Waisraeli watembee mbele za Mungu kama watu watakatifu. Kitabu hiki kiliandikwa ili kuwafundisha Waisraeli (1) jinsi gani ya kuabudu na kutembea na Mungu na (2) jinsi gani kama taifa linaweza kukamilisha wito wake kama taifa la makuhani. Kusudi kuu la kitabu cha Mambo ya Walawi ni utakatifu. Utakaso ni njia inayomfanya mtu kuwa Mtakatifu. Mungu mtakatifu hufikiwa kwa dhabihu kwa njia ya upatanishi wa Kuhani.

**Watu Muhimu:** Musa na Haruni

**Mwonekano Wa Yesu Katika Kitabu cha Mambo Ya Walawi:** Sawa na Kutoka, kuna mambo mengi yanayomwonyesha Kristo katika kitabu hiki.

**Dhabihu Tano** ni mfano wa kazi ya Yesu katika maisha yake yasiyo na dhambi,kujitoa kwakwe kwa Baba ili kwamba tuwe na ushirika na Mungu.

**Kuhani Mkuu** ni mfano wa Kristo.

**Karamu Saba** ni mfano wa mwokozi, zinatufundisha juu ya ukamilifu wake,kujitoa kwake,kufufuka kwake na kazi yake ya upakwa mafuta.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Sheria za Matoleo (1:1–17:16)**
   a. Kwa Ajili ya Kumfikia Mungu (1:1–7:38)

| | | |
|---|---|---|
| 1:1-17 | 4:1-35 | 6:8-30 |
| 2:1-16 | 5:1-19 | 7:1-38 |
| 3:1-17 | 6:1-7 | |

   b. Kwa Ajili ya Makuhani (8:1–10:20)

| | |
|---|---|
| 8:1-36 | 9:15-24 |
| 9:1-14 | 10:1-20 |

   c. Kwa Ajili ya Utakazo (11:1–15:33)

| | | |
|---|---|---|
| 11:1-12 | 13:1-59 | 15:1-33 |
| 11:13-47 | 14:1-32 | |
| 12:1-8 | 14:33-57 | |

   d. RKuponya Nchi (16:1–17:16)

| | | |
|---|---|---|
| 16:1-28 | 16:29-34 | 17:1-16 |

2. **Sheria za Utakaso (18:1–27:34)**
   a. Kwa ajili ya watu wa Mungu (18:1–20:27)

| | |
|---|---|
| 18:1-30 | 19:9-37 |
| 19:1-8 | 20:1-27 |

   b. Kwa Ajili ya Makuhani wa Mungu (21:1–22:33)

| | | |
|---|---|---|
| 21:1-24 | 22:1-16 | 22:17-33 |

   c. Katika Ibaada (23:1–24:23)

| | |
|---|---|
| 23:1-25 | 24:1-16 |
| 23:26-44 | 24:17-23 |

   d. Katika Nchi ya Kanaani (25:1–26:46)

| | | |
|---|---|---|
| 25:1-22 | 25:35-46 | 26:1-13 |
| 25:23-34 | 25:47-55 | 26:14-46 |

   e. Kuhusiana na Mahali za Ndoa (27:1-34)

| | |
|---|---|
| 27:1-13 | 27:14-34 |

# Hesabu

## (Mizunguko Jangwani)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Musa ndiye mwandishi. Hesabu imepata jina lake katika mambo mawili yalio katika sura ya 1 na 26 za kuhesabu watu wa Israeli kwa mara ya kwanza katika mlima Sinai na katika nchi ya Moabu.

**Muda wa Kuandikwa: 1450–1410 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Japo kitabu cha Hesabu kilipata jina lake kutokana na kuhesabiwa kwa watu wa Israeli lakini kusudi lake ni mizunguko ya miaka 40 jangwani. Safari ambayo ingechukua muda wa siku 11 ikawa miaka 38 ya mateso kwa sababu ya kutotii kwao. Hesabu inaonesha madhara ya kuchanganya desturi na ahadi ya Mungu (Waebrania 3:16–4:2). Kwa nyongeza Hesabu inatufundisha kwamba japo maisha yanaweza kuwa magumu, watu wa Mungu hawawezi kukaa katika magumu hayo. Uamuzi tunaoufanya ndiyo unaokaa katika maisha yetu. Yoshua ataeleza hii baadaye.

Kusudi jingine tunaloliona katika kitabu hiki ni ulinzi wa Mungu kwa watu wake. Bila kutazama uasi wao, Mungu aliwahudumia na kuwatimizia mahitaji yao. Aliwapa maji, Manna na Kware. Aliendelea kuwapenda na kuwasamehe walipokuwa wakinug'unika na kumlaumu.

**Watu Muhimu:** Musa, Haruni, Miriamu, Yoshua, Kalebu na Baraka

**Mwonekano wa Yesu Katika Kitabu cha Hesabu:** Labda hakuna sehemu nzuri inayomwonyesha Kristo zaidi ya **nyoka wa shaba** aliyeinuliwa (Hesabu 21:4-9 linganisha Yohana 3:14).

**Mwamba uliotoa maji** ni mfano wa Kristo (1 Wakorintho 10:4).

**Manna** inamwakilisha Yesu kama mkate uliotoka mbinguni (Yohana 6:31-33).

**Wingu na Moto** zinaonesha ulinzi wa Kristo na kambi ya wakimbizi inamwonesha Kristo kama mwokozi katika hukumu.

**Mwisho Beberu mwekundu** ni mfano wa Kristo (Hesabu 19).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Maandalizi katika Mlima Sinai (Kizazi Cha Kale) (1:1–10:36)**
   a. Sehemu na Hesabu ya Watu (1:1–4:49)

| | | |
|---|---|---|
| 1:1-46 | 3:1-24 | 4:1-20 |
| 1:47-54 | 3:25-39 | 4:21-28 |
| 2:1-34 | 3:40-51 | 4:29-49 |

   b. Utakaso wa Watu (5:1–9:14)

| | | |
|---|---|---|
| 5:1-10 | 6:22-27 | 8:5-22 |
| 5:11-31 | 7:1-89 | 8:23-26 |
| 6:1-21 | 8:1-4 | 9:1-1 |

   c. Ibaada Kuelekea Nchi ya Ahadi (9:15–10:36)

| | | |
|---|---|---|
| 9:15-23 | 10:1-10 | 10:11-36 |

2. **Kushindwa kwa Kizazi Kilichopita (11:1–25:18)**
   a. Mafarakano(11:1–12:16)

| | | |
|---|---|---|
| 11:1-9 | 11:16-30 | 12:1-16 |
| 11:10-15 | 11:31-35 | |

   b. Mapokeo katika Kadesh-Barnea (13:1–14:45)

| | | |
|---|---|---|
| 13:1-24 | 14:1-10 | 14:20-38 |
| 13:25-33 | 14:11-19 | 14:39-45 |

   c. Maonyo toka kwa Bwana (15:1–25:18)

| | | |
|---|---|---|
| 15:1-13 | 18:8-32 | 21:21-35 |
| 15:14-31 | 19:1-22 | 22:1-21 |
| 15:32-41 | 20:1-7 | 22:22-41 |
| 16:1-40 | 20:8-22 | 23:1-30 |
| 16:41-50 | 20:23-29 | 24:1-25 |
| 17:1-13 | 21:1-5 | 25:1-9 |
| 18:1-7 | 21:6-20 | 25:10-18 |

3. **Maandalizi ya Kizazi Kipya (26:1–36:13)**
   a. Kutambuliwa kwa Waisraeli (26:1–27:23)

| | | |
|---|---|---|
| 26:1-65 | 27:1-14 | 27:15-2 |

   b. Taratibu za Utoaji Sadaka na Hahari za Ndoa (28:1–30:16)

| | | |
|---|---|---|
| 28:1-31 | 29:1-40 | 30:1-16 |

   c. Kutambuliwa kwa Nchi (31:1–36:13)

| | | |
|---|---|---|
| 31:1-24 | 33:1-49 | 35:1-5 |
| 31:25-54 | 33:50-56 | 35:6-34 |
| 32:1-42 | 34:1-29 | 36:1-13 |

# Kumbukumbu la Torati

### (Kuangalia Sheria Tena)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Musa ndiye mwandishi. Ni neno la kiingereza linalotoka katika Lugha ya Septuagint, lenye maana ya kupewa sheria mara ya pili na linatoka katika tafasiri tofauti ya 17:18, ambayo inatafasiriwa kama nakala ya sheria hii. Kumbukumbu la Torati si sheria ya pili lakini ni upanuliwaji wa sheria zilezile katika mlima Sinai.

**Muda wa Kuandikwa: 1410 K.K.**

**Nia Na Makusudi:** ***Jitazame usije ukajisahau.*** Baada ya miaka 40 ya kuzunguka jangwani waisraeli walikuwa wakielekea kuingia katika nchi yao ya ahadi. Kabla hawajaingia ilikuwa ni lazima kukumbuka yote Mungu aliyowatendea na kuhusu sheria takatifu ya Bwana ambayo ilikuwa ni muhimu sana kubaki katika taifa na kutenda kama taifa takatifu na kama ufalme wa kuhani katika taifa (Kumbukumbu la Torati 4:1-8). Kama sehemu ya makusudi haya, kitabu kinakazia umuhimu wa kuwafundisha watoto kumpenda na kumtii Mungu.

Kumbukumbu la Torati linaishia na utengenezaji upya wa agano la Mungu na Israreli (Sura 29), Yoshua kama kiongozi mpya (Sura 31), na kifo cha Musa (Sura 34).

**Watu Muhimu:** Musa na Yoshua

**Mwonekano wa Yesu Katika Kitabu cha Kumbukumbu la Torati:** Maelezo ya Musa katika 18:15 ni moja ya mambo yanayomwonesha Kristo. Inasema ***"Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi msikilizeni yeye."*** Japo Musa anamwakilisha Kristo lakini ni picha kubwa zaidi ya Kristo kwa kukamilisha mambo yote matatu ya unabii (34:10-12), Kuhani (Kutoka 32:31-35), na Mfalme (japo Musa alitenda kama si mfalme, lakini alikuwa ni mtawala na kiongozi wa Israeli; 33:4-5).[2]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi (1:1-5)**

2. **Kuitazama Historia Tena (1:6–4:43)**
   1:6-18 | 2:26-37 | 4:1-43
   1:19-46 | 3:1-17
   2:1-25 | 3:18-29

3. **Kuitazama Sheria Tena (4:44–5:33)**
   4:44-49 | 5:1-21 | 5:22-33

4. **Kuitenda Sheria Tena (6:1–11:32)**
   6:1-25 | 9:1-29 | 11:1-32
   7:1-26 | 10:1-11
   8:1-20 | 10:12-22

5. **Kuongezwa kwa Sheria (12:1–26:19)**
   12:1-32 | 18:9-22 | 23:1-25
   13:1-18 | 19:1-13 | 24:1-5
   14:1-29 | 19:14-21 | 24:6-22
   15:1-23 | 20:1-20 | 25:1-19
   16:1-22 | 21:1-23 | 26:1-19
   17:1-20 | 22:1-12
   18:1-8 | 22:13-20

6. **Kulikubali Agano (27:1–30:20)**
   27:1-26 | 28:15-68 | 30:1-14
   28:1-14 | 29:1-29 | 30:15-20

7. **Badiliko la Uongozi (31:1–34:12)**
   31:1-13 | 32:1-52 | 34:1-12
   31:14-30 | 33:1-29

## Muhitasari: Mambo ya Kukumbuka

| | |
|---|---|
| Mwanzo | Kuchaguliwa kwa Taifa Teule |
| Kutoka | Kukombolewa kwa Taifa Teule |
| Mambo ya Walawi | Utakaso wa taifa Teule |
| Hesabu | Mwongozo wa Taifa Teule |
| Kumbukumbu la Torati | Mafunzo ya Taifa Teule |

# Sehemu ya 2
# Vitabu vya Kihistoria

**Utangulizi:** Maeneo tofauti tofauti ya vitabu vya Agano la Kale hufundisha yakituelekeza tu kwa Mtu mmoja Kristo. Kwa kuanza na Yoshua hadi Esta, vitabu vya pili vinavyohusika na historia ya wana wa Israeli. Vitabu hivi vinafunika kabisa umiliki wa taifa hadi kwenye mambo mawili ya kufukuzwa na kupotea kwa nchi hiyo kwa sababu ya kutotii na kufuata matakwa yake. Hii tunaiona ndani ya miaka 800 ya historia ya Israel,vitabu hivi kumi na mbili vinaeleza habari ya kutekwa na kutawaliwa kwa nchi ya Kanani, utawala wa Waamuzi, Wafalme, mgawanyo wa Israeli wa kaskazini na kusini, kuanguka kwa utawala wa kaskazini mikononi mwa Waasria na uhamisho wa utawala wa kusini kwenda Babeli na kurudi Yerusalemu chini ya utawala wa watu kama Nehemia na Ezra.

Vitabu vyote hivi vinatuandaa kuja kwake Kristo, Masihi na vinaeleza mambo yafuatayo:

| Vitabu vya Kihistoria: Maandalizi ya Kristo[3] | | |
|---|---|---|
| Yoshua<br>Waamuzi<br>Ruthu | Umiliki wa nchi kwa Taifa na ukandamizwaji wa Taifa | Utawala na Mungu: Vitabu hivi vinafunika kipindi cha Waisraeli walipokuwa wakitawaliwa na Mungu (1405-1043 K.K.). |
| 1 Samweli<br>2 Samweli<br>1 Wafalme 1-10<br>1 Wafalme 11-22<br>2 Wafalme 1-17<br>2 Wafalme 18-25<br>1 Nyakati<br>2 Nyakati | Uimarisho wa taifa<br>Kuongezeka kwa taifa<br>Utukufu wa taifa<br>Mgawanyo wa taifa<br>Kuharibiwa kwa ufalme wa kaskazini<br>Kuondolewa kwa ufalme wa Kusini<br>Maandalizi ya Hekalu<br>Kuharibiwa kwa Hekalu | Ufalme: Vitabu hivi vinaeleza historia ya ufalme wa Israeli tangu kusimamishwa kwake hadi kuharibiwa kwake 586 K.K. |
| Ezra<br>Nehemia<br>Esta | Kurejeshwa kwa Hekalu<br>Ujenzi wa Yerusalemu tena<br>Ulinzi wa watu wa taifa | Kurejeshwa: Vitabu hivi vinaeleza kurudi kwa wageni katika nchi baada ya miaka 70 kuwa mateka (605-536 K.K.). |

## Yoshua
### (Umiliki na Utawala)

**Mwandishi na Jina la Kitabu:** Yoshua aliandika kitabu hiki kikiwa tofauti kabisa na vitabu vingine vitano vilivyo tangulia. Jina la kitabu hiki linatoka kwa mtawala mwanadamu Yoshua mtumishi wa Musa. Jina halisi la Yoshua lilikuwa Hoshea (Hesabu 13:8, Kumb 32:44) lina maana ya “Wokovu.” Wakati wa safari ya kuzunguka jangwani Musa alibadili jina lake na kuwa Yehoshua likiwa na maana ya ’Yahwe” yaani Wokovu (Hesabu 13:16). Yoshua ni matokeo ya Yehoshua . Hii inaonesha mambo ya kiunabii na kumbukumbu ya Yoshua, wapelelezi na kwa watu kwamba ushindi dhidi ya maadui na umiliki wa nchi uko katika nguvu za Bwana na si kwa akili na nguvu za mwanadamu. Kitabu hiki kilipewa jina Yoshua kwa sababu japo Yoshua alikuwa amiri Jeshi mkuu wa kihistoria busara zake na hata utawala wake ulitoka kwa Bwana ambaye peke yake ni wokovu wetu. Ni Bwana peke yake ambaye alileta wokovu na ushindi kwa waisraeli na hata kuwashinda maadui wao na hata kuwapa kumiliki nchi.

**Muda wa Kuandikwa: 1400–1370 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Kumiliki, Kutawala, na kugawiwa kwa nchi ndiyo nia na makusudi ya Joshua. Kitabu cha Yoshua kimeandikwa kwa ajili ya kuonyesha uaminifu Wa Mungu katika ahadi zake alizozifanya kwa watu wake Israeli kama alivyokuwa amewaahidi (Mwanzo 15:18 Yoshua 1:2-6; 21:43-45). Matukio yaliyoratibiwa katika Yoshua yamechanganuliwa ili kuonesha mwingilio wa Mungu kwa niaba ya watu wake dhidi ya nguvu zote zilizo chafu. Katika kukamilisha ahadi ya Mungu kwa ushahidi wa uzazi wa Isaka kwa Ibrahimu na Sara na hata katika kumiliki nchi na miji yake ni kazi ya Mungu na kwamba hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kufanya yote haya ambayo Mungu aliyafanya hata kama angekuwa na nguvu gani (Warumi 4)
**Watu Muhimu:** Yoshua, Rahabu, Kalebu

**Mwonekano wa Yesu katika Kitabu cha Yoshua:** Japokuwa hakuna unabii wa moja kwa moja wa Masihi unaoonekana lakini kuna mambo yanayomwonyesha Yesu. Yoshua ni aina ya Kristo kwa mambo makubwa mawili: (1) Jina lake ambalo linageuka na kuwa Yeshua lenye maana ya “Yahwe” yaani Wokovu, hili ni la Kigiriki

lenye maana sawa na Yesu. Yoshua kwa kawaida anaitwa kwa jina la Yesu katika Matendo 7:45. (2) Yoshua anaonekana kama mfano wa Yesu katika kazi yake ya kuwaongoza wana wa Israeli katika nchi yao ya ahadi (Waebrania 2:9-10). Yoshua pia alikutana na kamanda wa jeshi la Mungu katika ile sura 5:13-15. Hii nayo ni picha halisi ya Kristo. Neno (christophany) lina maana ya kuwa Yesu alikuwa akimfundisha Yoshua asilegee bali awe Kamanda. Mwisho Rahabu (2:21) anatangaza wokovu kupitia damu ya Yesu (Waebrania 9:19-22). Kahaba huyu alisikia habari za Kazi ya Yesu, akaamini,akajificha, na aliokolewa kipindi Yeriko ilipoharibiwa na inaonekana katika ukoo wa Yesu (Mathayo 1:5)

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Uvamizi wa Wakanaani (1:1–5:12)**

| | | |
|---|---|---|
| 1:1-9 | 2:1-24 | 4:1-24 |
| 1:10-18 | 3:1-17 | 5:1-12 |

2. **Kutawala kwa Wakanaani (5:13–12:24)**

| | | |
|---|---|---|
| 5:13-15 | 8:1-35 | 10:29-43 |
| 6:1-27 | 9:1-27 | 11:1-23 |
| 7:1-15 | 10:1-15 | 12:1-24 |
| 7:16-26 | 10:16-28 | |

3. **Kutawala kwa Wakanaani (13:1–21:45)**

| | | |
|---|---|---|
| 13:1-33 | 17:1-18 | 20:1-9 |
| 14:1-15 | 18:1-10 | 21:1-45 |
| 15:1-63 | 18:11-28 | |
| 16:1-10 | 19:1-51 | |

4. **Hitimisho (22:1–24:33)**

| | |
|---|---|
| 22:1-34 | 24:1-28 |
| 23:1-16 | 24:29-33 |

# Waamuzi

### (Uasi, Hukumu na Wokovu)

**Mwandishi na Jina la Kitabu:** Historia inatueleza kuwa Samweli aliandika kitabu hiki lakini mfumo wa uandishi wake hauna hakika sana,Samweli anaweza kuwa alikuwa amekusanya mambo fulani toka kwa Waamuzi. Manabii kama vile Nathani na Gadi inaweza kuwa walihusika katika kukihariri kitabu hiki (1 Nyakati 29:29).

Kichwa cha habari kwa Kiebrania ni Shophetim, ikiwa na maana ya Waamuzi, Watawala Wakombozi au Mwokozi. Shophet siyo tu kwamba inabeba maana ya kulinda haki na kutengeneza mashtaka lakini pia ilikuwa na maana ya “mapinduzi na kukomboa”. Kwanza kabisa Waamuzi waliwaokoa watu halafu walitawala na kulinda haki.[4]

Kitabu kinapata jina lake kutoka kwa idadi ya viongozi wanaoitwa “Waamuzi” ambao Mungu aliwainua ili wapate kuwaokoa waisraeli kutoka katika kukandamizwa. Kichwa cha habari cha kitabu hiki kinaonekana vizuri 2:16, **“*Kisha Bwana akawainua waamuzi waliowaokoa na mikono ya watu hao waliowateka nyara.”*** Hata hivyo Mungu alikuwa mwamuzi wa Israeli na mwokozi kwa sababu alikuwa ni Mungu ambaye aliwaweka kakika Mateso kwa kuwa walikuwa wamekengeuka (waligeukia njia zao wenyewe na hivyo Mungu akainua Waamuzi ili walete uokoaji baada ya taifa kuwa limetubu na kujuta likihitaji msaada) (11:27 ;823).

**Muda wa Kuandikwa: 1050-1000 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Yoshua na Waamuzi wanashabiana. Waisraeli wanaondoka kwenye furaha ya ushindi na kwenda katika masumbuko makali,na kutoka katika hali ya juu kabisa ya mambo yao na kwenda katika hali ya chini kabisa. Sasa kwa nini kuna kitabu hiki?

**Kihistoria:** Waamuzi ni daraja kutoka nyakati za Yoshua hadi nyakati za Samweli na mwanzo wa utawala wa kifalme chini ya Sauli na Daudi. Kinatoa historia ya kushindwa kwao, ukandamizwaji, maombi, na hata wokovu pia. Kwa kufanya hivyo kinakuwa ni kitabu cha maelezo na cha sababu ya mahitaji ya ufalme katika Israeli. Kwa kuwa kila mtu alikuwa akifanya kitu kinachompendeza machoni pake (21:25) hivyo, hitaji la taifa lilikuwa ni kupata Mfalme atakayewaongoza katika haki.
**Kimafundisho,** Waamuzi kinatupa mambo mazuri yaliyo katika ukweli. Kama Mungu alivyotahadharisha katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati kutii kunatupa baraka, lakini kutotii ni laana. Waamuzi wanatukumbusha

kuwa ikiwa watu watamrudia Bwana wakamlilia na kutubu, Mungu ambaye anatuhangaikia sisi, mwingi wa neena atatusikia na kutuokoa. Waamuzii inatuonesha kusudi lake la jinsi walivyojifungua katika maelezo yao kwa kuonesha madhaifu na jinsi gani walivyofanya katika kutubu yote na Bwana akainua na kuokoa taifa lao.

**Watu Muhimu:** Mwamuzi-Othniel, Ehudi, Shamga, Debora na Baraka, Gideon, Tola na Yairo, Yeftam, Ibzan, Elon, na Abdoni, na Samsoni. Waamuzi wazuri wanaojulikana ni Debora, Gideoni na Samsoni.

**Mwonekano wa Yesu katika Waamuzi:** Japo kuwa kila mwamuzi alikuwa akitenda kama mwokozi na mtawala walionyesha picha kabisa ya Yesu katika kazi yake kama mwokozi, Mfalme mwenye haki ya kuokoa.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Kukana–Utangulizi: Sababu Zilizopelekea Waamuzi (1:1–3:8)**

| | | |
|---|---|---|
| 1:1-26 | 2:1-5 | 2:11-23 |
| 1:27-36 | 2:6-10 | 3:1-8 |

2. **Ukombozi–Historia na Utawala katika Kipindi cha Waamuzi (3:8–16:31)**

| | | |
|---|---|---|
| 3:8-14 | 7:19-25 | 12:8-10 |
| 3:15-30 | 8:1-27 | 12:11-12 |
| 3:31 | 8:28-35 | 12:13-15 |
| 4:1-24 | 9:1-22 | 13:1-25 |
| 5:1-31 | 9:23-57 | 14:1-11 |
| 6:1-8 | 10:1-2 | 14:12-20 |
| 6:9-27 | 10:3-18 | 15:1-20 |
| 6:28-35 | 11:1-28 | 16:1-17 |
| 6:36-40 | 11:29-40 | 16:18-27 |
| 7:1-18 | 12:1-7 | 16:28-31 |

3. **Udhaifu–Uasi na Utawala: Mabaki Kipindi cha Waamuzi (17:1–21:25)**

| | | |
|---|---|---|
| 17:1-13 | 20:1-17 | 21:8-25 |
| 18:1-31 | 20:18-48 | |
| 19:1-30 | 21:1-7 | |

# Ruthu

### (Nyongeza kwa Waamuzi)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama kwa Waamuzi, hakika mtunzi wa kitabu hiki pia hajulikani, japo Wayahudi wanasema kuwa ni Samweli. Kitabu cha Ruthu kilipata jina lake kutoka kwa mhusika wake binti, wa Kimoabu bibi mkubwa wa Daudi ambaye anazungumziwa sana na kumuashiria Yesu (Mathayo 1:5). Na kitabu kingine katika Biblia kilichoitwa baada ya mwanamke huyu ni Esta.

**Muda wa Kuandikwa : 1050 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Ruthu ni historia ya wanandoa wawili katika Israeli ambao wakati wa njaa walihamia Moabu. Huko mme wake na watoto walikufa wakamwacha mwanamke (Naomi ) peke yake akiwa na wakweze wa kike (Orpa na Ruthu). Naomi aliamua kurudi Israeli pamoja na Ruthu alimsihi arudi pamoja naye. Katika Israeli walirudi kwa ndugu yao Boazi ili awasaidie na Ruthu aliolewa na Boazi.

Kama dhahabu ing'aayo Ruthu alionekana kung'aa katika siku za giza nene za kitabu cha Waamuzi. Ruthu ni kitabu cha uaminifu,utakatifu,na upendo katika siku za vurugu na shida. Ubinafsi na ukengeufu ndio ulikuwa unatawala siku hizo. Hivyo katika kitabu hiki Ruthu anatupa picha ya imani na utii katika matatizo na anaonyesha ni kwa jinsi gani imani yaweza kuleta baraka . Ruthu anatumika kama mtumishi mwaminifu kwa mfalme Daudi na kama ilivyokwisha kusemwa hapo juu kuwa yeye anamwakilisha Yesu. Kusudi jingine la Ruthu linaonesha ukweli katika ukombozi wa *kinsmani*, uwepo wa mabaki ya watakatifu hata katika zile nyakati za shida na uaminifu wa Mungu kwa wale wanaomtegemea na kutembea naye kwa imani. Kwa kuwa Ruthu alikuwa mtakatifu, kitabu kinaonesha shauku ya Mungu ya kuuleta ulimwengu katika familia yake.

Inaweza kushangaza kuwa kwa yeyote yule anayemtumaini Mungu kwa hakika ni Moabu. Uaminifu wake katika familia ya Israeli ambako aliolewa (Ruthu) na kuomba kwake huko kwa wakweze inamthibitishia kuwa mtoto halisi wa Israeli na Mtumishi mwema wa Daudi mfalme. Anatoa mfano halisi katika ufalme ujao wa Mungu kuwa hii haitafanyika tu kwa sababu ya kuzaliwa au kwa sababu ya damu, hapana, ila ni kwa sababu ya kukiri katika

mapenzi ya Mungu kwa njia ya kutii kwa imani (Warumi 1:5).Na sehemu yake katika ukoo wa Daudi inaonyesha kuwa mataifa yote yatamilikishwa katika ukoo wa Mwana wa Daudi.[5]

**Watu Muhimu:** Ruthu, Naomi, Boazi

**Mwonekano wa Yesu Katika Kitabu cha Ruthu:** Katika Agano la Kale ikiwa mtu au nchi itakuwa katika hali ya kufungwa basi ingelikombolewa ikiwa mahitaji fulani yangeliweza kufikishwa kwa mkombozi wao Kinsmani. Mkombozi huyu katika lugha ya kiebrania anajulikana kama Goel ikiwa na maana "ndugu wa karibu" na hii tayari ni alama inayomwakilisha Yesu.

GOEL ni lazima awe ndugu wa damu (kinsman) kwa wale aliokuwa akiwaokoa (Kumb 25:5, 7-10; Yohana 1:14; Warumi 1:3; Wafilipi 2:5-8; Waebrania 2:14-15), alikuwa tayari kulipa gharama za kuwaokoa kabisa (2:1 linganisha 1 Petro 1:18-19), kuwa radhi kukomboa au kumlipa mfalme (3:11 linganisha Mathayo 20:28; Yohana 10:15, 19; Waebrania 10:7), kwa kweli alikuwa huru kabisa, kama vile Yesu alivyo huru kulipa dhambi zetu wakati yeye hana dhambi (2 Wakorintho 5:21; 1 Petro 2:22; 1 Yohana 3:5).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Ushupavu na Kurudi kwa Ruthu (1:1-22)**
   1:1-5 1:6-18 1:9-22

2. **Haki za Ruthu (2:1-23)**
   2:1-3 2:4-17 2:17-23

3. **Ombi la Ruthu (3:1-18)**
   3:1-4 3:5-9 3:10-18

4. **Zawadi ya Ruthu (4:1-22)** 4:1-12
   4:13-17 4:18-22

# 1 Samweli

### (Tafsiri toka Waamuzi hadi Wafalme)

**Mtunzi na Waandishi wa Kitabu:** Kwa hakika hatuna uhakika nani aliandika kitabu cha Samweli wa 1 na 2. Lakini kitabu cha kiyahudi cha Talmudic kinasema kiliandikwa na Samweli,hata hivyo 1 na 2 Samweli zilipata jina lake toka kwa nabii Samweli. Nabii Samweli asingeliweza kuandika zaidi ya Samweli wa 1 kwa sababu kifo chake kinaonekana katika sura ya 25. Katika 1 Samweli wa sura ya 10:25 tunaambiwa kwamba Samweli ndiye aliyeandika kitabu hiki na hata katika 1 Nyakati 29:29 inaonesha kuwa Nathani pamoja na Gadi waliandika matukio yaliyo katika kitabu cha Samweli.

Kwa kawaida kitabu cha Samweli wa 1 na 2 viliwekwa pamoja kama kitabu kimoja katika kitabu cha Kiyahudi. Vitabu hivi viwili vinatupa historia ya ufalme wa Israeli katika kipindi cha mwanzo kabisa cha utawala wa kifame. Hata hivyo 1Samweli inaeleza habari za mfalme Sauli na 2 Samweli inaeleza habari za mfalme Daudi.

Japokuwa kitabu hiki asili yake kilikuwa ni kitabu kimoja katika kitabu cha kiyahudi, lakini ilibidi kigawanywe katika vitabu viwili na mkarimani wake wa Septuagint (hii ni tafasiri ya kiyunani katika Agano la Kale). Mgawanyo huu baadaye ulifuatiwa na Yerome kwa kilatini ni Vulgate (tafasiri ya Biblia kwa Lilatini) na hata katika tafasiri zingine.

**Muda wa Kuandikwa: 1010 K.K.** na baadaye

**Nia na Makusudi:** Kwa kuanza na kuzaliwa kwa Samweli na hata katika kufundishwa kwake hekaluni 1Samweli inaeleza jinsi gani mtu huyu mkuu wa Mungu aliiongoza Israeli kama nabii,kuhani na Mwamuzi wa mwisho. Wakati wa uongozi wa Samweli watu wa Israeli walitaka wawe kama mataifa kabisa na wawe na mfalme wao. Chini ya uongozi wa Mungu Samweli alimpaka mafuta Sauli kuwa mfalme wa kwanza wa Israeli. Lakini Sauli aliondolewa na Mungu kwa sababu ya kutotii kwake. Na kwa uongozi wa Mungu tena Samweli alimpaka mafuta Daudi kuwa mtawala . Na sehemu ya kitabu iliyobaki inaeleza jitihada zilizokuwepo za wivu wa Sauli na Mungu wa Daudi.

1 Samweli inaendelea kueleza pia hisitoria ya Israeli ambapo Waamuzi walimuacha na Samweli wakamfuata Samsoni (Waamuzi 16:31). Kwa hiyo tunaona uongozi mzima katika taifa tangu Waamuzi hadi Wafalme. Kipindi cha waamuzi watu wa Israeli hawakumruhusu Yahwe atawale maisha yao isipokuwa kila mtu alifanya kile

kilichopendezesha macho yake (Waamuzi 17:6; 21:25). Mfame aliimarisha misimamo yake sana kwa sababu watu walikuwa wakimwabudu Mungu wao wa duniani. Mungu alimwambia Samweli ***"isikilize sauti ya watu hawa katika kila neno watakalokuambia kwa maana hawakukukataa wewe bali wamenikataa mimi ili nisiwe mfame juu yao***" (8:7).

Mungu alikuwa amekusudia kuwapa Israeli Mfalme (Mwanzo 49:10; Kumb 17:14-20). Lakini badala ya kusubiri Mungu awape, wakaamua kufanya ya kwao ili kupata mfalme waliyemtaka wao. Sauli aliondolewa na Mungu mwenyewe kwa sababu alishindwa kutii ile kweli ***"kutii ni bora kuliko dhabihu"*** (15:22) akawa kama kichaa mwenye wivu,mpumbavu na mwasherati. Daudi anaonyesha kanuni ya kuwa **"*Bwana haangalii kama mwanadamu aangaliavyo*"** (16:7). Mungu alimthamini Daudi kwa sababu ya utii wake, hekima na kumtegemea Mungu.[6]

Kihistoria kusudi kuu la 1 Samweli ni kuonyesha asili ya ibada kipindi cha utawala wa Daudi.

**Watu Muhimu:** Nabii Samweli, Sauli mtawala mwenye kiburi na Daudi Mchungaji

**Mwonekano wa Yesu katika Kitabu cha 1 Samweli:** Samweli anatengeneza mwijilio mzuri wa Yesu kwa kuwa yeye alikuwa ni nabii, kuhani, japo hakuwa mfalme, ila alikuwa ni mwamuzi ambaye Mungu alimtumia kuanzisha kizazi kipya ambacho wafalme walianza kutawala.

Masihi ni mpakwa mafuta na Samweli ni kitabu cha kwanza ambacho kinatumia neno mpakwa mafuta (2:10) na maelezo mazuri kabisa ya masihi yanaonekana katika maisha ya Daudi. Alizaliwa Bethlehemu akafanya kazi kama mchungaji. Alikuwa pia mtawala wa Israeli na akawa katika kizazi kabisa cha Yesu Kristo mfalme kupitia utawala wa Daudi. Katika Agano Jipya Yesu anaelezwa kama **"*aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa sababu ya Mwili*"** (Warumi 1:3).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Samweli, Mwamuzi wa Mwisho (1:1–8:22)**
   a. Wito wa Samweli (1:1–3:21)
      1:1-18 — 2:12-17 — 3:1-21
      1:19-28 — 2:18-21
      2:1-11 — 2:22-36
   b. Utume wa Samweli (4:1–7:17)
      4:1-22 — 6:1-21
      5:1-12 — 7:1-17
   c. Jukumu la Samweli (8:1-22)
      8:1-9 — 8:10-22

2. **Sauli, Mfalme wa Kwanza (9:1–15:35)**
   a. Kuchaguliwa kwa Sauli (9:1–12:25)
      9:1-14 — 10:17-27 — 12:12-25
      9:15-27 — 11:1-15
      10:1-16 — 12:1-11
   b. Kukataliwa kwa Sauli (13:1–15:35)
      13:1-23 — 14:24-46 — 15:1-9
      14:1-23 — 14:47-52 — 15:10-35

3. **Daudi, Mfalme Aliyefuatia (16:1–31:13)**
   a. Daudi, Mchunga Kondoo, Ateuliwa na Anapakwa Mafuta (16:1-23)
      16:1-11 — 16:12-23
   b. Daudi, Muuaji Mkubwa, Ashutumiwa katika Mahakama ya Sauli (17:1-58)
      17:1-19 — 17:20-30 — 17:31-58
   c. Daudi, Rafiki wa Yonathani Lakini Akataliwa na Sauli (18:1–19:24)
      18:1-9 — 18:20-30
      18:10-19 — 19:1-24

4. **Daudi, Mkimbizi, kwa Ajili ya Sauli (20:1–26:25)**
   a. Daudi Alindwa na Yonathani (20:1-42)
      20:1-29 — 20:30-42
   b. Daudi Alindwa na abimeleki (21:1-9)
   c. Daudi Alindwa na Akishi (21:10-15)

d. Daudi na Kundi Lake la Waimbaji (22:1–26:25)

| | | |
|---|---|---|
| 22:1-23 | 24:1-22 | 25:18-38 |
| 23:1-14 | 25:1 | 25:39-44 |
| 23:15-29 | 25:2-17 | 26:1-25 |

5. **Kukataliwa kwa Daudi katika Nchi ya Wafilisti (27:1–31:13)**
   a. Daudi Awa Mtumishi wa Wafilisti (27:1–28:2)
   b. Sauli Awasiliana na En-Dor (28:3-25)
   c. Daudi Aondolewa na Wafilisti (29:1-11)
   d. Daudi Awaangamiza Wamaaleki (30:1-31)
   e. Wafilisti na Kifo cha Sauli (31:1-13)

# 2 Samweli

## (Utawala wa Daudi – Kupanuka kwa Taifa)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Japo 1 na 2 Samweli kilikuwa kitabu kimoja lakini kiligawanywa mara mbili, rejea hapo nyuma kwa mtunzi wa kitabu.

**Muda wa Kuandikwa: 1010 K.K.** (na baadaye)

**Nia na Makusudi:** Bila makusudi yoyote ya kuharibu historia ya ufalme wa Waisraeli 2 Samweli anaendelea kueleza juu ya kuanzishwa kwa ufalme wa Waisraeli na hata mwanzo wa kifo cha Sauli na inaendelea na utawala wa Daudi. Na hii imechanganuliwa tangu miaka ya 40 ya utawala wa Daudi (5:4-5) na inaendeleza utawala huu kupitia ushindi na majonzi ya masikitiko yanayojumuisha dhambi zake, uuaji na hata matatizo katika jamaa yake na hata taifa. Kusudi katika 2 Samweli inaonesha utawala wake Daudi, na hii inaweza kufupishwa "***kwa kiasi gani dhambi inabadili furaha hata mafanikio kuwa shida na huzuni"*** Taifa lilisimama chini ya Sauli na kupanuka wakati wa Daudi. Utawala wa Sauli uliimarisha Israeli tangu wakati wa Waamuzi lakini utawala wa Daudi ulileta kupanuka kwa taifa hili na hata kukua zaidi. Kwa hiyo tunaweza kusema kuwa hii inatueleza kabisa kibiblia jinsi gani utawala wake ulikuwa, 2 Samweli inaonesha uzuri na ubaya wa mfalme Daudi.

**Watu Muhimu:** Daudi, Bathsheba, Nathani, Absalomu, Yoabu, Amnoni, na Ahithopheli.

**Mwonekano wa Yesu katika 2 Samweli:** Bila dhambi Daudi angelikuwa ni picha halisi ya Yesu kama mtawala wa Israeli na katika kitabu hiki Mungu alianzisha agano lake na Daudi ambalo kweli linaenda kumwonyesha Kristo.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Ushindi wa Daudi (1–10)**
   a. Kuvishwa taji (1:1–5:5)

| | | |
|---|---|---|
| 1:1-16 | 2:12-32 | 3:31-39 |
| 1:17-27 | 3:1-5 | 4:1-12 |
| 2:1-7 | 3:6-25 | 5:1-5 |
| 2:8-11 | 3:26-30 | |

   b. Kuimarishwa kwa Ufalme (5:6–6:23)

| | | |
|---|---|---|
| 5:6-25 | 6:1-11 | 6:12-23 |

   c. Agano Kuhusu Ufalme (7:1-29)

| | | |
|---|---|---|
| 7:1-7 | 7:8-17 | 7:18-29 |

   d. Utawala wa Mfalme (8:1–10:19)

| | | |
|---|---|---|
| 8:1-18 | 9:1-13 | 10:1-19 |

2. **Kuhamishwa kwa Mfalme (11:1-27)**
   a. Uzinzi wa Mfalme (11:1-13)
   b. Mauaji Yaliyosababishwa na Mfalme (11:14-27)

3. **Tabu za Mfalme (12:1–24:25)**
   a. Shida za Nyumbani (12:1–13:36)

| | | |
|---|---|---|
| 12:1-14 | 12:24-25 | 13:1-23 |
| 12:15-23 | 12:26-31 | 13:24-36 |

b. Tabu katika Ufalme (13:37–24:25)

| | | |
|---|---|---|
| 13:37-39 | 17:1-14 | 20:13-26 |
| 14:1-20 | 17:15-29 | 21:1-22 |
| 14:21-33 | 18:1-18 | 22:1-51 |
| 15:1-12 | 18:19-33 | 23:1-7 |
| 15:13-37 | 19:1-7 | 23:8-39 |
| 16:1-4 | 19:8-43 | 24:1-14 |
| 16:5-14 | 20:1-9 | 24:15-17 |
| 16:15-23 | 20:10-12 | 24:18-25 |

# 1 Wafalme

## (Kifo cha Daudi–Kuvunjika kwa Utawala)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Mtunzi wa kitabu hiki hajulikani japo wayahudi hudhani kuwa ni Yeremia kama anavyosema Dr. Charles Ryrie :

> Hata hivyo mwandishi wa kitabu hiki alitumia kumbukumbu za kihistoria (11:41; 14:19, 29). Na inavyoonekana alikuwa akiishi uhamishoni Babeli lakini hajulikani yamkini kuwa ni Ezra, Ezekia au Yeremia (ingawa mtu awae yote anaweza kuwa ameandika sura za mwisho za 2 Wafalme wakati Yeremia alipokufa huko Misri na si Babeli; Yeremia 43:6-7).[7]

1 na 2 Wafalme kwa asili yake ni kitabu kimoja kama vile Samweli na hata Nyakati na kwa haraka haraka kiliitwa Wafalme kwa Kiyahudi (Melechim). Viliitwa hivyo tangu historia ya Wafalme wa Israeli na Yuda tangu zama za Sulemani na hata kuelekea kwa mateka wa Babeli. Na 1 Wafalme inaishia kwa kueleza mwanzo wa utawala wa Mfalme Ahazia 853 K.K.

**Muda wa Kuandikwa:** Ni kama **550 K.K.** Kuachiliwa kwa Yehoakimu toka gerezani ilichukuliwa katika 2 Wafalme kama tukio la mwisho. Na hii ilifanyika miaka ya 37th kufungwa kwake (560 K.K.). Kwa hiyo 1 na 2 Wafalme yamkini ilikuwa bado haijaandikwa kabla ya tukio hilo. Inaonekana kabisa kuwa kurudi kwa mateka toka Babeli miaka ya 516 K.K tayari 1 na 2 Wafalme zilikuwa zimeandikwa. Na hata mtunzi na mwandishi alikuwa anahusiana nao na sasa 1 na 2 Wafalme zilikamilika kabisa kati ya miaka 560 na 516 K.K.[8]

**Nia na Makusudi:** Baada ya kifo cha Daudi sura ile ya 1-2, mtoto wake Sulemani alishika kuwa Mfalme. Sura ya 1-11 zinaeleza maisha na utawala wa Sulemani ikijumuisha Waisraeli walivyoweza kufaulu kwenda katika kilele cha utukufu na hata kusambaa kwa ufalme, ujenzi wa hekalu na huko Yerusalemnu. Na baadaye Sulemani alimwacha Bwana kwa sababu ya wake zake wapagani ambao walimchanganya na kumharibu kabisa akageuka na kuacha kumwabudu Mungu wake katika hekalu.

Moyo wa mfalme uligawanyika na hata aliacha ufalme uliogawanyika. Kwa karne zilizofuata kitabu cha 1 Wafalme kinaeleza habari za kufanana za watawala wawili na mataifa mawili ya watu wakaidi ambao kwa kweli walikuwa wakiendelea vibaya katika unabii wa Mungu na hata sheria zake.[9]

Mfalme aliyefuata alikuwa Rehoboam, ambaye alipoteza utawala wa kaskazini. Baadaye tu utawala wa kaskazini ambao ulikuwa na kabila 10 ulijulikana kama Israeli, ufalme wa kusini, uliojumuisha kabila ya Yuda na Benjamini na uliitwa Yuda. Na katika sura ya mwisho ya 1 Wafalme mtazamo uko katika maovu tu ya mfalme Ahabu na mwenye haki Eliya ambaye alimhukumu Ahabu na hata Israeli kwa kutotii kwao.

Kusudi la kati ni kwamba kutotii kunaleta madhara katika kuangushwa kwa ufalme. Hivyo haki ya taifa inategemea haki ya kiongozi wake na hata watu wake kupitia agano la waisraeli. Mfalme wa kwanza hatupi tu historia ya mlolongo wa wafalme ila pia inaeleza mafanikio ya kila Mfalme alivyo fanikiwa na hata taifa kwa ujumla kwa kutegemea hekima ya kila utawala uliokuwa ukiingia kwa kuangalia hekima ya Mungu na sheria yake. Methali 14:34 insema ***"Haki huinua taifa lakini dhambi ni aibu ya watu wowote."*** Kutokuwa waaminifu mbele za Mungu kulipelekea kuangushwa na kuwa mateka.

**Watu Muhimu:** Sulemani, Yeroboam, Rehoboam, Eliya and Elisha, Ahabu na Yezebeli

**Mwonekano wa Yesu katika 1 Walfame:** Kama Daudi, Sulemani ni mmoja wa watawala wanaomwakilisha Yesu katika Agano la Kale na anaashiria utawala wa Yesu wa baadaye duniani. Sulemani alifanya hii kwa utukufu, kujiamini na hata heshima na hii inamwakilisha Yesu kabisa.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Muunganikano wa Falme: Miaka Arobaini ya Utawala wa Sulemani (1:1–11:43)**
   a. Umaarufu wa Sulemani (1:1–2:46)
      1:1-10 2:1-9 2:28-35
      1:11-37 2:10-18 2:36-46
      1:38-53 2:19-27
   b. Hekima za Sulemani (3:2–4:34 )
      3:1-5 3:10-15 4:1-19
      3:6-9 3:16-28 4:20-34
   c. Hekalu la Sulemani (5:1–8:66)
      5:1-12 7:13-51 8:54-61
      5:13-18 8:1-11 8:62-66
      6:1-38 8:12-21
      7:1-12 8:22-53
   d. Umaarufu wa Sulemani (9:1–10:29)
      9:1-9 10:1-13
      9:10-28 10:14-29
   e. Kuanguka kwa Sulemani (11:1-43)
      11:1-13 11:14-40 11:41-43

2. **Kugawanyika kwa Ufalme: Miaka Minane ya Mwanzo ya Falme Mbili (12:1–22:53)**
   a. Sababu ya kugawanyika (12:1-24)
      12:1-15 12:16-24
   b. Kutawala kwa Yeroboamu katika **Israeli** (12:25–14:20)
      12:25-33 13:11-34
      13:1-10 14:1-20
   c. Kutawala kwa Rehoboamu katika **Yuda** (14:21-31)
   d. Kutawala kwa Abiya katika **Yuda** (15:1-8)
   e. Kutawala kwa Asa ktika **Yuda** (15:9-24)
   f. Utawala wa Nadabu katika **Israeli** (15:25-31)
   g. Utawala wa Baasha katika **Israeli** (15:32–16:7)
   h. Utawala wa Ela katika **Israeli** (16:8-14)
   i. Utawala wa Zimri katika **Israeli** (16:15-20)
   j. Utawala wa Omri katika **Isreli** (16:21-28)
   k. Utawala wa Ahabu katika **Israeli** (16:29–22:40)
      16:29-34 19:1-8 21:11-29
      17:1-16 19:9-21 22:1-12
      17:17-24 20:1-12 22:13-28
      18:1-19 20:13-25 22:29-40
      18:20-35 20:26-43
      18:36-46 21:1-10
   l. Utawala wa Yehoshafati katika **Yuda** (22:41-50)
   m. Utawala wa Ahazia katika **Israeli** (22:51-53)

# 2 Wafalme

## (Kutawanyika – Dhambi za Kujitakia Zina Majuto)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Hata 1 na 2 kilikuwa kitabu kimoja tu lakini kiligawanywa, tazama huko nyuma.

**Muda wa Kuandikwa:** Kati ya **550 K.K.** Rejea katika 1 Wafalme.

**Kusudi na Nia:** 2 Wafalme inaendeleza historia ya Eliya na aliyefuata baada yake, Elisha. Lakini pia kinaendeleza yale yanayofaa. Historia ya falme mbili kwa kinaganaga: ule falme wa kaskazini, Israeli na ule wa Kusini yaani Yuda na hadi kutawaliwa na kufanywa mateka. Israeli iliangukia kwa Assyria mwaka 722 K.K. na Yuda mikononi mwa Wababeli mwaka 586 K.K. na katika falme zote hizi unabii uliendelea kuwaonya kuwa Mungu atawaadhibu wasipogeuka na kutubu.

2 Wafalme inatuambia dhambi za kujitakia zina madhara yake katika taifa. Katika 1 Wafalme imegawanywa na 2 Wafalme imeachwa. Baada ya miaka mingi ya kukiri katika makosa yao na kujuta Mungu alighairi na kuwapa kama alivyokuwa amewaahidi. Na kwa sababu vitabu hivi vilikuwa pamoja hivyo vina kama kusudi moja tu. Vinatufundisha madhara ya kutotii amri ya Mungu kuwa hupelekea Mungu kuacha kusikiliza na kutimiza ahadi

zake kwetu . Falme hizi mbili zilianguka kwa kutofanya yale Mungu anataka zifanye. Watawala walitawala bila haki na kweli ya Mungu.

**Watu Muhimu:** Eliya , Elisha, Yosia, Naamani, Hezekia

**Mwonekano wa Yesu katika 2 Wafalme:** Eliya anamwakilisha Yesu na Yohana Mbatizaji (Mathayo 11:14; 17:10-12; Luka 1:17). Elisha katika mambo mengi anatukumbusha juu ya Yesu katika Huduma Yake. Irving L. Jensen alizilinganisha kazi zao katika tathimini hizi:

> Eliya anakaririwa kwa matendo makubwa ya hadharani wakati Elisha anatofautishwa naye kwa Kufanya miujiza mikubwa ambayo watu waliihitaji. Huduma ya Eliya inaeleza sheria ya Mungu ,hukumu, na ghadhabu . Elisha yeye ni juu ya neema upendo na unyenyekevu. Eliya alikuwa kama Yohana Mbatizaji akihubiri habari za toba juu ya dhambi, hivyo Elisha alifanya kama Yesu kwa wema na upole huku akifanya miujiza na akieleza kuwa maneno ya unabii yalitoka kwa Mungu.[10]

Tazama kwa makini Ryrie anatueleza vizuri katika 1 na 2 Wafalme.[11] Mifano hii inaonyesha kinaganaga kabisa ukweli wa kutotii na mwisho wake.

| Tofauti za Wafalme wa I & 2 | |
|---|---|
| **1 Wafalme** | **2 Wafalme** |
| Tuanze na Mfalme Daudi | Walimaliza na babeli |
| Inafunguliwa na utukufu wa Sulemani | Wanamaliza na aibu ya Johakimu |
| Baraka za kutii | Laana ya kutotii |
| Ujenzi wa hekalu | Kuungua kwa hekalu |
| Dalili za uasi | Matatizao ya uasi |
| Inaonesha jinsi mfalme alivyoshindwa kuwatawala watu wa Mungu | Madhara ya kushindwa |
| Inamtambulisha nabii Eliya | Inamtambulisha Eliya |
| Inafafanua huruma ya Mungu | Inathibitisha hasira ya Mungu juu ya dhambi |

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Falme Zilizogawanyika (1:1–17:41)**
    a. Utawala wa Ahazia katika **Israeli** (1:1-18 )
    b. Utawala wa Yehoramu (Yoramu) katika **Israeli** (2:1–8:15)
        1) Tafasiri ya Eliya (2:1-14)
        2) Mwanzo wa Huduma ya Elisha (2:15-25)
        3) Matumaini ya Yehoramu dhidi ya Moabu (3:1-27)
        4) Huuma ya Elisha (4:1–8:15)
            4:1-7 5:15-27 7:3-14
            4:8-17 6:1-7 7:15-20
            4:18-37 6:8-23 8:1-6
            4:38-44 6:24-33 8:7-15
            5:1-14 7:1-2
    c. Utawala wa Yoramu katika **Yuda** (8:16-24)
    d. Utawala wa Ahazia katika **Yuda** (8:25-29)
    e. Utawala wa Yehu katika **Israeli** (9:1–10:36)
        9:1-13 9:33-37 10:34-36
        9:14-26 10:1-17
        9:27-32 10:18-33
    f. Utawala wa Malkia Athalia katika **Yuda** (11:1-16)
    g. Utawala wa Yehoashi (Yoashi) katika **Yuda** (11:17–12:21)
        11:17-20 12:4-18
        11:21-12:3 12:19-21
    h. Utawala wa Yehoazi katika **Israeli** (13:1-9)
    i. Utawala wa Yehoashi katika **Israeli** (13:10-25)
    j. Utawala wa Amazia katika **Yuda** (14:1-22)
    k. Utawala wa Yeroboamu katika **Israeli** (14:23-29)
    l. Utawala wa Azalia (Uzia) katika **Yuda** (15:1-7)
    m. Utawala wa Zekalia ktika **Israeli** (15:8-12)
    n. Utawala wa Shalumu katika **Israeli** (15:13-15)

o. Utawala wa Menahemu katika **Israeli** (15:16-22)
p. Utawala wa Pekahia katika **Israeli** (15:23-26)
q. Utawala wa Peka katika **Israeli** (15:27-31)
r. Utawala wa Yothamu katika **Yuda** (15:32-38)
s. Utawala wa Ahazi katika **Yuda** (16:1-20)
t. Utawala wa Hoshea katika **Israeli** (17:1-41)
    1) Kushindwa kwa Waisraeli (17:1-6 )
    2) Dhambi za Israeli (17:7-23)
    3) Kutawanyika kwa Waisreli (17:24-41)

**2. Kudumu kwa Ufalme wa Yuda (18:1–25:30)**

a. Kutawala kwa Hezekia (18:1–20:21)

| | | |
|---|---|---|
| 18:1-6 | 19:1-7 | 19:20-37 |
| 18:7-12 | 19:8-13 | 20:1-11 |
| 18:13-37 | 19:14-19 | 20:12-21 |

b. Utawala wa Manase (21:1-18)
c. Utawala wa Amon (21:19-26)
d. Utawala wa Yosia (22:1–23:30)
e. Utawala wa Yehoahazi (23:31-33)
f. Utawala wa Yehoakimu (23:34–24:7)
g. Utawala wa Yehoakini (24:8-16)
h. Utawala wa Sedekia (24:17–25:21)
    1) Kuasi dhidi ya Babeli na Kuharibiwa kwa Hekalu (24:17–25:10)
    2) Kupelekwa Babeli Mara ya Tatu (25:11-21)
i. Ugavana wa Gedalia Gavana wa Madhabahuni (25:22-26)
j. Kuachiliwa kwa Yehoakimu katika Babeli (25:27-30)

# 1 Mambo ya Nyakati

## (Maandalizi ya Ujenzi wa Hekalu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Nyakati kwa kawaida kilikuwa ni kitabu kimoja kabisa na hakionyeshi mwandishi wake,lakini kwa mila za kiyahudi zinaonyesha kuwa alikiandika Ezra. Uandishi wa kitabu hiki uko katika namna ya kuhusika kwa mambo fulani fulani mengi yalihusika katika kukamilisha uandishi wa kitabu hiki na mwandishi mmoja alionyesha zao la mwisho katika kitabu. Mambo hayo pia yanajumuisha kama vile taarifa za Manabii katika Samwel (1 Nyakati 29:29). Isaya (2 Nyakati 32:32), na wengine wengi (2 Nyakati 9:29; 12:15; 20:34; 33:19); lakini matokeo ya haya yote yaliitwa " Kitabu cha wafalme wa Yuda na Israeli" (2 Nyakati 16:11; 25:26). Kitabu hiki kinaonesha kuwa ni cha ukuhani kwa sababu ya mtazamo wake wa Hekalu,ukuhani, ukoo wa Daudi na hata ufalme wa Yuda. Kwa hiyo hata uandishi wake kuwa ni Ezra alifanya yawezekana, hasa tunapoangalia katika nyaraka zake Ezra na hata Nyakati yenyewe kwa kuangalia uanzishwaji na ukamilishwaji wa hekalu.

Japo kitabu hiki kinachukua habari yote ya Wayahudi lakini mtazamo ni tofauti. Japo kinafanana fanana (1 na 2 Nyakati) lakini hakijirudii isipokuwa ni juu tu ya habari za kiroho juu ya Waisraeli. Kitabu cha Wafalme kinaeleza mtazamo wa watu, lakini Nyakati kinaeleza mtazamo wa Mungu.

Kwa kweli kilikuwa ni kitabu kimoja chenye 2 Nyakati hadi 180 K.K. kitabu cha wayahudi kilisomeka kama Kitabu cha nyakati ikiwa na maana ya historia ya Waisraeli tangu Adamu hadi Utumwani Babeli na amri ya Siria ya kuwaruhusu Wayahudi kurudi. Kwa maana kabisa ni mfano wa Agano la Kale.[12]

Wakati wa kuvumbuliwa kwa Septuagint, watafasiri walikigawa katika sehemu mbili. Katika nyakati hizo kiliitwa "Vitu Vilivyo Rukwa" wakiwa na maana ya yale yaliyorukwa tangu Samweli hadi Wafalme. Nyakati ni matokeo ya Biblia ya kilatini aliyoiandika Jerome (385-405 B.K.) akiwa na maana "Ya Nyakati za Kihistoria Zilizoachwa."[13]

**Muda wa Kuandikwa: 450-425 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Kitabu cha Nyakati kimeanza na historia ya Adamu hadi kifo cha Sauli. Na sehemu iliyobaki ni juu ya utawala wa Daudi. Na kitabu hiki kinaonekana kama ni marudio ya Samweli na Wafalme, lakini kimeandikwa kipindi cha kurudi kwa waliokuwa uhamishoni kuwakumbusha kuwa walirudi kwa sababu ya ukoo wa Daudi na kuwa Mungu aliwachagua. Na zaidi ya hapo ni kwamba ni ahadi ya Daudi aliyopewa kwamba kulikuwa na sababu kwa wale wote waliokuwa katika ahadi ya Ibrahimu kuwa yeye atamfanya kuwa baba wa taifa kubwa. Na kusudi kuu ni kwamba Mungu ni mwaminifu katika kutimiza ahadi zake.

Nyakati inafafanua sheria pia, ukuhani na hata juu ya hekalu. Japo hekalu la Sulemani halikuwepo lakini hekalu jingine lingelikuwepo kama kumbukumbu ya lile la kwanza. Kitabu hiki kinatueleza kuwa yaliyopita yalikuwa mambo ya yaliyopo, uasi kuabudu miungu, ndoa za mitaala, kukosa umoja ndiyo ilikuwa sababu ya wao kutawaliwa. Na hii inaonesha kabisa kuwa Israeli hawakurudia kuabudu miungu yao ya kigeni.[14]

**Watu Muhimu:** Kama ilivyotajwa kuwa ni kitabu kuhusu Daudi japo wengine waliokuwa wakionekana katika 1 Samweli ni muhimu kama Nathani, Bathsheba na Uria.

**Mwonekano wa Yesu katika 1 Nyakati:** Kama ilivyosemwa katika 1 na 2 Samweli Daudi anamwakilisha Yesu hivyo na hapa ni mfano wa Yesu.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Ukoo Tangu Adamu hadi Daudi (1:1–9:44)**
   a. Adamu hadi Abrahimu (1:1-27)
   b. Abraham hadi Yakobo (1:28-54)
   c. Yakobo hadi Daudi (2:1-55)
   d. Daudi hadi Kwenye Mateka (3:1-24)
   e. Ukoo wa Makabila Kumi na Mbili (4:1–8:40)

| | | |
|---|---|---|
| 4:1-23 | 7:1-5 | 7:20-29 |
| 4:24-43 | 7:6-12 | 7:30-40 |
| 5:1-26 | 7:13 | 8:1-32 |
| 6:1-81 | 7:14-19 | 8:33-40 |

   f. Wakazi wa Yerusalemu (9:1-34)
   g. Familia ya Sauli (9:35-44)

2. **Kuinuliwa na Kupakwa Mafuta kwa Daudi (10:1–12:40)**
   a. Kifo cha Sauli (10:1-14)
   b. Kufahamika kwa Daudi (11:1-3)
   c. Kukamatwa kwa Yerusalemu (11:4-9)
   d. Ushujaa wa Daudi (11:10–12:40)

3. **Utawala wa Daudi (13:1–29:21)**
   a. Daudi na Sanduku la Agano (13:1–17:27)
      1) Daudi Aleta Sanduku la Agano kwa Kidoni, Kifo cha Uza (13:1-14)
      2) Kufahamika kwa Audi na Ushindi Wake dhidi ya Wafilisti (14:1-17)
      3) Daudi Alileta Sanduku Yerusalemu (15:1-29)
      4) Sherehe za Daudi na Mipangilio Kuhusu Sanduku la Agano (16:1-43)
      5) Shauku ya Daudi Kulijenga Hekalu. Agano la Daudi (17:1-27)
   b. Vitavya Daudi (18:1–20:8)

| | |
|---|---|
| 18:1-17 | 19:10-19 |
| 19:1-9 | 20:1-8 |

   c. Hesabu ya Dhambi za Dausi (21:1-30)
   d. Maandalizi ya Daudi Kuhusu Kujenga Hekalu (22:1–23:1)
   e. Mpango wa Daudi Kuhusu Walawi (23:2–26:32)
      1) Hesabu na Majukumu ya Walawi (23:2-32)
      2) Kuwagawa Walawi katika Makundi Ishirini na Nne (24:1-31)
      3) Majukumu ya Waimbaji (25:1-31)
      4) Kuweka Walinzi wa Geti (26:1-19)
      5) Kuweka Watunza Hazina (26:20-28)
      6) Weak Viongozi (26:29-32)
   f. Watumishi wa Daudi (27:1-34)
   g. Maelekezo ya Mwisho ya Daudi kwa Watu na Sulemani (28:1-21)
   h. Sadaka za Daudi na Ibada (29:1-21)

4. **Umaarufu wa Sulemani na Kifo cha Daudi (29:22-30)**

# 2 Mambo ya Nyakati

**(Kuharibiwa kwa Hekalu)**

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama ilivyotajwa hapo juu 1 na 2 vilikuwa ni kitabu kimoja. Kama vile ambavyo 1 Nyakati haikutaja ni nani aliyeandika kitabu hicho isipokuwa ni tamaduni za kiyahudi zinazoeleza kuwa

mwandishi ni Ezra na hata mfumo wa uandikwaji wake unasadikika ni wa mtu fulani lakini waandishi labda tuseme ni Wakati wenyewe. Katika kumtetea Ezra kama mwandishi kunamambo mengi yanayomgusa kama vile wayunani, na hata hekalu. Kwa yeyote aliyeandika alikuwa na mambo mengi kabisa kama vyanzo vya kumsaidia katika uandishi kama vile:

1. Kitabu cha Wafame wa Israeli na Yuda (27:7; 35:27; 36:8)
2. Kitabu cha Wafalme wa Israeli na Yuda (16:11; 25:26; 28:26; 32:32)
3. kitabu cha Wafalme wa Israeli (20:34; 33:18)
4. Kumbukumbu za Kitabu cha Wafalme (24:27)
5. Kitabu cha Nathani, unabii wa Eliya na Hata Maono ya Iddo (9:29)
6. Historia ya Shemaia (12:15)
7. Kumbukumbu za Iddo (13:22)
8. Maandiko ya kumbukumbu za Isaya (26:22)
9. Semi za Hozai (33:19)
10. Maombolezo (35:25)
11. Maandiko ya Daudi na Mwanaye Sulemani (35:4)

**Muda wa Kuandikwa: 450-425 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Kwa kuwa 1 Nyakati zinashabiana na 1 na 2 Samweli hivyo 2 Nyakati inaendeleza ukoo wa Daudi na inashabiana na 2 Wafalme. Ni vizuri kunukuu kuwa 1 Nyakati inaacha kabisa utawala wa kaskazini kwa sababu ya kutoamini kwa watu na hata kule kukosekana kabisa kwa Mungu wao ambaye alichukua maisha yao baada ya Daudi. Kwa kuitazama 2 Nyakati tunaona maisha ya wafalme waliotembea baada ya Daudi. Sura ya 1-9 inaeleza juu ya ujenzi wa hekalu wakati wa utawala wa Sulemani na sura ya 10-36 inaeleza juu ya utawala wa Yuda hadi mwisho wa kuharibiwa kwa Yerusalemu na hata uhamishoni mwa Babeli. Hivyo inatupa sehemu nzuri ya kuelewa maisha ya wafalme walioleta ufufuo na kutengeneza taifa kama Asa, Yehoshephati, Yohashi, Hezekia na Yosia.

Nyakati inamaliza historia ya Samweli na Wafalme, lakini katika mitazamo tofauti ili kuonyesha vitu fulani: Katika 1 Nyakati Daudi ni muhusika lakini 2 Nyakati ni nyumba ya Daudi. Katika Wafalme historia ya taifa inapatikana katika kiti cha enzi wakati katika Nyakati inapatikana katika Madhabahu ya hekaluni. Katika Wafalme madhabahu ni kitu muhimu kilichozungumziwa lakini katika Nyakati ni hekalu. Katika Wafalme mtazamo uko katika hali ya kisiasa wakati katika Nyakati uko katika hali ya kidini.

Nyakati ni nzuri sana katika hali ya kumbukumbu. Na hii ni komentari ya Mungu katika mambo ya kiroho katika ukoo wa Daudi. Kwa sababu ya hii mtazamo uko katika ufalme wa Yuda katika ufame wa kusini ambako kulikuwa na ufufuo na hii ndiyo ilivyopelekea kuachwa kwa ufame wa kaskazini.

**Watu Muhimu:** Yosia, Rehoboamu, Sulemani

**Mwonekano wa Yesu katika 2 Nyakati:** Kiti cha Daudi kimekwisha haribiwa lakini ukoo wake upo,mauaji na vita na hata mateka zinaashiria Masihi lakini inabaki kuwa vizuri tu kwa Adamu hadi Zerubabeli. Na Yesu tunaweza kumwona katika kizazi na ukoo wa Mathayo 1 na Luka 3.[15]

Hekalu ni mfano wa Yesu (Mathayo 12:6; Yohana 2:19; Ufunuo 21:22).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utawala wa Sulemani (1:1–9:31)**
   a. Sulemani Kuwekewa Mikono. (1:1-17)
      1:1-13 1:14-17
   b. Hekalu la Sulemani (2:1–7:22)
      2:1-10 5:1-10 7:4-7
      2:11-18 5:11-14 7:8-10
      3:1-2 6:1-11 7:11-22
      3:3-17 6:12-42
      4:1-22 7:1-3
   c. Umaarufu wa Sulemani (8:1–9:28)
      8:1-18 9:1-12 9:13-28
   d. Kifo cha Sulemani (9:29-31)

2. **Mfalme wa Yuda (10:1–36:21)**
   a. Rehoboam (10:1–12:16)
      10:1-19 11:1-13 11:14-17

| | | |
|---|---|---|
| 11:18-23 | 12:1-8 | 12:9-16 |

b. Abija (13:1-22)

| | | |
|---|---|---|
| 13:1-3 | 13:4-19 | 13:20-22 |

c. Asa (14:1–16:14)

| | | |
|---|---|---|
| 14:1-15 | 15:8-19 | 16:7-14 |
| 15:1-7 | 16:1-6 | |

d. Yehoshaphati (17:1–20:37)

| | | |
|---|---|---|
| 17:1-2 | 18:28-34 | 20:14-19 |
| 17:3-19 | 19:1-4 | 20:20-25 |
| 18:1-7 | 19:5-11 | 20:26-34 |
| 18:8-11 | 20:1-4 | 20:35-37 |
| 18:12-27 | 20:5-13 | |

e. Yehoramu (21:1-20)

f. Ahazia (22:1–23:15)

| | | |
|---|---|---|
| 22:1-4 | 22:8-12 | 23:12-15 |
| 22:5-7 | 23:1-11 | |

g. Yoashi (23:16–24:27)

| | | |
|---|---|---|
| 23:16-21 | 24:3-7 | 24:20-22 |
| 24:1-2 | 24:8-19 | 24:23-27 |

h. Amazia (25:1-28)

| | | |
|---|---|---|
| 25:1-13 | 25:14-16 | 25:17-28 |

i. Uzia (26:1-23)

| | | |
|---|---|---|
| 26:1-5 | 26:6-15 | 26:16-23 |

j. Yothamu (27:1-9)

k. Ahazi (28:1-27)

| | | |
|---|---|---|
| 28:1-4 | 28:5-15 | 28:16-27 |

l. Hezekia (29:1–32:33)

| | | |
|---|---|---|
| 29:1-4 | 30:13-27 | 32:9-19 |
| 29:5-19 | 31:1-2 | 32:20-33 |
| 29:20-36 | 31:3-21 | |
| 30:1-12 | 32:1-8 | |

m. Manasse (33:1-20)

| | | |
|---|---|---|
| 33:1-9 | 33:10-20 | |

n. Amoni (33:21-25)

o. Yosia (34:1–35:27)

| | | |
|---|---|---|
| 34:1-7 | 34:22-30 | 35:20-27 |
| 34:8-13 | 34:31-33 | |
| 34:14-21 | 35:1-19 | |

p. Yoahazi (36:1-4)

q. Yehoiakimu (36:5-8)

r. Yehoiakini (36:9-10)

s. Sedekia (36:11-21)

**3. Amri ya Koreshi (36:22-23)**

# Ezra

## (Kujengwa Upya kwa Hekalu na Kurudishwa kwa Watu)

**Mtunzi na Mwandishi wa Kitabu:** Japo kuwa kitabu cha Ezra hakitaji mwandishi wake lakini wayahudi wametoa kumbukumbu katika talmudi kuwa Ezra ni Mwandishi. Aliandika kwa kutumia nyaraka mbalimbali (4:7-16), ukoo (2:1-70), na hata notsi zake binafsi (7:27-9:15) kwa uandishi.

Ukweli ni huu Ezra ni mhusika katika kitabu hiki. Alihusika katika matukio kama inavyoelezwa katika sura 1-10 na hata sura 8-10 ya Nehemia. Kwa mambo haya yote mawili sura zimeandikwa katika mtu wa kwanza.

Maelezo yanasema kwa Ezra na Nehemia kuwa walikuwa ndio wavumbuzi wa “Sinagogi Kubwa” ikiwa na maana kusanyiko kubwa ambako vitabu vya Agano la Kale vilihifadhiwa. Na hata historia nyingine inasema kuwa alikusanya vitabu vyote katika umoja na hata akakatalia sinagogi liwe la kuabudia.[16]

Katika Biblia ya Kiebrania Ezra na Nehemia vilikuwa vitabu kimoja na kikaitwa “Kitabu cha Ezra” na hata vitabu hivi vilitengenezwa kwa mara ya kwanza kabisa kwa kiingereza,hata hivyo Yosephas (mwana historia wa Kiyahudi) na Yoramu (mwandishi wa Kilatini) hawa nao walifikiri kitabu hiki kama kimoja.

**Muda wa Kuandikwa: 457-444 K.K.**
**Nia na Makusudi:** Tangu historia Ezra aliendelea pale 2 Nyakati iliishia na akaiweka ile historia ya kurudi kwa wayahudi toka uhamishoni na kuanza kumjengea Bwana hekalu. Katika mambo ya kiroho Ezra aneleza jinsi gani alivyotimiza ahadi yake baada ya miaka 70 ya uhamishoni Babeli kama ilivyokuwa imetamkwa na manabii. Kama katika Nyakati, Ezra kama kuhani anaonyesha umuhimu wa hekalu na kuabudu katika maisha ya taifa la Mungu. Hii imeanza na agizo la Sirasi mfalme wa Peresi aliyewaruhusu watu kurudi. Watu walianza kujenga hekalu lakini walikuwa wamechelewa kwa miaka 18. Na baadaye sheria ya Dario iliwaruhusu kumaliza (Ezra 1-6). Sura 7-10 inatueleza juu ya kurudi kwa kuhani Ezra ambaye aliwafundisha watu sheria na akarejesha kabisa roho ya taifa.

Kusudi laweza kuainishwa kama ni kitabu cha kiroho, maadili na hata marejesho ya jamii ya kiyahudi ambayo ilikuwa imekengeuka.

**Watu Muhimu:** Koreshi, Ezra, Jeshua (kuhani mkuu) na Zerubabeli

**Mwonekano wa Yesu katika Ezra:** Katika kutunza ahadi ya Daudi na hata ahadi yake Mungu, Mungu aliamua kutunza ukoo huu hai kwa ajili ya Masihi, mwana wa Daudi na Ezra pamoja na Nehemia wanaonyesha ni kwa jinsi gani Mungu anaendelea kutunza ahadi yake kwa kuwarudisha watu wake katika nchi yao.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Kurejeshwa: Kurudi Yerusalemu kwa Mara ya Kwanza Chini ya Zerubabeli (1:1–6:22)**
   a. Agizo la Koreshi (1:1-11)
      1:1-4 1:5-11
   b. Sensa ya Watu (2:1-70)
      2:1-35 2:40-60
      2:36-39 2:61-70
   c. Ujenzi wa Hekalu Waanza (3:1-13)
      3:1-7 3:8-13
   d. Upinzania (4:1-24)
      4:1-7 4:8-16 4:17-24
   e. Ujenzi Warudiwa Tena (5:1–6:12)
      5:1-5 5:6-17 6:1-12
   f. Kukamilika kwa Ujenzi wa Hekalu (6:13-22)
      6:13-18 6:19-22

2. **Kuletwa kwa Watu Tena; Kurudi Chini ya Ezra (7:1–10:44)**
   a. Kurudi Yerusalemu (7:1–8:36)
      7:1-10 8:1-14 8:33-36
      7:11-26 8:15-20
      7:27-28 8:21-32
   b. Kufufuliwa kwa Yerusalemu (9:1–10:44)
      9:1-4 10:1-17
      9:5-15 10:18-44

# Nehemia

### (Ujenzi Mpya wa Mji)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Japo wengine wanaamini kuwa Nehemia ndiye aliyeandika kitabu hiki kwa sababu ya maneno yake ***"Maneno ya Nehemia mtoto wa Hakalia"*** (1:1) na watu wengine pia wanaamini kuwa Ezra naye ni mwaandishi wa kitabu hiki na alitumia notsi za Nehemia. Na wasomi wengine wanaamini kuwa mwandishi ni Nehemia kwa sababu kinabeba jina lake (1:1–7:23; 12:31–13:31).[17]

Kwa asili hiki ni kitabu kimoja, na sehemu ya kitabu hiki inachukua kabisa jina la Nehemia ambaye kwa kweli alikuwa na Ezra mwandaa divai wa mfalme wa Perisia, na Jina la Nehemia lina maana ya faraja za YAHWE.

**Muda wa Kuandikwa:** Mambo ya kihistoria ni wazi tu kwamba mwishoni mwa ukoo wa Kiebrania katika kitabu cha Ezra ndipo kilipoandikwa kati ya **445 K.K. hadi 425 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Kitabu cha Nehemia kinaendeleza historia ya Wayahudi waliorudi toka uhamishoni. Na Nehemia anaonekana katika sehemu ya mwandaa divai kwa Artaxerxes, mfalme wa Perisia, ili awe gavana wa Yerusalemu na awaongoze watu katika kujenga upya ukuta wa Mji. Nehemia na Ezra waliishi katika kipindi

kimoja (Nehemia 8:2, 9). Wote wawili walikuwa watu wa Mungu lakini wakimtuimikia YAHWE katika uwezo tofauti tofauti. Wakati Ezra akiwa kuhani na akihusishwa sana katika marejesho ya dini Nehemia alikuwa ni Mlei tu akitumika katika uwezo wa kisiasa kama gavana katika kujenga upya ukuta wa Yerusalemu.

Nehemia pia aliandikwa kuonesha dhahiri mkono wa Mungu katika kuwarudisha watu wake katika nchi yao toka uhamishoni. Wakiwa katika utawala wa Nehemia walikamilisha kwa muda wa miaka 52 ambayo ilikuwa haijafanyika kwa miaka 94 tangu kurudi kwao chini ya uongozi wa Zerubbabeli. Kwa roho ya utiifu wa imani waliweza kushinda yote yaliyokuwa kipingamizi katika maisha yao.[18]

**Watu Muhimu:** Nehemia, Artaxerxes, Sanballet, Ezra

**Mwonekano wa Yesu katika Nehemia:** Nehemia anamwakilisha Yesu kwa kuacha nafasi yake ya juu kabisa ili awalete watu mahali pao. Pia agizo la Artaxerxes linatoa alama ya Unabii wa Danieli wa majuma 70 ya miaka ambayo iliingiliwa na nyakati zisizoeleweka ambazo sasa zinaanza kurejesha kurudi kwa Masihi (Danieli 9:25-27).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Ujenzi wa Kuta Tea (1:1–7:73)**
   a. Maandalizi ya Ujenzi (1:1–2:20)

| | | |
|---|---|---|
| 1:1-11 | 2:1-10 | 2:11-20 |

   b. Kujenga Tena (3:1–7:73)

| | | |
|---|---|---|
| 3:1-32 | 5:1-13 | 6:15-18 |
| 4:1-8 | 5:14-19 | 7:1-65 |
| 4:9-23 | 6:1-14 | 7:66-73 |

2. **Kuejeshwa kwa Watu Tena (8:1–13:31)**
   a. Mkataba Mpya wa Agano (8:1–10:39)

| | | |
|---|---|---|
| 8:1-8 | 8:13-18 | 10:1-27 |
| 8:9-12 | 9:1-38 | 10:28-39 |

   b. Utii wa Watu kwa Lile Agano (11:1–13:31)

| | | |
|---|---|---|
| 11:1-19 | 12:27-30 | 13:10-14 |
| 11:20-36 | 12:31-47 | 13:15-22 |
| 12:1-21 | 13:1-3 | 13:23-31 |
| 12:22-26 | 13:4-9 | |

# Esta

### (Ulinzi wa Watu wa Mungu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kitabu hakimtaji mwandishi. Lakini inaonekana kama mtu fulani katika tamaduni za Persia. Maandiko haya yanaonyesha kuwa alikuwepo katika mambo yote aliyoyaandika. Hivyo yamkini alikuwa ni myahudi. Wengine wanasema kuwa ni Nehemia au Ezra lakini hakuna kitu kinachounga mkono mawazo yao.[19]

Kitabu hiki kimepata jina lake toka katika mambo ya ukuhani, ambaye kwa jina la kiebrania ni Hadassa (Myrtle) na alibadilika jina na kuwa Esta ikiwa na maana ya “nyota”

**Muda wa Kuandikwa:** Matukio ya Esta yanaonekana kati ya sura za 6 na saba za Ezra na kati ya kurudi kwa waliokuwa uhamishoni chini ya uongozi wa Zerubbabel na hata kule kurudi kwa pili tena chini ya Ezra. Na kitabu cha Esta kiandikwa kati ya 470 na 465 K.K., wakati wa miaka ya utawala wa Xerxes’ (10:2-3), au katika utawala wa mtoto wake Artaxerxes (464–424 K.K.).

**Nia na Makusudi:** Esta anaeleza utawala wa mwanamke myahudi ambaye mfalme Xerxes wa Persia alimchagua kuwa malkia. Wakati Haman alipopanga kuwaua wayahudi wote. Binamu wa Malkia Esta alimwambia Esta ajaribu kuwaokoa watu wake. Akiamua kupoteza maisha yake alimsihi mfalme na akawaokoa wayahudi. Japo kitabu hiki ni kitabu ambacho hakimtamki Mungu lakini nia na makusdi ni kuonesha ukuu wa Mungu kwa watu wake katika matatizo na shida.

**Watu Muhimu:** Esta, Haman, Mordekai, Xerxes (Ahasuero, jina la kiebrania la Persia).

**Mwonekano wa Yesu katika Kitabu cha Esta:** Esta anatoa picha nzuri ya Yesu kwa kuwa alikuwa tayali kuyatoa maisha yake hata kufa kwa ajili ya kuwaokoa watu na hata akawa wakili wa wayahudi kwa mfalme. Na kwa nyongeza ni kwamba Mungu anazidi kuwatetea wayahudi ili kwamba aje awapatie Masihi.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Hatari kwa Wayahudi (1:1–3:15)**
   a. Kuchaguliwa kwa Esta kama Malkia kwa Niaba ya (1:1–2:23)
      1:1-9 2:1-7 2:17-20
      1:10-22 2:8-16 2:21-23
   b. Hila za Hamani dhidi ya Wayahudi (3:1-15)

2. **Ukombozi wa Wayahudi (4:1–10:3)**
   a. Maamuzi ya Esta kwa Wayahudi (4:1–5:14)
      4:1-8 4:15-17 5:9-14
      4:9-14 5:1-8
   b. Kushindwa kwa Hamani (6:1–7:10)
      6:1-9 7:1-6
      6:10-14 7:7-10
   c. Kushindwa kwa Mfalme Ahasuero (Xerxes) na Modekai (8:1-17)
      8:1-8 8:9-17
   d. Kushindwa dhidi ya Maadui wa Wayahudi (9:1-19)
      9:1-10 9:11-19
   e. Siku za Sherehe (9:20-32)
   f. Azimio la Umaarufu wa Modekai na Maonyo katika Mahakama (10:1-3)

# Sehemu ya 3
# Vitabu vya Mashairi

**Utangulizi:** Orodha ya vitabu 17 vya sheria na historia tulivyoviangalia Mwanzo hadi Nehemia vinachukua historia ya Agano lote la Kale. Hivi vilivyobaki vya Mashairi na Manabii vyote vinakamilisha tu vitabu vilivyopita 17. Sehemu inayofuatia ni ndogo sana na ina vitabu vitano tu–Ayubu, Zaburi, Methali, Muhubiri na Wimbo ulio Bora. Kabla hatujavitazama tuone mambo machace yaliyomo katika vitabu hivi.

Wasomo hawana budi kufahamu neno "pashairi" kwa sababu liko kulingana na jinsi yalivyoandikwa. Si matokeo ya wanadamu. Vitabu hivi vinaonesha maisha halisi ya mwanadamu.

**Mahusiano:** Kwa vitabu hivi ambavyo tayari tumeviona vya kihistoria hapo nyuma hivi vingine ni vya mashairi tu na vinatoa kama hisia. Vinaeleza matukio yaliyowapata watu, wakati vya kihistoria vinaeleza juu ya taifa, na hivi vya mashairi vinaeleza hisia za watu na vya kihistoria vinahusika na waebrania na vya mashairi vina eleza juu ya roho za watu. Vitabu vya mashairi si mashairi katika Agano la Kale. Kuna mashairi mengi katika maandiko ya manabii ambayo baadaye tutayaona.

Agano la Kale limegawanyika katika sehemu kuu nne inayohusu juu ya Waisraeli kama Wateule wa Mungu kwa kuangalia haya:

1. Sheria–Inashughulika na Maisha ya Israeli
2. Vitabu vya Kihistoria–Vinahusika na Maendeleo ya Taifa na Maisha
3. Mashairi–Maisha ya Kiroho ya Waisraeli
4. Manabii–Inahusika na Maisha ya Baadaye ya Israeli kuwa Itakamilishwa na Masihi

Vitabu hivi 5 vinaweza kulinganishwa na kingine.

1. Kitabu cha Ayubu–Baraka katika Mateso
2. Zaburi–Sifa kupitia Maombi
3. Methali–Hekima kupitia Maadili
4. Muhubiri–Kweli kupitia Uhalisi
5. Wimbo ulio Bora–Furaha kupitia Umoja

**Kipindi Ccha Mashairi ya Waebrania:** Japo kuwa mashairi ya Waebrania yanaonekana katika Agano la Kale lakini hivi ndivyo vipindi vya kuandikwa:

1. Enzi za Wazee–Ayubu (kati1750 K.K.)
2. Kipindi cha Daudi–Zaburi (kati ya 1050 K.K.)
3. Kipindi cha Sulemani (kati ya 950 K.K.)
   a. Wimbo ulio Bora–Upendo wa Kijana
   b. Methali–ya Kati-Hekima za Wazee
   c. Muhubiri–Kilio cha Mzee (kati ya 950 K.K.)[20]

**Kristo katika Vitabu vya Mashairi:** Kama ilivyosemwa hapo mwanzo Kristo ndiye Roho ya Biblia. Akiwa na wanafunzi wawili katika njia ya Emau walihuzunishwa na kuchanganyikiwa juu ya siku zilizokuwa zimepita za mateso, kifo na hata kufufuka kwake,lakini Yesu alijitokeza ghafla kati yao na kuanza kuwaeleza mambo yote yaliyokuwa yakimhusu katika maandiko (Luka 24:27). Na baadaye alipowatokea wale kumi na mmoja, Aliwaambia: ***"Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi ya kwamba ni lazima yatimie yote yaliyokuwa yameandikwa katika torati ya Musa na katika manabii na zaburi"*** (Luka 24:44).

Kabla ya kuanza kuchambua vitabu hivi ni vizuri tukapata mtazamo wa kihistoria kwanza na Orman Geisler aliandika:

> Palipojengwa Msingi katika sheria ulijengwa katika Yesu katika vitabu vya kihistoria. Vitabu hivi vya mashairi vinatupa hitaji la Kristo katika mioyo ya Watu.Vinahimiza maisha yaliyojawa na Yesu katika sehemu zote mbili za wazi na zilizofichika za kiroho zinazohitajika na zisizohitajika.[21]

Ayubu anaonesha haja ya Yesu. Zaburi anaonesha haja ya umoja katika Yesu,Methali anaonesha haja ya Hekima katika Kristo na Muhubiri ile hali ya kushiba katika Yesu na Wimbo ulio Bora umoja wenye upendo na Kristo.

# Mashairi ya Kiebrania

**Asili Yake:** Mashairi ya kiebrania si kama ya kiingereza na Kiswahili, yanayotoa burudani na lengo maalumu. Haya huwa yanakuwa katika mtazamo mwingine kulingana na mazingira yake. Neno Parallelism (ambalo ni mkusanyo wa mistari tofauti) ni msingi katika mashairi ya kibiblia. Na mashairi haya yana kusudi katika hotuba zake.

**Aina Tatu za Mashairi ya Kiebrania:** (1) mashairi ya Lyric, yenye muziki na vinubi. (Zaburi); (2) Mashairi ya Didactic (mafunzo), haya hutumia maelezo ya kweli na yaliwekwa ili kuwasilisha ujumbe halisi wa maisha (Mithali, Muhubiri); (3) Mashairi ya Dramatii (maigizo) haya yalitumia mazungumzo ili kuwasilisha lengo lake, (Ayubu na Wimbo wa Sulemani).

**Mambo Makuu Mawili katika Mashairi ya Waebrania**

**<u>Parallelism ni Msingi wa Kwanza</u>**
Mashairi haya ya Kiebrania yalipangwa na kurudiwa kwa ulinganifu .Na kuna aina nyingi za ulinganifu huu (parallel)

A. Synonymous–Wazo la mstari wa kwanza hurudiwa rudiwa kwa maneno tofauti katika mstari wa pili (Zaburi 2:4; 3:1; 7:17).
B. Antithetical–Wazo la mstari wa kwanza hukaziwa kabisa katika mstari wa pili na hii mara nyingi hutambuliwa kwa “lakini” (Zaburi 1:6; 34:10).
C. Synthetic–Mstari wa pili unaendeleza wazo la mstari wa kwanza (Zaburi 1:3; 95:3).
D. Climactic–Mstari wa pili unarudiwa kwa hiari mwishoni (Zaburi 29:1).
E. Emblematic–Mstari mmoja unabeba ujumbe wote na wa pili unatoa tu picha yake (Zaburi 42:1; 23:1).

**<u>Umbo katika Hotuba ni Jambo la Pili</u>**
Umbo katika hotuba linakuwepo wakati kitu kimoja kinataka kuwasilisha kingine. Na mashairi ya kiebrania hutumia umbo au vitu katika kueleza hisia au mawazo fulani.

Kwa mfano’ ***Bali sheria ya Bwana ndiyo impedezayo naye atakuwa kama mti uliopandwa*** (Zaburi 1:2-3). Neno impenezayo si kiini kwa “mti” isipokuwa anafananishwa na mti. Utaona neno “kama” katika aina hii ya sentensi (Zaburi 5:12; 17:8; 131:2).

Aina nyingine ya umbo katika hotuba inalinganisha kitu hiki na kingine kwa kutumia neno “ni” katika Zaburi 23:1, Daudi anasema, ***“Bwana ni mchungaji wangu”.*** Daudi si ng’ombe aliyekodiwa isipokuwa analindwa na Bwana kama mchungaji alindavyo kondoo wake (Zaburi 84:11; 91:4).

Kwa wakati mwingine hotuba zingine za juu hutumika kufafanua pointi. Zaburi 6:6, Daudi anasema “***kwamba kila usiku nakieleza kitanda changu nalilowesha godoro kwa machozi yangu.”*** Hii hotuba inaonesha huzuni yake. Kweli Daudi hawezi kulia hadi godoro lilowane kabisa (Zaburi 78:27; 107:26).

Pia hata maswali hutumika kuliko kutumia maombi. Wakati Daudi alipouliza ***“Ni nani kama wewe?”*** katika Zaburi 35:10 alikuwa aneleza kwa makini kuwa hakuna kama Bwana Mungu wala hakuitaji jibu la swali lake. (Zaburi 56:8; 106:2).

Na mwisho ni kutumia wanyama ili kueleza ukuu wa Mungu. Na hii hutumika kueleza ukweli wa Mungu mfano Zaburi 17:8 tunaona kwamba Daudi anamwambia Mungu amfiche katika mbawa zake, hapa Mungu si ndege lakini anaeleza ukuu wa Mungu kuwa kama mama wa ndege afichavyo vitoto vyake basi hata Mungu afanye hivyo (Zaburi 91:4).

# Ayubu
## (Baraka kupitia Mateso)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kitabu hiki tunajua kuwa kimepata jina lake toka kwa Mhusika wake Ayubu. Na hata hivyo alikuwa mtu wa kihistoria (Ezekiel 14:14, 20; Yakobo 5:11), lakini mwandishi hajulikani na hakuna vithibitisho vya mwandishi kuwa ni nani ila watu wanahisi kuwa ni Ayubu mwenyewe, Elihu, Musa, Sulemani na wengineo.

Angalia katika Nyakati: Ibraham, Isaka, Yakobo, na Yusufu, Kitabu hiki cha Ayubu kinapata jina lake toka kwa mhusika wake Ayubu, mtu mmoja aliyeitwa Ayubu aliyehangaika hata kupoteza utajiri ,jamaa na hata Kuugua sasa fikiri kwa nini? Kianze hivi nani mwandishi?

**Muda wa Kuandikwa:** Kwa kuwa hatujui ni nani aliyekiandika hivyo hata kujua kipindi cha kuandikwa kwake ni vigumu. Lakini historia yake ilikuwa kabla ya kutolewa kwa Sheria ya Musa (1445-1405 K.K.). Tangu kutolewa kwa sheria ya Musa na hata katika kusimikwa kwa ukuhani wa Walawi, mkuu wa familia alikuwa ni kuhani. Ayubu naye anaonekana kutoa sadaka yake kama jamaa wa (Ayubu1:5). Hii inaonesha kabisa mwanzo wa kipindi kabla ya kutolewa sheria ya Musa na hii ilifanyika katika nyakati za Ibrahimu.

**Nia ba Makusudi:** Hiki ni kitabu cha wema wa Mungu, haki, na hata mamlaka katika kipindi cha mapito. Kinaanza kwa maswali ni kwa nini watu wenye haki huhangaika ikiwa Mungu ni Mungu wa rehema na upendo? Hivyo kinafundisha mamlaka ya Mungu kuwa ni ya upendo na mwanadamu hana budi kushukuru. Na hata wale watu watatu waliokuwa rafiki wa Ayubu walitoa jibu la kufanana. Na walisema mateso yote ni kwa sababu ya dhambi. Elihu japo alidai kuwa mateso humsafisha mwenye haki. Kusudi la Mungu lilikuwa ni kumfundisha Ayubu apate kumtegemea yeye tu. Gleason Archer anatupa maelezo mazuri:[22]

> Kitabu hiki kinahusika na matatizo nadharia,majanga na maumivu katika maisha ya miungu. Hii tunaipata hapa kwa nini wenye haki wahangaike na hii inatoka katika mambo makuu matatu: (1) Mungu ni mwenye upendo mbali na baraka alilalamika; (2) Mungu anaruhusu matatizo kama njia ya kujitakasa katika miungu; (3) Mawazo na njia za Mungu ni pana ukilinganisha na za mwanadamu. Alisema, japokuwa mwanadamu hawezi kuona mambo yatakayompata katika maisha lakini Mungu anajua. Na hili lilikuwa ni jibu lililokuwa kinyume kabisa na mtazamo wa Ayubu kutoka kwa wafariji hawa: Eliphazi, Bildadi, na Zophari.[23]

Na zaidi ilikuwa ni kuonyesha mgogoro wa vipindi kati ya Mungu na Shetani na hata kuonyesha mahusiano ya tabu katika mgogoro huu. Na mwisho inaeleza ukweli wa Warumi 8:28.

**Watu Muhimu:** Ayubu, mlalamikaji na mwenye haki, shetani, watu waliomlaumu Ayubu, Eliphazi, Bildad, Zophari, na Elihu, kijana mdogo na mwenye hekima aliyemshauri Ayubu.

**Mwonekano wa Yesu katika Ayubu:** Yesu anaonekana katika nyanja mbalimbali katika kitabu hiki. Ayubu anamshukuru mwokozi (19:25-27) na anaomba kwa mpatanishi (9:33; 33:23). Alijua anahitaji msaada wa mtu ambaye ataeleza siri ya mateso ambayo inadhihirishwa pekee katika Kristo tu, na kutuonyesha kabisa ushindi (Waebrania 2:14-18; 4:15; Warumi 8:32-34).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Majanga: Mateso ya Ayubu (1:1–2:13)**
   a. Mapito Yake (1:1-5)
   b. Matatizo Yake na Vyanzo Vyake (1:6–2:10)
      1:6-12 1:13-22 2:1-10
   c. Wafariji Wake (2:11-13)

2. **Mazungumzo au Farija za Uongo za Marafiki Watatu (3:1–31:40)**
   a. Majadiliano ya Kwanza (3:1–14:22)
      1) Maombolezo ya Ayubu (3:1-26)
         3:1-19 3:20-26
      2) Majibu ya Eliphazi (4:1–5:27)
         4:1-11 5:1-7 5:17-27
         4:12-21 5:8-16
      3) Na Majibu ya Ayubu (6:1–7:21)
         6:1-7 6:24-30 7:11-21
         6:8-13 7:1-6
         6:14-23 7:7-10
      4) Majibu ya Bildadi (8:1-22)
         8:1-7 8:8-10 8:11-22
      5) Na Majibu ya Ayubu (9:1–10:22)
         9:1-12 9:25-35 10:8-17
         9:13-24 10:1-7 10:18-22
      6) Majibu ya Sofari (11:1-20)
         11:1-6 11:7-12 11:13-20
      7) Na Majibu ya Ayubu (12:1–14:22)
         12:1-6 13:13-19 14:13-17
         12:7-12 13:20-28 14:18-22
         12:13-25 14:1-6
         13:1-12 14:7-12

b. Mazungumzo ya Maa ya Pili (15:1–21:34)

1) Majibu ya Elifasi (15:1-35)

| | |
|---|---|
| 15:1-16 | 15:17-35 |

2) Na Majibu ya Ayubu (16:1–17:16)

| | | |
|---|---|---|
| 16:1-5 | 16:18-22 | 17:6-16 |
| 16:6-17 | 17:1-5 | |

3) Majibu ya Bildadi (18:1-21)

| | |
|---|---|
| 18:1-4 | 18:5-21 |

4) Na Majibu ya Ayubu (19:1-29)

| | | |
|---|---|---|
| 19:1-6 | 19:7-22 | 19:23-29 |

5) Majibu ya Sofari (20:1-29)

| | | |
|---|---|---|
| 20:1-11 | 20:12-19 | 20:20-29 |

6) Na Majibu ya Sofari (21:1-34)

| | | |
|---|---|---|
| 21:1-16 | 21:17-26 | 21:27-34 |

c. Mazungumzo ya tatu (22:1–31:40)

1) Majibu ya Elifasi (22:1-30)

| | | |
|---|---|---|
| 22:1-11 | 22:12-20 | 22:21-30 |

2) Na Majibu ya Ayubu (23:1–24:25)

| | | |
|---|---|---|
| 23:1-7 | 24:1-12 | 24:18-25 |
| 23:8-17 | 24:13-17 | |

3) Majibu ya Bildadi (25:1-6)

4) Na Majibu ya Ayubu (26:1–31:40)

| | | |
|---|---|---|
| 26:1-4 | 29:1-20 | 31:9-12 |
| 26:5-14 | 29:21-25 | 31:13-15 |
| 27:1-6 | 30:1-8 | 31:16-23 |
| 27:7-12 | 30:9-15 | 31:24-28 |
| 27:13-23 | 30:16-23 | 31:29-37 |
| 28:1-11 | 30:24-31 | 31:38-40 |
| 28:12-22 | 31:1-4 | |
| 28:23-28 | 31:5-8 | |

**3. Hekima ya Elihu (32:1–37:24)**

a. Maneno ya Kwanza: Maelekezo ya Mungukwa Mtu kwa Njia ya Mateso (32:1–33:33)

| | | |
|---|---|---|
| 32:1-10 | 33:1-7 | 33:19-22 |
| 32:11-14 | 33:8-12 | 33:23-28 |
| 32:15-22 | 33:13-18 | 33:29-33 |

b. Maeno ya Pili: Haki ya Mungu Yathibitishwa (34:1-37)

| | | |
|---|---|---|
| 34:1-9 | 34:16-20 | 34:31-37 |
| 34:10-15 | 34:21-30 | |

c. Maeno Mara ya Tatu: Faida za Utakatifu (35:1-16)

| | |
|---|---|
| 35:1-8 | 35:9-16 |

d. Maneno Mara ya Nne: Ukuu wa Mungu na Ghadhabu ya Ayubu kwa Kumwona Mungu kama Amemuacha (36:1–37:24)

| | | |
|---|---|---|
| 36:1-16 | 36:24-33 | 37;14-20 |
| 36:17-23 | 37:1-13 | 37:21-24 |

**4. Ufunuo wa Mungu (38:1–42:6)**

a. Ufunuo wa Kwanza (38:1–40:5)

1) Uwepo wa Mungu tangu Uumbaji (38:1–39:30)

| | | |
|---|---|---|
| 38:1-7 | 38:25-30 | 39:5-12 |
| 38:8-11 | 38:31-33 | 39:13-18 |
| 38:12-15 | 38:34-38 | 39:19-25 |
| 38:16-18 | 38:39-41 | 39:26-30 |
| 38:19-24 | 39:1-4 | |

2) Ayubu Ajilaumu Mwenyewe (40:1-5)

b. Ufunuo wa Pili :Nguvu ya Mungu na Udhaifu wa Mwanadamu. Unyenyekevu wa Ayubu (40:6–42:6)

| | | |
|---|---|---|
| 40:6-9 | 40:19-24 | 42:1-6 |
| 40:10-14 | 41:1-11 | |
| 40:15-18 | 41:12-34 | |

**5. Maneno yawisho (42:7-17)**

a. Hasira ya Mungu kwa Wafarii wa Uongo (42:7-9)

b. Kubarikiwa na Kuponywa kwa Ayubu(42:10-17)

# Zaburi
## (Sifa kupitia Maombi)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kitabu cha Zaburi ni kitabu kirefu katika Biblia na hata kitabu kipana katika matumizi ya maandiko kwa sababu kinagusa sana roho za watu juu ya maisha yao. Pia kiko katika hali ya kusifu na kuomba. Kwa sehemu kubwa ya Biblia kitabu cha Zaburi waadishi wameainishwa katika mlolongo ufuatao.[24]

| Utunzi wa Zaburi | | |
|---|---|---|
| Daudi | 78 | Zaburi 1-41; 51-70; 86; 103; 108-110; 122; 124; 131; 133; 138-145 |
| Asa | 12 | Zaburi 50, 73-83 |
| Korahiti | 12 | Zaburi 42-49; 84-85; 87-88 |
| Solomon | 2 | Zaburi 72, 127 |
| Musa | 1 | Zaburi 90 |
| Ethan | 1 | Zaburi 89 |
| Zingine Binafsi | 44 | Zaburi 71; 91-102; 104-107; 111-121; 123; 125-126; 128-130; 132; 134-137; 146-150 |

Katika lugha ya Kiebrania, kitabu cha Zaburi kinajulikana kama kitabu cha Sifa na Zaburi 145 inathibitisha hili. Zaburi ni mashairi yaliyoimbwa kwa kutumia vyombo vya muziki. Neno Zaburi linatokana na Kiebrania lenye maana ya piga chombo chenye nyuzi kwa ajili ya kuimba.

**Muda wa Kuandikwa:** Kwa upana wake kitabu hiki kiko katika nia na makusudi na hata mtazamo mkubwa katika hali fulani ya upana ambayo inamfanya msomaji apate kuelewa jinsi alivyokuwa akiishi kwa kuangalia muda na vipindi vya Zaburi Gleasoni aliandika:

> Kwa kuangalia kitabu cha Zaburi 90 kinaweza kuwa cha kwanza kilichoandikwa na Musa kati ya 1405 K.K. Zaburi za Daudi zinaweza kuwa lifanywa kati ya 1020 na 975 K.K na zile Zaburi za Asa nazo zaweza kuwa kwenye kipindi hicho. Zaburi imekuwepo tangu kipindi cha utawala wa Sulemani kati ya 950 K.K Ni vigumu kujua ukoo wa Kora na hata wale wawili akina Ezra waliotajwa labda walikuwepo kabla ya uhamishoni lakini Zaburi haijawaeleza. Labda wamekuwepo lakini kati ya miaka 500 K.K.[25]

**Nia na Makusudi:** Zaburi inatupatia ujumbe wa matumaini na faraja kwa njia ya sifa. Walikuwa katika mapito na woga na hata malalamiko katika kazi za mikono yao. Lakini wanatueleza vizuri juu ya sifa ,imani na hata maisha ya kiroho ya waisraeli. Hivyo katika katika Zaburi tunapata kioo cha roho za watu wa Mungu na hata ulimwengu unapata haki inayopatikana kupitia watu wa Mungu.

Katika mkusanyo wa zaburi zote 150 kuna mawazo mengi na hata makusudi mengi. Hii ina maana kuwa ni vigumu sana kuyajumuisha yote haya lakini tunaweza kusema kuwa Zaburi zote zinajumuisha hisia za watu zinazotupelekea kujua haki ya Mungu na wema wake. Pia zinajumuisha hisia za mtunzi wa Zaburi juu ya kukatishwa tamaa na shukurani zote alizozitoa hata alipokuwa akikutana na magumu. Japo zaburi imejaa majuto na wakati mwingine furaha. Lakini mtunzi wa kila Zaburi anaeleza ukuu wa Mungu aliye hai. Kweli kuna zaburi chache zenye Mawazo ya Mungu kama vile Zaburi ya 2 lakini hizi si za lazima sana.[26]

Zaburi zote zinahusu neno la Mungu na mtazamo wake na ni za kimasihi katika uishio wake kama kutabiri.

**Mgawanyo wa Zaburi:** Zaburi ni vitabu vitano katika kitabu kimoja. Kila kitabu kina sifa za Mungu na ile Zaburi ya 150 ina sifa za Mungu na ina hitimisho la Zaburi zote.

Epiphania alisema, “Waebrania waligawa Zaburi katika sehemu tano ili iwe Pentateuch nyingine.” Zaburi 1:1 inasema “Musa akawapatia Waisraeli vitabu vitano vya sheria na kwa kuangalia hapa Daudi naye akawapatia kitabu chenye vitabu vitano.”[27]

Orodha ya maandiko haya iko kama ifuatavyo:[28]

1. Zaburi Juu ya Uumbaji na Mwanadamu (1-41)–Hii ina Shabihiana na Mwanzo
2. Zaburi Juu ya Waisraeli na Kukombolewa (42-72)–Hii Inafanana na Kutoka
3. Zaburi Inayohusu Ibada na Hekalu (73-89)–Hii Ina Fanana na Walawi
4. Zaburi Juu Dunia (90-106)–Hii Inafanana na Hesabu
5. Zaburi Inayohusu Sifa na Neno la Mungu (107-150)–Hii Inahusu Kumbukumbu la Torati

Njia nyingine ya kutazama mgawanyo wa vitabu hivi:

| Kitabu | Zaburi | Mwandishi | Yaliyomo |
|---|---|---|---|
| I | Zaburi 1-41 | Daudi | Nyimbo za kuabudu |
| II | Zaburi 42-72 | Daudi & Kora | Nyimbo za kutukuza |
| III | Zaburi 73-89 | Asaph | Nyimbo za kutukuza |
| IV | Zaburi 90-106 | Anonymo | Nyimbo za kusifu |
| V | Zaburi 107-150 | Daudi & Anonymo | Nyimbo za kusifu |

**Makundi au Aina ua Zaburi:** Kama ilivyo katika aina zake ifuatayo inaonesha kabisa makundi yake:

1. **Maombolezo** (Huzuni) au **fadhaa**, au mtu (Zaburi 3) au katika mambo ya kijamii (Zaburi 44)
2. **Shukurani** au **Sifa** au mtu (Zaburi 30) au katika mambo ya jamii (Zaburi 65)
3. **Mtumaini Mungu** (Zaburi 4)
4. **Nyimbo za utenzi**: Zaburi juu ya Yerusalemu (Zaburi 48), na Zaburi za Zaburi za kifalme (zingine ni za kimasihi; Zaburi 2, 110)
5. Zaburi za **Mafundisho** na **Hekima** (Zaburi 1, 37, 119).
6. Zaburi za **Makusudi Maalumu**: Hivyo Zaburi zinaweza kugawanywa kulingana na makusudi kama vile zaburi za uumbaji (Zaburi 8, 19), Zaburi za asili (Zaburi 19;104), Zaburi za kumbukumbu na ushauri (Zaburi 111, 112, 119), Kutoka (Zaburi 78), Toba (Zaburi 6), Zaburi za hija (Zaburi 120), na Zaburi za Masihi, na zile zinazoingiza unabii kama vile Zaburi 2, 8, 16, 22, 40, 45, 72, 110, 118.

**Watu Muhimu:** Japo vichwa vya habari katika Zaburi vinahusiana na watunzi wake kama vile Daudi au mtoto wa Kora ujumbe wa Zaburi hizi unaangalia na kulenga watu wa Mungu katika kuabudu kwao na tembea yao katika Bwana.

**Mwonekano wa Yesu katika Zaburi:** Jumbe nyingi za Zaburi ni za kimasihi na zinazungumzia juu ya mtu na kazi ya Kristo. Na zinaangaliwa katika makundi yafuatayo:

1. **Za kimasihi:** Hizi ni Zaburi zilizo finyu sana. Mtunzi wa Zaburi hizi kwa namna nyingine anamwakilisha Masihi (linganisha 34:20; 69:4, 9), lakini zingine hazimwakilishi. Labda kwa jambo hili Yesu na mitume walionekana kama jamaa wa watunzi wa Zaburi ukiangalia katika maelezo yao. (Mfano, 109:8 na katika Matendo 1:20).
2. **Unabii ainishi:** Japokuwa mwandishi wa Zaburi anaeleza habari zake lakini habari zake za kihistoria ni kweli katika Yesu Kristo. (22).
3. **Masihi:** Zaburi ilipokuwa ikiandikwa katika ilihusu sana nyumba ya Daudi na hata ufalme mzima lakini mwisho wake ni kwa Kristo tu. (2, 45, 72).
4. **Unabii:** Zinahusika moja kwa moja kwa Kristo bila ya kutaja mtu yeyote, kitu chochote au mwana wa Daudi (110).
5. **Utawala:** Hizi ni Zaburi zinazomwakilisha Yesu na hata ufalme katika kukamilishwa na Mtu mmoja Masihi wa Mungu. (96-99).

**Unabii Halisi Uliopewa kwa Yesu:**

| Unabii | Zaburi | Ujumbe wa Agano Jipya |
|---|---|---|
| 1. Kuzaliwa | 104:4 | Waebrania 1:7 |
| 2. Uzalilisho | 8:4 | Waebrania 2:6 |
| 3. Uungu | 45:6 | Waebrania 1:8 |
| 4. Huduma | 69:9 | Yohana 2:17 |
| 5. Kuondoshwa | 118:22 | Mathayo 21:42 |
| 6. Kusaliti | 41:9 | Yohana 13:18 |
| 7. Kusulubiwa | 22 | Mathayo 27:39, 43, 46; Luka 23:35 |
| 8. Kufufuka | 2 na 16 | Matendo 2:27 |
| 9. Kupaa | 68:18 | Waefeso 4:8 |
| 10. Kutawala | 102:26 | Waebrania 1:11 |

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Kitabu I: Nyimbo za Kuabudu (Zaburi 1-41**)
   Zaburi 1: Mbarikiwa: Njia mbili: Neno na Dunia
   Zaburi 2: Masiha: Upingamizi kati ya Mungu na Kristo
   Zaburi 3: Ukimya katika Shida : Ulinzi katika Njaa
   Zaburi 4: Maombi ya Kumtumaini Mungu
   Zaburi 5: Maombi ya Asubuhi

Zaburi 6: Maombi ya Majuto
Zaburi 7: Maombi ya Ukimbizi
Zaburi 8: Utukufu wa Muumbaji
Zaburi 9: Maombi ya Shukurani
Zaburi 10: Maombi ya Ushindi
Zaburi 11: Mungu ni Mlinzi
Zaburi 12: Maombi ya Kuhitaji Msaada
Zaburi 13: Maombi ya Msaada Katika Matatizo
Zaburi 14: Udhaifu wa Mwanadamu
Zaburi 15: Mungu wa Mtu
Zaburi 16: Bwana ni Kimbilio Na Ngome
Zaburi 17: Maombi ya Kukombolewa
Zaburi 18: Maombi ya Kusifu
Zaburi 19: Ufunuo wa Mungu Katika Kazi Ya Mikono Yake
Zaburi 20: Maombi ya Ushindi Dhidi Ya Maadui
Zaburi 21: Bwana ni Mfalme
Zaburi 22: Msalaba Zaburi ya Sifa
Zaburi 23: Mchungaji Mwema
Zaburi 24: Zaburi ya Mfalme wa Utukufu
Zaburi 25: Maombi ya Kuokolewa, Ulinzi na Msamaha
Zaburi 26: Maombi ya Ukombozi na Ushindi
Zaburi 27: Maombi ya Hofu katika Bwana
Zaburi 28: Maombi ya Sifa kwa Majibu ya Mungu
Zaburi 29: Sauti ya Mungu
Zaburi 30: Maombi ya Shukurani
Zaburi 31: Maombi ya Kulaumu na Sifa
Zaburi 32: Baraka ya Kusamehewa
Zaburi 33: Sifa kwa Bwana Muumbaji na Mwokozi
Zaburi 34: Sifa kwa Bwana kama Mtoaji
Zaburi 35: Maombi kwa Ajili ya Haki na Kuokolewa Toka kwa Adui
Zaburi 36: Upendo wa Mungu kwa Mwanadamu
Zaburi 37: Faida za Kukaa na Bwana
Zaburi 38: Maombi ya Kuthibitisha Kutuliwa Mzigo
Zaburi 39: Maombi Hutoa Ujasiri
Zaburi 40: Maombi kwa Ajili ya Furaha
Zaburi 41: Sifa kwa Ajili ya Baraka za Mungu

**2. Kitabu cha II: Nyimbo za Maombi (Zaburi 42-72)**
Zaburi 42-43: Kumtumaini
Zaburi 44: Majuto ya Taifa na Maombi ya Kuokolewa
Zaburi 45: Wimbo wa Harusi wa Mwana wa Daudi
Zaburi 46: Mungu Ndiye Ngome Yetu
Zaburi 47: Bwana ni Mfalme Mshindi
Zaburi 48: Mlima Sayuni Mji Mzuri
Zaburi 49: Utupu wa Matajiri Wasio na Hekima
Zaburi 50: Sadaka ya Shukurani
Zaburi 51: Kukiri na Kusamehewa Dhambi
Zaburi 52: Watu Waovu
Zaburi 53: Uungu
Zaburi 54: Bwana ni Msaada
Zaburi 55: Bwana ni Mpaji kwa Wenye Haki
Zaburi 56: Kuwa na Imani katikati ya Hofu
Zaburi 57: Ukuu wa Bwana katika Shida
Zaburi 58: Zawadi ya Wenye Haki
Zaburi 59: Maombi ya Msaada kwa Maadui
Zaburi 60: Maombi ya Kukombolewa kwa Taifa
Zaburi 61: Maombi ya Woga
Zaburi 62: Kumsubiri Bwana
Zaburi 63: Kuhitaji Upendo wa Mungu
Zaburi 64: Maombi ya Ulinzi
Zaburi 65: Mungu ni wa Dunia na Mwanadamu
Zaburi 66: Kumbuka Alichokutendea Mungu
Zaburi 67: Mwito wa Kumsifu Mungu
Zaburi 68: Mungu ni Baba wa Waliolemewa

Zaburi 69: Maombi ya Kuokolewa na Mungu
Zaburi 70: Maombi ya Wahitaji na Maskini
Zaburi 71: Maombi ya Waliochoka
Zaburi 72: Utawala wa Masihi katika Utukufu

**3. Kitabu cha III: Nyimbo Zenye Utukufu (Zaburi 73-89)**

Zaburi 73: Maombi ya Mtazamo wa Milele
Zaburi 74: Maombi ya Msaada Wakati wa Ugumu katika Taifa
Zaburi 75: Haki Ni ya Bwana
Zaburi 76: Nguvu ya Ushindi katika Mungu wa Yakobo
Zaburi 77: Wakati wa Shida Mkumbuke Mungu
Zaburi 78: Somo Toka Historia ya Waisraeli
Zaburi 79: Maombi ya Kumkumbusha Mungu Akumbuke Watu wa Malisho Yake
Zaburi 80: Maombi ya Waisraeli
Zaburi 81 Kusikiliza kwa Waisraeli Toka kwa Bwana
Zaburi 82: Wasio Haki
Zaburi 83: Maombi Dhidi ya Adui wa Israeli
Zaburi 84: Nia ya Uwepo wa Mungu
Zaburi 85: Maombi ya Ufufuo
Zaburi 86: Maombi ya Neema kwa Taifa
Zaburi 87: Furaha ya Kuishi Sayuni
Zaburi 88: Maombi Wakati wa Giza la Kukata Tamaa
Zaburi 89: Ahadi za Mtu wa Mungu

**4. Kitabu cha IV: Nyimbo za Sifa (Zaburi 90-106)**

Zaburi 90: Inatufundisha Kuhesabu Siku Zetu
Zaburi 91: Katika Malazi ya Mungu Aliye Mkuu
Zaburi 92: Kumsifu Bwana
Zaburi 93: Yahwe Hutawala katika Utukufu
Zaburi 94: Yahwe ni Mwamuzi wa Ulimwengu
Zaburi 95: Tumpigie Magoti Bwana Wetu
Zaburi 96: Mwabudu Bwana
Zaburi 97: Furahini Bwana Anatawala
Zaburi 98: Mwimbieni Bwana Wimbo Mpya
Zaburi 99: Bwana Atukuzwe
Zaburi 100: Mtumikie Bwana kwa Furaha
Zaburi 101: Maisha Matakatifu
Zaburi 102: Maombi ya Mtakatifu
Zaburi 103: Mbariki Bwana Asiyeshindwa
Zaburi 104: Ulinzi wa Bwana
Zaburi 105: Uaminifu wa Bwana
Zaburi 106: Kumbukumbu ya Yahwe wa Upendo

**5. Kitabu cha V: Nyimbo za Sifa (Zaburi 107-150)**

Zaburi 107: Sifa Juu ya Wokovu wa Bwana
Zaburi 108: Sifa na Maombi Juu ya Ushindi
Zaburi 109: Maombi ya Hukumu dhidi ya Adui
Zaburi 110: Masihi Anaonekana kama Mfalme
Zaburi 111: Furaha ya Uaminifu wa Mungu
Zaburi 112: Washindi wa Imani
Zaburi 113: Sifa kwa Bwana
Zaburi 114: Sifa za Kutoka
Zaburi 115: Umuhimu wa Bwana
Zaburi 116: Sifa kwa Bwana
Zaburi 117: Sifa Za Watu Wote
Zaburi 118: Sifa kwa Wokovu wa Bwana
Zaburi 119: Sifa Katika Maandiko
Zaburi 120: Maombi ya Kukombolewa
Zaburi 121: Bwana ni Mlinzi Wangu
Zaburi 122: Maombi Juu ya Amani ya Yerusalemu
Zaburi 123: Neema
Zaburi 124: Msaidizi Wetu ni Muumba wa Mbingu na Nchi
Zaburi 125: Amani kwa Israeli
Zaburi 126: Sifa kwa Urejesho

Zaburi 127: Sifa kwa Watoto Zawadi toka kwa Mungu
Zaburi 128: Baraka za Bwana kwa Jamaa
Zaburi 129: Maombi kwa Wanaoudhiwa
Zaburi 130: Kusubiri Wokovu wa Bwana
Zaburi 131: Kumtumaini Bwana
Zaburi 132: Maombi ya Baraka za Bwana kwa Sayuni
Zaburi 133: Umoja wa Baraka
Zaburi 134: Msifu Mungu Wakati wa Usiku
Zaburi 135: Sifu Kazi za Ajabu za Mungu
Zaburi 136: Sifu Neema za Mungu Kusifu
Zaburi 137: Machozi ya Mateka
Zaburi 138: Bwana Hujibu Maombi
Zaburi 139: Bwana Ananitambua
Zaburi 140: Maombi kwa Kukombolewa
Zaburi 141: Mfano wa Maombi Yangu
Zaburi 142: Hakuna Awezaye Kutulinda Isipokuwa Bwana Tu; Yeye Peke Yake ni Sehemu Yangu
Zaburi 143: Maombi ya Ulinzi
Zaburi 144: Bwana ni Mwamba Wangu
Zaburi 145: Sifu Ukuu wa Mungu
Zaburi 146: Sifa kwa Bwana
Zaburi 147: Sifa kwa Bwana Awaponyaye Waliovunjika Moyo
Zaburi 148: Msifuni Bwana Muumbaji
Zaburi 149: Sifa kwa Bwana Awahurumiaye Watu
Zaburi 150: Sifa kwa Bwana

# Mithali

## (Hekima kupitia Maadili )

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kulingana na 1 Wafalme 4:32, Sulemani alisema Mithali 3,000 na nyimbo 1,005. Aliandika Mithali nyingi katika kitabu hiki lakini baadaye sura zinaonesha kuwa si yeye tu aliyehusika. Sehemu tatu za Mithali zinaeleza juu ya Sulemani, sura ya 1:1–9:18; 10:1–22:16, na 25:1–29:27. Hata hivyo methali katika sehemu ya barua. (25:1–29:27) zilichanganuliwa na baraza la Hezekia (25:1). Mithali 22:17 inazungumzia mambo ya hekima Mithali. 22:17-21 inatambulisha kuwa hizi sehemu zinatokana na watu wenye hekima. Na si tu Sulemani na sura ya 30 inasema juu ya Aga mwana wa Yake na 31:1-9 inazungumza juu ya mfalme Lemuel.

Mithali ilipata jina lake toka katika maneno ya semi yaliyokuwa mafupi. Na neno Mithali kwa kiebrania lina maana ya “Kulingana”. Inalingana na mambo ya kijamii. Si kwa jamii tu lakini hata katika kupingana na kichwa cha habari hiki kinatoka katika ukweli kuwa hii ni ufupisho wa maadili na maswala ya kiroho ili kwamba yamsaidie mtu kuishi kwa hekima na busara.

**Muda wa Kuandikwa: 950-700 K.K.** Kama kitabu cha hekima Methali si kitabu cha historia ila ni shule ya hekima . Mithali za Sulemani ziliandikwa kabla ya kifo chake mwaka 931 K.K., na zingine zilikusanywa na Hezekia kati ya 700 K.K.

**Nia na Makusudi:** Kama ilivyosemwa na jina la kitabu na maana ya kitabu kuwa ni Methali, hivyo nia na makusudi ya kitabu ni hekima katika kuishi na kuenenda. Kinatoa maelekezo ya kufanya katika maisha yetu: dhambi, wema, utajiri, ufukara, ndimi, mambo ya kuoa na kuolewa,upendo uvivu n.k. Na hivyo hakuna kitabu katika maisha yetu kinachoweza kutufanya tuwe na hekima zaidi ya Mithali.

Na kusudi kuu ni ***“Kumwogopa Bwana ni chanzo cha maarifa”*** (1:7a). Kutokuwa na hofu na woga na Mungu kunatufanya tuwe wapumbavu. Kumhofu Bwana ni kufanya yale anayotaka tufanye . Na wakati huo huo hekima inatufanya tuwe na woga wa ki-Mungu (2:1-5).

**Watu Muhimu:** Methali imeandikwa kwa kumhusu kila mtu kwa hiyo hakuna aliyetajwa.

**Mwonekano wa Yesu katika Methali:** Katika sura ya 8 hekima inaonekana kama mtu na hata ukamilifu wake (8:22-31), ni chanzo cha maisha ya kiroho (3:18; 8:35-36), ni haki na maadili (8:8-9), na kinapatikana kwa kila anayehitaji (8:1-6, 32-35). Hekima hii imekuja kwa njia ya mwili yaani Yesu. ***“ambaye ndani yake yeye hazina zote za hema na maarifa zimesitirika”*** (Wakolosai 2:3). ***“Bali katika yeye mmepata kuwa katika Kristo Yesu aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu na haki na utakatifu na ukombozi”*** (1 Wakoritho 1:30 linganisha 1 Wakorintho 1:22-24).[29]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi: Kusudi la Methali (1:1-7)**

2. **Hekima: Methali kwa Vijana (1:8–9:18)**
   a. Kuwatii Wazazi (1:8-9)
   b. Kuachana na Makundi Mabaya (1:10-19)
   c. Hekima na Mashauri (1:20-33)
   d. Epuka Uzinzi (2:1-22)
   e. Tumaini na Hesima kwa Mungu (3:1-12)
   f. Baraka za Hekima (3:13-20)
   g. Kuwa Mwema kwa Wengine (3:21-35)
   h. Kuwa na Hekima (4:1-9)
   i. Kuachana na Makundi (4:10-19)
   j. Zaidi ya Yote Tunza Moyo Wako (4:20-27)
   k. Usizini (5:1-14)
   l. Uwe Mwaminifu kwa Mke Wako (5:15-23)
   m. Usijiamini Sana (6:1-5)
   n. Uvivu (6:6-19)
   o. Epuka Uasherati (6:20-35)
   p. Achana na Uasherati (7:1-27)
   q. Hekima (8:1–9:18)

3. **Methali za Sulemani (10:1–24:34)**
   a. Heshima Huonesha Unyenyekevu wa Mtu (10:1–15:33)
   b. Heshima Huhamasisha Hata Mambo ya KIroho (16:1–22:6)
   c. Mithali Huonyesha Unadhifu (22:17–23:35)
   d. Heshima Hukufanya Uheshimiwe (24:1-34)

4. **Methali za Sulemani Zilizofanywa na Watu: Hezekia (25:1–29:27)**
   a. Mithali Inayohusisha Mahusiano na Wengine (25:1–26:28)
   b. Mithali ya Matendo (27:1–29:27)

5. **Maneno ya Aga (30:1-33)**
   a. Maneno Binafsi (30:1-14)
   b. Mithali Changanufu (30:15-33)

6. **Maneno ya Lemuel (31:1-9)**

7. **Mwanamke Mwema (31:10-31)**

# Muhubiri

### (Ukweli kupitia Mambo Halisi)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kuna sababu mbili (za ndani na nje) zinazoonyesha kwamba Sulemani ndiye mwandishi. Kwa undani kabisa inaonekana kwamba Sulemani ndiye mwandishi wa kitabu cha Muhubiri. Kwa nje desturi za kiyahudi zinaonyesha kwamba Sulemani ndiye mwandishi. Kwanza mwandishi anajitambulisha kama ***"Mwana wa Daudi, Mfalme katika Yerusalemu"*** (1:1). Halafu inaonekana hekima ya mwandishi (1:16), utajiri mwingi (2:7), nafasi za mali (2:3), na shughuli nyingi za ujenzi (2:4-6). Zote hizi zinaonesha kwamba mwandishi ni Sulemani. Hakuna ukoo wa Daudi uliotajwa humu.

Neno Muhubiri limetokana na lugha ya Septuagint. Neno hili kwa kiyunani lina maana ya "Kusanyiko" Kiebrania lina maana ya "Mtu anayesema na kushawishi katika kusanyiko au Muhubiri."

**Muda wa Kuandikwa: 931 K.K.** Kulingana na desturi za Wayahudi Sulemani aliandika Wimbo ulio Bora katika miaka yake ya kwanza kabisa akieleza upendo wa kijana mdogo. Aliandika Mithali wakati akiwa mkubwa akionesha hekima ya kijana wa makamo. Na aliandika Muhubiri katika miaka yake ya mwisho akionesha huzuni ya mtu mzee (linganisha. 12:1). Yamkini Muhubiri ni kitabu cha kumbukumbu za maombi ya toba ya makosa yaliyoandikwa katika 1 Wafalme 11. Kitabu cha Muhubiri kiliandikwa kabla ya kifo cha Sulemani na hata kabla ya mgawanyo wa ufalme wake miaka ya 931 K.K.[30]

**Nia na Makusudi:** Nia na makusudi ni maisha yasiyofaa mbele za Mungu. Katika kuendeleza nia na makusudi haya kuna mambo manne yameonekana:

Kwanza inaeleza kwamba maisha bila Mungu hayana maana, Sulemani anatafuta kuharibu ujasiri ulio katika mitazamo ya kibinadamu na hekima ya wanadamu; anaonyesha kwamba mitazamo yote ya mwanadamu au njia zinazoonekana kumfaa mwanadamu hazifai mbele za Mungu. Sulemani aliandika utupu wake aliokuwa nao ili apate kuwaeleza wasomi wake wapate kumtazama Mungu. Anaeleza kwamba maombi ya furaha hayawezi kukamilika kwa matakwa ya wanadamu katika maisha yao.

Pili Sulemani anasema wingi wa maisha hauwezi kueleweka ikiwa na maana ya kwamba tunapaswa kuishi kwa imani na si kwa kuona. Maisha yamejawa na matukio yasiyoelezeka. Kuna mambo mengi katika maisha ambayo mwanadamu hawezi kuyafanya lakini kwa imani tunaweza kukaa katika katika hekima kuu na kazi kuu ya Mungu. Kama katika kitabu cha Ayubu Muhubiri haimaanishi kwamba mwanadamu anazuiliwa lakini ni kwamba anahitaji aishi katika siri kubwa. Maisha ya duniani “maisha chini ya jua” hayawezi kusaidia. Katika mtazamo wa hili mwanadamu anapaswa kuwa na mtazamo ambao si wa kidunia anatakiwa amtazame Mungu akihofu na kumtumaini.

Tatu, Muhubiri inatuonesha mtazamo mzuri wa maisha yanayoshabihiana na Mithali. Inaonyesha kwamba maisha yanatofautina na mawazo ya Mithali. Methali 10:16 inaonesha kwamba uhuru ni kwa wanyonge na wa haki lakini Muhubiri 8:14 inaonyesha kwamba hili si tatizo na hasa si katika maisha haya. Je huku ni kuchanganya, hapana kwa ababu Methali inaonesha kwa ujumla kanuni za Mungu ikionesha kushindwa tunapoishi, katika ulimwengu wa dhambi. Muhubiri inaeleza kwamba kwa kuwa amri wa haki inakoma kama ilivyo katika Methali hivyo maisha si kitu kwa mwanadamu “chini ya jua” kwa mtazamo huu.

Nne, Sulemani inaonesha kwamba mwanadamu akiishi katika matakwa yake haitamfaidi kitu. Kitabu hakina maana ya kwamba maisha hayana majibu, kwamba maisha hayana maana au hayafai. Umuhimu na umaana unaweza kuonekana anaeleza, kwa kumuogopa Mungu. Migogoro hii inaweza kumalizwa na ushirika wetu wa karibu na Mungu.

**Watu Muhimu:** Sulemani

**Mwonekano wa Yesu katika Muhubiri:** Kwa kuwa Yesu ndiye njia ya mwanadamu kwa Mungu ambako mwanadamu anaweza kupata pumziko na furaha au maisha na maisha ya milele (Yohana 10:10; 7:37-38), na hivyo utupu huu wa maisha unaweza kukamilishwa na ushirika wetu na Mungu kwa njia ya ushirika wetu na Kristo. Umuhimu na uhakika wa wanadamu hupatikana kwa mwokozi tu.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi: Tatizo Linaelezwa (1:1-3)**

2. **Tatizo Linafafanuliwa (1:4–2:26)**
    a. Mapungufu ya Mzunguko wa Maisha (1:4-11)
    b. Mapungufu ya Hekima ya Mwanadamu (1:12-18)
    c. Mapungufu ya Utajiri ya Mwanadamu (2:1-11)
    d. Mapungufu ya Kuwa na Vitu (2:12-23)
    e. Mwisho: Furahi na Uwe Karibu na Msaada wa Mungu (2:24-26)

3. **Mungu anajua mpango wa Maisha (3:1-22)**
    a. Hufahamu Matukio ya Maisha Yetu (3:1-11)
    b. Hufahamu Hali ya Maisha (3:12-13)
    c. Huhukumu Yote (3:14-21)
    d. Mwisho (3:22)

4. **Mapungufu Mienendo ya Maisha (4:1–5:20)**
    a. Uovu (4:1-3)
    b. Mapungufu ya Kazi Nzito (4:4-12)
    c. Mapungufu katika Mambo ya Kisiasa (4:13-16)
    d. Mapungufu katika Dini za Kibinadamu (5:1-7)
    e. Mapungufu katika Utajiri wa Mwanadamu (5:8-17)
    f. Mwisho (5:18-20)

5. **Mapungufu ya Maisha kwa Ujumla (6:1-12)**
    a. Utajiri Hatuwezi Kuukamilisha (6:1-2)

b. Watoto Hawawezi Kukamilisha (6:3-6)
c. Kazi Haiwezi Kukamilisha (6:7-12)

6. **Ushauri (7:1–12:8)**
   a. Ushauri wa Mtazamo wa Mwanadamu (7:1-29)
   b. Ushauri katika Msaada wa Mungu (8:1–9:18)
   c. Ushauri kwa Yasiyofaa katika Maisha (10:1-20)
   d. Ushauri katika Mlolongo wa Maisha (11:1–12:8)

7. **Hitimisho (12:9-14)**

# Wimbo wa Sulemani
## (Furaha kwa Njia ya Umoja)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Sulemani ndiye mwandishi. Ametajwa mara saba (1:1, 5; 3:7, 9, 11; 8:11-12), na ameonyeshwa kama Bwana harusi. Mstari wa 1 unasema kwamba Sulemani aliandika wimbo huu vizuri kuliko zote alizoandika (1 Wafalme 4:32 inatuambia aliandika nyimbo 1,005). Elewa kwamba kitabu hiki hakisemi tu " Wimbo wa Sulemani" bali ni Wimbo ulio Bora ambao ni wa Sulemani."

Kuhusiana na jina la kitabu hiki Dr. Charles Ryrie aliandika:

> Kitabu hiki kimekuwa kikiitwa majina mengi: jina la kiebrania katika mstari wa kwanza, Wimbo ulio Bora ikiwa na maana ya kwamba wimbo bora, mzuri kuliko; na kiingereza umekiita kutoka katika msitari wa kwanza huo, wimbo wa Sulemani unaomuonesha mwandishi neno 'Wimbo' ni neno la Kilatini.[31]

**Muda wa Kuandikwa: 965 K.K.**

**Nia na Makusudi:** Wimbo wa Sulemani ni wimbo wa upendo uliosheheni ujumbe wa taswira ya Mungu ya upendo na ndoa: uzuri wa upendo huu wa mwili kati ya mwanaume na mwanamke. Kitabu kiko kwa namna ya igizo na mambo mengi yanayoonekana yameainishwa katika sehemu ya mambo muhimu.

Kitabu kiliandikwa mapema kati ya 965 K.K. Kwa wakati huu Sulemani alikuwa na wanawake 60 na masuria 80 (6:8), lakini baadaye katika maisha yake alikuwa na wanawake 700 na masuria 300 (1 Wafalme 11:3).

**Watu Muhimu:** Bwana harusi (Shulamite), Mfalme (Sulemani), na Korasi (Binti a Yerusalemu)

**Mwonekano wa Yesu katika Wimbo wa Sulemani:** Kitabu hiki kinaonesha upendo wa Yesu kwa wamuaminio.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Kichwa cha Habari (1:1)**

2. **Kuwa katika Upendo (1:2-3:5)**
   a. Hitaji la Bwana Harusi (1:1-8)
   b. Maelezo ya Upendo Uliokomaa (1:9-2:7)
   c. Safari ya Mfalme kwa Nyumba ya Bibi Harusi (2:8-17)
   d. Ndoto ya Kwanza ya Bwana Harusi ya Kutengana (3:1-5)

3. **Kuunganishwa katika Upendo (3:6-5:1)**
   a. Hatua za Ndoa (3:6-11)
   b. Sifa ya Uzuri wa Bibi Harusi (4:1-15)
   c. Ndoa (4:16-5:1)

4. **Jitihada katika Upendo (5:2-7:10)**
   a. Ndoto ya Pili ya Bwana Harusi ya Kutengana (5:2-7)
   b. Sifa ya Uzuri wa Bwana Harusi (5:8-6:3)
   c. Sifa za Uzuri wa Bibi Harusi (6:4-7:10)

5. **Kukua katika Upendo (7:11-8:14)**
   a. Nia ya Bwana Harusi ya Kutembelea Nyumba Yake (7:11-8:4)
   b. Safari (8:5-14)

# <u>Sehemu ya 4</u>
# Manabii Wakubwa

## Manabii wa Israeli Walivyotazamwa kwa Ujumla

**Utangulizi:** Katika utafiti wetu wa Agano la Kale tumeona "Vitabu vya sheria" vitabu vya "Kihistoria" vitabu vya "Mashairi" na sasa tunaanza sehemu ya mwisho inayojulikana "Manabii."

Manabii wametofautishwa kwa makundi ya Manabi wakubwa na Manabii wadogo. Vitabu vitano vya manabii wakubwa ni: Isaya, Yeremia, Maombolezo, Ezekieli na Danieli. Na vile kumi na mbili vya manabii wadogo ni: Hosea, Yoeli, Amosi, Obadia, Yona, Mika, Nahumu, Habakuki, Zephania, Hagai, Zekaria na Malaki.

Manabii hawa pia wanajulikana kama manabii waandishi kwa sababu waandishi wao waliandika maneno yao. Kulikuwa na unabiii wa mdomo kama vile wa Nathan, Ahija, Iddo, Jehu, Eliya, Elisha, Oded, Shemaya, Azaria, Hanani, Yahaziel, na Hulda ambao hawakuacha maandishi yoyote ya unabii wao.

**Waandishi:** Waandishi wa vitabu vya unabii wameelezwa kwa namna tofauti tofauti kulingana na asili ya huduma yao na wito. Waliitwa manabii, waonaji,walinzi, wajumbe, watu wa Mungu na watumishi wa Bwana.

Kusudi kuu la neno nabii maana yake ni mtu aliyepewa mamlaka ya kusema. Kwa hiyo nabii wa kweli ni yule anayezungumza kwa watu kwa niaba ya Mungu. Hii ni nzuri kulingana na maelezo ya unabii ulionakiliwa katika aya tatu za Agano la Kale: (1) Kutoka 6:28–7:2. Wakati Musa alipoteuliwa kuzungumza na Pharao na Mungu alimchagua Haruni awe nabii wa Musa na hii ina maana ya kwamba akaruhusiwa na kupewa mamlaka. Hii hufanyika mtu anapozungumza kwa ajili ya mwingine. (2) Hesabu 12:1-8. Haruni na Miriamu, yamkini nje na wivu aliangalia kuchukua nafasi ya Musa awe mpatanishi wa ufunuo wa Mungu na wao lakini Mungu hakupendezwa na hivyo aliamua kusema na Musa moja kwa moja na baadaye angelisema na wale walioitwa manabii kwa ndoto na maono na kwa hiyo maana ya nabii inaeleweka. (3) Kumbukumbu la Torati 18:9-22. kabla ya kifo cha Musa tunakua na tangazo la nabii katika kuendeleza mambo.[32] Mstari huu unafafanua vizuri kwamba nabii ni yule anayezungumza ujumbe wa kwanza kabisa ambao Mungu amemfunulia.

**Ujumbe Wao:** Kama msemaji wa Mungu jukumu la kwanza la nabii ilikuwa ni kusema ujumbe wa Mungu wa kwanza kwa watu kwa yale yaliyokuwa yakitukia katika historia kwa watu wa Mungu. Maana pana ya unabii inahusisha na kuhubiri mambo yanayofuatana na inaelezwa kuwa maneno ya kwanza. Maneno ya kwnza yanahusisha maono ya ndani ya mapenzi ya Mungu; ilikuwa ni muhimu, na ilitia changamoto kwa watu kutii. Kwa kulinganisha maneno ya utangulizi yanahusisha na kuona kwanza mpango wa Mungu, na ilikuwa ni ya kutabirika, na hata ilikuwa ni kuwatia moyo wenye haki kwa mtazamo wa ahadi ya Mungu au kuwatahadharisha na adhabu ijayo. Katika kutangaza ujumbe huu wa Mungu manabii walifunua yale yajayo mbele na hii ilikuwa ni sehemu ndogo sana ya ujumbe wa manabii. Nabii alikuwa ni mtu aliyechaguliwa na Mungu ambaye alipokea ujumbe wa Mungu na kuusema kwa mdomo au kwa vitendo au kwa kuuandika kwa watu. Kwa sababu hii, njia ya kawaida iliyotumiwa na manabii ilikuwa ni "Asema Bwana" .

Kwa msemaji wa Mungu ujumbe wao twaweza kuutazama katika aina tatu ya kazi waliyokuwa nayo kati ya watu wa Mungu katika Agano la Kale:

Kwanza walitenda kama Muhubiri ambaye alifundisha na kufafanua sheria ya Musa kwa taifa. Lilikuwa ni jukumu lao kuonya, kukaripia, kukemea, na kuwaepusha na hukumu, kuwarejesha katika kutubu na kuwapa faraja. Kazi yao ya kukemea dhambi na kuwarejesha katika kutubu ilikuwa ni muhimu sana katika muda wa nabii zaidi ya kazi yoyote. Ukemeaji ulifanyika nyumbani ukieleza adhabu ya Mungu aliyoikusudia kwa wale waliokuwa wakishindwa kutekeleza maneno ya nabii (Yona 3:4).

Pili walitenda kama watabiri waliokuwa wakitangaza adhabu inayokuja, ukombozi na matukio yanayohusiana na Masihi na ufalme wake. Utabiri wa yajayo haukuwa kwa ajili ya matakwa ya wanadamu bali ulikuwa umekusudiwa kufafanua kwamba Mungu anajua na anayeweza kuyatengeneza yajayo na kuwapa ufunuo wa makusudi. Unabii uliotolewa na nabii ulikamilika. Kushindwa kukamilika kwa unabii uliosemwa na nabii kulionesha kwamba amesema maneno yake mwenyewe na siyo maneno kutoka kwa YAHWE (Kumbukumbu la Torati 18:20-22). Katika 1 Samweli 3:19 inasema kwamba Bwana alikuwa naye na hakumwacha nabii wake ashindwe (Kimaandiko "kuanguka ardhini").

Tatu walitenda kama walinzi wa watu wa Isareli (Ezekieli 3:17). Ezekieli alisimama kama mlinzi katika kuta za Sayuni akiwa tayari kupiga tarumbeti kuwaonya dhidi ya uasi wa dini. Aliwaonya watu dhidi ya mambo ya kisiasa na jeshi na nguvu za kigeni na majaribu ya kujihusisha katika kuabudu miungu na hata Madhabahu ya Kanaani na hatari ya kuweka ujasiri mkubwa katika shughuli za dini.

Mwisho, kwa kuwa manabii walitenda kwa kuwasilisha ujumbe wa Mungu, walifanya jambo moja kubwa katika mfumo wa dini za Israeli. Manabii katika Israeli walitenda kama mawakili wakilionesha taifa juu ya ukiukaji wake wa Agalo la Musa.[33]

**Mlinganyo wa Manabii Wanne Wakubwa**[34]

| Mlinganyo wa Manabii Wanne Wakubwa | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Isaya** | **Yeremia** | **Ezekieli** | **Danieli** |
| Ilitabiriwa kwa: | Wayahudi katika Yudea | Wayahudi katika Yudea na watekwa | Watekwa wa kiyahudi katika Babeli | Watekwa wa Kiyahudi Babeli na mfalme mtakatifu |
| Kuhusiana na: | Yuda na Yerusalem (Isaya 1:1; 2:1) | Yuda na watu wake (Yeremia 1:5, 9-10; 2:1-2) | Nyumba yote ya Isareli (Ezekieli 2:3-6; 3:4-10, 17) | Israeli na taifa takatifu (Danieli 2:36-43; 9) |
| Wakati wa utawala wa: | Uzzia, Yotham, Ahazi, Hezekia (Mfalme wa Yuda) | Yosia, Yehoahaz, Yehoiakim, Yehoiakin, Zedekia (Wafalme) | Zedekiah (Mfalme wa Yuda); Nebukadneza (Mfalme wa Babeli) | Yehoiakim, Yehoiakin, Zedekia (Mfalme wa Yuda); Nebukadneza (Mfalme wa Babeli) |
| Muda: | 740-680 K.K. | 627-585 K.K. | 592-570 K.K. | 605-536 K.K. |
| Mambo ya Historia: | 2 Wafalme 15-21; 2 Nyakati 26-30 | 2 Wafalme 22-25 | Danieli 1-6 | Danieli 1-6 |

**Pitio la Agano la Kale katika Kumwonesha Kristo**[35]

Somo letu limeonesha kwamba sheria ilijenga msingi wa Kristo kwa kuchaguliwa (Mwanzo), Ukombozi (Kutoka), Utakaso (Mambo ya Walawi), uelekeo (Hesabu), na maelekezo (Kumbukumbu la Torati) ya taifa la Israeli kama mlinzi wa neno la Mungu (Warumi 3:1) na ukoo wa Masihi (Mwanzo 12:1-3; Warumi 9:4-5).

Maandalizi ya Kristo yalianza kwenye vitabu vya kihistoria kwa kulipa taifa nchi ya Isareli utawala wao (Yoshua). Taifa lilikuja kutawaliwa na mataifa mageni na haikuwa ni haki,mpaka Mungu alipoinua waamuzi na alipoona uaminifu katika taifa (Ruthu). Uimara ulikuwa katika taifa chini ya mfalme Sauli (1 Samweli), na kupanuka kwakwe chini ya Mfalme Daudi (2 Samweli), na utukufu wa taifa chini ya utawala wa Sulemani (1 Wafalme 1-10). Hii ilifuatiwa na mgawanyo katika taifa (1 Wafalme 11-22) katika makabila kumi ya kaskazini na makabila mawili ya kusini ya Yuda na Benjamini. Haya yote yaliharibu sana (2 Nyakati) iliyoleta mwishowe madhara ya kuhamishwa kwa wageni na Siria na Babeli (2 Wafalme). Hata hivyo hekalu liliingiwa na upungufu (1 Nyakati) na kuharibiwa (2 Nyakati). Hata hivyo haki ya Mungu ilibaki pale pale kwenye ahadi yake na hivyo hekalu likajengwa tena (Ezra) na kurudishwa kwa waliokuwa wabebaki katika taifa kwenda katika nchi yao (Nehemia) ikifuatiwa na ulinzi wa watu wa Mungu (Estha).

Katika vitabu vya mashairi kulikuwa na uvuvio wa Yesu na msingi wa maadili uliokuwa umewekwa katika sheria na kazi ya taarifa zlizokuwa zimeainishwa na kuendelezwa katika vitabu vya historia.

Vitabu vya unabii vinatazama mbele kwa tegemeo kubwa la Kristo. Hii inafanywa kama ifuatavyo:

> Manabii wa kwanza (Hosea, Yoeli, Amosi) zinatagemea Masihi kuliokoa taifa. Isaya na Mika walitabiri wokovu wa mataifa yote kwa njia ya Yesu anayekuja. Lakini Obadia, Yona, Nahumu, Habakuki na Sefania wanaonya juu ya dhuluma katika mataifa. Maombolezo inahuzunika juu ya dhuluma ya taifa na watu wake lakini Yeremia anatafuta ukamilishwaji wa Agano katika Kristo. Baada ya mateka wa babeli Hagai na Zekaria katika kujenga kwa jamii na maadili yao wanapomsubiri '***Jua la neema ambalo litaangaza na kuponya katika mbawa zake'*** (Malaki 4:2)."[36]

# Isaya

## (Wokovu wa YAHWEH)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama kitabu kinavyojieleza mwandishi ni Isaya mwana wa Amosi kiongozi wa utawala unaoonekana na kujitofautisha na jamaa za kiyahudi. Isaya anaonekana kuwa na ufahamu wa mahakama za kifalme na hata wakati wa utawala wa Ahazi. Alikuwa ni mtu msomi wa mambo ya kimataifa aliyetumia muda wake katika mji wa Yerusalemu ambako alikutana na wafalme na akawashauri juu ya mambo ya kigeni. Japo Isaya aliongozwa na Mungu alidharauliwa kwa sababu alipinga haki na nguvu za utawala wa kigeni (lwe Assiria au Misri). Kama alivyotahadharishwa na Bwana katika sura ya sita sababu zake

ziliangamizwa kabisa na serikali na hata watu walioamua kuweka imani zao katika mambo ya kisiasa ya wanadamu badala ya kumtegemea mtu wa uhakika na ambaye ni ahadi ya Mungu.

Desturi za kale zinaeleza kwamba aliuawa wakati wa utawala wa Manase kwa njia ya kukatwa msumeno (Webrania 11:37). Kwa kuwa amejaribu kuandika kifo cha Sennacherib katika Isaya 37:37-38, ni mbali sana kufikiri kwamba Isaya aliishi hadi baada ya kifo cha Sennacherib miaka ya 681 K.K.[37]

Jina hili Isaya limechukuliwa katika jina la mwanadamu mwandishi, ambaye kwa uongozi wa Roho Mtakatifu aliandika. Maana ya neno YAHWEH katika kiebrania ni wokovu, ambayo ni muhtasari wa kusudi la kitabu.

**Muda wa Kuandikwa: 740–680 K.K.** Isaya alikuwa na huduma ndefu sana iliyoanza 740 hadi 680 K.K. Huduma yake ilianza mapema kabisa mwishoni mwa utawala wa Uzia (790-739 K.K.) na ikaendelea hadi utawala wa Yotham (739-731 K.K.), Ahazi (731-715 K.K.), na Hezekia (715-686 K.K.). Tangu kusimama kwa wakuu wa watakatifu Isaya alitumika tangu nyakati za Tiglath-pileser (745-727 K.K.) hadi nyakati za Sennacherib (705-681 K.K.) wa Asiria.

**Nia na Makusudi:** Isaya alitoa kusudi la kitabu. “Wokovu ni wa YAHWEH.” Na hii ni dhahiri kwa ukweli kwamba neno “wokovu” linaonekana mara ishirini na sita zaidi ya manabii wengine waliojumuishwa. Kwa sababu ya hii Isaya amekua akiitwa “Nabii mwinjilisti” kwa sababu anasema mara nyingi sana kuhusu wokovu na kazi ya wokovu ya Masihi. Kwa kweli mengi yamesemwa katika kitabu hiki juu ya utu na kazi ya Masihi zaidi ya vitabu vyote katika Agano la Kale.

Kwa mtazamo mwingine Isaya ni kitabu kikubwa maana kina sura sitini na sita. Sura thelathini na tisa za kwanza zinashabihiana na vitabu vingine vya Agano la Kale zinazozungumzia kuja kwa Masihi, na sura ishirini na saba za mwisho zinashabihiana na vitabu ishirini na saba vya Agano Jipya kwa sababu zinazungumzia juu ya Masihi na mpango wake na ufalme wake kama mtumishi wa Mungu. Sura 1–39 zinazungumzia hitaji la mwanadamu juu ya wokovu na 40-66 zinaonesha wokovu wa Mungu katika Masihi na ufalme wake.

**Watu Muhimu:** Isaya nabii ni mwanadamu muhimu, lakini YAHWEH kwa namna fulani ametazamishwa kama mkuu wa Israeli, Mtakatifu wa Israeli na Bwana Mungu wa wote na ndiye mtegemewa mkuu wa kitabu cha Isaya.

**Mwonekano wa Yesu katika Isaya:** Hakuna kitabu katika Agano la Kale kilichomwonesha Yesu kwa ukamilifu na mapana kama Isaya. Isaya amemwonyesha Masihi katika mamlaka yake ya juu (6:1f), kuzaliwa na uanadamu wake (7:14; 9:6; 11: 1), katika huduma yake kwa njia ya Roho (11:2f), Asili yake ya Uungu (7:14; 9:6); Ukoo wake wa Daudi (11:1); kazi yake ya kuokoa kama wakili wetu (53), Huduma yake kama mwokozi mtumishi (49-52), na mengine mengi.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Unabii na Hukumu (1:1–39:8)**
   a. Unabii dhidi ya Yuda (1:1–12:6)
      1) Hukumu ya Yuda (1:1–5:30)

| | | |
|---|---|---|
| 1:1-9 | 2:12-22 | 5:1-7 |
| 1:10-17 | 3:1-12 | 5:8-30 |
| 1:18-31 | 3:13-26 | |
| 2:1-11 | 4:1-6 | |

      2) Kazi ya Mitume (6:1-13)

| | |
|---|---|
| 6:7 | 6:8-13 |

      3) Kuja kwa Masihi (7:1–12:6)

| | | |
|---|---|---|
| 7:1-9 | 8:9-22 | 10:20-34 |
| 7:10-16 | 9:1-7 | 11:1-10 |
| 7:17-25 | 9:8-21 | 11:11-16 |
| 8:1-8 | 10:1-19 | 12:1-6 |

   b. Unabii dhidi ya Watu wa Mataifa (13:1–23:18)
      1) Didi ya Babeli (13:1–14:23)

| | |
|---|---|
| 13:1-5 | 13:17-22 |
| 13:6-16 | 14:1-23 |

      2) Dhidi ya Ashuru (14:24-27)
      3) Dhidi ya Ufilisti (14:28-32)
      4) Dhidi ya Moabu (15:1–16:14)
      5) Dhidi ya Dameski na rRafiki Yake Israeli (17:1-14)
      6) Dhidi ya Ethiopia (18:1-7)

7) Dhidi ya Misri (19:1–20:6)

| | | |
|---|---|---|
| 19:1-10 | 19:11-25 | 20:1-6 |

8) Dhidi ya Babeli (21:1-10)
9) Dhidi ya Edom (21:11-12)
10) Dhidi ya Arabuni (21:13-17)
11) Dhidi ya Yerusalemu (22:1-25)
12) Dhidi ya Tiro (23:1-18)

c. Unabii wa Siku ya Bwana (24:1–27:13)
1) Hukumu ya Dhiki Kuu (24:1-23)
2) Furaha na Baraka za Ufalme (25:1–27:13)

| | |
|---|---|
| 25:1-12 | 26:11-21 |
| 26:1-10 | 27:1-13 |

d. Unabii dhidi ya Yuda (Ole na Baraka) (28:1–35:10)
1) Ole kwa Wasamalia (28:1-29)

| | |
|---|---|
| 28:1-13 | 28:14-29 |

2) Ole kwa Yuda (29:1–31:9)

| | | |
|---|---|---|
| 29:1-8 | 29:17-24 | 30:18-33 |
| 29:9-16 | 30:1-17 | 31:1-9 |

3) Tazama na Ufalme Wake (32:1-20)

| | |
|---|---|
| 32:1-8 | 32:9-20 |

4) Ole kwa Ashuru, Mwangamizi wa Yerusalemu (33:1-24)

| | |
|---|---|
| 33:1-12 | 33:13-24 |

5) Ole kwa Mataifa (34:1-17)
6) Tazama Ufalme Ujao (35:1-10)

e. Unabii dhidi ya Senakeribu. (36:1–39:8)
1) Dhihaka ya Ashuru (36:1-22)
2) Kweli Kutoka kwa Mungu (37:1-7)
3) Hofu Kutoka kwa Waashuru (37:8-35)

| | | |
|---|---|---|
| 37:8-13 | 37:14-20 | 37:21-35 |

4) Kipigo dhidi ya Waashuru (37:36-38)
5) Ugonjwa wa Hezekia (38:1-22)
6) Ujinga wa Hezekia (39:1-8)

**2. Unabii wa faraja (40:1–66:24)**

a. Unabii wa Ukombozi wa Israeli na Ukuu wa Mungu (40:1–48:22)

| | | |
|---|---|---|
| 40:1-20 | 43:8-13 | 45:8-25 |
| 40:21-31 | 43:14-21 | 46:1-13 |
| 41:1-20 | 43:22-28 | 47:1-15 |
| 41:21-29 | 44:1-8 | 48:1-16 |
| 42:1-13 | 44:9-20 | 48:17-22 |
| 42:14-25 | 44:21-28 | |
| 43:1-7 | 45:1-7 | |

b. Unabi wa Mkombozi wa Israeli; Wokovu wa Mtumishi Atabikae (49:1–57:21)

| | | |
|---|---|---|
| 49:1-13 | 52:1-15 | 56:1-12 |
| 49:14-26 | 53:1-12 | 57:1-21 |
| 50:1-11 | 54:1-17 | |
| 51:1-23 | 55:1-13 | |

c. Unabii wa Utukufu wa Israeli Ujao; Mpango wa Mungu wa Amani (58:1–66:24)

| | | |
|---|---|---|
| 58:1-12 | 61:1-11 | 65:1-16 |
| 58;13-14 | 62:1-12 | 65:17-25 |
| 59:1-8 | 63:1-6 | 66:1-2 |
| 59:9-21 | 63:7-14 | 66:3-9 |
| 60:1-14 | 63:15-19 | 66:10-24 |
| 60:15-22 | 64:1-12 | |

# Yeremia

## (Tahadhari dhidi ya Dhambi na Hukumu)

**Jina na Mtunzi wa Kitabu:** Kama ilivyo katika Isaya Kitabu hiki pia kinataja mwandishi wake kuwa ni Yeremia mwana wa Hilkia kutoka katika mji wa kikuani wa Anathan katika nchi ya Benjamin (1:1). Yeremia aliusema unabiii wake kwa baruku katibu wake. Yeremia anaitwa ni nabii wa Upweke (9:1; 13:17), au nabii wa peke yake kwa sababu alilazimishwa asioe (16:2). Pia anajulikana kama “nabii wa kulazimishwa” (1:6), lakini kwa uaminifu

alitangaza hukumu ya Mungu katika ufalme wa kusini wa Yuda japo alikutana na upinzani, kupigwa na kufungwa (11:18-23; 12:6; 18:18; 20:1-3; 26:1-24; 37:11–38:28).

Kitabu kilipata jina lake kutoka kwa mwandishi wake. Jina Yeremia lina maana ya “YAHWE hujenga.”

**Muda wa Kuandikwa: 627-585 K.K.** Yeremia aliishi muda mmoja na Zephania, Habakuki, Danieli na Ezekilei. Kazi yake ya unabii ilianza miaka ya 626 K.K. na ikaishia miaka ya 586. Na huduma yake iliendelezwa na ile ya Zephania. Kwa kuwa huduma yake ilianzia Babeli miaka ya 593 alikuwa amechelewa kwa huduma yake kubwa ya unabii katika Yerusalemu. Lini na kwa jinsi gani Yeremia alikufa haijulikani japo mila za kiyahudi zinasema Yeremia aliuawa wakati akiishi Misri (Webrania 11:37).

**Nia na Makusudi:** Makusudi mawili yanaonekana: (1) Tahadhari ya hukumu ya Mungu dhidi ya dhambi na (2) ujumbe wa tumaini na kurudishwa kwa taifa kama watatubu.

**Watu Muhimu:** Mtu wa muhimu kitabu chote ni Yeremia, mahubiri yake, upinzani na mateso.

**Mwonekano wa Yesu katika Yeremia:** Kuna sura nyingi katika Yeremia: Ameoneshwa kama msingi wa Chemchemi wa Maji Yaliyo Hai (2:13; linganisha Yohana 4:14), Msamaha wa Gileadi (8:22), Mchungaji Mwema (23:4), Tawi la Haki (23:5), na Bwana haki Yetu (23:6). Anaonekana kuwa ni yeye atakayeleta Agano Jipya (31:31-34).

Unabii mwingine katika Yeremia una matumizi mazuri ya umasihi. Laana ya Jehoakimu (Yekonia, Konia) ikimaanisha kwamba hakuna kizazi chochote kitakachomzidi katika ufalme (22:28-30). Mathayo 1:1-17 ukieleza uzazi wa Yesu kwa njia ya Sulemani na Rohaboamu kwa sheria zake (lakini kwa mwili wake) baba Yusufu. Hakuna mwana wa Yusufu atakayekaa katika kiti cha enzi cha Daudi,kwa maana atakuwa chini ya laana ya Yehoakimu. Luka 3:23-38. Tawi la Haki litatawala katika kiti cha enzi cha Daudi.[38]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Wito na Utume wa Yeremia (1:1-19)**
   a. Wito (1:1-10)
   b. Hakika ya Wito Wake (1:11-19)

2. **Unabi kwa Yuda (2:1–45:5)**
   a. Hkumu ya Yuda (2:1–25:38)
      1) Dhambi ya Yuda (2:1–3:5)
      2) Adabu ya Yuda (3:6–6:30)
         3:6-10 | 4:19-31 | 6:1-21
         3:11-25 | 5:1-13 | 6:22-30
         4:1-18 | 5:14-31
      3) Dini ya Uongo ya Yuda (7:1–10:25)
         7:1-34 | 9:1-26
         8:1-22 | 10:1-25
      4) Uvunjaji wa Agano la Mungu (11:1–13:27)
         11:1-17 | 12:1-6 | 13:1-11
         11:18-23 | 12:7-17 | 13:12-27
      5) Ukame wa Yuda (14:1–15:9)
         14:1-12 | 14:13-22 | 15:1-9
      6) Unabii wa Yuda Warudiwa (15:10–16:13)
         15:10-21 | 16:1-13
      7) Dhambi ya Yuda (16:14–17:27)
         16:14-21 | 17:1-18 | 17:19-27
      8) Yuda na Mwenye Mamlaka (18:1-23)
      9) Yuda kama Balasi lililovunjika (19:1–20:18)
         19:1-15 | 20:1-6 | 20:7-18
      10) Mfalme wa Yuda (21:1–23:8)
         21:1-14 | 22:13-30
         22:1-12 | 23:1-8
      11) Manabii wa Uongo wa Yuda (23:9-40)
      12) Mateka wa Yuda (24:1–25:38)
         24:1-10 | 25:12-31
         25:1-11 | 25:32-38

b. Migogoro ya Yeremia (26:1–29:32)
   1) Upinzani wa Yuda kwa Huduma ya Yeremia (26:1-24)

| | | |
|---|---|---|
| 26:1-6 | 26:7-15 | 26:16-24 |

   2) Mashauri ya Yuda Kutoka kwa Yeremia. Kuomba toba kwa Nebukadneza (27:1–29:32)

| | | |
|---|---|---|
| 27:1-22 | 28:1-17 | 29:1-32 |

c. Tumaini la Yuda Kuhusu Kurejeshwa (30:1–33:26)

| | | |
|---|---|---|
| 30:1-17 | 31:27-40 | 33:1-13 |
| 30:18-24 | 32:1-15 | 33:14-26 |
| 31:1-26 | 32:16-44 | |

d. Matukio Kablaya Kuanguka kwa Yerusalemu (34:1–38:28)

| | | |
|---|---|---|
| 34:1-22 | 36:20-26 | 38:1-16 |
| 35:1-11 | 36:27-32 | 38:17-28 |
| 35:12-19 | 37:1-10 | |
| 36:1-19 | 37:11-21 | |

e. Kunaguka kwa Yerusalemu (39:1-18)

| | |
|---|---|
| 39:1-10 | 39:11-18 |

f. Matukio Baada ya Kuanguka kwa Yerusalemu (40:1–45:5)

| | | |
|---|---|---|
| 40:1-16 | 42:1-22 | 44:20-30 |
| 41:1-10 | 43:1-13 | 45:1-5 |
| 41:11-18 | 44:1-19 | |

**3. Unabii kwa Mataifa (46:1–51:64)**

a. Unabii dhidi ya Misri (46:1-28)
b. Unabii dhidi ya Wafilisti (47:1-7)
c. Unabii dhidi ya Moabu (48:1-47)
d. Unabii dhidi ya Ammoni (49:1-6)
e. Unabii dhidi ya Edomu (49:7-22)
f. Unabii dhidi ya Dameski (49:23-27)
g. Unabii dhidi ya Arabuni (49:28-33)
h. Unabii dhidi ya Elamu (49:34-39)
i. Unabii dhidi ya Babeli (50:1–51:64)

| | | |
|---|---|---|
| 50:1-20 | 50:41-46 | 51:27-44 |
| 50:21-32 | 51:1-10 | 51:45-58 |
| 50:33-40 | 51:11-26 | 51:59-64 |

**4. Nyongeza ya Historia (52:1-34)**

a. Miungu ya Yerusalemu (52:1-23)
b. Miungu ya Watu Wengine (52:24-34)

# Maombolezo

## (Mto wa Machozi)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Mwandishi wa kitabu cha Maombolezo hakutajwa katika kitabu, lakini kuna mistari miwili inayoonyesha kwamba Yeremia ndiye mwandishi wa kitabu.

Kitabu ni “kwa jinsi gani” ambalo ni neno la kwanza linaloonekana katika 1:1, 2:1; na 4:1. Kwa sababu ya kichwa chake cha habari kinavyojieleza kitabu kunahusiana na desturi za kiyahudi kama “Maombolezo.”

**Muda wa Kuandikwa: 586 au 585 K.K.** Kitabu hiki kiliandikwa mapema kabisa baada ya kuharibiwa kwa Yerusalemu miaka ya 586 K.K na hivyo muda wa kitabu wa haraka kabisa yawezekana kuwa ni 586 K.K. Wengine husema kwamba yamkini kiliandikwa kati ya miaka ya 586 au 585 K.K.

**Nia na Makusudi:** Kusudi la kitabu hiki ni majuto au kilio cha maumivu yaliyojitokeza katika utawala wa kusini wa Yuda. Kinaeleza kuharibiwa kwa Yerusalemu na hekalu. Hukumu ya Mungu aliyoitangaza juu ya dhambi ya Yuda imekuja. Kusudi la pili ni hukumu ya dhambi. Kwa hiyo nabii alikuwa akieleza juu ya taifa hili kwamba anayo haki kuliangamiza na hivyo hawana budi kutafuta rehema zake kuepuka adhabu hii.

Michango mbalimbali ya nabii Yeremia imeonekana katika Yeremia na Maombolezo na hivyo twaweza kuvihusisha vitabu hivi kwani vinalandana:[39]

| Yeremia (tahadhari) Kusonga Mbele | Kushindwa na Kuharibiwa kwa Yerusalemu | Maombolezo (kilio) Kugeuka |
|---|---|---|

**Watu Muhimu:** Yeremia

**Mwonekano wa Yesu katika Maombolezo:** Maombolezo ina mambo mawili yanayomwonyesha Yesu: (1) Inamwonyesha kama mtu wa huzuni aliyejawa na simanzi kwa ajili ya kunyanyaswa na adui zake (1:12; 2:15-16; 3:14, 19, 30). (2) Yeremia anajutia kuharibiwa kwa Yerusalemu na hii yamkini ni picha ya Yesu ambaye aliililia Yerusalemu (Mathayo 23:37-38).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Kuharibiwa kwa Yerusalemu (1:1-22)**
    a. Maombolezo ya Nabii (1:1-11)
    b. Maombolezo ya Mji wa Yerusalemu (1:12-22)

2. **Hasira ya Bwana dhidi ya Watu Wake (2:1-22)**
    a. Hasira ya Mungu (2:1-10)
    b. Maombolezo ya Mwandishi (2:11-22)

3. **Mahangaiko ya Nabii (3:1-66)**
    a. Maombolezo Yake (3:1-18)
    b. Tumaini Yake (3:19-42)
    c. Mateso Yake (3:43-54)
    d. Maombi Yake (3:55-66)

4. **Watu wa Yerusalemu Walioshindwa (4:1-22)**
    a. Kuzingirwa kwa Mji (4:1-12)
    b. Sababu ya Kuzingirwa (4:13-20)
    c. Tumaini Lijalo (4:21-22)

5. **Maombi ya Kurejeshwa Tena (5:1-22)**
    a. Kukiri (5:1-18)
    b. Maombi (5:19-22)

# Ezekieli

### (Watanijua Kuwa Mimi ni YAHWEH)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Mwandishi ni Ezekieli kuhani, mwana wa Boazi ambaye alipokea wito wake kama nabii akiwa uhamishoni Babeli (1:1-3). Huduma yake kama nabii ilieleza mtazamo wa kikuhani na majukumu yake kwa hekalu, ukuhani, dhabihu na utukufu wa Mungu. Kinachojulikana kwa Ezekieli kinatoka katika kitabu chake Ezekieli. Alikuwa ameoa (24:15-18), akiishi katika nyumba yake akiwa na watu wenzake waliokuwa uhamishoni na walikuwa huru sana (3:24; 8:1).

Kama ilivyokuwa kwa Isaya na Yeremia kitabu cha Ezekieli kilipata jina lake kutoka kwa mwandishi wake Ezekieli inayomaanisha kwamba "Mungu hutuimarisha au tunaimarishwa na Mungu peke yake."

**Muda wa Kuandikwa: 593-571 K.K**. Kitabu cha Ezekieli kina nyakati nyingi ili kwamba unabii wake usipitwe na wakati bali uwe unaokwenda na wakati. Nyakati kuu na mbili kati ya 13 katika kitabu zinaeleza wakati Ezekieli alipopata ujumbe wake toka kwa Bwana. Tarehe nyingine ni kipindi alipofika mjumbe aliyeeleza kuangushwa kwa Yerusalemu (33:21). Alipata wito huu kama nabii mwezi wa Saba, 593 K.K., Ezekieli alidumu hadi miaka 22, na unabii wake wa mwisho ulipokelewa 571 K.K

**Nia na Makusudi:** Mtazamo wa Ezekieli uko katika hukumu (1-32) ya Israeli na faraja yake atakayoifanya Bwana wakati ujao (33-48).

**Watu Muhimu:** Ezekiel, mwana wa Boazi, kuhani aliyeitwa kuwa nabii wa Israeli kabla na baada ya mateka wa Babeli.

**Mwonekano wa Yesu katika Ezekieli:** Kristo, Masihi ameonekana kama tawi laini ambalo litapandwa katika mlima mrefu juu (17:23-24), picha sawasawa na ile ya Isaya (11:1), Yeremia (23:5; 33:15), na Zekaria (3:8: 6:12). Ezekieli pia anazungumza juu ya Masihi kama mfalme aliye na haki ya kutawala (21:26-27) na atakayetumika kama mchungaji mwema (34:11-31).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utume na Wito wa Ezekieli (1:1–3:27)**
   a. Ezekieli Autazama Utukufu wa Israeli Ezekiel (1:1-28)

| | | |
|---|---|---|
| 1:1-21 | 1:22-28 | |

   b. Ezekieli Atumwa Ujumbe wa Mungu (2:1–3:27)

| | | |
|---|---|---|
| 2:1-10 | 3:1-15 | 3:16-27 |

2. **Hukumu Iliyopo kwa Ajili ya Yerusakemu na Yuda (4:1–24:27)**
   a. Ishara Nne za Hukumu Ijayo (4:1–5:17)

| | | |
|---|---|---|
| 4:1-8 | 4:9-17 | 5:1-17 |

   b. Habai Mbili za Hukumu Ijayo (6:1–7:27)

| | | |
|---|---|---|
| 6:1-14 | 7:1-19 | 7:20-27 |

   c. Nabii Nne, kwa Njia ya Maono (8:1–11:25)

| | | |
|---|---|---|
| 8:1-18 | 10:1-22 | 11:14-25 |
| 9:1-11 | 11:1-13 | |

   d. Hukumu Kadha wa Kadha na Vyanzo Vyake (12:1–24:27)

| | | |
|---|---|---|
| 12:1-28 | 17:1-10 | 21:18-32 |
| 13:1-23 | 17:11-24 | 22:1-31 |
| 14:1-11 | 18:1-32 | 23:1-21 |
| 14:12-23 | 19:1-14 | 23:22-49 |
| 15:1-8 | 20:1-32 | 24:1-14 |
| 16:1-59 | 20:33-49 | 24:15-27 |
| 16:60-63 | 21:1-17 | |

3. **Unabii dhidi ya Wamataifa (25:1–32:32)**
   a. Dhidi ya Amoni (25:1-7)
   b. Dhidi ya Moabu (25:8-11)
   c. Dhidi ya Edomu (25:12-14)
   d. Dhidi ya Wafilisti (25:15-17)
   e. Dhidi ya Tiro (26:1–28:19)
   f. Dhidi ya Sido (28:20-26)
   g. Dhidi ya Misri (29:1–32:32)

| | | |
|---|---|---|
| 29:1-21 | 31:1-9 | 32:17-32 |
| 30:1-19 | 31:10-18 | |
| 30:20-26 | 32:1-16 | |

4. **Unabii wa Kurejeshwa Israeli (33:1–48:35)**
   a. Kurudi kwa Waisraeli katika Nchi Yao (33:1–39:29)

| | | |
|---|---|---|
| 33:1-20 | 36:1-21 | 37:24-28 |
| 33:21-33 | 36:22-38 | 38:1-23 |
| 34:1-10 | 37:1-10 | 39:1-24 |
| 34:11-31 | 37:11-14 | 39:25-29 |
| 35:1-15 | 37:15-23 | |

   b. Kurudiswa kwa Isareli katika Ufalme (40:1–48:35)

| | | |
|---|---|---|
| 40:1-4 | 44:1-14 | 47:13-23 |
| 40:5-49 | 44:15-31 | 48:1-9 |
| 41:1-26 | 45:1-6 | 48:10-20 |
| 42:1-20 | 45:7-25 | 48:21-22 |
| 43:1-12 | 46:1-18 | 48:23-29 |
| 43:13-17 | 46:19-24 | 48:30-35 |
| 43:18-27 | 47:1-12 | |

# Danieli

### (Mwisho wa Israeli)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama inavyoonekana (12:4) na kwa kutumia maneno yake "mimi" katika mstari wa 7:2 na kuendelea, Danieli ndiye mtunzi wa kitabu hiki. Akiwa kijana Danieli alichukuliwa kama mateka Babeli

miaka ya 605 K.K. na Nebukadnezza. Huko alikuja kuwa kiongozi katika mahakama ya Nebukadnezza na Dario. Japo hakutenda kama nabii lakini Kriso alimtambulisha kama nabii (Mathayo 24:15; Marko 13:14).

Kitabu kimetajwa baada ya mwandishi wake. Danieli inamaanisha "Mungu ni Hukumu" au Mungu ni Hukumu yangu".

**Muda wa Kuandikwa: 537 K.K.** Danieli iliandikwa kipindi cha mateka wa Babeli wakati Danieli na wenzake walipochukuliwa mateka huko Babeli miaka ya 605 K.K. baada ya Nebukadnezza kuishinda Yerusalemu.

**Nia na Makusudi:** Kusudi la kitabu cha Danieli ni uweza wa nguvu za Mungu ambaye anahukumu na kuharibu dunia iliyoasi na kwa uaminifu atawakomboa watu wake kulingana na imani zao kwake. Danieli iliandikwa ili kuwatia moyo wayahudi waliokuwa uhamishoni kwa njia ya nguvu za Mungu zinazoonekana.

**Watu Muhimu:** Watu muhimu ni Danieli ambaye alipelekwa Babeli kama kijana akatumika katika serikali na akaja kuwa msemaji mkuu wa Mungu kwa watakatifu na mataifa ya wayahudi; Shadrak, Meshak, na Abed-nego, na vijana wengine watatu zaidi waliokuwa wameteuliwa kwa mafunzo maalumu pamoja na Danieli (Majina yao walikuwa ni Hanania, Mishael, na Azaria.) Na watu wengine muhimu ni Nebukadneza, mfalme wa Babeli miaka ya 605 K.K.; Dario aliyemfanya Belshazzar kama mfalme; Cyrus; angel Gabriel; Michael, aliyetumika kwa Danieli, soma sura ya 10.

**Mwonekano wa Yesu katika Danieli:** Kitu muhimu katika Danieli kinachomwonyesha Yesu ni kwamba kuja kwa Masihi atakayeuawa (alama ya Msalaba; 9:25-26). Hata hivyo, Kristo ameoneshwa kama Jiwe kubwa atakayeuharibu utawala wa dunia hii (2:34, 45), mwana wa Mungu (7:13), mtu nyakati zote (7:22). Maono yamenakiliwa katika Danieli 10:5-9, na kweli yanamwonyesha Kristo (Ufunuo 1:12-16).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Historia Binafsi ya Danieli (1:1-21)**
   a. Uhamisho wake Babeli (1:1-7)
   b. Uaminifu Wake huko Babeli (1:8-16)
   c. Heshima Yake katika Babeli (1:17-21)

2. **Mpango wa Kinabii kwa Ajili ya Mataifa (2:1–7:28)**
   a. Ndoto ya Mfalme Nebkadneza (2:1-49)
      2:1-18 | 2:36-38 | 2:44-45
      2:19-30 | 2:39 | 2:46-49
      2:31-35 | 2:40-43
   b. Somo katika Imani (3:1-30)
      3:1-7 | 3:8-18 | 3:19-30
   c. Maono ya Nebkadneza Kuona Mti Mkubwa (4:1-37)
      4:1-3 | 4:19-27
      4:4-18 | 4:28-37
   d. Sherehe ya Belshaza na Mkono Unaoandika Uktani (5:1-31)
      5:1-12 | 5:13-29
   e. Ujinga wa Dario. Na Danieli katika Shimo la Simba (6:1-28)
      6:1-15 | 6:16-28
   f. Maono ya Danieli Kuhusu Dubu Wanne (7:1-28)
      7:1-8 | 7:13-14
      7:9-12 | 7:15-28

3. **Mpango wa Kinabii kwa Ajili ya Israeli (8:1–12:13)**
   a. Maono ya Danieli Kuona Kondoo, Mbuzi na Mapembe Madogo (8:1-27)
      8:1-8 | 8:15-19
      8:9-14 | 8:20-27
   b. Maono ya Danilei Kuhusu Majuma Sabini (9:1-27)
      9:1-19 | 9:20-23 | 9:24-27
   c. Unabii wa Danilei Kuhusu Matarajio ya Israeli (10:1–12:13)
      10:1-9 | 11:14-19 | 11:40-45
      10:10-21 | 11:20-28 | 12:1-4
      11:1-4 | 11:29-35 | 12:5-13
      11:5-13 | 11:36-39

# Sehemu ya 5
# Manabii Wadogo

**Neno "Manabii Wadogo":** Vitabu hivi kumi na mbili vinaitwa kwa kawaida Manabii wadogo. Neno hili wadogo lilitokana na karne ya nne B.K. manabii hawa ni wadogo kwa kigezo kwamba ni vitabu vifupi ukilinganisha na unabii wa Isaya, Yeremia, Ezekieli na Danieli wanaoitwa manabii wakubwa. Wakati wa Agano la Kale na Jipya ziliitwa "Sheria na manabii."

**Asili ya Unabii:** Asili ya unabii iko katika asili ya Mungu kwa taifa la Israeli ambalo kwalo mataifa yote yapate kubarikiwa. Wakati Mungu amewapatia Waisraeli sheria aliwaahidi kwamba kama watakuwa watiifu watakuwa ***"hazina yake Mungu"*** (hazina maalumu ya Mungu) kwa kusudi la kuwa "ufalme wa makuhani na taifa takatifu" kati ya mataifa yote (Kutoka 19:5-6 linganisha. Kumbukumbu la Torati 4:6-8). Kusudi hili halingeweza kutokea kama wangefuata njia na mapokeo ya mataifa mengine. Wakati wa maandalizi ya kuingia katika nchi yao kabla ya kifo cha Musa, kutofuata sheria na njia zisizofaa zilihusika sana katika mataifa ili kuharibu mambo mazuri yajayo na hata mapenzi ya Mungu. Hivyo hukumu ya Bwana ikaanza kupitia Musa (Kumbukumbu la Torati 18:9-14). Kwa hiyo ni kwa jinsi gani Mungu angeliweza kufahamika? Sheria na kweli zilitumika ili watu wapate kumfahamu Mungu na hii imeonekana katika Kumbukumbu la Torati 18:15-22, inasema,

> ***Bwana Mungu wako atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi. Msikilizeni yeye kama vile alivyotaka kwa Bwana Mungu wako huko Horebu siku ya Kusanyiko ukisema 'Nisikie tena sauti ya Bwana Mungu wangu wala nisiuoe tena moto huu mkubwa nisije nikafa' Bwana akaniambia wametenda vema kusema nilivyosema mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe nami nitatia maneno yangu kinywani mwake naye atawaambia yote nitakayomwamuru hata itakapokuwa mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu nitalitaka kwake lakini nabii atakayenena neno kwa kujikinai kwa jina langu ambalo sikumwagiza kulinena au atakayenena katika jina la miungu mingine nabii yule atakufa nawe ukisema moyoni wako tutajuaje neno asilolinena Bwana lisilofuate jabo wala kutimia hilo ndilo neno asilolinena Bwana kwa kujikinai amelinena huyo nabii usimwogope.***

Ufunuo huu unaleta asili ya Kibiblia na sababu ya manabii. Ili taifa lipate kutenda makusudi ya Mungu kama ilivyoelezwa katika agano la Ibrahimu (Mwanzo 12:1-3), aliwapa ahadi na tahadhari maalumu. Na hizi zimeelezwa katika Kumbukumbu la Torati 28-30 za baraka na laana katika sura hizi (wakati mwingine inahusika na agano la Parestina). Ikiwa watatii kuna baraka lakini kama hawatatii kuna laana. Je manabii wanahusika vipi hapa, watakuja na kusema, ***"Kwa kuwa umetengua agano, laana imekuwa juu yako au inakuijia."*** Kwa maneno mengine, imekwisha kutukia au inataka kutukia kama Bwana alivyokuonya katika Kumbukumbu la Torati 28-30. Unabii wa ujumbe wa dhambi na hukumu ni lazima uonekane katika historia hii na ieleweke katika Agano la Kale.

Manabii hawakutahadharisha tu bali walitoa ujumbe wa wokovu pia wa utukufu wa Bwana ajaye. Kwa undani kabisa kusudi la Mungu litakamilishwa na kazi ya mamlaka ya Mungu katika maisha ya watu wake. Wakati mwingine ujumbe huu wa wokovu unaeleza matukio fulani yaliyooonekana katika maono (Danieli 9:24-27 na majuma sabini). Wakati mwingine walikuwa wakitangaza ahadi ya Mungu kwa watu kama vile Ibrahimu na Daudi.

**Mwonekano wa Manabii Wadogo Kimaandiko:** Tunaposoma kuhusu manabii tunaona kwamba wana sifa za kufanana: (1) Tahadhari ya hukumu kwa sababu ya dhambi ya taifa; (2) maelezo ya dhambi; (3) maelezo ya hukumu ijayo; (4) wito wa kutubu; na (4) ahadi ya ukombozi.

Sababu za kutambua vitabu vya unabii ni kufahamu jinsi kilivyoanza na jinsi kilivyoishia.[40] Manabii walianza kwa neno kama hili "hiki ndicho Bwana anasema …" na waliishia na kielelezo au neno hilo hilo.

**Mfuatano wa Vitabu Hivi:**

**Mpango wa Manabii Wadogo katika Biblia ya Kiingereza:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Hosea | 4. Obadia | 7. Nahumu | 10. Hagai |
| 2. Yoeli | 5. Yona | 8. Habakuki | 11. Zekaria |
| 3. Amosi | 6. Mika | 9. Zephania | 12. Malaki |

**Makundi Yao Kulingana na Uhamisho na Ufalme wa Israeli na Yuda:**

| Kundi | Kitabu | Tarehe zinazofikiriwa (K.K.) |
|---|---|---|
| **KABLA YA UHAMISHO:** Manabii wa Israeli | Yona<br>Amosi<br>Hosea | 793-753<br>760<br>755-715 |
| Manabii wa Yuda | Obadia<br>Yoeli<br>Mika<br>Nahumu<br>Zephania<br>Habakuki | 840<br>835-796<br>700<br>633-612<br>630-625<br>600 |
| **BAADA YA UHAMISHONI:** Unabiiwa waliorudi kutoka uhamishoni | Hagai<br>Zekaria<br>Malaki | 520<br>520-518<br>450-400 |

# Hosea

## (Upendo wa Uvumilivu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama ilivyojieleza katika mstari wa 1 mwandishi ni Hosea mwana wa Beeri na mme wa Gomeri (1:3). Alikuwa ni raia wa Israeli ya kaskazini na yeye alikuwa katika utawala wa kaskazini na alimwita mfalme wa Samaria "mfalme wetu" (7:5). na wote tunafahamu kuhusu Hosea na tunasoma katika kitabu chake.

Kitabu kimejitaja baada ya mwandishi wake, ambaye Hosea yuko umri sawa na mfalme wa mwisho wa ufalme wa kaskazini Hoshea. Kusudi la utofauti Biblia imetupa jina la nabii mdogo kama Hosea. Kitu cha kufurahisha majina Hosea,Yoshua na Yesu yote yamepatikana kutoka maneno ya kiebrania, *HOSHEA*, yanayomaanisha "wokovu" Hata hivyo majina yote mawili Yoshua na Yesu yanaongeza maana nyinge kwamba "YAHWE ni wokovu". Kama mjumbe wa Mungu, Hosea anatoa wokovu katika taifa kama wataacha kuabudu miungu yao na kumrudia Bwana.

**Muda wa Kuandikwa: 755-715 K.K.** Kulingana na Hosea 1:1, Hosea alitumika kipindi cha Mfalme Uzia (767-739 K.K.), Yothamu (739-731 K.K.), Ahazi (731-715 K.K.), na Hezekia (715-686 K.K.), waliokuwa ni wafalme wa Yuda. Na pia alitumika kipindi cha Yeroboamu II (782-752 K.K.), mfalme wa Israeli.

Huduma ya Hosea ilidumu kwa milongo kadhaa, ikianzia karibu kabisa na mwisho wa utawala wa mfalme Uzia wa Yuda (790-739 K.K.) na Yeroboamu II wa (793-753 K.K.) na kuishia mwanzoni kabisa mwa utawala wa Hezekia. Sheria ya Barua zilianza mnamo miaka ya 715 K.K. baada ya utawala wa mwingiliano (kutawala kwa wakati mmoja) na baba yake Ahazia. Kwa kuwa Isareli walikuwa ni watu wa Hosea, inaonekana kuwa ni ngeni kwamba wafalme wanne wa Yudea lakini mfalme wa Isareli wametajwa katika 1:1. Sababu ya kuwaondoa wafalme sita wa Israeli waliomfuata Yeroboamu II hijulikani. Pengine inaweza kuwa ni mambo ya asherati kama ilivyokuwa kwa Daudi (3:5) na pia mambo ya kuanguka kwa (zile ngome mbili) za utawala wa Kaskazini (7:3-7).[41]

Labda hawa wafalme sita wa Israeli waliomfuatia Yerobomu II walifutwa kwa sababu ya mahusiano yao mabaya yaliyoendelezwa na dhambi mbaya ya Yeroboamu wa 1 mwana wa Nebat. Katika utawala hapakuwa na mfalme katika ufalme wa kaskazini aliyetenda kama ufalme wa kusini.

**Nia na Makusudi:** Hosea iliandikwa kueleza ustahimilivu au upendo usioshindwa wa Mungu kwa waisraeli pamoja na kutoamini kwao. kwa njia ya uzoefu wa ndoa wa Hosea kitabu kinatuonesha moyo wa kupenda na huruma ya Mungu anayetamani kutubariki watu wake kwa maarifa yake na sisi sote tumfahamu kwa undani zaidi ili amaanishe kwetu. Kwa kutunza kusudi hili nia ya Hosea ni ushuhuda wenye nguvu dhidi ya ufalme wa kaskazini kwa kutokuwa waaminifu katika agano lake la mahusiano na Bwana kama ilivyoeleza kwa upana katika maisha ya binafsi na hata ya watu wote. Nabii anataka watu wake watubu na warejee katika uvumilivu wao na upendo wa Mungu. Hii inaoneshwa kwa njia ya upendo imara wa Mungu kwa Waisraeli kama watoto wake wapendwa na kama mke wake wa Agano.

**Watu Muhimu:** Hosea, Gomeri na Yehu, mfalme wa Israeli.

**Mwonekano wa Yesu katika Hosea:** Katika Hosea Masihi anaoneshwa kama Mwana wa Mungu (11:1 linganisha Mathayo 2:15), kama mwokozi wa watu wake (13:4 linganisha Yohana 14:6), kama mmoja

atakayetuokoa na mauti (13:14 linganisha. 1 Wakorintho 15:55), kama mmoja atupendaye kwa kutuhurumia (11:4), kama aponyaye wale wamrudiao (6:1).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi. (1:1)**

2. **Ndoa ya Hosea: Mwonekano wa Mungu Atakavyohusika na Waisraeli (1:2–3:5)**
   a. Asili ya Unabii wa Hosea katika Jamaa Yake (1:2–2:1)
      1) Ndoa ya Hosea: Waisraeli Kutokuwa na Uaminifu (1:2-3a)
      2) Watoto wa Hosea: Hukumu ya Israreli (1:3b-9)
      3) Mtazamo wa Baadaye wa Isareli: Kurejeshwa (1:10-2:1)
   b. Kurejeshwa kwa Njia ya Adhabu (2:2-23)
      1) Adhabu ya Bwana kwa Israeli (2:2-13)
      2) Urejesho wa Bwana wa Waisraeli (2:14-23)
   c. Kurejeshwa kwa Ndoa ya Hosea (3:1-5)
      1) Amri ya Mungu (3:1)
      2) Utii wa Hosea (3:2-3)
      3) Mfano Unaelezwa (3:4-5)

3. **Ujumbe wa Hosea: Hukumu na Kurejeshwa kwa Israeli (4:1–14:9)**
   a. Hukumu ya Bwana dhidi ya Israeli (4:1-6:3)
      1) Ghadhabu ya Israeli Yadhihirishwa (4:1-19)
         4:1-3 4:7-10 4:15-19
         4:4-6 4:11-14
      2) Hukumu ya Isareli Yatangazwa (5:1-14)
         5:1-7 5:8-15
      3) Kurudi kwa Israeli Kwatabiliwa (6:1-3)
   b. Ghadhabu ya Bwana juu ya Israeli Yaongezeka (6:4–11:11)
      1) Adhabu ya Isareli (6:4–8:14)
         6:4-11 7:8-16 8:8-14
         7:1-7 8:1-7
      2) Adhabu na Hukumu ya Israel; I Yaelezwa Tena (9:1–11:7)
         9:1-6 9:15-17 10:11-15
         9:7-9 10:1-2 11:1-4
         9:10-14 10:3-10 11:5-7
      3) Huruma ya Bwana Yarejea Tena (11:8-11)
   c. Ghadhabu ya Bwana dhidi ya Isareli Yathibitishwa (11:12–14:9)
      1) Hitimisho la Mashitaka (11:12–13:16)
         11:12–12:11 13:1-3 13:9-11
         12:12-14 13:4-8 13:12-16
      2) Hutimisho la Furaha (14:1-9)
         14:1-3 14:4-7 14:8-9

# Yoeli

### (Siku Ijayo ya YAHWEW)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama ilivyooneshwa na 1:1, mwandishi ni Yoeli inayomaanisha "YAHWE ni Mungu" hatujui lolote kuhusu yeye zaidi ya jina la baba yake, Pethuel (1:1). Jina hili linalingana kabisa na ujumbe wa Yoeli linalolala na kuleta mtazamo wa kwamba Mungu kama mwenye mamlaka aliye na uumbaji wote na mataifa yote yako chini yake na kama Mungu wa Historia.

**Muda wa Kuandikwa: 835-796 K.K.** Japo tarehe hazijaainishwa katika Kitabu tunapaswa kutafakari tarehe kama iwezekanavyo kutoka katika uthibitisho wa ndani tunaouona katika kitabu na tuunganishe na matukio. Watu wanafikiri tarehe za 835-400 K.K., lakini kufikiri tarehe ni vigumu. Tumesema tarehe za 835-796 K.K. kulingana na uhusiano wake na Tiro, Sidon, Ufilisti, Misri na Edomu kama maadui (3:4, 19). Hawa walikuwa ni maadui wa kwanza kabisa wa ufalme wa Kusini kabla ya uhamishoni Babeli. Na baada ya uhamisho wao adui zao walikuwa ni Waashuru, Wababeli na Pesia.

**Nia na Makusudi:** Yoeli anatumia ukame na nzige zilizoshambulia Yuda bila kutahadharisha kwamba ni somo la kujihadhari na ubatilifu ujao wa Israeli katika siku za YAHWE. Kwa muda mfupi sana jambo la muda kila kipande cha mmea kitashambuliwa. Kama taifa litatubu na kurudi kwa Bwana na Bwana atarejesha uhusiano

wake na kuwabariki Israeli. Hii ilikuwa ni kweli katika mazingira ya historia ambamo Yoeli alikuwa akiandika na alikuwa kweli kwa wakati wowote ule ujao.

Kwa baraka za mwisho na urejeshwaji uliotabiriwa na Yoeli Wayahudi wanatakiwa kuona adhabu ya mateso na umwagaji wa Roho wa Mungu. Huu ni muungano utakaowafanya warudi kwa Bwana.

**Watu Muhimu:** Yoeli

**Mwonekano wa Yesu katika Yoeli:** Katika Yoeli Kristo ameoneshwa kama mmoja atakaye mwaga Roho Mtakatifu (2:28 linganisha. Yohana 16:7-15; Matendo 1:8), anayehukumu mataifa (3:2, 12), na mambo yake ni mkimbizi na nguzo ya Israeli (3:16).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Historia ya Siku ya Bwana (1:1-20)**
   a. Matukio ya Histori ya Nzige (1:1-12)
      1:1-3 1:4-7 1:8-12
   b. Matukio ya Historia ya Ukame. (1:13-20)

2. **Siku ya Kinabii ya Bwana (2:1–3:21)**
   a. Siku ya Bwana (2:1-27)
      1) Unabii wa Uvamizi wa Yuda (2:1-11)
      2) Hali Inayohitajika kwa Ajili ya Yuda (2:12-27)
         2:12-17 2:18-20 2:21-27
   b. Siku ya Bwana (2:28–3:21)
      1) Matukio ya Mwisho kabla ya Siku ya Bwana (2:28-32)
      2) Matukio ya Siku ya Bwana. (3:1-21)
         3:1-8 3:9-17 3:18

# Amosi

### (Adhabu ya Matumizi Mabaya ya Fursa Nzuri)

**Jina na Mtunzi wa Kitabu:** Tofauti na Isaya (aliyekuwa mtu wa mahakama) na Yeremia (aliyekuwa kuhani). Kitabu hiki kiliandikwa na Amosi (1:1; 7:14). Alikwa ni mtu kutoka Teko iliyokuwa karibu na Bethlehemu kama maili kumi kusini mwa Yerusalemu. Japo alikuwa ni mkulima na mfugaji lakini alilielewa vizuri neno la Mungu.

Jina Amosi ni neno la kiebrania linalomaanisha “mzigo” au “mbeba mzigo.” Hii inalingana kabisa na mzigo aliopewa. Japo Amosi alitokea ufalme wa kusini na si ufalme wa kaskazini alipewa mzigo wa kubeba ujumbe wa kuonya dhidi ya ulafi, dhuruma, ulimwegu na ubinafsi wa ufalme wa kaskazini. Amosi isichanganywe na Amoz, baba yake Isaya (Isaya 1:1).

**Muda wa Kuandikwa: Kati ya 760 K.K.** Kulingana na mstari wa 1, Amosi anatuambia kwamba alikuwa rika la Uzzia na Yeroboamu II na alitabiri (790-739) ***“Siku za Uzia mfalme wa Yuda na siku za Yeroboamu mwana wa Yoashi mfalme wa Israeli*** (793-753) ***miaka miwili kabla ya tetemeko la ardhi,”*** (1:1). Amosi yamkini alitabiri kipindi cha 767-753 K.K. Pia tunaambiwa kwamba alitabiri ***“miaka miwili kabla ya tetemeko la ardhi,”*** lakini kwa hakika tarehe au wakati wa kuandikwa kwake haujulikani.

**Nia na Makusudi:** Ujumbe uliotolewa kwa Amosi kusudi lake ni adhabu japo unaishia na maneno ya matumaini. Amosi alitahadharisha kwamba Bwana Mungu mtawala mwenye mamlaka wa ulimwengu atakuja kama mshindi kuhukumu mataifa yaliyoamua kuasi mamlaka yake. Isareli nayo pia itaadhibiwa kwa kuasi kwake agano la Mungu. Amosi alikuwa akitoa na kueleza makabila ya kaskazini yaliyokuwa chini ya Yeroboamu watubu kama njia pekee ya kuiepuka hukumu hii. Kwa kuendelea kitabu kinaeleza hasira ya Mungu juu ya maovu kwamba haki yake ni lazima itendeke dhidi ya dhambi ya Israeli kwa sababu hapendi iendelee bila kuadhibiwa.

Hata kama taifa litakuwa limeharibiwa Mungu ataacha kundi dogo la Waisraeli wale watakaokuwa wamekubali kutubu. Siku moja kundi hili dogo litakuwa rimerejeshwa katika agano lake la baraka wakati huo Bwana atakapokuwa anayachukua na mataifa mengine.

**Watu Muhimu:** Amos, Uzia, Mfalme wa Yuda, Yeroboam, Mfalme wa Israeli

**Mwonekano wa Yesu katika Amosi:** Amosi anamwakilisha Yesu Kama mtu atakayejenga ukoo wa Daudi (9:11) na kama mtu atakayewaokoa watu wake (9:11-15).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utanglulizi: Utunzi na Nia (1:1-2)**

2. **Hukumu Nane za Amosi (1:3–2:16)**
   a. Kuhusu Dameski (1:3-5)
   b. Kuhusu Wafilisti (1:6-8)
   c. Khusu Tiro (1:9-10)
   d. Kuhusu Edomu (1:11-12)
   e. Kuhusu Ammon (1:13-15)
   f. Kuhusu Moabu (2:1-3)
   g. Kuhusu Yuda (2:4-5)
   h. Kuhusu Israeli (2:6-16)

3. **Hotuba ya Amosi (3:1–6:14)**
   a. Isreli (3:1-15)
      3:1-8 3:9-10 3:11-15
   b. Ufisadi wa Isareli (4:1-13)
      4:1-3 4:4-5 4:6-13
   c. Wimbo wa Mazishi juu ya Isareli (5:1–6:14)
      1) Utawala wa Israeli na Hukumu Yao (5:1-17)
         5:1-3 5:8-9 5:14-15
         5:4-7 5:10-13 5:16-17
      2) Maonyo ya Watu wa Dini (5:18-27)
         5:18-20 5:21-24 5:25-27
      3) Kukemewa kwa Taifa Zima (6:1-14)
         6:1-3 6:8-11
         6:4-7 6:12-14

4. **Maono Matano a Amosi (7:1–9:10)**
   a. Maono ya Nzige (7:1-3)
   b. Maono ya Moto (7:4-6)
   c. Mono ya Kipimo cha Mstari (7:7-9)
   d. Upinzani wa Kuhani wa Betheli (7:10-17)
   e. Maono ya Kikapu cha Matunda ya Kiangazi (8:1-14)
   f. Maono ya Hukumu ya Bwana (9:1-10)

5. **Ahadi tano za Kurejeshwa kwa Isareli (9:11-15)**

# Obadia

### (Haki ya Mashairi)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Mtunzi ni nabii wa Yuda ambaye hajulikani kwa jina la Obadia (1:1). Jina lake lina maanisha “Mtumishi wa YAHWEH.”

Watu wengi wa agano la kale waliitwa Obadia. Hii inahusisha na mkuu wa jeshi la Daudi (1 Nyakati 12:9), mtumishi wa ahabu aliyefanya unabii wa Mungu (1 Wafalme 18:3), mlawi enzi za Yosia (2 Nyakati 34:12), na kiongozi aliyerejea kutoka uhamishoni na Ezra (Ezra 8:9). Hakuna kinachojulikana kuhusu mji wa Obadia au jamaa na kweli kwamba na hata baba yake hajatajwa ni kwa sababu hakuwa katika ukoo au ukuhani wowote.

**Muda wa Kuandikwa Kitabu: 840 K.K.** Kitabu kifupi katika Biblia, kina mistari 21 tu zinazoleta utofauti na ugumu katika kufahamu tarehe zake. Tunakadiria kuwa ni 840 K.K. kulingana na unabii wake kwa Edomu na Wafilisti na Waarabu inayoonekana kuwa ni kipindi cha utawala wa Yehoramu tangu 848-841 K.K. (2 Nyakati 21:16-17).

**Nia na Makusudi:** Kusudi la Obadia ni kwamba majivuno yataharibiwa kabla ya anguko. Obadia anaeleza kwamba Edomu itahukumiwa kwa sababu ya majivuno yake ya kufurahia maovu yaliyokuwa yakitokea Yerusalemu.

**Watu Muhimu:** Obadia

**Mwonekano wa Yesu katika Obadia:** Kristo anaonekana katika kitabu cha Obadia kama hakimu wa mataifa (15-16), mwokozi wa Israeli (17-20), na mmiliki wa Ufalme (21).[42]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Unabii wa Hukumu juu ya Edomu (1:1-9)**
   a. Hukumu (1:1-4)
   b. Mwisho wa Hukumu (1:5-9)

2. **Msigi wa Hukumu ya Edomu (1:10-14)**
   a. Kutopendana (1:10)
   b. Kutotii (1:11-12)
   c. Kwa Ajili ya Ukali (1:13-14)

3. **Wakati wa Hukumu (1:15)**

4. **Matokeo ya Hukumu (1:16-18)**

5. **Kukombolewa kwa Israeli (1:19-21)**

# Yona

## (Kukimbia Mpango wa Mungu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Mwandishi wa kitabu hiki ni Yona mwana wa Amitai nabii kutoka Galilaya katika ufalme wa kaskazini wa Israeli. Na hii imethibitishwa na kitabu chenyewe (1:1), historia ya kitabu inayoeleza sehemu halisi na watu na mambo mengine (2 Wafalme 14:25) pamoja na ushuhuda wa Yesu katika Agano Jipya (Mathayo 12:40). Jina lake linamaanisha "huwa."

**Muda wa Kuandikwa: 793-753 K.K.** Katika 2 Wafalme 14:27 Yona anahusishwa na utawala wa Yeroboamu II wa Israeli (793-753 K.K.). Yona alitumika baada ya Elisha na kabla ya Amosi na Hosea.

**Nia na Makusudi:** Yona anaeleza kwamba Mungu wa Waebrania (1) anahusika na ulimwengu wote kwa wokovu wa wote wanaotubu na kumrudia, (2) Ana mamlaka kwa kila kitu na kwa mambo yote ya mwanadamu na (3) mitazamo isiyo ya upendo kwa marika mabalimbali yaweza kutufanya tutengane na mapenzi ya Mungu.

**Watu Muhimu:** Yona

**Mwonekano wa Yesu katika Yona:** Kitabu chote cha Yona Kristo ameonyeshwa katika ufufuko wake (Mathayo 12:40), kama nabii kwa mataifa na mwokozi. Katika maisha ya Yona Kristo amedhihirishwa kama Mwokozi na Bwana (2:9).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Kukimbia kwa Yona (1:1-17)**
   a. Sababu ya Kukimbia (1:1-2)
   b. Safari ya Kukimbia Kwake (1:3)
   c. Matokeo ya Kukimbia Kwake (1:4-17)

2. **Maombi ya Yona (2:1-10)**
   a. Sifa za Maombi Yake (2:1-9)
   b. Majibu ya Maombi Yake (2:10)

3. **Mahubiri ya Yona (3:1-10)**
   a. Amri ya Mungu (3:1-3)
   b. Mambo Yaliyomo katika Mahubiri ya Yona (3:4)
   c. Matokeo ya Mahubiri ya Yona (3:5-10)

4. **Kujifunza kwa Yona (4:1-11)**
   a. Malalamiko ya Yona Mbele za Mungu (4:1-3)
   b. Utaratibu wa Mungu kwa Yona (4:4-11)

# Mika
## (Ni Nani kama Mungu?)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kitabu kimepata jina lake toka kwa Mwandishi wake nabii Mika. Ni kidogo sana kinachojulikana kuhusu mwandishi huyu zaidi ya kile ambacho unaweza kujifunza kutoka katika kitabu hiki na katika Yeremia 26:18. Jina la Mika limefupishwa toka katika jina la Mikaya linalo maanisha kwamba ni nani kama Yahweh? na Mika ameandika ukweli huu katika 7:18 aliposema, ***"nani Mungu kama wewe"*** Nyakati za Yeremia wazee walimwandika Mika 3:12 ili kulinda ujumbe wa Yeremia kuhusu hukumu katika taifa (Yeremia 26:18).

Mika alikuwa anatokea Moresheth (Mika 1:1 linganisha. 1:14), mji wa Yudea kama maili 25 kusini magharibi mwa Yerusalemu karibu na mji wa Wafilisti Gatha. Moresheth ilikuwa katika milima ya rutuba ya Yudakaribu na lakishi, mji wa biashara ya kimataifa.

**Muda wa Kuandikwa: 700 K.K.** Mika anatueleza katika mstari wa 1 kwamba alitabiri kipindi cha Yothamu (750-732 K.K.), Ahazi (736-716 K.K.) na Hezekia (716-687 K.K.). Mika alikuwa akizungumza na Yuda lakini wakati huo huo alizungumza na ufalme wa kaskazini wa Israeli na akatabiri kuanguka kwa Samaria (1:6), sehemu nzuri ya huduma yake ilitokea kabla ya mateka wa Assiria 722 K.K., yamkini kati ya 700 K.K.

**Nia Na Makusudi:** Mika anaonesha jinsi watu walivyoshindwa kuishi katika hali ya agano ambalo Mungu amelifanya na Israeli ambalo kulikuwa na baraka kama wangetii (Kumbukubu la Torati 28:1-14), na laana kama wasingetii na halafu kuondolewa katika nchi ya ahadi (Kumbukumbu la Torati 28:15-68). Katika kuendelea Mika anaonesha kukosekana kwa haki ya Yuda na anaeleza haki na uhuru wa YAHWEH na anaonyesha kwamba alikuwa katika kuwaadibisha. Alileta utawala dhidi ya Israeli na Yuda kwa ajili ya dhambi kama ukandamizwaji, kutoelewana, uongo, majivuno na hata ukiukaji wa sheria. Kuwaadibisha huku kwa taifa kunaeleza upendo wa Mungu kwao na kwamba anaweza.

Kusudi katika kila sura limetofautiana lakini pia anaeleza kweli ya kukombolewa. Mika pia anaeleza juu ya wageni kwa kila sura yake (Mika 2:12; 4:7; 5:7-8; 7:18). Anaeleza kwamba siku zijazo YAHWE atawakomboa watu wa Israeli na kuwapeleka katika nchi yao ya ahadi baada ya Masihi kuja.

Sehemu ya mwisho ya Mika inaeleza juu ya mahakama ya Mungu. Mungu anayo ghadhabu juu ya watu wake na amekusanya milima na mabonde kutengeneza baraza anapokuwa akihukumu. Watu wamegeukia njia zao wenyewe na wakifikiri kwamba Mungu anapendezwa na tamaa zao. Wameacha ukuu wa Mungu wa haki katika maisha yao ya kila siku na wamefuata mambo yao. Wameshindwa kuelewa kile Mungu anachokitaka kwa mwanadamu. Na hivyo Mungu lazima "agadhabike."

Kitabu kinamaliza na maneno ya matumaini. Mungu yule yule aliyeghadhabika ni Mungu yule yule atakayeturehemu. ***"Ni nani aliye Mungu kama wewe mwenye kusamehe uovu na kuliachilia kosa la watu wa urithi wake waliosalia hashiki hasira yake milele kwa maana yeye hufurahia Rehema"*** (7:18). Hakuna cha ajabu anachoeleza nabii, ***"lakini mimi nitamtazamia Bwana nitamngoje Mungu wa wokovu wangu Mungu wangu atanisikia"*** (7:7).[43]

**Watu Muhimu:** Mika, Yotham, Ahazi, Hezekia

**Mwonekano wa Yesu katika Mika:** Mika anamwonyesha Kristo kama Mungu wa Yakobo (4:2), Mhukumu wa ulimwengu (4:3), na mtawala atakayezaliwa katika mji wa Bethelehemu (5:2 linganisha. Mathayo 2:1-6). Makuhani walimnukuu Mika 5:2 kujibu swali la Herode la mahali atakapozaliwa Masihi.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi (1:1)**

2. **Ujumbe wa Kwanza: Hukumu ya Samaria na Yuda (1:1–2:13)**
    a. Utabiri wa Hukumu Ijayo (1:2-7)
    b. Maombolezo ya Watu (1:8-16)
        1) Maombolezo ya Mika. (1:8-9)
        2) Wito wa Mika (1:10-16)
    c. Dhambi ya Yuda (2:1-11)
        1) Dhambi ya Watu (2:1-5)
        2) Dhambi ya Manabii wa Uongo (2:6-11)
    d. Utabiri wa Kukusanywa (2:12-13)

3. **Ujumbe wa Pili: Maangamizi Yaliyofuatiwa na Wokovu (3:1–5:15)**
    a. Jukumu la Viongozi wa Taifa (3:1-12)
        1) Hukumu kwa Watawala (3:1-4)
        2) Hukumu ya Manabii wa Uongo (3:5-8)
        3) Hukumu ya Viongozi wa Ninawi (3:9-12)
    b. Baraka za Ufalme kwa Ajili ya Taifa (4:1–5:15)
        1) Sifa za Ufalme (4:1-8)
        2) Matukio Yaliyoendeleza Ufalme (4:9–5:1)
        3) Mtawala wa Ufalme (5:2-15)

4. **Ujumbe wa Mara ya Tatu: Hukumu ya Dhambi na Ahadi ya Baraka (6:1–7:20)**
    a. Mwonekano wa Bwana (6:1-5)
    b. Mwitikio wa Mika kwa Taifa (6:6-8)
    c. Hukumu ya Bwana kwa Ajili ya Dhambi (6:9-16)
        1) Dhambi (6:9-12)
        2) Adhabu (6:13-16)
    d. Mashitaka ya Mika na Bwana (7:1-20)
        1) Hudhuni ya Mika kwa Ajili ya Dhambi ya Taifa (7:1-6)
        2) Ujasiri wa Mika kwa Bwana (7:7-13)
        3) Maombi ya Mika ili Kwamba Mungu Aweze Kuchunga Kondoo Zake Tena (7:14)
        4) Ahadi ya Bwana ya Kufanya Miujiza kwa Watu Wake (7:15-17)
    e. Ukiri wa Mika Kwamba Mungu ni Mkuu (7:18-20)

# Nahumu

## (Maangamizi ya Ninawi)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Zaidi ya kile Nahumu anachotueleza kwenye sura ya 1:1 ni kwamba Kitabu hiki ni kwa ajili ya maono ya Nahumu, Muelikoshite na kwamba ni tiba ya Ninawi na hatujui lolote kuhusiana na mwandishi huyu. Nahumu ina maana ya "Faraja" lakini ujumbe huu haumaanishi faraja kwa taifa la Assiria lililokuwa limedhoofika. Labda ni faraja ya Yuda. Na hivyo yamkini alikuwa ni nabii wa Yuda kwa mtazamo wa 1:15, japo hatuelewi kwa usahihi uelekeo wa Elkoshi lakini wasomi wengi wanasema kwamba ,mji huu ulikuwa sehemu fulani katika Yuda ya kusini.

Kama ilivyo kwa manabii wadogo wote kitabu kilipata jina lake kwa nabii aliyekuwa akisema unabii.

**Muda wa Kuandikwa: 663-612 K.K.** Nahumu anazungumza juu ya kuanguka kwa Thebe (iko Misri) kama ilivyopita katika 3:8-10. Thebe ilianguka 663 K.K. Katika sura zote tatu, Nahumu anatabiri juu ya kuanguka kwa Ninawi mwaka 612 K.K. Nahumu yamkini alitoa tiba yake karibu na mwisho wa nyakati hizi kwa sababu ameeleza kuanguka kwa Ninawi (2:1; 3:14, 19). Na hii inaweza kufanya huduma yake kuwa kipindi cha utawala wa Yosia na inamfanya kuwa rika moja na Zephania na Yeremia.

**Nia na Makusudi:** Kusudi la Nahumu ni kuanguka kwa Ninawi na kama kisasi cha Mungu dhidi ya Waasiria wa Ninawi. Kile alichotaka kukiona Yona kinachoitwa hukumu ya Mungu kwa Assiria kilikuwa kimetabiriwa na Nahumu kiasi cha miaka mia na hamsini baadaye.

Kubadilika kwa Ninawi kwa kukubali mahubiri ya Yona ni wazi kabisa kwamba kulidumu muda mfupi kwa sababu mapema tu baada ya kubadilika walirudi tena katika njia zao mbaya. Sargon II wa Asiria aliiharibu Samaria na akachukua ufalme wa kaskazini wa Israeli kama mateka na kuyatawanya makabila yote kumi miaka ya 722 K.K. Baadaye, Sennacherib wa Assiria aliikamata Yerusalemu kipindi cha utawala wa Hezekia miaka ya 701 K.K. Bila kujali nguvu zao Ninawi imehukumiwa kwa kuangamizwa na Mungu Mtakatifu kwa njia ya nabii Nahumu. Majivuno ya Asiria na nguvu zake zitakoma kwa nguvu za Mungu. Japo kitabu kinatazama kwenye anguko la Asiria na hukumu lakini pia kimeandikwa ili kuwa faraja kwa Yuda.

**Watu Muhimu:** Nahumu

**Mwonekano wa Yesu katika Nahumu:** Japo hakuna unabii wa moja kwa moja wa Masihi katika Nahumu kwa kuhifadhi msingi wa Kiroho wa unabii wote, Kristo ameonekana kama Mungu mwenye wivu na mwenye kisasi kwa maovu (1:2-13).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi (1:1)**

2. **Unabii na Hukumu ya Haki ya Mungu kwa Ninawi (1:2-15)**
   a. Ghadhabu Takatifu ya Mungu kwa Ninawi (1:2-8)
   b. Kuasi kwa Ninawi Hii ya Yahwe Inakoma (1:9-11)
   c. Mateso ya Yuda Yatakoma kwa Sababu ya Hukumu ya Ninawi (1:12-15)

3. **Maelezo ya Hukumu ya Mungu kwa Ninawi (2:1-13)**
   a. Uvamizi Unaelezwa (2:1-6)
   b. Ushindi Unaelezwa (2:7-13)

4. **Sababu ya Hukumu ya Mungu kwa Ninawi (3:1-19)**
   a. Kwa Sababu ya Kutotii kwake na Aibu ya Dhambi (3:1-7)
   b. Utendaji Wake kwa Thebe Kulisababishwa Kushindwa (3:8-11)
   c. Kujihami Kwake Kutofaa (3:12-19)

# Habakuki

### (Jawabu la Kuchanganyikiwa)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Mwandishi ni Habakuki 1:1 na 3:1. Amejieleza vizuri yeye mwenyewe kama nabii na kweli kwamba maombi yake na sifa zake zimekamilishwa na mstari huu, ***"Kwa sababu ya ukurugenzi wa kwaya katika gitaa langu"*** inaonesha kwamba alikuwa ni kuhani.

Kitabu kimepata jina lake toka kwa mwandishi wake. Habakuki inatoka katika neno la kiyunani lenye maana ya "kukumbatia." Nabii anamweleza YAHWE kama Mungu wa wokovu wake na ngome yake.

**Muda wa Kuandikwa: 600 K.K.** Kwa sababu kitabu kinaonyesha uvamizi wa Wababeli na kinaonesha umakini wa Wababeli, yamkini Habakuki alitumika kipindi cha Yehoiakimu wa Yuda. inaonesha kwamba Babeli hakumbadili Yuda japo alikuwa mhamiaji (1:6; 2:1), Habakuki alitabiri kwa ufupi sana kabla ya uvamizi wa Wababeli miaka ya 605 K.K.

**Nia na Makusudi:** Kusudi la kitabu hiki linaonesha ni kuchanganyikiwa kwa Wababeli kwa kuvamiwa kwao. Inahusika na Imani ya Habakuki kwa mazingira makuu mawili: (1) kwa nini Mungu ameruhusu maovu mengi Yuda na hata hayaadhibu (1:2-4)? na kwa nini awe ni Mungu Mtakatifu (1:13) akitumia mataifa kama Babeli kama chanzo cha hukumu yake (1:12-2:1)? Habakuki alikuwa na ugumu wa kuelewa magumu haya ambayo yalijibiwa na ufunuo wa Mungu uliokuwa ukiendelea na Nabii anafunga kwa zaburi ya furaha ya tumaini. Kitabu hiki ni usalama na wema wa Mungu na nguvu ya mtazamo wa matatizo ya maovu.

**Watu Muhimu:** Habakuki

**Mwonekano wa Yesu katika Habakuki:** Kwa mtazamo wa unabii Kristo ameoneshwa kama mwokozi. Neno Wokovu linaloonekana mara tatu katika 3:13 na 18, ni mzizi ambao jina Yesu linapatikana (Mathayo 1:21). Pia ameoneshwa kama Mtakatifu (1:12 linganisha 1 Yohana 1:9), anayethibitisha haki kwa imani (2:4), na atakaye kuja duniani siku moja ***"kwa utukufu wa Bwana kama maji yaifunikavyo bahari"*** (2:14).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Kuchanganyikiwa kwa Habakuki: Imani Inajaribiwa na Kufundishwa (1:1–2:20)**
   a. Tatizo la Kwanza: Kwa Nini Mungu Anaruhusu Maovu Yaendelee katika Yuda? (1:2-4)
   b. Jibu la Kwanza la Mungu (1:5-11)
   c. Tatizo la Pili:Kwa Nini Mungu Atumie Watu Dhaifu Kuiadhibu Yuda? (1:12–2:1)
   d. Jibu la Mungu la Pili (2:2-20)

2. **Sifa za Habakuki: Imani ni Ushindi (3:1-19)**
   a. Sifa za Mtu wa Mungu (3:1-3)
   b. Sifa za Nguvu za Mungu (3:4-7)
   c. Sifa za Makusudi ya Mungu (3:8-16)
   d. Sifa za Imani katika Mungu (3:17-19)

# Sefania

## (Baraka kwa Njia ya Hukumu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama katika 1:1, kitabu kiliandikwa na Zephania mwana wa Kushi mwana wa Gedalia mwana wa Amaria mwana wa Hezekia. Ukilinganisha na ukoo wa mwandishi, jina la kitabu hiki ni sahihi kabisa. Baba wa mwandishi anafahamika na kujulikana (Isaya 1:1; Yeremia 1:1; Ezekieli 1:3; Hosea 1:1; Yoel. 1:1) wakati mwandishi alipokuwa anajieleza. Baba yake mkubwa alikuwa ni Mfalme mzuri wa Hezekia.

Kitabu kimepata jina lake toka kwa nabii Zephania ambaye jina lake lina maana ya "YAHWEH aliyejificha" (2:3).

**Muda wa Kuandikwa: 630-625 K.K.** Kulingana na utangulizi (1:1) Zephania alitabiri kipindi cha utawala wa Yosia (640-609 K.K.). Unabii wake uliendelea kipindi cha anguko la Ninawi miaka ya 612 K.K. na mabadiliko ya Yosia 622-621 K.K. Hii ni dhahiri kwa sababu kitabu cha Zephania kinaeleza mambo ya kipagani yalivyoendelea katika Yuda (1:4-6) ambayo yaliondoshwa na mabadiliko ya Yosia. Hii inasadikika kuwa ni kipindi cha 630 na 625 K.K.

**Nia na Makusudi:** Nabii anazungumza kwa manabii wa Yuda ambao maisha yao yalitawaliwa na uovu kipindi cha utawala wa Manase na Amoni (3:1-7). Kwa kulinda kutotii na laana katika Mambo ya Walawi 28, nia ni hukumu au siku ya Bwana inayokuja. Katika utakatifu wa YAHWE anaonyesha utakatifu wake dhidi ya dhambi kwa kuyaita mataifa katka ulimwengu yaje mbele zake. Lakini Mungu ni Mungu wa rehema na baraka kwa hiyo kuna ufafanuzi mkuu na wito wa kutubu katika ahadi ya baraka. Kwa hiyo Zephania imegawanyika katika sehemu tatu: hukumu ya dhambi, wito wa toba, na ahadi ya kukombolewa au baraka.

**Watu Muhimu:** Zephania, Yosia

**Mwonekano wa Yesu katika Zephania:** Japo haijatajwa katika kitabu hiki Masihi ameonyeshwa kama mtu wa haki katika taifa la Israeli (3:5) ambaye pia ni mfalme wao (3:15).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi (1:1)**

2. **Hukumu ya Siku ya Yahwe (1:2–3:8)**
   a. Hukumu ya Dunia (1:2-3)
   b. Hukumu ya Yuda (1:4–2:3)
      1) Sababu ya Hukumu (1:4-13)
      2) Maelezo ya Hukumu (1:14-18)
      3) Mahubiri kwa Taifa: Tubu na Kumtafuta Mungu (2:1-3)
   c. Hukumu ya Mataifa Yanayozunguka (2:4-15)
      1) Philistia (2:4-7)
      2) Moabu na Amoni (2:8-11)
      3) Ethiopia (2:12)
      4) Asiria (2:13-15)
   d. Hukumu ya Yerusalemu (3:1-7)
      1) Maelezo ya Nabii (3:1-5)
      2) Hukumu ya Bwana (3:6-7)
   e. Hukumu ya Wote Duniani (3:8)

3. **Kurejeshwa kwa Siku ya Yahweh (3:9-20)**
   a. Kurudishwa kwa Taifa (3:9-10)
   b. Kukombolewa kwa Israeli (3:11-20)

# Hagai

## (Kujipa Moyo)

**Utangulizi:** Sasa tunakuja kwa manabii walioandika baada ya uhamisho wa Babeli. Hagai, Zekaria na Malaki walisema wote kwa wayahudi waliorudi Israeli. Kusudi lilikuwa ni kuwatia moyo na maadili ya kundi dogo lililokuwa limebaki wakati wa kurudi katika nchi yao huku wakifikiri kujenga hekalu na taifa pia.

Hagai na Zekaria alihusika na mahitaji ya Kiroho kwa sababu walikua katika kujenga hekalu na Malaki alihusika na maadili na mambo ya kimwili katika kulijenga taifa.

**Jina na Mtunzi wa Kitabu:** Jina la Hagai linamaanisha “sikukuu” ikiwa na maana kwamba alizaliwa kati ya siku moja kubwa ya sikukuu japo hakuna mstari unaoeleza hili. Hagai inajulikana sana katika kitabu hiki kwani ametaja mara tisa na hata ametajwa katika Ezra 5:1-2 na 6:14. haijulikani vizuri. Lakini anajieleza kama Nabii Hagai” (1:1), na hatuelewi ukoo wake wala wazazi wake. Alikuwa sawa na Zekaria nabii na Zerubabeli Gavana.

Kitabu kimepewa jina na mwandishi mwenyewe kama ilivyo kwa vitabu vingine vya kinabii.

**Muda wa Kuandikwa: 520 K.K.** Chini ya sera za Kiro mkuu mfalme wa Persia ni kama Wayahudi 50,000 waliruhusiwa kurudi Yerualemu. Kati yao alikuwa Zerubabeli (Ezra 1:2-4 linganisha Isaya 44:28), Yoshua kuhani Mkuu Hagai na Zekaria. Mamlaka yaliwaruhusu Wayahudi kurudi katika nchi yao na kujenga hekalu lao katika miaka ya 538 K.K.

Dhabihu ilianzishwa tena mapema baada ya kujenga madhabahu kwa kuziteketeza (Ezra 3:1-6), na katika mwaka wa pili wa kurudi kwao, msingi wa hekalu ulijengwa (Ezra 3:8-13; 5:16). Hata hivyo, kushurutishwa kwao na Wasamaria na kisha misukosuko ya Wapersia zilileta usumbufu katika kujenga upya Hekalu. Lakini mambo ya kiroho yalianza ndani kwa muda wa miaka 16 hadi utawala wa mfalme Dario (521-486 K.K.) – ujenzi wa hekalu ulikomeshwa. Katika mwaka wa pili wa Dario (520 K.K.) Mungu alimwinua Hagai nabii kuwatia moyo Wayahudi katika kulijenga tena hekalu (Ezra 5:1-2; Hagai 1:1).

Kilichoelezwa katika Hagai 1:1, ujumbe wake wa kwanza alipewa siku ya kwanza ya Elul (August - September) katika mwaka wa pili wa Dario na hii ilikuwa kati ya miaka ya 520 K.K.

**Nia na Makusudi:** Kitabu cha Hagai ni kitabu cha pili kwa ufupi katika Agano la Kale na Obadia ndicho cha pili tu. Uandishi wa Hagai ni rahisi sana. Kitabu hiki ni taarifa ya jumbe nne muhimu na nabii huyu huduma yake iliisha kwa muda tu.

Japo Hagai ni kitabu cha pili kwa ufupi katika Agano la Kale lakini pia hatuwezi kufupisha jumbe za Hagai katika jukumu lake la kuwatia moyo katika kulijenga tena hekalu. Manabii wengi wamegusia katika swala hili pia.Sifa moja ya Hagai ni ule uimara wake na umakini katika ujumbe wake. Ni kama mara 25 ameeleza mamlaka ya Mungu katika jumbe zake. Alitambulisha ujumbe wake kama ***“Hiki ndicho Bwana mweza anachosema,”*** na akahitimisha kwa maneno sawa (“asema Bwana mweza”).

Hagai aliandika kutia moyo na kuwahimiza katika kurudi kwao kulijenga hekalu katika Yerusalemu. Alisema (1) Mungu huwabariki watu wake wanapomtanguliza, (2) hatupaswi kuchoka katika huduma ya Bwana na kwamba, (3) ahadi ya Mungu ya kesho ni msingi wa ujasiri wetu leo.

**Watu Muhimu:** Hagai, Dario, Zerubbabel, Yoshua kuhani mkuu

**Mwonekano wa Yesu katika Hagai:** Hapa Masihi anaoneshwa kama mrejeshaji wa utukufu wa hekalu (2:7-9) na kama mmoja anayeng’oa utawala wa dunia hii (2:22).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Ujumbe wa Kwanza: Wito wa Kujenga Hekalu (1:1-15)**
   a. Utangulizi (1:1)
   b. Karipio la Kwanza (1:2-6)
   c. Marekebisho (1:7-8)
   d. Karipio la Pili (1:9-11)
   e. Mwitikio wa Ujumbe wa Nabii (1:12-15)

2. **Ujumbe wa Pili: Wito wa Kutafuta Ujasiri Katika Ahadi ya Mungu (2:1-9)**
   a. Utangulizi (2:1-2)
   b. Ahadi ya Uweza wa Utukufu Ujao (2:3-9)

3. **Ujumbe wa Tatu: Wito wa Maisha Safi (2:10-19)**
   a. Utangulizi (2:10)
   b. Tatizo: Kutotii kwa Wageni (2:11-14)
   c. Jibu: Kutii kwa Wageni (2:15-19)

4. **Ujumbe wa Nne: Wito wa Ujasiri Ujao (2:20-23)**
   a. Utangulizi (2:20-21a)
   b. Ahadi ya Ushindi Ujao wa Ufalme wa Watakatifu (2:21b-22)
   c. Ahadi ya Urejeshwaji wa Ufalme wa Daudi (2:23)

# Zekaria

## (Wivu wa YAHWEH)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Zekaria nabii alikuwa mwana wa Berekia mwana wa Iddo kuhani aliyewaongoza Walawi (Zekaria 1:1). Alikuwa sawa na nabii aliyepita (Ezra 6:14).

Jina la Zekaria lina maana ya "YAHWE hukumbuka" au "YAHWE amekwisha kumbuka" na hili ndilo kusudi la kitabu linaloendelea katika kitabu hiki.

**Muda wa Kuandikwa: 520-518 K.K.** Mstari wa kwanza unamwakilisha Zekaria kama mwana wa Berekia na mjukuu wa Iddo aliyekuwa ni kuhani yule yule aliyetajwa katika Nehemia 12:4, kama rika moja na Zerubabeli. Katika Zekaria 2:4 nabii amezungumzwa kama kijana. Yamkini alikuwa ni kijana mdogo kwa muda alioshirikiana na Hagai katika kampeni za kuijenga tena miaka ya 520 K.K. na unabii wake wa mwisho (7:1-14) uliptolewa miaka miwili baadaye 518 K.K. Sura ya 9-14 inaonyesha nyakati mabalimbali za unabii na hii yamkini ilikuwa ni 480 K.K. kwa mtazamo wa Kigiriki (9:13).

Hatuna habari nzuri kuhusiana na Zekaria labda katika Mathayo 23:35, inayoonyesha kwamba aliuawa na Bomu katika maeneo ya hekalu (Zekaria aliyemtaja Yesu anasemekana kuwa ni mwana wa Berekia na si wa Yehoiada ambaye mwisho wake ulikuwa unafanana katika nyakati za mfalme Yoashi kulingana na 2 Nyakati 24:20-21).[44]

**Nia na Makusudi:** Zekaria iliandikwa ili kuwatia moyo Wayahudi waliokuwa wamerudi ili walijenge hekalu. Nabii alionyesha kwamba Mungu yuko katika kazi ya kuwarejesha Waisraeli katika urithi wao wa kiroho katika kuandaa majilio ya Masihi. Kimafundisho Zekaria anaeleza mambo ya hekalu katika ukombozi wa Mungu wa Waisraeli na anaonesha jinsi Mungu anavyowaleta watu wake tena katika nchi yao, na anakuza ubora wa Kristo katika mambo ya kiroho yajayo ya taifa.

**Watu Muhimu:** Zekaria, Yoshua Kuhani

**Mwonekano wa Yesu katika Zekaria:** Labda katika Agano la Kale ni Masihi tu zaidi ya Zekaria. Kitabu hiki kinamwakilisha Masihi au Kristo katika mambo makuu mawili kama mtu na kama Mungu na kama malaika wa Bwana (3:1), tawi la haki (3:8), jiwe la macho saba (3:9), masihi aliyesulubishwa (12:10), mfalme mnyenyekevu ajaye (9:9-10), mchungaji atakayekataliwa (13:7), na hakimu na mfalme wa haki ajaye (14).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Wito wa Kutubu (1:1-6)**

2. **Maono Nane ya Zekaria (1:7–6:8)**
    a. Farasi na Mpanda Farasi (1:7-17)
    b. Pembe Nne na Wahunzi Wanne (1:18-21)
    c. Mtalii (2:1-13)
    d. Kuhani Mkuu (3:1-10)
    e. Stendi ya Dhahabu (4:1-14)
    f. Gombo lirukalo (5:1-4)
    g. Mwanamke Epha (5:5-11)
    h. Tera Nne (6:1-8)

3. **Taji ya Joshua (6:9-15)**

4. **Maswali Kuusu Kufunga (7:1–8:23)**

| | | |
|---|---|---|
| 7:1-7 | 8:9-13 | 8:20-23 |
| 7:8-14 | 8:14-17 | |
| 8:1-8 | 8:18-19 | |

5. **Nabii Mbili Kuhusu Yajayo (9:1–14:21)**
    a. Kukataliwa kwa Masihi (9:1–11:17)

| | |
|---|---|
| 9:1-10 | 10:1-12 |
| 9:11-17 | 11:1-17 |

    b. Kutawala kwa Masihi (12:1–14:21)

| | | |
|---|---|---|
| 12:1-5 | 13:1-6 | 14:1-8 |
| 12:6-14 | 13:7-9 | 14:9-21 |

# Malaki
## (Toba na Kugeuka)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Malaki ametajwa katika kitabu hiki sura ya 1:1 kwamba ndiye mwandishi wa kitabu. Jina lake linamaanisha “Mjumbe Wangu” na hii inamaanisha vizuri kwani inaashiria kuja kwa “mjumbe wa agano” (linganisha na 3:1), unabii wa Yohana Mbatizaji (Mathayo 11:10).

**Muda wa Kuandikwa: 450-400 K.K.** Kuhusiana na muda wa kitabu cha Malaki, Gleason Archer anaandika:

> Kutoka katika ushahidi wa ndani inaonekana vema kwamba unabii wake ulitolewa karne ya pili na nusu ya karne ya hamsini labda miaka ya 435 K.K. Tunathibitisha hii kwa kuangalia yafuatayo: (1) Hekalu tayari lilikuwa limekwisha jengwa na dhabihu za Musa zikiendelea (1:7, 10; 3:1). (2) Gavana wa Persia alikuwa katika mamlaka wakati huo; labda isiwe kipindi cha utawala wa Nehemia (miaka ya 445 na 433 K.K.). (3) Dhambi anazozisema Malaki ni sawa na za Nehemia (a) Uzembe wa makuhani (1:6; Nehemia 13:4-9), (b) Kukataliwa kwa zaka (3:7-12 linganisha na Nehemia 13:10-13), (c) Ndoa za mitaala na wanawake wa kigeni (2:10-16 linganisha na Nehemia 13:23-28). Ni rahisi kusema kwamba Malaki alikuwa ameshagoma kufanyika kwa vitu hivi katika iaka ili kuendeleza kurudi kwa Nehemia; kwa hiyo inaweza kuwa ni 435 K.K.[45]

**Nia na Makusudi:** Chini ya Utawala wa Nehemia kumekuwa na kipindi cha uamusho (Nehemia 10:28-39), lakini wakuu na watu alikuwa wamepoa katika kutembea kwao na Mungu na hivyo kuyaacha mapenzi ya Mungu. Japo walikuwa wanahukumiwa na dhambi, Malaki alikuwa amekomesha (Uzembe, kutotoa zaka, na ndoa za mitaala), watu walichanganyikiwa kwa nini Mungu hakubarikiwa nao. Malaki aliandika kulijibu swali la makuhani na watu kuonesha na kuwakemea dhambi zao, kugeukageuka kwao, na mawazo mabaya. Na halafu alimalizia na neno la kuwafariji la kuja kwa mjumbe wa Bwana ambaye ataitengeneza njia ya Masihi.

Malaki aliwakemea kwa kumkataa kumwabudu Bwana wa kweli na akawaambia watubu (1:6; 3:7). Gleason Archer alisema:

> Nia ya Malaki ni kwamba wamtafute Mungu na hali ya utakatifu iwe katika maisha yao kwani ndicho kinachohitajika machoni pa Bwana. Furaha yake ni kuwa zawadi ya zao la ustawi wa uchumi wa taifa. Israeli itaishi hadi pale ilipopangiwa kama taifa takatifu na litasubiri masihi, ambaye kwa huduma yake ya uponyaji na hukumu itaifanya taifa lielewe matumaini yake.[46]

**Watu Muhimu:** Malaki

**Mwonekano wa Yesu katika Malaki:** Kwa mtazamo wa kimasihi katika malaki, Wilkinson anasema vizuri:

> Kitabu cha Malaki ni kitabu cha mwanzo cha miaka mia nne cha ukimya na kimekatishwa na nabii aliyefuatia Yohana Mbatizaji: ***‘Tazama mwana kondoo wa Mungu asafishaye dhami za ulimwengu!’*** (Yohana 1:29). Malaki anatabiri kuja kwa mjumbe atakayesafisha njia ya Bwana (3:1 linganisha na Isaya 40:30). Yohana mbatizaji ndiye aliyekamilisha unabii lakini kwa mistari michache inayofuatia (3:2-5) anarukia mbele kwa Kristo kwa kuja kwake mara ya pili.[47]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Mahali Pazuri pa Israeli (1:1-5)**
   a. Upendo wa Mungu Unaelezwa (1:1-2a)
   b. Upendo wa Mungu Unatiliwa Mashaka (1:2b)
   c. Upendo wa Mungu Unadhihirishwa (1:3-5)

2. **Uharibifu wa Israeli (1:6–3:15)**
   a. Uongo (1:6-14)
   b. Kukosa Uaminifu. (2:1-9)
   c. Ndoa za Mitaala (2:10-12)
   d. Taraka (2:13-16)
   e. Dhambi (2:17)
   f. Mjumbe Ajaye (3:1-6)
   g. Wizi (3:7-12)
   h. Ufisadi (3:13-15)

3. **Ahadi kwa Watu (3:16–4:6)**
    a. Ahadi ya kitabu cha Kumbukumbu (3:16-18)
    b. Ahadi ya Kuja Kristo (4:1-3)
    c. Ahadi ya Kuja Eliya (4:4-6)

## Sura ya 3

# Agano Jipya

# Utangulizi

Agano Jipya ni kumbukumbu ya matukio ya kihistoria, habari njema matukio ya mwokozi wa maisha Bwana wetu Yesu Kristo-maisha yake, kifo, ufufuko, kupaa kwake na mwendelezo wa kazi yake katika ulimwengu ambao umeelezwa na kufanywa na mitume ambao aliwachagua na kuwatuma katika ulimwengu. Na pia ni ukamilisho wa matukio hayo ambayo yalitendwa kipindi cha Agano la Kale. Zaidi inatoa historia ambayo siyo ya ulimwengu huu, bali iliyoandikwa kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hivi ndivyo ilivyo kama vile Agano la Kale, agano hili liko chini ya Mungu kwa ulinzi wake ili lisipotoshwe na wanadamu walio na mawazo mabaya kwa ajili ya kanisa na hata historia ya mwanadamu hadi pale Yesu atakaporudi.

**Maana ya Asili ya Neno "Agano Jipya":** Biblia yetu imegawanyika katika sehemu kuu mbili yaani Agano la Kale na Agano Jipya lakini hiyo inaamnisha nini. Neno la Kiyunani linaonyesha Agano linamaana ya "mapenzi, makubalino au mkataba." Agano la Kale linaeleza historia ya matukio jinsi Mungu alivyotenda kwa waisraeli katika misingi ya sheria ya Musa alizompa katika mlima Sinai. Kwa upande mwingine Agano Jipya lililosemwa katika Yeremia 31:31 likitawaliwa na Bwana wetu Yesu linaeleza mpango mpya wa Mungu kwa kila kabila taifa na kwa wale wanaopaswa kuupokea wokovu chini ya msingi wa Bwana Yesu.

Agano la Kale linaonesha utakatifu wa Mungu kwa njia ya sheria na linaahidi juu ya mkombozi. Agano Jipya linaonesha utakatifu wa Mungu kwa njia ya mwana wake Yesu Kristo mwokozi aliyekuja kwa wanadamu. Agano Jipya lina haya ili kuonesha mpango mzima uliomo katika Agano hili.

Ujumbe wa Agano Jipya uko katika (1) mtu ambaye alijitoa kwa wanadamu kwa ajili ya dhambi zao (Mathayo 26:28) na (2) watu waliopokea wokovu wake. Msingi wa Agano Jipya ni wokovu.[48]

Majina ya Agano Jipya na la Kale yametumika kwa kuhusiana kwa jinsi Mungu alivyojihusisha na wanadamu na historia zake. Agano Jipya lina nguvu ya Mungu ambayo Mungu amekuwa na amani na mapatano na wanadamu."[49]

**Maandalizi ya Kiungu (Mungu) katika Agano Jipya:** Wakati wa Agano Jipya Rumi ilikuwa ndiyo ikitawala kwa nguvu katika ulimengu huu. Kwa hiyo katika mji mdogo katika Palestina, Bethlehem ya Yudea, alizaliwa mtu mbaye aliubadilisha ulimwengu. Kuhusiana na mtu huyu Paulo aliandika, ***"Waktati wa kukamilika kwa sheria ulipotimia Mungu alimtuma Mwana ambaye alizaliwa na mwanamke, alizaliwa chini ya sheria"*** (Agano la Kale). Kwa njia ya ajabu sana Mungu ameutayarisha ulimwengu kwa ajili ya Masihi atakayekuja. Sababu nyingi zilichangia katika maandalizi haya.

**Maandalizi kwa Njia ya Taifa la Wayahudi:** Maandalizi ya kuja kwa Kristo ni historia ya Agano la Kale. Wayahudi walichaguliwa na Mungu kutoka katika mataifa mbalimbali kuwa hazina ya ufalme wa makuhani, na taifa takatifu (Kutoka 19:5-6). Kwa mtazamo huo kwa kuanza na ahadi ambayo Mungu aliitoa kwa jamaa ya Ibrahimu, Isaka na Yakobo (Mwanzo 12:1-3; Warumi 9:4), walikuwa ni waangalizi wa neno la Mungu (Agano la Kale (Warumi 3:2), na walikuwa ni ukoo wa mwokozi (Mwanzo 12:3; Wagalatia 3:8; Warumi 9:5). Kwa hiyo Agano la Kale lilikuwa limejaa habari na kutabiri kwa kuja Kristo kama mtu Atakayeteseka na atakayetukuzwa, mwokozi. Si kwa sababu kulikuwa na manabii wengi, lakini hata kulikuwa na habari nyingi zinazohusiana na ukoo wa Masihi, kuzaliwa kwake na sehemu ya kuzaliwa kwake, maisha yake,kifo chake na hata kufufuka kwakwe.

Japokuwa Waisraeli walikuwa si watiifu na hata kuchukuliwa kama watumwa kama hukumu ya Mungu kwa ugumu wa mioyo yao. Mungu aliwarejesha tena katika nchi yao baada ya miaka sabini kwa sababu alikuwa ameahidi katika maandalizi ya kumleta mkombozi Masihi. Miaka mia nne ilipita baada ya uandishi wa Agano la Kale. Udini ulikuwa umetawala na ilikuwa ni tatizo kubwa, pamoja na hayo kulikuwa na uijilio masihi wa Bwana katika anga.

**Maandalizi Kupitia Lugha ya Kiyunani:** Ni muhimu sana kuelewa kwamba wakati Yesu amewatuma wanafunzi wake duniani kuitanganza injili (Mathayo 28:19-20), kulikuwa na lugha ya kiulimwengu. Hii ilikuwa ni matokeo ya utawala wa Alexanda mkuu, mwana wa mfalme Philimon wa Makedonia ambaye kwa zaidi ya miaka 300 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu alitawala taifa moja hadi jingine. Shauku ya Alexanda ilikuwa ni kugawanya taifa moja na lugha moja. Baada ya ushindi huu aliweka lugha ya kiyunani kama lugha ya kawaida, na utamaduni mmoja kama kielelezo cha fikra na maisha. Utawala wa Alexanda ulikoma muda mfupi lakini lugha ya kiyunani ilidumu muda mrefu.

Jambo muhimu lilikuwa kwamba Mungu alikuwa akiuandaa ulimwengu kwa lugha ya kawaida kabisa ambayo ilijulikana kwa mwanadamu. Lugha hii ilitumika katika kumtangaza mwokozi, na matokeo yake yalikuwa ni kuandikwa kwa kitabu cha Agano Jipya kwa lugha ya kiyunani. Haikuandikwa kwa luga ya kiebrania au

kiamaraiki japo waandishi wa Agano Jipya walikuwa ni wayahudi isipokuwa Luka, mmataifa. Lugha ya kiyunani ya Kikoine ilkuwa ni lugha ya pili ambayo kila mtu wakati ule alionekana kuifahamu.

**Maandalizi kupitia Warumi:** Mungu hakuwa ameumaliza ulimwengu katika kuuandaa ulimwengu kwa ajili ya Kristo. Wakati Kristo alipozaliwa Palestina Warumi walikuwa wakiutawala ulimwengu. Palestina ilikuwa chini ya utawala wa Kirumi, na zaidi ya yote Rumi ilijulikana kwa uongozi wake na utawala wake. Vita vya kumwaga damu katika historia ya warumi viliishia katika utawala wa kaisaria Agusto na matokeo ya vita hivi vya zaidi ya miaka 100 vilikoma na Rumi ikaweka mipaka yake. Warumi walikuwa na barabara ambazo zililindwa na jeshi lake na kila msafiri alisafiri akaenda na kurudi salama. Augustino alikuwa ni mtawala wa kwanza wa kirumi kuvaa taji ya kifalme kama mtawala. Alikuwa mtu wa busara na hekima na mwenye kufikiri kwa watu wake na akaleta amani na mafanikio na kuifanya Rumi iwe ni sehemu ya watu kuishi na kusafiri. Na hii ilileta kitu kinachoitwa “Pax Romana,” yaani amani ya Rumi (27 K.K.–B.K. 180). Kwa sababu ya yale Agustino aliyoyakamilisha wengi walisema alipozaliwa, Mungu alizaliwa. Ilikuwa na maana ya kwamba amezaliwa yeye hasa ambaye ni wakweli ni chanzo cha amani ya watu na amani ya ulimwengu. Hakika ni amani ya muda na ya uongo tu ambayo wanadamu wanaweza kuitenda wala haikujalisha ni kwa hekima gani hapana na ndivyo Yesu alivyokuwa Mungu mwanadamu. Uwepo wa utawala wa kirumi na sheria zilisaidia ulimwengu katika kuupa uhai wake huduma yake ili kwamba injili ipate kuhubiriwa.

**Dini Wakati wa Agano Jipya:** Kabla hatujaendelea na utafiti wa Agano Jipya, ni vizuri kuwa na wazo angalau la jumla wakati Yesu alipokuja na badaye akalituma kanisa lake ulimwenguni, unaposoma maelezo yafuatayo kutoka kwa Merrill C. Tenney, akilinganisha au kufananisha na ulimwengu huu wa leo:

> Kanisa la Kikristo lilizaliwa katika ulimwengu uliokuwa umejawa na mashindano ya dini nyingi zilizokuwa zimetofautiana lakini zenye sifa moja– zilikuwa na jhudi za kumfikia mung au miungu. Zaidi ya imani hiyo dini hizi zilifundisha kwamba Mungu alihusika na Musa na manabii wengine hapakuwa na imani nyingine zaidi ya hii iliyofundisha vizuri kuhusu Mungu au wazo lolote la dhambi na wokovu. Maadili ya sasa hayana mafundisho mazuri juu ya dhambi au namna ya kwa na njia nyingine (Wokovu).
>
> Hata katika mafundisho haya ya kale ukweli ulionekana katika njia za mila au hata kama walikataa. Upagani na dini zote zilizo nje ya ufahamu na imani ya Neno la Mungu zinatoa asili ya Mungu jinsi alivyojifunua kwa mwanadamu. Mila hizi zinaonesha ukweli japo watu wanajaribu kuzibadilisha. Mamlaka ya kimungu ni ya muhimu na yanaleta maana, haki huthibitika katika mamlaka zote; ibaada hupungua, maombi yanakuwa niyabinafsi na nguvu ya asili huonekana kama nguvu za giza. Kwa hiyo Nuru ya Mungu imefunikwa na uongo mwingi. Kwa mitazamo mingine (kufanya kila mtu anachotaka) imekuwa ni fikra iliyotawala katika maisha ya watu; kama hakutakuwa na mwongozo mzuri wa ndani kabisa basi hakutakuwa na kanuni nzuri ya kuenenda pia, na kama hakuna kanuni nzuri maalumu mtu anaweza kuishi anavyoweza bila kujali; kama hakuna kanuni za moja kwa moja mtu anaweza kusihi kwa kuona faida tu katika maisha bila kujali nini kitatokea punde. Kwa sababu miungu wa kale hawana nguvu tena na hakna miungu mingine iliyotokea. Kuna vitabu vingi vinaeleza maebndeleo ya mwanadamu katika mila lakini hakuna msaada hata hivyo. Wat hawana furaha tena na hata sehemu bora itakayofanya maisha ya mwanadamu kuwa ni bora.[50]

**Utunzi na Mpangilio wa Agano Jipya:** Agano Jipya lina vitabu 27 na vimeandikwa na watunzi tisa tofauti. Kulingana na uandishi wao wamegawanywa katika makundi makuu matatu:

1. **Vitabu Vitano vya Jistoria:** Injili na Matendo
2. **Nyaraka Ishirini na Moja:** Warumi hadi Yuda
3. **Kitabu Kimoja cha Unabii:** Ufunuo

Jedwali mbili zifuatazo zinaonyesha mgawanyo huu na zinaangalia katika mipangilio hii mitatu ya Agano Jipya.[51]

<table>
<tr><th colspan="7">Agano Jipya</th></tr>
<tr><th>Historia</th><th colspan="5">Nyaraka (Barua)</th><th>Unabii</th></tr>
<tr><td rowspan="3">Mathayo<br>Marko<br>Luka<br>Yohana<br>Matendo</td><th colspan="4">Paulo</th><th>Kwa Ujumla</th><td rowspan="3">Ufunuo</td></tr>
<tr><th>Mapema<br>(wakati wa safari za kimisionari)</th><th colspan="3">Baadaye<br>(Baada ya kukamatwa Yerusalemu)</th><td rowspan="2">Yakobo<br>Waebrania<br>Yuda<br>1 Petro<br>2 Petro<br>1 Yohana<br>2 Yohana<br>3 Yohana</td></tr>
<tr><td>Wagalatia<br>1 Wathesalonike<br>2 Wathesalonike<br>1 Wakorintho<br>2 Wakorintho<br>Warumi</td><td>Kufungwa kwa Mara ya Kwanza<br>Wakolosai<br>Waefeso<br>Philimoni<br>Wafilipi</td><td>Kuachiliwa<br>1 Timotheo<br>Tito</td><td>Kufungwa kwa Mara ya Pili<br>2 Timotheo</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th colspan="3">Mtazamo wa Agano Jipya</th></tr>
<tr><td rowspan="2">Vitabu vya Kihistoria</td><td>Injili:<br>Mathayo, Marko, Luka, Yohana</td><td>Mwonekano:<br>Kuja kwa mwokozi, Utu wake na kazi yake</td></tr>
<tr><td>Matendo:<br>Matendo ya Roho Mtakatifu kwa Mitume</td><td>Matokeo:<br>Kuitangaza habari ya Mwokozi aliyekuj.</td></tr>
<tr><td>Nyaraka</td><td>Nyaraka:<br>Barua kwa makanisa na kwa watu.<br>Warumi hadi Yuda</td><td>Maelezo:<br>Inaeleza kazi na umuhimu wa Yesu jinsi inavyoweza kusaidia katika kutembea kwa mkristo katika dunia hii</td></tr>
<tr><td>Unabii</td><td>Ufunuo:<br>Kuja kwa Bwana</td><td>Ukamilifu:<br>Inaeleza nyakati za mwisho na kurudi kwa Bwana, muda wake, utawala wake na sehemu ya milele</td></tr>
</table>

**Msingi wa Vitabu vya Agano Jipya:** Msingi wa vitabu vya Agano Jipya ni wa msingi kama aelezavyo ndugu Ryrie,

> Kwanza inakuja injili inayoeleza maisha ya Yesu, halafu matendo yanayoeleza historia ya kuenea kwa ukristo,halafu nyaraka zinazoeleza mafundisho ya kanisa na matatizo yake na baadaye maono ya kurudi kwa Kristo katika ufunuo.[52]

Vitabu vya Biblia hutofautiana kulingana na uandishi wake, katika Agano Jipya tunaweza kukubaliana kulingana na mpangilio ufuatao:

| Kitabu | Tarehe (B.K.) | Kitabu | Tarehe (B.K.) |
|---|---|---|---|
| Yakobo | 45-46 | Matendo | 61 |
| Wagalatia | 49 | 1 Petro | 63-64 |
| Marko | 50s or 60s | 1 Timotheo | 63 |
| Mathayo | 50s or 60s | Tito | 65 |
| 1 & 2 Wathesalonike | 51-52 | Waebrania | 64-68 |
| 1 Wakorintho | 55 | 2 Petro | 67-68 |
| 2 Wakorintho | 56 | 2 Timotheo | 66 |
| Warumi | 57-58 | Yuda | 70-80 |
| Luka | 60 | Yohana | 85-90 |
| Wakolosai, Waefeso | 60-61 | 1, 2, 3 Yohana | 85-90 |
| Wafilipi, Philimoni | 60-61 | Ufunuo | 96 |

**Ukusanywaji wa Vitabu vya Agano Jipya:** Kwa asili vitabu vya Agano Jipya havikuwa pamoja na baadaye vilikusanywa na kutengeneza Agano Jipya sehemu ya Biblia. Kwa ulinzi wa Mungu vitabu vyetu hivi ishirini na saba viliandikwa kutokana na vitabu vingine wakati wa kanisa la kwanza. Vilitengwa kwa sababu vilikuwa na uvuvio wa pumzi ya Mungu. Na Ryrie ana hitimisho zuri sana la muhtasari wa uandishi huu:

> Baada ya kuwa vimeandikwa vitabu vya watu havikukusanywa mara moja na kuwekwa katika maandiko ambavyo vinafanya Agano Jipya. Kundi la viabu kama vya Paulo na injili vilihifadhiwa kabisa hapo mwanzo na kanisa na watu wengine walikuwa wametumwa na vitabu vyote ishirini na saba vilikusanywa na kupokelewa na kanisa.
>
> Kitendo hiki kilichukua miaka kama 350. Katika karne ya pili mzunguko wa vitabu vilivyokuwa vikisambaza uongo vilianza kuonekana. Vigezo vifuatavyo vilianza kutumika ili kupata kipi ni kitabu kinachofaa kuingizwa.
>
> 1. Je kitabu kiliandikwa au kuthibitishwa na mtume?
> 2. Je yaliyomo ni ya asili ya Kiroho?
> 3. Je kina thibitisha kuwa na uvuvio wa pumzi ya Mungu?
> 4. Je kilipokelewa na makanisa kwa shangwe?
>
> Si vitabu vyote vilivyopokelewa na kanisa na hii haimanishi kwamba vile ambavyo havikupokelewa vilikuwa ni vya uongo. Nyaraka zililenga watu (Philimoni, 2 na 3 Yohana) havikusambazwa kama zile zilizosambazwa katika kanisa. Vitabu vilivyoleta shida ni Yakobo, Yuda, 2 Petro, 2 na 3 Yohana, na Philimoni, lakini hatimaye vilikubalika na kuingizwa na kitabu kilithibitishwa katika baraza la Carthage miaka ya. 397 B.K.
>
> Japo hakuna nakala halisi ya maandiko ya Agano Jipya lakini yamekuwepo tangu 4,500. Maelezo ya Kiyunani au sehemu ya maandiko, na mengine 8,000 Kilatini na 1,000 maandiko mengine ambayo kitabu orijino kiliandikwa. Usomaji wa makini na ulinganishaji wa maandiko haya unatupa kuliamini Agano Jipya.[53]

# Sehemu ya 1
# Vitabu vya Kihistoria

**Utangulizi:** Kama ilivyoelezwa Agano Jipya liko katika migawanyiko mitatu kulingana na uandaliwaje wake – vitabu vya kihistoria, Nyaraka (barua), na unabii. Injili nne zinafanya asilimia 46 ya Agano Jipya. Kitabu cha Matendo kinaleta asilimia kama 60 inayomaanisha kwamba asilimia 60 ya Agano jipya na inaeleza vizuri ukristo. Ukristo umejengwa katika historia zilizokweli zinazorithika kiinjili. Injili ni habari njema iliyofanywa na kwa ushahidi wa wengine: ni historia, ushuhuda wa historia ya kweli.

Kwa kuwa historia zetu zinazungumzia juu ya Yesu kuzaliwa kwake, kifo na hata kufufuka kwake, Matendo inatupa historia inayofaa ya huduma ya Mitume katika kanisa la kwanza. Hivyo Matendo ni nzuri sana katika uelewa wetu kwa kile tulicho nacho katika nyaraka zetu. Nyaraka hizi zilikuwa ni barua za watu walioishi katika miji inayofahamika. agano jipya, hivyo, ni kitabu cha historia ya habari njema ya Mungu aliye hai kwa wanadamu si kwa wakati uliopita tu bali hata kwa sasa na hata kwa wakati unaokuja katika nuru ya ahadi ya Mungu.

**Injili Zifananazo:** Kabla hatujaanza kuangalia kila injili hebu tuangalie neno, "Synoptic Gospels." Kila injili inatofauti zake na makusudi yake, Mathayo, Marko na Luka zinatambulikana kama Synoptic Gospels kwa sababu zinafanana na zina mtazamo mmoja wa Yesu Kristo zinakubaliana. Zinaonyesha maisha ya Yesu halisi yaliyoelezwa katika kitabu cha Yohana. Yafuatayo yanaonyesha mambo fulani ya kawaida katika kila injili:

- Tangazo la Yohana Mbatizaji la kuja kwa Masihi (Mathayo 3, Marko 1, Luka 3).
- Ubatizo wa Yesu (Mathayo 3, Marko 1, na Luka 3).
- Kujaribiwa kwa Yesu (Mathayo 4, Marko 1, na Luka 4).
- Mafundisho na miujiza ya Yesu (sehemu kubwa ya kila injili).
- Kubadilika kwa sura (Mathayo 17, Marko 9, na Luka 9).
- Mateso, Kifo, na kuzikwa kakwe (Mathayo 26-27, Marko 14-15, Luka 22-23).
- Kufufuka kwa Yesu (Mathayo 28, Marko 16, Luka 24).

**Kusudi na Utofauti wa Mtazamo wa Injili Hizi Nne:** Kusudi la injili zote nne ni kuonyesha utu wa Yesu Kristo. Mathayo 16:13-16 inasema,

> ***Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria Filipi akawauliza wanafunzi wake akasema watu hunena mwana wa adamu kuwa ni nani? wakasema wengine husema kuwa u Yohana mbatizaji, wengine Eliya wengine Yeremia au mmojawapo wa manabii. Akawaambia nanyi mwaninena kuwa mimi ni nani? Simoni Petro akajibu akisema wewe ndiwe Kristo mwana wa Mungu aliye hai.***

Mathayo 16:14 Inatupa mwanga mzuri wa watu kipindi cha Yesu. Ni wachache sana waliomtambua Yesu kuwa yeye ni mwana wa Mungu. Kwa hiyo kwa uongozi wa Roho Mtakatifu waliandika ili kumuonyesha kuwa Yesu ni nani na kazi zake. Katika injili hizi tunakuta kwa kila tofauti yake kuna sehemu zinapokutana na kukubaliana kwa sababu zinaeleza zote kuwa Yesu ni nani. Zinaeleza kuwa yeye ni Masihi wa Agano la Kale, mtumishi wa Bwana, mwana wa mtu, mwana wa Mungu na ni mkombozi wa ulimwengu. Injili zinatupa mwanga mzuri juu ya kazi ya Yesu na tofauti zake ka njia ya picha nne.

**Mathayo** anaeleza katika injli yake kwa wayahudi akiwaeleza kwama Yesu wa Nazareti ni Masihi wao mfalme wa Wayahudi. Kwa ukoo wa Yesu Mathayo anatumia sifa kumi ili kuonyesha kwamba Yesu huyu japo amekataliwa na kusulubiwa lakini yeye ni Masihi aliyesubiliwa tangu Agano la Kale (Mathayo 1:23; 2:15; 2:18; 2:23; 4:15; 8:15; 12:18-21; 13:35; 21:5; 27:9-10). Japo Yesu alisulubiwa na kukataliwa na mataifa, mfalme alionyesha uwezo kwa kuacha kaburi wazi.

**Marko** anaonekana kuwaeleza Warumi watu wa matendo wachache wa maneno na anamuonyesha Yesu kama mtumishi wa Bwana aliyekuja ***"Kuwaweka huru."*** katika kulieleza hili Marko aliye na injiil fupi kuliko injili zote anaonekana mjasiri na anaonyesha uandishi wake kwa weupe na upeo kabisa hasa wakati wa mwisho wakati Yesu akiwa hapa duniani. Zaidi ya theruthi ya injili hii inaeleza matukio ya mwanzo na ya mwisho ya juma muhimu la Yesu.[54]

**Luka**, daktari anamweleza Yesu kuwa ni Mtu kamili aliyekuja ***"kutafuta na kuokoa kilichopotea"*** (Luka 19:10). Luka anaeleza uanadamu halisi wa Yesu, ni wakati huohuo anaeleza uungu wake. Na wengine wanaamini kwamba Luka alikuwa ni Myunani katika fikra kwa sababu ya uelezaji wake na mawazo yake yalivyokuwa mapana.

**Yohana** anawatazamisha wasomaji uungu wa Yesu kwa kumwonyesha Yesu kama, mwana wa Mungu anayetoa uzima wa milele kwa wale wote wanaompokea na kumwamini (Yohana 1:1-2, 12; 3:16-18, 36; 10:10). Japo imeandikwa kwa watu wote Injili ya Yohana iliandikwa kwa ajili ya kanisa. Sura tano zinaeleza mwanzo wa ujumbe wa Yesu Kristo kwa wanafunzi wake ili kuwafaraji kwa muda mchache kabla ya kifo chake. Kwa nyongeza ishara za miujiza zimeainishwa kumdhihirisha Yesu Kristo kuwa ni mwokozi na kuwatia moyo watu popote pale wamwamini ili wawe na uzima (Yohana 20:30-31).

# Mathayo

## (Mfalme wa Wayahudi)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kila injili imepata jina kutoka kwa mwandishi wake. Japo kitabu hiki cha kwanza hakitaji mwandishi wake na hata injli zingine lakini ushuhuda wa ulimwengu wa kanisa la kwanza unaeleza kwamba Mathayo ndiye mwandishi wa kitabu hiki na hata vitabu vingi vya kwanza vinathibitisha kuwa yeye Mathayo ndiye mwandishi kwa kujitaja, na alivyoanza kwa "Kama ilivyoandikwa na Mathayo." Mathayo, aliyekuwa mmoja wa wanafunzi wa Yesu alikuwa ni myahudi akiwaandikia Wayahudi kuhusu masihi wao. Jina lake halisi alikuwa ni Myunani mwana wa Alphayo. Alikuwa ni mtoza ushuru huko Palestina kwa Warumi hadi pale alipoitwa na Bwana kumfuata (Mathayo 9:9, 10; Marko 2:14-15). Kukubali kwake kwa haraka kulimfaya awe na huduma nzuri ya Bwana Yesu.

**Muda wa Kuandikwa: Kati ya Miaka ya 50 au 60 B.K.** Muda wa Mathayo ulikuwa tangu miaka ya 40 B.K. hadi 140 B.K. lakini "ukweli kwamba kuharibiwa kwa Yersalemu katika miaka ya 70 B.K. ni tkio linalotazamwa kama tukio lijalo (24:2) na hivyo ni vema tukawa na raehe za mwanzo. Wengine wanasema kuwa hiki ndicho kitabu cha kwanza kuandikwa (miaka ya 50 B.K.) na wengine husema kuwa si kitabu cha kwanza kwa sababu hudai kwamba kiliandikwa miaka ya 60.[55]

**Nia na Makusudi:** Kama ushahidi wa swali alilouliza Yesu kwa wanafunzi wake katika sura ya 16:13-15, Mathayo aliwaandikia wayahudi kuwajibu maswali yao juu ya Yesu Mnazareti. Yesu alikuwa amewaeleza kwamba yeye ni Masihi wao. Je alikuwa ni masihi aliyeelezwa katika Agano la Kale aliyetabiriwa na manabii? Kama ni hivyo kwa nini walimu wa dini walishindwa kumpokea na kwa nini aliweka ufalme ulioahidiwa. Je utakuwepo kweli na kama utakuwepo ni lini? kwa hiyo Mathayo akawa anawaandikia kuwajulisha kuwa masihi ni huyu ambaye amekuwa akisubiriwa. Hii inaonekana katika ukoo wa Yesu (1:1-17); kumtembelea Magidalena (2:1-12); kuingia kwake Yerusalemu (21:5); hukumu ya mataifa (25:31-46); kutajwa tajwa kwa "ufalme wa mbinguni" na hizi ni sawa na injili zingine na katika Agano la Kale unabii unakamilika.

**Mwonekano wa Yesu katika Mathayo:** Kama ilivyokwisha kuelezwa kusudi la Mathayo lilikuwa ni kumweleza Yesu kwamba yeye ni Masihi aliyetegemewa tangu Agano la Kale. Ni mwana wa Ibrahimu na Daudi. Kwa hiyo ni mfalme aliyekuja akitoa ufalme. Neno "mfalme wa mbinguni" linaonekana mara thelathini na mbili katika injili. Ili kuonyesha kwamba Yesu huyu anakamilisha yaliyotegemewa tangu Agano la Kale. Mathayo ametumia mifano mingi ya vifungu vya Agano la Kale kuliko kitabu kingine cha Agano Jipya maana ni mara 130.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utu na Wonekano wa Mfalme (1:1–4:25)**
   a. Kuzaliwa Kwake (1:1-25)
      1:1-17 1:18-25
   b. Kujulikana Kwae (2:1-12)
   c. Njozi zake (2:13-23)
      2:13-15 2:16-23
   d. Watangulizi Wake (3:1-17)
      3:1-12 3:13-17
   e. Majaribu Yake (4:1-11)
   f. Wanafunzi Wake (4:12-25)
      4:12-17 4:18-22 4:23-25

2. **Kutangazwa au Kuhutubiwa kwa Mfalme (5:1–7:29)**
   a. Kuhusu Mambo ya Mwili (5:1-12)
   b. Kuhusu Majukumu ya Waumini (5:13-20)
   c. Kuhusu Mahusiano (5:21-48)
   d. Kuhusu Kutoa, Maombi na Kufunga (6:1-18)
      6:1-6 6:7-15 6:16-18
   e. Kuhusu Hazina ya Kweli (6:19-34)
      6:19-24 6:25-34

f. Ckuhusu Kutimizwa kwa Sheria (7:1-29)

| | | |
|---|---|---|
| 7:1-6 | 7:13-14 | 7:24-29 |
| 7:7-12 | 7:15-23 | |

**3. Uweza wa Mfalme (8:1–11:1)**

a. Uponyaji (8:1-17)

| | |
|---|---|
| 8:1-13 | 8:14-17 |

b. Kuita Wengine (8:18-22)
c. Kutuliza Dhoruba (8:23-27)
d. Kukemea Mapepo (8:28-34)
e. MUponyaji Zaidi (9:1-38)

| | |
|---|---|
| 9:1-8 | 9:14-17 |
| 9:9-13 | 9:18-38 |

f. Kuwaelekeza Wafuasi Wake (10:1–11:1)

| | |
|---|---|
| 10:1-15 | 10:24-39 |
| 10:16-23 | 10:40–11:1 |

**4. Mipango na Kuendelea Kukataliwa kwa Mfalme (11:2–16:12)**

a. Sifa ya Yesu kwa Yohana (11:2-19)
b. Wito wa Kutubu (11:20-30)

| | |
|---|---|
| 11:20-24 | 11:25-30 |

c. Uvamizi wa Mafarisayo (12:1-50)

| | | |
|---|---|---|
| 12:1-7 | 12:30-32 | 12:46-50 |
| 12:8-21 | 12:33-37 | |
| 12:22-29 | 12:38-45 | |

d. Mifano (13:1-58)

| | | |
|---|---|---|
| 13:1-9 | 13:31-32 | 13:45-46 |
| 13:10-17 | 13:33-35 | 13:47-52 |
| 13:18-23 | 13:36-43 | 13:53-58 |
| 13:24-30 | 13:44 | |

e. Kukatwa kichwa kwa Yohana (14:1-12)
f. Miujiza Zaidi (14:13-36)

| | |
|---|---|
| 14:13-21 | 14:22-36 |

g. Mila na Unafiki (15:1-20)

| | |
|---|---|
| 15:1-14 | 15:15-20 |

h. Uponyaji zaidi (15:21-39)

| | | |
|---|---|---|
| 15:21-28 | 15:29-31 | 15:32-39 |

i. Uvamizi Zaidi (16:1-12)

**5. Maandalio ya Wanafunzi wa Mfalme (16:13–20:28)**

a. Ukiri wa Petro (16:13-28)

| | | |
|---|---|---|
| 16:13-20 | 16:21-23 | 16:24-28 |

b. Kubadilika Sura (17:1-13)
c. Mapepo (17:14-23)
d. Imani na Ushuru (17:24-27)
e. Imani na Upendo (18:1–19:12)

| | | |
|---|---|---|
| 18:1-6 | 18:12-14 | 18:21-35 |
| 18:7-11 | 18:15-20 | 19:1-12 |

f. Imani na Watoto (19:13-15)
g. Imani na Ufuasi (19:16-30)

| | |
|---|---|
| 19:16-26 | 19:27-30 |

h. Kuheshimu Makubaliano (20:1-16)
i. Mamlaka au Huduma (20:17-28)

| | |
|---|---|
| 20:17-19 | 20:20-28 |

**6. Mwonekano wa Mfalme (20:29–23:39)**

a. Kuponya Kipofu (20:29-34)
b. Kuingia Yerusalemu (21:1-27)

| | |
|---|---|
| 21:1-11 | 21:18-22 |
| 21:12-17 | 21:23-27 |

c. Kufundisha Mifano (21:28–22:14)

| | | |
|---|---|---|
| 21:28-32 | 21:33-46 | 22:1-14 |

d. Kuvamiwa Tena (22:15-46)
   22:15-22 | 22:23-46
e. Mafarisayo Wajidhihirisha (23:1-39)
   23:1-12 | 23:13-36 | 23:37-39

**7. Kutabiliwa kwa Mfalme (24:1–25:46)**

a. Maandalizi ya Kurudi Kwake (24:1-51)
   24:1-14 | 24:29-31 | 24:42-51
   24:15-28 | 24:32-41
b. Mifano ya Maandalizi (25:1-30)
   25:1-13 | 25:14-30
c. Hukumu (25:31-46)

**8. Shauku au Kukataliwa kwa Mfalme (26:1–27:66)**

a. Kukanwa na Kukamatwa (26:1-56)
   26:1-5 | 26:20-25 | 26:47-56
   26:6-13 | 26:26-35
   26:14-19 | 26:36-46
b. Mateso na Kukanwa (26:57-75)
   26:57-68 | 26:69-75
c. Majuto (27:1-10)
d. Kusulubiwa (27:11-56)
   27:11-26 | 27:27-32 | 27:33-56
e. Mazishi (27:57-66)

**9. Uthibitisho wa Mfalme (28:1-20)**

a. Amefufuka (28:1-10)
b. Kuonekana Kote (28:11-15)
c. Utume Mkuu (28:16-20)

# Marko

## (Mtumishi wa Bwana)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Injili ya Marko haina jina kwa sababu mtunzi wake hajulikani. Kichwa cha habari, “kama ilivyoandikwa na Marko” iliongezwa baadaye kabla ya miaka ya 125 B.K., lakini kuna sababu za nguvu na zinazoeleweka (za ndani na nje) kwamba Marko ndiye mwandishi. Ushuhuda wa kwanza katika kanisa la kwanza ni kwamba Marko alikuwa ni mmoja wa waliokuwa na mtume Petro na hivyo ndiye mwandishi.”[56] Miaka ya 112 B.K. Papia alimweka Marko kama “Mkarimani wa Petro.” Walter M. Dunnett anaeleza, “ulinganifu wa hotuba ya Petro katika Matendo 10:36-43 na Marko zinaonesha umuhimu wa maisha ya Yesu ambayo Marko katika injili yake ameieleza kwa undani zaidi.”[57]

Ijapokuwa Marko hakuwa mwanafunzi wa Yesu alikuwa ni mwana wa mwanamke aitwaye Maria, mtu mwenye utajiri na alikuwa na nafasi Yerusalemu (Matendo 12:12), msaidizi wa Petro (1 Petro 5:13), na mpwa wa Barnaba (Wakolosai 4:10). Umoja huu, hasa umoja wake na Petro ambaye kwa kweli alikuwa ni sababu kubwa ya habari nyingi za Marko inataja mamlaka ya kitume katika injili ya Marko. Japo Petro amejisemea Marko kijana wangu (1 Petro 5:13), yamkini Petro ndiye aliyemfanya Marko ampokee Yesu.

Kwa nyongeza Marko alikuwa ni mtu wa karibu sana na Paulo na Charles Ryrie anaandika:

> Alikuwa na faida kubwa ya kufuatana na Paulo pamoja na Barnaba katika safari yao ya kwanza ya kimisionari lakini hakuweza kukaa nao. Kwa sababu Paulo alikataa kufuatana naye katika safari yake ya pili ya kimisionari na akaondoka na Barnaba hadi Kipro (Mdo. 15:38-40). Baada ya miaka kadhaa aliungana na Paulo tena (Wakolosai 4:10; Philimoni 24), na hata kabla ya kukataliwa kwa Paulo alitumwa na mitume (2 Timotheo 4:11). Historia yake inathibitisha kwamba kushindwa kwa mara moja katika maisha haina maana ya kwamba umeisha kosa maana au umesha shindwa hapana.[58]

**Muda wa Kuandikwa: Karne ya 50 au 60 B.K.** Muda wa kitabu hiki ni mgumu sana japo wasomi wengi husema yamkini hiki ni kitabu cha kwanza katika injili hizi nne, lakini mistari mingi ya injili hii imenakiri katika injili zingine tatu. Injili hii ya Marko iliandikwa kabla ya miaka ya 70 B.K. na wakati wa kuharibiwa kwa hekalu la Yerusalemu (13:2).

**Nia na Makusudi:** Nia ya Marko ni "Kristo Mtumishi." Mkazo wa huduma na dhabihu umeelezwa vizuri katika 10:45, ***"kwa sababu mwana wa mtu hakuja kutumikiwa bali kutumika na kutoa nafsi yake iwe fidia kwa wengi."*** Usomaji wa makini katika kifungu hiki utaona Huduma na Dhabihu yamedhihirishwa na Marko.

Marko amehusika sana na Warumi au wasomaji watakatifu. Kama matokeo uzazi wa Yesu unafutwa sambamba na hotuba ya mlimani. Hukumu ya viongozi wa dini inamaliza nguvu kwa sabau walitaka waonekane sana na wayahudi. Kwa kuwa Marko anamwonesha Yesu kama mtumishi, mtumishi wa Bwana, hivyo kitabu kinatazama katika kazi za Yesu kama mtumishi mwaminifu katika kazi zake.

**Mwonekano wa Yesu katika Marko:** Kwa kweli Marko amemwonyesha Yesu kama mtumishi ambaye ni dhabihu aliyekubali kuyatoa maisha yake kwa ajili ya fidia ya wengi. Na mtazamo uko katika kazi zake za kimwili na kiroho ambapo anaonekana kuwatanguliza wengine kuliko yeye. Utumishi huu wa Yesu unaonekana katika misingi ifuatayo:

> Mifano kumi na nane nje ya ile saba inaonekana katika Marko – baadhi yake iko katika sentensi iliyokamili lakini anaorodhesha miujiza thelathini na tano kiwango kikubwa kabisa katika injili zote.[59]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Maandalizi ya Mtumishi kwa Ajili ya Huduma (1:1-13)**
    a. Mtangulizi Wake (1:1-8)
    b. Ubatizo Wake (1:9-11)
    c. Majaribu Yake (1:12-13)

2. **Mahubiri ya Mtumishi katika Galilaya (1:14–9:32)**
    a. Ujumbe Wake (1:14–2:12)
    1:14-28 | 1:29-45 | 2:1-12
    b. Vipingamizi vya Mwanzo (2:13–3:35)
    2:13-22 | 3:1-12
    2:23-28 | 3:13-35
    c. Mifano (4:1-34)
    4:1-12 | 4:26-29
    4:13-25 | 4:30-34
    d. Miujiza (4:35–5:43)
    4:35-41 | 5:1-20 | 5:21-43
    e. Kukua kwa Upinzania (6:1–8:26)
    6:1-6 | 6:33-52 | 7:14-23
    6:7-13 | 6:53-56 | 7:24-37
    6:14-32 | 7:1-13 | 8:1-26
    f. Ukiri wa Petro kwa Yesu (8:27-33)
    g. Gharama ya Ufuasi (8:34–9:1)
    h. Kubadilika sura Sura (9:2-13)
    i. Kuponywa kwa Kijana Aliyepagawa na Pepo (9:14-29)
    j. Maneno ya Yesu ya Kwanza juu ya Kifo Chake (9:30-32)

3. **Mahubiri ya Mtumishi Huko Perea (9:33–10:52)**
    a. Yesu Anafundisha ili Kuwaandaa Wafuasi (9:33–10:45)
    9:33-37 | 10:1-12 | 10:17-31
    9:38-50 | 10:13-16 | 10:32-45
    b. Kipofu Batromayo Aponywa (10:46-52)

4. **Shauku ya Mtumishikatika Yerusalemu (11:1–15:47)**
    a. Htambulisho Wake wa Kawaida (11:1-19)
    11:1-14 | 11:15-19
    b. Maelekezo Yake juu ya Maombi (11:20-26)
    c. Upnzani Wake na Viongozi (11:27–12:44)
    11:27-33 | 12:13-27 | 12:41-44
    12:1-12 | 12:28-40
    d. Maelekezo Yake juu ya Yajayo (13:1-37)
    13:1-2 | 13:14-23 | 13:33-37
    13:3-8 | 13:24-27
    13:9-13 | 13:28-32

e. Shauku Yake (14:1–15:47)

| | | |
|---|---|---|
| 14:1-11 | 14:43-52 | 15:16-21 |
| 14:12-21 | 14:53-65 | 15:22-41 |
| 14:22-31 | 14:66-72 | 15:42-47 |
| 14:32-42 | 15:1-15 | |

5. **Mafanikio ya Mtumishi katika Kufufuka Kwake (16:1-20)**
   a. Kufufuka Kwake (16:1-8)
   b. Mwonekano Wake (16:9-18) *Kitabu cha Maswali*
   c. Kupaa Kwake (16:19-20) *Kitabu cha Maswalit*

# Luka

## (Mwana wa Mtu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kitabu cha Luka na Matendo vyote vinavyoelekezwa kwa Theophilo, kama vitabu viwili vimeandikwa na Luka na Luka hapa anaonekana kuwa mwandishi wa Luka na matendo na kunazo sababu nyingi kwamba luka ndiye aliyeandika “daktari mpendwa” (Wakolosai 4:14) .

Vitabu hivi vinafanya robo ya Agano Jipya la Kiyunani, na sehemu pekee ambapo tunaweza kuliona jina hili ni katika Wakolosai 4:14; 2 Timotheo 4:11; na Filimoni 24, na anasemekana kwamba anajisema yeye mwenyewe katika sehemu ya Matendo anaposema “sisi” (16:10-17; 20:5–21:18; 27:1–28:16). Neno hili sisi katika Matendo linaonekana kwamba mtunzi alikuwa karibu sana ni mmoja wa watu waliosafiri na Paulo. Japo ni wote lakini wawili waliofuatana na Paulo wametajwa na orodha hii inapunguziwa kwa watoto na Luka. Kwa njia hiyo ya kondoa rafiki wa Paulo “mpenzi, Luka daktari” (Wakolosai 4:14), na “Mtumishi mwenzake” (Philimon 24) alikuwa ni mtu sawa na Paulo.

Inaonekana dhahiri kabisa katika Wakolosai 4:10-14 kwamba Luka alikuwa ni Mataifa kwa sababu Paulo alionyesha utofauti kati yake na waebrania ayahudi. Mtume anaeleza kwamba wafanyakazi, Aristarchus, Marko, na Yohana walikuwani wayahudi. Hii inaonyesha kwamba Epaphra, Luka na Dema pia wametajwa katika mstari huu walikuwa ni Mataifa na si Wayahudi. Ufahamu wa Luka wa lugha ya Kiyunani na kabila yao katika Matendo 1:19 pia inaonyesha kwamba hakuwa ni Myahudi.”[60]

Hatuelewi kuhusiana na maisha yake wala kuongoka kwake lakini hakuwa mshuhudiaji wa maisha ya Yesu (Luka 1:2). Japo alikuwa ni daktari alikuwa kabisa ni Mwinjilisti akiandika injili hii na kitabu cha Matendo na akimsaidia Paulo katika safari zake za Kimisionari. Luka alikuwa na Paulo kipindi cha kifo cha Mitume (2 Timotheo 4:11), lakini hatuelewi mwisho wa maisha yake kwa uhakika.[61]

**Muda wa Kuandikwa: 60 B.K.** Nyakati mbili zinazosadikiwa kuwa ni muda wa injlili ya Luka ni: (1) B.K. 59-63, na (2) Karne ya 70 au karne ya 80, lakini hitimisho la matendo linaonyesha kuwa Paulo alikuwa Rumi na Luka alikuwa kiandika na aliandika kabla ya kitabu cha Matendo (Mdo. 1:1), Injili ya Luka imeandikwa mapema kati ya miaka ya 60 B.K.

**Nia na Makusudi:** Kusudi la Luka limeelezwa katika mistari minne ya kwanza ya injili hii.

> ***Kwa kuwa watu wengi wamenitia mkono kutunga kwa taratibu habari ya mambo yale yaliyotimizwa katikati yetu, kma walivyotuhadithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyanena watumishi wa lile neno tokea mwanzo nimeona vema mimi nami kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa yale mambo toka mwanzo kukuandikia kwa taratibu theofilo mtukufu, upate kujua hakika ya mambo uliyofundishwa.*** (Luka 1:1-4)

Vitu vingi vinapaswa kuangaliwa kulingana na uelezaji huu ili kuiwakilisha injili:

Luka anaeleza kwamba kazi yake imetiwa nguvu na watu wengine (1:1), na kwamba ameshuhudia (1:2), na ameamua kuandika kwa utaratibu (1:3) chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu kumwandikia Theofilo maswala ya imani aliyoisikia (1:4). Huu ni utafiti wa kina na makini sana ulioleta kitabu hiki.[62]

Kama Mtakatifu Luka alijisikia kuwandika vitabu vyake viwili juu ya maisha ya Kristo ili viwe ni faida kwa wasomaji watakatifu. Na hii ni kweli kulingana na ukweli kwamba Luka “alitafasiri neno la Kiaramaiki kwa neno la kiyunani na anaeleza mila za kiyahudi na jinsi walivyo ili kuifanya injili yake ikubalike kwa uongozi wake halisi aliokuwa nao wa kiyunani.”[63]

Luka, aliandikwa kama “daktari mpendwa,” na imeonekana mara nyingi kwa urefu sana katika injili. Inamwakilisha masihi kama Mwana wa Mtu aliyekuja kutafuta na kuokoa waliopotea (19:10). Katika Mathayo tunamwona Yesu kama mwana wa Daudi, Mfalme wa Israeli, katika Marko tunamwona Bwana mtumishi, akiwatumikia wengine na katika Luka tunamwona kama mwana wa Mtu akikutana na mahitaji ya wanadamu, mtu mkamilifu kati ya watu wote, aliyechaguliwa kutoka watu, aliyejaribiwa katika watu na aliyestahili kuwa mwokozi na kuhani mkuu. Katika Mathayo tunaona umuhimu mwingi wa matukio yake na katika Marko tunaona ufupi wa maelezo yake lakini katika Luka tunaona kwa undani kabisa matukio haya kwa njia ya daktari/mwana historia.

Maisha yake makamilifu kama mwana wa Mtu na wakati huo huo mwana wa Mungu unaonekana wazi kwa ukweli kwamba kuzaliwa kwake katika ukoo kumeanzia tangu enzi za Adamu (3:38; na angalia kuwa Mathayo inakwenda nyuma hadi enzi za Ibrahimu). Hekima zake zinaonekana katika 2:40-52 na maadili yake na ukamilifu wake unashuhudiwa wakati wa ubatizo wake kwa njia ya sauti ya Baba yake kutoka mbinguni na kwa upako wa Roho Mtakatifu (3:21-22). Yesu ndiye pekee tuliyenaye na ni mkamilifu Kimwili, kiakili na Kiroho.

**Mwonekano wa Yesu katika Luka:** Utu na Huruma ya Yesu vimerudiwa na kukaziwa katika injili ya Luka. Luka anatupa kwa ukamilifu kabisa juu ya Kristo, kuzaliwa kwake na hata maendelkeo yake. Ni mwana wa mtu kimawazo ili kwamba apate kubeba huzuni za dhambi ya wanadamu na atupatie zawadi ya wokovu. Yesu peke yake ndiye anayekamilisha wazo la mwanadamu aliye kamili.[64]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi: Njia na Kusudi la Kuandika (1:1-4)**

2. **Kutambuliwa kwa Mwana wa Mtu na Wanadamu (1:5–4:13)**
   a. Matukio Yaliyopelekea Kuzaliwa kwa Yesu (1:5-56)
      1:5-25 — 1:39-45
      1:26-38 — 1:46-56
   b. Matukio Yaliyoambatana na Kuzaliwa kwa Yesu (1:57–2:38)
      1:57-66 — 2:1-20
      1:67-80 — 2:21-38
   c. Matukio Kipindi cha Utoto wa Yesu (2:39-52)
      2:39-40 — 2:41-52
   d. Matukio Yaliyopelekea Kuonekana kwa Yesu (3:1–4:13)
      3:1-20 — 3:23-38
      3:21-22 — 4:1-13

3. **Huduma ya Wana wa Mtu kwa Wanadamu (4:14–9:50)**
   a. Kutambulikana kwa Yesu (4:14-30)
   b. Kuonekana kwa Uweza za Yesu (4:31–5:28)
      4:31-37 — 5:1-11 — 5:27-28
      4:38-44 — 5:12-26
   c. Maelezo ya Mpango wa Yesu (5:29–6:49)
      5:29-39 — 6:12-19 — 6:46-49
      6:1-11 — 6:20-45
   d. Kukua kwa Mpango wa Yesu (7:1–9:50)
      7:1-17 — 8:16-21 — 9:12-27
      7:18-39 — 8:22-25 — 9:28-45
      7:40-50 — 8:26-39 — 9:46-50
      8:1-3 — 8:40-56
      8:4-15 — 9:1-11

4. **Kukataliwa kwa Mwana wa Mtu na Wanadamu (9:51–19:27)**
   a. Kuongezeka kwa Upinzani dhidi ya Yesu (9:51–11:54)
      9:51-56 — 10:30-37 — 11:29-36
      9:57-62 — 10:38-42 — 11:37-54
      10:1-16 — 11:1-13
      10:17-29 — 11:14-28

b. Maelekezo katika Kumkataa Kristo (12:1–19:27)

| | | |
|---|---|---|
| 12:1-12 | 14:7-15 | 17:1-10 |
| 12:13-34 | 14:16-24 | 17:11-21 |
| 12:35-48 | 14:25-35 | 17:22-37 |
| 12:49-59 | 15:1-7 | 18:1-8 |
| 13:1-9 | 15:8-10 | 18:9-17 |
| 13:10-17 | 15:11-32 | 18:18-34 |
| 13:18-21 | 16:1-13 | 18:35-43 |
| 13:22-35 | 16:14-18 | 19:1-10 |
| 14:1-6 | 16:19-31 | 19:11-27 |

**5. Mateso ya Mwana wa Mtu kwa Ajili ya Wanadamu (19:28–23:56)**

| | | |
|---|---|---|
| 19:28-44 | 21:25-28 | 22:54-65 |
| 19:45-48 | 21:29-33 | 22:66-71 |
| 20:1-8 | 21:34-36 | 23:1-7 |
| 20:9-18 | 21:37-38 | 23:8-12 |
| 20:19-26 | 22:1-13 | 23:13-25 |
| 20:27-47 | 22:14-23 | 23:26-32 |
| 21:1-9 | 22:24-38 | 23:33-49 |
| 21:10-19 | 22:39-46 | 23:50-56 |
| 21:20-24 | 22:47-53 | |

**6. Umuhimu wa Mwana wa Mtu kwa Wanadamu (24:1-53)**

| | |
|---|---|
| 24:1-12 | 24:36-49 |
| 24:13-35 | 24:50-53 |

# Yohana
## (Mwana wa Mungu Milele)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Tangu mwanzo wa karne ya pili, desturi za kanisa zilikuwa zimeshajenga injili nne na kuzipeleka kwa Yohana mtume,mwana wa Zebedayo kaka wa Yakobo. Yesu aliwaita Yohana na Yakobo "Wana wa Ngurumo" (Marko 3:17). Salome, mama yake, aliyemhudumia Yesu kule Galilaya na alikuwepo kipindi cha kusulubiwa kwake (Marko 15:40-41). Hakuwa karibu sana na Yesu kama mmoja wa wanafunzi lakini alitambulikana kama "mwanafunzi mpendwa" (13:23; 18:15-16; 19:26-27). Yohana ndiye aliyekuwa mwanafunzi wa ndani sana kati ya wanafunzi wote na mmoja wa wale watatu aliowachukua Yesu kwenda nao kwenye mlima aliogeuka sura (Mathayo 17:1) na alikuwa karibu sana na Petro. Baada ya Yesu kupaa Yohana alikuwa mmoja wa wale Paulo aliowatambua kama Msingi wa kanisa (Wagalatia 2:9).

Kwa kusema kabisa injili hizi nne hazieleweki waandishi wake maana hakuna jina lililoandikwa kwa kila kitabu kuonyesha kuwa ni nani aliyeandika. Hii hata hivyo, haishangazi kwa sababu injili hutofautiana na nyaraka (barua). Barua za Paulo zinaanza na jina lake ambacho ni kitu cha kawaida kwa barua katika ulimwengu. Hakuna mwandishi wa injili aliyejitaja jina lakini, kadri unavyooendelea kusoma utakuta mwandishi amejulikana katika kitabu chake alivyoandika, na walijulikana sana kulingana na desturi.

**Muda wa Kuandikwa: 85-90 B.K.** Injili hii ilikuwa ikijulikana katika kanisa kama ya "Nne" na kanisa linasadiki kwamba iliandikwa wakati Yohana akiwa mzee. Kwa hiyo kati ya miaka ya 85 na 95 inasadikika hivyo. Yohana 21:18, 23 inahitaji mpito wa muda, na Petro kuwa mzee na Yohana akaingia katika nafasi yake.[65]

**Nia na Makusudi:** Kitabu hiki ni zaidi ya kitabu kingine katika Biblia. Yohana anaeleza kwa ufasaha nia na makusudi ya Yesu katika injili yake. Kwa ufasaha kabisa kusudi la injili hii linafuatana na Thomaso aliyeshuhudia wakati wa kufufuka kwa Yesu. Thomaso alikuwa na mashaka ya kufufuka kwa Yesu (Yohana 20:24-25) na ghafla Bwana alijitokeza kwa wanafunzi na akamwambia Thomaso maneno haya,

> ***Lete hapa kidole chako uitazame mikono yangu uulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu wala usiwe asie amini bali aaminiye, Thomaso akajibu; Bwana wangu na Mungu wangu Yesu akamwambia wewe kwa kuwa umeniona umesadiki wa heri wale wasiioona wakasadiki.'*** (20:26-29)

Inafuata mabadiliko haya kwa kutazama hitaji la kumwamini Yesu ambayo sasa Yohana anaeleza nia na makusudi ya kitabu hiki,

***Basi kuna ishara nyingi yingine alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake zisizoandikwa katika kitabu hiki, lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo mwana wa Mungu; na kwa kuamini muwe na uzima kwa jina lake.*** (20:30-31)

Katika malezo haya Yohana alichagua ishara saba za miujiza ili aoneshe utu na ujumbe wa Kristo ili kwamba upate kuwasaidia watu kuja kwa Yesu Kristo kama mwokozi. Ishara hizi zinaonesha utukufu wa Yesu (Yohana 1:14; Isaya 35:1-2; Yoeli 3:18; Amosi 9:13). Ishara hizi saba zina haya yafuatayo:

1. Kubadili maji kuwa divai (2:1-11)
2. Mwana wa diwani (4:46-54)
3. Kumponya kiwete (5:1-18)
4. Kulisha umati mkubwa (6:6-13)
5. Kutembea juu ya maji (6:16-21)
6. Kuwaponya vipofu (9:1-7)
7. Kumfufua Lazaro (11:1-45)

Nia na makusudi ya injili ya Yohana imetofautika kulingana na jinsi ilivyo ukiilinganisha na injili za akina Mathayo, Marko, na Luka.

Ikiwa mtu atailinganisha injili ya Yohana na injili zingine atakuta kuna utofauti mkubwa sana. Yohana hakueleza kuzaliwa kwa Yesu, kubatizwa, majaribu, kukemea mapepo, mifano, kubadilika sura, meza ya Bwana, Gethsemane au hata kupaa kwake. Yohana ameeleza huduma ya Yesu kule Yerusalemu, Karamu ya wayahudi, mazungumzo ya Yesu ana kwa ana na watu (3:1–4:38; 18:28–19:16), na huduma kwa wanafunzi wake (13:1–17:26). Mwili mzima wa injili ya Yohana uko katika “Kitabu cha Ishara” (2:1–12:50) kilicho na ishara saba zinazomtangaza Yesu kama Masihi wa Mungu, mwana wa Mungu. Kitabu hiki cha ishara kinaeleza umuhimu wa ishara hizi. Kwa mfano tukichukua kuwalisha watu 5,000 (6:1-15), Yesu alijionyesha mwenyewe kama kwamba yeye ni mkate wa uzima ambao Baba ameutoa kwa ajili ya ulimwengu (6:25-35). Kitu kingine ambacho ni cha muhimu lakini hakikuonyeshwa ni neno “MIMI NI” neno lililosemwa na Yesu mwenyewe (6:35; 8:12; 10:7, 9, 11, 14; 11:25; 14:6; 15:1, 5).

Tofauti hizi ni lazima ziangaliwe kwa umakini sana. Injili haikukusudiwa kuwa kama ni historia. Kila injili ina lengo lake linalokamilisha makusudi yake. Na imekadiriwa kwamba ikiwa maneno yote aliyoyazungumza Yesu yangeandikwa katika Mathayo, Marko, Luka na Yohana yangesemwa kwa sauti kwa muda wa masaa kama matatu tu.[66]

**Mwonekano wa Yesu katika Yohana:** Kwa kuwa uungu wa Yesu ndio unaotawala katika biblia na wala hakuna kitabu kingine kinachomweleza Yesu kwa nguvu tofauti na biblia kama mwana wa Mungu. Ukweli ni kwamba Yeye anajulikana kama “Mtu aitwaye Yesu” (9:11) na pia anaitwa “Mungu na ni Mmoja na hakuna Mwingine” 1:18), “ Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai (6:69) au “Mtakatifu wa Mungu” (6:69).

Maelezo haya ya uungu wa Yesu yameelezwa na maneno saba ya “MIMI NI” aliyoyasema Yesu na yamenakiriwa katika injili ya Yohana. Na maelezo haya saba ni:

1. “Mimi ni Mkate wa Uzima” (6:35)
2. “Mini ni Nuru ya Ulimwengu” (8:12)
3. “Mimi ni Mlango” (10:7, 9)
4. “Mimi ni Mchungaji Mwema” (10:11, 14)
5. “Mimi ni Ufufuo na Uzima” (11:25)
6. “Mimi ni Njia na Kweli na Uzima” (14:6)
7. “Mimi ni Mzabibu wa Kweli” (15:1, 5).

Tofauti nyingine ya injili ya Yohna inatazama katika utu wa Yesu na kuna ushahidi wa aina tano unaothibitisha kwamba Yesu ni mwana wa Mungu. Katika Yohana 5:31-47, Yesu alijibu katika mabishano. Walimshutumu kwamba ushuhuda wake haukuwa wa kweli na Yesu akaamua kuwaeleza ukweli na kuwaonesha kuwa madai yao hayakuwa ya kweli kwa kuwaonyesha mambo mengine ya kumthibitisha na kuthibitisha alichokuwa akikisema. Na shuhuda zingine zinamuhusisha baba yake (5:32, 37), Yohana mbatizaji (5:33), Miujiza yake (5:36), Maandiko (5:39), na Musa (5:46). Baadaye, katika 8:14 alisema kwamba ushuhuda wake ni wa kweli hakika. Kwa namna nyingine Yesu alitumia Agano la Kale kuthibitisha uungu wake kwa kusema “MIMI NI” au YAHWE (4:25-26; 8:24, 28, 58; 13:19; 18:5-6, 8). Na zinginge zinaonekana katika 1:1; 8:58; 10:30; 14:9; 20:28.[67]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi: Uanadamu wa Mwana wa Mungu (1:1-18)**
   a. Uungu wa Kristo (1:1-2)

b. Kazi ya Yesu (1:3-5)
c. Watangulizi wa Yesu (1:6-8)
d. Kukataliwa kwa Yesu (1:9-11)
e. Kukublika ka Yesu (1:12-13)
f. Ubinadamu wa Kristo (1:14-18)

**2. Kujitambulisha kwa Mwana wa Mungu (1:19–4:54)**

a. Yohana Mbatizaji (1:19-34)
b. Wanafunzi wa Yohana (1:35-51)
c. Katika Harusi huko Kana (2:1-11)
d. Hekaluni huko Yerusalemu (2:12-35)
e. Kwa Nikodemo (3:1-21)
f. Kwa Yohana Mbatizaji (3:22-36)
g. Mwanamke Msamaria (4:1-42)
h. Kwa Watawala wa Kapernaumu (4:43-54)

**3. Upinzani kwa Mwana wa Mtu (5:1–12:50)**

a. Katika Karamu katika Yerusalemu (5:1-47)

| | | |
|---|---|---|
| 5:1-17 | 5:33-35 | 5:39-47 |
| 5:18-24 | 5:36 | |
| 5:25-32 | 5:37-38 | |

b. Kipindi cha Pasaka katika Galilaya (6:1-71)

| | | |
|---|---|---|
| 6:1-14 | 6:26-40 | 6:59-65 |
| 6:15-25 | 6:41-58 | 6:66-71 |

c. Katika Sherehe Kwenye Hema huko Yerusalemu (7:1–10:21)

| | | |
|---|---|---|
| 7:1-24 | 8:12-30 | 9:13-34 |
| 7:25-39 | 8:31-47 | 9:35-41 |
| 7:40-53 | 8:48-59 | 10:1-21 |
| 8:1-11 | 9:1-12 | |

d. Kwenye Ubariki huko Yerusalemu (10:22-42)

| | |
|---|---|
| 10:22-30 | 10:31-42 |

e. Hata Bethania (11:1–12:11)

| | | |
|---|---|---|
| 11:1-16 | 11:38-46 | 12:1-11 |
| 11:17-29 | 11:47-53 | |
| 11:30-37 | 11:54-57 | |

f. Hata Yerusalemu (12:12-50)

| | | |
|---|---|---|
| 12:12-19 | 12:27-36 | 12:44-50 |
| 12:20-26 | 12:37-43 | |

**4. Maelekezo ya Mwana wa Mtu (13:1–16:33)**

a. Kuhusu Msamaha (13:1-20)

| | |
|---|---|
| 13:1-4 | 13:5-20 |

b. Kuhusu Kukanwa Kwake (13:21-30)
c. Kuhusu Kuondoka Kwake (13:31-38)
d. Kuhusu Mbingu (14:1-15)

| | |
|---|---|
| 14:1-6 | 14:7-15 |

e. Kuhusu Roho Mtakatifu (14:16-26)
f. Kuhusu Amani (14:27-31)
g. Kuhusu Matunda (15:1-17)

| | |
|---|---|
| 15:1-11 | 15:12-17 |

h. Kuhusu Ulimwengu (15:18–16:4)

| | |
|---|---|
| 15:18-27 | 16:1-4 |

i. Kuhusu Roho Mtakatifu (16:5-15)
j. Kuhusu Kurudi Kwakwe (16:16-33)

| | |
|---|---|
| 16:16-22 | 16:23-33 |

**5. Maombezi ya Mwana wa Mungu (17:1-26)**

| | | |
|---|---|---|
| 17:1-12 | 17:13-21 | 17:22-26 |

**6. Kusulubiwa kwa Mwana wa Mungu (18:1–19:42)**

| | | |
|---|---|---|
| 18:1-11 | 19:1-15 | 19:31-37 |
| 18:12-24 | 19:16-22 | 19:38-42 |
| 18:25-27 | 19:23-27 | |
| 18:28-40 | 19:28-30 | |

7. **Kufufuka kwa Mwana wa Mungu (20:1-31)**
   a. Kaburi Tupu (20:1-10)
   b. Mwonekano wa Bwana Aliyefufuka (20:11-31)
      20:11-18 20:24-29
      20:19-23 20:30-31

8. **Hitimisho: Kuonekana katika Ziwa (21:1-25)**
   a. Kuonekana kwa Wanafunzi Wake (21:1-14)
      21:1-11 21:12-14
   b. Maneno kwa Petro (21:15-23)
      21:15-17 21:18-23
   c. Hitimisho la Injili (21:24-25)

# Matendo

## (Kueneza Injili)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Japo mwandishi wa kitabu hakutajwa lakini inasadikika kuwa ni Luka. Matendo ni kitabu cha pili cha kuandikwa na Luka daktari kwa Theophilo juu ya "yale ambayo Yesu aliyaanzisha na kuyafundisha."

Kulingana na kichwa chake cha habari "Matendo" au kwa kichwa chake cha habari Matendo ya Mitume. "Matendo ya Mitume" si jina zuri kwa sababu hakijumuishi matendo yote ya mitume. Ni Petro na Paulo tu ndio walioelezwa katika kitabu na si mitume wote, ijapokuwa Roho Mtakatifu aliahidiwa kwa mitume wote (1:2-8) ambao walipaswa kwenda ulimwengu wote kuihubiri injili kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Na wengi wamekuwa wakidai bora kingepewa jina "La Matendo ya Roho Mtakatifu" kwa sababu kinaeleza kuenea kwa ukristo tangu kuja kwa Roho Mtakatifu katika Matendo 2. Watu muhimu katika Matendo ni Petro, Yohana, Stefano, Philipo, Yakobo, Sila na Paulo.

**Muda wa Kuandikwa: 61 B.K.** Kuandikwa kwa kitabu hiki kumeelezwa vizuri na Stanley Toussaint kama ifuatavyo:

> Kuandikwa kwa kitabu cha matendo kunaweza kuwa kabla ya kuaharibiwa kwa Yerusalemu miaka ya 70 B.K. lakini watu wake hawataweza kusahaulika. Hii ni kweli kwa sababu ya msingi mmoja tu katika kitabu: kurudi kwa Mungu kwa wayahudi kwa sababu ya wayahudi kumkataa Yesu.
>
> Luka alikuwa na mambo mengi ya kifo cha Paulo 66-68 B.K. kama angetokea baada ya kukiandika kitabu cha Matendo.
>
> Luka hakumtaja Neronia a shida zake alizozipata zilizoanza baada ya moto mkubwa wa Rumi miaka ya 64 B.K.
>
> Hata hivyo, kujihami kwa ukristo mbele ya Nero kwa kutumia kitabu cha Matendo kupinga kwa yale yaliyokuwa yakifaywa na wakuu wa utawala wa Kirumi kwa kumwangalia Paulo yalikuwa ni mateso makali. Kwa kipindi hicho Nero alitamani kuliharibu kanisa na kujihami kwake kukatoka katika kitabu cha Matendo.
>
> Muda wa kuandikwa kitabu hiki unakubaliwa na wasomi wengi kuwa ni kati ya miaka ya 60-62 B.K. Sehemu yawezekana kuwa ni Rumi au sehemu zote mbili Kaisaria na Rumi. Muda wa kuandikwa, kuachiliwa kwa Paulo kulikuwa ni karibu na yawezekana alikuwa amekwisha achiliwa.[68]

**Nia na Makusudi:** Kitabu cha Matendo ni kitabu cha pekee sana katika Agano Jipya kwa sababu ndicho pekee kinachotoa uunganiko na vitabu vingine katika Agano Jipya. Kama kitabu cha pili cha Luka Kitabu hiki kinaendeleza kile Yesu ***"alianzisha na kufundisha"*** (1:1) kama ilivyonakiliwa katika injili, kinaanza na kupaa kwa Yesu na kinaendelea na kipindi cha nyaraka za Agano Jipya. Katika kitabu hiki tuna mwendelezo wa huduma ya Yesu kwa njia ya Roho Mtakatifu kwa mitume ambao waliendelea katika kuifundisha na kuhubiri na kuazisha kanisa, mwili wa Kristo. Matendo ni kitabu cha historia kati ya injili na Nyaraka.

Si kwamba inatuunganisha sisi tu lakini pia inaeleza maisha ya Paulo na inatupa matukio ya Kihistoria kwa barua zake. Katika hatua hii Matendo inatupa hesabu ya miaka 30 ya mwanzo ya uhai wa kanisa.

Baada ya muhtasari wa kitabu cha Matendo ndugu, Stanley Toussaint anaandika:

> Kusudi la kitabu cha Matendo linaweza kuelezeka kama ifuatavyo: Kwa kueleza injili ya Luka na mamlaka yaliyoelekezwa katika ufalme kutoka wayahudi hadi watakatifu na kutoka Yerusalemu hadi Rumi. Katika injili ya Luka swali linajibiwa' "kama ukristo una mizizi yake katika Agano la Kale na katika Yuda iweje sasa uwe ni wa ulimwengu?" Kitabu cha Matendo kinaendelea kwa uwazi kabisa katika kujibu swali hili.[69]

Matendo 1:8 inaeleza nia ya matendo–kutawaliwa na Roho Mtakatifu kunawawezesha watu wa Mungu kuwa mashahidi wa Yesu kuanzia Yerusalemu hadi Yudea na Samaria na hata mwisho wa nchi (Dunia)

**Mwonekano wa Yesu katika Matendo:** Yesu aliyefufuka ndiye kiini cha ujumbe katika Matendo. Maandiko ya Agano la Kale, habari za kufufuka, ushuhuda wa mitume na nguvu itendayo kazi ya Roho Mtakatifu zote zinaeleza kwamba Yesu ni Bwana na Kristo (2:22-36; 10:34-43). ***"Huyo manabii wote humshuhudia ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapataondoleo la dhambi"*** (10:43). ***"Wala hakuna wokovu mwingine katika awaye yote kwa maana hakuna jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu itupasalo sisi kuokolewa kwalo"*** (4:12).[70]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Mashahidi katika Yerusalemu (1:1–6:7)**
   a. Tegemeo la Walioteuliwa (1:1–2:47) Taarifa Endelevu ya 1
      1:1-8 1:12-26 2:14-36
      1:9-11 2:1-13 2:37-47
   b. Kupanuka kwa Kanisa katika Yerusalemu (3:1–6:7) Taarifa Endelevu ya 2
      3:1-10 4:13-31 5:17-32
      3:11-26 4:32-37 5:33-42
      4:1-12 5:1-16 6:1-7

2. **Mashahidi katika Yudea Yote na Samalia (6:8–9:31)**
   a. Mateso ya Stefano (6:8–8:1a)
      1) Kukamatwa kwa Stefano (6:8–7:1)
      2) Kujielezakwa Stefano (7:2-53)
         7:2-8 7:17-29 7:44-53
         7:9-10 7:30-34
         7:11-16 7:35-43
      3) Kukamatwa kwa Stefano (7:54–8:1a)
   b. Huduma ya Filipi (8:1b-40)
      8:1b-3 8:4-24 8:25-40
   c. Ujumbe wa Sauli (9:1-19a)
   d. Mgogoro wa Sauli (9:19b-31) Taarifa Endelevu ya 3

3. **Mashahidi hadi Mwisho wa Nchi (9:32–28:31)**
   a. Kupanuka kwa Kanisa hadi Antiokia (9:32–12:24) Taarifa Endelevu ya 4
      9:32-43 10:34-48 12:1-19
      10:1-23 11:1-18 12:20-24
      10:24-33 11:19-30
   b. Kupanuka kwa Kanisa katika Asia Ndogo (12:25–16:5) Taarifa Endelevu ya 5
      13:1-25 14:8-18 15:30-35
      13:26-43 14:19-28 15:36-41
      13:44-52 15:1-11 16:1-5
      14:1-7 15:12-29
   c. Kupanuka kwa Kanisa katika Fligia (16:6–19:20) Taarifa Endelevu ya 6
      16:6-13 17:1-9 18:1-21
      16:14-21 17:10-15 18:22-28
      16:22-34 17:16-21 19:1-10
      16:35-40 17:22-34 19:11-20
   d. Kupanuka kwa Kanisa hadi Rumi (19:21–28:31) Taarifa Endelevu ya 7
      19:21-41 22:1-30 26:1-32
      20:1-12 23:1-11 27:1-13
      20:13-16 23:12-22 27:14-44
      20:17-38 23:23-35 28:1-10
      21:1-14 24:1-27 28:11-29
      21:15-26 25:1-22 28:30-3
      21:27-40 25:23-27

# Sehemu ya 2
# Nyaraka za Paulo

**Utangulizi:** Tumemaliza vitabu vya kihistoria (Injili na Matendo), sasa tunakuja kwenye nyaraka ishirini na moja za Agano Jipya, ni ishirini na mbili iwapo na kitabu cha ufunuo kingeingizwa kama nyaraka, ambacho kwa kweli ni mojawapo ya nyaraka (angalia Ufunuo 1:4). Kwa sababu ya asili yake na jinsi kinavyojieleza tunakitofautisha na tunakiita kuwa ni kitabu cha unabii cha Agano Jipya. Nyaraka zimegawanywa katika makundi ya nyaraka za Paulo na nyaraka zisizo za Paulo na ziko katika makundi mawili. Nyaraka tisa ziliandikwa kwa ajili ya kanisa na nne kwa ajili ya wachungaji. Na baadaye zikafuatwa na tisa za Waebrania Wakristo. Maswali mengi yanaweza kuinuka kama maana ya matumizi ya injili ya Wakristo. Kwa hiyo nyaraka zinajibu maswali haya na kutoa tafasiri za mtu na kazi ya Kristo na kuitumia kweli ya injili kwa waaminio.

**Historia ya Paulo:** Paulo alikuwa anajulikana kwa muda mrefu kama Sauli wa Tarso. Alikuwa amezaliwa katika familia ya Kiyahudi katika mji uitwao Tarso ya Kirikia. Hakuwa Myahudi tu lakini kwa ushuhuda wake alikuwa ni mfarisayo wana wa mfarisayo (Matendo 23:6), Muebrania wa waebrania (alizungumza Kiebrania na Kiaramaiki), wa kabila ya Benjamini (Wafilipi 3:4-5), na alikuwa amefundishwa kufanya biashara ya mahema wakati wa ujana wake (Matendo 18:3). Wakati wa ujana wake alikuwa ameshawahi kwenda Yerusalemu na kulingana na ushuhuda wake alikuwa amejifunza kwa mwalimu aitwaye Gamalieli mwalimu wa shule ya Hillel (Matendo 22:3). Katika masomo yake alikuwa amekomaa sana katika dini ya wayahudi na wafuasi wake wengi (Wagalatia 1:14).

Shauku yake kama Myahudi wa dini alikuwa ameielekeza katika kulitesa kanisa. Kama mfarisayo kijana alikuwepo na akaidhinisha kifo cha kupondwa mawe Stefano hadi kufa (Matendo 7:58-83). Katika hali yake ya kupinga ukristo wanaume kwa wanawake aliotembea nao kutoka kwa kuhani mkuu aliendа nao katika miji na kuriharibu kanisa la Kristo (Matendo 26:10-11; Wagalatia 1:13). Ilikuwa ni katika moja ya safari zake Paulo akakutana na Yesu akielekea Dameski na akampokea Yesu (Matendo 9).

Paulo pia alikuwa akizifahamu tamaduni za Kiyunani kwa sababu alikuwa tayari amekwisha pokea elimu ya Kiyunani (Matendo 17:28; Tito 1:12). Kwa hiyo ilimfanya aelewe na kuwaelewa wayunani. Kwa kusoma kwake huku kulimfanya aelewe hata vile vilivyokuwa vikiandikwa katika lugha hii wakati akiwa nao hata kabla ya yeye kuzaliwa. Kwa nyongeza Paulo alikuwa raia wa Rumi, kwa sababu alizaliwa huko (Matendo 22:28). Kwa sababu ya Hii aliweza kukata rufaa kaisaria kama raia wa Rumi wakati akiwa amefungwa Filipi (Matendo 16:37-39).

Paulo aliweza kuwa ni mmoja wa walioteuliwa kubeba ujumbe wa Bwana wa injili kwa mataifa. Paulo anasema, ***"Nimekuwa hali zote kwa watu wote ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu"*** (1 Wakorintho 9:22).

**Kubadilishwa kwa Paulo:** Kadri alivyozidi kuliharibu kanisa la Kristo akiwa katika njia ya kwenda Dameski Paulo alikutana na utukufu wa aliyefufuka, Kristo ambaye alileta mapinduzi katika maisha yake (Matendo 9:3-30).

Alikuwa amewakanusha Wakristo wadi kwamba Yesu ni mwana wa Mungu. Lakini hakuamni kwamba alifufuka kama alivyokuwa akidai Stephano kipindi analia, ***"tazama, naona mbingu zimefunguka na mwana wa Mungu amesimama upande wa kuume wa Mungu"*** (Matendo 7:56). "Iyaa!" alilia huku wakimpiga mawe. Sauli akiwa amesimama pembeni ***"akiwahimiza hadi wamuue."*** Lakini Yesu aliposimama na kuzungumza naye akiwa safarini kwenda Dameski alijua ya kwamba Stephano alikuwa kweli ila alipotoka. Yesu alikuwa hai hata hivyo na yeye alikwa ni mwana wa Mungu. Kwa hiyo katika sinagogi la Dameski Sauli (kwa sasa ni Paulo) alimnena Yesu kama mwokozi. Yesu alikuwa hai, na ni mwana wa Mungu. Kwa kuwa hali hii ilikuwa ni ya ghafla na ya kuvutia ilileta changamoto sana maana madhara yaliisha. Matokeo yake yalikuwa ni ya kisaikolojia na yenye kueleweka na kila mtu. Alikaa Arabia na Dameski kitambo kabla ya kwenda Yerusalemu (Wagalatia 1:16-19). Na baadaye alirudi nyumbani kwake na kwa muda wa miaka minane hadi kumi shughuli yake ilianza kueleweka.[71]

**Mchanganuo wa Nyaraka za Paulo:** Kabla ya kuzipitia nyaraka za Paulo ni vizuri tukaona mchanganuo wake.[72]

**Nyaraka za Gerezani**

Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, na Philimoni ni "Nyaraka Zinazoitwa za Gerezani" kwa sababu ziliandikwa kipindi Paulo akiwa katika vifungo.Kila barua hizi ina kumbukumbu ya hali hii (Waefeso 3:1; 4:1; 6:20; Wafilipi 1:7, 13; Wakolosai 4:10, 18; Philimoni 1, 9, 10).

Ukweli wa kwamba nyaraka hizi ziliandikwa wakati Paulo akiwa katika kifungo cha Warumi au minyororo ya jeshi la Rumi katika nyumba yake binafsi (Matendo 28:30), ni wazi kabisa kwamba Mungu hutumia mateso ya wazazi wetu na kuyatumia katika utukufu wake na kuongeza nafasi katika huduma (Wafilipi 1:12-13). Inaonyesha ni kwa jinsi gani tunaweza kufungwa, kuteswa au hata kuzuiliwa, lakini Neno la Mungu linaendelea (2 Timotheo 2:9).

**<u>Nyaraka za Kichungaji</u>**
Nyaraka zingine ambazo ni kubwa zinaitwa ni "Nyaraka za Wachungaji." Neno hili limetumika katika kuonyesha barua tatu zilizoandikwa kwa Timotheo na Tito (1 na 2 Timotheo, na Tito). Mwanzoni kabisa kama barua za watu na Philini ndiye aliyezipanga lakini kwa sababu ya ujumbe wake mkubwa kwa maisha ya kanisa zilianza kuitwa kuwa ni "Nyaraka za Kichungaji." zilizoandikiwa watu, vitabu hivi vimeandikwa kwa watu na kwa mawasiliano binafsi lakini habari ni za kiofisi na zina sifa. Paulo aliziandika kwa Timotheo na Tito ili awaelekeze katika maswala ya kuwa makini katika uchungaji wa kanisa ambalo ni chombo cha Bwana (1 Timotheo 3:14-15; 4:6-15 linganisha na 2 Timotheo 2:2).

Nyaraka hizi zinahusika na utawala wa kanisa, Sera, kutenda kwake na mambo yote yanayohusiana na afya ya kichungaji. Kwa ufupi vitabu hivi Mungu alivipangilia kutusaidia katika majukumu yetu ya Kichungaji na katika kuliendeleza na kulielekeza kanisa.

Kwa mtazamo huu kuna mtazamo wa muhimu sana wa kufanya. Nyaraka kumi na tatu za Paulo ni vitabu vya mwisho alivyoviandika. Ni nini cha muhimu sana kuhusiana na hilo; vitabu hivi vinahusika na kanisa, huduma, mfumo, na kwa nini havikuwekwa kwanza? Kama ni wewe au ningekuwa nafanya haya (hasa leo) kwanza ningeanza na uongozi na utawala, muundo na halafu ndiyo ningekuja katika mafundisho.

Hapa kuna maoni ya kufikiri:

Oni la 1: Kwa kweli, muundo na utawala ni muhimu. Kanisa ni mwili wa kiroho na kila muumini ni mshirika kwa kazi maalumu katika mwili huu. Japo la muhimu la kufikiri katika hili ni kutumia theologia inayofaa (mafundisho) na kulielewa neno na zaidi ya yote kutenda kama Kristo. Hii italipa kanisa misingi ya kimaadili na kiroho kwa kila tutakachokitenda na kukitawala. Kwa hiyo japo njia zetu zitabadilika hazipaswi kuleta mchanganyiko katika maadili na maswala ya kiroho ya neno la Mungu.

Kwa mfano, kulisaidia kanisa kwa kutoa ni kushiriki na ni jukumu la mtu lakini kutoa na kukusanya pesa ni lazima kufanyike pasipo kukiukwa kanuni za Biblia. Waumini wanatakiwa kujitolea na siyo kulazimishwa ambako kunaweza kuharibu kanuni ya Mungu (2 Wakor. 9:6-10).

Oni la 2: Mpango unatakiwa uwe katika mafundisho yanayofaa yaliyotokana na neno la Mungu (2 Timotheo 2:15). Kusudi la Mungu la kweli linatenda kazi kwa watu anaolitumia vizuri neno la Mungu (1 Timotheo 3:1-10) ambalo ni muhimu katika kukua kiroho kwa kanisa. Ni muhimu sana kwa afya ya kanisa. Muumini anapotaka kuliendesha kanisa kama desturi au mila fulani mara nyingi kanisa hilo litatenda tofauti na misingi na kanuni za Biblia na halitakuwa na shauku ya kiroho na wala nguvu ya kutenda kama Mungu alivyokusudia.

Vitabu hivi vinahusika na kanisa na si kitu kingine. Kabla Mungu hajalipa kanisa majukumu na maelekezo, alitupa Warumi, 1 na 2 Wakorintho, Wagalatia, Waefeso, Wafilipi, na Wakolosai. Je, ni kwa sababu muundo ndani ya kanisa ni muhimu sana? Hapana kwa sababu muundo na utawala si vitu muhimu lakini ni vitu vinavyofuatia katika kukua kwa kanisa. Ni kwa sababu mafundisho ya kweli na ya kiroho huzaa huduma ambazo ni muhimu sana kulingana na Mungu wetu na humuonyesha roho na Yesu katika huduma hata uinjilisti wa mikutano.

Kila nyaraka ya Paulo zina mambo yanayofanana na kutofautiana, mkazo wa Bwana Yesu, ujumbe wa injili na umoja wa waumini na Kristo. Jedwali zifuatazo zinaonyesha utofauti huu:

| Mkazo juu ya Bwana Yesu | |
|---|---|
| Warumi | Kristo ni Nguvu ya Mungu kwetu |
| 1 Wakorintho | Kristo ni Hekima ya Mungu kwetu |
| 2 Wakorintho | Kristo ni Karaja ya Mungu kwetu |
| Wagalatia | Kristo ni Nguvu na Haki ya Mungu kwetu |
| Waefeso | Kristo ni Utajiri wa Mungu kwetu |
| Wafilipi | Kristo ni Hatima ya Mungu kwetu |
| Wakolosai | Kristo ni Wingi wa Mungu kwetu |
| 1 Wathesalonike | Kristo ni Ahadi ya Mugu kwetu |
| 2 Wathesalonike | Kristo ni Zawadi ya Mungu kwetu |
| 1 Timotheo | Kristo ni Upatanishi wa Mungu kwetu |
| 2 Timotheo | Kristo ni Hukumu ya Mungu kwetu |
| Tito | Kristo ni Wema wa Mungu kwetu |
| Philimoni | Kristo ni Ujasiri wa Mungu kwetu |

| Mkazo wa Ujumbe wa Injili | |
|---|---|
| Warumi | Injili na Ujumbe wake |
| 1 Wakorintho | Injili na Huduma yake |
| 2 Wakorintho | Injili na Watumishi wake |
| Wagalatia | Injili na Viungo vyake |
| Waefeso | Injili na Mbingu yake |
| Wafilipi | Injili na Dunia yake |
| Wakolosai | Injili na Falsafa yake |
| 1 Wathesalonike | Injili na Yajayo ya kanisa |
| 2 Wathesalonike | Injili na Mpinga Kristo |
| 1 Timotheo | Injili na Wachungaji wake |
| 2 Timotheo | Injili na Upinzani wake |
| Tito | Injili na Matumizi yake |
| Philimoni | Injili na Ufunuo wake |

| Mkazo wa Injili juu ya Umoja wa Waaminio | |
|---|---|
| Warumi | Katika Kristo ni Uthibitisho |
| 1 Wakorintho | Katika Kristo ni Utakaso |
| 2 Wakorintho | Katika Kristo ni Faraja |
| Wagalatia | Katika Kristo ni Uhuru |
| Waefeso | Katika Kristo ni Furaha |
| Wafilipi | Katika Kristo ni Shangwe |
| Wakolosai | Katika Kristo ni Kamili |
| 1 Wathesalonike | Katika Kristo ni Tafasiri |
| 2 Wathesalonike | Katika Kristo ni Sawa |
| 1 Timotheo | Katika Kristo ni Faida |
| 2 Timotheo | Katika Kristo ni Kuburudika |
| Tito | Katika Yesu ni Imara |
| Philimoni | Katika Kristo ni Raha |

# Warumi

## (Kristo: Nguvu ya Mungu kwetu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama barua zielezavyo, Paul ndiye mtunzi (1:1). Bila matatizo yoyote yale kutoka katika kanisa la kwanza waraka huu ulihusishwa na Paulo. Barua ni historia inayokubaliana na maisha ya Paulo. Mafundisho yaliyomo katika kitabu yanahusisha na mitume wengine.

Warumi linaitwa ni kazi kubwa ya Paulo kwa ukweli kwamba iliandikwa kwa ajili ya kanisa lililokuwa Rumi (1:7, 15). Paulo hakuanzisha kanisa Rumi lakini kama mtume kwa watakatifu alikuwa hajawatembelea kwa muda mrefu (15:22-23), kwa hiyo, akawaandikia ili kuwatia moyo katika imani yao na waendelee kuihubiri injili (1:13-15).

Akitamani kutumika Rumi aliamua kuwaandikia kabla ya kuwatembelea huko (15:14-17). Aliiandika kutoka Korintho baada ya makusanyo kwa ajili ya maskini waliokuwa Palestina. Kuanzia pale alienda Yerusalemu kuchukua Pesa ili aende Rumi (15:24). Paulo alikwenda Rumi akiwa kama mfungwa. Inaonekana kwamba Phoebe, mwanamke aliyekuwa katika kanisa la Cenchrea karibu na Korintho aliipeleka barua hii (16:1).

**Muda wa Kuandikwa: 57-58 B.K.** Kitabu cha Warumi kiliandikwa kati ya miaka ya 57-58 B.K. mwishoni mwa safari yake ya tatu ya kimisionari (Matendo 18:23–21:14; Warumi 15:19). Kwa mtazamo wa malezo ya Paulo kwa Warumi 15:26, alikuwa amepokea mchango kutoka makanisa ya Makedonia na Akaya (ilipokuwa Korintho). Hii inamaana ya kwamba alikuwa ameshafika Korintho, lakini alikuwa hajarudi Korintho kipindi anaadika barua hii kwa kanisa (linganisha 1 Wakorintho 16:1-4; 2 Wakorintho 8-9), uandishi wa Warumi ni lazima ufuate mlolongo wa 1 na 2 Wakorintho.

**Nia na Makusudi:** Warumi iliandikwa kueleza matatizo fulani, na hii ilikuwa ni nia ya nyaraka nyingine pia. Mambo matatu tunayaona katika waraka huu. **Kwanza** ilikuwa ikiwajulisha kuwatembelea kwa Paulo baada ya kurudi kwake kutoka Rumi ili kanisa lijiandae kwa ajili ya kufika kwake (15:24, 28-29 linganisha na Matendo 19:21). Paulo alitaka awajulishe nia yake na si hivyo tu, bali hata waanze kuomba kwa ajili ya wito wao (15:30-32). Jambo la **pili** alitaka awajulishe ujumbe na injili aliyokuwa amepewa na Mungu apate kuhubiri na kutangaza. Mtume hakusomwa tu kwamba ***"kuihubiri injili kwa Warumi tu"*** (1:15), lakini litaka wamwelewe msimamo wake katika maisha yake: ikiwemo yaliyopita (uthibitisho ikimaanisha kuitangaza haki), yaliyopo (Inamaana ya utakaso), na yajayo (utukufu ina amana ya kushiriki utukufu wa Mungu). **Tatu** ilikuwa ni kuhusiana na maswali yaliyo kuwa yakiinuka kutoka kwa Wayahudi na watakatifu wa Rumi juu ya injili, kuhusiana na sheria na kutahiriwa. Je, Mungu alikuwa amewatenga Wayahudi, Je Mungu alikuwa ameshasahau ahadi zake kwa Wayahudi? Paulo alijibu maswali haya na akaeleza mpango wa Mungu wa wokovu kwa Wayahudi na watakatifu.

Nia ya Paulo katika Rumi imeelezwa katika 1:16-17. Hapa mtume anaeleza jinsi Mungu anavyowaokoa wenye dhambi. Katika mistari hii nia na makusudi ya waraka huu yanaonekana hapa: Injili, nguvu ya Mungu, wokovu, kila aaminiye, haki kutoka kwa Mungu, Wayahudi na watakatifu. Charles Ryrie anaeleza:

> zaidi ya waraka huu wa Paulo, Warumi walikuwa na uimara wa imani ipasavyo. Nia ya waraka huu ni haki ya Mungu (1:16-17). Mafundisho mengi ya kikristo yameelezwa: kiasili ufunuo (Warumi 1:19-20), dhambi (Warumi 3:9-20), uthibitsho (Warumi 3:24), Kufaa (Warumi 3:25), Imani (Warumi 4:1), dhambi ya asili (Warumi 5:12), Umoja na Kristo (Warumi 6:5), Kuteuliwa na kuchaguliwa kwa waisraeli (Warumi 9-11), karama za Roho (Warumi 12:3-8), na heshima ya serikali (Warumi 13:1-7).[73]

Kutoka katika utangulizi (1:1-17) na maneno ya mwisho (15:14–16:27), Warumi imegawanyika katika sehemu kuu tatu:

1. Sura nane za kwanza ni mafundisho na zinachanganua mafundisho muhimu ya injili ya haki (Uthibitisho na utakaso) kutoka kwa Mungu kwa njia ya Imani.
2. Sura tatu zinazofuatiana (9-11) zinahusika na wayahudi pamoja na watakatifu na mahusiano yake kwa kila injili.
3. Sura zinazobaki (12-16) zinatoa matumizi ya vitendo ya injili kwa waaminio katika maisha yao ya kila siku.

**Mwonekano wa Yesu katika Warumi:** Paulo anamuonyesha Yesu kama Adamu wa pili ambaye haki yake na kifo chake vimetoa uthibitisho kwa wale wote wanaomwamini. Hutoa haki yake kama zawadi kwa watu wenye dhambi waliokuwa wanahitaji hukumu ya Mungu na ghadhabu ya Mungu kwa ajili ya dhambi zao. Kifo na kufufuka kwake ni msingi wa wokovu wa anayeamini, kuthibitika, wokovu, na utukufu.[74]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi (1:1-17)**
   1:1-7 | 1:8-15 | 1:16-17

2. **Hukumu: Hitaji la Haki kwa Sababu ya Dhambi kwa Watu Wote (1:18–3:20)**
   a. Hukumu ya Mtu Mzinzi (Mmataifa) (1:18-32)
      1:18-23 | 1:24-27 | 1:28-32
   b. Hukumu ya Mtu wa Mungu (2:1-16)
      2:1-11 | 2:12-16
   c. Hukumu ya Mtu wa Dini ( Myahudi) (2:17–3:8)
      2:17-24 | 2:25-29 | 3:1-8
   d. Hukumu ya Watu Wote (3:9-20)
      3:9-18 | 3:19-20

3. **Kuthibitishwa: Haki ya Mungu kwa Njia ya Kristo (3:21–5:21)**
   a. Maelezo ya Haki (3:21-31)
      3:21-26 | 3:27-31

b. Picha ya Haki (4:1-25)

| | |
|---|---|
| 4:1-8 | 4:13-15 |
| 4:9-12 | 4:16-25 |

c. Baraka za Haki (5:1-11)

d. Mwonekano wa Haki na Hukumu (5:12-21)

| | | |
|---|---|---|
| 5:12-14 | 5:15-17 | 5:18-21 |

**4. Utakaso: haki Yawekwa na kuelezwa (6:1–8:39)**

a. Kutakaswa na Dhambi (6:1-23)

| | | |
|---|---|---|
| 6:1-7 | 6:12-14 | 6:20-23 |
| 6:8-11 | 6:15-19 | |

b. Utakaso na Sheria (7:1-25)

| | | |
|---|---|---|
| 7:1-3 | 7:7-13 | 7:21-25 |
| 7:4-6 | 7:14-20 | |

c. Takaso na Roho Mtakatifu (8:1-39)

| | | |
|---|---|---|
| 8:1-8 | 8:18-25 | 8:28-30 |
| 8:9-17 | 8:26-27 | 8:31-39 |

**5. Uhalalishaji: Myahudi na Mmataifa, Mtazamo wa Mungu (9:1–11:36)**

a. Isareli Iliyopita : Uteuzi wa Mungu (9:1-29)

| | | |
|---|---|---|
| 9:1-5 | 9:14-18 | 9:27-29 |
| 9:6-13 | 9:19-26 | |

b. Israeli Iliyopo: Kukataliwa na Mungu (9:30–10:21)

| | | |
|---|---|---|
| 9:30-33 | 10:5-13 | 10:16-17 |
| 10:1-4 | 10:14-15 | 10:18-21 |

c. Israeli Ijayo: Kurejeshwa na Mungu (11:1-36)

| | | |
|---|---|---|
| 11:1-6 | 11:11-16 | 11:25-32 |
| 11:7-10 | 11:17-24 | 11:33-36 |

**6. Matumizi: Utendaji wa Waliohaki katika Huduma (12:1–15:13)**

a. Katika Mahusiano na Mungu (12:1-2)

b. Katika Mahusiano Binafsi (12:3)

c. Katika Mahusiano na Kanisa (12:4-8)

d. Katika Mahusiano na Jamii (12:9-21)

| | |
|---|---|
| 12:9-13 | 12:14-21 |

e. Katika Mahusiano na Serikali (13:1-14)

| | | |
|---|---|---|
| 13:1-7 | 13:8-10 | 13:11-14 |

f. Katika Mahusiano na Wakristo Wengine (14:1–15:13)

| | | |
|---|---|---|
| 14:1-4 | 14:10-12 | 15:1-6 |
| 14:5-9 | 14:13-23 | 15:7-13 |

**7. Ujumbe Binafsi na Rehe (15:14–16:27)**

a. Mpngo wa Paulo (15:14-33)

| | | |
|---|---|---|
| 15:14-21 | 15:22-29 | 15:30-33 |

b. Salamu Binafsi za Paulo (16:1-16)

| | |
|---|---|
| 16:1-2 | 16:3-16 |

c. Hitimisho la Paulo na Rehema (16:17-27)

| | | |
|---|---|---|
| 16:17-20 | 16:21-24 | 16:25-27 |

# Wakorintho wa Kwanza

## (Kristo: Hekima ya Mungu Kwetu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Paulo ndiye mtunzi. Hii inakuwa katika maswala ya nje na ya ndani. Tangu karne ya kwanza na kuendelea (96 B.K.), kuna ushahidi mkubwa na unaoendelea kwamba Paulo ndiye mtunzi. Clement wa Rumi (Mchungaji wa karne ya Pili) ameandika 1 Wakorintho "Waraka wa mtume Paulo mbarikiwa," kwa waraka wake kwa Wakorintho na hata ameweka 1 Wakorintho kwa mtazamo wa kazi zinazoendelea. Ushahidi wa ndani uko wazi. Mwandishi amejitaja mwenyewe mara nyingi (1:1; 16:21 linganisha na 1:12-17; 3:4, 6, 22).

Usomaji wa makini wa kitabu cha Matendo na hata nyaraka mbalimbali unaonyesha muhtasari wa Paulo alivyojihusisha na kanisa: (1) Kulikuwa na safari yake ya kwanza iliyofuatiwa na, (2) barua ya kwanza kwa wakorintho (iliyopotea). Halafu hii ilifuatiwa na (3) barua ya pili kwa Wakorintho (1 Wakorintho). (4) na baadaye

ilifuatiwa na kuwatembelea Wakorintho yeye mwenyewe ("Safari ya maumivu," 2 Wakorintho 2:1), (5) halafu kulikuwa na barua ya tatu kwa Wakorintho (nayo ilipotea), (6) na baadayeilifuatiwa na 2 Wakorintho, barua ya nne kwa Wakorintho, (7) mwisho kulikuwa na safari ya tu kwa Wakoritho (Matendo 20:2-3). Ieleweke kwamba barua mbili zilizopotea ni kwa sababu hazikuwa zimekusudiwa na Mungu kuwa sehemu ya maandiko.

**Muda wa Kuandikwa: 55 B.K.** Paulo alihubiri kwa mara ya kwanza Korintho alipokuwa safarini mnamo 50 B.K. alipouwa huko alitumika na kuishi na Akila na Priska waliokuwa wakifanya biashara moja, ya kuuza mahema (Matendo 18:3). Kwa kuwa ilikuwa ni desturi ya Paulo, alihubiri katika Sinagogi kwa mara ya kwanza lakini alifanyiwa upinzani na wayahudi. Hata hivyo, aliondoka tena kuelekea mlango mwingine katika nyumba ya Tito ambapo aliendelea na huduma yake (Matendo 18:7). Japo alikataliwa na wayahudi mbele ya gavana wa Kirumi Galli,o Paulo alikaa miezi 18 huko Korintho (Matendo 18:1-17; 1 Wakorintho 2:3). Barua hii iliandikwa miaka ya 55 B.K. ikieleza mwisho wa miaka mitatu ya kukaa kwa Paulo huko Efeso (16:5-9; Matendo 20:31). Kulingana na kumbukumbu zake ni kwamba alikaa Efeso hadi kipindi cha Pentecoste (16:8), Inaonesha alitaka kukaa huko nusu mwaka alipokuwa akiandika waraka huu.

**Nia na Makusudi:** Ili kuelewa nia na makusudi ni vizuri tukaelewa historia fupi. Korintho ulikuwa ni mji mkubwa (kiasi cha watu 700,000; kama theluthi mbili ya wale waliokuwa watumwa) ilikuwa pembeni mwa isthmus (sehemu ya ardhi iliyoingia katika maji) kati ya bahari ya Aegean na bahari ya Adriatic inayounganisha Peloponnesus na Northern Greece. Paulo na wenzake walikuwa wameshangazwa na mafanikio ya Injili ya haki ya Mungu ilivyokuwa imeenea Korintho. Kama mji ilikuwa na vitu vingi na mji wa anasa. Mji ulikuwa na madini na mahekalu yaliyokuwa ni mazuri hasa kwa hekalu la Aphrodite lililokuwa juu futi 1800- (550 mita) kilele kiliitwa Acrocorinthus. Katika maandishi ya kiyunani ilikuwa ni nchi ya utajiri sana. Neno "Msichana wa Kikoritnho" lilimaanisha ni Malaya. Neno "kutenda kama mkorintho" ilimaanisha kufanya anasa. Utajiri na vitu vya Korintho viliwekwa kuzunguka hekalu la Aphrodite na hata malaya wake. Kwa maana hii kukawa na methali iliyosema na kutahadharisha, "Si kila mtu ni msafiri wa Korintho."

Kulingana na Matendo, Paulo alikuwa na waongofu kutoka kwa wayahudi na hawa walikuwa ni watakatifu. Wengi wao walitoka katika maeneo ya kuheshimiwa japo wengine walikuwa katika nafasi mbaya (1:26-31). Hali ya kiuchumi ilikuwa nzuri kwao (7:20-24; 11:21-34); na wengine wao walitoka katika upagani (6:9-11). Kwa kuwa wengine walikuwa ni wayunani walijivuna (1:17; 2:1-5).[75]

Waweza kuona ni kwa jinsi gani anasa ilivyokuwa imeliharibu kanisa la Korintho kiroho na hata kimaadili. Nia ya waraka huu ni maisha mapya ya kikristo na watakatifu walioitwa na utakaso wa kila namna ya maisha. Maisha haya mapya katika Kristo yanaitwa kwa njia mpya ya Roho Mtakatifu (3:16, 17; 6:11, 19-20). Hekima ya Mungu imedhihirishwa ili itubadili katika sehemu zote za, kibinafsi na hata kijamii.

Kwa hiyo, 1 Wakorintho iliandikwa kama ya kichungaji ili kurekebisha matatizo na fujo zilizokuwa katika kanisa (1:11), kumtumaini mwanadamu au ulimwengu zaidi ya Mungu (1:21-30), uasherati (5:1-13; 6:9-20), na maswali kuhusiana na talaka na ndoa, chakula, Ibada, karama za roho, na hata ufufuko. Kwa sababu ya mashaka yao ya dini na uasi waliokuwa wakifanya, mafundisho ya uongo na imani potofu zilitawala kanisa.

**Mwonekano wa Yesu katika 1 Wakorintho:** Umuhimuu wa Yesu ni uungu wake, mambo yake na maana ya maisha ya ukristo, imeelezwa katika 1:30, ***"Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu na haki na utakatifu na ukombozi."***

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi (1:1-9)**
   a. Salamu (1:1-3)
   b. Maombi ya Shukrani (1:4-9)

2. **Migawanyiko katika Kanisa (1:10–4:21)**
   a. Taarifa ya Migawanyiko (1:10-17)
   b. Sababu za Kugawanyika (1:18–2:16)
      1:18-25 2:1-5
      1:26-31 2:6-16
   c. Matokeo ya Mganwanyiko (3:1–4:5)
      3:1-4 3:10-15 3:18-23
      3:5-9 3:16-17 4:1-5
   d. Mfumo na Mfano wa Paulo (4:6-21)
      4:6-7 4:8-13 4:14-21

**3. Uharibifu wa Maadili katika Kanisa (5:1–6:20)**

a. Tatizo la Kujamiiana Ndudu kwa Ndugu (5:1-13)

5:1-5 5:6-8 5:9-13

b. Magomvi (6:1-8)

c. Maonyo juu ya Kutojali Maadili (6:9-20)

6:9-11 6:12-20

**4. Maelekezo Kuhusu Ndoa (7:1-40)**

a. Ndoa (7:1-9)

b. Ndoa na Talaka (7:10-24)

7:10-11 7:17-20

7:12-16 7:21-24

c. Ndoa na Huduma za Kikristo (7:25-38)

7:25-31 7:32-35 7:36-38

d. Kuoa na Kuolewa Tena (7:39-40)

**5. Maelekezo Kuhusu Yakula Itolewayo kwa Mizimu (8:1–11:1)**

a. Swali: Je Mkristo Awezakuchangia Chakula cha Iungu ya Wapagani? (8:1-13)

8:1-3 8:4-6 8:7-13

b. Mfano wa Paulo (9:1-27)

9:1-2 9:8-14 9:19-23

9:3-7 9:15-18 9:24-27

c. Mashauri/Kusihi (10:1–11:1)

10:1-5 10:14-22 10:31-33

10:6-13 10:23-30 11:1

**6. Maelekezo Kuhusu Ibaada za Nje (11:2–14:40)**

a. Wanawake Kufunika Vichwa (11:2-16)

b. Meza ya Bwana (11:17-34)

11:17-22 11:27-32

11:23-26 11:33-34

c. Matumizi ya Karama za Kiroho (12:1–14:40)

12:1-3 13:1-3 14:13-19

12:4-11 13:4-7 14:20-25

12:12-13 13:8-13 14:26-33

12:14-26 14:1-5 14:34-36

12:27-31 14:6-12 14:37-40

**7. Mafundisho ya Ufufuko (15:1-58)**

a. Umuhimu wa Ufufuko (15:1-11)

15:1-2 15:3-11

b. Matokeo ya Kuukana Ufufuko (15:12-19)

c. Tumaini la Wakristo (15:20-34)

15:20-28 15:29-34

d. Mwili Uliofufuka (15:35-50)

15:35-41 15:42-49

e. Ushindi wa Mkristo Kupitia Kristo (15:51-58)

15:51-57 15:58

**8. Kukusanywa kwa Yerusalemu (16:1-4)**

**9. Hitimisho (16:5-24)**

16:5-9 16:13-14 16:21-24

16:10-12 16:15-20

# Wakorintho wa Pili

## (Kristo: Faraja ya Mungu Kwetu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama ilivyoanza katika salamu, Paulo ndiye mwandishi wa kitabu hiki. Kuna ushahidi wa ndani na nje unaothibitisha kwa nguvu kabisa. Kwa kweli “una namna yake tu katika kuandikwa kwa sababu ya historia iliyomo katika kitabu hiki inakifanya kiwe ni tofauti na vingine.”[76]

**Muda wa Kuandikwa: 56 B.K.** Kwa sababu ya fujo zilizosababishwa na Demetrio (Matendo 19:23-41). Paulo aliondoka Efeso na kwenda Makednia (Matendo 20:1) wakati wa mvua miaka ya 56 B.K. Akiwa katika safari yake alisimama Troa akitumaini aonane na Tito (2 Wakorintho 2:13) ili apate habari za hali ya Korintho. Alipomkosa aliendelea Makedonia akiwa na hakika ya kwamba Tito ni mzima (7:5-6). Alikutana na Tito aliyeleta habari njema za kanisa la Korintho, lakini wakati huo huo alimpa habari mbaya za kundi lililokuwa likimpinga Paulo na utume wake. Akiwa Makedonia, Paulo aliandika barua nyingine ya nne, 2 Wakorintho. Paulo alirudi tena Korintho kipindi cha baridi 56-57 B.K. (Matendo 20:2-3).

**Nia na Makusudi:** Barua ya Paulo ya 2 Wakorintho, ni barua ya kibinafsi na inaonyesha undani wake. Katika barua hii anafungua moyo wake na anasema ujasiri wake wa upendo kwa Wakorintho; anawataka wale ambao alikuwa akipingana nao. Kusudi na nia limeelezwa vizuri na James K. Lowery:

> Alichohusika nacho Paulo ni kuwepo kwa walimu wa uongo waliokuwa wameingia kanisani. Alieneza mawazo yao na wakati huo huo waliharibu utu na ujumbe wa Paulo. 2 Wakorintho iliandikwa ili kulinda maana ya ujumbe na hata Paulo kujihami. Hii hakufanya kwa yeye binafsi, ila kukubalika kwa huduma na ujumbe wake uliokuwa unaendelea sana katika maisha binafsi ya kanisa.[77]

Katika kujihami kwake mambo matatu aliyaandika: (1) Paulo alionyesha furaha yake katika kanisa kulingana na kanisa lilivyoipokea huduma yake (1:1–7:16); (2) Alikuwa akifikiri kuwakumbusha Wakristo kujitoa kwao kwa ajili ya Wakristo waliokuwa Yudea (8:1–9:15); na (3) alikuwa akilinda mamlaka yake ya Kitume (10:1–13:14).

**Mwonekano wa Yesu katika 2 Wakorintho:** Katika nyaraka tunamwona Yesu kama Mfariji (1:5), Mshindi (2:14), Mkombozi (3:17), Bwana (4:5), Nuru (4:6), Hukumu (5:10), Uthibitisho (5:19), Zawadi (9:15), Mmiliki (10:7), na Nguvu (12:9).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza[78]

1. **Maelezo ya Palo Kuhusu Huduma Yake ya Kitume (1:1–7:16)**
   a. Salamu (1:1-2)
   b. Shukurani kwa Ajili ya Faraja ya Mungu Kipindi cha Mateso (1:3-11)
      1:3-7 1:8-11
   c. Umakini wa Paulo katika Tendaji (1:12–2:4)
      1:12-14 1:23-24
      1:15-22 2:1-4
   d. Kuwasamehe Waliokuwa Wakimpinga Hko Korintho (2:5-11)
   e. Mwongozo wa Mungu katika Huduma (2:12-17)
      2:12-13 2:14-17
   f. Wamini wa Korintho- Barua Kutoka kwa Kristo (3:1-11)
      3:1-3 3:4-11
   g. Kuona Utukufu wa Mungu (3:12–4:6)
      3:12-18 4:1-6
   h. Hazina katika Barasiza Udongo (4:7-15)
      4:7-12 4:13-15
   i. Umaana wa Kifo kwa Wakristo (4:16–5:10)
      4:16-18 5:1-5 5:6-10
   j. Huduma ya Upatanisho (5:11–6:10)
      5:11-15 5:20-21
      5:16-19 6:1-10
   k. Hurma ya Mngu kwa Watoto Wake (6:11–7:4)
      6:11-13 7:1
      6:14-18 7:2-4
   l. Ukutana na Tito (7:5-16)
      7:5-12 7:13-16

2. **Mabishano (Kutokuelewana). Kusanyiko kwa Ajili ya Wakristo katika Yerusalemu (8:1–9:15)**
   a. Wenye Moyo Watiwa Moyo (8:1-15)
      8:1-6 8:7-15
   b. Tito na Wenzake Watumwa Kwenda Korintho (8:16–9:5)
      8:16-24 9:1-5
   c. Matokeo ya Kutoa kwa Moyo (9:6-15)

3. **Kuhalalisha Mamlaka ya Huduma Yake ya Kitume (10:1–13:14)**
   a. Kujihami kwa Paulo Kulingana na Ujumbe Wake wa Kitume Aliokuwa Nao na Mamlaka (10:1-18)
      10:1-6 10:7-11 10:12-18
   b. Paulo Adhalauliwa (11:1–12:21)
      11:1-6 11:21-29 12:11-13
      11:7-11 11:30-33 12:14-18
      11:12-15 12:1-6 12:19-21
      11:16-20 12:7-10
   c. Maonyo ya Mwisho (13:1-10)
      13:1-4 13:5-10
   d. Hitimisho (13:11-14)

# Wagalatia

## (Kristo: Haki ya Mungu Kwetu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Paulo anaonekana kuwa mwandishi wa waraka huu kwa ushahidi wa neno aliloanza nalo la "Paulo mtume."

**Muda wa Kuandikwa: 49 B.K.** Barua iliandikwa kwa ajili wa Wakristo waliokuwa Galatai ya kusini. Makanisa haya yalianzishwa na Paulo kipindi cha safari yake ya kimisionari. Barua hii iliandikwa mwishoni mwa safari yake (nafikiri kutoka Antiokia kati ya 49 B.K, na akaifanya kuwa barua ya haraka kabisa ya Paulo) ya kwenda katika baraza Yerusalemu (Matendo 15).

**Nia na Makusudi:** Waraka huu umekuwa ukiitwa na wasomi wengi kuwa ni "Msingi wa Ukombozi wa Wakristo." Wagalatia wanakuwa ni changamoto kwa Judaizers na mafundisho yao ya sheria (kuishi chini ya sheria badala ya Neema). Walifundisha, kati ya vitu vyao, vitu vingi vilivyotendeka Agano la Kale vililifunga kanisa lao kabisa. Kwa hiyo, mtume anaandika kuwakatalia injili yao ya uongo ya kazi na kueleza ubora na uthibitisho wa imani na utakatifu wa njia ya Roho Mtakatifu.

Kwa nyongeza, hizi Judaizers hazikuhubiri injili ya uongo tu, lakini hata zilipinga utume wa Paulo. Katika sura mbili za mwanzo Paulo anajitetea juu ya ujumbe wake na utume wake, kwamba umekuja kwa ufunuo wa Kristo aliyefufuka. Halafu katika sura ya 3 na ya 4 anaeleza kwa kubishana na mafundisho ya kweli kuhusu neema, mafundisho ya hakika ya Imani. Anaeleza kwamba mafundisho kama hayo yanaweza kusababisha dhambi, kwa hiyo mitume anafafanua ukombozi wa ukristo kwamba siyo leseni ya dhambi. Kwa hiyo Sura ya 5 na 6 inaonesha kwamba ukristo ni lazima uishi kwa nguvu ya Roho Mtakatifu na kwamba Roho ataongoza kutembea na ataonyesha si kazi za mwili bali ni zaidi ya matunda ya Roho.

**Mwonekano wa Yesu katika Wagalatia:** Kwa njia ya kifo chake ambacho Wakristo wamekufa kwa sheria na amefufuka kwa njia ya Kristo (2:20), Wakristo wako huru na siyo katika vifungo (5:1f.) na wako katika ukombozi. Nguvu ya msalaba huleta kukombolewa na laana ya sheria, dhambi na hata ubinafsi (1:4; 2:20; 3:13; 4:5; 5:16, 24; 6:14).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Binafsi: Injili ya Neema, Kuthibitishwa kwa Imani Kwali Kwalindwa (1:1–2:21)**
   a. Utanglizi (1:1-10)
      1:1-2 1:3-5 1:6-10
   b. Injili ya Neema Ilikuja kwa Ufunuo (1:11-24)
      1:11-12 1:13-17 1:18-24
   c. Injili ya Neema Ilithibitishwa na Kanisa huku Yerusalemu (2:1-10)
   d. Injlili ya Neema Ilihalalishwa katika Kkemewa kwa Petro (2:11-21)
      2:11-14 2:15-21

2. **Mafundisho: Injili ya Neema, Kuthibitishwa kwa Imani Kwaelezwa (3:1–4:31)**
   a. Ahamu wa Wagalatia: Roho Hutolewa kwa Imani (3:1-5)
   b. Mfano wa Abrahamu, Alithibitishwa kwa Lamni na Si kwa Ajli ya Kazi (3:6-9)
   c. Tumethibitishwa kwa Imani, Siyo kwa Njia ya Sheria (3:10–4:11)
      3:10-14 3:19-22 4:1-7
      3:15-18 3:23-29 4:8-11
   d. Wagalatia Walipokea Baraka Zao kwa Imani na Sikwa Ajili ya Sheria (4:12-20)
   e. Sheria na Neema ni Vit Viwili Tofauti (4:21-31)

3. **Kiutendaji: Injili ya Neema, Kuthibitishwa kwa Imani Kwaoneshwa (5:1–6:18)**
   a. Sehemu ya Uhuru, Simama Imara (5:1-12)
      5:1 5:2-6 5:7-12
   b. Utendaji wa Huru. Tumika na Mpendane (5:13-15)
   c. Nguvu ya Huru, Kkutembea kwa Roho (5:16-26)
      5:16-24 5:25-26
   d. Utendaji wa Kiuhuru. Fanya Mema kwa Watu Wote (6:1-10)
      6:1-5 6:6-10
   e. Hitimisho (6:11-18)

# Waefeso

## (Kristo: Utajiri wa Mungu Kwetu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama ilivyoanza katika mstari wa kuanzia katika waraka wa gerezani, Paulo ndiye anayeonekana kuwa ni mwandishi, kichwa chake kinaanza "Kwa Waefeso"

**Muda wa Kuandikwa: 60-61 B.K.** Paulo alikuwa ni mfungwa alipokuwa anaandika barua hii (Waefeso 3:1; 4:1; 6:20). Japo wasomi wengi anasema aliandika barua hii akiwa kifungoni Kaisaria (Matendo 24:27) miaka ya 57-59 B.K, au Rumi (28:30) miaka ya 60-62 B.K, inayoonyesha kuwa alikuwa kifungoni Rumi. Inaaminika kwamba Wafilipi, Wakolosai na Philimoni ziliandikwa pia kwa wakati mmoja (Wafilipi 1:7; Wakolosai 4:10; Philimoni 9). Kwa kuwa Waefeso haituoneshi kuachiliwa kwa Paulo kama ilivyo katika Wafilipi (1:19-26) na Philimoni (1:22), wengi wanasadiki kwamba Waefeso iliandikwa mapema kabisa kabla ya kufungwa kwake huko Rumi miaka ya 60 B.K, alipokuwa akihifadhiwa na kulindwa katika nyumba aliyokuwa amekodiwa (Matendo 28:30).,na baada ya Paulo kuachiliwa aliandika 1 Timotheo na Tito na akakamatwa tena, aliandika, 2 Timotheo, na baadaye alikufa kishujaa katika Rumi.

**Nia na Makusudi:** Katika Waefeso Paulo anaonyesha siri kubwa "kisa ambacho ni mwili wa Kristo" Kristo kama Kichwa cha kanisa (1:22, 23), waumini kama washirika wake na waliobarikiwa kwa kila namna ya Kiroho katika Kristo (1:3; 2:11-22). Kusudi la Paulo ni kupanua mtazamo usiokuwa na kikomo katika utajiri wa baraka zake Kristo ambaye ni kichwa cha kanisa, mwili wa Kristo. Nje ya hii kuna makusudi mawili yaliyo katika waraka huu. Moja ni kueleza utajiri wa baraka waliokuwa nao Waumini katika Kristo, na kwa namna gani, kwa kupitia wao, na kusudi la ndani la Mungu limeonyeshwa kwa njia ya Mtu aitwaye Kristo, vitu vya mbinguni na duniani (1:3-12). Kusudi la pili ni kujua kuwa waumini jukumu lao, ni kushika,na kutembea katika hali inayolandana na nafasi ya mbinguni na wito wa Kristo (1:18-23; 3:14-21; 4:1).

Kwa kuwa haikuandikwa kukosoa makosa yoyote, Paulo ameandika kama tahadhari ya matatizo ambayo mara nyingi hutokea kwa sababu ya uchanga au kutoelewa na kutotumia kile Wakristo walicho nacho katika Kristo. Na pia imeunganishwa na sehemu ya vita vya Ibilisi kwa Wakristo (6:10-18). Kwa hiyo, Paulo anaandika juu ya maisha ya Kiroho ya waumini, kutembea kwao na hata ustawi wao.

**Mwonekano wa Yesu katika Waefeso:** Neno "Kristo" katika Waefeso linaonekana mara 35. Hii ni namna ya kawaida ya kueleza kwa Paulo; lakini limeonekana humu zaidi ya nyaraka zingine. Kwa hivyo, tunaona mengi waumini waliyonayo kwa njia ya Mwokozi wao. Wako katika Kristo (1:1), wamebarikiwa na baraka zote katika Kristo (1:3), wameteuliwa katika yeye (1:4), wamefananishwa naye (1:5), katika kupendwa (1:6), wamekombolewa katika yeye (1:7), ni warithi katika yeye (1:11), wanatumaini na kusifu utukufu wake katika yeye (1:12), wamepigwa muhuri na Roho Mtakatifu katika yeye (1:13-14), wana uzima, na wanakaa naye mbinguni (2:5-6), wameumbwa na Kristo kwa kazi nzuri (2:10), washiriki wa baraka katika Kristo (3:6), na wana haki mbele za Mungu ya kufanya lolote kwa njia ya imani katika Kristo (3:12).

# Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Salamu (1:1-2)**

2. **Sehemu ya Mafndisho ya Nyaraka. Kuitwa kwa Kanisa (1:3–3:21)**
   a. Sifa za Kukombolewa (1:3-14)
   b. Maombi kwa Ajili ya Funuo wa Hekima (1:15-23)
   c. Maelekezo (2:1-22)
      2:1-10 2:11-22
   d. Maelezo ya Ziada (3:1-13)
   e. Maombi kwa Ajili ya Kutambua (3:14-21)
      3:14-19 3:20-21

3. **Sehemu ya Kiutendaji katika Nyaraka. Mwenendo wa Kanisa (4:1–6:24)**
   a. Mwenendo wa Waumini katika Umoja (4:1-16)
      4:1-6 4:7-16
   b. Mwenendo wa Waumini katika Haki (4:17–5:21)
      4:17-24 5:1-2 5:6-14
      4:25-32 5:3-5 5:15-21
   c. Mwenedo wa Mkristo katika Ulimwengu (5:22–6:9)
      5:22-24 6:1-8
      5:25-33 6:9
   d. Mwenendo wa Mkristo katika Vita (6:10-20)
      6:10-17 6:18-20
   e. Hitimisho (6:21-24)

# Wafilipi

## (Kristo: Hatima ya Mungu Kwetu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Paulo ndiye mwandishi. Waraka hu uliandikwa kwa ajili kanisa la Filipi, kanisa la kwanza alilolianzasha Paulo huko Makedonia, na nasema, "Kwa Wafilipi ."

**Muda wa Kuandikwa: 60-61 B.K.** Kama kwa waefeso, waraka huu uliandikwa kipindi Paulo akiwa gerezani. Kumbukumbu ya walinzi wake Praetorian (Wafilipi 1:13) akiambatanisha na hali ya uwezekano wa Kifo (1:20-26) na alikuwa akiuandika kutoka Rumi. Japo kifo kilikuwa kiko karibu, lakini Paulo alionekana kuwa jasiri na kuachiliwa kwakwe. Hii inaonyesha kwamba, Wafilipi iliandikwa baada ya Waefeso: baadaye miaka ya 60 au 61 B.K.

**Nia na Makusudi:** Kama Waefeso inavyoonyesha siri ya Utukufu "kanisa ambalo ni mwili wa Kristo" na Kristo kama Kichwa cha kanisa (1:22-23), na washiriki kama kiungo, waliobarikiwa na kila baraka za kiroho kuwa katika Kristo (1:3; 2:11-22), Wafilipi inatumia kitabu cha Waefeso. Wafilipi inalinda umoja na kuwahimiza waumini kufurahi katika nafasi yao na baraka walionavyo katika Kristo. (Wafilipi 1:27; 2:2; 4:1f.). Kusudi la Wafilipi ni "Furaha na umoja katika Kristo."

Paulo alikuwa na kila sababu ya kuandika kwake barua hii kwa Wafilipi: (1) Aliwashukuru na kueleza upendo wake kwa zawadi walizokuwa wamempelekea (1:5; 4:10-19); (2) na kuwataarifu kwa yale yaliyokuwa yakimpata (1:12-26; 4:10-19); (3) na kuwatia moyo Wafilipi wasimame imara wakati wa mateso na wafurahi yanapowapata (1:27-30; 4:4); (4) kuwahimiza wakae katika umoja (2:1-11; 4:2-5); (5) kumthibitisha kwao Timotheo na Epaphradito kwa ajili ya kanisa la Filipi (2:19-30); na (6) na kuwatahadharisha Wafilipi na mambo ya watu wa mataifa ambao walikuwa kati yao (sura ya 3).

**Mwonekano wa Kristo katika Wafilipi:** Hakuna aya katika maandiko inayoeleza kwa uwazi asili, ukweli na hata kusudi la mwili wa Kristo kama Wafilipi (2:5-8). Kwa mtazamo wa jinsi Yesu alivyokuwa na alivyo, aliyoyafanya, na atakayo yakamilisha, Paulo anamweleza Kristo kama maisha ya (1) waumini (1:21); (2) mwanadamu kamili na dhabihu ya upendo (2:4-5); (3) atakayebadilisha miili yetu iwe kama ya utukufu wake katika ufufuko (3:21); na (4) kuimarika kwetu katika mambo yote ya maisha (4:12).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza[79]

1. **Salamu na Shukrani kwa Wafilipi (1:1-11)**
   1:1-2 1:3-11

2. **Mambo Binafsi ya Paulo katika Rumi: Kumuhubiri Kristo (1:12-30)**
   1:12-18 1:21-26
   1:19-20 1:27-30

3. **Mfamo wa Maisha ya Kikristo: Kuwa na Akili ya Kristo (2:1-30)**
   2:1-4 2:12-13 2:19-30
   2:5-11 2:14-18

4. **Thawabu ya Maisha ya Kikristo: Kuwa na Ufahamu wa Kristo (3:1-21)**
   3:1 3:7-11 3:17-21
   3:2-6 3:12-16

5. **Amani ya maisha ya kikristo: Kufahamu uwepo wa Kristo (4:1-23)**
4:1-3
4:4-7
4:8-9
4:10-14
4:15-20
4:21-23

# Wakolosai

## (Kristo: Wingi wa Mungu Kwetu)

**Jina na Mtunzi la Kitabu:** Kwa sababu ya salamu za Paulo katika 1:2, Wakolosai iliandikwa "Kwa Wakolosai."

**Muda wa Kuandikwa: 60-61 B.K.** Paulo aliandika nyaraka nne zote kipindi cha kufungwa kwake kwa mara ya kwanza huko Rumi. Hii ina maana ya kwamba aliandika 60-61 B.K. (Rejea katika Waefeso na Wafilipi).

**Nia na Makusudi:** Kusudi ni nguvu ya matunda ya ujumbe wa injili unaotangaza nguvu, uongozi, na jumla ukamilifu wa Kristo katika kanisa ambalo ni mwili wake. Katika waraka huu tunaona "picha kamili ya Kristo."[80] Wakolosai inaeleza kwamba, kwa sababu ya yale Yesu aliyonayo katika utu wake na ameshakamilisha kazi yake, yeye kama Msingi wa Imani ya waumini wote kwa hiyo tunapaswa kumhitaji ili tukamilike (2:10). Kwa upeo, Wakolosai inaonyesha ufansisi, ukamilifu na hata utu wake kamili na kazi yake Kristo kama Mungu mwanadamu mwokozi, muumbaji na msimamishaji wa ulimwengu huu, na njia kamili ya hitaji la mwanadamu katika umilele na kimahitaji. Na mwisho Kristo kama muumbaji na mwokozi wa wanadamu na ulimwengu wote.

**Mwonekano wa Yesu katika Wakolosai:** Wilkinson na Boa anaeleza:

> Kitabu hiki kimoja kiini chake ni Kristo kama "kichwa wa mamlaka na nguvu zote" (2:10), Bwana wa uumbaji (1:16-17), mwanzilishi wa ukombozi (1:20-22; 2:13-15). Ni msingi wa tumaini la waumini wote (1:5, 23, 27), chanzo cha nguvu ya maisha mapya ya waumini (1:11, 29), mkombozi na mwisho wa waumini (1:14, 20-22; 2:11-15), mwenye mamlaka (1:15, 19; 2:9), Muumbaji wa vitu vyote (1:16-17), Kichwa cha kanisa (1:18), Mungu mwanadamu aliyefufuka (1:18; 3:1), na mwokozi wa yote (1:28; 2:3, 20; 3:1-4).[81]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza[82]

1. **Mafundisho: Ut na Kazi za Kristo (1:1–2:5)**
1:1-2
1:3-8
1:9-12
1:13-14
1:15-20
1:21-23
1:24-29
2:1-5

2. **Mchanganuo: Asi Nanru ya Shirika na Kristo (2:6–3:4)**
2:6-7
2:8-15
2:16-19
2:20-23
3:1-4

3. **Kivitendo: Utendaji wa Waumini katika Kristo (3:5–4:6)**
3:5-11
3:12-17
3:18-21
3:22-25
4:1
4:2-4
4:5-6

4. **Binafsi: Mpango Pekee na Mambo ya Mitume (4:7-18)**
4:7-9
4:10-17
4:18

# Wathesalonike wa Kwanza

## (Kristo: Ahadi ya Mungu Kwetu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama ilivyoelezwa katika 1:1 na 2:18, Paulo ndiye mwandishi wa 1 Wathesalonike.

**Muda wa Kuandikwa: 51-52 B.K.** Barua mbili kwa Wathesalonike ziliandikwa kutokea Korintho, wakati wa miezi kumi na nane ya mtume alipokuwa akiishi huko (Matendo 18:1-11). Barua ya kwanza iliandikwa mapema ya kipindi hicho bada ya Timotheo kuwa amerudi kutoka Thesalonike akiwa na taarifa za kanisa. Na barua ya pili ilitumwa baada ya majuma machache (au miezi michache) baadaye. Kila kipindi kilichoandikwa kinakadiliwa kuwa kati ya 51-52 B.K.

**Nia na Makusudi:** Paulo ndiye aliyekuwa Thesalonike kwa kipindi cha majuma matatu (Matendo 17:2), na hivyo hakuwa tayari kutoa maelekezo yoyote kwa kanisa. Kwa hiyo, kusudi la waraka huu kwa Wathesalonike unaweza kufupishwa kama ifuatavyo: alikuwa akishukuru kwa kile Mungu anachotenda kwa maisha ya Wathesalonike (1:2-3), alikuwa akiwatakia na kuwatahadharisha na maneno yaliyokuwa yakidhoofisha huduma yake (2:1-12), alikuwa akiwataka waimarike katika mateso na hata msongamano ili wasije wakarudia upagani wao (3:2-3; 4:1-12), kujibu maswali ya mafundisho yaliyokuwa yakifanywa na kwa majaliwa ya Wakristo waliokwisha kufa (4:1-13), kujibu maswali kuhusiana na "Siku ya Bwana" (5:1-11), na alikuwa akihusika na matatizo yaliyokuwa yakiinuka katika maisha yao kama kanisa (5:12-13; 19-20).

**Mwonekano wa Yesu katika 1 Wathesalonike:** Kuja kwa krisrto ambako kumetajwa katika sura Kristo anaoneshwa kama tumaini la waaminio katika wokovu: sasa, na hata atakapokuja. Atakapokuja atatuokoa na ghadhabu kama kumbukumbu ya mateso (1:10; 5:4-11), na atatupa tuzo (2:19),atatuimarisha (3:13), atatufufua (4:13-18), na kututakasa wale wote waliokuwa wakimtumaini (5:23).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Yaliyopita: Kazi ya Imani (1:1–3:13)**

| | | |
|---|---|---|
| 1:1-5 | 2:9-12 | 3:1-5 |
| 1:6-10 | 2:13-16 | 3:6-10 |
| 2:1-8 | 2:17-20 | 3:11-13 |

2. **Yaliyopo Sasa: Kazi ya Upendo (4:1-12)**

| | |
|---|---|
| 4:1-8 | 4:9-12 |

3. **Yatarajiwayo: Matmaini ya Uvumilivu (4:13–5:28)**

| | | |
|---|---|---|
| 4:13-18 | 5:12-13 | 5:23-24 |
| 5:1-11 | 5:14-22 | 5:25-28 |

# Wathesalonike wa Pili

**(Kristo: Zawadi ya Mungu Kwetu)**

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama ilivyo katika 1 Wathesalonike, barua hii pia imeandikwa na Paulo (2 Wathesalonike 1:1; 3:17).

**Muda wa Kuandikwa: 51-52 B.K.** Kwa sababu historia zinalingana na ile ya 1 Wathesalonike na uamini kwamba haikundikwa mbali sana baada ya barua ya kwanza, labda baada ya miezi sita. Kwa kuwa hali ya kanisa ilikuwa ni sawa, hivyo, hata mateso yalionekana kuongezeka (1:4-5), hii pamoja na sababu zingine zilimfanya Paulo aandike barua hii akiwa Korintho 51 au 52 B.K. baada ya Sila na Timotheo wabebaji wa barua ya kwanza na walikuwa wamerudi tena na habari mpya za maendeleo.

**Nia na Makusudi:** Wathesalonike wa pili ina makusudi matatu ya maendeleo ambayo Paulo aliyasikia: (1) habari za mateso waliyokuwa wakikabiliana (1:4-5), (2) taarifa ya barua ya uongo ya Paulo na upotofu mwingine wa mafundisho ya Paulo kuhusianana na "Siku ya Bwana" (2:1f.), na (3) njia ambayo wengine walikuwa wakiamini kutokana na kurudi kwa Bwana. Imani hii ilitumika vibaya kwani hawakujishughulisha na kazi yoyote, hivyo, Paulo akaandika ili kuwahimiza na kukemea uvivu huo uliokuwa unaendelea kukomaa (3:5-15).

Ili kutoshereza mahitaji yaliyo katika waraka huu, Paulo aliandika waraka huu ili awafariji na kuwasahihisha. Kwa kufanya hivi aliandika ambo matatu: (1) alikuwa kiwaeleza zawadi na adhabu ambayo itatukia mbeleni katika hukumu ya Mungu (1:3-10); (2) kufafanua matukio yanayohusiana na siku ya Bwana ili kukomesha uongo ya kwamba siku imekwisha wadia (2:1-2); (3) kutoa maelekezo ya ndani ambayo kanisa lilipaswa liyatende ili kuwakosoa waliokuwa wakipinga kufanya kazi (3:6-15).

**Mwonekano wa Yesu katika 2 Wathesalonike:** Kusudi la kitabu hiki hasa sura ya 1-2 ni Kurudi kwa Kristo katika hukumu takapoweka chini uasi wote na kuleta kuhukumu na pili ni kumwonesha Kristo hukumu ijayo.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Salamu au Tangulizi (1:1-2)**

2. **Anasema na Kfariji Kuhusiana na Mateso (1:3-12)**

3. **Anasahihisha na Kutia Changamoto Kuhusiana na Siku ya Bwana (2:1-17)**
   2:1-12 2:13-15 2:16-17

4. **Anaamuru na Kushauri Kuhusianan na Miungu (3:1-15)**
   3:1-5 3:6-13 3:14-15

5. **Baraka Zake za Mwisho na Salamu (3:16-18)**

# Waraka wa Kwanza kwa Timotheo

### (Kristo: Mpatanishi wa Mungu Kwetu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Timotheo alikuwa ni mtumishi kijana huko Efeso, akikabiliana na matatizo mengi katika kanisa na hata katika jamii. Paulo kama baba yake wa Kiroho alimwandikia barua mbili za ushauri na maelekezo. Kwa sababu zinazofanana, Paulo aliandika kwa Tito katika Krete. Nyaraka hizi tatu tunaziita kuwa ni za Kichungaji.

**Muda wa Kuandikwa: 63 B.K.** Ni vizuri kulinganisha Matendo ya Mitume na waraka wa 1 Timotheo na Tito kwa sababu uliandikwa baada ya kuachiliwa kwa Paulo na kuwekwa huru katika Rumi. Kwa sababu ya hili 1 Timotheo yawezekana iliandikwa baada ya kuachiwa kwake kati ya 63 B.K., lakini kabla ya kuanza kwa mateso chini ya mtawala wa Warumi, Nero 64 B.K. Waraka huu yamkini uliandikwa 63 B.K. mapema baada ya kuachlikwa kwake. Tito iliadikwa kati ya 65 B.K. na 2 Timotheo 66 B.K. Paulo alifariki 67 B.K. kulingana na taarifa za baba mmoja wa kanisa aitwaye Bassabius. Kama raia wa Rumi aliuawa kwa upanga alikata kichwa) na si kwa kusulubiwa kama Petro.

Safari za Paulo za kimisionari zilifanyika kati ya miaka 48-56 B.K. Tangu 56-60 B.K. Paulo alikuwa akipitia kwa utaratibu katika mahakama za Rumi hatimaye akiwasili Rumi. Kwa miaka miwili, 61-62 B.K. Paulo alikuwa amewekwa katika nyumba huko Rumi na mwishoni mwa wakati huo aliachiliwa. Tangu 62-67 B.K. Paulo alitembea kwa uhuru kiasi akiwaacha Timotheo katika Efeso na Tito katika Krete na hapo ndipo akawaandikia kila mmoja barua. Kwa hiyo Muda wa 1 Timotheo na Tito yamkini ni 63-65 B.K. Baada ya kuwa amekamatwa tena na kufungwa Paulo aliandika 2 Timotheo kwa hiyo 2 Timotheo iliandikwa miaka ya 66 B.K., na inawakilisha waraka wa Paulo.[83]

**Nia na Makusudi:** Kuna kama makusudi matano yanayoonena katika 1 Timotheo. Paul aliandika: (1) kuhamasisha na kumtia moyo, na kuhimiza Roho na hata ujasiri wa Timotheo kwa kumkumbusha majukumu yake (1:3), karama zake za Kiroho (4:14), kukiri kwake kwema (6:12), na mafundisho aliyokuwa amepewa (6:20); (2) kumpa maono ya kibiblia ili ahusike na makosa ya walimu wa uongo na kumtia moyo Timotheo ili aendelee na mafundisho ya kweli (1:3-11, 18-20; 4:1-16; 6:3-10); (3) na kumpa maelekezo katka kuliongoza kanisa (2:1-15); (4) na kumpa ulinzi na tahadhari za zinazoweza kujiinua na kumwonesha ni jinsi gani anaweza kuhusika nazo. Hii inahusisha vitu kama: mashemasi na wazee wanaofaa (3:1-16), tabia nzuri kuhusiana na wazee na wajane (5:1-20); na, (5) kumtahadharisha na vitu vya uovu (6:11-19).

Nia ya 1 Timotheo, na hata ile ya Tito na 2 Timotheo zinahusisha watu na kanisa. Kwa watu nia ni ***"Kupigana vita vizuri"*** (1:18). Kwa kanisa ni jinsi ya kutenda katika kanisa au nyumba ya Bwana (3:15).

**Mwonekano wa Yesu katika 1 Timotheo:** Sura nyingi zinatuelekeza kwa mtu na huduma ya Mwokozi. Ndiye chanzo cha wito, nguvu, Imani na upendo unaohitajika katika huduma (1:12-14); aliyekuja kuwaokoa wenye dhambi (1:15); ***"Mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu"*** (2:5); ***"Mungu alidhihirishwa katika mwili akajulikana katika haki katika roho, akahesabiwa haki katika roho, akaonekana na Malaika, akahubiriwa katika mataifa akaminiwa katika ulimwengu akachukuliwa juu katika utukufu"*** (3:16); na ***"aliye mwokozi wa watu wote hasa waaminio"*** (4:10).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Salamu (1:1-2)**

2. **Maelekezo Khusiana na Mafundisho (1:3-20)**
   1:3-7 1:12-17
   1:8-11 1:18-20

3. **Maelekezo Kuhusiana na Lbada (2:1–2:15)**
   2:1-7 2:8 2:9-15

4. **Maelekezo Khusiana na Viongozi (3:1-16)**
   3:1-7 | 3:8-13 | 3:14-16

5. **Maelekezo Kuhusiana na Hatari (4:1-16)**
   4:1-5 | 4:6-10 | 4:11-16

6. **Mahusiano Kuhsiana na Majukumu (5:1–6:10)**
   5:1-2 | 5:17-22 | 6:1-2
   5:3-8 | 5:23 | 6:3-10
   5:9-16 | 5:24-25

7. **Maelekezo ya Mwisho kwa Timotheo (6:11-21)**
   6:11-16 | 6:17-19 | 6:20-21

# Waraka wa Pili kwa Timotheo

**(Kristo: Hukumu ya Mungu Kwetu)**

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Angalia 1 Timotheo

**Muda wa Kuandikwa: 66 B.K.** Angalia 1 Timotheo

**Nia na Makusudi:** Tunaporudi katika 2 Timotheo tunaona kitu kingine kabisa. Katika 1 Timotheo na Tito Paulo alikuwa huru na aliweza kusafiri lakini hapa ni mfungwa na anakabiliwa na kifo. Katika barua hii Paulo ana mambo mawili katika kichwa chake: (1) Anamhimiza Timotheo aje Rumi haraka iwezekanavyo ili aone kifo chake (linganisha 4:9, 21 with 4:6-8); and (2) Anamhimiza Timotheo ayashike mafundisho ya kweli ili yamsaidie katika mafundisho ya uongo, aweze kuvumilia magumu kama askari mwema na aelewe kwamba tunaishi katika nyakati za uasi.

Kama ilivyo katika 1 Timotheo, mtazamo wa kibinafsi na wa ushirika katika nia ya kitabu: Kwa mtu, Nia ni au lengo hasa ni ***"Kuchochea karama ya Mungu iliyo ndani yake "*** (2 Timotheo 1:6), japo kuna mistari mingi ya kufanana na huu wa kibinafsi na ushirika (1:14; 2:1-2; 2:15; 4:5). Kwa kanisa, Nia ni kukabidhi mafundisho yanayofaa kwa watu waaminifu ambao watakuwa waaminifu kuwafundisha na wengine kwa njia ya mateso na kutumika kama askari mwaminifu wa Kristo (2:2-4) na labda kupigana vita vyema hadi mwisho (4:6-7).

**Mwonekano wa Yesu katika 2 Timotheo:** Kiini cha huduma zote na uwezo wetu wa kuvumili katika huduma ni mafundisho ya mtu na kazi ya Kristo. Haishangazi, kwa hiyo, kwa vile hata katika kitabu inaeleza uvumilivu katika huduma na mafundisho ya yesu ndiyo msingi. Hapa anaelezwa kama ndiye ***"aliyebatilisha mauti na kuufunua uzima na kutoharibika kwa ile injili"*** (1:10), kama mmoja aliyefufuka toka wafu (2:8), kama mmoja atoaye wokovu na utukufu wa milele (2:10), kama mmoja ambaye wote waaminio wamekufa katika yeye na kwa yeye watazawadiwa kwa kazi ya uaminifu (kama kwenye taji ya haki) na katika faida ya kutawala pamoja naye (2:11-13; 4:8).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Salamu (1:1-2)**

2. **Shukrani kwa Ajili ya Timotheo (1:3-7)**

3. **Wito wa Kkumbuka Majukumu Yake (1:8-18)**
   1:8-14 | 1:15-18

4. **Sifa za Mtumishi Mwaminifu (2:1-26)**
   2:1-7 | 2:14-19
   2:8-13 | 2:20-26

5. **Tahadhari ya Mtumishi Mwaminifu (3:1-17)**
   3:1-9 | 3:10-17

6. **Jkumu la Khubiri Neno (4:1-5)**

7. **Faraja ya Mtumishi Mwaminifu (4:6-18)**
   4:6-8 4:9-15 4:16-18

8. **Kumaliza Salamu (4:19-22)**

# Tito

## (Kristo: Wema wa Mungu Kwetu)

**Jina la Mtunzi wa Kitabu:** Barua za kichungaji zimekwisha elezwa mtunzi wake tazama katika 1 Timotheo.

Tito haikutajwa katika Matendo lakni kuna kumbukumbu zinazomhusu Timotheo nyaraka za Paulo (mara 13). Sura hizi zinafafanua kwamba alikuwa ni mtu wa karibu na Paulo na mmoja wa watumishi walioaminiwa katika injili. Paulo alipoondoka Antiokia kwenda Yerusalemu kueleza habari za injili ya Neema (Matendo 15:1f.) na viongozi wa huko; alimchukua Tito pamoja naye (Wagalatia 2:1-3) kama mfano wa waliokubaliwa kwa neema bila tohara. Hii inaonyesha msimamo wa Paulo katika swala hili (Wagalatia 2:3-5). Inaonesha pia kwamba Tito alifanya kazi na paulo huko Efeso wakati wa safari yake ya tatu ya kimisionari. Tangu pale mtume alimtuma kwenda Korintho ambako alilisaidia kanisa katika kazi zake (2 Wakorintho 2:12-13; 7:5-6; 8:6).

**Muda wa Kuandikwa: 65 B.K.** Muhitasari wa matukio katika waraka huu utatupa angalau wazo la wakati wa Tito japo wakati wenyewe haujulikani. Paulo alikuwa ameachiliwa kutoka katika nyumba alikokuwa amekamatwa Rumi (ambapo tunaona mwishoni mwa kitabu cha Matendo). Labda kwa kuwa Paulo alikuwa ni raia wa Rumi na hata washitaki wake hawathibitishi na alifanya hivyo dhidi yake mbele ya kaisaria (Matendo 24-25; 28:30). Kesi yo ilipotea na paulo aliachiliwa. Mtume alikwenda Efeso ambako alimwacha Timotheo asimamie kanisa na akaendelea Makedonia. Na kutoka Makedonia aliandika 1 Timotheo (1 Timotheo 1:3). Halafu alitembelea Krete akimwacha Tito apangilie na kurekebisha mambo yaliyokuwa yamebakia katika kanisa la Krete. kufuatiwa na hili Paulo alikwenda Nekapoli katika Akaya (Kusini mwa Ugiriki, Tito 3:12). Halafu kutoka Makedonia au Nekapoli Paulo aliandika waraka kwa Tito kumtia moyo na kumwelekeza. Na baadaye alitembelea Troa (2 Timotheo 4:13) ambako alikamatwa tena, akapelekwa Rumi, akafungwa na halafu akauwa. Kama ilivyosemwa hapo mwanzo wakati wa kufungwa kwake kwa mara ya pili katika "dungeon" aliandika 2 Timotheo. na matukio haya yalifanyika kati ya 62-67 B.K.

**Nia na Makusudi:** Malengo na makusudi yanaonekana katika waraka huu: (1) kumwelekeza Tito kipi cha kufanya katika yale mambo yaliyokuwa yakipungua ili aweze kuanzisha katika katika Krete; (2) kumpa Tito mamlaka ya pekee katika upinzani aliokuwa akiupata (2:15; 3:1-15); (3) kumpa maelekezo jinsi ya kukabiliana na upinzani; na maelekezo maalumu kuhusiana na Imani na jinsi ya kutenda; (4) kumtahadharisha dhidi ya walimu wa uongo (1:5, 10-11; 2:1-8, 15; 3:1-11); na (5) kueleza shauku yake ya kukutana na Tito tena katika Nikapoli wakati wa baridi (3:12). Hatujui kama walikutana. Inaeleweka tu kwamba baadaye Tito alirudi Krete na akatumika huko kwa maisha yake yote.

Nia ni kuonyesha ni jinsi gani neema ya Mungu ilivyodhihirishwa kwetu katika maisha yetu yaliyookolewa; na kifo cha Yesu kinatuonesha kukana miungu na tuishi kwa haki na utauwa kama watu tuliojaa kazi jema iliyotunzwa kwa mafundisho mazuri ya Mungu (2:10–3:9).

Mambo mengi yamezungumziwa katika waraka huu Zikiwemo sifa za wazee wanaofaa (1:5-9), melekezo ya watu wa makundi mbalimbali ya umri (2:1-8), uhusiano na serikali (3:1-2), uhusiano wa kizazi na kizazi za wanadamu kwa Roho (3:5), na kazi ya neema ya kuinua kazi njema kati ya watu wa Mungu (2:11–3:8).

**Mwonekano wa Yesu katika Kitabu cha Tito:** Pamoja na mafundisho mengine ya Paulo tunaona jinsi kutenda kwa wakristo kunavyounganishwa na kazi ya Yesu Kristo, kwa wakati uliopita, uliopo na ujao. Katika kitabu hiki tunamuona Mungu (2:13) na kazi ya ukombozi ya mwokozi (2:12). Hapa Kristo anaelezwa kama ***"Mungu na mwokozi wetu, Yesu Kristo ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe wale walio na juhudi katika matendo mema"*** (2:13-14).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Salam na Mwanzo wa Salamu (1:1-4)**

2. **Sifa za Wazee katika Kanisa (1:5-9)**

3. **Wapinzani wa Kanisa (1:10-16)**

4. **Utendaji katika Kanisa (2:1–3:11)**
   2:1-2 2:9-10 3:1-11
   2:3-5 2:11-14
   2:6-8 2:15

5. **Maelekezo na Salamu za Mwisho (3:12-15)**

# Filemoni

## (Kristo: Ujasiri wa Mungu Kwetu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Kama nyaraka zingine za gerezani (Waefeso, Wafilipi, na Wakolosai), Philimoni kilindikwa na Paulo wakati wa ujasiri wake Rumi. Barua imeandikwa Kirumi kwa Philimoni mmiliki wa Onesmo aliyekuwwa mmoja wa mamilioni ya wafungwa katika utawala wa Rumi ambaye alikuwa ameibiwa toka kwa Bwana wake. Onesimo alikuwa akielekea Rumi ambako alikuja kujuana na Paulo ambaye alikuja kumleta kwa Kristo (1:10). Kwa hiyo wote wawili Onesmo na Philimoni walikuwa wakitumikiana katika ukristo wao. Onesmo alikuwa anataka kurudi kwa bwana wake na Philimoni alimpokea kama ndugu yake katika Kikristo. Kifo ilikuwa ni adhabu ya kawaida ya mfungwa aliyekimbia lakini Paulo alijitolea badala ya Onesmo.

**Muda wa Kuandikwa: 60-61 B.K.** Kwa kuwa kiliandikwa kipindi cha Paulo akiwa amefungwa kiliandikwa kati ya 60-61 B.K.

**Nia na Makusudi:** Kusudi kuu la waraka huu ilikuwa ni kumwomba Philimon amsamehe Onesmo na amkubalie kurudi kama ndugu na mtumishi mwenzake katika Kristo (1:10-17). Paulo anamwambia Philimoni amweleze deni lolote alilokuwa nalo Onesmo. Waraka huu unaonesha sura ya Yesu ambaye alichukua nafasi badala yetu (1:18). Na jambo la pili ni kufundisha kivitendo upendo wa kikristo tunapotafuta kueleza mabadiliko ya maisha ya Kikristo kwa sababu hubadili maisha yetu na wengine haijalishi ni nyumbani au na wakuu wetu wa kazi. Katika nyaraka zingine za gerezani Paulo aliongelea mahusiano mapya (Waefeso 6:5-9; Wakolosai 3:22; 4:1). Katika barua hii tuna mfano mzuri. Kusudi la Paulo jingine ni kumshukuru Philimoni na kuomba amwandalie malazi atakapokuwa ameruhusiwa (1:4-7, 22). Nia, halafu injili ni nguvu inayobadili maisha ili kutoka katika vifungo na kuiingia katika uhuru wa kiungu katika Yesu.

Philimoni hakuwa mmiliki pekee wa wafungwa katika kanisa la Kolosai (Wakolosai 4:1), barua hii iliwapa maelekezo viongozi wengine wa kanisa katika mahususiano yao na ndugu wafungwa wakristo wenzao. Paulo hakukana haki ya Filemoni kuhusiana na haki ya wafungwa wake ila alimomba Philimoni awe na mahusiano ya Kikristo na Onesmo (1:16). Wakati huo huo Paulo alikuwa tayari kulipa deni lolote la Onesmo alilokuwa akidaiwa. Barua hii siyo ya kuvamia utumwa ila ni maoni ya ijnsi wakristo mabwana na watumwa waache imani yao katika mfumo huo. Ni kweli Philimoni alimwacha Onesmo huru na akamrudisha kwa Paulo (1:14). Inasemekana kwamba Onesmo alikuja kwa mtumishi na Askofu wa kanisa huko Efeso.[84]

**Mwonekano wa Yesu katika Filemoni:** Msamaha walio nao wakristo katika Kristo ni mzuri mno, unataswira na unonekana katika Filemoni. Makosa ya Onesmo (1:11, 18), Paulo anayebeba (1:10-17). Paulo anaacha mambo yake (1:8) na anasimama badala yake na madeni yake (1:19). Kwa matendo ya neema ya Philimoni Onesmo anaingizwa katika uhusino mzuri (1:15-16). Kwa maneno haya sisi ni kama Onesmo. Kazi ya uwakili wa Paulo unafananishwa na Yesu alivyotutetea kwa Baba. Onesmo alishitakiwa kwa sheria lakini akaokolewa kwa neema.[85]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Maombi ya Shukrani kwa Ajili ya Filimoni (1:1-7)**
   1:1-3 1:4-7

2. **Furaha ya Paulo kwa Ajili ya Onesmo (1:8-18)**
   1:8-9 1:10-16 1:17-18

3. **Ahadi za Paulo kwa Filemoni (1:19-21)**

4. **Mambo Binafsi (1:22-25)**

# Sehemu ya 3
# Nyaraka za Jumla

**Utangulizi:** Sasa tunakuja kwenye nyaraka nane za mwisho za Agano jipya, saba zinaitwa nyaraka za jumla au nyaraka Katoliki japo Waebrania haiingizwi katika maelezo haya. Neno Catholic lilitumika kwa maana ya jumla au ulimwengu ili kutofautisha nyaraka hizi na za Paulo zilizokuwa zikiyahusu makanisa au watu.[86] Katika maelezo yake (ukiwemo waraka wa 2 na 3 Yohana) hazijalenga eneo moja tu. Kama Vielelezo Yakobo inaeleza ***"Makabila kumi na mbili yaliyotawanyika,"*** ambayo ni muundo wa waaminio wote popote pale (kama vile Wakristo wa Kiyahudi kipindi cha mwanzo kabisa). Halafu 1 Petro inaeleza "Kwa wale aliokuwa wakiishi ambao si raia waliokuwa wametawanyika kote ulimwenguni Ponto, Galatia, Kapadokia, Asia, na Bethania," kama mfano kwa waaminio katika maeneo haya yote. Na nyaraka za 2 na 3 zimeunganishwa katika kundi hili japo ziliandikwa kwa watu maaalumu. Kwa sababu ya utofuti huu, katika somo hili nyaraka hizi nane zinaitwa "Nyaraka za Jumla." Leleweke kwamba nyaraka za Jumla hazikuwa zimeandikwa kuhusiana na wahusika wao sawa na waebrania lakini hizi nyaraka za jumla zina majina ya watu walioandika.

Kwa ujumla tunaweza kusema Yakobo na 1 Petro zina mchanganyo (zinahusika na kanuni ya Mungu kwa mazuri na Mabaya) zinawaita waumini wawe katika mwenendo mtakatifu na Mwokozi. 2 Petro na Yuda ni za kinabii zikiwaonya waumini dhidi ya walimu wa uongo na zinawahimiza katika Imani. Waebrania na waraka wa Yohana ni zinahusu Kristo na maadili, zikiwahimiza waumini kukaa katika Kristo kama ufunuo wa Mwisho wa Mungu wa Agano la Kale wawe waishi katika mapenzi yake na si kwenda tofauti na Injili.

Nyaraka hizi nane zina urefu wake tofauti tofauti (chini ya asilimia 10 ya Agano Jipya). Zinaongeza katika nyaraka zile 13 kwa kutoa mitazamo tofauti tofauti katika utajiri wa Ukweli wa Ukristo. Kwa kila mwandishi kati ya hawa watano (Yakobo, Petro, Yohana, Yuda na mtunzi wa Waebrania) ana mchango tofauti kulingana na mtazamo wake. Kama nyaraka za Paulo zilivyo ufunuo wa Agano Jipya baada ya matendo ungesitishwa na mtazamo wa nabii mmoja kama watu hawa watano wasingeliingizwa.[87]

## Waebrania
### (Kristo: Mkuu Kuliko Wote)

**Jina na Mtunzi la Kitabu:** Kwa miaka 1,200 (400 hadi 1600 B.K.) kitabu hiki kiliitwa "Waraka wa Paulo kwa Waebrania," lakini kukawa na mabishano kulingana na mwandishi wake. Kwa hiyo jina lake likawa "Waebrania."

Mawazo mengi yamekuwa yakizunguka hasa na wasomi, lakini kwa kweli ukweli ni kwamba mwandishi wa kitabu hiki hajatajwa katika sehemu yoyote ya kitabu hiki na kiko katika ungu tu maana tarehe, Sehemu ya kuandikiwa na hata uongozi wake haujulikani.

Kitabu hiki hakikueleweka kwa wasomaji wa kale na hata walifikiri juu ya mwandishi wake (13:18-24). kwa sababu fulani fulani, hata hivyo, desturi za kanisa la kwanza zilikuwa zikijaribu kufikiri mwandishi wake. Watu wengine katika kanisa walisema kuwa ni Paulo, wengine Barnaba, Luka au Clementi na wengine wakasema hajulikani. Undani wa kiroho na ubora wake wa Waebrania unatuonesha uvuvio wake ijapokuwa hakijulikani mwandishi wake.

Kwa kuwa hata mhusika wa kitabu hicho haujulikani kama walivyokuwa wakitajwa katika nyaraka za Paulo lakini twaweza kusema neno kuhusiana na wao, asili ya kitabu hiki na nakara zake za maandiko kutoka Agano la Kale na mkazo wake wa utoaji dhabihu yamkini wakawa ni Waebrania na ndugu, Mwandishi Zane C. Hodges anasema:

> Watambuzi wa kwanza wa kitabu cha Waebrania, kama ilivyo kwa mwandishi wake, hawajulikani. Lakini hata hiyo walikuwa ni wa jamii fuani. Na hii inaonekana kutoka katika mawazo mbalimbali. Wasomaji walikuwa na historia inayoeleweka na mwandishi anasema juu ya Siku zao za mwanzo (Waebrania 10:32-34); alijua juu ya vizazi vyao vya zamani na hata vya sasa kwa Wakristo wengine (6:10); na alikuwa wazi katika maswala yao ya Kiroho (5:11-14). Mwandishi ameeleza mambo mengi na ameeleza kusudi lake la kuwatembelea, akiwa na Timotheo (13:19, 23). na halafu anahitaji maombi yao (13:18).
>
> Kwa namna yeyote wasomi wake walikuwa ni wakuu wa Kiyahudi. Japo hii imekuwa ikihojiwa na yaliyomo katika kitabu yanapingana nayo. Kwa kichwa chake cha "kwa Waebrania" inaweza kuwa ni kiunganishi lakini ni cha asili. Kitu chochote kinaposemwa kwa ajili ya Watakatifu vyovyote kitakavyosemwa, ukweli unabaki kwamba mkazo wa mwandishi ulikuwa ni juu ya

destruri za Kiyahudi na mabishano yao dhidi ya mfumo wa kiyunani ulikokuwepo. Ukubwa na uzito wa mamlaka ya Agano la Kale ulikuwa ni wa muhimu sana kwao.[88]

**Muda wa Kuandikwa: 64–68 B.K.** Maoni mbalimbali yanasema yamkini muda ulikuwa ni kati ya 64-68 B.K. kwanza, kitabu kilionekana na Clementi huko Rumi (Mchungaji wa kanisa la kwanza) 95 B.K. yamkini kilikuwa kimeandikwa mapema kabla ya wakati huo. Pili Inaonekana kwamba kitabu kiliandikwa kabla ya kuharibiwa kwa Yerusalemu 70 B.K. kwa sababu zifuatazo: (1) kwa sababu mwandishi angekuwa ametaja kuharibiwa kwa hekalu na mwisho wa dhabihu za kiyahudi; (2) Mwandishi anazungumzia hekalu na kazi za makuhani kwa hali inayoonesha kwamba walikuwa bado wanaendelea (5:1-3; 7:23, 27; 8:3-5; 9:6-9, 13, 25; 10:1, 3-4, 8, 11; 13:10-11); (3) mwandishi anarejea katika kuachiliwa kwa Timotheo katika 13:23, ambayo, kwa kuungnisha na huduma yake na Paulo zinonyesha miaka ya 60.

**Nia na Makusudi:** Nia ya Waebrania iko katika ukuu wa Kristo au mamlaka yake na Ukristo wa mifumo ya Agano la Kale. Maneno mbalimbali, nzuri, kamilifu na mbinu yametumika kueleza hii. Japo kusudi lake la kwanza mwandishi anatafuta kueleza njia tano bora za Ubora wa Kristo. Yesu ni: (1) Mkuu wa manabii wa Agano la Kale (1:1-3); (2) kwa malaika (1:4–2:18); (3) kwa Musa (3:1-6); (4) Kwa Yoshua (3:7–4:16); na, (5) Aroni Kuhani (5:1–10:18). Lengo la nia hii ni kuwatahadhalisha wasomaji hatari ya kuchoka kwa yale mambo waliyonayo katika Kristo kwa mambo yasiyofaa ya Agano la Kale (10:1). Wasomaji wanahimizwa kuendelea katika ukomavu na zawadi yao kama waumini waaminifu wakiutimiza wito wao wa mbinguni. Katika kufanya hili kuna aya tano za kutahadharisha zilizoingizwa ili kuwatia changamoto katika Imani yao ya Ukristo (2:1-4; 3:1–4:13; 5:11–6:20; 10:26-39; 12:14-29).

**Mwonekano wa Yesu katika Waebrania:** Katika kulikamilisha lengo la kumuonyesha Yesu kama mkuu Waebrania kinakuwa ni kitabu kimoja kizuri cha kumweleza Yesu katika Agano Jipya. Hapa ameelezwa kama Mwana, kama Nuru na mwakilishi wa Mungu (1:3, 13), kama mmoja aliye kaa mkono wa kuume (1:3), kama mmoja aliyeelezwa na Mungu baba kama Mungu (1:8-9), Muumbaji (1:10-12), na kuhani kulingana na amri za Melkizedeki (7). Hapa Kristo anaonekana kuwa ni nabii wa Mungu, Kuhani, na Mfalme. Ni mwokozi wetu, aliyefanywa kama ndugu zake aliyetuokoa sisi tuliokuwa hatusitahili. Na yuko mbinguni kama kuhani anayetuombea.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Ukuu wa Kristo kwa Viongozi wa Agano la Kale (1:1–7:28)**
   a. Kristo ni Mkuu kwa Manabii wa Agano la Kale (1:1-3)
   b. Krsito ni Mkuu kwa Malaika (1:4–2:18)
      1:4-14   2:5-8   2:14-18
      2:1-4   2:9-13
   c. Kristo ni Mkuu kwa Musa (3:1-6)
   d. Kristo ni Mkuu kwa Yoshua (3:7–4:13)
      3:7-11   4:1-5
      3:12-19   4:6-13
   e. Kristo ni Mkuu kwa Ukuhani wa Haruni (4:14–7:28)
      1) Furaha ya Kufunga (4:14-16)
      2) Sifa za Kuhani (5:1-10)
         5:1-4   5:5-10
      3) Sifa za Kachanan na Uvivu katika Maswala ya Kiroho (5:11–6:12)
         5:11-14   6:1-8   6:9-12
      4) Uhalisi wa Ahadi za Mungu (6:13-20)
      5) Ukuu wa Kristo ni Zaidi ya Amri za Makuhani (7:1-28)
         7:1-3   7:11-22
         7:4-10   7:23-28

2. **Kazi kbwa ya Dhabihu ya Kuhani Wetu (8:1–10:39)**
   a. Agano Jema (8:1-13)
      8:1-6   8:7-13
   b. Ibada Njema (9:1-10)
      9:1-5   9:6-10
   c. Dhabih Njema (9:11–10:18)
      9:11-14   9:23-28   10:11-18
      9:15-22   10:1-10
   d. Sifa (10:19-39)
      10:19-25   10:26-31   10:32-39

3. **Kuitunza Imani (11:1–12:29)**
    a. Mfano wa Mashujaa wa Imani Waliopita (11:1-40)
        11:1-2 11:13-16 11:30-31
        11:3-7 11:17-22 11:32-38
        11:8-12 11:23-29 11:39-40
    b. Kuwahimiza katika Kutnza Imani (12:1-11)
        12:1-2 12:3-11
    c. Shauri katika Kuitunza Imani (12:12-17)
        12:12-13 12:14-17
    d. Furaha ya Kuitnza Imani (12:18-29)
        12:18-24 12:25-29

4. **Hitimisho (13:1-25)**
    a. Kanuni za Kiutendaji kwa Ajili ya Maisha ya Kikristo (13:1-17)
        13:1-6 13:7-14 13:15-16
    b. Hitaji la Maombi (13:18-19)
    c. Baraka (13:20-21)
    d. Maazimio Binafsi (13:22-23)
    e. Salamu na Baraka za Mwisho (13:24-25)

# Yakobo
## (Kristo: Mfano)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Waraka huu unaanza na ***"Yakobo mtume wa Mungu na wa Bwana Yesu Kristo wa kabila kumi na mbili waliotawanyika"*** (1:1). Kuna watu wanne walio na majina ya Yakobo katika Agano Jipya. Hawa ni: (1) Mwana wa Zebedayo na ndugu yake Yohana (Marko 1:19), (2) Mwana wa Alphayo (Marko 3:18), (3) Baba wa Yuda (siyo Iskariote; Mathayo 10:3; Marko 3:18; Luka 6:16), na (4) Ndugu yake wa karibu na Yesu (Wagalatia 1:19). Kulingana na hili, Mwandishi Ryrie anaandika:

> Hawa watu ni wanne wenye jina moja Yakobo katika Agano Jipya wawili wao wanasadikika kuwa ndiyo waandishi wa waraka huu wa Yakobo. Yakobo mwana wa Zebedayo na Yakobo Ndugu yake wa karibu na Yesu. Alijulikana kama mwana wa Zebedayo ndiye aliyekuwa mwandishi kwa sababu aliuawa miaka ya 44 B.K. (Matendo 12:2). Mwandishi wa kitabu hiki anasemekana kuwa ni Yakobo ndugu yake wa karibu na Yesu wa Agano Jipya ambaye alikuwa ni kiongozi wa kanisa la Yerusalemu (Matendo 12:17; 15:13; 21:18). Ushahidi huu unathibitishwa katika Kiyunani katika huu waraka na hotuba ya Yakobo Yerusalemu (Yakobo 1:1 na Matendo 15:23; Yakobo 1:27 na Matendo 15:14; Yakobo 2:5 na Matendo 15:13).[89]

Njia ambayo Yakobo aliitumia kwa wale alikuwa akiwaandika ni lazima ielezwe. Yakobo inaelezwa ***"kwa makabila kumi na mbili yaliyokuwa yametawanyika"*** (1:1). Kama ilivyoelezwa kutoka "ndugu zangu" katika sura 1:19 na 2:1, 7, hii ni kumbukumbu si kwa kule kutawanyika kulikotokea kati ya B.K. 66-70, bali ni kwa wale wayahudi waliokuwa wakristo lakini wametawanyika kutoka katika nchi yao (Mathayo 1:11, 12, 17). Katika sura za mwanzo ya kitabu cha Matendo, wayahudi walikuwa Yerusalemu kutoka katika sehemu mbalimbali za Ulimwengu kwa ajili ya Pentekosti (Matendo 2:5). Wengi wao waliona na kusikia miujiza ya Pentekoste na wakamwamini Yesu. Baadaye walirejea katika miji yao katika sehemu mbalimbali ulimwenguni. Ilikuwa ni kwa haya Yakobo aliyokuwa akiyaandika.

**Muda wa Kuandikwa: 45 au 46 B.K.** Yakobo yamkini kikawa ni kitabu cha kwanza kuandikwa na wasomi wengi wana sema kati ya miaka ya B.K. 45. Sababu ni kama zifuatazo: (1) Kuna sifa nyingi za wayahudi katika kitabu ambazo zinathibitisha kwamba kiliandikwa kipindi cha wayahudi; (2) hakuna kumbukumbu ya mambo ya Tohara; (3) Neno Sinagogi lina maana ya mahali pa kukusanyikia na ni zaidi ya neno kanisa (2:2); (4) Kukosekana kwa habari nyingi kunaonekana katika baraza la Yerusalemu ambayo ni kama mahusiano ya Wakristo wa kiyahudi na watakatifu (Matendo 15:1 na kuendelea; B.K. 49) na inasadikiwa mapema; na (5) "Mafundisho ya Yesu yaliwasaidia sana katika kuwaendeleza."[90]

**Nia na Makusudi:** Yakobo inaeleza juu ya Imani thabiti,ambayo ni ya muhimu sana, ya nguvu na itendayo kazi. Yakobo anawaandikia waumini kuwatahadharisha na imani iliyokufa na isiyokuwa na imara kwa mtu binafsi na hata kwa wao wote na kuwahimiza wao kukua na kukomaa katika mambo ya roho.

**Mwonekano wa Yesu katika Yakobo:** Katika sura ya 1:1 na 2:1, Yakobo anamzungumzia "Bwana Yesu Kristo" na kuja kwake (5:7-8). Katika mistari 108 ya waraka huu, kuna rejea za vitabu kama 22 kutoka katika Agano la Kale na vielelezo 15 ya mafundisho ya Kristo kutoka katika Hotuba ya Mlimani.[91]

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza[92]

1. **Simama kwa Ujasiri (1:1-27)**
   a. Salamu (1:1)
   b. Furaha katika Dhiki (1:2-12)
      1:2-4 1:5-8 1:9-12
   c. Upinzani katika Majarib Yaliyokufa (1:13-18)
   d. Kupmzika katika Ukweli wa Mungu (1:19-27)
      1:19-25 1:26-27

2. **Tumika kwa Huruma (2:1-26)**
   a. Wakubali Wengine (2:1-13)
      2:1-7 2:8-13
   b. Wasaidie Wengine (2:14-26)
      2:14-17 2:18-26

3. **Zungumza kwa Uangalifu (3:1-18)**
   a. Kuwa Makini katika Mazngumzo (3:1-12)
      3:1-5 3:6-12
   b. Kutawala Mawazo (3:13-18)

4. **Kuungama (4:1-17)**
   a. Kugeuka (4:1-6)
   b. Kugeuza Hukumu Kuwa Haki (4:7-12)
      4:7-10 4:11-12
   c. Geuza Majivuno Kuwa Imani (4:13-17)

5. **Shiriki kwa moyo wa ndani (5:1-20)**
   a. Shiriki katika Umiliki (5:1-6)
   b. Shiriki kwa Uvumilivu (5:7-12)
   c. Shiriki katika Maombi (5:13-20)
      5:13-18 5:19-20

# Petro wa Kwanza
### (Kristo: Mfano wa Mateso)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Mstari wa kwanza tu unatuonyesha kwamba mwandishi ni Petro (1:1). Petro wa kwanza ni kazi ya Petro iliyotambuliwa na ulimwengu wote na kanisa la kwanza.

Waraka unaandikwa kwa ***"wale waliokuwa wakikaa kwa muda tu katika mtawanyiko*** (katka Ponto, Galatia, Padokia, Asia, na Bethania) ***waliokuwa wamechaguliwa"*** (1:1). Petro alitumia maneno mawili makubwa kuwaeleza wahusika "Wakazi wa Muda" (inayowakilisha wakazi wa Muda na raia) na mtawanyiko. Mtawanyiko unahusika na Wayahudi waliokuwa hawaishi Palestina lakini walikuwa wametapakaa katika ulimwengu wa Mediterraneani. Hapa nafikiri ni watakatifu waliokuwa wamesambaa katika ulimwengu huu mchafu wa miungu.[93] Petro alikuwa ni muumini wa kiyahudi na watakatifu pamoja

Petro wa Kwanza inahusika na wakristo waliokuwa wamesambaa katika maeneo matano ya Rumi katika Peninsula ya Asia ndogo. Kwa sasa eneo hilo ni Uturuki ya kaskazini. Makanisa katika maeneo haya yalikuwa na wayahudi pamoja na watakatifu. Waraka huu una kumbukumbu nzuri za nakara za Agano la Kale. Wayahudi Wakristo walikua wameona umuhimu katika neno DIASPORA, lililotafasiliwa "Kutawanyika," lilitumika katika salamu (1:1). Wayahudi walioishi nje ya Yerusalemu waliitwa kuwa ni DIASPORA.

Watakatifu walikuwa wameisha pona juhudi za Petro katika maisha matakatifu katika nuru ya historia ya ujinga wa neno la Mungu (1:14). Wakristo walikuwa wametiwa moyo kwa ukweli kwamba japo kuwa walikuwa katika ujinga lakini sasa waliitwa watu wa Mungu (2:10). Petro anawahusisha watu wote wayahudi na watakatifu katika barua yake hii akiwatia moyo makanisa ya Asia ndogo.[94]

**Muda wa Kuandikwa: 63-64 B.K.** Desturi za kanisa zinamunganisha Petro na miaka yake ya baadaye na mji wa Rumi. Kumbukumbu ya Babeli katika 5:13 ni kile kiini cha Rumi na barua hii iliandikwa kipindi Petro akiwa Rumi wakati wa mwisho wa karne ya maisha yake ya mwisho 63 B.K., kabla ya kuvunjwa kwa mateso ya Nero 64 B.K. Petro haiandikii Rumi kama adui wa Ukristo (1 Petro 2:13-17) ambayo ingekuwa ni ngumu sana (lakini siyo kwamba haiwezekani) kipindi cha mateso ya Nero.

**Nia na Makusudi:** Kwa kuwa Petro anaongelea mafundisho mengi na ana mengi ya kusema kuhusu maisha ya mkristo na majukmu ya mkristo nia na makusudi ya 1 Petro inasimama katika matatizo ya mateso, mateso kw ajiri ya imani ya mwingine. Kitabu hiki kimelezwa kama kitabu cha kubeba mikononi kuwaonesha wakristo ni jinsi gani wanaweza kuishi kama wakazi wa muda na mabalozi wa Kristo katika ulimwengu (1:1, 13-21; 2:11-12; 3:14, 17; 4:1, 13, 15, 16, 19).

Kuna makusudi mengi katika kitabu hiki. Kimeandikwa ili kutoa mwelekeo kwa waumini: (1) inalenga ujio wa ufunuo wa Yesu Kristo na wokovu wake (1:3-12); (2) kwa kumfuata Kristo kama kielelezo kamili katika mateso (2:21-24); na (3) kwa kuishi katika ulimwengu kulingana na wito wao kama watu muhimu wa Mungu kwa kutunza taarifa njema ya watakatifu wa duniani (2:4-12; 4:1-19). Kusudi jingine ni daraja kati ya mafundisho na utendaji (5:12) na kuwatia moyo kuzichunga kondoo za Mungu (5:1-4), ambayo ni lazima na katika uwezo wa kanisa katika kutenda kwa ufanisi katika ulimwengu huu.

**Mwonekano wa Yesu katika 1 Petro:** Kitabu kimejaa utu na kazi ya Yesu. Kwa njia ya ufufuko wa Yesu Kristo wakristo wana "tumaini hai" na "urithi usioharibika" (1:3-4). Katika sehemu nyingi Petro anazungumza juu ya kuja kwa utukufu wa ufunuo wa Kristo (1:7, 13; 4:13; 5:1). Na pia anaongea juu ya utu na kazi ya Kristo kama mwanakondoo wa Mungu anayetukomboa kwa kuzichukua dhambi zetu pale (1:18-19; 2:24), Kristo kama kielelezo chetu kamili katika mateso (2:21-24), and (3) Kristo kama mchungaji mkuu na mlinzi wa waumini (2:25; 5:4).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Wokovu wa Waaminio (1:1-12)**
   a. Salamu (1:1-2)
   b. Tumaini Lijalo na Mateso Yaliyopo (1:3-9)
   c. Wokovu wa Sasa na Ufunuo Uliopita (1:10-12)

2. **Utakatifu wa waaminio (1:13-2:12)**
   a. Wito wa Utakatifu (1:13-21)
   1:13-16 1:17:21
   b. Wito wa Kuwapenda Wengine (1:22-25)
   c. Wito wa Kuyatamani Maziwa Yasiyoghoshiwa (2:1-3)
   d. Wito wa Kutoa Dhabihu Takatifu (2:4-10)
   2:4-8 2:9-10
   e. Wito wa Kuachana na Tamaa za Mwili (2:11-12)

3. **Kujitoa kwa Waumini (2:13–3:12)**
   a. Katika Serikali (2:13-17)
   b. Katika Shughuli (2:18-25)
   c. Katika Ndoa (3:1-8)
   d. Katika Nyanja Zote za Maisha (3:9-12)

4. **Mateso ya Waaminio (3:13–5:14)**
   a. Mawasiliano Yanayohitajika katika Mateso (3:13-17)
   b. Kielelezo cha Yesu katika Mateso (3:18–4:6)
   c. Amri kwa Ajili ya Mateso (4:7-19)
   d. Mchungaji na Mateso (5:1-9)
   e. Mwisho au Baraka (5:10-14)

# Petro wa Pili
## (Kristo: Ukamilifu wa Neno)

**Jina na Mtunzi wa Kitabu:** Mwandishi anajitambulisha mwenyewe kama Simoni Petro (1:1). Sababu nyingi zinathibitisha kwamba Petro ndiye mwandishi. Kwa kila sehemu yake ya ujumbe wa mwisho anaonekana kama baba anayekufa na neno hili amelitumia kwake yeye mwenyewe (1:14) anaeleza kwamba yeye alikuwepo kipindi cha Yesu anabadilika sura (1:16-18 linganisha Mathayo 17:1-5). Na anaeleza kwamba barua hii ya pili ni yake (3:1), na naonyesha ukaribu wake na Paulo aliyemwita, "ndugu yetu mpendwa" (3:15). Waraka huu unaitwa Waraka wa "Pili wa Petro" ili kuitofautisha na ule wa kwanza.

Petro aliandika barua hi kwa watu walewale (3:1) sawa na ile ya kwanza. Ni agano la mwisho, onyo, na barua ya siku ya mwisho (1:14; 2:1-22; 3:3). Alikuwa akiiandika kwa wakristo wenye imani nzuri,wasio na mashaka, kwa kanisa la wayahudi na watakatifu la "Ponto, Galatia, KappadoKia, Asia, na Bethania" (1 Petro 1:1).

**Muda wa Kuandikwa: B.K. 67-68** Kama barua ya wosia Petro aliandika barua hii mwishoni kabisa mwa mateso (1:12-14). Kulingana na historia ya kanisa la kwanza, Mwana historia wa kanisa la kwanza Eusebius, Petro aliuawa wakati wa mateso ya Nero (miaka 67-68 B.K.). Kwa hiyo barua iliandikwa kati ya miaka hii.

**Nia na Makusudi:** Kama mtume Paulo alivyotahadharisha kuhusiana na hatari zijazo mwishoni mwa maisha yake na huduma (2 Timotheo), kwa hiyo Petro alikuwa anatahadharisha juu ya hatari zinazoinuka za waalimu wa uongo kama ilivyokuwa imetabiriwa na manabii na Bwana mwenyewe kwa mitume wake (2:1; 3:1-3). Barua hii ya kutahadharisha ilikuwa ni kuhusu kanisa hasa kulingana na kuinuka kwa waalimu wa uongo.

Kuonyesha kwamba Mungu amekwisha toa yote yanayohitajika kwa ajili ya maisha na mambo ya utaua (1:3), 2 Petro ni mwenye huruma kwa watu wake ili wapate kukua na kukomaa katika Kristo wasiwe wavivu au wasiozaa matunda (1:8), kwa hiyo ni kama msingi wa kulinda dhidi ya walimu wa uongo waliokuwa wakiinuka. Hii ilisababishwa na kweli kwamba Petro alijua muda wake wa hapa duniani kuwa ni mfupi (1:13-15) na kwamba mwili wa Kristo ulikabiliana na hatari ya haraka (2:1-3). Hivyo pia akatamani kuamsha fikra zao na kuwakumbusha (1:13; 3:1-2) ili kwamba wapate kuwa na mafundisho yake kwa wingi katika akili zao (1:15). Kwa kufanya hili aliwaeleza wakristo waliokomaa kwa umakini sana, akiwa himiza wakue katika neema na ufahamu wa mwokozi (1:2-11; 3:18).

Kama msingi wa kukabiliana na walimu wa uongo Petro alielezea asili ya neno la Mungu kama uhakika wa msingi wao (1:12-21) na kuwatahadharisha tena juu ya hatari zinazokuja za walimu wa uongo ambao kwa kweli alieleza na hakika ya hukumu yao (2:1-22). Baadaye aliwatia moyo wasomi wake kwa kurudi kwa Yesu (3:1-16), na kwa maelezo haya ya mwisho ya kurudi kwa Bwana Petro alitoa changamoto ya mwisho,

> ***Kwa hiyo wapenzi kwa kuwa mnatazamia mambo hayo fanyeeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake. Nanyi uhesabuni uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu kama vile na ndugu yetu mpenzi Paulo aliyewaandikia kwa hekma aliyopewa, vilevile kama katika nyaraka zake zote pia akitoa humo habari za mambo hayo katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara huyapotoa kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine kwa uvunjifu wao wenyewe utukufu una yeye sasa na hata milele, Amen.***

**Mwonekano wa Yesu katika 2 Petro:** Petro anamzungumzia Yesu kama chanzo cha maisha na mambo ya Mungu na anazungumza juu ya Yesu kama Bwana na Mwokozi mara Nne. Kwa nyongeza anarejea juu ya kubadilika kwa sura katika mlima mtakatifu na anaangalia mbele kuja kwake Yesu mare ya pili. kwa wakati huu ulimwengu utaona kile Petro na mitume wengine wawili walivyofaidika kuona katika mlima ule mtakatifu.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Salamu (1:1-2)**

2. **Maendeleo ya Mkristo (1:3-21)**
   a. Kukua kwa Imani (1:3-11)
      1:3-4    1:5-8    1:9-11
   b. Misingi ya Imani (1:12-21)
      1:12-15    1:16-18    1:19-21
3. **THukum ya Walimu wa Uongo (2:1-22)**
   a. Hatari na Utendaji Wao (2:1-3)
   b. Kuharibiwa Kwao (2:4-10)
   c. Maelezo na Sifa Zao (2:11-22)

4. **Ujasiri kwa Ajili ya Mambo Yajayo (3:1-18)**
   a. Dhihaka ya Walimu wa Uongo (3:1-7)
      3:1-2    3:3-7
   b. Kukawia kwa Siku ya Bwana (3:8-9)
   c. Utata naofata ya Bwana (3:10-13)
   d. Uvmilivu Unaohitajika katika Kuiona Hatari (3:14-18)

# Waraka wa Kwanza wa Yohana
## (Kristo: Upendo wa Mungu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Japo jina la mwandishi halionekani lakini inasemekana kuwa ni mtume Yohana. Mwandishi alikuwa ni shahidi aliyekuwa na Yesu aliyemjua kwa undani (1:1-5).

Kitabu chote hiki kinazo sababu zinazoeleza kwamba Yohana alikuwa akiandika kwa waliokuwa wameamini (2:1, 12-14, 19; 3:1; 5:13), lakini Yohana haonyeshi walikuwa wapi au haoni waliishi wapi. Inaonyesha kuwa ilikuwa ni barua iliyokuwa imeandikwa ili isambazwe katika makanisa. Yamkini yalikuwa ni makanisa yaliyokuwa yakiuzunguka mji wa Efeso kwa kuwa waandishi wa mwanzo kabisa wamemuonyesha Yohana akiwa Efeso kwa miaka yake iliyokuwa imebakia.

Waandishi wa kwanza wanasema matumizi wa 1 Yohana yalikuwa Asia (kwa sasa Uturuki), ambako ilikuwako Efeso. Clement wa Alexanda (mchungaji wa kanisa la kwanza) anaonesha kwamba Yohana alikuwa ametumika katika makanisa mbalimbali yaliyokuwa yamesambaa katika mji huo. Kwa hiyo tunaweza kusema kwamba 1 Yohana ilitumwa kwa makanisa ya mji wa Asia.[95]

**Muda wa Kuandikwa: 85-90 B.K.** Ni vigumu kueleza tarehe au kipindi cha kuandikwa nyaraka za Yohana lakini nia na makusudi yanafanana na injili ya Yohana na hivyo tunaweza kusema kwamba yamkini ziliandikwa baada ya injili lakini kabla ya mateso ya Domitie miaka ya 95 B.K. Kwa hiyo kipindi chake tunachoweza kusema ni kati ya 85-90 B.K.

**Nia na Makusudi:** Kusudi la kitabu ni ushirika na Mungu kwa njia ya Bwana Yesu Kristo (1:3-7). Kwa kuangalia kwa hawa waumini, yamkini ni aina ya unostiki (imani ya kwamba mambo yote yanapatikana kupitia akili peke yake na kuleta uhuru), Yohana aliandika kueleza asili ya ushirika na Mungu ambaye ameelezwa kama mwanga, upendo, na uzima (1:5), Mungu ni upendo (4:8, 16), Mungu ni uzima (1:1-2; 5:11-13). Kutembea katika ushirika na Mungu, halafu, ina maana ya kutembea katika nuru inayotupa kujua uhai wake, upendo wake kwa wengine na haki yake. Waraka unatupa uhakika mbalimbali ya ushirika japo mengine yanaonekana kama majaribu ya wokovu. Lakini kutunza kusudi mafundisho ya walimu wa uongo na siri yake kwa wamuaminio ni vizuri kuyatazama haya kama uhakika wa ushirika wetu,kumjua kwetu Yesu kwa undani kabisa unaoleta mabadiliko ya maisha kwa waumini.

Ni vigumu kuelewa na hata kuyatenda haya kama wakristo lakini kutoka katika yaliyomo kwenye 1 Yohana inaonesha kuukana kabisa mwili na kudai kwamba dhambi hii isivunje ushirika wetu na Mungu. Yohana akaandika kwa watoto wake wadogo (2:1, 18, 28; 3:7, 18; 5:21) sababu kama tano hivi: (1) kuendeleza ushirika wa kweli (1:3f.); (2) kwa na furaha kamili (1:4); (3) kudumisha utakatifu kwa njia ya ushirika (1:6–2:2); (4)Kupinga uasi (2:18-27); na (5) kutoa uhakika (5:11-13).

**Mwonekano wa Yesu katika 1 Yohana:** Kitabu hiki kinaonyesha huduma ya Yesu iliyopo ndani ya maisha ya wakristo na inaonesha kurudi kwake tena. Damu yake husafisha kabisa waaminio (1:7) kutoka katika dhambi za mtu na udhalimu wote kwa njia ya kukiri dhambi (1:9). Lakini hata hivyo inaeleza kwamba Kristo ndiye wakili wetu wa haki mbele ya Baba (2:1) na kwamba dhabihu hii si kwa walioamini tu bali ni kwa ulimwengu (2:2), kwamba Yesu ni Kristo aliyekuja katika mwili (2:22; 4:2-3), alikuja kwa maji na damu kama kumbukumbu ya ubatizo na msalaba wake (5:6), na kwamba anakuja tena tutamwona na tutafanana naye (2:28–3:3).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi na Kusudi la Barua (1:1-4)**

2. **Hali Inayohitajika katika Ushirika (1:5–2:2)**
   a. Kutembea katika Nuru (1:5-7)
   b. Kuungama Dhambi (1:8–2:2)
   1:8-10 2:1-2

3. **Kudumu katika Ushirika (2:3-27)**
   a. Kusudila Ushirika ni Kuwa kama Kristo (2:3-11)
   2:3-6 2:7-11
   b. Amri za Ushirika, Kutokuupenda Ulimwengu (2:12-17)
   2:12-14 2:15-17
   c. Tahadhari za Ushirika-Ulinzi Dhidi ya Mpinga Kristo (2:18-27)
   2:18-25 2:26-27

4. **Sifa za Ushirika (2:28–5:3)**
   a. Usafi katika Mitazamo Yetu (2:28–3:3)
      2:28-29 3:1-3
   b. Utendaji wa Haki kwa Mtazamo wa Kifo cha Kristo (3:4-24)
      3:4-10 3:13-22
      3:11-12 3:23-24
   c. Kumjaribu Roho Mtakatifu (4:1-6)
      4:1-3 4:4-6
   d. Kielelezo cha Ushirika Kupendana kama Kristo Aalivyotupenda (4:7–5:4)
      4:7-14 4:15-21 5:1-4

5. **Matokeo ya Ushirika (5:5-21)**
   a. Ushindi Dhidi ya Dunia (5:5)
   b. Kuthibitisha Madai ya Kristo (5:6-12)
   c. Kuthibitisha Wokovu wa Waumini (5:13)
   d. Kuthibitisha Majibu ya Maombi (5:14-17)
   e. Ushindi wa Dhambi (5:18-21)

# Waraka wa Pili wa Yohana

## (Kristo: Mungu katika Mwili)

**Jina na Mwandishi wa Kitabu:** Japo hakutajwa lakini mwandishi ni Yohana mtume, amejitaja yeye mwenyewe kama "Mzee," inayotupa kutulia na kukubali kwamba yeye ndiye mwandishi wa injili ya Yohana na 1 Yohana. Na huu ndiyo utambulisho wa mwisho uliotumiwa na mwandishi wa 3 Yohana. Kwa kuwa amejitambulisha yeye kama "mzee," inaonekana kwamba alikuwa ni mtu anayejulikana na hata aliokuwa akiwaandikia walimfahamu. Hii ilikuwa ni heshima ya cheyo cha mzee lakini alikuwa anatumia maneno haya kwa kibinafsi kwa kuwa alikuwa anajulikana na wasomaji wake.

Kwa kuwa kinajisema chenyewe kwamba mwandishi ni Yohana. Kwa hiyo kilipewa jina la Waraka wa Pili wa Yohana, barua ilikuwa inawahusu ***"Mama mteule na watoto wake"*** (1:1, 4-5).

**Muda wa Kuandikwa: 85-90 B.K.** Ni vigumu kuipa wakati barua hii lakini mambo na matendo yaliyomo katika barua hii yanaonekana kuwa kiliandikwa wakati mmoja na waraka wa kwanza wa Yohana (B.K. 85-90). Na usawa ulioko hapo juu unathibitisha (tazama muda katika 1 Yohana).

**Nia na Makusudi:** Kusudi la 2 Yohana ni himizo la mtume kwamba wasomaji wake waendelee kutembea katika kweli ya mafundisho ya kitume na kulingana na amri (1:4-6). Kwa sababu ***"Kwa maana wadanganyifu wengi wametokea duniani wasiokiri ya kwamba Yesu Kristo yu aja katika mwili"*** (1:7), Yohana alikuwa anawaandikia ili kuwatahadharisha na wale walikuwa wanakataa kukaa katika mafundisho ya Yesu na walikuwa wakiipotosha ile kweli (1:9). Katika hii kuna makusudi mawili yanaonekana: (1) aliwaandikia wsomi wake ili kuwatahadharisha wasije kuipoteza ile tuzo yao (1:9) na (2) ili kuwapa maelekezo mazuri katika miji zao na hata kanisa na kuwapa salamu za Kikristo. Yohana hakutaka wajulikane katika makanisa yao ya nyumbani na watambulikane kama walimu wa ukweli. Yohana hakuwaeleza wawe wavunja sheria au wasiwashuhudie.

**Mwonekano wa Yesu katika 2 Yohana:** Kama katika 1 Yohana, 2 Yohana inahusika na kuwatahadharisha na mafundisho ya kimwili. Aliandika kuthibitisha uongo kwa wale waliokuwa wanakana kwamba Yesu alikuja katika mwili.

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Salamu (1:1-3)**

2. **Uthibitisho wa Kutembea katika Kweli (1:4)**

3. **Amri ya kuendelea Kuwapenda Wengine (1:5-6)**

4. **Tahadhari na Melekezo Dhidi ya Walimu wa Uongo (1:7-11)**

5. **Hitimisho na Salamu za Mwisho (1:12-13)**

# Waraka wa Tatu wa Yohana
### (Kristo: Jina)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Mtume Paulo ndiye mwandishi wa kitabu hiki. Katika 2 Yohana na 3 Yohana mwandishi anajitambulisha yeye mwenyewe kama "mzee." Na uelewe maneno yanayofana katika nyaraka zote mbili "upendo katika kweli" (1:1 barua zote mbili) na "kutembea katika kweli" (1:4 na barua zote mbili).

Hii inaonyesha wazi kuwa ni barua ya mtume Yohana aliyoiandika kwa "mpendwa Gayo" (1:1) kuhusiana na matatizo ya kanisa ambayo Gayo alikuwa akikabiliana nayo. Mhusika anaeleweka kwa sababu anajulikana na wale wa kanisa la Asia ndogo ambako Yohana alitumika kwa miaka ya mwisho ya maisha yake. Gayo ni jina linalojulikana katika Agano Jipya. Jina linaloonekana katika Warumi 16:23 (Gayo wa Korintho), Matendo 19:29 (Gayo wa Makedonia) na Matendo 20:4 (Gayo wa Derbe), lakini hakuna mahusiano yoyote yaliyopo kati ya watu hawa na Yohana.

**Muda wa Kuandikwa: 85-90 B.K.** Kufanana kwa 1 Yohana na 2 Yohana tena kunaashiria nyakati sawa na 3 Yohana, miaka kati ya 85-90 B.K.

**Nia na Makusudi:** Yohana anamwandikia Gayo akimueleza kuhusiana na ukarimu na msaada wa kimwili kwa watumishi waliokuwa wakisafiri (wamisionari) hasa walipokuwa ni wageni. Kusudi ni kati ya huduma ya Gayo na upendo wake wa Kikristo uliokuwa ukieleza na kuonesha kama mmoja wa wale waliokuwa wakitembea katika kweli na ubinafsi wa Diotrephe ambaye badala ya kutembea katika kweli alikataa yale Yohana aliyoyasema na alikuwa akitaka matakwa yake mwenyewe (1:9).

Zipo sababu mbalimbali katika waraka huu: (1) kumlazisha Gayo (1:1-6a), (2) kueleza na kumtia moyo kwa msaada wake aliokuwa akiufanya kwa watumishi waliokuwa wakitumwa na Yohana (1:6b-8), (3) kumkemea Diotrephe kwa tabia yake ya ubinafsi (1:9-11), (4) kutoa maelekezo kwa Demetrio (1:12), and (5) kumtaarifu Gayo shauku ya Yohana na kusudi la kumtembelea na kuhusika na matatizo (1:10a, 13-14).

**Mwonekano wa Yesu katika 3 Yohana:** Kwa kuwa jina la Yesu halijatajwa moja kwa moja lakini anaonekana katika maelezo, ***"Waliaibishwa kwa jina hilo.'"*** Bila shaka hii inahusika na huduma ya Bwana Yesu (Matendo 5:40-41 ambapo tuna neno la kufanana katika kiyunani lililo katika 5:41). Paulo alitumia neno sawa katika Warumi 1:5. katika 1 Yohana 2:12, Yohana aliandika, ***"Kwa sababu dhambi zenu zimesamehewa kwa ajiri ya jina lake."*** Injili ya Yohana pia ina neno sawa linalotufanya tuamini ***"katika jina la Yesu"*** (Yohana 1:12, 3:18).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Salamu au Utangulizi (1:1)**

2. **Amri ya Gayo (1:2-8)**
    a. Utu Wake (1:2-4)
    b. Asili Yake (1:5-8)

3. **Hukumu ya Diotrephe (1:9-11)**
    a. Ubinafsi Wake (1:9)
    b. Kazi zake za Binafsi (1:10-11)

4. **Maneno ya Demetrio (1:12)**

5. **Maoni ya Mwisho (1:13-14)**

# Yuda
### (Kristo: Usalama wa Mwanadamu)

**Mtunzi na Jina la Kitabu:** Mwandishi anajitambulisha mwenyewe kuwa ni Yuda (1:1). Kwa Kiyunani ni Yuda tu. Kwa asili Kiingereza imetofautishwa kidogo na yule Yuda aliyemsaliti Yesu. Mwandishi anajitambulisha kwamba ni ndugu yake na Yakobo na mtumishi wa karibu na Yesu anaonyeshwa kama ndugu wa karibu na Yesu katika Mathayo 13:55 na Marko 6:3.

Itasaidia tukielewa kwamba :

> Japo Yuda alikuwa ni ndugu wa Karibu wa Yesu lakini alifuatana na Yakobo ndugu yake kabisa. Kwa mara ya kwanza kujiita yeye mwenyewe mtumwa wa Yesu ni wazi kwamba hataki watu wamhesabu vingine. Kwa muda huo huo amejitambulisha yeye mwenyewe. Kwa kuwa Yuda lilikuwa ni jina la kawaida katika karne ya kwanza (wanafunzi wawili wa Yesu waliitwa akiwemo na msaliti wake), kulihitajika habari nyingi ili kuthibitisha kwamba alikuwa ndugu yake na Yakobo.[96]

Yuda anahusika na wakristo wote na si kundi fulani tu la watu. Na kwa hiyo waraka huu unaelekezwa kwa ***"kwa hao walioitwa Waliopenda katika Mungu Baba na kuhifadhiwa kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo"*** (1:1). Na baadaye anawaita "wapendwa" au "rafiki wapenzi" (1:3).

**Muda wa Kuandikwa: 70-80 B.K.** Japo lengo ni sawa na la 2 Petro lakini utofauti mkubwa uliopo kati ya Yuda na 2 Petro ni kwamba kipindi Petro anatahadharisha kwamba "kuna walimu wa uongo" (2 Peter 2:1), Yuda anaeleza kwamba "Kuna watu waliojificha kati yenu" (1:4). 2 Petro anaonyesha matatizo na Yuda anaongelea kwamba sasa yapo, na Yuda aliandika baada ya 2 Petro. Kama Yuda iliandika 7-68 B.K., hivyo Yuda inaweza kuwa ni miaka ya 70-80 B.K.

**Nia na Makusudi:** Yuda alikusudia kuandika kuhusu wokovu wetu, lakini kwa sababu ya maasi na hatari ya kulihofisha kanisa badala yake alikuwa akilazimika kuwatia Moyo waumini ili awaepushe na imani dhidi ya mafundisho ya uongo ambayo kwa siri yalikuwa yameanza kuingia katika kanisa kwa upotofu mkubwa. "Gnostics" inaagalia kila kitu cha kimwili kama uovu na vitu vya kiroho kama vizuri. Kwa hiyo walikuwa na juhudi katika maisha yao ya Kiroho na kuiacha miili yao itende inavyotaka na matokeo yake yalikuwa ni kujisikia kushitakiwa katika kila namna ya sheria.[97]

Kulingana na hili mambo mawili makubwa tunayaona katika Yuda: (1) Kuhukumu matendo ya uasherati yaliyokuwa yakiharibu kanisa na kuwaangusha waumini na (2) aliwashauri wasimame imara, ili waendelee kukua katika imani wakidumu katika ukweli wa mitume uliokuwa ukifundishwa katika kanisa.

**Mwonekano wa Yesu katika Yuda:** Yuda inalenga katika usalama wa muumini katika Kristo (1:24), katika maisha ya milele yeye hutoa (1:21) na kwa uhakika atarudi tena (1:21). Ni Yesu Kristo atupaye kushinda katika uwepo wa Mungu (1:25).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Salamu na Makusudi (1:1-4)**

2. **Maelezo na Tahadhari ya Walimu wa Uongo (1:5-16)**
   a. Hukumu Iliyopita. (1:5-7)
   b. Sifa Zao za Sasa (1:8-13)
   c. Hukumu Ijayo (1:14-16)

3. **Tahadhari na Ushauri kwa Waumini (1:17-23)**

4. **Baraka (1:24-25)**

# Sehemu ya 4
# Kitabu cha Unabii

## Ufunuo
### (Kristo: Atakayerudi Tena)

**Utangulizi:** Katika kitabu cha ufunuo tunayo hatima na ukamilifu wa Biblia kwa ufunuo wa Mungu kwa wanadamu. Kama vile Mwanzo kilivyo ni kitabu cha kwanza, ufunuo ni kitabu cha mwisho. Kinaeleza nyakati za mwisho, kurudi kwa Bwana, utawala wake wa mwisho na uzima wa milele. Mtu anapokua anasoma katika Biblia mambo mengi na makusudi mbalimbali yameelezwa na yameanishwa kama vile; Mbingu na dunia, dhambi, huzuni na laana, mwanadamu na wokovu, shetani, kuangushwa na hukumu yake, Israeli, uteuzi wake, baraka, nidhamu, taifa, Babeli na wababeli,na falme za ufalme. Kwa undani zaidi haya yote yanaonekana mwisho wake katika kitabu cha ufunuo. Injili na nyaraka zinaanza kuonyesha haya lakini tunapokuja katika ufunuo tunaona mwisho wake.

Tunaweza kuonesha kama ifuatavyo:

**Ufunuo: Ukamilifu wa Biblia**

| Agano la Kale na Jipya | |
|---|---|
| Mbingu na Jehanamu →<br>Mtu – uumbaji, anguko, wokovu →<br>Dhambi – chanzo, laana, huzuni →<br>Shetani – sifa zake, anguko, kuangamizwa →<br>Mataifa – kutotii, dini →<br>Israeli – uteuzi, baraka, kutii →<br>Mwokozi Sliyeahidiwa – kazi, utawala →<br>Ufalme – ahadi, mipango → | Kitabu cha Ufunuo |

**Mwandishi na Jina la Kitabu:** Kulingana na kitabu chenyewe jina la mwandishi ni Yohana (1:4, 9; 22:8). Alikuwa ni nabii (22:9) na mwandishi aliyekuwa anajulikana na makanisa ya Asia ndogo ambako ndiko alikokuwa akiwaandikia kitabu cha ufunuo (1:4).

Kwa desturi Yohana alitambulikana kama Mtume mmoja wa wanafunzi wa Yesu. Uandishi wake unatofautiana na injili ambao unaonyesha unabii wa kitabu hiki.

**Muda wa Kuandikwa: 96 B.K.** Domitian alitawala Rumi tangu 81-96 B.K. na Irenaeus anatuambia kwamba Yohana aliandika kutoka Patmo wakati wa utawala wa Domitian, kwa kuwa hii imethibitishwa na watu wa makanisa ya kwanza kama vile Alexander na Eusebius, wasomi wengi wanaamini kwamba kitabu kiliandikwa kati ya B.K. 81-96. Na hiki ndicho kitabu cha mwisho cha Agano la Jipya muda mfupi baada ya injili ya Yohana na nyaraka (1, 2, na 3 Yohana).

**Nia na Makusudi:** Katika Ufunuo nia na mkusudi inahusika na migogoro na uovu kwa mfano wa majukumu ya wanadamu yaliyowezeshwa na Ibilisi na mifumo yake ya kiulimwengu na ushindi wa shangwe wa Bwana dhidi ya adui hawa ili aweke ufalme wake katika maiaka elfu (miaka 1,000 ya Ufunuo 20) na ufalme wake wa milele.

Hii inakamilishwa na kumchukua msomaji na msikiaji (1:3) kwa njia ya maono yaliyotolewa na Yohana kueleza asili ya ibilisi na chanzo cha maovu duniani. Ufunuo inaeleza nguvu ya utawala iliyo katika Simba wa kabila la Yuda, uzao wa Daudi. Simba huyu pia ni mwanakondoo kama ilivyo katika machinjioni lakini yu hai kabisa na analeta hukumu ya Mungu wa furaha dhidi ya uasi na dhambi za uliwengu.

Kuna watu mbalimbali katika kitabu hiki kulingana na walivyotenda. Hawa kwanza ni Yesu, halafu Yohana mwandishi, halafu mashahidi wawili, mnyama dubu na manabii wa uongo na mwisho ni Bibi harusi ajaye na Bwana.

**Mwonekano wa Yesu katika Ufunuo:** Ufunuo ni kitabu cha "Ufunuo wa Bwana Yesu Kristo" kinaeleza utukufu wake, hekima na nguvu (1:1-20), mamlaka yake katika kanisa (2:1–3:22) nguvu na haki ya kuuhukumu ulimwengu (5:1–19:21). Kama ufunuo wa Kristo una maelezo mengi. Kinaeleza juu ya Yesu Kristo (1:1) kama Shahidi mwaminifu, mzaliwa wa kwanza aliyefufuka. Mtawala wa wakuu wa ulimwengu huu (1:5), Mwanzo na Mwisho (1:17), Anayeishi (1:18), Mwana wa Mungu (2:18), Mtakatifu wa Kweli (3:7), ni Amina, Mwaminifu na Shahidi wa Kweli, Mwanzo wa Uumbaji wa Mungu (3:14), Simba wa Kabila la Yuda, Uzao wa Daudi (5:5), Mwanakondoo (5:6), Mwaminifu na wa Kweli (19:11), Neno la Mungu (19:13), MFLME WA WAFALME, BWANA WA MABWANA (19:16), Alpha na Omega (22:13), Nyota ya Asubuhi (22:16), na Bwana Yesu Kristo (22:21).

## Kwa Masomo Binafsi: Eleza

1. **Utangulizi (1:1-8)**
   1:1-3 | 1:4-8

2. **Mambo Yaliyopita (1:9-20)**
   1:9-11 | 1:12-16 | 1:17-20

3. **Mambo Yaliyopo (2–3)**
   a. Ujumbe wa Waefeso (2:1-7)
   b. Ujumbe kwa Smirna (2:8-11)
   c. Ujumbe kwa Pergamo (2:12-17)
   d. Ujumbe kwa Thiatira (2:18-29)
   e. Ujumbe kwa Sardi (3:1-6)
   f. Ujumbe kwa Philadelfia (3:7-13)
   g. Ujumbe kwa Laodikia (3:14-22)

4. **Mambo Yajayo (4:1–22:5)**
   a. Kipindi cha Dhiki Kuu (4:1–19:21)
      1) Kiti cha Enzi Mbinguni (4:1-11)
         4:1-4 | 4:5-11
      2) Vitabu Saba Vilivyotiwa Muhuri na Simba Ambaye Pia ni Mwana Kondoo (5:1-14)
         5:1-5 | 5:6-10 | 5:11-14
      3) Hukumu (6:1-17)
         6:1-2 | 6:5-6 | 6:9-11
         6:3-4 | 6:7-8 | 6:12-17
      4) Mapumziko: Satakaookoka na Dhiki Kuu (7:1-17)
         7:1-3 | 7:9-12
         7:4-8 | 7:13-17
      5) Tarumbeta Nne za Hukumu (8:1-13)
         8:1-2 | 8:8-9 | 8:13
         8:3-5 | 8:10-11
         8:6-7 | 8:12
      6) Tarmbeta ya Tano Nay a Sita na Ole Mbili (9:1-21)
         9:1-6 | 9:12 | 9:20-21
         9:7-11 | 9:13-19
      7) Malaika na Kitabu Kidogo (10:1-11)
         10:1-7 | 10:8-11
      8) Hekalu, Mashahidi Wawili na Tarumbeta ya Saba (11:1-19)
         11:1-6 | 11:11-13 | 11:15-18
         11:7-10 | 11:14 | 11:19
      9) Migogoro ya Malaika (12:1-17)
         12:1-2 | 12:5-6 | 12:10-12
         12:3-4 | 12:7-9 | 12:13-17
      10) Manyama na Manabii wa Uongo (13:1-18)
         13:1-6 | 13:7-10 | 13:11-18
      11) Matangazo Maalumu (14:1-20)
         14:1-5 | 14:9-12 | 14:17-20
         14:6-7 | 14:13
         14:8 | 14:14-16
      12) Makanisa Saba (15:1-8)
         15:1 | 15:2-4 | 15:5-8

13) Hukumu (16:1-21)
    - 16:1
    - 16:2
    - 16:3
    - 16:4-7
    - 16:8-9
    - 16:10-11
    - 16:12
    - 16:13-16
    - 16:17-21

14) Hukumu ya Wanadini wa Babeli (17:1-18)
    - 17:1-7
    - 17:8-14
    - 17:15-18

15) Hukumu ya Babeli ya Biashara (18:1-24)
    - 18:1-3
    - 18:4-8
    - 18:9-10
    - 18:11-20
    - 18:21-24

16) Kuja kwa Yesu Mara ya Pili (19:1-21)
    - 19:1-4
    - 19:5-6
    - 19:7-8
    - 19:9-10
    - 19:11-16
    - 19:17-18
    - 19:19-21

b. Utawala wa Yesu ( Miaka Elfu) na Kiti cha Rnzi Kikubwa Cheupe (20:1-15)
1) Kufungwa kwa Shetani (20:1-3)
2) Ufufuo wa Watakatifu (20:4-6)
3) Watenda Dhambi katika Uasi (20:7-9)
4) Kuangamizwa kwa Shetani (20:10)
5) Hukumu ya Wenye Dhambi (20:11-15)

c. Maisha ya Milele (21:1–22:5)
1) Kushuka kwa Yerusalemu Mpya (21:1-8)
    - 21:1-4
    - 21:5-8

2) Maelezo ya Yerusalemu Mpya (21:9-27)
    - 21:9-14
    - 21:15-21
    - 21:22-27

3) Zuri wa Yerusalem Mpya (22:1-5)

d. Mwisho (22:6-21)
- 22:6
- 22:7
- 22:8-9
- 22:10-11
- 22:12-13
- 22:14-15
- 22:16
- 22:17
- 22:18-19
- 22:20
- 22:21

## Sura ya 4

# Kanuni Muhimu za Ufasi

# Utangulizi

Sura ya nne imekusudiwa kumwezesha Msomaji kujua sheria nne na kanuni kumi na tano za ufasiri. Katika sura hii sheria maana yake ni kitu kilichowekwa na kinapaswa kuangaliwa na kufuatwa muda wote wakati tunaposoma neno la Mungu. Kanuni ni mwongozo unaopatikana katika sheria lakini si kwamba ufuatwe wakati wote. Tunapoendelea na sura hii mwanafunzi ataelewa ni kwa jinsi gani na wakati gani anapoweza kutumia kanuni hizi.

Tafasiri sahihi ya Neno la Mungu ni mlolongo mkubwa unaopaswa kufuatiliwa.Ni vigumu kwa mtu kufungua Biblia halafu akasoma na kuelewa hapo hapo inamaanisha nini. Na msomaji hatakiwi kukata tamaa ya kuyachunguza maneno ya Mungu kwa sababu Mungu kaweka maneno magumu katika neno lake kwa makusudi maalumu ili tuhitaji msaada wa Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 3:10-16). Japo kweli kuna sehemu zingine waweza kuelewa lakini kweli zingine ni vigumu sana (1 Wakorintho 13:12).

Kama neno la Mungu lingeweza kufafanuliwa kirahisi basi hata wasioamini wangeweza kujua nini kilicho katika Biblia. Huu ugumu kaweka Mungu ili wanaomfuata wapate kumtafuta na kuyachunguza maandiko yake ili waendelee kujengwa na kukua (2 Timotheo 2:15). Tafadhari tumia sheria hizi na kanuni hizi kama mwongozo wako lakini mtegemee Roho Mtakatifu akuongoze katika ukweli (Yohana 16:13).

Ufuatao ni muhitasari wa sheria na kanuni tunapotaka kujifunza neno la Mungu.

**Sheria ya Kwanza: Tafuta Kupata Ukweli Kuhusu Mungu na Kristo kwa Kusoma Maandiko Yote**

A. Kanuni ya 1: Jifunze asili ya Mungu
B. Kanuni ya 2: Tafuta njia ambayo Yesu anavyofunuliwa

**Sheria ya Pili: Tafuta Kuelewa Ukweli kwa Kutumia Sura Mbalimbali kama Mwongozo Wako**

A. Kanuni ya 3: Tambua kuwa ufunuo ni kitu kisicho na mwisho
B . Kanuni ya 4: Fasiri kwa njia ya maandiko
C. Kanuni ya 5: Chunguza mambo maalumu
D. Kanuni ya 6: Soma sura muhimu.
E. Kanuni ya 7: Tambua haki ya mwanadamu
F. Kanuni ya 8: Kumbuka Maagano.

**Sheria ya Tatu: Kuwa Mwenye Hekima kwa Kuyalinganisha Maandiko**

A. Kanuni ya 9: Tafuta tofauti.
B. Kanuni ya 10: Chunguza yaliyomo.
C. Kanuni ya 11: Fasiri kwa kulinganisha maandiko.
D. Kanuni ya 12: Tafuta mwafaka
E. Kanuni ya 13: Fikiria mpango wa Mungu
F. Kanuni ya 14: Kuwa makini na unabii

**Sheria ya Nne: Tafuta Jinsi ya Kuishi Maisha ya Kikristo kwa Kutumia Neno la Mungu**

A. Kanuni ya 15: Matumizi mazuri hujengwa juu ya tafasiri nzuri.
B. Hatua tano za matumizi mazuri
C. Vipingamizi sita vya tafasiri nzuri
D. Njia nane za kushindwa kutumia matumizi

# Sehemu ya 1
# Sheria ya Kwanza

**Tafuta Kupata Ukweli Juu ya Mungu na Yesu Kristo kwa Kusoma Maandiko**

Sheria inatambulisha asili na sifa za Mungu, na hii inajulikana kama Matokeo yake Mungu. Hivyo ni muhimu kuyachunguza maandiko na kuyafafanua ili kujua. Mwanzo wake Mungu haujulikani. Na hii sheria inaonyesha kuwa kadri tunavyojua ndivyo kadri tunavyojua asili ya Mungu (Wafilipi 3:10), na si hivyo tu kadri tunavyochunguza na kuyatafasiri maandiko ndivyo Mungu atakavyosema na sisi.

Ukweli ni kwamba "utatu mtakatfu" Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, wote ni kitu kimoja kwa uthibitisho wa utatu mtakatifu wa Mungu. Neno "UTATU" inaonesha kuwa Baba; Mwana na Roho Mtakatifu ni nafsi tatu katika Mungu mmoja. Hawa wana mambo makuu matatu. Baba ni mpangaji wa yote (Matendo 2:23) Mwana ni wakala (Yohana 5:36) na Roho Mtakatifu ndiye anayetufunulia (Yohana 16:13). Wakati tunajifunza majukumu yao hatupaswi kuwagawa. Kuna Mungu mmoja (Kumb. 6:4). Kwa kuwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu wanakuwa na sifa moja ambazo ndizo za Mungu hivyo wote ni Mungu mmoja.

Tutaona utatu huu baadaye kwa undani zaidi katika sehemu zijazo.

**A. Kanuni ya Kwanza: Jifunze Aasili ya Mungu**

Kuna sifa kumi muhimu ambazo Mungu anazo. Zinapaswa kukumbukwa na kuangaliwa sana.

1. **Mamlaka**
   Mungu ni MAMLAKA. Hii ina maana ya kwamba ni mfalme na anatenda kama anavyoona yeye. Mamlaka ni kile kitendo cha kuwa na madaraka ya juu kabisa katika mambo fulani. Hivyo Mungu hana mpaka kwa sababu ana mamlaka juu ya vitu vyote alivyoviumba. Yeye ni muumbaji wala hakuumbwa (Warumi 1:20, 25). Kwa hiyo ana uwezo wa kuanzisha mipango yake yeye mwenyewe, sheria zake na hata hukumu. Kwa ufupi anafanya kama apendavyo japo kwa kweli sisi ni vigumu sana kuelewa.

2. **Haki**
   Mungu ni HAKI na hii ina maana kuwa yeye ni mkamilifu na hana upendeleo. Yeye ndiye kiwango halisi cha haki. Ni mkamilifu na hutengeneza vitu kwa ajiri yetu kwa kiwango chake (Waefeso 5:1).

3. **Mwaminifu**
   Mungu ni MWAMINIFU na hii inamaana kuwa yeye ni wa kweli katika kufanya wala hana upendeleo (Warumi 2:11), habagui. Palipo na dhambi (uvunjaji wa sheria zake) Warumi 5:13 Haki yake kutimiza.

4. **Upendo**
   Mungu ni UPENDO, ikiwa na maana kuwa upendo wa Mungu haufananishwi na kitu chochote. Upendo una maana ya kufanya yaliyo sawa na wanayoyapenda na wengine. Na Wakristo wanapaswa kuufuata upendo wa Mungu na kuuonyesha kwa wengine ili kwamba watu wamjue Mungu (Yohana 13:34-35).

5. **Uzima wa Milele**
   Mungu ni UZIMA WA MILELE. Yeye amekuwepo na atazidi kuwepo. Na uzima wa milele hauna mwanzo wala mwisho. Na sisi kama wakristo tuna uzima wa milele ulio na mwanzo lakini hauna mwisho. Uzima wa milele wa Mungu unatufundisha kuwa Yeye hafi.

6. **Ni mwenye Nguvu (Omnipotent)**
   Mungu ni nguvu au "OMNIPOTENT", ikiwa na maana kuwa ana uwezo wa kufanya kila kitu. Na mfano wake kwa hili ni kwamba aliumba mbingu na nchi (Mwanzo 1:1). Tunaelezwa kuwa "neno la kinywa chake" liliumba mbingu na pumzi yake vitu vyote (Zaburi 33:6).

7. **Yu mahali Pote (Omnipresent)**
   Mungu ni mahali pote au "OMNIPRESENT," ina maana kuwa yuko kila sehemu kwa wakati mmoja. Na hii haina maana kuwa Mungu ni kila kitu unachokiona (Pantheism), lakini yuko mahali pote. Na hii inatupa fikira za uasili wake Mungu.

8. **Anajua Yote (Omniscient)**
   Mungu anajua yote au "OMNISCIENT," Anajua yaliyopita yaliyopo na yajayo. Na Mungu anajua asili ya kila kitu si asili tu ila hata uwezo wake. Anajua madhara yake kwa wakati wote ambayo kila kitu kitapata kupitia maamuzi yake. Mpango wake wa milele umezingatia vigezo vyote.(Warumi 8:28-30).

9. **Habadiliki (Immutable)**
   Mungu HABADILIKI ina maana kuwa yeye ni yule yule jana na leo na hata milele, yaani IMMUTABLE.

10. **Kweli**
    Mungu ni KWELI. Sifa hii inatueleza kuwa kila alichokisema Mungu ni kweli na kinaaminika (Hesabu 23:19). Mungu kamwe hadanganyi (Tito 1:2).

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 1A

1. **Kariri sifa kumi za Mungu zilizotolewa.**

2. **Soma Zaburi 11 na orodhesha sifa nyingi za Mungu kwa kadri unavyoweza.**

**B. Kanuni ya Pili: Tafuta Njia Jinsi Yesu Anavyofunuliwa**

Kanuni ya pili inaonesha kuwa historia yote inamhusu Yesu. Na inatudhihirishia kuwa Yesu ni Muumbaji (Yohana 1:1, 3, 14; Wakolosai 1:16-17), yeye ni Alpha na Omega “mwanzo na mwisho” (Ufunuo 1:8), ni mmoja na Mungu ndiye aliyefanyika mtu (Wafilipi 2:6-8).

Tunapotaka kuelewa neno la Mungu tunapaswa kuelewa kuwa ni kwa jinsi gani ufasiri wetu wa neno tulilopewa unazungumza juu ya kweli ya Bwana Yesu Kristo. Njia moja ya kuelewa ni kuwa mtu, sehemu, kitu au jambo lolote lilo katika Biblia linamhusu Yesu. Tunapaswa kujifunza na kutafuta “vitu vizuri” vya kweli juu ya Kristo. Na si kuangalia tu katika sheria za kale ambazo kwa kweli ni kama kivuli cha mambo mazuri (Waebrania 10:1; Yohana 14:6). Watu wote, sehemu zote na vitu vyote viliwekwa kama mfano wa Yesu ili kutusaidia kuelewa na kumjua yeye (1 Wakorintho 10:1-6).

Mfano wa ***mtu*** anayetufunza kama Kristo katika vitabu vya Manabii ni Yona. Kama unakumbuka Yona hakutaka kwenda Ashuru (Ninawi) kama alivyoamriwa na Mungu matokeo yake akataka kwenda sehemu nyingine. Upepo mkali ulitokea na alitupwa Baharini na akamewa na samaki na baada ya siku tatu alitapikwa na yule samaki ufukweni mwa Ashuru na hapo ndipo alipoamua kutii na kufanya kama Bwana alivyo muagiza. Siku tatu zinakuja kuwa “ishara ya Nabii Yona” (Mathayo 12:39-40), zilizoashiria kukaa kwa Yesu Kristo kaburini siku tatu.

***Sehemu*** inatufundisha pia juu ya Yesu inatuonyesha juu ya Kristo. Yesu alitakiwa azaliwe Bethelehemu (Mika 5:2) ikiwa na maana “nyumba ya mikate” Yesu alikuwa mkate ambao ulishuka toka mbinguni na kama mwanadamu atakayewapa watu maisha ya kiroho (Yohana 6:35).

Sehemu pia inatufundisha kuhusu Bwana. Hekalu na hema pia vinaingia katika sehemu hii. Kama tutafikiri juu ya sehemu takatifu katika hekalu ile ya mwanakondoo, sehemu ya kutubia na hata ile madhabahu, vyote vinamwakilisha Yesu. Yeye ni mkate(Yohana 6:35). Yeye pia ni nuru ya watu (Yohana 8:12) na ndiye pekee anayesikia maombi yetu ( ufunuo 8:3-4) na maombi ni dhabihu. Waebrania 13:15-16).

***Matukio*** kama dhabihu iliyofanywa na Walawi pia zinatufundisha juu ya Kristo. Sadaka zote zilizoelezwa katika Mambo ya Walawi 1-7 zilikuwa zinatuonyesha juu ya Yesu kama sadaka ya mara moja (Waebrania 10:10-12). Kweli alikuwa ni ***“Mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu”*** (Yohana 1:29).

Wanafunzi pia wanaweza kutazama katika kusudi la kila kitabu katika Biblia na kuona kwamba Yesu ni mzungumziwaji katika kila kitabu.[98]

| | |
|---|---|
| Mwanzo: | Muumbaji na Uzao ya Mwanamke (1:1; 3:15) |
| Kutoka: | Mwanakondoo wa Mungu (12:1-13) |
| Mambo ya Walawi: | Kuhani Mkuu |
| Hesabu : | Nyota ya Yakobo (24:17) |
| Kumbukumbu la Torati: | Nabii kama Musa (18:15) |
| Yoshua: | Kapteni (5:13-15) |
| Waamuzi: | Mwamuzi (11:27) |
| Ruthu: | Mpatanishi na Mkombozi wa Mwanadamu (Ch. 3) |
| Samweli: | Bwana wa Wafalme (2 Samweli 7:18-20) |
| Wafalme/Nyakati: | Bwana wa Mbingu na Nchi (Vitabu) |
| Ezra: | Mrejeshaji (1:1) |
| Nehemia: | Mwaminifu (9:32) |
| Estha: | Mordekai (Ch. 10) |
| Ayubu: | Mwokozi Aliyeinuliwa na Kuletwa (19:25) |

| | |
|---|---|
| Zaburi: | Mbarikiwa Kati ya (1) |
| | Mwana wa Mungu Kati ya (2) |
| | Aliyesulubiwa Kati ya (22) |
| | Aliyefufuka Kati ya (23) |
| | Aliye kuja Kati ya (24) |
| | Mtawala Kati ya (72) |
| | Kiongozi wa Sifa (150) |
| Mithali: | Hekima (sura ya 4) |
| Muhubiri: | Mwenye Hekima Aliyesahaulika (9:14-15) |
| Wimbo ulio Bora: | Mpendwa Wangu (2:16) |
| Isaya: | Mateso (53) |
| Yeremia: | Bwana Mwenye Haki (23:6) |
| Maombolezo: | Mtu wa Huzuni (1:12-18) |
| Ezekieli: | Kiti cha Enzi (1:26) |
| Danieli: | Jiwe lililogawanyika (2:34) |
| Hosea: | Daudi Mfalme Mkuu (3:5) |
| Yoeli: | Bwana wa Ukarimu (2:18-19) |
| Amosi: | Mwokozi wa Isareli (3:12) |
| Obadia: | Mwokozi dhidi ya Mlima Sayuni (V17) |
| Yona: | Mwokozi Aliye Zikwa na Kufufuka (kitabu kizima) |
| Mika: | Mungu wa Milele (5:2) |
| Nahumu: | Ujasiri (1:7) |
| Habakuki: | Nguzo ya Imani (2:4) |
| Zephaniah: | Wakati wa Hukumu na Kutakaswa (3:5,15) |
| Hagai: | Mwanakondoo wa Kweli (2:17) |
| Zekaria: | Tawi (3:8) |
| Malaki: | Jua la Neema (4:2) |
| | |
| Mathayo: | Mfalme wa Wayahudi (2:1) |
| Marko: | Mtumishi wa Yehova (kitabu chote) |
| Luka: | Mwana Mkamilifu (3:38; 4:1-13) |
| Yohana: | Mwana wa Mungu (1:1) |
| Matendo: | Bwana Aliyepaa (1:8-9) |
| Warumi: | Haki (3:22) |
| 1 Wakorintho: | Matunda ya Kwanza Kutoka Wafu (15:20) |
| 2 wakorintho: | Alifanywa Dhambi kwa Ajili Yetu (5:21) |
| Wagalatia: | Mwisho wa Sheria (3:10,13) |
| Waefeso: | Mlinzi Wetu (6:11-18) |
| Wafilipi: | Mtoa Mahitaji Yetu (4:19) |
| Waefeso: | Mshindi (1:18) |
| 1 Wathesalonike: | Bwana Atakayerudi (4:15-18) |
| 2 Wathesalonike: | Mwamuzi wa Ulimwengu (1:7-9) |
| 1 Timotheo: | Mpatanishi (2:5) |
| 2 Timotheo: | Mpakwa Mafuta (4:8) |
| Tito: | Mungu Mkuu (2:13) |
| Philimoni: | Mfungwa (1:9) |
| Waebrania: | Mwingi wa Imani na Mtoshelezaji (9-11) |
| Yakobo: | Bwana wa Sabato (5:4) |
| 1 Petro: | Nia na Makusudi ya Unabii wa Agano la Kale (1:10-11) |
| 2 Petro: | Mwokozi Aliyeteseka (3:9) |
| 1 Yohana: | Neno la Uzima (1:1) |
| 2 Yohana: | Mlengwa Mpinga Kristo (1:7) |
| 3 Yohana: | Mwaminifu na Mkweli (1:3-4) |
| Yuda: | Usalama wa Waamini (1:24-25) |
| Ufunuo: | Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana (19:11-16) |

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 1B

1. **Soma Yohana 1:1, 3 na 14; Wakolosai 1:16-17; na Wafilipi 2:6-8. Yes Kristo ni nani?**

2. **Soma Waebrania 10:1-18 na Yohana 14:6. Ni kitu gani hakiwezi kusafisha dhambi? Onesha kitu halisi na kivuli.**

**3. Soma Mathayo 12:39-40 na Yona 1. Andika usawa wa Yona na Yesu Kristo.**

**4. Soma Mika 5:2 na Yohana 6:32-51. Sura hizi zinaonesha nini kuhusu Yesu?**

**5. Soma Kutoka 25:23-40, Yohana 6:35 na 8:12. Vitu vya hema vinaelezaje kuhusu Yesu Kristo?**

**6. Soma Mambo ya Walawi 3, Waebrania 10:10-12 na Yohana 1:29. Sadaka za Amani na Yesu Kristo zinawakilisha nini kwa kawaida?**

**7. Iangalie mistari hiyo inayoeleza juu ya Yesu na ione sura ya Yesu wewe mwenyewe inavyoonekana.**

# Sehemu ya 2
# Sheria ya Pili

**Sheria ya Pili: Tafuta Kuelewa Ukweli kwa Kutumia Sura Mbalimbali kama Mwongozo Wako**

Sheria hii inatufundisha kuyachunguza maandiko rahisi kuyaelewa na tuyaruhusu yatuongoze katika kuelewa kwetu kwa hata sura zilizo ngumu.

Tutajifunza kanuni sita zinazohusiana na sheria hii. Kanuni hizi zitamsaidia mwanafunzi kutathimini sura mbalimbali zilizo katika Maandiko.

Katika sehemu hii tutajifunza ukweli kuhusu ufunuo unaendelea na jinsi Mungu anavyopanua mahusiano yake . Ili kuona mipango hii ni lazima tufasiri kimaandiko kwa kuangalia mambo muhimu na kujifunza sura muhimu. Tutaona kuwa uovu wa mwanadamu unakoma kwa kuyachunguza lakini kwa njia ya ufasiri wa Mungu.

**A. Kanuni ya Tatu: Tambua Kuwa Ufunuo ni Kitu Kisicho na Mwisho**

Kanuni hii inatufundisha kuwa Mungu hujionyesha kwa vipindi. Kwa mfano unabii wa kwanza wa Masihi unaonekana katika Mwanzo 3:15 ni ahadi ya mbegu za mwanamke. Agano la Kale kwa uandishi wake wote linatupa habari za mbegu. Tunaambiwa kwamba Masihi atakuwa mbegu katika ukoo wa Ibrahimu (Mwanzo 12:3) mbegu ya Isaka (Mwazo 21:12), mbegu ya Yakobo (35:10-12). Wa kabila la Yuda (Mwanzo 49:8-11) wa ukoo wa Yese (Isaya 11:1), wa nyumba ya Daudi (2 Samweli 7:12-16), atazaliwa Bethelehemu (Mika 5:2) atakuwa Mungu na Mwanadamu (Zaburi 110:1). Ataitwa Emanueli (Isaya 7:14). Atakuwa nabii (Kumbukumbu la Torati 18:18), Kuhani (Zaburi 110:4) Mwamuzi (Isaya 33:22) na Mfalme (Yeremia 23:5) atakuwa Mpakwa mafuta wa Roho Mtakatifu (Isaya 11:2) na Moyo wa nyumba ya (Mungu 69:9).

Ufunuo uliopanuka kwa kipindi (kama hapo juu zinatengeneza kitu kinachoitwa "Ufunuo Unaoendelea." Unabii wote umefanyika na mambo muhimu yameonekana wazi.

Kwa hiyo inaleta maana kwa kuangalia katika mtazamo wa kwanza na inatulinda katika uelewa wetu juu ya matukio muhimu. Kwa mfano biashara na uasi wa shetani inaonekana kwanza katika Mwanzo 3:1. Tunapojifunza juu ya mwasi huyu tunapata kuelewa kuwa yeye ni mpinzani wa Mungu. Shetani haonekani kupata mabadiliko katika historia yote hii ya mwanadamu maana yeye ni mwasi (Ufunu 12:9; 20:2-3, 10). Yeye hubadili staili tu lakini mtazamo wake ni ule ule (Isaya 14:12-14; Ufunuo 12:9; 20:7-8), na hata matendo yake. Hii inaonyesha wazi kuwa Mtu asiyejua haki na sheria ya Mungu hupenda kujifanya kama Mungu (2 Wathesalonike 2:4).

Wakati mwingine tunaona kwamba ukweli wa dunia kuhusu kupata historia yake umefundishwa kwa mahusiano ya vitabu vya mwanzo kabisa. Hata hivyo masomo mbalimbali katika Biblia yameoneshwa katika kitabu cha mwanzo. Kwa hiyo masomo ya Biblia katika kitabu cha mwanzo ni muhimu sana kwa wale wanaotaka kujifunza neno la Mungu.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 2A

1. **Soma Mathayo 1:1-25, 2:1; 3:16; Yohana 1:1, 14; 2:17; 5:22; 7:40; Waebrania 5:9-10; na Ufunuo 19:16. Oanisha mistari ya kinabii na ilke mistari inyomwonesha akitimiliza unabii.**
   a. Uzao wa mwanamke–Mwanzo 3:15
   b. Uzao wa Abraham–Mwanzo 12:3
   c. Uzao wa Isaka–Mwanzo 21:12
   d. Zao wa Yakobo–Mwanzo 35:10-12
   e. Kabila la Yuda–Mwanzo 49:8-11
   f. Ukoo wa Yese–Isaya 11:1
   g. Nyumba ya Daudi –2 Samweli 7:12-16
   h. Alizaliwa Bethelehemu–Mika 5:2
   i. Mungu na mwanadamu – Zaburi 110:1
   j. Anaitwa Imaneli–Isaya 7:14
   k. Nabii –Kumbkumbu la Torati 18:18
   l. Kuhani–Zaburi 110:4
   m. Hakimu–Isaya 33:22
   n. Mfalme–Yeremia 23:5
   o. Makwa mafta maalum ya Roho Mtakatifu–Isaya 11:2
   p. Shauku kwa ajili ya nyumba ya Mungu–Zaburi 69:9

2. **Mistari hii inathibitisha nini?**

**B. Kanuni ya Nne: Fasiri kwa Njia ya Maandiko**

Kanuni inafundisha kuwa Mungu husema kile anachokikusudia na anachokikusudia husema. Ni kanuni ya muhimu sana kwa sababu inatulinda katika kuelewa kwetu maneno ya Mungu. Tunapokuwa tukiwaelekeza watoto wetu tunajaribu kuwasiliana nao kadri tuwezavyo ili wafanye yale tunayotaka sisi wafanye na kukumbuka. Mara kwa mara tutajadili vitu vingi katika njia mbalimbali ili kwamba kwa uelewa wao mdogo wapate kuyatunza na kuyashika (Waebrania 1:1). Na pia huwa tunawaeleza mara nyingi juu ya kitu kimoja. Je sisi si watoto wa Mungu (1 Yohana 3:1)? na yeye si baba yetu ("ABBA" katika warumi 8:15)? Ufasiri wa maandiko inamaana kuwa sisi (kama watoto wa Mungu) kwa kupitia maandiko tunapaswa kukubali yale Mungu anayotueleza kwa sababu ni ya kweli.

Ina leta maana kwa kuangalia kwanza katika maneno ya Mungu kwa urahisi kabisa, kiumakini, kwa uelewa na hata kwa kuangalia dunia yenyewe. Kwa kweli zile sura rahisi zitakuwa kivuli cha sura zilizo ngumu.

Mfano mmoja wa sura rahisi ni Yohana 3:16 inasema ***"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanae wa pekee ili kila mtu amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele."*** Hakuna neno linalo fafanua upendo wa Mungu. Moja kwa moja linaeleza upendo wa Mungu kwa ulimwengu na sasa inasema "Yeyote anaye amini" anao huo uzima. Kwa hiyo hapa hatuna haja ya kuhoji maana inajitosheleza.

Pia tunaona habari ya kufanana katika Warumi 3:23 inayosema ***"wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."*** Hali ya dhambi kwa mujibu wa Biblia imetawala maisha ya kila mwanadamu duniani kote isipokuwa haikumgusa Yesu peke yake (1 Petro 2:22). Biblia peke yake imeanzisha sheria kwa hiyo Biblia peke yake inaweza tena kuonesha hali ya kutoka katika sheria. Sisi kama wanafunzi hatuko katika mapinduzi ya kufanya chochote katika ulimwengu uliofanywa kwa sheria ya Mungu kupitia neno lake. Kwa hiyo ukimtoa Yesu sisi sote ni watenda dhambi.

Kwa kawaida Biblia ni pori na imefichika na iko ndani sana kama tulivyokwisha kusema tunapaswa kupokea kama ilivyo na si kuhoji. Neno "mythological" *Kuhoji* si zuri maana linatuondoa katika kuelewa maneno ya Mungu. Mungu amekuwa makini sana katika kutuonya sisi (Ufunuo 22:18-19) kwa njia ya maneno yake.

Biblia imewekwa katika maandishi ya kihistoria na hivyo ni muhimu sana kwa historia zote (1 Wakorintho 15). Kushindwa kufikiri vizuri juu ya uandishi wa Biblia kumepelekea kuwa na theologia nyingi potofu katika sehemu zote za historia ya Waisraeli na kanisa.

Mifano mingine ya maneno yanayoihusu dunia tunayopaswa kuyafasiri kimaandiko ni Warumi 8:35-39; Yohana 3:16, 18, 36; Waefeso 2:8-10; 1 Yohana 2:1-2; na Tito 3:5.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 2B

1. **Andika kwa maneno yake mwenyewemaelezo sahihi kufuatana na sura hizi:**
   a. Warumi 8:35-39
   b. Yohana 3:16
   c. Yohana 3:18
   d. Yohana 3:36
   e. Waefeso 2:8-10
   f. 1 Yohana 2:1–2
   g. Tito 3:5

2. **Tafakari mistari hii inamaanisha nini kwako na kwa umpendae. Je unaiamini?**

**C. Kanuni ya Tano: Chunguza Mambo Maalumu**

Kanuni hii inaonyesha maswali muhimu yanayopaswa kujibiwa wakati unajifunza biblia na kufasiri maana ya Biblia. Mfano tunapaswa kujiuliza "nani alisema haya na kwa sababu gani na yalikuwa yakimhusu nani?"

Kanuni pia inatueleza kuwa Mungu alikuwa amehusika na watu watatu katika historia wajulikanao kama Wayahudi, mataifa na Kanisa (1 Wakorintho 10:32). Kwa hiyo tunapaswa kutafuta ili kujua nani sasa anapaswa kuyafanya haya na ili tupate kujua kama ni ahadi, agano au onyo linalotuhusu.

Tutaona katika masomo yajayo ya Maagano kuwa kwa yeyote ambaye agano linamhusu ni muhimu sana. Taifa takatifu kwa mfano wanaweza kutoweshwa kwa sababu ya maovu na hali ya kutotii mbele za Bwana.

Wasamalia, Wababeli, Waashuru, na utawala wa Pesha ni mifano ya mataifa (watu) ambayo mambo haya yaliwapata.

Mungu si kwamba aliwaahidi tu kuwa anaweza kuwaharibu Waisraeli lakini hata kuwarejesha pia. Na hakuna taifa lolote lenye ahadi hii. Kama tungechukua ahadi za Israeli na kuzipeleka katika taifa jingine basi tungekuwa na makosa.

Mfano wa pili ni ahadi ya taifa, nchi na watu wa Israeli katika nchi ya Kanani (Mwanzo 12:1-3, 13:15),lakini hii inaonesha uraia wa kanisa huko mbinguni (Wafilipi 3:20). Mambo ya taifa na nchi hayakuahidiwa kwa kanisa.

Mfano wa mwisho ni baraka za Israeli zikihusisha uhusiano wao na Mungu (Kumbukumbu la Torati 8:7-10) na baraka kwa mataifa na Israeli (Mwanzo 12:3). Hakuna ahadi iliyo ahidiwa kwa wale watakaobariki kanisa au watu wa mataifa.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 2C

1. **Soma mwanzo 12:1-3. Ni nani Mngu anaahidi kumbariki?**

2. **Katika Mwanzo 12:1, ni mashariti gani yaliyokuwa yametolewa kwa baraka alizopewa Ibrahimu?**

3. **Mwanzo 26:5. Kwa nini Mungu alimbariki Isaka?**

4. **Soma waebrania 11:8. Kwa nini Ibrahimu alimtii Mungu?**

5. **Je masharti aliyopewa Abraham namba 2 yanahitajika kwa kanisa pia?**

6. **Je ahadi zilizoahidiwa kwa Abraham pia zimeahidiwa katika kanisa?**

7. **Soma Wagalatia 3:28-29. Je twaweza kushiriki baraka za Abrahamu?**

**D. Kanuni ya Sita: Soma Sura Muhimu**

Kanuni hii inaonyesha kwamba sura zingine zinapaswa kusomwa kwanza kabisa ili kuona mtazamo wa Mungu ambao ni muhimu sana katika maisha yetu ya kiroho. Mara nyingi katika Biblia Mungu hukusanya mambo mengine pamoja ili kufanya ukweli wa haraka na kuziweka pamoja. Mifano michache imeoneshwa hapa chini:

- Kufufuka kwa Yesu–1 Wakoritho15
- Lugha za Watu–Yakobo 3
- Israeli na Ukombozi Wake–Warumi 11
- Furaha ya Imani–Waebrania 11
- Heshima ya Mungu kwa Watoto Wake–Waebrania12:1-11
- Kanisa–Waefeso 1-3
- Haki kwa Wenye Imani–Warumi 3:10-21
- Sheria–Kutoka 20
- Silaha Kamili za Mungu–Waefeso 6:10-17
- Upendo–1 Wakorintho 13

Kanuni hii inatusihi tusome sura za muhimu za maandiko ili kujua mambo muhimu na baadaye tusome sura zinazofuata lakini zinazolingana na tulizosoma kwa uelewa zaidi (rejea).

Kwa mfano hotuba kubwa kabisa katika Biblia inayohusu upendo bora kabisa iko katika 1 Wakorintho 13:4-8a, hapa kuna upendo bora wa aina kumi na sita ambao tukitaka kujifunza ni lazima tukae juma moja darasani tukijifuza juu ya mistari hii. Lakini elewa kuwa:

> ***Upendo huvumulia, hufadhili, hauhusudu, upendo hautakabari haujivuni, haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, hauoni uchungu, hauhesabu mabaya, haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli, huvumilia yote, hauamini yote, hutumaini yote, hustahimiliyote, upendo haupuingui neno wakatikwote, bali ukiwapo unabii utabatilika, zikiwako lugha zitakoma yakiwapo maarifa yatabadilika.***

Tunaposoma katika Marko 12:29-31, tunaona kwamba Yesu alijibu maswali yanayohusu amri iliyokuwa kuu:

***Iliyo kubwa ni hii, 'sikia, O Israeli! Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; na mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote, kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote.' Na umpende jirani yako kama unavyojipenda wewe mwenyewe.'na hakuna amri iliyo kuu zaidi ya hizi.***

Amri hizi mbili zina upendo bora zinatafuta kujua upendo unahusisha nini. Hivyo twaweza kutathimini sisi wenyewe na mbele za Mungu na hata kwa wengine-hii ni maana nzuri sana. Na umuhimu wa upendo unaonekana katika Marko 12 na hata matokeo yake yanaonekana katika 1 Wakorintho 13.

Kama unataka kujaribu upendo wako unaosemwa katika 1 Wakorinth 13 jiulize maswali haya je mimi ni mvumilivu, ni mpole na hata je nina wivu?

Na mfano mwingine uko katika maelezo yaliyoelezwa katika silaha kamili za Mungu (Waefeso 6:10-17). Hii ndiyo sehemu peke ya sisi waamini wa silaha za kiroho zimetajwa. Mkanda unaouvaa hali umejifunga kiunoni unahusiana na Isaya 11:5. Ngao na kofia zinaoana na 1 Wathesalonike 5:8. Upanga kama sehemu ya silaha huu unaoana na Waebrania 4:12.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 2D

1. **Soma 1 Wakorintho 15. Toa kichwa cha habari kinachohsika na ufufuko kutoka katika kila sura hapa chini:**
   a. 15:1-11
   b. 15:12-19
   c. 15:20-28
   d. 15:29-34
   e. 15:35-49
   f. 15:50-58

2. **Katika 1 Wakorintho 15:3-5, nini mahitaji ya Injili kwa ajili ya wokovu?**

**E. Kanuni ya Saba: Tambua Haki ya Mwanadamu**

Kanuni hii inaonyesha uhuru ambao mwanadamu kapewa na Mungu ili kufanya maamuzi.na majukumu yanayolingana na uhuru huu (Yohana 3:18; Wagalatia 6:7). Kanuni ya uamuzi wa mwanadamu umeonyeshwa bayana katika uasi wa Adamu na Hawa katika Mwanzo 2-3. Kwa sababu ya akili ya kujua mema na mabaya. Mungu alijua kuwa wanaweza kula mti wa ***"ujuzi wa mema na mabaya,"*** lakini Mungu hakuwa chanzo cha hiyo. Adamu na Hawa waliamua kula mti waliokatazwa kwa sababu waliamua wao wenyewe. Na baadaye walijuta kwa uamuzi wao kwa sababu hata ilipelekea kufukuzwa katika bustani ya Edeni.

Kuna maneno mengi yanayoonyesha uwezo wa mwanadamu katika kuchagua, maneno kama Amini na Imani yana maana moja katika katika kiyunani. Kwa sababu ya uelewa wa Mungu alijua ni nani ananyeweza kumwamini mwana wake Yesu na akaokolewa (Warumi 8:29; 1 Petro 1:1-2). Ujuzi wa Mungu kwa vyovyote hauondoi swala la kuamini.

Biblia inarekodi maamuzi yote mawili mazuri na mabaya yaliyofanywa na mwanadamu. Hii inakuwa inatunza ushaida kwa ajili ya uaminifu wake wa milele. Tunatambua katika kanuni hii kwamba neno la Mungu linatunza mambo mabaya ya mwanadamu. Huu ni uasi uliofanywa na mwanadamu kwa kuruhusiwa na Mungu ili kumleta mwana wake lakini hakumaanisha iwe hivyo. Kwa sababu hii Biblia inapotunza kumbukumbu za matendo ya mwanadamu haimaanishi Mungu ameyaridhia. Yesu alijua kuwa Yuda atamsaliti na kwa kweli alimtahadhalisha (Mathayo 26:24), lakini Yuda alimsaliti na akapata majuto makali.

Mungu kampa uhuru wa kuchagua lakini siyo uwezo wa kufanya uchaguzi sahihi wakati wote. Kwa hiyo tunapaswa kuona uchaguzi mbovu wa dhambi wa mwanadamu kwenye fasiri za Maandiko

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 2E

1. **Soma Yohana 3:16-18. Ni nini mahitaji ya mwanadamu ili aweze kuepuka hukumu?**

2. **Soma Warumi 3:21-26. Je mwanadamu anahitaji nini ili kupata haki ya Mungu?**

3. **Soma Mwanzo 2-3. Je mwaname na mwanamke hawakumtii Mungu?**

4. **Kutotii kwao kunahakikisha nini?**

5. **Soma kitab cha Yakobo. Utaona kuna kama amri 60. Kila amri inataka kwamba kila aliyepokea afanye maamuzi. Sasa kila amri hiyo inalenga nini?**

**F. Kanuni ya Nane: Kumbuka Maagano**

Kanuni hii inatuonyesha makubaliano au mkataba uliofanywa kati ya Mungu na mwanadamu. Kuna mkataba wa hiari ambao mwanadamu anaweza kuafikiana nao na kunausiokuwa wa hiari ambao ni lazima ufanye na unatokana na uaminifu wa Neno la Mungu.

Agano ni muhimu kwa sababu hutupa mtazamo wa historia ya jinsi gani Mungu hushirikiana na watu wake. Kama tutaelewa agano la Mungu na tuliruhusu lituongoze tutakuwa safi na sawa kabisa katika kufasiri hata vifungu na sura zilizongumu. Kwa mfano Waisraeli wangeweza kuonywa na kuadhibiwa katika historia ya mwanadamu wakati wa kipindi kigumu na majanga (Mambo ya Walawi 26), lakini Mungu hakufanya hivyo kwa sababu yeye aliwa ahidi.

Kuna maagano tisa yanayohitajika kujifunza. Tutanukuu vichwa vya habari na kuonesha kwa ufasaha wa kila agano kwa kulinganisha na kufuata maandiko.

1. **Agano katika Bustani ya Edeni**

Hili lilifanyikia katika bustani ya Edeni kati yake Mungu na Adamu (Mwanzo 1-2). Hili lilikuwa ni la masharti likitegemea utii wa mwanadanu na linaingiza ahadi ya Mungu kwa kumbariki mazingira mazuri. (2:8), chakula kizuri, furaha (2:9),hali nzuri ya hewa (1:6-7, 3:8), mapenzi mazuri (2:21-25), na mahusiano mazuri na Bwana (1:26-27, 3:8). Agano hili mwanadamu alilikubali, lakini lilivunjika baada ya mwanadamu kuasi kwa kula lile tunda toka katika mti aliokuwa kakataliwa.

Agano hili halina madhala lakini baraka zake zitarejeshwa kwa mwanadamu wakati wa mbingu mpya na nchi mpya (Ufunuo 21-22). Kwa hiyo hatupaswi kufasiri Agano hili kwamba tusihusike tena na bustani ya Edeni. Mwanadamu hatafanya au kupata baraka tena tofauti na kumpokea Yesu Kristo.

2. **Agano la Adamu**

Agano hili lilifanywa kati ka Mungu na Adamu kwenye bustani ya Edeni baada ya anguko kabla ya kufukuzwa. Hili halikuwa na masharti. (Mwanzo 3:14-19).

Hili lilikuja kama matokeo ya dhambi ya asili na linajulikana kama anguko. Mungu alilaani (3:14), na akaleta mgogoro katika historia kati ya uzao wa Adamu na nyoka. (3:14-15). Mwanamke alipewa uchungu katika kuzaa na kuwa msaidizi wa mwanaume (3:16). Dunia ililaaniwa (3:17-19), na ikapewa kuwa ngumu katika kutoa mazao na mimea ya chakula. Mwanaume na mwanamke walilaaniwa kufa kimwili kabisa (3:19 linganisha na 2:17), na wote walifukuzwa toka bustanini (3:17-19).
Agano la Adamu linatoa mpango wote wa historia na linakuwa na madhara kwa wanadamu wote hadi pale Mungu atakapomtupa shetani katika ziwa la moto katika mwisho wa millennia (miaka elfu) (Ufunuo 20:7-10). Tunapaswa kujua kuwa madhara ya Adamu yalifika kwa kila mwanadamu (Warumi 5:12-14).

3. **Agano la Nuhu**

Agano la Nuhu linaloonekana katika Mwanzo 8:20–9:17, lilifanywa kati ya Nuhu na Mungu baada ya gharika kubwa. Hili lilikuwa halina masharti kwa sababu lilikuwa ni kuangamiza kila kiumbe. Linajumuisha ahadi tena ya kwamba hakutakuwa na gharika kubwa la maji litakalo waangamiza wanadamu. Linajumuisha pia amri ya Mungu ya kuongeza idadi ya watu katika dunia (9:1), kupatikana kwa wanyama wa kula (9:2-4), na ghadhabu kubwa ya mji kama adhabu ya kuuwa (9:5, 6). Upinde wa mvua uliwekwa kama alama ya uaminifu wa agano hili.

Agano la Nuhu lilianzia kwenye mafuriko na likaisha milele. Japo kuwa kuna mafuriko yanayoharibu hata mali na kupoteza uhai lakini hakutakuwepo na mafuriko yatakayoharibu ulimwengu wote. Uhuru wa kula wanyama ulitolewa na kwa hiyo hatupaswi kuhoji juu ya vyakula (Danieli 1). Na sehemu ya mwisho kabisa ya Agano hili ni adhabu ya mauaji ambayo hadi leo bado ipo.

4. **Agano la Ibrahimu**

Agano hili tunaliona katika kitabu cha Mwanzo 12:1-3, na kuendelea na hata maelezo ya ziada yameongezwa. Alipewa Ibrahimu na lilikuwa la masharti mpaka pale alipokutana na mahitaji ya Bwana na Agano hili likawa halina masharti kwa Uzao wake.

Agano la Ibarahimu linajumuisha ahadi za mtu binafsi, ukoo, nchi, miji, taifa, umoja na hata ulinzi pamoja na Ukoo wa Masihi ukawekwa (Mwanzo 17:1-8).

Agano la Ibrahimu lilianza kwa ahadi. Na ukoo wa Yesu ulikamilishwa baada ya kuzaliwa Yesu Kristo (Wagalatia 3:16). Ahadi ya kubariki vitu imetolewa katika nyanja mbalimbali za historia na hii itakamilika kabisa katika utawala wa miaka elfu. Agano hili linakusanya tangu ahadi ya uzao wa Ibrahimu na hadi utawala wa miaka elfu.

Hivyo maana ya sura zilizo ngumu katika Biblia zinakuja kuwa rahisi ikiwa mtu ataanza kwa kuangalia agano la Ibrahimu. Na sura hii inaonekana katika Mathayo 11:20-24 na inasema,

> ***Ndipo akaanza kuikemea miji ile ambayo ndani yake ilifanyika miujiza yake iliyo mingi kwa sababu haikutubu. Ole wako Korazini, Ole wako Bethsaida, kama miujiza iliyofanyika kwenu ingelifanyika katika Tiro na Sidoni wangelitubu zamani kwa kuvaa magunia na majivu. Walakini nawaambieni itakuwa rahisi Tiro na Sidoni kustahimili adhabu zao siku ya hukumu kuliko ninyi. Nawe Kapernaumu je utakuzwa mpaka mbinguni? Utashushwa mpaka kuzimu;kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwako ingalifanyika katika Sodoma ungalikuwapo mji huo mpaka leo. Walakini nawaambieni itakuwa rahisi nchi ya Sodoma kustahimili adhabu yake siku ya hukumu kuliko wewe.***

Kwa neema Israeli imepewa muda wa kutubu mwingine kwa sababu ya ahadi ya Ibrahimu. Kama haitatubu adhabu itakuwa kubwa lakini taifa halitaangamizwa wala kutolewa katika historia yake.

5. **Agano la Musa**
Hili alipewa Musa katika mlima Sinai. Na linaonekana katika Kutoka 20 na hata katika sura zingine kama Mambo ya walawi, Hesabu na kumbukumbu la Torati. Agano hili ni la masharti linataka utii. Kwa wale walitii walibarikiwa na wale ambao hawakutii walilaaniwa (Mambo ya Walawi 26).

Kusudi kuu la agano hili ilikuwa kuonyesha hitaji la Mwokozi (Wagalatia 3:24-25). Na linaonesha sheria ya Mungu. Na Agano hili pia lilitolewa kwa Waisraeli ili kutoa mwongozo kwa wakuu wa kiyunani na hema ya kuabudia.

Yesu alikuja kutimiliza Agano hili kwa kutunza sheria (Mathayo 5:17). Agano hili ni la kipindi cha Waisraeli inayoingiza hata kipindi cha kwanza kabisa cha Musa kupewa sheria (Kutoka 20) mpaka kipindi cha pentecoste ambapo kanisa lilianza. Itaingiza hata kipindi cha mateso makali ambacho ni miaka saba ya historia ya mwanadamu ambayo itakuja baada ya unyakuo wa kanisa.

Tunapaswa kujua kwamba sura nyingi katika agano la kale zinahusiana na sheria ya Musa kwa mfano wanyama wengi walisemekana kuwa ni najisi na hairuhusiwi kuwala (Mambo ya Walawi 11). Hii haiji kwetu leo kwa sababu Yesu Kristo aliisha takasa kila aina ya chakula (Marko 7:14-18).

6. **Agano la Daudi**
Agano la Daud lilifanywa na Daudi na linaonekana katika 2 Samweli 7:8-19 na Zaburi 89. Agano hili halina masharti linaloonyesha utawala wa taifa katika nyumba ya Daudi na ahadi ya mtoto ambaye atatawala mataifa yote milele.

Agano la Daudi lilianza kuwa na nguvu wakati wa utawala wake. Na sehemi nyingine ya Agano hili limekamilishwa na mtoto mkuu ambaye ni Yesu Kristo kwa mara ya kwanza kuja kwake duniani (Luka 1:32). Matokeo yake yatadumu milele.

Kwa wakati mmoja ukoo wa Daudi ulikuwa mikononi mwa mfalme Yosia kwa miaka minane ya utawala wake (2 Wafalme 22:1). Wayahudi walioishi nyakati hizi walikuwa bado na tumaini la msingi lililojengwa juu ya ahadi ya Mungu. Yesu alipewa mamlaka yote mbinguni na duniani baada ya kufufuka kwake (Mathayo 28:18) ili kukamilisha agano. Waamini wa leo wanatumaini la kwamba Yesu yuko katika kiti cha Enzi cha mbinguni. (Waebrania 8:1) na kwamba atarudi kutengeneza kiti chake cha utawala hapa duniani (Mathayo 25:31).

7. **Agano la Palestina**
Agano hili ni mwendelezo wa agano la Ibrahimu. Agano hili la masharti linaonyesha mgawanyo wa Wayahudi kwa sababu ya kutotii kwao, lakini mwisho linaonyesha kukusanywa tena katika nchi pamoja baada ya kutubu. (Kumbukumbu la Torati 30:1-10).

Agano hili lipo katika kipindi cha Waisraeli na litakamilika wakati Wayahudi watakapo kusanywa pamoja baada ya kurudi kwa Yesu mara ya pili (Mathayo 24:31; Marko 13:27) na nchi iliyoahidiwa Ibrahimu

toka mto wa misri hadi ule mkubwa flati umejengwa (Mwanzo 15:18). Tangu kutolewa kwa agano hili na kuendelea mfasiri anapaswa kujua kuwa mgawanyo tangu Israeli kutka katika nchi ni wa muda tu.

8. **Agano Jipya la Waisreli**
   Hili walipewa nyumba ya Israeli katika Yeremia 31:31-34, na limerudiwa tena katika Waebrania 8:8-12. Hili agano liko katika damu ya Yesu Kristo (Waebrania 9:11-14), na ni Aganolisilo na masharti ili kuwaendeleza Wayahudi (Wayahudi wanaozaliwa).

   Agano linalosema juu ya ahadi ya makao ya ulimwengu wa Roho Mtakatifu na utajiri mwingi (Yeremia 32:41; Isaya 61:8), litakamilika wakati wa utawala wa miaka elfu. Ni vizuri kukumbuka wakati tunasoma Biblia kuwa ahadi alizozifanya Mungu katika agano hili linawahusu Wayahudi waliomwamini Yesu. Wayahudi hawataweza kubarikiwa kupitia agano hili kwa sababu ya asili yao tu.

9. **Agano Jipya kwa Kanisa**
   Agano jipya lilifanywa katika kipindi cha Kanisa la Agano Jipya (Mathayo 26:26-28). Hili ni Agano lisilo na Masharti kwa waamini wa Yesu Kristo (Waebrania 9:11-14), na ni kumbukumbu katika taratibu za dini kwa njia ya kushiriki meza ya Bwana (1 Wakorinto 11:25). Inadunisha utawala wa ulimwengu na wa waamini (Waebrania 9:11), na inaahidi kuwa itakamilika katika kipindi na itakuwa ni milele. Yesu alikuja kuwa mpatanishi wa agano hili (Waebrania 9:15).

   Agano hili lilianza siku ya pentekoste Kanisa lilipoanza (Matendo 2) na halitaisha milele. Wanafunzi wanapaswa kukumbuka kuwa baraka zilizopatikana kupitia Agano hili hazitaisha na hakuna atakayezichukua. Kwa hiyo waamini wa kanisa la Agano Jipya wana ulinzi na haijalishi kwa ugumu gani mtu anaweza kuhangaika katika maisha yake Bwana atampigania na hatamwacha (Mathayo 28:18-20).

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 2F

1. **Ni Maagano yapi yalikuwa ni yamasharti?**
   a.
   b.
   c.

2. **Ni Maagano yapi hayakuwa na masharti?**
   a.
   b.
   c.
   d.
   e.
   f.

3. **Soma sra zinazohusiana na kila Maagano na one kama unaweza kuongeza kulingana na maelezo yaliyotolewa.**

# Sehemu ya 3
# Sheria ya Tatu

**Tafuta kwa Hekima kwa Kulinganisha Sura Mbalimbali katika Maandiko**

Sheria ya tatu inasema juu ya kutafuta hekima ambayo inapatikana kwa usahihi kutoka katika maneno ya Mungu. (1 Wakorintho 14:33), kushindwa kuelewa hili ni tatizo letu. Mungu kaweka aina mbalimbali za maneno ambayo sisi tunaweza kupata kuwekewa na hata kutupa hekima ya kuenenda (Methali 1:2-6).

Kutokukubaliana huku hutokana na kushindwa kuyalinganisha maandiko. Mfasiri anahitaji kuichunguza sura na kujua sura hiyo inahusiana vipi na sura zingine. Ni baraka sana kwa wale wanaolichunguza neno la Mungu na kulitenda katika maisha yao. Kwa wale wanaoshindwa kuelewa mstari hata mmoja au neno moja mara nyingi huishia vibaya katika fasiri zao na kuzua uzushi.

Kuna mambo sita yanayohusiana na sheria hii. Tunatakiwa kuangalia utofauti ambao Mungu hutumia katika maneno yake. Huwa tunafanya hivyo kwa kuiangalia sura yenyewe. Usomaji wa neno la Mungu ulio mzuri ni ule wa kuyalinganisha maandiko, na kuangalia utofauti wake unavyohusiana na hata unabii wake.

**A. Kanuni ya Tisa: Tafuta Tofauti**

Hii inatuelewesha jinsi ya kuuona utofauti wa sura mbali mbali katika maneno ya Mungu. Kwa maneno mengine tunatambua utofauti wa maandiko katika Biblia kwa kuiangalia Imani hai, wokovu, na dhambi sheria na neema na mengineyo. Biblia kwa kweli ina mambo mengi yaliyo tofauti. Changa moto yetu tunataka uelewe aina mbalimbali za kuitafsiri Biblia.

Mfano mmoja wa kujua tofauti hizi ni Imani na Kazi ni katika Waefeso 2:8-10:

> ***Kwa maana mmeokolewa ka neema kwa njia ya imani ambayo haikutokana na nafsi zenu ni kipawa cha Mungu wala si kwa matendo mtu awaye yote asije akajisifu. Maana tu kazi yake tuliumbwa katika Kristo Yesu tutende matendo mema ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.***

Wokovu ulio mzuri ni wa neema kwa njia ya imani na si kwa sababu ya Matendo yetu. Kwa hiyo basi umuhimu wa kazi haujachambuliwa. Kwa hiyo matendo si sababu ya kukufanya upate wokovu lakini matendo ni muhimu katika maisha ya Kikristo.

Imani haina sifa kwa yenyewe peke yake kwa sababu sifa zote ziko ndani ya imani. Kwa mtu kuwa na imani katika imani ni lazima ajiamini yeye mwenyewe. Tunajua ya kwamba sisi sote ni watenda dhambi kwa hiyo si vizuri kujiamini na si hekima (Warumi 3:23).

Kama mtu mzito atabembea kutoka juu hadi chini halafu juu hadi chini karibu na shimo kubwa halafu bembea yake imefungwa kwenye kimti kidogo hawezi kuwa na imani ya kupona kutoka lakini kama itafungwa kwenye mti mnene atakuwa na imani ya kupona.

Yesu Kristo aliyechukua dhambi zetu msalabani ni mti mbichi mkubwa na imara na tunapaswa kuwa na imani kubwa juu ya Yesu.

Kazi huwa na matendo mazuri katika asili yake kama vile kuwasaidia maskini (Wagalatia 2:10). Lakini pamoja na matendo mazuri hatuwezi kujiokoa sisi (Tito 3:5). Kazi kazifanya Mungu ili kuonyesha imani yetu katika Kristo Yesu. Kwa kweli tutapata ujira wetu kwa Yesu kulingana na jinsi tulivyotenda (2 Wakorintho 5:10). Kazi lazima ifanywe kwa shukurani kwa kadri Bwana anavyotuwezesha. Na si tufanye kazi kwa sababu ya manufaa yetu wenyewe.

Tofauti nyingine tunayoweza kuiona ni kati ya usalama wa wokovu wa waaminio na hali halisi ya dhambi.

Tunaambiwa kwamba Bwana alifanya kazi kubwa sana ya kutuokoa wakati sisi tulipokuwa adui zake. Unadhani kwa sasa anaweza kufanya kidogo wakati tayari tuko katika familia yake, hapana. (Warumi 5:6-10)?
Biblia inasema juu ya hili kwamba muamini anaweza kufanya dhambi hata kama kaokoka.

> ***Tukisema kwamba hatuna dhambi twajidanganya wenyewe wala kweli haimo ndani yetu. Tikiziungama dhambi zetu yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote. Tukisema kwamba hatukutenda***

***dhabi twamfanya yeye kuwa muongo wala neno lake halimo mwetu.*** (1 Yohana 1:8-10)

Ni kweli kabisa kuwa sura hii inahusiana na waaminio. Hatupaswi kusoma kwa undani sana Agano Jipya ili tupate kuvumbua maonyo ya waamini dhidi ya dhambi. Maswali yanakuja je sisi waaminio kama wakristo twaweza kupoteza wokovu wetu tunapofanya dhambi au hapana?

Katika kitabu cha Warumi na hata katika vitabu vingine katika Biblia wokovu ni kitu ambacho hakipotei na Paulo alisema, ***"Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru mbali na sheria ya dhambi na mauti"*** (Warumi 8:1-2). Kanisa la Wakorintho lilikuwa limetawaliwa na dhambi kubwa na Paulo aliwaita wao kuwa ni wa mwili (1 Wakorintho 3:1-2), lakini si kwamba walikuwa hawajaokoka. Na yeye alikwenda katika kanisa hilo kama la watu watakatifu na Wakristo kabisa (1 Wakorintho 1:2).

Kweli wakristo wakati mwingine hujikuta wameanguka katika hali ya maisha magumu. Pamoja na hiyo wokovu huwa haupotei: ***"Kama sisi hatuamini, yeye hudumu wa kuaminiwa"*** (2 Timotheo 2:13).

Maisha ya dhambi ya mkristo mara nyingi matokeo yake huwa ni shida na masumbufu tu.Na hii inatupelekea kukosa zawadi ***"Kama tutastahimili tutamiliki pamoja naye na kama tutamkana na yeye atatukana sisi."*** (2 Timotheo 2:12). Mazingira yanatuonyesha kwamba kama tunamkana Yesu basi hatutatawala pamoja naye.

Kutokana na mifano hii miwili tunaweza kuanza kuona tofauti kwamba Mungu amekwisha sema tayari katika maneno yake.Tutumie muda wetu kwa kuyachunguza maandiko na kuelewa mahusiano ya tofauti zilizomo katika maandiko.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 3A

1. **Soma Waefeso 2:8-10. Ni nini karama ya Mungu katika wokovu?**

2. **Ni nini sehemu ya mwanadam katika wokovu?**

3. **Mara unapookolewa, Mumini anakuwa ameumbwa kwa ajili ya kazi gani?**

4. **Soma Tito 3:5. Je kazi njema zitatuokoa ?**

5. **Soma 1 Yohana 1:8. Je muumini anawza ktenda dhambi?**

6. **Soma 1 Yohana 1:9. Mumini anapaswa kfanya nini anapotenda dhambi?**

7. **Soma 1 Yohana 1:10. Ni nani tnamwita mwongo kama tukisema kwamba hatuwezi kufanya dhambi?**

8. **Soma Waebrania 13:15-16. Ni kazi njema zipi zimetajwa katika mistari hii?**

9. **Soma Wakolosai 3:12-17. Ni kazi zipi njema zimeorozeshwa hapa?**

10. **Soma 2 Wakorintho 5:10. Nini waumini watapata kwa ajili ya matendo mema?**

**B. Kanuni ya Kumi: Chunguza Yaliyomo**

Kanuni inaonyesha kwamba kila neno, sentensi au mstari katika Biblia ina habari inayoeleza (isipokuwa maneno machache ya mwanzo na machache ya mwisho wa sentensi au mstari). Hii inaonesha hali halisi ya kila neno au mstari na mahusiano yake katika kila neno na mstari. Mungu kaweka mwanga katika kila sura ili kuelewa nia na makusudi ya sura hiyo na hata kama haieleweki sura zingine zipo zinazofanana ili upate kuelewa ndani ya Biblia yenyewe.

Hatutakiwi kuugeuza mstari na kuupa maana nyingine. Kuhamisha maana ya mstari ni kujaribu kuingiza vitu vya kimwili ambavyo kamwe haviwezi kuoana na agenda zako. Na hii hali ya kufasiri tofauti maneno ya Mungu ilisemwa kabla katika maandiko.

Ufafanuzi wa maandiko kwa kawaida una maana ya kwamba msomaji anaangalia ni nani anayezungumza, na ujumbe huu ni wanani na nini kusudi na nia ya ujumbe huu; na ni wakati gani ujumbe huu unazungumzwa.

Kuna mambo matatu ya kuangalia wakati ukisoma sura katika biblia:

1. **Yaliyomo ya Karibu**
   Mazingira ya karibu yanahusisha mistari mingi katika sura moja. Mfano, Wagalatia 5:1 inatuambia, ***“katika ungwana huo Kristo alituweka huru kwa hiyo; simameni wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa.”*** Ni lazima tuwe na tabia ya kutumia neno “utumwa” kwa tamaduni fulani kwa wakati fulani na sehemu fulani kwa sababu neno utumwa lina maana ya kuwa chini ya au kumilikiwa kimwili au kuendeshwa kimwili au kisiasa. Katika mazingira haya tunaona kuwa sura hii inahusiana na utumwa wa kiroho. Na sura hii inasema tena kwa wale waliochini ya utumwa wa sheria hawako huru na hawawezi kutumikiana kwa upendo (Wagalatia 5:13).

2. **Yaliyomo ya Kati**
   Mazingira ya kati yanahusisha mistari ile inayoonekana katika kitabu kimoja. Mfano wa hii unaonekana katika Mathayo 24:40, inayosema, ***“Kutakuwa na watu wawili wakilima katika konde mmoja atatwaliwa na mmoja ataachwa.”*** Mazingira haya yanaonyesha siku ya mwisho. Swali linakuja ni nani atakaye achwa na ninani atakaye twaliwa, je watachukuliwa wenye haki tu na waovu wataachwa kama ilivyo katika unyakuo wa kanisa au watachukuliwa walio waovu na wenye haki wataachwa kama ilivyo katika kuja kwa yesu mara ya pili kutawala miaka elfu? Mazingira ya karibu hayawezi kujibu swali hili.

   Mathayo 13:49, kwa vyovyote inatupa jibu. Sura hii pia inahusika na siku za mwisho tunaelezwa kwamba ***“waovu watatengwa mbali na wenye haki.”*** Kwa hiyo swali hili limekwisha jibiwa ni nani atakaye achwa na nani atatwaliwa na kwa hiyo sura hii inahusiana na kurudi kwa Yesu.

   Mazingira ya kati yanatuhabarisha umuhimu wa kujifunza msitari kwa msitari katika kitabu ili kuelewa na kutunza maana yake. Ikiwa mwanafunzi atarukia kwanza kwenye Mathayo 24 hataweza kulipata jibu lakini kama atasoma kitabu kizima jibu atalipata vizuri.

3. **Yaliyomo ya Mbali**
   Mazingira ya mbali inakazia mazingira ya kati ya kusoma neno la Mungu. Inajumuisha vifungu mbalimbali katika Biblia ili kuweza kumaliza shida ya kifunu ulichokisoma.

   Masomo ya kusoma kwa kuichambua Biblia kwa mtazamo wa mbali hii inaonesha kuwa sehemu moja inaweza kuwa na majibu mazuri kutoka katika sehemu mbalimbali za Biblia. Kusoma maneno yaliyoorodheshwa kama “neema,” “imani,” au “upendo,” ikiwa na maana ya rejea, kwa mfano, hii hupelekea kusoma sura nyingi zenye maneno hayo. Rejea ni vitabu vilivyoorodheshwa na watu kulingana na vifungu ili kukuwezesha kuona kifungu unachokitafuta. Rejea zinakupa orodha ya vifungu na mistari yenye maneno kama hayo. Habari zaidi ya rejea tutaiona baadaye katika kitabu hiki.

   Mazingira ya usomaji huu ni lazima ufanyike ili kupata kuangalia kanuni mbalimbali kama vile ufasiri wa unabii au uelewa wa aina na hata alama. Kwa mfano pazia katika hekalu (Kutoka 26:31-35), lilikuwa likitenga kati ya mahali patakatifu na mahali patakatifu pa watakatifu limefafanuliwa katika Waebrania 10:20 na lina maana ya mwili wa Kristo Yesu.

   Kuchunguza kwa undani sana na mapana ni muhimu katika maisha yetu kwani Biblia inasema ***“ukitumia neno la kweli”*** (2 Timotheo 2:15). Tunapotengeneza mambo ya imani ni lazima tuyaangalie kutoka katika maandiko kuthibitisha kwamba Biblia ni kiongozi. Kama imani yetu haiko katika kupatana na maandiko hivyo hata kuamini na kufuata kwetu kutakuwa kwa maswali, na ni bure.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 3B

1. **Soma Wagalatia 5:1 na Warumi 8:2. Tunapaswa kufanya nini na huru wetu katika Kristo?**

2. **Soma Wagalatia 5:13. Tunapaswa kutmiaje uhru wetu?**

3. **Soma 1 Korintho 10:28-31. Je tunapaswa kukabiliana vipi na mtu anayetuvamia katika kutumia uhuru wetu?**

4. **Soma 2 Wakorintho 3:17. Roho mtakatif huleta nini?**

5. **Soma Yakobo 1:25. Tunapaswa kushika sheria gani ili kupata baraka?**

6. **Soma Yakobo 2:12. Tnapaswa kusema na kutenda namna gani?**

7. **Soma 1 Petro 2:16. Tunapaswa kuutumiaje uhuru wetu?**

8. **Soma 2 Petro 2:1, 17-19. Walimu wa uongo wanaahidi nini?**

9. **Anza na Wagalatia 5:1 (yaliyomo ya karibu) na 5:13 (yaliyomo ya karibu). Tumia misatri mingine hapo juu (yaliyomo ya mbali) kuonesha sifa za uhuru.**

**C. Kanuni ya Kumi na Moja: Fasili kwa Kuyalinganisha Maandiko**

Kanuni hii ya kulinganisha maandiko inakuwa katika mtazamo wa kati wa neno la Mungu. Hii inatuonyesha umuhimu wa kuyalinganisha maandiko kwa maandiko ili kupata usawa wake ili tuweze kupata maana iliyo sahihi na kweli.

Ni vizuri kuchukua kifungu kimoja na kukilinganisha na kingine kama vile neema na huruma ni maneno yanayotofautiana. Lakini tunapoyaangalia kufanana kwake tunayaona kama yanarandana lakini kweli haya ni tofauti kama vile Mungu na Shetani. Tunapokuwa tunalinganisha makusudi ya vifungu katika mitazamo ya mbali kabisa tunaleta picha ambayo ilikuwa imekatwakatwa vipande na kuifanya iwe moja. Kwa hiyo Theologia imefanyika hivyo ili tupate kuyakusanya maandiko na kuyaweka pamoja.

Hii si kwa mwanafunzi tu hapana bali hata kwa waliokwisha pea katika theologia (1 Timotheo 3:6), (Methali 3:5-6), tunapaswa kujua kuwa ndani ya sura 31,000+ katika Biblia zinatakiwa kuchunguzwa. Furaha kubwa tunayoipata katika kuyachunguza maandiko ni pale tunapojua sasa upotoshwaji wa neno la Mungu ulivyo na kwa hiyo tunakuwa makini na waangalifu katika kuenenda kwetu.

Kadri tunavyolinganisha andiko na andiko tunakuja kuona kwamba theologia iko katika sehemu nyingi kwenye Biblia. Kwa mfano swala la "Kuthibitishwa katika Imani" (Mwanzo 15:6; Warumi 3–4). Tunaposoma sasa neno la kuthibitishwa kwa sababu ya kazi zetu katika Yakobo 2:14-26, hivyo sura hizi mbili tunapaswa kuzifikiri sana. Tunapoziunganisha sura hizi pamoja, tunaelewa kuwa "kazi" ni kitu muhimu katika mipango ya Mungu kwa sababu huongeza Imani ambayo hupelekea kupata wokovu lakini haina maana kuwa ndiyo sababu ya kupata wokovu kama ilivyofundishwa katika Waefeso 2:8-10. Sisi ***"tunaokolewa kwa njia ya Imani"*** na hii ***"haijafanywa kwa sababu ya kazi zetu nzuri."***

Kwa hiyo kanuni hii inatuonyesha na kutufundisha tuwe waaminifu tunapoanza kuweka theologia katika maneno ya Mungu . kwa mfano sura ya kiyunani katika Marko 16:9 hadi mwishoni mwa kitabu iko kwa jinsi yake. Na watu wengine wamejenga katika sura hizi ambazo sasa zimewapotosha kabisa katika theologia zao.

Mfano mwingine muhimu wa kuyalinganisha maandiko unaonekana katika "siri" (kitu kisichojulikana) ambacho kwa kweli kinatawala katika Agano Jipya. Kama tungekuwa tunasoma Waefeso 3 na tuende katika neno "siri' tungelijaribu kujibu swali linalosema siri ni nini na kwa vyovyote jibu letu lingepatikana katika Wakolosai 1:25-27, inayosema:

> ***ambalo nimefanywa mhudumu wake sawasawa na uwakili wa Mungu niliopewa kwa faida yenu nilitimize neno la Mungu. Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyoutajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa nao no Kristo ndani yenu tumaini la utukufu.***

Siri imeonyeshwa katika maandiko kama kipatanisho chetu cha mahusiano na Masihi. Uhusiano huu ni wa waaminio wapya wajulikanao kama kanisa la Agano Jipya.

## Kwa Masomo Binafsi: Sra ya 4, Sehemu ya 3C

1. **Soma Warumi 3:21-28. Mtu anaweza kthibitishwa kuwa mwenye haki <u>mbele za Mungu</u>?**

2. **Soma Waefeso 2:8-9. Mt anaokolewaje?**

3. **Soma Yakobo 2:14-26 na Waefeso 2:10. Muumini anapaswa kuzaa nini?**

4. **Katika Yakobo aya ya 2 mwandishi anasema nini kuhusu Imani bila Kutenda?**

5. **Inamaana ya kwamba mumini asipotenda vizuri hatapata wokovu? (Pitia Tito 3:5)**

6. **Katika Yakobo 2 kama rejea kwa Abraham, Je Abrahamu alikuwa ni muumini alipomtoa mwana wake Isaka?**

7. **Katika Yakobo 2, ni mt yupi anapaswa kuomba "Wewe nayo Imani na Mimi ninayo matendo hivyo nioneshe Imani yako isiyo na matendo na nitakuonesha Imani yangu iliyo na matendo?"**

8. **Soma Waebrania 11:1. Je Imani inaonekana?**

9. **Tafakari aya hizi zote na halafu lielezee neno Kuokoka katika Yakobo 2:14 na kuthibitishwa katika 2:22 na 2:24.**

**D. Kanuni ya Kumi na Mbili: Tafuta Mwafaka**

Kanuni hii inaonyesha uaminifu na ukweli wa Mungu kwamba yeye si mtunzi wa Uongo (1 Wakorinto 14:33). Kwa maana nyingine hakuna mchanganyo katika Biblia. Biblia ni neno lililo na pumzi ya Mungu kwa hiyo yaliyomo ni kweli na amina. Kutokukubaliana na neno la Mungu hii iko katika mwanadamu tu na ni hatari sana.

Hii husababishwa na watu kwa kuyatii mawazo yao na maandiko yanaonya juu ya hili (Yohana 5:37; Mithali 3:5-6; 2 Wakorintho 5:7). Hatuwezi kabisa kuelewa neno la Mungu katika Biblia hadi tukutane na Bwana uso kwa uso. (1 Wakorintho 13:12). Kwa hiyo ni hivi tunatembea kwa imani (Waebrania 11:6; Wakolosai 2:6), tukimtegemea Bwana atufikishe mbinguni.

Tutakapofikia kuyakubali maneno ya Mungu jinsi yalivyo hapo ndipo Bwana atatupatia hekima na maarifa. Tunaambiwa kwamba katika mwanzo wa kitabu cha Methali tunapojifunza kuyaelewa yaliyo magumu na hata mengine zaidi yanayochanganya tunakuwa na hekima (Methali 1:2-6). Hii ninahitaji kujifunza kwa bidii. Kwa mfano kama tulivyokwisha kujadili tunahitaji Yakobo 2 na Warumi 3-4 zote hizi zitueleze kwa ufasaha kati ya imani na kazi.

Tunapoangalia mahusiano ya sura tunahitaji vilevile kuwa makini na waoneshaji wa nyakati na mahali kwa sababu kila jambo lililodogo si kwamba limeandikwa hivyo bila kuwa makini tunaweza vilevile kuchanganya fasiri. Hivyo tuelewe kuwa hakuna ujanjaujanja wala uongo katika neno la Mungu.

Tunatakiwa kukumbuka kwamba kanuni ya Mungu inaeleza kanuni katika njia mbalimbali ili kwamba kilichokuwa ni cha muhimu tukifahamu. Kwa mfano; Warumi 3:23 inasema, "wote wamefanya dhambi..." hata, kitabu cha Walawi kinaamuru kutoa dhabihu kwa ajili ya ondoleo la dhambi kwa hiyo sura zote mbili zinahimiza kitu kimoja.

Kitu kingine kinachotupa kuelewa neno la Mungu ni mahusiano yetu na Mungu.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehem ya 3D

1. **Je mtazamo liochkuliwa katika kuendeleza masomo ya sehem ya (3C) Yanaonesha kanni hii?**

2. **Soma Warumi 3:21-28; 5:1-2, 8-10; 8:35-38 na Yohana 10:27-29. Ni pointi gani inayoonekana kuhusu wokovu ?**

3. **Soma 1 Wakorintho 6:9-10. Je mistari hii inafndisha nini?**

4. **Je kuna mgogoro hapo?**

5. **Soma 1 Wakorintho 3:10-15. Je mt anawezaje kuwa mpatanishi katika migogoro inayotokea?**

6. **Soma Yakobo 1:12. Je mtu anapaswa kfanya nini ili kupata taji ya uzima?**

7. **Soma 1 Petro 5:1-4. Je mtu anapaswa kufanya nini ili kupata taji ya utukufu?**

8. **Soma 2 Timotheo 4:7-8. Je mtu anapasa kfanya nini ili kupata taji ya haki?**

**E. Kanuni ya Kumi na Tatu: Fikiria Mpango wa Mungu**

Mgawanyo ni vipindi vya historia ambavyo Mungu aliweka majukumu kwa watu wake. Kwa hiyo watu wa Mungu wamegawanya katika majukumu na historia. Tunaelezwa katika Waebrania 7:12, ***"Maana ukuhani ule ukibadilika hapana budi sheria nayo ibadilike."*** Mstari huu unatufundisha majukumu mbalimbali katika historia mbalimbali.

**Kuna Vipindi Vinne tangu Anguko la Adamu:**

1. **Kipindi cha Mataifa tangu Anguko la Adamu hadi Kutoka Misri**
Kipindi hiki kinazungumziwa katika Mwanzo na Ayubu. Na hiki kimekuwepo kati ya miaka 3900 K.K. hadi 1445 K.K.

2. **Kipindi cha Waisraeli tangu Misri hadi Kipindi cha Pentekoste**
Kipindi cha waisraeli kinaonekana katika Agano la Kale isipokuwa katika kitabu cha Mwanzo na Ayubu. Na pia kinasimama katika injili nne na Matendo 1, na pia kuna vitabu kama vya Isaya 61-66 na Ezekieli 40-48.

   Na tarehe zake ni kati ya 1445 K.K. hadi B.K. 33. Nyakati hizi pia zinaingiza vipindi vya kunyakuliwa kwa kanisa hadi kurudi kwa Yesu mara ya Pili na kipindi kinajulikana kama Dhiki kuu au majuma 70 ya Danieli. (Danieli 9:24-27).

3. **Kipindi cha Kanisa tangu Siku ya Pentekoste hadi Kunyakuliwa**
(Ni kipindi cha mateso na dhiki ambacho ni miaka saba ya Israeli itakayoisha kutoka kunyakuliwa kwa kanisa hadi kurudi kwa Yesu mara ya Pili.)

   Kipindi cha kanisa kimetazamwa katika Matendo 2–28, Nyaraka na Ufunuo. 2–3. Miaka ya dhiki na mateso inakamilisha miaka ya Waisraeli iliyo katika Ufunuo 4–19.

   Kipindi hiki kinaanza katika 33 na hakitakamilika hadi kunyakuliwa kwa kanisa.

4. **Kipindi cha Miaka Elfu tangu Kurudi kwa Yesu hadi Kwenye Kiti Kikubwa cha Enzi cha Hukumu**
Kipindi hiki kiko katika Ufunuo 20 na hata katika sura zingine kwenye Agano la Kale.

   Mgawanyo kwa kweli unaeleweka hasa pale tunapofikiri juu ya ukuhani ambao Mungu kaweka juu ya mtu. Kwa mfano kabla ya Israeli kuwa taifa la haki baada ya kutoka mwanadamu alikuwa katika “kipindi (mgawanyo) cha mataifa.” Ukuhani wa mgawanyo ulifanywa na wazee ndani ya familia moja na uliitwa ukuhani wa jamaa. Ulifanywa na Nuhu (Mwanzo 8:20), Ibrahimu (Mwanzo 22:2) na Ayubu (Ayubu 1:5). Sheria walizopaswa kuzifuata ni zile ***“zilizoandikwa mioyoni mwao”*** (Warumi 2:15).

   Muda mfupi baada ya kutoka kwa wayahudi katika nchi ya misri wakati wa kipindi cha mgawanyo wa Waisreli na kabila la Walawi liliitwa na Mungu kama ukuhani mpya na tofauti ambao ulikuja kuwa ukuhani wa walawi. Ukuhani huu ulifanyia kazi yake katika hema na baadaye katika hekalu. Kuhani wa kipindi kile alipaswa kutoa mnyama kama dhabihu kwa ajiri ya kufanyia ibada na hata kufikisha ujumbe wa neno la Mungu lakini kwa kutumia kanuni na misingi ya Musa aliyopewa na Mungu. Sheria walizozifuata ziliandikwa katika kitabu cha kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati. Kwa maneno ya ziada inafurahisha na inahuzunisha kwamba njia hizi ziliachwa kabisa wakati wa Yesu alipozaliwa kwamba desturi za dini zilikuwa za maana sana kuliko zilivyoonekana (Waebrania 10:8).

   Baada ya msalaba na kufufuka kwa yesu katika siku ya pentekoste Mungu alianza kizazi kingine kabisa na hiki kiliitwa kanisa la Agano Jipya. Katika kipindi cha mgawanyo huu kwa wale waliomwamini Yesu walikuwa ni wakuu kwa Mungu (1 Petro 2:5, 9). Kwa hiyo “waamini wakuu wapya” hawakutakiwa kutoa mnyama badala yake “***waliitoa miili yao iwe dhabihu hai takatifu inayompendeza Bwana kwa maana ndiyo ibada yao”*** (Warumi 12:1). Wakati huu ukuhani na maana yake ulibadilishwa kabisa. Dhabihu zote zilizotolewa zilimfikia Mungu lakini Mungu aliamua kubadili mfumo kabisa. Kanisa lilibidi lifuate sheria na kanuni (Yakobo 1:25; 2:12) “katika swala la upendo” (Warumi 13:8-10; Wagalatia 5:14; Yakobo 2:8).

   Utawala wa miaka elfu nao utakuwa na taratibu zake ambazo zitaongozwa na ukoo wa Zadoki wa kabila la Walawi (Ezekieli 40:46; 43:19; 44:15; 48:11). Sheria zitatwaliwa kwenye Agano Jipya la wana wa Israeli (Yeremia 31:31-33; Waebrania 8:8-10) na litawekwa na Bwana mwenyewe kwa sababu atakuwa mtawala wa mataifa yote. (Ufunuo 12:5).

   Kwa hiyo, fasili hizi zinatambulisha mabadiliko kwa njia ya namna fulani lakini msingi wake ni wa kiroho. Kwa mfano katika mgawanyo wetu huu wa majukumu hatuhitaji kutoa wanyama kwa Mungu wetu kama kumbukumbu kwa sababu tuna Bwana wetu Yesu (Waebrani 10:10). Badala ya kutoa wanyama kanisa lilianza kushiriki meza ya Bwana kama kumbukumbu (1 Wakorintho 11:23-34). Wakati wa utawala wa miaka elfu wanyama wataruhusiwa tena kama kumbukumbu ya kazi aliyoifanya Kristo katika msalaba. (Ezekieli 43:18-27).

Mgawanyo wa historia umepatikana kutoka katika mafunzo ya kujifunza maneno ya Mungu nab ado hayajatengenezwa bado. Kuna mitazamo mbalimbali ya muhimu inayoeleza mabadiliko toka kipindi hadi hadi kipindi. Hii haimanishi kanuni za vipindi katika nyakati ambazo Mungu anazo kwa watu wake bali ni majukumu ya watu wake katika historia.

Kuna namna ya kufuata mpango huu unaoweka mipango midogomidogo katika mipango mikubwa tunapaswa kuona kwamba mwelekeo huu unaharibu mambo fulani ya maandiko. Hii inaweza kuhusika katika kuhamasisha mihitasari na kuigeuza muhitasari katika ufafanuzi usiofaa. Kanuni hii inaweza kutupelekea kwenye sheria na ikatufanya tushindwe kumtumikia Mungu katika maisha yetu ya kikiristo. Kwa mfano, kukosa thamani katika hotuba za milimani kwa kanisa. Yesu alisema; kanuni hii ya Waisraeli iko tofauti na ile ya Paulo katika 1 Timotheo 6:3 kwamba mafunzo yanayofaa na maneno yanayofaa ni yale ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Tunachopaswa kufuata ni kanuni zile za migawanyo inayofaa, mifumo ya ukuhani imebadilika kupitia mafunzo ya Biblia, lakini kanuni zinazofanya kazi ziko palepale. Wakuu wote katika nyakati zote zimeamriwa kufuatwa ili zilete dhabihu kwa Bwana na kutufundisha Neno la Mungu.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu 3E

1. **Soma Waebrania 7:12. Ukuhani napobadilika je nini kinatakiwa kibadilike pia?**

2. **Soma Mwanzo 8:20, na Ayubu 1:5. Hii ni mifano ya ukuhani kipindi cha mataifa. Kinaitwa "Ukuhani wa Familia." Nani aliwajibika kutoa dhabihu?**

3. **Soma Warumi 2:15. Kipindi cha mataifa ni sheria ipi ilipaswa kufuatwa?**

4. **Soma Kutoka 28:1. H ni mfanowa kuhani kipindi cha Waisraeli. Ni nani anawajib wa kutoa dhabihu?**

5. **Soma kumbukumbu la Torati 4:44-46. Ni sheria ipi Waisraeli walipaswa kuifuata?**

6. **Soma 1 Petro 1:1-2 na 2:5, 9. Ni nani amabye ni khani katika kipindi cha kanisa?**

7. **Soma Warumi 13:8-10 na Yakobo 2:8. Ni sheria ipi makuhani wa kanisa wanapaswa kufuata?**

8. **Soma Ezekieli 40:46; 43:19; 44:15; na 48:11. Ni akina nani watatakiwa kuwa makuhani kipindi cha miaka?**

9. **Soma Waebrana 8:8-10. Ni sheria ipi itawaongoza kizazi hiki?**

10. **Makuhani wa kilawi walitoa wanyama. Na makuhani wakifalme walijitoa wenyewe. Nini tofati yake?**

**F. Kanuni ya Kumi na Nne: Kuwa Makini na Unabii**

Kanuni hii inaeleza utangulizi wa matukio uliomo katika Biblia. Biblia inatueleza kwa ufasaha kabisa kwamba unabii wa kweli ulitoka kwa watu walioijiliwa na Roho Mtakatifu na kwa hiyo hakuna unabii wa maandiko ambao mtu anaweza kuujenga na kuuleta yeye binafsi (2 Petro 1:19-21). Kumekuwepo na mambo mengi juu ya ufasiri wa unabii; na cha kuhuzunisha watu wengi wamepotoshwa na unabii kama huo. Kumbuka kwamba kama Mkristo sisi ni wakuu; kwa hiyo tunapaswa kuwa makini sana na unabii wa mtu au watu kama uko tofauti na maandiko unahitaji kuuchunguza kwa makini sana, kwani wengine wamekuwa wakitoa unabii ili wakubalike na kundi au jamii waliyonayo.

Tafsili ya unabii kwa kawaida inaleta picha kubwa ambayo kwa kweli ilikuwa imegawanywa katika vipande vingi mno na kufanywa kuwa moja. Picha inapokuwa iko tayari ni lazima tuuone uso wa Yesu ambaye yeye ni mwanzo wa Historia yote iliyopita, iliyopo na ijayo. Picha hiyo ya unabii ni lazima ilingane na maandiko na kuonesha ile kweli na lazima itoe uthibitisho katika udhahili na vizuri kukataa unabii usiolingana na maandiko ambao hauna hata chembe ndogo ya picha ya Yesu.

Masomo juu ya ufasiri wa unabii ni masomo marefu ambayo yanachukua kama ¼ ya maandiko matakatifu ya vitabu vya manabii. Kusudi letu katika somo hili tutaliangalia katika miongozo mitatu inayofuata.

1. **Angalia kama Nabii Anafasiri Unabii Wake**

Kwanza jaribu kuangalia kama nabii anatoa ufasiri katika unabii wake kama Yesu alivyofanya katika Yohana 2:19-21 kuhusiana na hekalu. Sura inasema:

> ***Yesu akajibu akawaambia livunjeni hekalu hili nami katika siku tatu nitalisimamisha basi wayahudi wakasema hekalu hili lilijengwa katika muda wa miaka arobaini na sita nawe utalisimamisha katika siku tatu lakini yeye alinena juu ya hekalu la mwili wake.***

Unabii mwingine kama huu ni rahisi kutafsili. Kwa sababu Mungu anaweza kufanya kitu ambacho ni cha miaka elfu kwa siku moja kama vile tunaweza kuona sura zingine zinazofanana fanana za Luka 4:18-21 na Isaya 61:1-2, ambazo Yesu alizisema kwetu.

2. **Chunguza Kama Unabii Unakamilika kwa Njia ya Historia**
   Ni lazima tuchunguze ili tuone kama sura zingine katika maandiko zitaweza kukamilisha unabii huu. Hii inatujulisha kwa usahihi ni unabii gani unaweza kuhitajika kukamilisha unabii huu katika siku zetu zijazo.

   Mfano hai wa kanuni hii ni gharika la Nuhu ambalo lilitabiriwa miaka 120 (Mwanzo 6:3). Na maandiko yanatueleza kwamba ulikamilishwa (Mwanzo 7-8).

   Maandiko pia yanatueleza kwamba Bwana atalikusanya taifa la Israeli kwa jinsi yake (Zekaria 9:14; Mathayo 24:31). Unabii huu bado haujakamilishwa. Kwa hiyo tunaona hii si kutoka katika maandiko bali katika historia.

   Tunahitaji kufasiri lugha kwa kurejea katika vitabu vya kihistoria ili kujua ni lini na vipi unabii utakamilika. Kumbuka kwamba historia ya dunia haijavuviwa na Mungu na kwa kweli historia ya kidunia haikubaliani kabisa na neno la Mungu kwa hiyo tunapaswa kujua hili.

3. **Tambua Lugha za Unabii**
   Katika unabii tunapaswa kuelewa namna za lugha (kama vile neno lililofasiriwa la “Simba wa kabila la Yuda” katika Ufunuo 5), alama (kaa vile “Dubu” katika Ufunuo 13), na aina (kama vile hema la duniani lililo katika Kutoka 25-40). Na hii inatakiwa iwe dhahili kwa kuangalia katika lugha za ufasiri wa unabii katika maandiko ili kujhua lugha za manabii zilivyo.

   Kumbuka kuwa kuhisi si kufasiri. Kuhisi kunakuwepo wakati mtu anapohisi juu ya lugha ya unabii. Ni rahisi sana mtu kupata msisimko na kuanza kutoa unabii na kuufanya kana kwamba ni kweli. Tunapaswa kuelewa kuwa lugha za manabii japo lugha zingine za manabii huwa hazieleweki (Danieli 12:4, 8-10) hadi pale wakati uliotabiliwa uwadie.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehem ya 3F

1. **Soma 2 Petro 1:19. Tangu Yesu alipozaliwa, akafa na akafufuka katika kukamilisha nabii je tnaweza kusema nini katika neno la unabii?**
2. **Soma 2 Petro 1:20. Nini mhimu wa unabii wa kweli?**
3. **Soma 2 Petro 1:21. Kwa nani na kwa kweli gani nabii hu ulitolewa?**
4. **Soma Luka 4:18-21 na Isaya 61:1-2. Yesu alikwa anasema nini kilichokuwa kikitokea wakati huo?**
5. **Soma Mwanzo 6-8. Unabii umetolewa katika 6:3. Je umekamilika?**
6. **Soma Isaya 7:14 na Mathayo 1:18-25. Je unabii huu ulikamilika?**
7. **Soma Yohana 14:1-3. Unabii umekamilika?**
8. **Soma 1 Wathesalonike 4:16-17. Unabii huu umekamilika?**
9. **Soma Zakaria 14:1-8. Unabii huu umekamilika?**
10. **Tafuta tofauti ya matukio yaliyooneshwa katika 1 Wathesalonike 4:16-17 na Zakaria 14:1-8.**
11. **Soma Ufunuo 5:4-6 orodhesha sura tofauti zilizotumika kumuonesha Yesu Kristo.**

# Sehemu ya 4
# Sheria ya Nne

**Ishi Maisha ya Kikristo kwa Kutumia Neno la Mungu**
Sheria hii inatoka moja kwa moja kwenye hotuba ya Yesu aliyoisema katika Yohana 7:17. Kama kweli tunahitaji kulijua neno la Mungu ni lazima tutende yale yaliyo katika neno lake. Kanuni hii inaonyesha uaminifu wa kushi katika maneno ya Mungu. Tunapaswa kuweka kando mambo yetu na kuangalia neno la Mungu kwa kwa uweza wa Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 2:14). Katika kutumia kanuni hii inahusiha roho ya mwanadamu, kwa mfano kutathimini utakatifu wa mawazo yetu na hisia zetu (2 Wakorintho 13:5).

Ni rahisi mno kwa sisi kuangalia mapenzi yetu na hisia zetu halafu tunazilinganisha na neno la Mungu ili kuthibitisha. Lakini sawa tunaweza kuthibitisha kwa sababu hali hii inatufanya kuwa vipofu kwa hiyo hata tutakavyofikiri tunadhania tuko sawa.

Kwa mfano mtu anaweza kuangalia matendo ya Daudi juu ya Bathsheba mke wa mtumishi mwaminifu (2 Samweli 11). Watu wengine wanaweza kutumia sura vibaya; jambo la rahisi la kusoma kabisa ni zile sheria amri kumi (Kutoka 20:1-17) ili kujua kuwa kuzini ni dhambi mbele za Mungu. Daudi aliwekwa kuwa mfalme kwa sababu neema ya Mungu ilionekana kwa sababu ya kutubu kwake (Zaburi 51).

**A. Kanuni ya Kumi na Tano: Matumizi Mazuri Yamejengwa juu ya Ufasiri Unaofaa**

Matumizi mazuri ya neno la Mungu hutoka katika matumizi mazuri ya kufasiri neno la Mungu. Kuna matumizi mengi lakini kuna ufasiri mmoja tu katika kila mstari. Kwa mfano, 1 Timotheo 3:1-7 inatupa mambo yanayofaa katika kanisa. Ufasiri huhusika na mtu kulingana na jinsi alivyo katika sehemu yake. Lakini matuzi yake yanaweza kuwahusisha hata wale ambao si waamini na yaliyoorodheshwa hapa chini yanawakilisha ubora unaofaa katika fasiri ambao unapaswa uwe kwa kila mshirika na hasa viongozi ili kujua maana ya unabii huo na ufasiri wake.

Matumizi mazuri ya neno la Mungu inamaana ya kwamba mtu katumia kanuni na misingi iliyokwisha tajwa na anatumia kwa uaminifu na na katika hali inayokubalika. Mtu anafikiri ufahamu wa Mungu kwa ajiri ya uhusiano mzuri yeye na Mungu chini ya Imani inayofaa na Neema ya Mungu. Na pia hata anweza kufikiri juu ya Yesu kwa nguvu za Roho Mtakatifu kupitia huduma ya Roho Mtakatifu.

Sura hizi ni mwongozo wa maisha ya mtu na wanafunzi wanatakiwa kufikiri juu ya neno la Mungu ili kwamba waishi maisha ya haki yanayompendeza Mungu na siyo kwa fikira na mitazamo yao wenyewe katika kufanya kila kitu.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehem ya 4A

1. **Soma 1 Timotheo 3:1-7 na uorodheshe sifa za kiongozi.**
2. **Kwa wale wanaotamani kuwa wachngaji waache wajipime kupitia mahitaji haya.**

**B. Hatua Tano za Matumizi Mazuri**

**Hatua ya 1:** Omba kwa ajili ya ufahamu sahihi na matumizi mazuri ya kanuni za kiroho (Yakobo1:5).

**Hatua ya 2:** Fikiri sana juu ya sura unayoisoma. Hii hujumuisha pamoja na kushirikisha mistari mingine katika neno la Mungu katika sentensi,sentensi katika aya na aya katika sura na sura katika vitabu vingine. (2 Timotheo 2:15).

**Hatua ya 3:** Jaribu kuruhusu ufasiri wa kiroho toka katika sura hizo. Mara nyingi neno la Mungu hulandana hata katika mazinigra na tamaduni zake. Kwa mfano uzinzi (tendo la ndoa nje ya ndoa) hii ni dhambi katika mazingira na hata tamaduni za kibiblia. Kwa hiyo kusudi na wazo la Biblia uzinzi hautakiwi (Warumi 13:8-10).

**Hatua ya 4:** Uaminifu ni kipimo chako kuona kama unatoka katika maandiko na kuhusisha upuuzi wako na maandiko. Hii huhusisha ufasiri mbaya sana mbele za Bwana (1 Yohana 1:9) na hata mwenendo wa kiimani (Wakolosai 2:6). Wanafunzi itakuwa vizuri kusoma Zaburi ya 51 na wanakili mambo fulani toka katika toba ya Daudi aliyoifanya juu ya dhambi aliyoifanya kwa Bethsheba (2 Wakorintho 13:5).

**Hatua ya 5:** Tembea katika neema na Imani. Mtume Paulo anatuambia ***"basi kama mlivyompokea Yesu Kristo Bwana enendeni vivyo hivyo katika yeye"*** (Wakolosai 2:6). Tumepokea kwa neema kwa njia ya imani (Waefeso 2:8-9) na hivyo hatuna budi kutenda matendo yanayolingana na neema tuliyoipokea (Waefeso 2:10).

## Kwa Masomo Binafsi: Sra ya 4, Sehemu ya 4B

1. **Soma Yakobo 1:5. Inatuambia tuombe kwa ajili ya nini?**

2. **Soma 2 Timotheo 2:15. Kipi ni lazima katika kuelewa na kuyatumia maandiko?**

3. **Kuhusu 1 Timotheo 3:1-7, Je nafikiri naweza kuchkua nini kama kamni za Kiroho?**

4. **Kwa kuwa sifa hizi zinahitajika na kiongozi je hazitakiiw kuwa na mumini yeyote?**

5. **Tathimini maisha yako kwa kutumia kanuni hizi.**

6. **Je kunaeneo lolote unalodhani kutubu mbele za Bwana labda umekwenda vibaya na limekuwa kama dhambi kwako, ikiwa ndiyo fanya hivyo.**

7. **Je kunaeneo ambalo nahisi kwamba unataka kbadili mwenendo wako wa Imani. Ikiwa ndiyo unakusudia kabisa?**

**C. Vipingamizi Sita vya Tafasiri Nzuri**

Yamkini kukawa na sababu nyingi zinazoleta au kusababisha ufasili mbaya wa neno la Mungu. Tutaangalia sababu sita tu zinazopotosha ufasili unaofaa. Kumbuka kwamba hakuna ambaye hakosei. Lakini ni busara kwa kuongeza kukumbuka maonyo aliyoyasema Paulo katika 1 Wakorintho 10:12, ***"Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke."***

**1. Mwili**

Kipingamizi cha kwanza ni mwili. Mwili kamwe hautendi yaliyo ya Mungu kwa sababu ni wenye dhambi (1 Wakorintho 3:3). Ina maana ya kwamba waamini wamechagua kutenda dhambi kwa sababu ya matendo ya mwili badala ya kuongozwa na Roho Mtakatifu na waone matunda yake (Wagalatia 5:19-23). Haya ni maisha ya bila kuungama dhambi (1 Yohana 1:9) na yamepungukiwa hata toba (2 Wakorintho 12:21).

Iwapo mtu anayejifunza neno la Mungu ataongozwa na matendo ya mwili, uasherati, uchafu, ufisadi, baada ya sanamu uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi na mambo yanayofanana na hayo (Wagalatia 5:19-21)–kwa kweli ufasili wa neno hili utakuwa ni mchafu mno. Kwa mfano, mwalimu ambaye ni mzinzi kwa kweli lazima tu hawezi kukubaliana na vifungu vinavyokataza uzinzi kamwe.

Kwa kuwa ukweli umedhihirishwa na Roho Mtakatifu (Yohana 16:13) na mtu wa mwili kaamua kufuata matendo ya mwili badala ya kukubali kuongozwa na Roho Mtakatifu hata basi kwa muda mfupi tu, lakini aeleza kuwa mtu wa mwilini kamwe ukweli juu ya neno la Mungu haupo, badala yake atakuwa akigeuza maandiko.

Mtu wa mwili ni sawa na mtu asili (1 Wakorintho 2:14), lakini wametofautiana kidogo. Mtu wa asili ni yule ambaye hajaamini ***"basi mwanadamu wa asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu maana kwake hayo ni upuzi wala hawezi kuyafahamu kwa kuwa yatambulikana kwa njia ya Roho"*** (1 Wakorintho 2:14). Mtu wa asili hana lolote mbele za Roho lakini mtu wa mwilini ni muumini lakini hana ushirika na Roho na kamwe hawezi kuyaelewa maneno ya mungu.

**2. Kiburi na Majivuno**

Kiburi ni kitu ambacho mtu anakuwa nacho na kinakuwa ndani ya mtu anayependa kusifiwa na watu. Kiburi na majivuno ni chanzo kikubwa cha kuyabadili maneno ya Mungu. Tumetahadharishwa katika Methali 16:18: ***"Kiburi hutangulia uangamifu, na roho yenye kutakabali hutangulia maanguko"*** huu ni ushauri mzuri kwa wafasiri.

Kwa kweli tunapaswa kujifunza neno la Mungu na "***tulishike lituongoze kabisa kwa usahihi"*** (2 Timotheo 2:15). Kujifunza kwetu kunapaswa kuongozwe na upendo wetu kwa Bwana na wengine (Marko 12:29-31), na siyo tu tusifiwe kwa ajili ya mambo yetu. Kujifunza kitu kipya kinachopanua uelewa wetu ni muhimu sana katika maisha ya kiroho lakini kama tutalitafiti neno la Mungu kwa sababu

ya mabo mengine ili kuwaridhisha wengine tutakuwa tuko katika pazia kwa sababu kamwe hatutatenda kama neno lilivyo.

Hatupaswa kujisifu kwa sababu ya matendo yetu na njia zile tunazozipata katika kuelewa neno la Mungu kwa sababu hii nitatutoa katika msingi mkuu unaofaa wa Roho Mtakatifu katika kulielewa neno la Mungu.

3. **Upendeleo wa Usomaji**
Kitu kingine ni ule upendeleo wa kusoma neno la Mungu kwa yale nayoyataka tu. Hii iko katika baadhi ya watu na hii hupelekea kulielewa neno la Mungu tofauti "sipendi kitu hiki kiwe hivi" sasa mawazo haya yakiwa na nguvu utakuta kwamba tunashindwa kulifafanua neno la mungu ipasavyo.

Jambo la kuhudhunisha kabisa watu wengine wamekuwa wakitumia mawazo yao potofu kwa kualinganisha na neno la Mungu hata kama Neno la Mungu linapingana na hicho.

> ***Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo hapana myahudi wala myunani hapana mfungwa wala huru hapana mtu mme wala mtu mke maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Yesu Kristo na kama ninyi ni wakristo mme kuwa uzao wa Ibrahimu na warithi sawasawa na ahadi zake.*** (Wagalatia 3:27-29)

Kama Mungu angelikuwa mpotoshaji pasingekuwepo na watakatifu waliookolewa ambao si wayahudi.

4. **Kutokuwa na Msimamo**
Tunapotaka kulitafasiri neno la Mungu lakini tunakosa msimamo hii nayo hupelekea katika kushindwa kuelewa maneno ya mungu.

a. **Jaribu Tathmini ya Binafsi na Toba**
Tunaelezwa katika 2 wakorintho 13:5 to, *"jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani jithibitisheni wenyewe!"* tunahitajika kupeleka si tu matendo yetu bali hata mawazo yetu tupate kuyapima kwa kiwango chake. Tunapojisikia hali ya kushindwa tunapaswa kumweleza Bwana na atusafishe. 1 Yohana 1:9 inasenma, *"tukiziungama dhambi zetu yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee na kutusafisha na udhalimu wote."* Tunaposhindwa kumpelekea Yesu mambo yetu ya kushindwa hii ndiyo ninasababisha sisi tulitafasiri neno la Mungu tofauti.

b. **Omba Bila Kukoma**
Tunaelezwa katika Mathayo 7:7-8, *"omba utapewa, tafuta utaona bisha utafunguliwa kwa kuwa kila aombaye hupewa na atafutaye huona na abishaye hufunguliwa"* tunapaswa kumwomba Mungu atusaidie katika kuelewa ili tusipotoshe neno lake. Tunaposhindwa kufanya hivi uhusiano wetu na Mungu unavunjika na hivyo hata neno lake unalotaka kulielewa huwezi kuelewa.

c. **Jifunze Bila Kukoma**
Tunaelezwa katika 2 Timotheo 2:15 kwamba jambo la muhimu katika kulibeba neno la mungu ni jitihada: *"jitahidi kujionesha kuwa umekubaliwa na Mungu mtenda kazi usiye na haja ya kutahayari ukilishika neno la kweli."* Kupungukiwa na kujifunza neno la Mungu inapelekea kushindwa kuelewa ni nini neno linasema.

5. **Dosari za Utaratibu**
Namna ya ufasiri pia hupelekea kushindwa kuelewa. Desturi zetu katika maandiko zitaathiri hata uelewa wetu. Kwa mfano kama tutashindwa kuelewa kuwa Biblia yote ina uvuvio wa Mungu (2 Timotheo 3:16-17), hivyo hata miujiza inayofanyika tuitashindwa kuielewa maana tutadhani ni aina fulani ya Sayansi au Uchawi, lakini kama tutaelewa kwamba Biblia ni kweli hivyo hata miujiza inayofanyika tutaiamini kulingana na Biblia.

Kuna watu wanaoamini kuwa kuna watu wachache waliobarikiwa katika kufasiri neno la Mungu. Biblia inasema wakristo wote ni makuhani (1 Petro 2:5, 9). Kama ni makuhani basi tuna sehemu katika kiti cha enzi cha Mungu (Waebrania 4:16), ambapo tutafundishwa moja kwa moja na Mungu Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 2:15).

Wengine huipotosha Biblia tu. "Allegory" ina maana ya kuweka tafsiri ngeni katika Biblia. Kama tutadhani kuwa ghalika la Nuhu lilikuwa nila dunia tu si kwamba kwa sababu ya Mungu basi tutakuwa na hatari kubwa kwa sababu hata Maandiko yamesema watu walihangaika na hivyo kama wanadamu tunapaswa kuvumilia hadi mwisho tunapokuwa katika shida ili tusiyageuze Maandiko na kuyapotosha.

"Mythology/Elimu ya asili" hii ina maana ya kuwa na ukweli mdogo na upotofu mkubwa. Kama tutafikiri kuwa gharika ya Nuhu ilikuwa ni kitu kidogo tutakuwa tukipotosha Biblia. Kwa kweli katika neno mythology maana yake ni kwamba, mtu anaweka ukweli mdogo na uongo unakuwa mwingi.

Na hii hata imeathiri sana katika kumfafanua Yesu, msalaba na hata kufufuka kwake. Kama kweli ingekuwa hivyo basi Yesu asingelikufa kwa ajili ya dhambi zetu, hata asingelizikwa wala kufufuka kwa ajili ya kutuokoa. Kulingana na mtume Paulo tuko katika shida kubwa kama matukio haya yasingelitokea (1 Wakorintho 15).

Njia ya kujiona kwamba wewe ni mtakatifu pia haiwezi kukusaidia katika kufasiri. Kwa mfano kitabu cha Wimbo Ulio Bora ni kazi ya uandishi wa asili ambayo haileti maana yoyote. Na hii tutaiona zaidi baadaye.

6. **Sababu Zisizo za Msingi**
Fikra za mwanadamu kamwe haziwezi kumweleza Mungu sawasawa. Kama tungeweza kumtambua Mungu kwa mawazo ya kibinadamu basi tungejisifu sana. Tunaelezwa katika Methali 3:5-7 kwamba, ***"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote wala usitegemee akili zako mwenyewe katika njia zako zote mkiri yeye naye atayanyosha mapito yako usiwe mwenye hekima machoni pako mche Bwana ukajiepushe na uovu."*** Mungu anataka tutembee kwa imani na si kwa uelewa wetu.

Tumekwisha kuahidiwa kwamba siku moja tutamjua Bwana. Paulo aliandika katika 1 Wakorintho 13:12, ***"Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo wakati ule tutaona uso kwa uso wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana."*** Maswali yote ambayo yatakuwa hayajajibiwa sasa siku ile yatajibiwa tutakapoonana uso kwa uso na Bwana wetu (2 Wakorintho 3:18).

Wayahudi wa kwanza walikuwa na matatizo na ikapelekea katika upotofu mwingi wa kutomwelewa Yesu kama masihi. Hebu fikiri juu ya mazungumzo kati ya Yesu na Mafarisayo yaliyoratibiwa katika Mathayo 22:41-46:

> ***Na Mafarisayo walipokusanyika, Yesu aliwauliza, akisema, 'Mwaonaje katika habari za Kristo? Ni mwana wa nani?' Wakamwambia, 'ni wa Daudi' Akawauliza, 'imekuwaje basi Daudi katika Roho kumwita "Bwana" akisema, Bwana alimwambia Bwana wangu, "uketi mkono wangu wa kuume, hata niwawekapo adui zako kuwa chini ya miguu yako?" Basi Daudi akimwita "Bwana", imekuwaje ni mwanawe wala hakuweza mtu kumjibu neon?'; wala hakuthubutu mtu yeyote tangu siku ile kumwuuliza neno tena.***

Yesu alisema katika Zaburi 110:1, akiwauliza Mafarisayo imekuwaje hata Masihi awe "mwana" wa Daudi? Na halafu awe "Bwana" wa Daudi? Jibu ni hili Masihi ni Mungu na ni fikra hii ndiyo tatizo katika fikira za watu na ndivyo ilivyo.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 4, Sehemu ya 4C

1. **Soma 1 Wakorintho3:3. Ni vitu gani viwili ambavyo palo alivionesha kama sehemu ya kuwa " wa Mwili"**
2. **Soma Wagalatia 5:19-21. Wivu nasemwa kuwa ni nini ?**
3. **Je mtu wa wivu anawezaje kbadili katika kulitafasiri Neno?**
4. **Soma Methali 3:5-6 na 1 Wakorintho 8:1. Mambo gani hatupaswi kyatmaini na kwa nini?**
5. **Je twaweza kuwa wakaidi katika kujifnza kwetu neno au ktokana na njia zetu za kujifunza neno na kwahiyo kuwa watu wa mwili na hata kukosea kulifasiri neno ipasavyo?**
6. **Je tunapaswi kulitafasiri neno kulingana na tamaa zetu? Kwa nini?**
7. **Ni kitu gani cha maana katika kujifunza Neno la Mungu?**
8. **Soma 2 Wakorintho 13:5 na 1 Yohana 1:9. Mambo gani mawili niyamhimu katika kusoma kwetu Neno la Mungu?**

9. **Soma Mathayo 7:7-8 na Yakobo 1:5. Tnatakiwa kutafuta nini katika kujifunza kwetu Neno la Mungu?**

10. **Kwa nini tunapasw kudmu katika Neno?**

11. **Soma 2 Timotheo 3:16-17. Tnapaswa kuamini nini kuhusu Biblia kabla hata ya kuanza kuitafasiri?**

12. **Soma Isaya 55:8-9. Tnapaswa kukumbuka nini hata kabla hatjaweka mawazo ya wanadam katika Neno la Mungu?**

13. **Soma Yakobo 3:14. Ni mambo gani matatu yanapelekea kushindwa kulitenda neno la Mungu.**

## D. Njia Nane za Matumizi Mabaya

Njia hizi zimeelezwa kwa urahisi kabisa, lakini lazima zitazamwe na wanafunzi wa neno la Mungu kwa sababu kuna mambo ndani yale ambayo yanaweza kupinga. Ni lazima sasa tuone mstari huu kama mwongozo Methali 3:5-6 inasema, ***"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote wala usizitegemee akili zako mwenyewe katika njia zako zote mkiri yeye naye atanyosha mapito yako."***

1. **Kushindwa kumtegemea Bwana ili akuimarishe katika kutenda.**

2. **Upingamizi wa mtazamo au matendo yanayoharibu ukweli wa Mungu.**

3. **Kutotii kanuni zinazofahamika zilizo kweli na sahihi.**

4. **Kupotosha kiwango cha maneno ya Mungu.**

5. **Kushindwa kupenda kutenda maneno ya Mungu katika maisha yako.**

6. **Kutenda dhambi ukifikiri kuwa hii ni ndogo na hii ni kubwa nitasamehewa.**

7. **Kuruhusu hisia zako ukifikiri kuwa ni sahihi katika kuamua.**

8. **Upungufu katika kufikiri kunakosababishwa na kutokuwa na juhudi katika kufuatilia maneno ya Mungu na kuchukulia urahisi rahisi.**

## Sura ya 5

# Mafundisho juu ya Nafsi ya Mungu

# <u>Sehemu ya 1</u>
# Utatu Mtakatifu

**A. Maanay ya Utatu**

Tunaamini kwamba kuna Mungu mmoja tu (Kumbukumbu la Torati 4:35; 6:4; 1 Wakorintho 8:4-6; Waefeso 4:3-6; Yakobo 2:19) ambaye alijionyesha kama Baba (Yohana 6:27) Mwana (Yohana 1:1) na Roho Mtakatifu (Matendo 5:3-4). Kwa kweli uhalisi wa Mungu kabisa tumeshindwa kuuelewa.

Ni vigumu kueleza kabisa uhalisi wa utatu kwa sababu ni kwamba Mungu yuko nje kabisa na ufahamu wetu na hii ni kwa sababu yeye ni Mungu. (Warumi 11:33). Mwenendo wetu wa kikristo unapaswa kuwa ni wa imani ili tumpendeze (Webrania 11:6). Ni jambo la muhimu sana kumjua Mungu lakini katika uelewa wetu na kila kitu kinapaswa kumjua Mungu. Siku hizo tuliweza kumjua Mungu (1 Wakorinto 13:12), lakini kwa sasa tunapaswa kumkubali kwa njia ya imani jambo ambalo ni gumu sana katika uelewa wetu. Mfano mmoja wapo wa utatu unaonekana katika Yai. Lina ngozi ngumu yaani gamba lake, lina kiini na lile yai jeupe na bado linabaki kuwa yai moja.

Katika mfano huu tunaona kwamba utatu una mambo makuu matatu. Baba ni mpangaji wa mambo (Matendo 2:23), mwana ni yule anayetekeleza mipango ya Baba (Yohana 5:36); na Roho Mtakatifu ni Yule anayeonesha na kujidhihirisha (Yohana 16:13). Tunapokuwa tunajifunza tofauti zao hatupaswi kuugawa utatu. Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wote hawa wanasifa moja ambayo ni ya Mungu.

Hii isiwe tatizo kwetu. Kamwe hatuwezi kuelewa utendaji kazi wa ndani katika gari lakini tunaona matokeo tunapokuwa tumeliwasha na kuliendesha. Hivyo twaweza kuona matokeo ya uasili wa Mungu kwa yale aliyoyaumba na kuyafanya. (Warumi 1:20).

**B. Uhakika**

Uhakika wa Utatu unaonekana katika kweli kwamba Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wote hawa wanaitwa ni Mungu mmoja kama tulivyoeleza hapo juu. Katika Baba, Mwana na Roho matakatifu kuna mambo yale yale ambayo Mungu huyafanya na hivyo ieleweke kwamba hawa watatu ni Mmoja ambaye ni Mungu kamili.

Katika sura ya nne sehemu ya 1 Tafuta ukweli juu ya Mungu. Uasili wa Mungu umeonekana. Hatutaweza kueleza sifa za Mungu na kuzioanisha na Utatu wake.

Hii ni sehemu nzuri ya kujifunza. Mistari hii miwili inaweka misingi ya Biblia kwa njia ya theologia kwa hiyo wanaojifunza neno la Mungu hawataweza kusahau. Msingi wa kwanza ni kuna mmoja na Mungu mmoja tu na msingi wa pili ni mimi si Yeye.

**C. Sifa Kumi za Mungu**

Mabano ya kwanza ( ) yataonyesha mistari inayomhusu Baba Mungu na yale ya pili < >, yataonyesha Mwana na haya ya tatu [ ], Roho Mtakatifu.

**1. Enzi**

Mungu ni ENZI, ina maana ya kwamba yeye ni mfalme na anatenda kama anavyopenda. (Danieli 4:17; 1 Timotheo 1:17; Zaburi 47:2, 7), <Ufunuo 19:16; Yohana 5:21,> [Zekaria 4:6; 1 Petro 4:14; 1 Wakorintho 12:11].

Enzi ina maana ya kwamba ni kitendo cha kuwa na mamlaka katika mambo. Mungu, haendeshwi, yeye ana mamlaka na vitu vyote alivyoviumba. Ni muumbaji, wala hakuumbwa (Warumi 1:20,25).

Mungu ana mamlaka ya kufanya yale anayoyafikiri katika mipango yake, sheria zake na hata katika hukumu zake. Kwa ufupi hufanya kama anavyotaka japo wakati mwingine makusudi yake huwa ni mazito kuyaelewa.

**2. Haki**

Mungu ni HAKI ina maana kuwa yeye ni mkamilifu katika njia zake. (Yohana 17:25; 1 Yohana 1:5), <1 Yohana 2:1; Luka 1:35; Waebrania 7:26 >, [Isaya 32:15-18; Zaburi 143:10; Nehemia 9:20]. Yeye Mungu ni wa haki zote ni mkamilifu na anaonesha kiwango ambacho hata sisi hatuna budi kukiiga (Waefeso 5:1).

**3. Mwaminifu**

Mungu ni MWAMINIFU. Yeye ni mwaminifu kabisa (Isaya 45:21; Ayubu 37:23), <Yohana 5:22, 30; Ufunuo 19:11>, [Isaya 4:4; 28:6]. Uhuru wa Mungu ni mwitikio katika haki yake. Mungu hamwogopi

wala kumweshimu Mtu (Warumi 2:11), hababaishi. Palipo na dhambi lazima uaminifu na haki yake vidhihirike (Warumi 5:13),

Mwanadamu hawezi kutenda haki ya Mungu na hivyo anamwitaji Masihi wa kumwezesha kuitenda haki ya Mungu. Yesu pale msalabani alikamilisha hii alipokufa kwa ajiri ya kulipa dhambi za ulimwengu (1 Yohana 2:1-2).

4. **Upendo**

Mungu ni UPENDO ina maana kuwa upendo wake ni kamili wala hauelezeki. (1 Yohana 4:8-10; Tito 3:4; Yohana 17:24-26), <Yohana 15:9>, [Wagalatia 5:22].

Sifa hii ya Mungu inadhihirisha alipomtuma mwana wake wa pekee kuuokoa ulimwengu (Yohana 3:16). Upendo ndiyo sababu iliyomfanya Yesu awe msalabani ili apate kulipa deni za dhambi zetu <Luka 23:34>; na ni kitu cha kwanza katika matunda ya Roho Mtakatifu [Wagalatia 5:22].

Upendo una maana ya kufanya kilicho sahihi kwa watu wengine hata kama hautaki wala hujisikii. Wakristo ni lazima wawe na upendo huu wa Mungu na wausambaze kwa watu wengine ili wapate kumjua Mungu. (Yohana 13:34-35).

5. **Uzima wa Milele**

Mungu ni UZIMA WA MILELE kwa sababu yeye amekuwepo kabla ya kila kitu hapa duniani. (Isaya 57:15), <Yohana 8:54; 1 Yohana 5:11-12; Mika 5:2; Ufunuo 1:8, 17>, [Waebrania 9:14].

Uzima wa milele hauna mwanzo wala mwisho. Sisi kama wakristo tuna uzima wa milele ulio na mwanzo lakini hauna mwisho. Umilele wa Mungu unatufundisha kwamba yeye hatakufa wala hategemei kufa.

6. **Mwenye Nguvu Zote (Omnipotent)**

Mungu ni NGUVU, ina maana ya kwamba yeye anaweza kufanya chochote kile. (Marko 14:36; 1 Petro 1:5), <Mathayo 28:18; Ufunuo 19:6>, [2 Timotheo 1:7; Warumi 15:13].

Mfano wa nguvu zake unaonekana katika uumbaji wa mbingu na nchi (Mwanzo 1:1). Tunaambiwa kwamba Neno la kinywa chake liliumba mbingu na pumzi yake ikawa juu ya kila kitu (Zaburi 33:6).

7. **Yuko Sehemu Zote (Omnipresent)**

Mungu ni SEHEMU ZOTE ina maana ya kwamba yeye hupatikana popote kwa wakati mmoja. (Methali 15:3; 2 Nyakati 2:6), <Mathayo 18:20; 28:20>, [Zaburi 139:7-16]. Hii haina maana kwamba Mungu ni kila kitu (Pantheism), lakini yuko sehemu zote na hii inatuonesha uasili binafsi wa Mungu.

Tunaona pia katika sifa hii kwamba Mungu hajitengi katika maeneo (Zaburi 139:7-17). Yeye hapungui kwa wengine halafu aongezeke kwa wengine. Kwa hiyo yeye yupo mahali pote na huonekana mara moja katika sehemu zote kwa wakati mmoja.

8. **Anajua Yote (Omnscient)**

Mungu ANAJUA YOTE anajua kila kitu yaliyopita, yaliyopo na yajayo (Zaburi 139:1-6; Waebrania 4:13), <Yohana 2:24,25; 18:4; Mathayo 9:4 >, [1 Wakorintho 2:10-11; Isaya 11:2].

Mungu anajua matokeo ya kila kitu na si asili yake tu ila hata uwezo wake. Anajua hadhara yote katika vipindi vyote na maamuzi ya kila kitu yatakayokuja. Na mipango yake ya milele imeyafanya haya yote (Warumi 8:28-30).

9. **Habadiliki (Immutable)**

Mungu HABADILIKI ina maana tangu mwanzo ndivyo alivyo. (Yakobo1:17; Webrania 6:17; Malaki 3:6), <Waebrania 13:8>, [1 Wakorintho 12:4; Waefeso 1:13].

Sifa hii ni faida kwa mwanadamu kwa sababu Mungu mara zote hufanya kile alichoahidi. Habadili nia na akili zake tangu aliposema ***"Hakuna hukumu tena kwao walio katika Kristo Yesu"*** (Warumi 8:1), hii inatutia moyo kwamba yeye hatabadili tena akili zake. Aliahidi uzima wa milele kwa wale wanaomtumaini Bwana na hivyo tunajua kabisa kwamba hatabadilika (Yohana 3:16). Kama Mungu atabadili ahadi zake atakuwa ni mwongo na si mwenye haki (Waebrania 6:17-18).
Kila kitu duniani hubadilika lakini Mungu ni yule yule na hii ndiyo ngao yetu katika Roho zetu (Waebrania 6:19).

10. **Mkweli**
Mungu ni MKWELI. (Kumbukumbu la Torati 32:4; Yohana 7:28; 17:3), <Yohana 14:6; 1 Yohana 5:20>, [1 Yohana 5:7, 8; 4:6; Yohana 14:17; 15:26; 16:13].

Sifa hii inatueleza kabisa kwamba kila kitu ambacho Mungu anatuambia ni amina na ni cha kuaminika (Hesabu 23:19). Mungu hadanganyi (Tito 1:2).

Ukweli ni kwamba Mungu alijidhihirisha katika mwili wa Yesu Kristo <Yohana 14:6>. Katika historia yote ukweli umeonekana katika mawazo, maelezo na hata kanuni zake. Kwa hiyo katika hili jambo lolote mwanadamu analoliamini lazima alilinganishe na neno la Yesu <1 Timotheo 6:3>.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 5, Sehemu ya 1

1. **Kwanza soma Kumbukumbu la Torati 6:4-5. Halafu soma Yohana 6:27, Yohana 1:1, na Matendo 5:3-4. Kuna Mungu wangapi wa kweli katika mistari hiyo?**

2. **Kutokana na vifungu hapo ju Mungu ni nani ?**

3. **Soma Matendo 2:23. Ni nini jukumu mhimu la Baba?**

4. **Soma Yohana 5:36. Ni nini jukumu la muhimu la Mwana?**

5. **Soma Yohana 16:13-14. Ni nini jukumu la Roho Mtakatifu?**

6. **Tnawezaje kuthibitisha kwamba Baba, Mwana na Roho Mtakatif kwamba wote ni Mungu mmoja?**

7. **Soma sura zifuatazo kuhusu mamlaka ya Mungu:**
   a. Baba–Danieli 4:17; 1 Timotheo 1:17 na Zaburi 47:2, 7
   b. Mwana–Ufunuo 19:16 na Yohana 5:21
   c. Roho Mtakatifu–Zakaria 4:6; 1 Petro 4:14 na 1 Wakorintho 12:11

   **Je Utatu unamamlaka?**

8. **Soma sura zifuatazo kuhusu Mungu mwenye Haki:**
   a. Baba–Yohana 17:25 na 1 Yohana 1:5
   b. Mwana–1 Yohana 2:1; Luka 1:35 na Waebrania 7:26
   c. Roho Matakatifu–Isaya 32:15-18; Zaburi 143:10 na Nehemia 9:20

   **Je Utatu una Haki?**

9. **Soma sra zifuatazo kuhusu Mungu Mwaminifu:**
   a. Baba–Isaya 45:21 na Ayubu 37:23
   b. Mwana–Yohana 5:22, 30 na Ufunuo 19:11
   c. Roho Mtakatifu–Isaya 4:4 na 28:6

   **Je utatu ni Uaminifu?**

10. **Soma sura zifuatazo kuhusu upendo wa Mungu:**
    a. Baba–1 Yohana 4:8-10; Tito 3:4 na Yohana 17:24-26
    b. Mwana–Yohana 15:9
    c. Roho Mtakatif–Wagalatia 5:22

    **Je Utatu namiliki Upendo kamili?**

11. **Soma sura zifuatazo kuhusu uzima wa milele wa Mungu:**
    a. Baba-Isaya 57:15
    b. Mwana–Yohana 8:54; 1 Yohana 5:11–12; Mika 5:2 na Ufunuo 1:8, 17
    c. Roho Mtakatifu–Waebrania 9:14

    **Je utatu unauzima wa Milele?**

12. **Soma sura zifuatazo kuhusu Nguvu za Mungu:**
    a. Baba - Marko 14:36 na 1 Petro 1:5
    b. Mwana - Mathayo 28:18 na Ufunuo19:6
    c. Roho Mtakatifu –2 Timotheo 1:7 na Warumi 15:13

    **Je utatu na Nguvu?**

13. **Soma sura zifuatazo kuhusu Mungu yu Sehemu zote:**
    a. Baba–Methali 15:3 na 2 Nyakati 2:6
    b. Mwana–Mathayo 18:20 na 28:20
    c. Roho Mtakatifu– Zaburi 139:7-16

    **Je utat uko sehemu zote?**

14. **Soma suza zifatazo kuhusu Mungu anajua yote:**
    a. Baba–Zaburi 139:1-6 na Waebrania 4:13
    b. Mwana–Yohana 2:24-25; 18:4 na Mathayo 9:4
    c. Roho Mtakatifu–1 Wakorintho 2:10-11 na Isaya 11:2

    **Je Utatu unajua yote?**

15. **Soma sra zifuatazo kuhusu Mung habadiliki:**
    a. Baba–Yakobo 1:17; Waebrania 6:17 na Malaki 3:6
    b. Mwana–Waebrania 13:8
    c. Roho Mtakatifu–1 Wakorintho 12:4 na Waefeso 1:13

    **Utatu haubadiliki?**

16. **Soma sura zifuatazo kuhusu Ukweli wa Mungu:**
    a Baba–Kumbkmbu la Torati 32:4; Yohana 7:28 na 17:3
    b. Mwana–Yohana 14:6 na 1 Yohana 5:20
    c. Roho Mtakatifu–1 Yohana 5:7-8; 4:6; Yohana 14:17; 15:26 na 16:13

    **Je utatu ni wa Kweli?**

# Sehemu ya 2
# Majina ya Mungu

Sehemu hii inamulika na kuonyesha majina ya Mungu yaliyo katika Maandiko. Kuna majina ya aina mbalimbali katika Lugha ya kiyunani na hata Kiebrania na haya yote yanahusika katika kuitisha na kuonesha utofauti wa sifa zake na mitazamo yake.

Katika tafasiri zingine za kiebrania na kiyunani maneno yamehamishwa hadi kwenye lugha mpya inayojulikana (transliteration) kulingana na matamshi yake bila kuangalia msaada wa kuyaelewa. Somo hili linamsaidia mwanafunzi majina yote mawili kwa kiebrania na kiyunani na tafasiri zake.

**A. Majina ya Kiebrania**

**1. Mungu**

Neno la kiebrania lilitafasiri neno "Mungu" kuwa ELOHIM. Linaonekana katika Mwanzo 1:1 na zaidi ya mara 2,500 katika Agano la Kale. Maana ya neno hili linahusisha uasili wa Mungu na kuonesha mtazamo wake kwa mara moja. Wakati mwingine neno hili lilitumika kueleza kama baba, na wanafunzi nafikiri watajua kuwa pia lilihusika katika kueleza Mwana na Roho Mtakatifu kwa sababu Utatu ni Mungu mmoja.

ELOHIM ni wingi (ina maana ya kitu zaidi ya kimoja) lililoelezwa kama ufahari wa Mungu na ukuu wake. Neno hili japo kuwa liko katika wingi lakini linajumuisha umoja na hapohapo linaonyesha kuwa yupo lakini ni Mungu mmoja (Kumbukumbu la Torati 6:5).

Neno ELOHIM limeunganishwa katika neno jingine linalotupa habari zingine kuhusu Mungu na inakuja kuwa jina jingine la kwake.

**a. Mungu Mwenye Nguvu**

"Mungu Mwenye Nguvu" ni tafasiri ya kawaida ya neno EL SHADDAI. "EL" Ni kifupi cha neno ELOHIM. Ilitumika kueleza Baraka alizokuwa akiweka Mungu juu ya watu wake. Linaonekana katika : Mwanzo 17:1; 28:3; 35:11; 43:14; 48:3; 49:25; Kutoka 6:3; Hesabu 24:4,16; Ruthu 1:20, 21; Job 5:17; 6:4, 14; 8:3, 5; 11:7; 13:3; 15:25; 21:15, 20; 22:3, 17, 23, 25, 26; 23:16; 24:1; 27:2, 10, 11, 13; 29:5; 31:2, 35; 32:8; 33:4; 34:10, 12; 35:13; 37:23; 40:2; Zaburi 68:14; 91:1; Isaya 13:6; Ezekieli 1:24; 10:5; Yoeli 1:15

**b. Mungu Aliye juu**

"Mungu Aliye juu" ni tafasiri ya EL ELYON, inaonesha mamlaka katika mambo yote. Inaonekana katika: Mwanzo 14:18, 19, 20, 22; 40:17; Hesabu 24:16; Kumbukumbu la Tolari 26:19; 28:1; 32:8; Yoshua 16:5; 2 Samweli 22:14; 1 Wafalme 9:8; 2 Wafalme 15:35; 18:17; 1 Nyakati 7:24; 2 Nyakati 7:21; 8:5; 23:20; 27:3; 32:30; Nehemia 3:25; Zaburi 7:17; 9:2; 18:13; 21:7; 46:4; 47:2; 50:14; 57:2; 73:11; 77:10; 78:17, 35, 56; 82:6; 83:18; 87:5; 89:27; 91:1, 9; 92:1; 97:9; 107:11; Isaya 7:3; 14:14; 36:2; Yeremia 20:2; 36:10; Maombolezo 3:35, 38; Ezekieli 9:2; 41:7; 42:5.

**c. Mungu wa Milele**

Neno "Mungu wa Milele"ni tafasiri ya EL OLAM. Neno la Kiebrania OLAM ni zuri sana lenye maana ya milele (yaani halina mwanzo wala mwisho) kuliko ile ya wakristo ya (kuwa na mwanzo bila mwisho). Liko katika Mwanzo 21:33 na Isaya 40:28. umilele wa Mungu umeonekana mara nyingi hasa palipo na neno milele (OLAM)

**2. Bwana**

YAHWEH ni neno lililotafasiriwa kama "BWANA" Kwa Herufi kubwa ili kwamba lipate kutofautishwa na maneno mengine yenye maana sana na hili yaani "Bwana." YAHWEH limejumuishwa na maneno mengine ili kueleza ukuu wake.

Jina la Mungu "BWANA" ni tafasiri ya kiebrania yaani YAHWEH. YAHWEH ni jina Mungu (Kutoka 3:14) na limetumika zaidi ya 5,300 katika Agano la Kale. Linaonesha ukuu wa Mungu. Na matumizi ya kwanza ya neno Bwana yanaonekana katika kitabu cha Mwanzo 2:4 ambapo limeunganishwa na neno ELOHIM na likatafsiriwa kama BWANA MUNGU.

Jina Mungu lilikuja kuwa na maana sana katika Israeli baada ya kuhamishwa toka uhamishoni Babebli (586-516 K.K.); hawakuweza kumwita jina lake ila walimwita ADONAI. Wakati wa karne ya sita na ya saba B.K. ilabu za ADONAI zilijumuishwa na herufi za YHWH na zikaleta neno "Yehova" kumkumbusha msomaji kutamka YHWH kama ADONAI.

**a. Bwana Atatoa**
"BWANA atatoa" ni tafasiri ya neno YAHWEH YIREH. Na hii iko katika Mwanzo 22:14 na inahusika kipindi cha Ibrahimu Bwana alipompa Beberu la kondoo alipotaka kumtoa mwanae Isaka kama dhabihu.

**b. Bwana ni Bendera yangu**
"BWANA ni Bendera "ni tafasiri ya neno YAHWEH NISSI. Na iko katika Kutoka 17:15 na hii aliisema Musa baada ya kuwashinda Waamaleki.

**c. Bwana ni Amani**
Neno "Bwana ni Amani" ni tafasiri ya YAHWEH SHALOM. Lilitumika katika Waamuzi 6:24.

**d. Bwana wa Majeshi**
"BWANA wa Majeshi" ni tafasiri ya YAHWEH SABBAOTH, ni neno la kijeshi lenye maana ya Bwana ni Komandoo wa jeshi zima la malaika na hata Israeli yote. Na lilitumika kwa mara ya kwanza katika 1 Samweli 1:3 na hli liko zaidi ya mara 100 katika Biblia.

**3. Bwana, Mkuu, Mmiliki**
ADONAI ni neno lenye wingi kama ELOHIM, linaloeleza ukuu wa Mungu. Hata hivyo neno ELOHIM, liko katika umoja kama ADON. Neno ADON linamaanisha "Bwana" likiwa na maana ya mkuu au mmiliki. Linatumika kuonyesha mamlaka. Limetumika kwa mara ya kwanza katika Mwanzo 18:3 ambapo Ibrahimu alilitumia kumwonesha Bwana.

Neno sawa kwa kiyunani ni KURIOS.

**B. Majina Ya Kiyunani**

**1. Mungu**
Neno Mungu kwa kiyunani ni THEOS. Kama vile neno la kiebrania ELOHIM, jina hili linaonyesha mtazamo wa Mungu kwa wakati mmoja. Ni neno la pekee lilichaguliwa kueleza neno ELOHIM kwa kiyunani.

Katika Yohana 1:1, ambalo kwa usahihi linaeleza na kukusanya Mwanzo 1:1, tunaona neno THEOS lililotumika badala ya ELOHIM, linahusisha na kueleza uhusiano mzuri.

**2. Bwana**
Neno Bwana kwa kiyunani ni KURIOS. Neno hili limetamkwa mara 700 katika Agano Jipya na linafafanua ukuu wa Bwana na mamlaka yake. Na pia neno hili hutumika katika kuonyesha heshima ya Mungu.

Tumeona katika masomo yaliyopita kwamba THEOS na neno ELOHIM yana maana sawa kabisa. Tutaona pia KURIOS na YAHWEH yana maana sawa pia. katika Marko 11:9, mwandishi anarejea kitabu cha Zaburi 118:26, inayosema ***"Na abarikiwe yeye ajaye kwa jina la Bwana"*** neno la Kiebrania katika Zaburi 118 ni YAHWEH wakati neno lililotumika katika kutafasiri ni KURIOS.

**3. Mkuu**
"Mkuu" ni tafasiri ya neno DESPOTES, japo wakati mwingine lina maana sawa na Bwana (Luka 2:29; Matendo 4:24). "Mkuu" limaanisha hali ya kutawala na ni zaidi ya mamlaka kama ilivyo katika KURIOS. Linaonekana katika: 1 Timotheo 6:1, 2; 2 Timotheo 2:21; Tito 2:9; 1 Petro 2:18; 2 Petro 2:1; Yuda 1:4; Ufunuo 6:10.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 5, Sehemu ya 2

**1. Oanisha majina haya ya Mungu ya Kiebrania na neno la kiebraba lenye maana sawa na Jina:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a. | MUNGU | 1) | YAHWEH SABBAOTH |
| b. | Mungu mwenye Nguvu | 2) | YAHWEH NISSI |
| c. | Mungu aliye juu | 3) | ELOHIM |
| d. | Mungu wa Milele | 4) | ADONAI |
| e. | BWANA | 5) | EL SHADDAI |
| f. | BWANA atatoa | 6) | YAHWEH SHALOM |
| g. | BWANA ni bendera yangu | 7) | EL OLAM |
| h. | BWANA ni Amani | 8) | EL ELYON |
| i. | BWANA wa Majeshi | 9) | YAHWEH |
| j. | BWANA, MKUU, MMILIKI | 10) | YAHWEH JIREH |

**2. Oanisha majina ya Mungu wa kiyunani kwa kuangalia neno la Kiyunani lililo sahihi:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a. | MUNGU | 1) | KURIOS |
| b. | BWANA | 2) | DESPOTES |
| c. | MKUU | 3) | THEOS |

# Sehemu ya 3
# Mungu Baba (Paterology)

**A. Nafsi Yake**

Njia nzuri ya kumweleza Baba ni kuangalia namna alivyojidhihirisha katika neno lake. Katika somo letu la utatu ni kama tumekwisha maliza kwa sababu tuumeona kwamba Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni kitu kimoja. Sasa tutajifunza maelezo yaliyomo katika Biblia yanayotufunza sisi juu ya Baba wetu mbinguni.

Na lakini elewa kuwa japo kunautofauti katika utendaji kazi wa Roho Mtakatifu Mwana na Baba lakini bado ni Mungu mmoja (Kumbukumbu la Torati 6:4). Mara nyingi katika Maandiko Matakatifu ni vigumu kutofautisha mshirika wa utatu hasa alivyo katika mistari ya Biblia. Ugumu huu lazima uchukuliwe kama ulivyo kwa sababu Mungu hawezi kugawanywa au kutengwa katika Utatu wake (Yohana 10:30;14:9). Katika mtazamo wa nafsi ya Mungu Baba maneno na sura zimechanganuliwa ili kuwezesha uelewa wetu tupate kumfahamu kuwa yeye ni nani.

Mara nyingi neno la kueleza kama vile “yangu” Limetumika katika neno la “Baba”. Hii inaeleza uhalisi wa Mungu na asili yake. Lakini maneno kama “yako”, ”yake” yameongezwa katika neno Baba ili kuonyesha mahusiano. Na maneno ya wingi kama “Yetu” au “Wao” nayo yamewekwa ili kuonesha mahusiano ya ushirika.

**B. Utu Wa Baba Mungu Umeelezwa Kama:**

- “**Mweza”** hii inajumuisha nguvu zake na uwezo wa kubariki. Mwanzo 49:25; Hesabu 24:4,16; Ruthu 1:20,21; Ayubu 5:17; 6:4, 14; 8:3, 5; 11:7; 13:3; 15:25; 21:15, 20; 22:3, 17, 23, 25, 26; 23:16; 24:1; 27:2, 10, 11, 13; 29:5; 31:2, 35; 32:8; 33:4; 34:10, 12; 35:13; 37:23; 40:2; Zaburi 68:14; 91:1; Isaya 13:6; Ezekieli 1:24; Yoeli 1:15; Ufunuo1:8
- **“Wa siku zote za kale”** hii inaonyesha uasili wake. Danieli 7:9, 13, 22
- **“Mungu wa milele”** hii nayo inaeleza umilele wake. Mwanzo 21:33; Isaya 40:28
- **“Mungu mwaminifu**” hii inaonyesha upendo wake wa asili. Kumbukumbu la Torati 7:9
- **“Baba wa utukufu”** hii inaeleza kwamba utukufu wote uliopo hutoka kwake. Waefeso 1:17
- **“Baba wa Rehema”** hii inaonyesha rehema zake zisizo na mwisho. 2 Wakorintho 1:3
- **“Mungu aliye juu”** inaeleza mamlaka yake yaliyo juu katika ulimwengu huu. Mwanzo 14:18, 19, 20, 22; Zaburi 57:2; 78:35; Waebrania 7:1
- **“Mungu mwaminifu...hana choyo”** hii ina maana kwamba yeye hakosei. Kumbukumbu la Torati 32:4
- **“Mungu wa utukufu”** hii ni kumbu kumbu ya ukuu wa asili yake. Zaburi 29:3; Matendo 7:2
- **“Mungu wa miungu”** hii inonyesha ukuu wake dhidi ya miungu wengine wa dini za Dunia hii. Kumbukumbu la Torati 10:17; Zaburi 136:2; Danieli 2:47; 11:36
- **“Mungu wa amani”** hii ina maana kwamba Mungu hapendi migogoro na shida. Warumi 15:33; 16:20; Wafilipi 4:9; 1 Wathesalonike 5:23; Waebrania 13:20
- **“Mungu wa walio hai”** hii iaonesha uasili wa milele. Mathayo 22:32; Marko 12:27; Luka 20:38
- **“Mungu aliye juu”** hii inaonyesha ubora wa mamlaka yake katika enzi. Mika 6:6
- **“Mungu wa kweli”** inaonyesha ukweli kwamba Yeye ndiye mkweli peke yake. Zaburi 31:5; Isaya 65:16
- A **“Mkubwa na Mungu wa ajabu”** hii inaonyesha ukuu na heshima zake. Kumbukumbu la Torati 7:21; Nehemia 1:5; Danieli 9:4
- **“Mungu mkuu na mweza”** hii inaonyesha nguvu zake**.** Yeremia 32:18; Nehemia 9:32
- **“Mfalme wa miungu yote”** ni mkuu kuliko wafalme wote wa wanadamu. Zaburi 95:3
- **“Mungu wa kuogopwa”** ni heshima aliyonayo. Zaburi 76:11
- **“Mtakatifu”** yeye ni mmoja aliye mtakatifu,makamilifu na wa haki. 2 Wafalme 19:22; Ayubu 6:10; Zaburi 22:3; 71:22; 78:41; 89:18; Methali 9:10; 30:3; Isaya 1:4l; 5:19, 24; 10:17, 20; 12:6; 17:7; 29:19, 23; 30:11-12, 15; 31:1; 37:23; 40:25; 41:14, 16, 20; 43:3, 14-15; 45:11; 47:4; 48:17; 49:7; 54:5; 55:5; 60:9, 14; Yeremia 50:29; 51:5; Ezekieli 39:7; Hosea 11:9; 11:12; Habakuki 1:12; 3:3; 1 Yohana 2:20
- **“Mungu mwenye wivu”** hii inaonyesha hamu yake kwa watu wake kwamba hapendi washirikiane na miungu mingine. Kutoka 34:14
- **“Mungu wa wivu na hulipa kisasi”** ina maana kuwa atahukumu wale wote wanaotafuta kuiba watu wake. Nahumu 1:2

- **“Mfalme wa utukufu”** hii kweli kwamba anastahili utukufu waajuu kuliko wote. Zaburi 24:7, 8, 9, 10
- **“Anaishi na ni Mungu wa kweli”** ni juu ya umilele wake na uhalisi wake wa asili. 1 Wathesalonike 1:9
- **“Bwana Mungu mwenye Nguvu”** Hii inaonyesha mamlaka yake (Bwana), Asili (Mungu) na Nguvu (Uwezo). Ufunuo 4:8; 11:17; 15:3; 16:7; 19:6; 21:22
- **“Mungu wa Amani”** hii inaonyesha ukweli wake wa ndani kabisa. Waamuzi 6:24
- **“Bwana aliye juu”** hii inaonyesha ukweli kwamba anamiliki mamlaka ya juu aliyonayo. Zaburi 7:17; 47:2
- **“Bwana Mungu wetu”** hii iunaonyesha utu wake wa asili na mamlaka yake. Zaburi 90:17; Danieli 9:9, 15; Marko 12:29; Matendo 2:39
- **“Upendo”** hii ni asili ya Mungu tangu mwanzo. 1 Yohana 4:8,16
- **“Mwema”** hii inaonyesha sifa ya upendo wa Mungu. Kutoka 34:6, 7; Tumbukumbu la Torati 5:10; 7:9, 12; 1 Wafalme 8:23; 1 Nyakati 16:34; 2 Nyakati 6:14; Ezra 3:11; Nehemia 1:5; 9:17; Job 37:13; Zaburi 6:4; 13:5; 26:3; 31:16; 32:10; 36:5, 7; 63:3; 89:2, 14; 103:8, 11; 136:1, 2-28; 138:8; Maombolezo 3:22, 32; Yoeli 2:13
- **“Mwamba wa utukufu”** hii ni asili yake kabisa. 2 Petro 1:17
- **“Mwamba aliye juu ”** hii ni asili ya ukuu wake. Waebrania 1:3; 8:1
- **“Mwamba”** hii ni asili ya ujuwaji wa mambo. Isaya 33:21
- **“Aliye juu”** ni maelezo rahisi yenye ukweli kwamba yeye yuko juu ya vyote. Hesabu 24:16; Kumbukumbu la Torati 32:8; 2 Samweli 22:14; Zaburi 7:17; 9:2; 18:13; 21:7; 46:4; 47:2; 50:14; 57:2; 73:11; 77:10; 78:17, 35, 56; 82:6; 83:18; 87:5; 91:1, 9; 92:1; 97:9; 107:11; Isaya 14:14; Maombolezo 3:35, 38; Danieli 3:26; 4:2, 17, 24, 25, 32, 34; 5:18, 21; 7:18, 22, 25, 27; Hosea 7:16; 11:7; Marko 5:7; Luka 1:32, 35, 76; 6:35; 8:28; Matendo 7:48; 16:17; Waebrania 7:1
- **“Wimbo wangu”** hii inarejesha hisia za usanii wa mtu fulani. Kutoka 15:2; Zaburi 118:14; 119:54; Isaya 12:2
- **“Mungu tu”** hii ni kweli kwamba hakuna mwingine ila ni Mungu tu. Yohana 5:44; 1 Timotheo 1:17; Yuda 1:25
- **“Mungu mwenye hekima”** hii inaonyesha hekima yake tu. Warumi 16:27
- **“Mkamilifu”** ina maana ya kwamba hana dhambi wala kosa ndani yake. Mathayo 5:48
- **“Mungu wa kweli”** hii ina maana ya kwamba alimuumba Mwanadamu na wala mwanadamu hakumuumba Mungu. 2 Nyakati 15:3; Yeremia 10:10; 1 Yohana 5:20

**C. Kanuni ya Mungu Baba:**

Kanuni ya Mungu Baba katika Utatu unahusisha mpango ambao aliuweka kabla ya kuumba mbingu na Dunia (Waefeso 1:11; 3:11).

**D. Kanuni za Mungu Baba Zimeelezeka kama Ifuatavyo:**

- **“Mbunifu”** hii inaonyesha uwezo wa kupanga na kubuni mpango uliomo ndani na nje ,mahusiano na mwonekano wa kitu na vitu vingine katika ulinganifu. Waebrania 11:10
- **“Mjenzi”** hii inaonyesha ufanyaji wake wa mipango ambayo baadaye huwa ni kitu kinachoonekana. Waebrania 3:4; 11:10
- **“Mungu wa rehema na neema”** hii inaonesha huruma yake kwa mwanadamu. Kutoka 34:6
- **“Mlinzi”** hii inaonyesha utetezi wake kwa wanyonge wanaokandamizwa. Isaya 25:4
- **“Mfalme wa milele”** hii inaonyesha mamlaka yake. Yeremia 10:10
- **“Baba wa nuru”** hii inaonyesha yule aliyekuja akiwa mwanga wa Ulimwengu. Yakobo 1:17
- **“Baba wa neema”** hii inajumuisha neema ya uumbaji wake. 2 Wakorintho 1:3
- **“baba wa Roho”** hii inaonyesha Roho aliyeweka juu ya wamwaminio Yesu Kristo. Waebrania 12:9
- **“Baba wa wasio na baba”** hii inasema juu ya mayatima wasio na wazazi. Zaburi 68:5
- **“Mungu wa msamaha”** hii inaonyesha shauku ya kumwokoa mwanadamu kutoka katika dhambi zake. Nehemia 9:17; Zaburi 99:8
- **“Chemchemi za maji hai”** hii ni kweli kwamba yeye ndiye anayewapa watu uzima wa milele. Yeremia 2:13; 17:13
- **“Mzabibu”** hii ina maana kwamba yeye huzalisha matunda ya kiroho kwa wanaomwamini. Yohana 15:1
- **“Utukufu wa Waisraeli”** ni ukweli alioufanya juu ya waisraeli. 1 Samweli 15:29; Mika 1:15

- **“Mungu na Baba wa Bwana Yesu Kristo”** hii inaonyesha uumbaji wa mwili wa Yesu Kristo. Warumi 15:6; 2 Wakorintho 1:3; Waefeso 1:3; 1 Petro 1:3
- **“Mungu Muumbaji wangu”** hii inaonyesha uumbaji wa mwili wa Mwanadamu. Ayubu 35:10
- **“Mungu mwamba wangu”** hii inaonyesha uwezo anaowatendea waumini wanao mwamini. Zaburi 42:9
- **“Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo”** hii inasema juu ya Agano la Kale na Ibrahimu. Kutoka 3:16; Matendo 3:13; 7:32
- **“Mungu wa faraja zote”** hii inaonyesha msaada anaoutoa kwa watu wakati wa shida na matatizo. 2 Wakorintho 1:3
- **“Mungu wa wote wenye mwili”** hii ni kweli kwamba yeye ni chanzo cha wanadamu wote. Yeremia 32:27
- **“Mungu wa matumaini”** hii inaonyesha mipango aliyo nayo kwetu kwa wakati ujao. Warumi 15:13
- **“Mungu wa amani na upendo”** hii inaonyesha juhudi aliyo nayo katika kutetea. 2 Wakorintho 13:11
- **“Mungu wa wokovu wangu”** hii inaeleza asili ya mwanadamu na wokovu wake wa milele. Zaburi 18:46; 25:5; 27:9; 51:14; 88:1; Mika 7:7; Habakuki 3:18; Luka 1:47
- **“Mungu ngome yangu”** hii inaonyesha ulinzi wa Mungu kwa mwanadamu. Zaburi 43:2
- **“Mungu wa Fidia”** Mungu Atawahukumu wote wasio haki. Yeremia 51:56
- **“Mungu wa roho za binadamu”** hii ina maana ya maisha ya asili. Hesabu 27:16
- **“Mungu baba yetu”** hii inaonyesha mahusiano ya kijamaa kati ya waaminio na yeye. Warumi 1:7; 1 Wakorintho 1:3; 2 Wakorintho 1:2; Wagalatia 1:3; Waefeso 1:2; Wafilipi 1:2; Wakolosai 1:2; 2 Wathesalonoke 1:1; 2:16; Filemoni 1:3; Yakobo 1:27
- **“Mungu nguzo yetu”** yeye ni nguzo yetu katika mapito yetu. Zaburi 81:1
- **“Mungu wa falme zote”** hii ianeleza juu ya mamlaka ya malaika wote waliowekwa na mwanadamu. 2 Wafalme 19:15; Isaya 37:16
- **“Mungu baba”** hii inaonyesha jinsi anavyotupa mahitaji yetu. Yohana 6:27; 1 Wakorintho 8:6; 15:24; Wagalatia 1:1; Waefeso 5:20; 6:23; Wafilipi 2:11; Wakolosai 1:3; 3:17; 1 Wathesalonike 1:1; 2 Wathesalonike 1:2; 1 Timotheo 1:2; Tito 1:4; 1 Petro 1:2; 2 Petro 1:17; 2 Yohana 1:3; Yuda 1:1
- **“Mungu alipaye makosa”** hii inaonyesha yale anayoyafanya kwao wanaowaonea watu wengine. 2 Samweli 22:48; Zaburi 18:47
- **“Mungu aliye nguvu yetu”** yeye huwapa nguvu wanaomwamini wakati wa shida. Warumi 15:5
- **“Mungu anaye epusha majanga”** ina maana ya kwamba yeye anaweza kufuta hukumu juu ya taifa. Yona 4:2
- **“Mungu anayeona”** hii inaeleza juu ya umakini wake juu ya watu wake, Mwanzo 16:13
- **“Msaada kwa mayatima”** hii ina maana ya kuwa yeye nii Baba wa wasio na wazazi, Zaburi 10:14
- **“Mfariji”**yeye huwatuliza walioumizwa. Isaya 51:12
- **“Yeye hujua mawazo ya mwanadamu”** hii inaonyesha ufunuo wake kwa mwanadamu. Amosi 4:13
- **“Hutengeneza roho za watu”** hii inaonyesha uumbaji wake, Zaburi 33:15
- **“Ni mweza”** hii inaonyesha uweza wa kazi ya milele. Waefeso 3:20
- **“Alimfufua Yesu”** hii inaonyesha uwezo wa kumfufuYesu. Warumi 8:11
- **“Baba Mtakatifu”** hii inaoneonyesha haki yake kamilifu. Yohana 17:11
- **“Mtakatifu”** hii inaonyesha uwepo wake. Hosea 11:9
- **“Mme”** hii inaonyesha upendo wa uumbaji wake**.** Isaya 54:5
- **“Mwamuzi wa wajane”** hii inaonyesha ulinzi wake kwa walioachwa. Zaburi 68:5
- **“Mwamuzi wa Dunia yote”** hii inaonyesha kweli kwamba yeye ni hakimu wa dunia yote. Mwanzo 18:25
- **“Mfalme wa Mbingu”** hii inaonyesha enzi yake. Danieli 4:37
- **“Baba anayeishi”** hii pia inaonyesha uwepo wake. Yohana 6:57
- **“BWANA”** hii ina maana ya kwamba yeye ni mkuu. Luka 2:29
- **“BWANA bendera yangu”** hii ina maana kuwa yeye ndiye anayepaswa kufuatwa kama vile bendera ya taifa. Kutoka 17:15
- **“BWANA mwamba wangu”** huu ni uwezo alionao kwa wanaomwamini. Zaburi 19:14; 28:1; 144:1
- **“BWANA wa dunia yote”** hii ina maana kwamba dunia yote iko chini ya mamlaka yake. Yoshua 3:11, 13; Zaburi 97:5; Mika 4:13; Zekaria 4:14

- **“BWANA wa mbingu na dunia”** hii ina maana kwamba dunia na mbingu iko katika mamlaka yake. Mathayo 11:25; Luka 10:21; Matendo 17:24
- **“BWANA wa wafalme”** hii inaonyesha mamlaka juu ya wafalme wote wa dunia. Danieli 2:47
- **“BWANA muumbvaji”** hii inaonyesha mamlaka ya kumuumba mwanadamu. Zaburi 95:6
- **“BWANA ni mwamvuri”** hii inaonyesha uwezo wa kumhifadhi mwanadamu. Zaburi 59:11
- **“BWANA anayeponya”** hii inaonyesha mamlaka juu ya wanaougua na magonjwa. Kutoka 15:26
- **“BWANA anayetakasa”** inaonyesha uwezo wake wa kututenga na dhambi ya dunia hii. Kutoka 31:13; Mambo ya Walawi 20:8; 22:32
- **“BWANA anayewapigania waumizwao”** hii inaonyesha juhudi anayoifanya kwa watu wake katika nyakati mabalimbali. Ezekieli 7:9
- **“BWANA atatoa”** hii ina maana ya kwamba huwatetea watu wake. Mwanzo 22:14
- **“Muumbaji”** inaonyesha mkono wa uumbaji. Isaya 54:5
- **“Muumbaji wa vyote”** hii inaonyesha uumbaji. Muhubiri 11:5; Yeremia 10:16; 51:19
- **“Mkuu wa mbingu”** hakuna mwingine ila yeye tu. Wakolosai 4:1
- **“Mtetezi wangu”** yeye hututetea. Ayubu 16:19
- **“Ni tumaini langu”** hii inaonyesha asili ya mwanadamu katika kutegemea. Zaburi 71:5
- **“Msaada wangu”** anatusaidia. Kutoka 18:4; Zaburi 27:9; 40:17; 54:4; 63:7; 70:5; 118:7; 121:1; Waebrania 13:6
- **“Maficho yangu”** yeye hutuficha na kutuhifadhi. Zaburi 32:7
- **“Tumaini langu”** hii inaonyesha jinsi tunavyomtegemea Mungu. Zaburi 25:5, 21; 39:7; 62:5; 71:5; 119:74, 81,114, 147; Acts 23:6; 26:6
- **“Nuru yangu”** inaonyesha ulinzi juu ya mwanadamu. Zaburi 27:1; Mika 7:8
- **“Ngome yangu wakati wa shida”** inaonyesha ulinzi wa Mungu wakati wa shida. Yeremia 17:17; Zaburi 59:16
- **“Nguzo yangu”** inaonyesha ulinzi na msaada. 2 Samweli 22:19; Zaburi 18:18
- **“Yeye hufuta makosa yangu”** hii inaonyesha msamaha wake. Isaya 43:25
- **“Makao yetu”** hii ni kweli kwamba yeye ni nyumba yetu. Zaburi 90:1
- **“Hakimu”** yeye ni mwamuzi wa wanadamu wote. 1 Samweli 24:15; Isaya 33:22
- **“Mwelekezaji”** yeye hutupa sheria na miongozo. Isaya 33:22
- **“Mwokozi wetu”** ina maana kwamba yeye kanunua wokovu kwa ajiri yetu. Isaya 47:4; 63:16
- **“Ngome na nguzo yetu”** ina maana ya kwamba yeye ni mlinzi wa watu wake wanaomwamini. Zaburi 46:1
- **“Mmiliki wa mbingu na nchi”** ina maana kuwa yeye ni mmiliki wa kila kitu. Mwanzo 14:19, 22
- **“Mbebaji”** ina maana kuwa yeye hubeba na kufanya kila kilicho katika viganja vyake. Isaya 29:16; 45:9; 64:8; Yeremia 18:4, 6; Zekaria 11:13; Warumi 9:21
- **“Mwokozi wangu”** ina maana kuwa wokovu aliounununua ni wa watu. Isaya 54:5
- **“Ni ngome ya wanaomwamini”** huu ni ulinzi kwa ajili ya watu wake. Yoeli 3:16
- **“Ngome katika dhoruba”** ulinzi alionao kwa ajiri ya uasi wa mwanadamu. Isaya 25:4
- **“Baba wa haki”** huu ni ukamilifu wake. Yohana 17:25
- **“Mwamuzi wa haki”** hii inaonyesha maamuzi na haki aliyonayo juu ya watu. Zaburi 7:11; Yeremia 11:20; 2 Timotheo 4:8
- **“Mwamba ninaojificha”** inaonyesha ulinzi wa Mungu. Zaburi 94:22
- **“Mwamba wangu”** hii inaonesha nguvu inayopatikana kutoka kwake. Zaburi 62:7
- **“Mwamba wa wokovu wangu”** inaonyesha uimala katika wokovu wetu. Zaburi 95:1
- **“Mtakatifu”** hii inaonyesha kweli kwamba yeye ni sehemu ya kupumzika kama malazi. Isaya 8:14; Ezekieli 11:16
- **“Mlinzi”** yeye ni ngome. Zaburi 28:8
- **“Kivuli”** huu pia ni ulinzi katika yanayojiinua. Isaya 25:4
- **“Kinga”** ni kumbukumbu ya nguvu zake. Isaya 28:6
- **“Kinga ya moyo wangu”** inaonyesha ngu anayoitoa kwa wanaomwamini. Zaburi 73:26
- **“Kinga ya wokovu wangu”** hii inaonyesha nguvu iliyo katika wokovu wetu. Zaburi 140:7

- **“Mtetezi wa waliokandamizwa”** hii inaonyesha ulinzi wake juu ya walio chini ya mamlaka ya watu. Zaburi 9:9
- **“Nguzo wakati wa shida”** hii inaonyesha ulinzi wakati wa shida. Zaburi 9:9
- **“Hurejesha Roho”** hii inaonyesha roho wake juu ya watu. Zaburi 54:4
- **“Mwalimu”** hii inaonyesha uwezo wa kuwaelekeza watu. Ayubu 36:22; Isaya 30:20
- **“Anajibu maombi”** anajua nia na hitaji la mwanadamu. Zaburi 65:2
- **“Hutunza agano lake na upendo”** ina maana kuwa hutunza agano lake nje ya upendo. 1 Wafalme 8:23; 2 Nyakati 6:14
- **“Msaada upatikanao wakati wa shida”** hii ina maana yeye yupo tunapohitaji msaada wake. Zaburi 46:1

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 5, Sehemu ya 3

1. **Maneno ya umoja (yanayokuwa kwenye kiwakilishi hayataji mtu kwa jina) kama vile “angu” ‘ako” “ake” yatumikapo na majina ya Mungu je yanaonesha mahusiano gani?**

2. **Maneno ya wingi (Yanayokuwa kwenye kiwakilishi yaani hayataji mt kwa jina) kama vile “etu” au “Awo” je yanaonesha mahusiano gani?**

3. **Chukua tofauti ya maelezo yaliyoorozeshwa katika sehemu “B” na uyaowanishe na sifa za asili ya Mungu hapo chini. Maelezo mengine yanaweza kutumika zaidi ya mara moja lakini katika zoezi hili jitahidi kila moja liendane na jina moja. Waweza kuoanisha kwa kuweka alama za a, b, c, n.k.**
   a. Mwenye mamlaka
   b. Haki
   c. Mwaminifu
   d. Upendo
   e. Uzima wa Milele
   f. Mwenye nguv zote
   g. Yuko mahali pote
   h. Anajua yote
   i. Habadiliki
   j. Mkweli

4. **Chukua tofauti ya maelezo ya majukumu ya Baba yaliyoorozeshwa sehemu “D” na yaunganishe na kazi za Baba hapa Chini. Narudia tena kazi hizi zaweza kujirdia zaidi ya mara moja. Waweza kuweka alama kama hizi wakati ukioanisha a, b, c, n.k.**
   a. Mamlaka
   b. Muumbaji
   c. Mlinzi
   d. Mfano
   e. Mtoaji
   f. Hakimu
   g. Leader
   h. Upendo
   i. Mzalishaji na mtoaji
   j. Mvumilivu

# Sehemu ya 4
# Mungu Mwana (Christology)

**A. Nafsi Ya Yesu Kristo**

Yesu Kristo Mwana wa Mungu ni Mungu katika mwili. Si mtu mwema aliyebadilika kuwa ni Mungu lakini ni Mungu aliyebadilika kuwa ni mwanadamu (Yohana 1:1, 14). Yeye ni Mungu anayeonyesha asili ya Mungu kabisa (Yohana 14:8-9; Waebrania 1:3).

**1. Asili Yake**

Yesu amekuwepo hata kabla ya kuzaliwa kwake kama mwanadamu. Tunaambiwa kwamba ***"kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi vinavyoonekana na visivyoonekana au usultani au enzi au mamlaka vitu vyote viliumbwa kwa njia yake"*** (Wakolosai 1:16). Hata Yesu mwenyewe aliwaambia Wayahudi kwamba kabla ya Ibrahimu kuzaliwa mimi nimekuweko. (Yohana 8:58).

Injili ya Yohana inaeleza vizuri. Inaanza kwa kusema***"hapo mwanzo palikuwepo neno naye neno alikuwa kwa Mungu naye neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwa kwa Mungu. Na vitu vyote vilifanyika kwa huyo wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika"*** (Yohana 1:1-3). Na baadaye katika sura hii Yohana anasema , ***"naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli."*** (Yohana 1:14).

**2. Ubinadamu wa Mungu**

Yesu ni Mungu na hapo hapo ni mwanadamu. Ni mwanadamu kabisa na pia ni Mungu kabisa. Ukweli huu ni vigumu kuuamini na kuuelewa lakini ni kweli kabisa na ndivyo ilivyo.

Yesu aliwauliza Mafarisayo kabla ya kifo chake msalabani (Mathayo 22:41-46). Aliuliza; imekuwaje basi Daudi katika Roho kumwita Bwana na halafu awe ni mtoto wake? Njia rahisi ya hii ni kwamba Masihi ni Mungu na ni mwanadamu kabisa.

**3. Ukamilifu Wake**

Yesu alikuwa makamilifu katika njia zote kama Mungu alivyo mkamilifu lakini wengi wameuliza ukamilifu wake katika ubinadamu wake.

Tunajifunza kutoka katika kitabu cha Warumi kwamba ***"kwa hiyo kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni na kwa dhambi hiyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi"*** (Warumi 5:12). Mtu huyo ni Adamu ambaye anguko lilieneza dhambi na mauti kwa watu wote (Warumi 5:13-19). Yesu hakuwa wa ulimwengu huu wala hana historia ya ulimwengu huu maana hana baba ila ubaba wote ni wake kwa njia ya Roho Mtakatifu (Luka 1:35). Na ndiyo pekee anayeitwa mwana wa Mungu kwa sababu dhambi ilikuwa juu ya mwanadamu wa kwanza, kwa hiyo, Yesu hana dhambi maana haimuhusu. Yesu hana dhambi ya Adamu. Wakati Adamu anaumbwa na kuwekwa katika Bustani alikuwa ni mkamilifu ila alianguka na tofauti ni hii kwamba Yesu alipozaliwa kama Mwanadamu alikuwa ni mkamilifu na wala hakuanguka wala kufanya dhambi.

Neno la Mungu linatueleza kwamba Yesu aliishi maisha makamilifu na hakufanya dhambi. Yeye hashitakiwi na Dhambi wala yeye hana uongo wa aina yoyote ile (1 Petro 2:22). Kwa sababu hakuwa na dhambi hata alipokuwa katika mwili huu hivyo yeye amekuwepo na ni mkamilifu milele ikiwa na maana ya "kwamba hatafanya dhambi" (Waebrania 5:9; 7:28)

**B. Mpango wa Yesu**

Mpango wa Yesu kwa Mungu ulikuwa ni kufanya kile ambacho kilikuwa kimepangwa (Yohana 8:28-29). Alikamilisha deni la dhambi ya mwanadamu ili kwamba mwanadamu apate kuokolewa (2 Wakorintho 5:21).

**1. Kuja kwa Yesu Kama Mwana**

Kuzaliwa kwa Yesu kulitabiliwa tangu Agano la Kale hasa katika unabii wa Isaya (Isaya 7:14; 9:6; 11:1; 53:2). Yesu ni mbegu ya mwanamke iliyoahidiwa (Mwanzo 3:15).

Ilitabiriwa kwamba atazaliwa Bethelehemu (Miaka 5:2) na atakuwa ni mbegu ya Ibrahimu (Mwanzo 22:18; Mathayo 1:1; Wagalatia 3;16), kupitia ukoo wa Isaka (Mwanzo 21:12), Yakobo (Mwanzo 35:10-12), Yuda (Mwanzo 49:8-11), Yesse (Isaya 11:1) na Daudi (2 Samweli 7:12-16; Yeremia 23:5; Zaburi 132:11).

2. **Kuzaliwa na Bikra**
Mpango wa Mungu kwamba Yesu Masihi (Kristo) atazaliwa na Bikra (Isaya 7:14). Japo kuwa hii ni kitheologia na ni muhimu kujua kwamba uzazi wa Yesu ulikuwa ni wa kimuujiza.

Unabii huu ulikamilika kupitia Mariamu (Mathayo 1:20, 25).

3. **Kifo cha Yesu Kristo**
Kifo cha Yesu kilikamilisha mambo mengi. Alikuwa hastahili kufa (Luka 23:4). Wote waliotenda dhambi (Warumi 3:23; 6:23) walistahili kifo hiki. Yesu hakustahili kwa sababu hakutenda dhambi ila alikuwa huru ili kwamba apate kulipa deni hili mbele ya Mungu Mtakatifu na mwenye haki. (Yohana 10:15-17).

a. **Kujitoa Kwake**
"Badala ya" ina maana ya kwamba Yesu alijitoa badala Yetu pale msalabani. Tunaambiwa kwamba ***"Yeye mwenyewe alichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi tuwe hai kwa mambo ya haki na kwa kupigwa kwake mliponywa."*** (1 Petro 2:24). Yesu hakuwekwa msalabani kwa ajili yetu ila alikwenda kwa niaba yetu, alibeba dhambi zetu "laana". (Wagalatia 3:13).

b. **Kukombolewa**
"Kukomblewa" ina maana ya kwamba mtu mmoja anakuwa huru kwa sababu amekwisha lipwa deni lake. Hii inaonyesha hali ya hiari kwamba gharama ya uhuru Yesu kaisha lipa. Kukombolewa ni msamaha wa dhambi unaotuhamisha kutoka kwa shetani na kwenda katika mamlaka ya Mungu (Wakolosai 1:13-14).

Yesu alilipa deni la wanadamu wote. (2 Petro 2:1), ili kwamba wote waokolewe kutoka katika sheria ya dhambi na mauti (Warumi 8:2). Gharama ilikuwa ni damu yake iliyomwagika msalabani (Ufunuo 5:9-10). Sasa kwa kuwa gharama imekwisha kulipwa kwa hiyo tunapaswa sasa tuwe huru katika kumtumikia Bwana (1 Wakorintho 6:19-20) si kwa kumshukuru wala kwa lazima ila ni kwa neema ambayo yeye katupatia. Tunahitaji kuwa katika uongozi wa Yesu na wala si wamwanadamu. (1 Wakorintho 7:19-23).

Tunapaswa kuendelea na uhuru ambao Yesu katupatia (Wagalatia 5:1). Sisi wanadamu kawaida yetu ni kuwa katika majaribu na utumwa ambao unatesa Roho zetu na tunaonekana kama wapagani (Waefeso 5:1-14). Uhuru aliolipa Yesu ni neema ya pekee na wala si kwa juhudi zetu ila tunapaswa kuongozwa na neema hiyo hata katika kuwatendea wengine (Mwanzo 5:13).

c. **Hitimisho**
"Hitimisho" ni vizuri kuondoa upinzani kati yako, na hatima yake utapata amani.

Wasioamini ni adui wa Mungu (Warumi 5:10) na kwa sababu hiyo watakabiliana na ghadhabu yake (Warumi 5:9). Hii ina maana kuwa kila mtu kabla ya kumpokea Yesu (Yohana 3:16, 18, 36), yeye anahesabika kuwa ni mwenye dhambi mbele za Mungu (Waefeso 2:3). Yesu alikuja kuhitimisha kati ya Wayahudi na Watakatifu kwa kuweka amani (Waefeso 2:16), kwa njia ya mwili wake ulioteswa pale msalabani (Wakolosai 1:22).

Dhambi lazima ilipwe ili kwamba hatima ya Mungu ipate kuonekana (2 Wakorintho 5:19). Yesu aliwaangalia sana watu na kuwahurumia hata akatupa huduma ya kuwaeleza wengine kweli yake ili wapate kumjua Mungu (2 Wakorintho 5:18-21). Na matumizi mazuri ya hatima ya huduma ya mtu ni pale tunapopatanisha watu waliokosana (Mathayo 5:9).

Ukweli ambao tumekwisha uthibitisha Kwa Mungu ni kuonyesha upendo wake mkuu (Warumi 5:8; Luka 6:31-35). Uthibitisho ni muhimu kwa kila mtu (Wakolosai 1:20).

d. **Baraka**
"Baraka" ina maana ya utoshelezo wa Mungu Mtakakatifu. Na hii hufanywa kwa njia ya matoleo.

Mungu ana ghadhabu kwa wenye dhambi wote. Na ukweli wa hii umefundishwa katika Agano la Kale na Jipya (Kumbukumbu la Torati 6:14; Yoshua 23:16; Zaburi 78:21; Yohana 3:36; Warumi 1:18; Waefeso 2:3; 1 Wathesalonike 2:16 na vingine vingi). Mungu ni wa upendo na mwenye rehema kama Charles Ryrie alivyosema,

> Mawazo ya Agano la Kale si ya kipagani yanayotaka Mungu atoshelezwe lakini ni ya Mungu mwenye haki ambaye hawezi kuangalia dhambi sana ila ushirika wake ni kama sehemu nzuri ya makazi na watu wanaomwamini.[99]

Ghadhabu ya Mungu inapaswa kukamilishwa na kifo cha Yesu ndicho pekee kilichokamilisha ghadhabu hiyo (Warumi 3:23-25). Alikamilisha ghadhabu ya Mungu kwa wanadamu wote (1 Yohana 2:2), kwa kuonesha upendo wake (1 Yohana 4:10). Na hii kwa kweli ilikuwa kama sehemu ya mpango wa Mungu na ilikuwa ni sababu muhimu sana hata iliyomfanya Yesu aje kama Mwanadamu (Waebrania 2:17-18).

**4. Kufufuka kwa Yesu**

"Kufufuka" ni neno linalotumika kumweleza mtu aliyerudiwa na uhai na kwamba hatakufa tena (1 Wakorintho 15:42, 54). Na hii imetofautishwa kutoka katika neno Kuzinduka lenye maana ya kuwa umekufa halafu unarudia uhai baadaye unakufa tena (1 Wafalme 17:21-22; 2 Wafalme 4:34-35; Yohana 11:43).

Yesu alifufuka toka wafu. Na maandiko yanayakinisha kwamba Yesu alikuwa amekufa kabisa na siyo kwamba alikuwa kalala au kazimia (Mathayo 27:62-66; Marko 15:39, 44; Luka 23:48, 49; Yohana 19:33). Kaburi lilitolewa ili kukamilisha unabii (Isaya 53:9; Mathayo 27:57-58; Marko 15:42-45; Luka 23:50-52; Yohana 19:38) na Yesu alifungwa katika sanda (Mathayo 27:59-60; Marko 15:46; Luka 23:53-54; Yohana 19:40-42) na akawekwa katika kaburi (Mathayo 27:62-66). Na hata wayahudi walijua sehemu alipozikwa na wakaweka walinzi wanne katika mlango na alama waliweka (Mathayo 27:62-66). Na baadaye Wayahudi walianza kueneza uongo kwamba wanafunzi wake wamemwiba (Mathayo 28:11-15; Marko 14:15).

Siku ya tatu jiwe liliviringishwa mbali (Mathayo 28:2 walitumia neno la kiyunani KULIO likiwa na maana ya kuvingirisha Marko 16:3-4 na walitumia neno ANAKULIO lenye maana ya zungusha Luka 24:2 walitumia APOKULIO maana yake wekwa mbali na Yohana 20:1 alitumia AIRO ikiwa na maana ya inuliwa." Jiwe liliviringishwa milimani na baadaye liliinuliwa na kaburi likabaki wazi (Mathayo 28:5-8; Marko 16:2-8; Luka 24:1-8; Yohana 20:1).

Yote yaliyosalia kaburini ni sanada zake tu. Yalikuwa yamewekwa kwa namna ya kwamba ilikuwa nivigum kwa mwili kuibiwa labda kwa nguvu za kimiujiza (Yohana 20:2-10). Yesu alikuwa amefungwa katika sanda. Ilikuwa ni vigm kwa mtu kufika kuiba mwili wa Yesu halafu akaweza kuzifunga hizo sanda kama zilivyokuwa hapo awali. Mwili ulikuwa umeondoka peke yake na sanda zikabaki kama zilivyokuwa na mwili.

Baada ya kufufuka kwake aliwatokea Maria Magdalena (Yohana 20:14); na aliwatokea wengine (Mathayo 28:9-10); Petro (Luka 24:34; 1 Wakorintho 15:5); wanafunzi wawili waliokuwa wakielekea Emau (Luka 24:13-33); mitume (Luka 24:36-43; Yohana 20:19-24) baadaye alijiunga nao (Yohana 20:26-29); wanafunzi saba (Yohana 21:1-23); na alionekana kwa wanafunzi 500 katika mlima Galilaya (1 Wakorintho 15:6); kwa ndugu yake yakobo (1 Wakorintho 15:7); alionekana kwa wanafunzi kumi na moja (Mathayo 28:16-20; Luka 24:33-52; Matendo 1:3-12); na kwa Paulo (Matendo 9:3-6; 1 Wakorintho 15:8).

Kufufuka kwa Yesu ni kusudi kamili la injili ya Yesu (1 Wakorintho 15:1-3). Ufufuo unamfanya umtenganishe na viongozi wengine wa dunia hii kwa sababu hakuna hata mmoja aliyefufuka.

Yesu mwenyewe alidai kuwa atafufuka toka wafu (Mathayo 16:21; 17:9, 22-23; 20:18-19; 26:32; Marko 9:10; Luka 9:22-27) na hii ndiyo inayowakilisha historia nzima na hata huduma nzima ya Yesu kwa wenye dhambi (1 Wakorintho 15:16-17).

Mungu Baba yake alikuwa chanzo cha ufufuo huo (Wakolosai 2:12; 1 Wathesalonike 1:10; 1 Petro 1:21; Waebrania 13:20), kwa sababu alikuwa ni Roho Mtakatifu (Matendo 2:24; Warumi 8:11; 1 Petro 3:18).

Ufufuo wa Yesu ni wa uhakika kwa sababu; kile alichokisema kilitendeka na kilikuwa ni chema.

Kuukubali ufufuko wa Yesu ni uimara katika kutembea kwetu kama wakristo (Warumi 6:4).

5. **Kupaa kwa Yesu**
"Kupaa" kuna maana ya Yesu kurudi mbinguni baada ya kufufuka kwake. Amekaa mkono wa kuume wa Mungu Baba (Zaburi 110:1; Waefeso 1:20; Wakolosai 3:1; Waebrania 1:3, 13; 8:1; 10:12; 1 Petro 3:22).

Kupaa kwa Yesu kulifanyika siku kumi kabla ya siku ya Pentekosti. Yeye alimtuma Roho Mtakatifu (Matendo 2:33), kama alivyoahidi (Yohana 14:16-17), na akalisimamishja kanisa lake (Matendo 1:9-11 linganisha Matendo 2). Kupaa kwake kunathibitisha kwamba ameshinda (Waebrania 1:3-13).

Wakati Yesu kafufuka alifufuka na watu wengi na wakaka katika kifua cha Ibrahimu (Luka 16:22; Waefeso 4:7-10). Na pia alitoa karama (Wefeso 4:8) ambazo ziligawanywa na Roho Mtakatifu katika kanisa (1 Wakorintho 12:11).

**C. Kupaa kwa Yesu Kristo**
Yesu Kristo yuko upande wa mkono wa kuume wa Mungu Baba hadi atakaporudi mara ya pili kwa ushindi. Maana neno linasema uketi mkono wangu wa kuume hata niwafanyapo adui zako kuwa chini ya miguu yako (Zaburi 110:1).

Yesu kuwa upande wa kuume wa Mungu Baba kunamaanisha sifa ya Kristo alipopaa na sasa anamtukuza Mungu mwanadamu. Ni picha ya Kwamba ***"Mamlaka yote amepewa"*** (Mathayo 28:18) na kwamba ***"kwa jina lake kila goti lipigwe"*** (Wafilipi 2:9). Ni ukamilifu wa unabii wa Danieli 7:13-14.

Wakati huu Yesu anatawala kama:

1. **Mwombezi**
Kama "Mwombezi" Yesu huwaombea watakatifu (Webrania 7:25). Hufanya pamoja na Roho Mtakatifu (Warumi 8:26, 27, 34) na anamwomba Baba ***"kufanya vitu vyote kwa wema"*** (Warumi 8:28) kwa mapenzi ya Baba yake.

2. **Mtetezi**
Kama "Mtetezi" Yesu husimama kama mtetezi kwa yale yote Ibilisi anayowafanyia watoto wa Mungu yaliyo kinyume kabisa na Mungu (1 Yohana 2:1; Ufunuo 12:10).

3. **Mpatanishi**
Kama "Mpatanishi" Yesu yuko katikati kama muunganishi wetu kwa Mungu. Mpatanishi ni mtu anayesuruhisha vyama viwili vilivyokosana iwe kwa kukiumiza kimoja au kuvifanya vyote vifikie mwafaka.

Yesu ni mpatanishi kati ya Mungu na Mwanadamu (1 Timotheo 2:5). Katika nafasi yake yeye hupatanisha Agano Jipya kati ya Mungu na mwanadamu lililo katika rehema na si katika sheria (Waebrania 8:6-13). Agano Jipya limekuja kwa sababu ya yeye kujitoa kama Dhabihu ya dhambi ili apate kulipa deni hili la dhambi ambalo lilikuwa limewekwa tangu Agano la Kale katika sheria ya Musa (Waebrania 9:13-15). Agano Jipya halitaisha milele (Webrania 12:22-24).

Yesu mwenyewe alisema kuwa ni mpatanishi kati ya mwanadamu na Mungu aliposema ***"hakuna awezaye kufika kwa Baba ila kwa kupitia kwangu"*** (Yohana 14:6).

4. **Kuhani Mkuu**
Kristo ni kuhani mkuu. Hakuzaliwa katika ukoo wa kikuhani wa Kiyunani (Waebrania 5:4-10; 7:5-28). Na ukuhani wa Yesu ni kusudi kuu katika kitabu cha waebrania.

Yesu ni kuhani mkuu kama Melikizedeki aliyeishi miaka 400 kabla ya utawala wa makuhani wa kilawi wakati wa Ibrahimu (Waebrania 7:1-3). Ubinadamu wake ulikuwa tayari kujaribiwa ili kwamba rehema za uaminifu wake zipate kuonekana kwa wanadamu na zimdhihirishe Mungu (Webrania 2:17; 4:14-15). Na ukuu wake ni wa milele (Waebrania 6:20; 7:3, 24).

Kazi ya kuhani kutoa dhabihu (Waebrania 8:1-3). Yesu alijitoa (Waebrania 9:6-14) kama ***"Dhabihu ya mara moja kwa wakati wote"*** (Waebrania 10:10, 12).

Hata hivyo watu wote kanisani ni makuhani (1 Petro 2:5, 9; Ufunuo 1:6), hivyo tunapaswa tumuige Yesu (1 Wakorintho 11:1) kwa kujitoa kama dhabihu mbele za Mungu (Warumi 12:1).

5. **Kichwa cha Kanisa**
   Yesu ni kichwa na kiongozi wa kanisa (Waefeso 1:22-23; Wakolosai 1:18). Wote wanaomwamini Yesu ni mabibi harusi au ni mwili wa Kristo yaani kanisa (1 Wakorintho 12:13).

   Yesu ni mme wa Kanisa (Waefeso 5:23) na ana upendo usio na mwisho (Waefeso 5:25-27). Na harusi au sherehe hii itafanyika mbinguni kabla ya Yesu kurudi mara ya pili (Ufunuo 19:7-10 linganisha 11-16), lakini upendo na uaminifu wake upo hata sasa. Kanisa kama Bibi harusi limeandaliwa kwa ajili yake (Waefeso 4:15; 5:26-27).

6. **Mchungaji**
   Neno "Mchungaji" lina maana ya kuangalia au kuchunga. Yesu Kristo kama mchungaji mwema aliyatoa maisha yake kwa ajili ya kondoo wake (Yohana 10:11), na hivyo yeye ni "Mchungaji mkuu" (Waebrania 13:20).

   Katika mkono wa kuume wa Mungu Baba aliko yeye ni Mchungaji mkuu (1 Petro 5:4), anayelinda na kuwatunza kondoo wake.

**D. Yesu Kristo ni Kama Nani Sasa**

- **"Wakili"** ina maana ya kwamba yeye anatutetea mbele za Baba. 1 Yohana 2:1
- **"Alpha na Omega**", Mwanzo na Mwisho hii ina maana ya kwamba yeye ni msingi wa mawasiliano. Ufunuo 1:8; 21:6; 22:13
- **"Amina"** yeye ni neno la Mwisho. 2 Wakorintho 1:20; Ufunuo 3:14
- **"Mpakwa mafuta**" hii ina maana ya kwamba tangu mwanzo na hata milele Yesu ni masihi wa Mungu. 1 Samweli 2:35; 2 Nyakati 6:42; Zaburi 2:2; 28:8; 84:9; 89:38, 51; 132:10, 17; Danieli 9:25-26; Matendo 4:26
- **"Mtume**" yeye alitumwa kwa mamlaka yote. Waebrania 3:1
- **"Mwanzilishi wa Imani"** hii ina maana kwamba kama Mungu Kristo aliweka mpango na kama mwanadamu aliutenda. Waebrania 12:2
- **"Mwanzilishi wa wokovu"** hii ina maana ya kwamba yeye ndiye aliyeleta wokovu. Waebrania 2:10
- **"Mwanzo na mwisho** " hii ina maana kwamba yeye ndiye aliye na maisha yote. Ufunuo 21:6; 22:13
- **"Muumbaji"** hii ina maana ya kwamba yeye ndiye mkuu wa uumbaji wa Mungu. Ufunuo 3:14
- **"Mbarikiwa na mwenye mamlaka"** inaonyesha madaraka yake ya juu. 1 Timotheo 6:15
- **"Tawi la Bwana"** hii inaonyesha jinsi anavyoshugulika na mahitaji ya watu. Isaya 4:2
- **"Mkate"** hii inaonyesha uhai anaotupatia Mungu. Yohana 6:33, 51
- **"Mkate wa uzima"** hii inaonyesha jinsi yeye anavyoshughulika na maisha yetu. Yohana 6:35, 48
- **"Bwana harusi"** inaonyesha ulinzi juu waumini na mahusiano aliyonayo. Isaya 62:5; Mathayo 9:15; 25:1, 5, 6, 10; Marko 2:19, 20; Luka 5:34, 35; Yohana 2:9; 3:29; Ufunuo 18:23
- **"Nyota ya asubuhi**" hii ina maana ya kwamba yeye ni nyota ing'aayo kati ya wawingu mazito. Ufunuo 22:16
- **"Mchungaji mwema"** hii ina maana kuwa yeye anawajibu juu ya kondoo wake. 1 Petro 5:4
- **"Jiwe lililochaguliwa, jiwe la msingi**" hii ni kweli kwamba yeye alichaguliwa ili kuonyesha kipimo katika kiwango cha utimilifu. Jiwe la msingi linaonyesha ujenzi wa kanisa lake. Waefeso 2:20; 1 Petro 2:4, 6
- **"Yesu Kristo Bwana wangu**" ina maana ya kwamba mwanadamu Yesu ni Masihi na ana mamlaka katika maisha yangu. Wafilipi 3:8
- **"Yesu tumaini letu"** hii inaonyesha Yesu kuwa ni nguzo katika maisha yetu yote. 1 Timotheo 1:1
- **"Kristo wa Mungu**" hii ina maana pale alipochaguliwa kuwa ni masihi wa Mungu. Luka 9:20; 23:35
- **"Amiri jeshi mkuu**" hii inaonyesha mamlaka ya juu kabisa aliyonayo. Danieli 8:11
- **"Mfariji wa Israeli**" hii inaonyesha jinsi Yesu anavyotutia moyo. Luka 2:25
- **"Agano**" Yesu ni msingi wa waaminio. Isaya 42:6
- "**Malango"** yeye ni mlango wa kuingia katika ufale wa Mungu. Yohana 10:7, 9
- **"Baba wa milele"** Ina maana ya kuwa yeye ni Mungu**.** Isaya 9:6
- **"Uzima wa melele"** hii inatufundisha kuwa unapatikana kwake. 1 Yohana 1:2
- **"Mwamba wa milele"** hii inaonyesha uimara alionao. Isaya 26:4

- **“Anawakilisha uasili wake**” katika kuonyesha ubinadamu anaitwa Kristo kwa sababu ya mwili na hapo hapo ni mwanadamu. Waebrania 1:3
- **“Mwaminifu na mkweli**” hii inaonyesha uaminifu alionao. Ufunuo 19:11
- **“Mashahidi mwaminifu”** hii inaonyesha uaminifu alionao hasa kulingana na unabii uliotabiriwa. Ufunuo 3:14
- **“Shahidi wa kweli**” hasa ushuhuda baada ya kufufuka. Ufunuo 1:5
- **“Wakwanza na wa Mwisho**” Yeye ndiye aliyeumba. Ufunuo 1:17; 2:8; 22:13
- **“Mtu wa kwanza kutoka wafu”** hii inaonyesha ushindi wake baada ya kushinda mauti. Wakolosai 1:18; Ufunuo 1:5
- **“Mzazi wa kwanza katika uumbaji**” ina maana ya kwamba yeye ni muumbaji wa kwanza. Wakolosai 1:15
- **“Tunda la kwanza la walio lala**” ina maana ya kwamba yeye ni baraka ya walio lala mauti kwani atawafufua. 1 Wakorintho 15:20
- **“Aroma”** hii ni baraka katika dhabihu yake. Waefeso 5:2
- **“Rafiki wa watoza ushuru na wenye dhambi”** yeye ni mwangalizi na mlinzi wa waliotengwa na pia huwapenda waliona dhambi ili awaokoe. Mathayo 11:19; Luka 7:34
- **“Utukufu wa Israeli”** Bwana anahitaji sifa zinazostahili. Luka 2:32
- **“Mungu wa dunia yote”** inaonyesha uasili na mahusiano na watu wote. Isaya 54:5
- **“Mungu wa wote**” inaonyesha kuwa yeye ni Mungu wa Israeli. Warumi 9:5
- **“Mchungaji mwema”** inaonyesha ulinzi na uongozi juu ya watu wake. Yohana 10:11
- **“Kuhani mkuu”** hii inaonyesha jinsi anavyotenda kazi katika ofisi yake. Waebrania 4:14
- **“Nuru kuu”** yeye hung’aa gizani. Isaya 9:2; Mathayo 4:16
- **“Mchungaju mkuu”** inaonyesha ulinzi na utekelezaji kwa watu wake. Waebrania 13:20
- **“Ni mweka maagano mema”** Yesu ndiye aliyekuwa kaahidiwa na Mungu. Waebrania 7:22
- **“Mlinzi wa Roho zetu”** analinda roho zetu. 1 Petro 2:25
- **“Kichwa”** hii inaonyesha umahili wake katika uongozi. 1 Wakorintho 11:3; Waefeso 4:15; Wakolosai 2:19
- **“Mweka madalaka”** hii inaonyesha mamlaka aliyonayo hata kwa wale wasiyo wayahudi. Warumi 15:12
- **“Anatakasa”** hii inaonyesha uwezo wa Mungu katika kutusafisha. Waebrania 2:11
- **“Mtambuzi wa Roho na fikra”** inaonyesha uwezo wa Yesu katika kujua hisia na mawazo ya mwanadamu. Ufunuo 2:23
- **“Kichwas cha mwili ”** inaonyesha uwezo wake katika kuliongoza kanisa. Wakolosai 1:18
- **“Kichwa cha kanisa”** hii inaonyesha uweza wake katika kuwaongoza waumini. Waefeso 5:23
- **“Mkuu wa mamlaka na tawala zote”** inaonyesha mamlaka ya Yesu. Wakolosai 2:10
- **“Mrithi wa vyote”** kama mwana ana haki na vitu vyote. Waebrania 1:2
- **“Kuhani mkuu”** inaonyesha madaraka aliyoyashika. Waebrania 2:17; 3:1; 4:14, 15; 5:5, 10; 6:20; 7:26; 8:1; 9:11; 13:11-12
- **“Anatupenda**” inaonyesha msamaha aliotusamehe kwa sababu ya Pendo lake. Ufunuo 1:5
- **“Mwana wake wa pekee”** Yesu Kristo kweli ni muumbaji. Yohana 3:16; Waebrania 11:17; 1 Yohana 4:9
- **“Mtakatifu na wa haki”** hii inaonyesha sifa ya ukamilifu wake. Matendo 3:14
- **“Mtakatifu wa Mungu”** inaonyesha utakatifu alioishi akiwa kama mwanadamu. Marko 1:24; Luka 4:34; Yohana 6:69
- **“Mtumishi Mtakatifu”** alitii. matendo 4:27, 30 (Neno la kiyunani PAIS maana yake ni “Mwana”)
- **“Tumaini la Israel.”** Yeremia 14:8; 17:13; Matendo 28:20
- **“Bwana wa wokovu”** Yesu analeta wokovu. Luka 1:69
- **“Sura ya Mungu asiyeonekana**” ina maana Yesu ni Mungu katika Mwili. Wakolosai 1:15
- **“Immanueli”** neno la Kiebrania yaani Mungu pamoja nasi. Isaya 7:14; 8:8; Mathayo 1:23
- **“Zawadi isiyoelezeka”** ina maana hatuwezi kumweleza Yesu na ukuu wake. 2 Wakorintho 9:15

- **“Yesu wa Nazarethi”** hii inaonyesha mji aliokulia. Mathayo 26:71; Marko 1:24; 10:47; Luke 4:34; 18:37; 24:19; Yohana 1:45; 18:5, 7; Matendo 2:22; 6:14; 10:38; 22:8; 26:9
- **“Hakimu wa walio hai na wafu”** inaonyesha mamlaka ya Yesu katika hukumu. Matendo 10:42; 2 Timotheo 4:1
- **“Mfalme wa wafalme”** hii inaonyesha mamlaka ya Yesu hata kwa wakuu wa dunia hii. Ufunuo 19:16
- **“Mfalme wa mataifa”** hii inaonyesha utawala juu ya wanasiasa wote. Ufunuo 15:3
- **“Mwana kondoo wa Mungu”** hii inaonyesha dhabihu ambayo Yesu aliitoa ili kukamilisha lengo la Mungu. Yohana 1:29, 36
- **“Adamu wa Mwisho”** Yeye ni mwanandamu wa mwisho aliyeishi bila dhambi. 1 Wakorintho 15:45
- **“Uzima”** hii ina maana ya kwamba yeye ndiye aliye na uzima. Yohana 1:4; 11:25; 14:6
- **“Roho ya uzima”** hii inaeleza umoja alionao katika Roho. 1 Wakorintho 15:45
- **“Nuru ya ufunuo kwa watakatifu**” kweli Yesu alikuwa  kabisa ni wanadamu. Luka 2:32
- **“Nuru ya uzima**” inaonyesha ulinzi katika safari zetu zilizo ngumu. Ayubu 33:30; Zaburi 49:19; 56:13; Yohana 8:12
- **“Nuru ya watu**” inaonyesha ulinzi alionao juu ya watu wote. Yohana 1:4
- **“Nuru ya ulimwengu**” ulinzi alionao katika roho za giza. Yohana 8:12; 9:5
- **“Anaishi”** inaonyesha sili yake hasa katika kufufuka. Ufunuo 1:17-18
- **“Jiwe lililo hai”** huu ni uhusisho alionao katika maisha yake. 1 Petro 2:4
- **“Bwana”** ina maana ya mamlaka. Matendo 4:24; Ufunuo 6:10
- **“Bwana na mwokozi Yesu Kristo”** inaonyesha kwamba yeye alitumia mamlaka katika kumwokoa mwanadamu**.** 2 Petro 1:11, 20; 3:18
- **“Bwana wa utukufu”** inaonyesha uajabu katika uasili wake. 1 Wakorintho 2:8
- **“Bwana wa mabwana”** yeye ana mamlaka katika mamlaka zote. Ufunuo 19:16
- **“Bwana wa amani”** hii inaonyesha nia yake ya kutuliza watu wanapokuwa wamekwenda kinyume na Mungu. 2 Wathessalonike 3:16
- **“Bwana wa mavuno”** ana mamlaka katika kueneza injili. Mathayo 9:38; Luka 10:2
- **“Bwana wa sabato”** anaonyesha mamlaka katika sheria ya nne katika zile amri kumi. Mathayo 12:8; Luka 6:5
- **“Bwana haki yetu”** yeye ndiye anayestahili katika kutupatia haki zetu. Yeremia 23:6; 33:16
- **“Mwanadamu aliyeletwa na Mungu”** hii inaonyesha idhini ya Mungu kwake. Matendo 2:22
- **“Mtu kutoka mbinguni” I**naonyesha asili yake. 1 Wakorintho 15:47
- **“Mtu wa huzuni”** hii inaonyesha huruma yake kwa wanadamu waliomkataa. Isaya 53:3
- **“Mkuu”** inaonyesha ubora na ufahamu wake katika mamlaka. Luka 5:5; 8:24, 45; 9:33; 17:13; Waefeso 6:9; Wakolosai 4:1; 2 Timotheo 2:21
- **“Mpatanishi wa agano jipya”** ina maana ya kuwa ndiye pekee anaye kamilisha agano na Mungu. Waebrania 9:15; 12:24
- **“Mwingi wa rehema na mwaminifu”** hii inaonyesha huruma yake katika utendaji wake. Waebrania 2:17
- **“Mjumbe wa agano”** atakayeleta habari katika Agano Jipya na Mungu. Malaki 3:1
- **“Masihi”** ina maana kuwa yeye ndiye aliyechaguliwa na Mungu ili awaokoe watu. Yohana 1:41; 4:25
- **“Mungu mweza”** inaonyesha nguvu zake. Isaya 9:6
- **“Nyota ya asubuhi”** inaonyesha kung’aa kwake kati ya giza nene. 2 Petro 1:19; Ufunuo 22:16
- **“Mnazorayo”**. Mathayo 2:23
- **“Mwana wa Daudi”** inaonyesha jinsi alivyopitia katika ukoo wa Daudi. Ufunuo 22:16
- **“Mmoja na Baba”** inaonyesha umoja kati yake na Mungu. Yohana 10:30
- **“Mwana wa pekee”** inaonyesha jinsi alivyo. Yohana 1:14, 18
- **“Mungu mwokozi wetu”** inaonyesha kazi na utu wake. Yuda 1:25
- **“Bwana wa utukufu”** inaonyesha ukuu wa mamlaka yake. Yakobo 2:1
- **“Mungu na Mwokozi wetu”** Inaonyesha mahusiano ya Yesu na kanisa. 2 Petro 1:1
- **“Uzima wetu”** uhai anaolipa kanisa. Wakolosai 3:4

- “**Bwana wetu”** hii inaonyesha kibali chake katika mamlaka yake. Warumi 1:4; 5:21; 7:25; 1 Wakorintho 1:9; Yuda 1:25
- **“Bwana wetu”** inaonyesha mamlaka yake katika kanisa. Yuda 1:4
- **“Pasaka wetu”** kumbukumbu ya mateso yake badala ya kanisa. 1 Wakorintho 5:7
- **“Amani yetu”** Inaonyesha uimara wa amani kati ya kanisa na Mungu. Waefeso 2:14
- **“Mwokozi wetu”** Inaonyesha wokovu alioufanya katika kanisa. Tito 3:6
- **“Tabibu”** Anaponya. Luka 4:23
- **“Mokozi”** anatuonyesha jinsi ya kuufikia wokovu. Matendo 5:31
- **“Bwana wa maisha”** yeye anaongoza maisha yetu. Matendo 3:15
- **“Hodari wa amani”** Yeye hutupa furaha. Isaya 9:6
- **“Hodari wa mahodari”** ina maana ya kwamba hakuna kiongozi zaidi yake. Danieli 8:25
- **“Nabii”** inaonyesha jinsi alivyokamilisha unabii wake. Kumbukumbu la Torati 18:18 linganisha. Matendo 3:22
- **“Anastahili kusamehe dhambi”** yeye anakamilisha haki na nia ya Baba. 1 Yohana 2:2
- **“Anasafisha”** anatuondolea dhambi. Malaki 3:3
- **“Wautukufu”** hii ni sifa ya juu kabisa ya Baba. Waebrania1:3
- **“Mkombozi wa wote”** ina maana ya kwamba alilipa gharama ili tuwekwe huru. 1 Timotheo 2:6
- **“Ufufuo na Uzima”** ina maana ya kwamba ufufuo unatokana na Yesu tu. Yohana 11:25
- **“Mwamuzi wa haki”** ina maana yeye hufanya kulingana na haki. Zaburi 7:11; 2 Timotheo 4:8
- **“Wa haki”** inaonyesha ukamilifu. Isaya 24:16; Matendo 3:14; 7:52; 22:14; 1 Yohana 2:1
- **“Shina la Daudi”** inaonyesha kuwa yeye amekuwepo na kamfanya Daudi. Ufunuo 22:16
- **“Mtawala wa wafalme wa dunia”** ana mamlaka juu ya wakuu wote. Ufunuo 1:5
- **“Mwokozi wa ulimwengu”** yeye ndiye aokoaye. Yohana 4:42; 1 Yohana 4:14
- **“Mchungaji”** anawaangalia wampendao. Mwanzo 49:24; Zaburi 80:1; Muhubiri 12:11
- **“Mchungaji wa roho yako”** anamlinda mwanadamu**.** 1 Petro 2:25
- **“Dira ya watu”** watu wanapaswa kumtafuta Yesu tu. Isaya 11:10
- **“Mwana wa Mungu”** inaonyesha uhusiano katika Utatu wake. Yohana 10:36; 11:4
- **“Mwana wa Mungu aliye hai”** inaonyesha mahusiano yake na Mungu wa kweli. Mathayo 16:16
- **“Mwana wa Mungu aliye juu**” inaonyesha jinsi anavyotazamwa na malaika. Marko 5:7; Luka 8:28
- **“chanzo cha uzima wa milele”** Yeye ni msingi wa wokovu. Waebrania 5:9
- **“Ngome”** Anatupa uwezo wa kuvumilia majaribu. Isaya 33:6
- **“Jiwe”** inaonyesha uwezo katika kumlinda mwanadamu. Isaya 28:16
- **“Jiwe lililokataliwa na waashi”** inaonyesha uvumulivu aliokuwa nao wakati viongozi wa Israeli walipotaka kumvamia. Zaburi 118:22; Mathayo 21:42; Marko 12:10; Luko 20:17; 1 Petro 2:7
- **“Mwalimu” (Rabboni)** yeye huelekeza. Yohana 20:16
- **“Jiwe”** ufahamu wa Yesu katika maisha. Isaya 28:16
- **“Ushuhuda”** inaonyesha kuwa Yesu alidhihirishwa wakati ulipotimia. 1 Timotheo 2:6
- **“Mkate wa kweli**” Yesu hututia nguvu**.** Yohana 6:32
- **“Nuru ya kweli”** inaonyesha ukweli wake katika kudhihirishwa.Yohana 1:9; 1 Yohana 2:8
- **“Mzabibu wa kweli”** Yesu ndiye hutoa matunda ya kiroho (kazi njema). Yohana 15:1
- **“Kweli”** hii inaonyesha ukamilifu wa Yesu. Yohana 5:33; 8:31-32; 14:6
- **“Njia”** yeye ni wokovu. Mathayo 7:14; Yohana 14:5-6
- **“Tajiri wa wokovu”** Yesu anathamani katika kumwokoa mwanadamu. Isaya 33:6
- **“Hekima”** inaonyesha jinsi anavyoweza kuelewa na kutumia vyema kila kilicho katika maneno ya Mungu. Isaya 33:6
- Ndiye “**aliyekuja kwetu akiwa na haki, akitakasa na kukomboa”** ina maana ya kwamba wokovu wa kweli uko kwa Yesu tu.. 1 Wakorintho 1:30
- Ndiye **“aliekuwa hekima kwetu toka kwa Mungu”** ina maana ya kwamba hekima iko kwa Yesu tu. 1 Wakorintho 1:30
- **“Mashahidi kwa watu”** hii inaonyesha ushuhuda alioutoa kwa watu wote. Isaya 55:4

- **“Mshauri wa ajabu”** yeye hutoa msaada wa pekee wakati wa shida. Isaya 9:6
- **“Neno”** yeye ndiye msingi wa mawasiliano yote. Zaburi 119:81; Yohana 1:1, 14; 1 Yohana 1:1; Ufunuo 19:13
- **“Neno la Mungu”** Yesu ndiye njia pekee ya kuwasiliana na Mungu. 2 Petro 3:5; Yohana 1:1-5; Ufunuo 19:13
- **“Neno la Uzima”** yeye ndiye tofali la kujengea. Wafilipi 2:16; 1 Yohana 1:1
- **“Mme”** inaonyesha mahusiano kati yake na mwanadamu. Isaya 54:5
- **“Muumbaji”** yeye ndiye aliyeumba. Isaya 54:5
- **“Mwokozi”** Yeye alilipa dhambi zetu. Isaya 54:5
- **“Wokovu wako”** Yeye ndiye huwaokoa wanadamu wote kutoka katika dhambi zao. Luka 2:29-30

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 5, Sehemu ya 4

1. **Soma Wakolosai 1:16 na Yohana 8:58. Hizi zinatueleza nini kuhusu Nafsi Ya Kristo?**

2. **Soma Mathayo 22:41-46. Inawezekanaje masihi kuwa Bwana wa mfalme Daudi na hapo hapo ni Mwana wa Mfalme Daudi?**

3. **Soma 1 Petro 2:22. Inatueleza nini kuhusu dhambi kwenye maisha ya Yesu Kristo?**

4. **Soma Isaya 7:14; 9:6; 11:1-2 na 53:2. Andika mhitasari kuhusu kuja kwa Masihi.**

5. **Soma vitabu hivi na halafu tueleze kifo cha Yesu kilifanya nini kwa ajili yetu:**
   a. Wagalatia 3:1
   b. Wakolosai 1:13-14
   c. Waefeso 2:14-16
   d. 1 Yohana 2:1-2

6. **Soma sura hizi na teleze ukweli kuhusu ufufuko wa Yesu:**
   a. Mathayo 27:62-66
   b. Yohana 20:2-10
   c. Yohana 20:14; Mathayo 28:9-10; Yohana 20:26-29; 21:1-23 na 1 Wakorintho 15:6
   d. 1 Corinthians 15:1-3

7. **Soma Matendo 1:9 na Wakolosai 3:1. Yesu alifanya n baada ya kufufuka?**

8. **Soma sura hizi na utuambie Yesu anafanya awapo katika mkon wa kuume wa Baba:**
   a. Waebrania 7:25
   b. 1 Yohana 2:1
   c. 1 Timotheo 2:5
   d. Waebrania 4:14

9. **Soma Waefeso 1:22-23. Kristo ni nini katika kanisa?**

10. **Soma Yohana 10:11; Waebrania 13:20 na 1 Petro 5:4. Bwana wetu ni mchungaji wa namna gani?**

11. **Chukua maelezo ya majukumu ya Nafsi ya Mwana yaliyoorozeshwa katika sehemu “D” na uyaoanishe na kazi za Mwana hapo chini. Kumbuka tena kazi hizi zaweza kujirudia. Waweza kuweka alama za 1, 2, 3, n.k.**
    a. Maisha yako hapo kale
    b. Mungu mwanadamu
    c. Ukamilifu wake
    d. Kuzaliwa na kuishi kwakwe
    e. Kifo chake
    f. Kufufuka kwake
    g. Kupaa kwake na kukaa kwa Baba
    h. Huduma yake

# Sehemu ya 5
# Mungu Roho Mtakatifu (Pneumatology)

**A. Nafsi Yake**[100]

Imekwisha thibitishwa kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu. Roho Mtakatifu ni nafsi si kwa sababu inaeleza tu hali ya Uungu au kwa sababu ya uamsho wake. Hii inathibitishwa kwamba anazo sifa zote tatu: Ufahamu, hisia au kuwaza na Hiari pia.

Kumekuwa na hali ya kutokukubaliana katika historia ya kanisa juu ya nafsi yake na kazi ya Roho Mtakatifu. Tunahitaji kuwa waangalifu sana katika kanuni ya ***"kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha imani"*** (Waefeso 4:3). Uelewa mzuri juu ya Roho Mtakatifu unatupatia upendo (Wagalatia 5:22), ambao si wa kumpenda Mungu tu bali hata wengine (1 Yohana 4:20).

"Hekalu" la Roho Mtakatifu ni mwili wa Kristo na Mtume Paulo aliuliza ***"au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu mlipewa na Mungu wala si mali yenu wenyewe?***" (1 Wakorintho 6:19). Na hata zamani Paulo aliserma katika 1 Wakorintho Paulo aliuliza swali linalofanana, ***"hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?"*** (1 Wakorintho 3:16). Roho wa Mungu huwaunganisha watu ndani ya Kristo pamoja. Tunaonywa kwamba tusiliharibu hekalu hilo (1 Wakorintho 3:17). Kuna bibi harusi mmoja tu wa Yesu Kristo. Hebu hii ituongoze katika kujifunza kwetu somo hili. Roho Mtakatifu ni nafsi nyingine iliyo na.

**1. Ufahamu**

Roho Mtakatifu ana uwezo wa kujua na kutafuta mambo ya Mungu (1 Wakorintho 2:10-11). Hii inatufundisha kuwa anakiri (Warumi 8:27) na uwezo wa kuwafundisha watu (1 Wakorintho 2:13).

**2. Fikra**

Maneno ya Mungu yanasema wazi kwamba Roho Mtakatifu anaweza kuhuzunishwa (Isaya 63:10; Waefeso 4:30), hii inaonyesha kwamba ana mawazo ya kufikiri. Kama angelikuwa ni wa kuambukiza au kusisimua tu basi asingelikuwa na mawazo hayo. Na huu ni uthibitisho kwamba yeye anaweza kukufuriwa (Marko 3:29).

**3. Hiari**

Ana sifa pia ya kuamua kuchagua; yaani hiari. Roho Mtakatifu kwa mamlaka yake anagawa vipawa katika mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12:11). Na ni wazi kwamba analinda na kumwongoza Mkristo (Matendo 16:6-11).

**4. Umbo**

Ni mara moja katika Maandiko tunamwona Roho Mtakatifu anakuwa na umbo kama njiwa likionyesha amani. Mathayo 3:16; Marko 1:10; Luka 3:22; Yohana 1:32

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 5, Sehemu ya 5A

1. **Nini sifa tatu za Mtu?**
   a Soma 1 Wakorintho 2:10-11. Hii inatfndisha nini kuhusu Roho Mtakatifu?
   b. Soma Waefeso 4:30. Hii inatufndisha nini kuhsu Roho Mtakatifu?
   c. Soma 1 Wakorintho 12:11. Hii inatufundisha nini kuhusu Roho Mtakatifu?

**B. Majukumu Yake**

**1. Uumbaji**

Ni wazi kwamba Roho Mtakatifu ana sehemu katika uumbaji na alizifanya mbingu na Dunia. Dunia ikiwa haina umbo wala haina kitu ***"Roho wa Mungu alikuwa juu ya uso wa maji"*** (Mwanzo 1:2) kama ndege (Tai) anayepapatika juu ya makinda yake (Kumbukumbu la Torati 32:11). Maandiko yanasema Bwana alizifanya mbingu kwa kutamka neno tu na Roho wa Bwana alifanya nyota katika mawingu hayo (Zaburi 33:6). Na Roho Mtakatifu anatawala uumbaji wake (Ayubu 26:13).

Roho wa Mungu ana majukumu katika uumbaji na hata katika kumfanya mwanadamu (Ayubu 33:4) na hata katika kuwaumba wanyama (Zaburi 104:24-25 linganisha. 104:30).

Majukumu yake katika uumbaji ni kumdhihirisha Bwana kupitia uumbaji wake (Isaya 40:12-13 linganisha. Warumi 1:20 linganisha. Yohana 16:13-14).

2. **Ufunuo**
Majukumu ya Roho Mtakatifu katika ufunuo ni kumuhabarisha mwanadamu juu ya mambo mapya (Yohana 16:13). Anatumia wanadamu katika kuthibitisha kweli (2 Samweli 23:2) na wakati mwingine ukweli huo huwa ni habari mbaya (Mika 3:8).

   Maandiko peke yake ni ufunuo wa Roho Mtakatifu (Mathayo 22:42-43; Matendo 1:16; 4:24-25; 28:25-26; Waebrania 10:15-16).

3. **Utambuzi**
Roho Mtakatifu huhabarisha mambo ya kiroho kwa watu lakini mambo mengine huwa ni magumu kuyaelewa (1 Wakorintho 13:12). Kwa hiyo yeye hutusaidia katika uelewa wetu juu ya neno la Mungu (1 Wakorintho 2:12-16) na sehemu ambapo neno linahitaji katika maisha yetu (Luka 12:11-12; Waebrania 3:7-8). Na matumizi haya ya uelewa wa Kiroho yanaitwa "Hekima."

4. **Uvuvio**
Roho wa Mungu aliwajalia watu fulani kuandika neno la Mungu (2 Petro 1:21). Tunaelezwa na neno la Mungu kwamba Maandiko yote yana uvuvio wa Pumzi ya Mungu (2 Timotheo 3:16-17). Mtume Paulo kipindi anaandika sura hiyo alitumia maneno ya Kiyunani ambayo hayakuonekana popote pale. Neno THEOPNEUSTOS ni la kiyunani lililo na maneno mawili THEOS na PNEUMA, yenye maana "Mungu" na "Roho." Biblia yote ina uvuvio wa Mungu kwa uweza wa Roho Mtakatifu

5. **Miujiza**
Yesu alitenda miujiza kwa uweza wa Roho Mtakatifu (Luka 4:18).

   Roho Mtakatifu alikuwa ni chanzo cha miujiza mingine kutendeka. Mfano mzuri ni pale Filipo alipombatiza Muethipia na halafu akapotea (Matendo 8:39). Na mwingine ni uzazi wa Bikira.

6. **Uzazi wa Bikra**
Bikira Mariamu, aliambiwa na malaika Gabrieli kwamba atamzaa mwana kwa uweza wa Roho Mtakatifu na atamwita jina lake "Mwana wa Mungu" (Luka 1:27, 35). Katika sura hii tunajifunza kwamba hata Roho Mtakatifu ni Mungu.

   Baada ya Mariam kuwa mjamzito akiwa na mimba ya Yesu, malaika alimtokea Yusufu ambaye alikuwa mme mtarajiwa na kumwambia kuwa Mariam amepata uja uzito kutokana na uwezo wa Roho Mtakatifu (Mathayo 1:18-20).

7. **Kujutia Dhambi**
Jukumu jingine la Roho Mtakatifu ni kumfanya mwanadamu atambue dhambi. Hii ina maana kuwa anaiweka wazi si katika ulimwengu lakini katika mtu mwenyewe ili atambue kwamba kaisha vunja sheria ya Mungu na hivyo kawa ni mwenye dhambi na anamhitaji Yesu (Yohana 16:8). Anadhihirisha dhambi hizi kupitia utambuzi katika nafsi zetu. (Warumi 9:1).

8. **Utakaso**
Utakaso ina mana ya kwamba ni kuzaliwa tena. Na hii ina maana ya kile kinachotokea katika wokovu na si kwa kitu kinachotokea baada ya wokovu. Roho Mtakatifu ndiye anayetuumba upya na hii ni ahadi ya Mungu katika neno lake. (1 Petro 1:23 linganisha Tito 3:5).

9. **Ubatizo**
Kuna kuchanganyikiwa sana katika swala la ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa wakristo wengi. Ngoja tuone na tutambue sasa nini Biblia inasema juu ya hili swala.

   Neno kubatiza kwa kiyunani ni (BAPTIDZO) likiwa na maana ya kwamba "Kuzamisha" na lilitumika na wayunani wengi ili kutambulisha "Rangi ya Vazi" au kuchota maji kwa kutumia bakuri au chombo chochote au kushtushwa na maswali fulani."[101] Wakati ubatizo ulipoanza (mtu anazamishwa au mkuki unazamishwa katika damu na askari kabla ya vita ilikuwa ni alama ya kukubali na kujitoa. Ilikuwa ni alama ya kutangaza mahusiano, aidha kwa kusema, kimwili, kihisia, yaliyofanywa na mtu au kitu au chama fulani. Kwa mfano Yesu alisema anao Ubatizo wa kufanya na huu ulikuwa kweli kumbukumbu katika msalaba (Marko 10:38) sasa kwa kuwa ubatizo wake wa maji ulikwisha fanywa (Marko 1:9). Ubatizo wa Yesu wa Maji ulikuwa ni picha ya kukubaliana na mpango wa baba yake alioufanya katika maisha yake.

   Ujumbe wa Yohana mbatizaji ulikuwa ukitabiri ahadi ya Kwamba Masihi ***"atabatizwa kwa Roho Mtakatifu"*** (Mathayo 3:11; Marko 1:8; Luko 3:16; Yohana 1:33; Matendo 1:5). Kwa hiyo ubatizo wa

Roho Mtakatifu haukutokea hadi pale Yesu alipomtuma Roho Mtakatifu siku ya Pentecoste (Yohana 14:16-17; Matendo 2:1-4), ambao Petro aliita ni mwanzo (Matendo 11:16). Katika kipindi hiki waumini hawakuwa na kitu kingine hadi siku hiyo alipowaijilia. Ilikuwa ni mpya kwa kanisa kwa sababu na ndiyo pale lilipoanza siku ya Pentecoste.

Ni vigumu kuelewa ubatizo wa Roho Mtakatifu bila kutambua kwamba kusudi lake lilikuwa kuwahamisha waumini toka siku ya Pentekositi hadi kwenye mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12:12-13), au kanisa (Waefeso 5:22-30). Tafadhali tambua kwamba dhambi na mwili haviwezi kumhamisha yeyote katika mwili wa Kristo kama ni hivyo basi wakorinto wangelihamishwa (soma 1 Wakorintho 1-11 jinsi umati wa wenye dhambi ulivyokuwa ukitenda).

Hakuna amri katika maandiko inayomwamrisha mtu kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo ni kitu kinachotokea wakati muumini mmoja katika Kristo anapokubali kifo cha Yesu, kuzikwa na kufufuka (1 Wakorintho 15:1-4). Si ubatizo wa kulowana ila ni ubatizo zaidi ya kuwa mkavu.

Ukweli wa Kiroho juu ya ubatizo kwa waumini umeelezwa vizuri na mtume Paulo akisema,

> ***Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika Mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake.*** (Warumi 6:3-5)

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kile kitendo cha Muumini kuishi akitawaliwa na Roho Mtakatifu (Yohana 14:17; Warumi 5:5) na hii inatokea pale mtu anapompokea Yesu kama mwokozi na kwa hiyo anatambuliwa na kazi zake kwa niaba ya Yesu mwenyewe.

**10. Mhuri**

"Mhuri" hii ina maana ya chapa inayofanyika. Wayahudi walifanya hii katika kaburi la Yesu ili kwamba wangeweza kueleza ikiwa kama jiwe lile lililokuwa katika kaburi lingeliondolewa (Mathayo 27:66). Roho Mtakatifu huweka mhuri wa Mungu usioonekana wakati mtu anapompokea Yesu Kristo (Waefeso 1:13).

Ni utaratibu wa kujisajili kwamba mtu anakuwa na chapa ya Roho Mtakatifu ili kuonyesha kwamba amekubalika. Wakristo huingizwa katika umoja wa moja kwa moja wa Yesu Kristo na Roho Mtakatifu huthibitisha umoja huo kwa kusaini jina lake. Roho Mtakatifu ni Mungu na hivyo hutumia mhuri wa Mungu (2 Wakorintho 1:22) katika kuweka alama isiyoonekana.

Kwa kuwa Roho Mtakatifu amekwisha wapiga mhuri wakristo hatupaswi kumhuzunisha kwa kukaa tukitenda dhambi (Waefeso 4:30).

Tumepigwa mhuri wa wokovu (Waefeso 4:30; Waefeso 1:14) ambayo inaeleza katika siku zijazo kwamba kuwa itakamilika pale tutakapofufuliwa (Warumi 8:23).

**11. Makao**

Makao ya Roho Mtakatifu yanafanyika wakati unapopata wokovu tu. Na hii ni kwa sababu ya ahadi aliyoifanya Yesu inayosema ***"Nami nitamwomba Baba naye atawapa Msaidizi mwingine ili akae nanyi hata milele, ndiye Roho wa kweli ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea kwa kuwa haumwoni wala haumtambui bali ninyi mnamtambua maana anakaa kwenu naye atakuwa ndani yenu"*** (Yohana 14:16-17).

Siku ya Pentekositi Roho Mtakatifu aliwaijilia waumini wote. Na tangu siku hiyo yeye yuko ndani yetu na anaishi nasi kama waumini. Hivyo makao ya Roho Mtakatifu ni muhimu katika kanisa (Warumi 8:9; 1 Wakorintho 3:16; 6:19; 2 Timotheo 1:14).

Huduma mbalimbali za Roho Mtakatifu kama vile kuonyesha dhambi ili uitambue na hata mafunuo ni vitu vilivyo sawa, lakini mwelekeo wake umetofautiana.

Roho Mtakatifu anaingia kwa Muumini mara moja kama ubatizo wa Roho Mtakatifu na hii ni wakati unapompokea Yesu tu. Hivyo ubatizo na makao ya Roho Mtakatifu ni kama zawadi kutoka ya kutoka kwa Mungu (Matendo 11:16-17; Warumi 5:5), na hakuna anayeweza kukupokonya (Warumi 11:29). Makao ya Roho Mtakatifu hayaondolewi na dhambi maana imeelezwa katika kanisa la Korintho. Katika

1 Wakorintho 1:2; 3:16; na 6:19, waumini huko Korintho walihesabika kuwa ni Wakristo japo walikuwa na dhambi nyingi na Paulo kaeleza katika sura za 5 & 6.

Kuna mifano miwili iliyotolewa katika kitabu cha Matendo ambapo Roho Mtakatifu alitolewa baada ya Wokovu (Matendo 8:14-17; 19:1-6). Na tumaini utakumbuka maswali ya kujiuliza wakati unasoma Biblia kwamba, "nani?" "Nini?" na "Lini?" katika sehemu zote mbili watu waliamini kwamba Masihi atakuja na hawakujua kwamba tayari yupo. Baada ya kuelekezwa kuwa masihi yupo na wakaamini ujumbe huo hapo hapo walimpokea Roho Mtakatifu na akaingia. Si hekima kujadili jadili matukio na kuyarahisisha kwamba ni ya kawaida.

**12. Anajaza**

Katika somo letu la kujazwa na Roho Mtakatifu itatubidi tena turudi katika neno la Mungu ili tupate majibu sahihi. Tutaangalia katika maelezo ya Biblia juu ya kujazwa na Roho Mtakatifu na halafu tutaona umuhimu wa kufanya katika maisha yetu.

**a. Tunaona kwamba kujazwa na Roho Mtakatifu ni**

**1) Kupewa huduma muhimu kama vile ufundi stadi na uongozi**

Kujazwa na Roho Mtakatifu kulifanyika kipindi cha wana wa Israeli kwa watu baadhi ili kubeba majukumu muhimu. Roho Mtakatifu alihitajika (Luka 11:13), lakini haikuwa lazima. Maandiko yanasema kwamba alitolewa kwa Bezaleli, mmoja wa watumishi wa Hema ya kuabudia ili kwamba ujuzi wake umtukuze Mungu (Kutoka 31:3; 35:31). Ina sema tena ***"Yoshua alikuwa na Roho wa Hekima"*** (Kumbukumbu la Torati 34:9) ili kwamba awaongoze wana wa Israeli baada ya Kifo cha Musa.

**2) Kupewa huduma muhimu, kutia moya na unabii**

Katika injili ya Luka tunaona kwamba Yohana mbatizaji (Luka 1:15), mama yake Elizabeth (Luka 1:41) na Baba yake Zakaria (Luka 1:67) walijazwa na Roho Mtakatifu. Na hii inatuonyesha kwamba ujazo wa Roho Mtakatifu ni kumbukumbu ya nguvu muhimu iliyotolewa ili kubeba majukumu nyeti.

**3) Kwa ajili ya mawasiliano muhimu na jamii Fulani**

Baada ya kufufuka kwake na hata baada ya kunyakuliwa kwake aliwaambia wanafunzi wake wajazwe na Roho Mtakatifu (Yohana 20:22). Hili ni jukumu muhimu ili kwamba wasikie toka Roho Mtakatifu (Matendo 1:2), na wasubiri nguvu ambayo baada ya siku chache wangeipata (Matendo 1:8). Hii ingewawezesha kuwapa neema ya kuwasamehe wale waliomsulubisha Yesu (Yohana 20:23).

Roho alipowajaza na kuwawezesha siku hii ya Pentekositi walianza kunena kwa Lugha mpya za wanadamu ambazo hapo awali hakuweza kuzisema wala kuzijua (Matendo 2:1-11, hasa mstari wa 4, 8, 11). Petro aliwezeshwa kuhubiri ujumbe ambao tunauona katika sura hiyo hiyo (2:14-40) na hata kuahidi uweza wa Roho kwa wale wote watakaomkubali Yesu (2:38-40). Huu ni uthibitisho kwamba kama ilivyokuwa katika kipindi cha Israeli ujazo wa Roho Mtakatifu unahusisha mambo mengi ili kuweza kubeba huduma muhimu na nyeti.

**4) Ametolewa kwa ajili ya ulinzi wa kiroho na ujasiri**

Mfano mwingine wa kujazwa na Roho Mtakatifu ulionekana pale Petro alipojitetea kwa Wayahudi (Matendo 4:5-12), na baadaye aliwajulisha rafiki zake. Petro na rafiki zake walikuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu na wakawezeshwa kunena kwa ujasiri (Matendo 4:31). Elewa kwamba vitu hivi viwili havikuwafanya wazungumze lugha nyingine. Kwa hiyo kuamini kwamba ujazo wa Roho Mtakatifu unasababisha mtu azungumze lugha nyingine isiyojulikana hii si kweli.

Kwa kuangalia mifano hii iliyotangulia juu ya kujazwa kwa Roho Mtakatifu tunaweza kuona kwamba kukaa kwa Roho Mtakatifu kwetu huwa ni mara moja tu na ni kitu kinachoendelea kuwepo na hakitoki ila kujazwa ni kitu kinachofanyika kila wakati zaidi ya mara moja. Na uthibitisho wa kwamba Mkristo hapaswi kuwa makao ya Roho Mtakatifu ila anapaswa kujazwa na Roho Mtakatifu ni katika (Waefeso 5:18). Makao ya Roho Mtakatifu yanahusisha sehemu ya sisi kuwa katika Kristo na Roho wa Mungu kuwa ndani yetu na kujazwa kunaonyesha nguvu yake katika waumini yaani wakristo.

**5) Kuwezesha huduma**

Ujazo wa Roho Mtakatifu umelengwa katika kanisa ili kutuwezesha matendo yetu ya huduma yaonekane hata kwa wengine.tatizo lilipoinuka katika kanisa la kwanza juu ya kutojaliwa

wajane (Matendo 6:1), wanafunzi wa Yesu waliwaeleza waumini wachague watu wanaofaa waliojazwa na Roho Mtakatifu ili wapate kuwaangalia na kushughulika juu ya swala hilo (Matendo 6:2-5), kitu walichokifanya kama jamii. Wanafunzi waliona hitaji la uweza wa kiroho ili waweze kubeba huduma zilizokuwa kanisani.

6) **Kuonyesha Udanganyifu wa Shetani**
Sauli (Paulo), katika safari yake ya kwanza ya Umissionari, ilikuwa ikionyesha neno la Mungu kwa Mkuu wa Warumi Sergio Paulo aliyekuwa kashindana na Mchawi Elima (Matendo 13:6-7). Paulo, akiwa amejawa na Roho Mtakatifu alijua kuwa Elima alikuwa akijaribu kulipotosha neno la Mungu (Matendo 13:8-10).

7) **Kuhusika na kutengwa**
Mfano huu wa kujazwa na Roho Mtakatifu unamuhusisha Paulo na Barnaba walipoondolewa na Wayahudi huko Pisidia Antiokia (Matendo 13:42-51). Kujazwa kwa Roho Mtakatifu katika sura hii inaonesha kwamba ni zaidi ya uhusiano unaoendelea katika Roho Mtakatifu katika huduma zetu. (13:52).

**b. Ujazo wa Roho Mtakatifu kwa Wakristo wanaokua**
Kwa kuwa waumini wameamuriwa kujazwa na Roho Mtakatifu (Waefeso 5:18), tunaweza kuhitimisha kwamba si kila muumini anajazwa na Roho Mtakatifu wakati wote.

Kwa kuwa dhambi inavuruga ushirika kati ya waumini na Mungu tuinahitimisha kwamba inaweza hata kupinga uweza na ujazo wa Roho Mtakatifu (1 Yohana 1:6). Kujazwa kwa Roho Mtakatifu ni kitu kinachoonekana katika maisha ya Kikristo ambacho kwetu kinaonekana kama “kutembea katika Nuru” (Yohana 8:12; 12:35-36; Waefeso 5:7-10; 1 Yohana 1:7). Wakati mwingine wakristo huanguka katika dhambi (1 Yohana 1:8, 10). Dhambi hii huharibu ushirika wetu na Mungu; hivyo tunapaswa kuiungama na kuamini kwa Imani kwamba Mungu ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee kabisa na kutusafisha na udhalimu wote (1 Yohana 1:9).

Tafadhali elewa kwamba kujazwa na Roho Mtakatifu ni tendo ambalo tayari limekwisha kamilika na ni kitu ambacho ni cha mara moja, na hakiendelei na kikiingia hakitoki na wala si cha muda tu. Hakuna ilipoelezwa kwamba mtu alijazwa Roho Mtakatifu nusu au alijazwa kidogo na ieleweke kwamba ujazo wa Roho Mtakatifu hautokei kwa Mkristo wa muda mrefu au aliyekwisha komaa. Hivyo ujazo wa Roho Mtakatifu ni (1) kwa waumini wote na haitegemei kwamba wawe wamekomaa au bado katika Ukristo na (2) ni kamili. Na pia Roho anaweza kuzimishwa (Matendo 7:51), hivyo kama wakristo ni lazima wajitoe kikamilifu ili wajazwe na Roho Mtakatifu.

Katika ukweli tuliouona hapo nyuma tunaweza kuhitimisha kwamba ujazo wa Roho Mtakatifu ni tendo lililokamili linalomwezesha mkristo kuishi maisha ya Kikristo. Na si kwa sababu ya maisha ya kikristo tu lakini pia ni ufunguo unaoanza na kukamilisha maisha ya Kikristo.

Mambo manne kama matokeo ya kukua katika kujazwa na Roho Mtakatifu ni nguvu ya kumsifu Mungu (tendo la nje), kumwabudu Mungu (tendo la ndani), Kumshukuru Mungu na kujitoa/kuwasaidia wengine (Waefeso 5:19-21).

**13. Kuomba**
Katika sehemu ya kujazwa na Roho Mtakatifu tumeona umuhimu wake. Tunafundishwa kwamba ni muhimu kuomba katika Roho ili kuonyesha mahusiano yetu kwa Mungu Roho Mtakatifu (Waefeso 6:18; Yuda 1:20-21). Katika maisha yetu ya maombi ni lazima tuwe na ushirika na Mungu tunapokuwa tukiomba; hivyo ni muhimu sana kuungama dhambi zetu kabla hatujapeleka mahitaji yetu. (1 Yohana 1:9).

Kuna wakati ambao sisi hatujui kuomba na hatujui hata maneno ya kuanza nayo na hata jinsi tutakavyojaribu kjusema. Tunapoona hali hii Roho Mtakatifu hutusaidia kuomba ili tupate mahitaji yetu mbele za Mungu Baba (Warumi 8:26-27).

**14. Uhakika**
Jukumu jingine la Roho Mtakatifu ni kutuhakikishia wokovu wetu na baraka zetu za milele. Tunaambiwa kwamba ***“Roho mwenyewe hushuhudia… ya kwamba sisi tu watoto wa Mungu,”*** na kwamba ***“ni warithi pamoja na Kristo”*** (Warumi 8:16-17).

Roho Mtakatifu ni Arabuni wa urithi wetu. (Waefeso 1:13-14).

**15. Mtetezi**
Roho Mtakatifu huhakikisha kwamba Baba anajua mahitaji yetu hata kama bado hatujamweleza (Warumi 8:26).

**16. Karama**
Yesu Kristo aliposhuka toka kwa Baba alimpa karama nyingi kwa ajili ya mwanadamu (Waefeso 4:11). Karama hizi za kiroho zinagwawiwa kwa walioamini na Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 12:11, 18; Waebrania 2:4).

Karama za kiroho ni zawadi ya Mungu (uwezo wa ziada) katika maeneo nyeti katika maisha ya mwanadamu ili kunufaika na mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12). Kila Mkristo ana karama yake na naitumia kwa waumini wengine (1 Petro 4:10).

Kwa kuwa karama si kitu cha asili au uwezo wa asili hivyo Roho Mtakatifu anatumia kipaji na uwezo wako kupitia karama hiyo. Kwa mfano kipaji cha mziki kinaweza kutumika katika karama ya kushawishi. (Warumi 12:8).

Pia unahitaji uwezo wa ziada kwa ajiri ya karama yako ili kutosheleza shughuli. Kwa mfano kama una karama ya kufundisha (Warumi 12:7; 1 Wakorintho 12:28; Waefeso 4:11), unahitaji kusoma neno la Mungu (2 Timotheo 2:15) na jifunze jinsi ya kufundisha somo lako.

Tutaona kwa upana somo la karama baadaye katika sehemu inayofuatia.

**17. Kufundisha**
Jukumu muhimu kabisa la Roho Mtakatifu ni kutufundisha juu ya mambo ya Mungu (Yohana 14:26). Anaweza kutufundisha kwa uharaka kulingana na hitaji (Luka 12:11-12) au anaweza kutuongoza kwa njia ya kujifunza taratibu (Yohana 16:13-15).

Katika huduma ya kutufundisha Roho Mtakatifu anatuwezesha kujifunza vitu vya kiroho (1 Wakorintho 2:10-16).

**18. Ulinzi**
Roho Mtakatifu ni mlinzi katika maisha yetu. Kama mlinzi wetu jukumu lake kuu ni kutufundisha juu ya Yesu Kristo (Yohana 16:13) ili kwamba tuwe kama yeye (1 Wakorintho 11:1; Waefeso 5:1).

Ambapo mapenzi ya Mungu huonekana kupitia neno lake kama vile mambo ya madili (1 Timotheo 1:8-11; Warumi 8:12-14), ulinzi wa Roho Mtakatifu uko wazi. Roho Mtakatifu ndiye aliyevuvia Biblia (2 Timotheo 3:16-17; 2 Petro 1:21), twaweza kujua mapenzi yake kwa kuyaangalia maandiko na hayo ndiyo yanakuwa ni ulinzi wetu.

Mahali ambapo mapenzi ya Mungu hayaeleweki vizuri katika neno lake kama vile kuchagua vitu viwili vilivyo vizuri, hivyo tunahitaji tumwendee yeye kama dhabihu iliyo hai na takatifu (Warumi 12:1) ili kwamba tuipate kujua mapenzi yake juu ya jambo hilo (Warumi 12:2).

Kwa ulinzi wa Roho Mtakatifu tazama Matendo 8:29; 10:19-20; 13:2-4; 16:6-7; 20:20-23.

**19. Matunda**
Katika makao Roho Mtakatifu anapenda kuzaa matunda kupitia sisi. Matunda haya ni “upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, Upole na kiasi” (Wagalatia 5:22-23). Ili haya yatokee ni lazima tumruhusu Roho Mtakatifu awezeshe mienendo yetu ya Kikristo (Wagalatia 5:16, 25) ili kwamba mwili na dhambi zake zitawaliwe (Wagalatia 5:17-21).

**20. Furaha na Shangwe**
Roho Mtakatifu huleta furaha ndani yetu na shangwe ndiyo inayoonekana nje. Furaha hii yaweza kuja hata wakati wa shida (1 Wathesalonike 1:6). Ni jibu la haraka la baraka za Baba kwa wengine na si jibu la baraka binafsi (Luka 10:21).

**21. Upendo**
Roho Mtakatifu anapokaa ndani ya Mkristo analeta furaha na matumaini. (Warumi 5:5).

**22. Haki, Amani na Furaha**
Katika maisha ya Wakristo Roho Mtakatifu huonyesha baraka hizo za muhimu kutoka katika ufalme wa Mungu na ni za kiroho na si za kimwili (Warumi 14:17).

23. **Uweza**
Roho Mtakatifu hutia nguvu ili kwamba Wakristo wapate kuwa na tumaini tele (Warumi 15:13) ili waweze kuhubiri injili ya mbinguni na uzima wa milele (1 Petro 1:12).

24. **Utakaso**
Sisi "Tumetakaswa" na Mungu ili kwamba tupate kumrudishia sifa na dhabihu zinazokubalika na tutende mema kwa wengine pia (Warumi 15:16 linganisha Waebrania 13:15-16). Dhabihu hii inahusisha maadili mema kwa sababu wale wanaojiingiza katika uasherati na uzinzi wamedhoofishwa na kudumazwa katika mambo ya Kiroho (1 Wathesalonike 4:1-8). Sehemu ya utakaso wetu ni kumruhusu Roho Mtakatifu atutakase kama yeye alivyo Mtakatifu (1 Petro 1:16).

25. **Ushirika**
Roho Mtakatifu ndiye anayedumisha ushirika kati ya walioamini kwa njia ya neema ya Yesu Kristo na Upendo wa Mungu Baba (2 Wakorintho 13:14).

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 5, Sehemu ya 5B

2. **Soma mistari hii na eleza kazi za Roho Mtakatifu:**
   a. Ayubu 33:4
   b. Yohana 16:13
   c. 1 Wakorintho 2:12-16
   d. 2 Petro 1:21
   e. Luka 4:18
   f. Luka 1:27 and 35
   g. Yohana 16:8
   h. Tito 3:5
   i. Mathayo 3:11
   j. Waefeso 1:13
   k. Yohana 14:16-17
   l. Waefeso 5:18
   m. Waefeso 6:18
   n. Waefeso 8:16-17
   o. Warumi 8:26
   p. 1 Wakorintho 12:11 and 18
   q. Yohana 14:26
   r. Galatians 5:22-23
   s. 1 Wathesalonike 1:6
   t. Warumi 5:5
   u. Warumi 14:17
   v. Warumi 15:13
   w. Warumi 15:16
   x. 2 Wakorintho 13:14

**C. Roho Mtakatifu Ameelezwa Kama**

- **"Msaidizi mwingine"** hii inaonyesha huduma yake ya faraja, na kutia moyo kama vile Yesu. Yohana 14:16
- **"Pumzi ya Uweza"** inaonyesha uweza wake wa kututia uhai. Ayubu 32:8; 33:4
- **"Karama"** hii inaonyesha uwepo wake kwamba yeye ni karama au zawadi kutoka kwa Mungu. Matendo 2:38; 8:19-20; 10:45
- **"Msaidizi"** yeye huwafundisha watu ukweli na kuwatia moyo. Yohana 14:26
- **"Mwakilishi"** hii ni alama ya wokovu wetu. 2 Wakorintho 1:22; 5:5; Waefeso 1:14
- "**Aliyeahidiwa**" inaonyesha jukumu la mpango wa Mungu. Matendo 2:33; Waefeso 1:13
- **"Roho"** hii inaonyesha jinsi atakavyotuleta katika familia ya Mungu. Warumi 8:15
- **"Roho wa hukumu na moto"** inaonyesha haki yake kama Mungu. Isaya 4:4
- **"Roho wa Kristo"** hii inaonyesha majukumu yake kwa ubinadamu wa Yesu krito. Warumi 8:9; Wafilipi 1:19; 1 Petro 1:11
- **"Roho wa kushauri na kuimarisha"** inaonyesha huruma na msaada alionao kwa walio wahitaji. Isaya 11:2
- **"Roho wa Imani"** inaonyesha haki yake ya kuaminiwa. 2 Wakorintho 4:13
- **"Roho wa utukufu"** inaonyesha ufahari wake. 1 Petro 4:14
- **"Roho wa Mungu"** inaonyesha asili ya utaratibu wake. Mwanzo 1:2; Kutoka 31:3; 35:31; Hesabu 24:2; 1 Samweli 10:10; 11:6; 19:20, 23; 2 Nyakati 15:1; 24:20; Ayubu 33:4; Zaburi 106:33; Ezekieli 11:24; Mathayo 3:16; 12:28; Warumi 8:9, 14; 1 Wakorintho 2:11, 14; 7:40; 12:3; Waefeso 4:30; Wafilipi 3:3; 1 Yohana 4:2
- **"Roho wa Utaratibu"** inaonyesha asili yake kama Mungu. Mwanzo 41:38
- **"Roho wa Neema"** inaonyesha mtazamo wake wa neema na mapenzi yake katika kusikiliza maombi. Zakalia 12:10
- **"Roho wa Mwana wake"** inaonyesha Utatu. Wagalatia 4:6
- **"Roho wa utakatifu"** si Roho Mtakatifu tu bali hudhihirisha hata utakatifu. Warumi 1:4
- **"Roho wa hukumu"** inaonyesha ufunuo wa hukumu yake**.** Isaya 4:4

- **"Roho wa haki"** inaonyesha haki yake. Isaya 28:6
- **"Roho wa maarifa na anamwogopa Bwana"** ana maarifa kwani anamuheshimu Bwana. Isaya 11:2
- **"Roho wa Uzima"** anatoa Uzima. Warumi 8:2
- **"Roho wa Mungu wetu"** inaonyesha majukumu aliyonayo katika maisha ya kanisa kwa kumdhihirisha Mungu. 1 Wakorintho 6:11
- **"Roho wa Mungu aliye hai"** hii ni tofauti kati ya Mungu na miungu (sanamu). 2 Wakorintho 3:3
- **"Roho wa Bwana"** inaonyesha msaada kwa Mkuu wake. Luka 4:18; Matendo 5:9; 8:39; 2 Wakorintho 3:17
- **"Roho wa Bwana Mungu"** inaonyesha msaada wake kwa Mungu ambaye ni Mkuu wake. Isaya 61:1
- **"Roho wa Kweli"** hadanganyi wala hana uongo. Yohana 14:17; 15:26; 16:13; 1 Yohana 4:6
- **"Roho wa hekima na ufahamu"** ana uwezo wa kutoa ujumbe na kutumia neno la Mungu kama lilivyo. Isaya 11:2
- **"Roho wa hekima na mafunuo"** ana uwezo wa kuelekeza katika yanayofaa kwa kutumia Neno la Mungu ili Mkristo aelewe. Wefeso 1:17
- **"Sauti ya Mungu mweza"** yeye ni muunganishaji wa mawasiliano ya neno la Mungu. Ezekieli 1:24
- **"Sauti ya Bwana"** inaonyesha mamlaka ya mawasiliano yake makuu. Isaya 6:8

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 5, Sehemu ya 5C

3. **Chukua maelezo tofauti ya nafsi ya Roho Mtakatifu na kazi zake zilizoorozeshwa sehemu "B" hapa chini. Kumbuka kazi hizi zinaweza kuingia kwenye sehemu nyingi. Waweza kuweka alama za A na B ili kuoanisha.**
   a. Jukumu lake
   b. Nafsi yake

## Sura ya 6

# Misingi ya Mazao ya Mungu

# Sehemu ya 1
# Uumbaji (Cosmology)

Mstari wa kwanza katika Biblia unatuambia kwamba "H***apo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi"*** (Mwanzo 1:1). Neno la kiebrania limetafasiri neno "Kuumba" ni neno BARA lililo na maana ya "kuanzisha kitu kipya"[102] likiwa na ukweli kwamba "kuumba kitu kutoka sehemu pasipo na kitu" ni Mungu pekee aliyetamka "BARA" kukawa na vitu.[103]

Ukweli wa kwamba Mungu aliumba mbingu na dunia umeelezwa katika sehemu mbalimbali za Biblia (Isaya 40:26-28; 42:5; 45:12, 18). Ni muhimu sana kuukubali ukweli huu kwa sababu unajibu swali kubwa sana la mwanadamu la " Mwanadamu alitoka wapi?" na jibu ni kwamba Mungu alimuumba.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anatuambia kwamba, ***"Kwa imani tunaelewa kwamba ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri"*** (Waebrania 11:3). Hi inatufundisha kwamba Mungu alisema na Mbingu zikatokea. Uumbaji umekuwa dhahiri kwa sababu ya nguvu na mamlaka ya Mungu na si kwa mabadiliko yaliyoendelea (Zaburi 33:6; 148:4-5).

Biblia inasema kwamba Mungu aliumba viumbe vyote (Mwanzo 1:21) ikiwemo na roho ya mwanadamu (Mwanzo 1:27; 5:2; 6:7; Isaya 45:12) na halafu " akapumzika" akaacha kazi ya uumbaji (Mwanzo 2:3-4). Siku moja katika siku za usoni ataumba mbingu mpya na nchi mpya (Isaya 65:17; 2 Petro 3:10-13; Ufunuo 21:1).

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 6, Sehemu ya 1

1. **Soma Mwanzo 1:1. Nani aliumba mbingu na nchi?**

2. **Soma Waebrania 11:3. Mungu aliwaumbaje?**

3. **Soma Mwanzo 1:2-31. Mungu alimba nini tena?**

4. **Soma 2 Petro 3:10-13 na Ufunuo 21:1. Mngu atamba nini hapo baadaye?**

# <u>Sehemu ya 2</u>
# Malaika (Angelology)

**A. Nafsi Zao**

Neno la Mungu linatueleza kwamba kuna uumbaji wa viumbe vyenye akiri sana kuliko ile ya mwanadamu unajulikana kama MALAIKA. Wametajwa mara nyingi na wanaonekana katika Biblia nzima kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo. Maana halisi ya neon "Malaika" kwa Kiebrania (MALAAK) na kiyunani (AGGELOS) ni "Mjumbe." hawa wanauwezo wa kufikiri na kuwasiliana. Kwa kuwa wana akiri (Mathayo 8:29; 2 Wakointho 11:3; 1 Petro 1:12), wanafikiri (Luka 2:13; Yakobo 2:19; Ufunuo 12:17) na wana uwezo wa kufanya maamuzi (Luka 8:28-31; 2 Timotheo 2:26; Yuda 6), na wana nafsi.

Malaika ni "roho" (Waebrania 1:14) huchukua umbo la binadamu wanapokuwa wameruhusiwa na Mungu kufanya hivyo (Luka 2:9; 24:4). Na hawaonekani; wako juu sana kuliko Mwanadamu (Waebrania 2:7). Hii ina maana ya kwamba wana nguvu na akili zaidi ya mwanadamu (Ufunuo 10:1-3), lakini pamoja na hayo hawaelewi mambo yote (1 Petro 1:12) hawana nguvu zote (Mathayo 25:41) wala hawako sehemu zote kama Mungu alivyo.

Tumepewa majina matatu ya malaika katika Maandiko. Mikaeli (Daniel 10:13, 21; 12:1; Yuda 1:9; Ufunuo 12:7), Gabrieli (Danieli 8:16; 9:21; Luka 1:19, 26) na shetani (Ufunuo 12:9).

**B. Muumbaji Wao**

Malaika waliumbwa na Mungu (Zaburi 148:2-5) kabla ya ulimwengu (Ayubu 38:7). Malaika hawazai "watoto" kama mwanadamu azaavyo watoto (Luka 20:35) na hawafi (Luka 20:36), idadi yao ni sawa. Japo hatuelezwi kuwa ni wangapi lakini ni wengi (Waebrania 12:22; Ufunuo 5:11).

Tunajua na kukubali kwamba Mungu ni mkamilifu (Mathayo 5:48) na hana dhambi (2 Wakorintho 5:21). Kwa kuwa ni mkamilifu tunaelewa kwamba hata alivyoviumba aliviumba katika njia ya ukamilifu ***"hakuna uovu katika Yeye"*** (Zaburi 5:4). Hii inatuonesha kwa shetani aliyeumbwa bila dhambi na halafu akaamua kumuasi Mungu (Ezekieli 28:12-15; Isaya 14:12-14).

Watu wengine huamini kwamba malaika ni watu waliokwisha kufa. Malaika wamekuwepo tangu zamani kabla ya mwanadamu na si wanadamu waliokwisha kufa bali wana uumbaji wao tofauti kabisa.

**C. Muundo Wao**

Tunaelewa kwamba malaika wana uongozi na muundo wao kwa sababu hawa wako pamoja (Zaburi 89:5,7) na wamepangwa kwa ajiri ya vita (Ufunuo 12:7).

Daraja la juu kabisa ni "archangel", ikimaanisha kuwa ni malaika mtawala. Mikaeli (Yuda 9), anayesemekana kuwa ni Mkuu (Danieli 10:13) na ndiye mwenye cheo cha archangel. anatajwa kama malaika kiongozi wa Bwana katika vita dhidi ya shetani (Ufunuo 12:7), kwa hiyo inaonekana kwamba kuna malaika wa cheo cha archangel mmoja, ana sauti ya pekee (1 Wathesalonike 4:16).

Tunaona kwamba malaika wanaweza kupangwa kama "watawala" (Warumi 8:38; Waefeso 1:21; 3:10; 6:12; Wakolosai 1:16; 2:10, 15), "mamlaka" (Waefeso 1:21; 2:2; 3:10; 6:12; Wakolosai 1:16; 2:10, 15; 1 Petro 3:22), "nguvu" (2 Petro 2:11), or "enzi" (Waefeso 1:21; Wakolosai 1:16; 2 Petro 2:10; Yuda 1:8). Hii ni namna tu ya vile walivyo katika utawala wao.

Kuna makundi mawili ya malaika yanayojulikana kama "Maseraphi" na "Makerubi." Maseraphi wametajwa katika sura moja tu kwenye Biblia na wanaelezwa kuwa na Mabawa sita na wana mfano wa miili kama ya mwanadamu (Isaya 6:2, 6). Ni malaika wanaotakasa kwa moto (jina lao lina maana ya Kuunguza).

Makerubi ni aina nyingine ya malaika walio na nafasi ya juu kabisa katika uongozi wa malaika na shetani alikuwa katika kundi la malaika hawa (Ezekieli 28:14, 16). Baada ya anguko la Adamu na Eva matokeo yao ilikuwa ni kufukuzwa katika Bustani ya Edeni, na makerubi waliwajibika katika kuilinda bustani ili mtu asije kuingia na kula tena mti wa uzima katika bustani (Mwanzo 3:24).

Tunaona makerubi walikuwa ni Muhimu sana hata katika hekalu walikuwa wamechorwa kwenye sanduku la agano (Kutoka 25:18-22), nguo za kitani (Kutoka 26:1) na pazia (Kutoka 26:31). Musa alimsikia Bwana akimwambia kutoka katika kiti cha rehema amekaa katikati ya makerubi wawili (Hesabu 7:89).

Makerubi walikuwa ni muhimu sana katika hekalu ya Sulemani. Walikuwepo makerubi wawili waliotengenezwa kwa miti ya mizeituni, wamefunikwa kwa dhahabu na walikuwa na urefu wa futi 15 (5.5

mita) upana (1 Wafalme 6:23-28). Walinyoosha mabawa yao juu ya mahali pa sanduku na kulifunika (1 Wafalme 8:6-7). Walikuwa wamenakshiwa katika kuta na milango (1 Wafalme 6:29-35). Waliwekwa katika baadhi ya samani zilizokuwa katika Hekalu (1 Wafalme 7:29, 36).

Katika maono ya Ezekieli tuynaona Makerubi wakihamisha chumba cha kiti cha enzi cha Mungu (Ezekieli 10:1-22). Inaeleweka katika sehemu ya Biblia kwamba Makerubi wanasehemu katika historia japo sehemu hii haieleweki kwa urahisi. Majukumu yao si hayo tu bali hata katika utawala wa Yesu wa miaka elfu katika hekalu (Ezekiel 41:18, 20, 25).

Kitu cha muhimu kwa Makerubi ni kwamba ni muhimu sana katika sehemu ya mpango wa Mungu tutawaona kwa upana zaidi baadaye katika masomo yetu.

**D. Huduma Yao**

Malaika wamekuwepo na kuhusika katika matukio makubwa ya historia ya mwanadamu. Walifurahi na kushangilia wakati Mungu alipoumba dunia ya kuishi (Ayubu 38:6-7). walihusika katika kutoa sheria za Musa (Wagalatia 3:19; Waebrania 2:2) na hata katika mafunuo ya kweli ya Mungu (Danieli 7:15-27; 8:13-26; 9:20-27; Ufunuo 1:1; 22:6, 8). Hawahusiki na Israeli tu (Danieli 12:1), bali na mataifa mengine pia (Danieli 4:17; 10:21; 11:1; Ufunuo 8-9, 16).

Malaika walisema juu ya kuzaliwa kwa Yesu (Mathayo 1:20), waliwatahadhalisha wazazi wake wakimbilie Misri (Mathayo 2:13-15), wakawaeleza wakati wa kurudi kutoka Misri (Mathayo 2:19-21), walitumika moja kwa moja kwake wakati wa kujaribiwa na shetani (Mathayo 4:11), na hata katika bustani ya Gethsemane (Luka 22:43). Walikuwepo wakati wa kufufuka kwake (Mathayo 28:1-2) na hata katika kupaa kwake kwenda kwa Baba (Matendo 1:10-11).

Malaika walikuwa na nguvu kipindi cha kanisa la kwanza wakiwaelekeza wainjilisti kwa wale walikuwa tayari kuipokea injili (Matendo 8:26; 10:3), wakitoa maono kwa wale waliokuwa wakihitaji maelekezo (Matendo 10:3, 7), wakileta majibu kwa wanaoomba (Matendo 12:5-10) na kutahadharisha watu kutoka katika hatari (Matendo 12:11). Watahusika pia katika mazingira ya kurudi kwa Yesu Kristo (Mathayo 25:31; 2 Wathesalonike 1:7), pamoja na hukumu (Ufunuo 7:1; 8:2).

Malaika humsifu Mungu (Zaburi 148:1-2; Isaya 6:3), wanamwabudu (Waebrania 1:6; Ufunuo 5:8-13) na kubeba maelekezo yake (Zaburi 103:20; Ufunuo 22:9).

Malaika pia huhusika katika hukumu ya wasio haki. wanatangaza hukumu iliyo karibu (Mwanzo 19:13; Ufunuo 14:6-7; 19:17-18), hufanya hukumu kulingana na maelekezo ya Mungu (Matendo 12:23; Ufunuo 16:1) na watahusika katika kuwagawa wenye haki na wasio haki (Mathayo 13:39-40).

Malaika huwasaidia waumini (Waebrania 1:14) na tunaelezwa kwamba ***"tusichoke kuwakaribisha wageni kkwa sababu kwa njia hii tumewakaribisha malaika pasipo kujua"*** (Waebrania 13:2). Wanaangalia kile Wakristo wanachotenda (1 Wakorintho 4:9) na wakati mwingine huja kututia moyo (Waefeso 3:8-10; 1 Petro 1:10-12). wakati wa shida na mahitaji (Matendo 27:23-24). Tunapokufa malaika hutuchukua kwenda mbinguni kwa Baba (Luka 16:22).

**E. Shetani**

**1. Shetani ni Nani**

Shetani ni kiumbe aliye na akiri (2 Wakorntho 11:3), Hisia (Ufunuo 12:17; Luka 22:31) na uwezo wa kuamua (Isaya 14:12-14; 2 Timotheo 2:26). Kuna watu wengine wanaamini kwamba Shetani si kiume bali ni maovu. Yesu anaeleza kwamba na Shetani naye atahusika kwa matendo yake na siku moja atahukumiwa katika ziwa la Moto (Mathayo 25:41). Ni vigumu sana kuhukumu maovu na kutoamini kwamba shetani si kiumbe ni kukana Ukweli wa Mungu. Shetani amekuwa na hali ya kukataa neno la Mungu tangu bustani ya Edeni (Mwanzo 3:1-5).

**2. Nini Kilitokea**

Shetani alikuwa na nafasi ya juu aliyeumbwa kamili kabisa lakini akatenda dhambi (Ezekieli 28:12-15 ambapo "Mfalme wa Tiro" anahusika kama kielelezo cha nini kilitokea kwa shetani. Mfalme wa Tiro alikuwa na Bustani nzuri lakini haikuwa katika eneo la Bustani ya Edeni). Jiwe zuri llilo kuwa kifuniko chake (28:13) na ukweli kwamba aliasi "utakatifu wake" (28:18) unaonesha kwamba alikuwa ni malaika kuhani mkuu. Kama kuhani mkuu na kupitia "biashara yake isiyo na mwisho" (inahusika na kujiinua kwake bibafsi), alikuwa na uwezo wa kuongoza theruthi ya kundi la Malaika wengine (Ufunuo 12:4).

Shetani akaamua kumjaribu Mungu. Hii inaonekana katika maelezo yake yaliyo katika Isaya 14:12-14. Dhambi yake ilikuwa ni majivuno (1 Timotheo 3:6) na inaonekana katika maelezo matano yake binafsi

(kile ninachotaka, si kile Mungu anachotaka) imenakiliwa katika Isaya. Shetani aliye umba dhambi (Ezekieli 28:15) na atawajibika nayo (Mathayo 25:41). Ilitokea Moyoni mwake (Isaya 14:13).

Maneno yake ya kwanza yalikuwa, ***"Nitapanda hadi mbinguni"*** inayoonesha tamaa ya kuwa sawa na Mungu. Maneno yake ya pili, ***"Nitainua enzi yangu juu ya nyota za Mungu,"*** inaonyesha nia yake ya kutawala uumbaji wa malaika wa mbinguni. Tatu, ***"Nitakaa katika mlima wa kusanyiko,"*** inaonyesha sehemu ya mambo yaliyofanyika katika miungu ya Babeli, walioaminiwa na Wababeli kutawala ulimwengu. Shauku yake ya nne, ***"Nitapanda juu ya kimo cha mawingu,"*** inaonyesha tamaa ya kuchukua utawala wa Mungu (ambaye mara zote anahusishwa na Mawingu). Tano, ***"Nitakuwa kama aliye juu,"*** inaonyesha shauku ya mamlaka na nguvu ili kwamba achukue nafasi ya Mungu.

Baada ya kuona asili ya dhambi ya shetani ni rahisi kuona kwamba kwa nini tunaelezwa ***"Msitende neno lolote kwa mashindano wala kwa majivuno bali kwa unyenyekevu kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake"*** (Wafilipi 2:3). Kama tunakuwa na majivuno na Ubinafsi tunamuiga shetani.

**3. Majina ya Shetani na Kazi Zake**

Majina na kazi aliyopea zinatuonessha sifa zake. anaitwa "Nyota" ya asubuhi" (Isaya 14:12), inayomaanisha "Mbeba Nuru" na limetafasiriwa toka Lugha ya Kilatini kama "Lusifa." Yesu Kristo ndiye "Nyota ya Asuhuhi" (Ufunuo 22:16) inayotufundisha kwamba shetani amekuwa mtu wa kutapeli tangu kuasi kwake.

Anaitwa shetani; neno hili linatokana na neno la Kiebrania, ambalo ni "SHETANI." Lina maanisha "anayetawala" (Hesabu 22:22, 32; 1 Samweli 29:4; 2 Samweli 19:22; 1 Wafalme 5:4; 11:14, 23, 25; 1 Nyakati 21:1; Ayubu 1:6, 7, 8, 9, 12; 2:1, 2, 3, 4, 6, 7; Zaburi 109:6; Zekaria 3:1,2; Mathayo 4:10; 12:26; 16:23; Marko 1:13; 3:23, 36; 4:15; 8:33; Luka 10:18; 11:18; 13:16; 22:3, 31; Yohana 13:27; Matendo 5:3; 26:18; Warumi 16:20; 1 Wakorintho 5:5; 7:5; 2 Wakorintho 2:11; 11:14; 12:7; 1 Wathesalonike 2:18; 2 Wathesalonike 2:9; 1 Timotheo 1:20; 5:15; Ufunuo 2:9, 13, 24; 3:9; 12:9; 20:2, 7). Shetani huwaudhi Waumini kila wakati (Ufunuo 12:10), lakini Kristo Bwana hutulinda (1 Yohana 2:1-2). Shetni huwajaribu wetu watende dhambi (Mwanzo 3:1-5; Mathayo 4:3; 1 Wathesalonike 3:5; Matendo 5:3; 1 Wakorintho 7:5).

Anaitwa Ibilisi. Neno hili linatoka katika Kiyunani "DIABOLOS" linalomaanisha "Muongo" (anayedanganya) (Mathayo 4:1, 5, 8, 11; 13:39; 25:41; Luka 4:2, 3, 6, 13; 8:12; Yohana 6:70; 8:44; 13:2; Matendo 10:38; 13:10; Waefeso 4:27; 6:11; 1 Timotheo 3:6, 7; 2 Timotheo 2:26; Waebrania 2:14; Yakobo 4:7; 1 Petro 5:8; 1 Yohana 3:8, 10; Yuda 1:9; Ufunuo 2:10; 12:9, 12; 20:2, 10).

Anaitwa nyoka wa kutu, hii inaonyesha ujanja wake (Mwanzo 3:1, 2, 4, 13, 14; 2 Wakorintho 11:3; Ufunuo 12:9, 14, 15; 20:2).

Shetani anaitwa pia ni "Joka kubwa jekundu" inayoonyesha asili yake katika vita (Ufunuo 12:3, 4, 7, 9, 13, 16, 17; 13:2, 4, 11; 16:13; 20:2).

Anahusishwa na "Beelzebul" inayomaanisha "bwana wa machafu."[104] Ni sifa aliyopewa kwa sababu ni mtawala wa mapepo (Mathayo 10:25; 12:24, 27; Marko 3:22; Luka 11:15, 18, 19).

Mtume Paulo alimwita "Mnafiki" inayoonyesha uasi wake na udhaifu wake (2 Wakorintho 6:15).

Shetani anaitwa ***"mtawala wa ulimwengu huu"*** (Yohana 12:31), ni ***"mungu wa dunia hii"*** (2 Wakorintho 4:4), ***Mkuu wa anga"*** (Waefeso 2:2) na ***"roho inayotenda kazi hata sasa kwa wasiotii"*** (Waefeso 2:2). Kile maandiko haya yanasema ni kwamba Shetani ni mpinzani wa Mungu.

**4. Kazi Anazozifanya Sasa**

Kusudi la Shetani ni kuvamia mpango wa Mungu kwa kusudi la kuuharibu ili kwamba aweze kufanikiwa katika tamaa zake (Isaya 14:12-14). Kusudi la Shetani ni kuharibu mipango ya Mungu na kumwacha Mungu. Atatumia njia yoyote ili afanikiwe. Hii ni pamoja na malaika zake wanaoitwa mapepo (1 Timotheo 4:1), na watu ambao ***"hujigeuza kama watumishi wa haki"*** (2 Wakorintho 11:13-15).

Mipango ya shetani ya kuvamia mipango ya Mungu inahusisha ushindani mkubwa wa mifumo yake ya kuwa mkuu katika nafasi ya Mungu. Mifumo ya utawala huu inatoka katika neno la Kiyunani "Dunia" yaani "COSMOS." Kusudi kuu la neno "COSMOS" ni "Utawala."[105]

Kukamilisha mpango wake, Shetani kwanza "Hupofusha akili" (2 Wakorintho 4:4) ili kwamba wasioamini wasiikubali injili ya Yesu Kristo na hujaribu kulichukua neno la kweli walilolisikia (Luka 8:12). "Kupofusha akili" kwa wasioamini mara nyingi hutumia kuwageuza Wakristo wengine walioasi kwamba ***"wajifanye kama watu wa Mungu lakini wanaikana nguvu yake"*** (2 Timotheo 3:5). Kwa nje wanaonekana kama " Wakristo" lakini kwa ndani ni Shetani (Mathayo 23:25-26). Huu mfumo unakuwa na maumbo mengi unaohusisha na kukana neno la Mungu (Wakolosai 2:16-23) kwa kuendeleza dhambi (Warumi 1:32; Ufunuo 2:24). Shetani anatumia kila njia katika Ulimwengu ili amfanye mtu asiingie katika ufalme wa Mungu (Wakolosai 1:13; 1 Yohana 2:15-17).

Mtu anapompkea Yesu Kristo kama mwokozi anakuwa ameushinda ulimwengu, mifumo aliyoiweka shetani (1Yohana 5:4-5). Shetani hawezi kuwaacha waliookoka; anakuja kama "lusifa" ili "aibe, auwe na kuharibu" (Yohana 10:10) kwa sababu ya chuki aliyo nayo na Mwanadamu (Zaburi 69:1-4; Mathayo 10:22).

Kitu cha muhimu anachotaka kukiharibu ni ushuhuda wa kweli wa Wakristo ili wengine wasiingie katika ufalme wa Mungu. Anawajaribu Waumini kwa kuwafariji na kuwapa kuitamani dunia na mambo yake (1 Wathesalonike 3:5; 1Yohana 2:15-17). Anawajaribu waumini wajaribu kuficha ubinafsi wao (Matendo 5:1-3) na kweli anawajaribu katika kutenda mambo mabaya (1 Wakorintho 7:5).

Shetani ***"anazungukazunguka kama Simba aungurumaye, akitafuta mtu ammeze"*** (1 Petro 5:8). Hii ina maana ya kwamba anatafuta mtu fulani ambaye ataanguka katika majaribu yake ili kwamba "awahuzunishe ndugu zake katika Kristo" (Ufunuo 12:10); ataweka nguvu yake yote aliyoruhusiwa kwa waumini ili kwamba ampate mtu atakaye mfanya asiwe mfuasi wa Bwana (Luka 22:31).

Waumini wanatakiwa kuelewa kwamba Shetani, kwa sababu ya asili yake (Yohana 8:44), hatendi lililo jema. Atatumia mtu yeyote au kitu chochote kukamilisha malengo yake.

**F. Malaika wa Shetani**

Malaika wa shetani ni wale wanaoamua kujiunga naye, hii ni pamoja na theluthi moja ya idadi ya malaika, (Ufunuo 12:4). malaika hawa wanaitwa "mapepo" au "roho chafu." Huwa ni viumbe walioasi pamoja na shetani na yeye ni "mkuu wao" (Mathayo 12:24). Neno la Kiyunani limetafasiri "mapepo" ni neno linalotokana na miungu wachafu. "Roho chafu" ni roho zinazotumiwa na ibilisi katika maovu. Kama tulivyokwisha zungumza, wana nafasi mbalimbali za mamlaka katika serikali ya shetani. Mapepo yana nguvu (Marko 5:3; Matendo 19:16) na hivyo shetani anaweza kukamilisha mambo mengi kwa ajiri ya nguvu zao.

Malaika wa shetani wana akili inayoonekana katika utambulisho wa Yesu (Marko 1:24), utambuzi wa mamlaka zao (Mathayo 8:29), na maendeleo ya mafundisho yao (1 Timotheo 4:1-3). Wanafahamu mpango wa wokovu lakini hawaukubali (Yakobo 2:19).

Kazi ya malaika wa shetani ni pamoja na kutuma chochote kinachopingana na Mungu. Wanajaribu kuiharibu Ufunuo wake au anajaribu kudai kwa Bwana wao ni chanzo cha mema yote.

Mapepo yamehusishwa katika mambo yote ya miungu ya asili (Matendo 16:16). Miungu hufanyika pale mtu anapoweka kitu chochote au jambo lolote kati ya mila fulani na Mungu aliye hai. Sanamu inaweza kuwa imetengenezwa kwa mbao,jiwe au anaweza kuwa ni mtu kama tutakavyooona katika kumwabudu mpinga Kristo (Ufunuo 13:15). Mwanadamu anaweza kuabudu hata akili yake (Yohana 5:39-40). Mapepo yanataka mwanadamu aabudu kitu chochote lakini si Mungu.

Mapepo huleta hata dini za uongo. Dini za uongo ni mfumo wa kumuhimiza "Kristo" bandia (1 Yohana 4:1-4), wokovu kwa sababu ya kazi (1 Timotheo 4:3-4 linganisha Waefeso 2:8-9), au uhuru wa kutenda dhambi huku ikidai kwamba maovu ni mazuri (Ufunuo 2:20-24 linganisha Wagalatia 5:13; Warumi 6:1).

Mapepo yanauwezo wa kuleta magonjwa ya mwili (Mathayo 9:33) au kichaa (Marko 5:4-5) kwa watu. Hata hivyo si kila ugonjwa ni wa shetani au kazi ya mapepo Biblia imetofautisha hapa kati ya ugonjwa wa asili na ugonjwa wa mapepo (Mathayo 4:24; Marko 1:32, 34; Luka 7:21; 9:1).

Mapepo humiliki watu (Luka 8:28-31) wanyama (Luka 8:32-33). "Kumiliki" ina maana ya kuchukua nafasi ya kuongoza mtu fulani kwa kuingia ndani ya mtu huyo. Tunaelezwa kwamba ***"Mkuu ni yule aliye ndani yako (Roho Mtakatifu) zaidi yabyule aliye katika ulimwengu huu"*** (1 Yohana 4:4), ni vigumu kwa Muumuni kumilikiwa na mapepo. Jpo waumini wanaweza kuwa chini ya msukosuko wa mapepo si kwamba watakuwa wamemilikia na mapepo. Tutakapotegemea kwamba mapepo yanamiliki italeta mabadiliko ya kuyakimiza katika watu (Luka 8:28-31), tusisahau Shetani mwenyewe anaweza kuonekana kama "malaika

wa nuru" (2 Wakorintho 11:13-15). Kitu cha muhimu kuamua kama "roho" ina danganya ni kwa ujumbe uliotolewa na Yesu (1 Yohana 4:1-4).

Ni muhimu kufahamu njia shetani anatumia kujaribu "kuwameza" waumini (2 Wakorintho 2:11). atatupatia utambuzi, pesa au utajili wa nama yoyote ile, mamlaka, au heshima. Njia yake ya kawaida ni kuwapa waumini kile Mungu alimpa. Mungu aliwapa waumini "akili za utambuzi" kwa sababu nio wana wake (1 Yohana 3:1). Mungu amempa bahati kwa sababu ameshawapa watu wake maisha ya milele na wenyeji wa mbinguni (Waefeso 2:19-20). Muuumini amepewa nguvu kwa sababu yko pamoja na Bwana Mungu mwenyewe (Warumi 8:1-2). Amewapa heshima kamba ae na ***"amani inayopita akili zote"*** (Wafilipi 4:7).

Tunapaswa kuwa waangalifu tunapojifunza njia ya shetani kwa sababu kama atatufanya tujifunze njia zake zaidi ya njia za Mungu atakuwa ameshinda. Shetani amekuwa akitumia njia zake miaka elfu na amekwisha fanikiwa katika watu wengi. Njia ya kutambua njia za shetani ni kufahamu kitu chenyewe ili kwamba upate kukiepuka haraka iwezekanavyo.

Kama tukishindwa kumwelewa shetani au mapepo katika maisha yetu tutakuwa katika kipindi kigumu cha Mungu na Ibilisi. Mtume Paulo anatuonya kwamba,

> ***Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu mpate kuweza kushindana siku ya uovu na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama.*** (Waefeso 6:12-13)

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 6, Sehemu ya 2

1. **Soma sura hizi na utuambie sifa za malaika walizonazo:**
   a. 1 Petro 1:12
   b. Luka 2:13
   c. Waaamuzi 6
2. **Soma Luka 24:4. Je malaika anaweza kuchukua umbo la wanadamu?**
3. **Soma Waebrania 2:6-7. Je mwanadamu anawakilisha umbo la juu au la chini katika viumbe?**
4. **Soma Zaburi 148:2-5. Nani aliwaumba malaika?**
5. **Soma Luka 20:35. Je wana watoto?**
6. **Soma Waefeso 6:12. Je malaika wa shetani wanampangilio wa kiutendaji?**
7. **Soma Ufuno 12:7. Ni malaika yupi ndiye kiongozi wa Jeshi la Mungu?**
8. **Ni malaika yupi ametajwa sana katika maandiko, ni Makerubi au Maserafi?**
9. **Soma Waebrania 1:14. Nini kusdi la malaika?**
10. **Soma Ufunuo 12:7-9. Shetani ni nani?**
11. **Soma Mathayo 25:41. Nini mwisho wa shetani?**
12. **Soma Isaya 14:12-14. Dhambi ya asili ya shetani ilikuwa ni nini?**
13. **Jina "Shetani" linamaanisha nini?**
14. **Je jina "Ibilisi" linamaanisha nini?**
15. **Je maelezo yake ya kwamba yeye ni "nyoka" inamaanisha nini?**
16. **Soma 2 Wakorintho 11:13-15. Shetani na wafanyakazi hutumia nini katika kudanganya?**
17. **Soma 2 Wakorintho 4:4. Shetani na jeshi lake wanataka kukamilisha nini?**
18. **Nini kazi mbili za malaika wa Shetani?**

**19. Soma 1 Yohana 4:1-4. Ni sifa zipi zinazotumika kuonesha kwamba roho huyu ni kweli au si wa kweli?**

**20. Soma Waefeso 6:12-13. Vita halisi ya wakristo iko nyume ya nini?**

# Sehemu ya 3
# Mwanadamu (Anthropology)

**A. Uumbaji wa Mwanadamu**

Uumbaji wa mwanadamu ulipangwa na Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu (ambaye ameoneshwa kuwa ni Mungu). Mpango umenakiliwa katika mstari unaosema, ***"Tufanye mtu kwa mfano wetu"*** (Mwanzo 1:26). Utatu wote wa Mungu ulihusika katika uumbaji wa mwanadamu.

Mpango ulihusika na kumuumba mwanadamu kwa "Sura" na "mfano" wa Mungu. Maneno mawili ya "sura," "TSELEM" katika Kiebrania na "EIKON" Kiyunani unahusika na sehemu ya vitu vya mwanadamu. Maneno mawili ya "mfano," "DEMUTH" katika Kiebrania na "HOMOIOSIS" Kiyunani na sehemu ya vitu vya mwanadamu. Maelezo haya sehemu ya vitu na kutokuwa na sehemu ya vitu ni ya jumla na hayatakiwi kutumika katika hali ya kipinga. Mpango wa Mungu ulikuwa ni kumfanya mwanadamu kwa sehemu ya vitu na kwa sehemu isiyo na vitu. Mwanadamu awe hai,mwenye akili,mwenye maadili, mwenye maamuzi kama Mungu na bila kuwa Mungu. Ili kwamba awe na ushirika na Mungu.

Mungu mwenyewe aliomfanya mtu wa kwanza. Tunaambiwa kwamba, ***"akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai, na mtu akawa nafsi hai"*** (Mwanzo 2:7). Neno lililotafasiri "kiumbe" ni neno la Kiebrania "NEPHESH" lenye maana ya "nafsi". Mungu alitengeneza vitu sehemu ya mwanadamu tofauti na vitu alivyokuwa ameviumba–mavumbi ya ardhi. Alifanya nafsi ya Mtu (sehemu ya mtu si kutoka katika vitu) kutoka katika sehemu ambayo haina kitu (Mwanzo 1:27). halafu aliviunganisha vyote viwili na kufanya kitu kinachoitwa "mwanadamu."

Wasomaji ni vizuri kuelewa kwamba Adamu alikuwa ni kiumbe kamili. Hakuzaliwa kwa hali ya kawaida. Aliumbwa akiwa ni mwanaume mzima na akawekwa aishi akiwa na akiri timamu. Mungu akamweka katika Bustani ya Edeni na Mungu akamwambia aviite majina viumbe vyote (Mwanzo 2:8, 19).

Mungu alisema kwamba, ***"si Vizuri mtu huyu aishi peke yake"*** (Mwanzo 2:18), hivyo akaamua kumfanyia Adamu msaidizi atakaye mkamilisha. Ataitwa mwanamke kwa sababu ametoka katika ubavu wa mwanaume kwa njia ya upasuaji wa Kiungu (Mwanzo 2:18-23) na jina lake atakuwa ni Eva kwa sabu alikuwa ni ***"mana wa viumbe vyote"*** (Mwanzo 3:20). Inasema kwamba Mungu "alimfanya" mwanamke kwa vitu vinavoonekana ("Ubavu" wa Adamu), akaufunika kaika mwili wa mwanamke na akampulizia pumzi (Mwanzo 2:21-23). Wote wawili mwanaume na mwanamke walikuwa ni matokeo ya uumbaji maalumu wa moja kwa moja. hawakuumbwa toka katika uumbaji wa chini.

Mungu aliumba wanyama ***"nje ya vumbi la ardhini,"*** na akawapa uhai (Mwanzo 2:19). Wanyama hwakuumbwa kwa sura ya Mungu*.* Mtu anaweza sema kwamba wana uhai na pia wana akili lakini hawana uwezo wa kufanya maamuzi (maamuzi ya mema na mabaya). Wana uhai lakini hawana uwezo wa kufikiri (2 Petro 2:12; Yuda 1:10).

**B. Anguko la Mwanadamu**

Mwanaume na mwanamke (Adamu na Eva) ambao Mungu aliwaumba akawaweka katika Bustani ya Edeni (Mwanzo 2:10, 15). Kazi ya mwanaume ilikuwa ni kuitunza na kuilima bustani (Mwanzo 2:15). Mungu akamwambia waweza kula kutoka katika kila mti isipokuwa mmoja ***"mti wa ujuzi wa mema na mabaya,"*** ambao ulikuwa katikati ya bustani karibu na "mti wa uzima" (Mwanzo 2:16). Adamu alitahadharishwa (kabla Bwana hajamuumba Eva) kwamba kama atakula kutoka katika mti wa ujuzi wa mema na mabaya ni hakika "atakufa" (Mwanzo 2:17) ikionesha kwamba hukumu ya kuvunja neno la Mungu itaathiri vyote viwili mwili na Roho (neno la Kiebrania limerudia neno "kufa" kama inavyosema katika maandiko "utakufa hakika utakufa").

"Nyoka" (kwa ufunuo wa shetani Ufunuo 12:9) aliweza kwenda kwa mwanaume kwa njia ya mwanamke. Aliweza kumdanganya Eva (2 Wakorintho 11:3; 1 Timotheo 2:14) na hivyo akachuma lile tunda lililokuwa limekataliwa. Eva akampa na Adamu na yeye akavunja amri ya Mungu (Mungu 3:6).

Ngoja tuainishe kwa undani mambo yaliyopelekea anguko la mwanadamu. Elewa kwamba nyoka alikuja kwa mwanamke ambaye hakuwa na mwanaume kwa kipindi hicho. Mwanaume alikuwa ni mwenye mamlaka katika bustani hiyo kwa sababu alipewa majukumu ya kuitunza (ina maana ya kuilinda) Bustani (Mwanzo 3:1). Nyoka akenda kwa mtu ambaye kwake ilikuwa ni rahisi kumnasa.

Shetani alianza mazungumzo kwa swali ambalo lilikuwa kinyume kabisa na kile Mungu alichokuwa amekiamuru. Nyoka alimuuliza kama Mungu alikuwa amewakatalia kula matunda ya miti yote katika Bustani (Mwanzo 3:1). Kwa mtazamo hili ni swali la mtego la kujua kama hawaruhusiwi kula tunda lolote

ndani ya bustani. Swali lilianza kwa mtego wa wema wa Mungu. Swali pia lilitaka kujua kipi mwanamke anachokifahamu na anachukuliaje amri za Mungu.

Mwanamke alimjibu nyoka kwa sauti ya upole (Mwanzo 3:2-3). Akijaribu kusahihisha kauli ya nyoka na akamjibu, tatizo lilikuwa ni kwamba akajaribu kujibu bila kutumia amri za Mungu na badala yake akaongeza kitu kingine; aliongeza "usiliguse." Watu wengine hufikiri kwamba labda Adamu aliongeza kipande hicho alipokuwa akimweleza Eva amri hizo. Kama ilikuwa ni Adamu au Eva aliyeongeza kipande hicho matokeo yalikuwa ni sawa kwamba walikuwa wamanza kuongeza katika neno la Mungu. Hapa haijalishi kama ni Adam au Hawa aliyeongeza vifungu vya maneno matokeo ni yale yale kwamba walikuwa wanaanza. Shetani akatumia nyongeza hiyo na kuleta hukumu ya Mungu (Mungu 3:4) na hisia zake (Mwanzo 3:5). Akaonyesha ufahamu wake wa mema na mabaya kama kitu ambacho Mungu amewaficha na hataki wao wafahamu.

Kumbuka kwamba "wema" umeelezwa kwamba ndicho kitu Mungu hufanya (Mwanzo 1:4, 10, 12, 18, 21, 25, 31; 2:9, 12). Aina ya wema si jambo la kutamani kujua kwa sababu linaweza kuwa na kitu ambacho Mungu hayumo lakini si la madhara kwa wengine. Kwa mfano mtu anaweza kumpa mtu mwenye kiu kitu cha kunywa akifikiri kwmba mtu yule ni wa msaada badala ya kumpa yule mtu mwenye kiu kitu cha kunywa kwa sababu ndicho kile Mungu anataka (Marko 9:41). Ni neno la wema linalomwacha Mungu nje. Kama tulivyojadili kazi ya shetani ni kuunda mbinu katika ulimwengu huu unaompinga Mungu.

Nyoka akaelewa mawazo na akili ya Mwanamke (Mwanzo 3:6). Kwa hali hii mwanamke akasimamishwa katika imani, akashindwa kumwamini Mungu na akaanza kujiamini mwenyewe. Shetani akamwamba atakuwa na akili kama Mungu (Mwanzo 3:5). Kama atakuwa na Busara kama Mungu hatakuwa na sababu ya Kumtegemea na badala yake atafanya mambo yake mwenyewe. Alikuwa katika dhabihu ya kuharibu kama yeye alivyokuwa akitaka kuharibu (Isaya 14:12-14). Tunafahamu kwamba ***"bila imani hatuwezi kumpendezesha Mungu"*** (Waebrania 11:6). Mwanamke hakumtumaini Mungu baada ya kula tunda lililokuwa limekataliwa. Shetani alikuwa amekwisha mpandikizia mawazo mwanamke huyu kwamba Mungu si mwema na hivyo hamwitaji tena na hivyo ataishi kwa furaha yake bila kumwamini Mungu tena (2 Wakorintho 11:3). Alikula.

Maandiko yanasema kwamba, ***"akampa na mumewe akala"*** (Mwanzo 3:6). hatuelezwi mazungumzo yoyote ya wote wawili kabla ya Adamu kula. Tunachoelewa ni kwamba adamu hakuongea na nyoka (1 Timotheo 2:14). Adamu akamtenda dhambi. Maandiko yanatueleza kwamba " Alikula" (Mwanzo 3:6). Wote alitenda dhabi lakini hukumu zikatofautiana.

Adamu na mwanamke mara wakajua kwamba wamekwisha vunja amri za Mungu na wakaogopa. akawa uchi (Mwanzo 2:25 linganisha 3:7) na wakaanza kutafuta namna ya kuficha aibu yao kwa kuvaa majani ya miti ili wajisitiri (Mwanzo 3:7). Halafu wakajificha ili Mungu asiwaone (Mwanzo 3:8). Hii ni mara ya kwanza ya mwanadamu kujaribu kujiokoa.

**C. Hukumu ya Mwanadamu Baada ya Anguko**

Nyoka alikuwa ni wa kwanza kupata hukumu. Alilaaniwa kuwa mla mavumbi ya Dunia (Mwanzo 3:14). Nyoka hakuwa shetani lakini (Shetani alkikuwa ndani ya nyoka [Ayubu 1:6; 2:1] pamoja na kwenda mbinguni kuwalaumu ndugu [Ufunuo 12:10]). Nyoka kama chombo shetani alihukumiwa kuogopa na mnyama ataambaaye katika dunia (Mwanzo 3:14).

Kwa kuwa shetani alikuwa ndiye anamwezesha nyoka kuzungumza na yeye pia alilaaniwa. Kulikuwa na kitu cha kuendelea kati yake na zao za mwanamke (Mwanzo 3:15). Na hii ndiyo kumbukumbu ya unabii wa Yesu Masihi. Inaonesha umuhimu wa kuzaliwa kwake neno "mbegu" imezungumzwa kama kitu kinachokuja kwa njia ya mwanaume (Mwanzo 12:7; 22:17, 18). Kwamba Masihi atazaliwa na Bikra imeelezwa baadaye katika maandiko (Isaya 7:14). Huu ni unabii ambao unabii wote wa Masihi unaanzia (linganisha Ufunuo 12:4-5). Nyoka atamuuma kisigino Masihi (ambayo ni picha ya msalaba), lakini masihi atamponda kichwa nyoka (ambao ni ushindi).

Laana ya kwanza ya dhambi ilikuwa ni maana ya hukumu ("wakaona aibu kwa utupu wao" Mwanzo 3:7) na kupoteza kwa ushirika wao ("wakajificha" Mwanzo 3:8).
Mwanamke aliambiwa ***"atazaa kwa uchungu"*** (Mwanzo 3:16) na kwamba atapenda kumtawala mme wake na wakati huo huo atapenda atawaliwe na mmme wake. Hili ndili jaribu Eva alilipata alipotaka kumtawala mme wake (kumpa tunda), lakini alimzuia.

Baadaye bwana alisikia malalamiko ya Adamu dhidi ya mwanamke (Mwanzo 3:17). Ni dhahiri kwamba Adamu hakumsikiliza. Mtu asipoelewa mstari huu anaweza kusema kwamba labda alikuwa hamsikilizi mkewe. Hiyo si kweli kwa sababu Mungu alimwambia Ibrahimu kumsikilia mkewe sara (Mwanzo 21:12).

Makubaliano ya maneno ya kila mtu yako katika nini Mungu alichokisema. Dhambi ya Adamu ilikuwa si kumsikiliza mkewe bali ilikuwa katika kukubali kula lile tunda lililokatazwa. Laana ya Adamu ilikuwa ni kazi nzito zitakazo mfanya apate riziki yake (Mwanzo 3:17-19).

Asili ya kukatazwa kula tunda haijasahaulika. Adamu alipotenda dhambi alikufa kiroho kwa hiyo akapoteza ushirika wake na Mungu. Kifo chake cha mwili kilikuwa miaka ya 930 baadaye (Mwanzo 5:5). Mungu alionyesha neema kwa Adamu na Eva alipowafunika kwa ngozi ya mnyama (Mwanzo 3:21). Kuwa na ngozi ya mnyama ina maana ya kwamba mnyama asiye na hatia aliuawa kama dhabihu. Hii ni picha ya hitaji la dhabihu kwa ajiri ya dhambi ambayo ilikua ikakamilishwa na Masihi (Waebrania 10:10, 12).

Adamu na Eva walivalishwa na Bwana na wakatolewa katika bustani ya Edeni (Mwanzo 3:22-24). Na hii ilikuwa inafanyika, ***"asije, akachuma kutoka katika mti wa uzima akala na akaishi milele."*** Si vigumu kueleza kwa nini Mungu alifanya kwa sababu ya anguko la mwanadamu isingelikuwa vizuri kuishi milele katika sehemu ya anguko chini ya laana. Kifo kwa walioamini ni kizuri kwa sababu watafufuliwa katika miili mipya mitakatifu kama Masihi wao Yesu Kristo (1 Yohana 3:2) na kutwaliwa mbinguni kuliko na mti wa uzima na hakuna laana (Ufunuo 22:2-3).

**D. Asili ya Mwanadamu**

**1. Mwili**

Mwili wa mwanadamu ulifanywa na Mungu kutoka katika vumbi la udongo katika sura yake (Mwanzo 2:7, 21). Adamu na Eva waliijuana na wakazaa watoto. Watoto wao wa kwanza walikuwa ni wawili kaini na habili (Mwanzo 4:1, 2). Na wanadamu wengine walitokana na Adamu na Eva. Jina la Eva linamaana ya, ***"mama wa viumbe vyote"*** (Mwanzo 3:20).

Mwili ni sehemu ya ndongo ya mwanadamu. Ina ogani za kuona, kugusa, kusikia kuonja na kunusa. Wote tunafahamu juu ya sehemu kuu za mwili kama vile kichwa, mikno na miguu. Ni muhimu kuelewa kwamba havina kazi inayofanana. Hatutembei kwa mikono yetu na wala kula kwa miguu yetu. Mwili wetu umeumbwa kutufundisha mwili wa Kiroho unaojulikana kama "Kanisa," "mwili wa Kristo" (Warumi 12:4-5). Waumini wote ni sehemu ya mwili wa Kiroho na wote wana umuhimu lakini wanakazi tofauti katika mwili (1 Wakorintho 12).

Mwili ni kitu cha ajabu, ulioumbwa na Mungu kuwa nyumba ya kitu ambacho hakikutokana na vitu vya dunia hii. Bwana aliutoa mwili wake kama dhabihu ya dhambi zetu (1 Wakorintho 11:24) na halafu akatuthibitisha kwa Baba ili tuwe ***"watakatifu, tusio na mawaa wala lawama"*** (Wakolosai 1:21-22). Bwana alilipa dhambi zetu kwa njia ya mwili wake (1 Petro 2:24).

Kwa namna fulani kama "wafananishwaji na Kristo" (1 Wakorintho 11:1), mwili wetu unapaswa kuonekana mbele za Mungu kama dhabihu hai ili kwamba apate kuitumia kulingana na mapenzi yake (Warumi 12:1-2). Kristo anapaswa kuonekana katika mwili wetu kwa kila namna ya maisha na hata kifo (Wafilipi 1:20).

Tunahimizwa kufanya sehemu yetu ili kuifanya miili yetu kuwa tayari kwa Ibaada (1 Wakorintho 9:27), tukijua kwamba siku moja tutawajibika kwa Bwana kwa matendo yote yaliyofanywa na mwili (2 Wakorintho 5:10). Sehemu ndogo ya mwili wetu inayojulikana kama, ulimi unapaswa kulindwa katika matamshi (Yakobo 3:2-5). Miili yetu inapaswa kutumika katika kubeba ujumbe wa kifo cha Yesu Kristo ili tuwe na uzima (2 Wakorintho 4:10).

Siku moja miili hii ya hapa duniani itabadilishwa na kuwa miili mipya ambayo haitakufa (1 Wakorintho 15:40-44). Itakuwa kama mwili wa Kristo uliofufuliwa na kutukuzwa (Wafilipi 3:20-21). Miili hii mipya itatufanya tuwe na uhusiano kamili na Bwana wetu Yesu Kristo (2 Wakorintho 5:6-8).

**2. Nafsi**

Nafsi ni sehemu ya vitu visivyotokana na vitu dhahiri katika mwili wa mwanadamu. Haionekani, haigusiki, haisikiki, kuonjeka wala kunusika. Kwa kuwa mwili hauwezi kuishi bila nafsi (Mwanzo 35:18), mara nyingi neno la Kiebrania "NEPHESH" na neno la kiyunani "PSUCHE" yametafasiriwa si nafsi tu bali ni "uzima."

Wakati Adamu alipoumbwa Biblia inasema, ***"Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi akampulizia puani pumzi ya uhai mtu akawa nafsi hai (nafsi)"*** (Mwanzo 2:7; 1 Wakorintho 15:45). Si katika upeo wa mwili huu kueleza neno lililotumika kueleza neno uzima na maana zake zingine. Hebu tuamini kwamba Mungu alimuumba Adamu na Eva akawapulizia pumzi ya uhai na kwamba wakawa wanadamu (Kutoka 1:5). "NEPHESH" linatumika katika uhai wa wanyama (Mwanzo 1:20, 21, 24, 30; 2:19).

Tunapotafuta kile hasa nafsi hutendaje ndani ya mwili tunapaswa kwanza kuelewa kwamba Mungu alifanya nafsi (Mathayo 12:18; Waebrania 10:38) na kwamba mwanadamu ameumbwa kwa mfano wake (Mwanzo 1:26-27).

Tunapaswa kuelewa kwamba ndani ya nafsi ya mwanadamu kuna hali ya kufanya maamuzi (maamuzi mazuri au mabaya). Inamaanisha kwamba ndani ya nafsi kuna hiari ya kufanya kabla ya kufanya maamuzi. Uwezo wa kuamua unaitwa Matakwa. Kwa kuwa katika nafsi ndipo kulipo na maamuzi hivyo tunapaswa kusema kwamba nafsi inahitaji iokolewe (Zaburi 33:18-19; Matendo 2:41; Waebrania 10:39; Yakobo 1:21; 1 Petro 1:8-9) na uponyaji wa dhambi (Zaburi 41:4). Yesu hakutoa mwili wake tu bali hata na nafsi yake ili kuwaokoa waliopotea (Mathayo 20:28; Marko 3:4; Yohana 10:11, 15, 17; 15:13) na hivyo kuwa ***"Mchungaji na Mlinzi wa nafsi zetu"*** (1 Petro 2:25). Kama nafsi haitaokoka itatupwa jehanamu (Mathayo 10:28; 16:26).

Baadhi ya maamuzi ambayo mwanadamu anapaswa kuyafanya ni pampja na kumpenda Mungu (Kumbukumbu la Torati 6:5; 10:12-13; 30:6), tujitoe kwa muumbaji wetu kwa kuyatenda yaliyo haki (1 Petro 4:19) na tujitoe maisha yetu (nafsi) kwa ajiri ya ndugu (1 Yohana 3:16). Nafsi ya mwanadamu ndiyo iliyo na vita (1 Petro 2:11) na ndipo walimu wa uongo huharibu na kuvuruga (2 Petro 2:12-14).

Kwa nyongeza kuwa sehemu ya maamuzi nafsi pia ni sehemu ya kufanyia hisia. Nafsi inaweza kuhurumia (Ayubu 30:25), Uchungu (2 Wafalme 4:27), huzuni (Zaburi 43:5; Yeremia 13:17; Mathayo 26:38), kuharibiwa (Luka 2:35), hatarini (Warumi 2:9) na kutopenda (2 Samweli 5:8). Yaweza kupenda (Wimbo ulio Bora 1:7; 3:1-4), kumwinua Bwana (Luka 1:46) na kuwa furaha (Luka 12:19).

**3. Roho ya Mwanadamu**

Neno kwa ajili ya roho ni "RUACH" kiebrania na "PNEUMA" Kiyunani. Hii ni sehemu ndogo kujifunza kutoka katika maandiko kwa sababu maneno yote mawili yametumika na yanaweza kutoa hewa, pumzi, Roho Mtakatifu, roho chafu, na roho ya mwanadamu kwa kutegemea naye ale yaliyozungumzwa na kutumiwa.

Roho ya mwanadamu ni nguvu ya kiroho na ni sehemu ya vitu vilivyoumbwa kutokana na vitu visivyoonekana katika sehemu ya mwanadamu na Mungu (Muhubiri 12:6-7; Zekaria 12:1; Waebrania 12:9), katika Roho Mtakatifu (Yohana 3:6; 6:63). roho ya mwanadamu ni muhimu kwa uzima (Luka 8:55; Yakobo 2:26).

Kwa kulinganisha na kanuni za ufasiri ambazo tumekwisha jifunza tutachukua sura muhimu tuitumie katika kuangalia kanuni muhimu za kweli juu ya roho ya mwanadamu. Tunapoangalia katika sifa za roho ya manadamu tutaona kwa haraka sifa nyingi za roho ya mwanadamu, nafsi na moyo (majadala wetu wa baadaye) ziko sawa. Tunapaswa kuelewa kwamba Neno la Mungu linatuambia kwamba roho ya mwanadamu ni tofauti na moyo wa mwanadamu na nafsi (Waebrania 4:12).

Tunapojifunza mistari inayohusiana na roho ya mwanadamu tunaona kuwa ina kazi nne:

**a. Kupokea Habari**

Inaweza kupokea habari zinazokuja kama vile neema (Wagalatia 6:18; Philemoni 1:25), maadili ya kweli (Malaki 2:15-16), na ufunuo (Waefeso 1:16-17). Inaweza pia kukemewa (Matendo 17:16) na kuvurugwa (1 Nyakati 5:26; Ezra 1:1, 5).

**b. Kutathmini Habar**

Roho ya mwanadamu inaweza kutathmini habari ambazo imepokea. Inaweza kutambua matukio (Ayubu 6:4), kujua mawazo yetu (1 Wakorintho 2:11), kutafakari (Zaburi 77:6), kuelewa (Ayubu 20:3; 32:8) na kuwa wazi na kutahmini (Kutoka 28:3; Kumbukumbu la Torati 34:9; Waefeso 1:16-17).

**c. Kufanya Maamuzi**

Roho ya mwanadamu inapopokea na kutahmini habari inaweza kuamua kipi cha kufanya. Yaweza kuamua kuvumilia kuongozwa na Roho Mtakatifu (Matendo 20:22-23), na kujitoa kwa Mungu (Zaburi 31:5), kuwa na imani (2 Wakorintho 4:13-14), kuungama (Isaya 57:15; 66:2), au kugeuka na kumwacha Mungu (Ayubu 15:13) na kukosa uaminifu kwake (Zaburi 78:8).

**d. Kubali**

Hali inapokuwa imejulikana tathmini na maamuzi hufanyika na roho ya mwanadamu inaweza kukubaliana kwa mambo mengi na hata yaliyo maovu.

**Roho ya mwanadamu imeelezwa katika mazingira mbalimbali kama ilivyo:**

- Yaweza kukasirishwa. Waamuzi 8:3; Muhubiri 7:9; 10:4
- Yaweza kukasirishwa upesi. Mithali 14:29
- Yaweza kuumizwa. Ayubu 7:11
- Yaweza kuwa na kiburi. Zaburi 76:12; Mithali 16:18; Muhubiri 7:8
- Yaweza kuumia. Zaburi 51:17; Mithali 15:13; 17:22; 18:14; Isaya 65:14
- Yaweza kutulia. Methali 17:27
- Yaweza kulazimisha. Ayubu 32:18
- Yaweza kupinga. Zaburi 34:18; Mithali 15:4
- Yaweza kudanganya . Zaburi 32:2
- Yaweza kuchafuka. 2 Wakorintho 7:1
- Yaweza kukandamizwa. Kutoka 6:9
- Yaweza kuwa na huruma. 1 Wakorintho 5:3-5; Wakolosai 2:5
- Yaweza kupotoka. Isaya 29:24
- Yaweza kusikia uwepo wa Bwana. 2 Timotheo 4:22
- Yaweza kujiendesha. Mithali 29:11
- Yaweza kunyong'onyea. Zaburi 77:3; 143:7; Isaya 57:16; 61:3; Ezekieli 21:7
- Yaweza kuwa na uaminifu kwa mtu. Methali 11:13
- Yaweza kuwa na bidii. Matendo 18:25; Warumi 12:10-11
- Yaweza kuwa na ujinga. Ezekieli 13:3
- Yaweza kupoa. 1 Wakorintho 4:21; Wagalatia 6:1; 1 Petro 3:4
- Yaweza kupelekwa kwa Bwana. Matendo 7:59
- Yaweza kuhuzunishwa. Isaya 54:6
- Yaweza kuwa na ugumu. Kumbukumbu la Torati 2:30
- Yaweza kuwa takatifu. 1 Wakorintho 7:34
- Yaweza kuwa na heshima. 2 Wakorintho 12:18
- Yaweza kunyenyekea. Mithali 16:19; 29:23
- Yaweza kuwa na Wivu. Hesabu 5:14
- Yaweza kuishi katika mapenzi ya Mungu. 1 Petro 4:6
- Yaweza kuwa tajiri. Hesabu 14:24
- Yaweza kukomaa. Waebrania 12:23
- Yaweza kuwa hamasisha watu. Kutoka 35:21; Mithali 16:2; Ufunuo 19:10
- Yaweza kuondoshwa. John 11:33
- Yaweza kutengenezwa upya. Ezekieli 11:19; 18:31; 36:26
- Yaweza kuwiwa. 1 Samweli 1:15
- Yaweza kushtushwa. Zaburi 142:3; 143:4
- Yaweza kupanga. Matendo 19:21
- Yaweza kuwa Maskini. Mathayo 5:3
- Yaweza kuomba. 1 Wakorintho 14:14-16
- Yaweza kuhifadhiwa. Ayubu 10:12; 1 Wathesalonike 5:23
- Yaweza kunyamaza. 1 Petro 3:4
- Yaweza kupambanua. Isaya 19:3; Yeremia 51:11
- Yaweza kurejeshwa. 2 Wakorintho 7:13
- Yaweza kufurahi. Luka 1:47
- Yaweza kuumbika upya. Waefeso 4:21-24
- Yaweza kuhitaji pumziko. 2 Wakorinth 2:13
- Yaweza kuhuishwa. Mwanzo 45:27; 1 Samweli 30:12
- Yaweza kujitawala. Mithali 16:32

- Yaweza kuhuzunika. 1 Wafalme 21:5
- Yaweza kumtafuta Bwana. Isaya 26:9
- Yaweza kutumika. Warumi 1:9
- Yaweza kuvumilia. Mithali 18:14
- Yaweza kupumua. Marko 8:12
- Yaweza kustahimili. Zaburi 51:10
- Yaweza kuwa Imara. Luka 1:80
- Yaeza kuchukuliana. 1 Wakorintho 14:31-32
- Yaweza kujitoa. Waebrania 12:9
- Yaweza kuvumilia. 2 Timotheo 1:7
- Yaweza kuhangaika. Mwanzo 41:8; Job 21:4; Danieli 2:1-3; Yohana 13:18-21
- Yaweza isiendeshwe. Mithali 25:28
- Yaweza kuungana na Bwana. 1 Wakorintho 6:17
- Yaweza kuungana na waumni wengine. Wafilipi 1:27
- Yaweza kudhoofishwa. Yoshua 2:11; Waamuzi 15:19; 1 Wafalme 10:4-5
- Yaweza kufurahi. Zaburi 51:10-12
- Yaweza kuabudu. Yohana 4:23
- Yaweza kuthibitisha wokovu wetu. Warumi 8:16

**4. Moyo**

Moyo wa mwanadamu ndicho kitu kinachozungumziwa katika Biblia yote. Neno la Kiebrania "LEBH" na Kiyunani "KARDIA" yote yametumika mara 1,000. Maneno yametumika kama ogani ya mwili inayosukuma damu katika ateri na veini (2 Samweli 18:14; 2 Wafalme 9:24). Neno hili limetumika kuonyesha kitovu cha shughuli ndani ya mwanadamu.

Tunapoangalia njia mbalimbali ambazo neno "moyo" limetumika katika Biblia tunaona maana nne:

**a. Kitovu cha Maarifa**

Moyo ni kitovu cha maarifa. una uwezo wa kutathmini (Kubukumbu la Torati 8:5), kukubali (Zaburi 119:11) na kupanga (Waebrania 4:12). Moyo pia waweza kuwa ni chanzo cha mawazo na matendo maovu (Mathayo 15:19-20).

**b. Kitovu cha Hisia**

Moyo ni kitovu cha hisia. Waweza kupenda (Kumbukumbu la Torati 6:5), kutamani (Zaburi 37:4), kushangilia na kufurahi (Zaburi 104:15; Isaya 30:29; Wakolosai 3:16). Na moyo pia waweza kuhuzunika (Nehemia 2:2; Warumi 9:2), Uchungu (Zaburi 73:21) na kujikemea (Ayubu 27:6).

**c. Kitovu cha Uhuru**

Moyo ni kitovu cha uhuru. Waweza kumtafuta Mungu (Kumbukumbu la Torati 4:29), na kubadilishwa (Kutoka 14:5), au kuwa mgumu kumwendea Mungu (Kutoka 8:15; Waebrania 4:7).

**d. Kiini cha Maisha ya Kiroho**

Moyo ni kitovu cha maisha ya Kiroho. Neno la Mungu linasema, "Kwa moyo mtu huamini na kupata haki (Warumi 10:9-10)." Kwa waumini moyo ni nyumba ya Mwana (1 Petro 3:15; Waefeso 3:17) na Roho Mtakatifu (2 Wakorintho 1:22).

**5. Dhamiri**

Neno "dhamiri" linaonekana katika Agano Jipya na kazi ya dhamiri imeelezwa na neno "moyo" katika Agano la Kale (1 Samweli 24:5; Ayubu 27:6). Neno la kiyunani "SUNEIDESIS" linaamnisha kimaandiko, "kujua kwa" au "kuwa na maarifa binafsi." Inahusika na mawazo ya watu mazuri au mabaya. Dhamiri ni sehemu ya mtu inayomweka katika kufanya kile alichofundishwa kuwa ni sawa. Dhamiri haitufundishi kwamba kipi ni sawa na kipi si sawa. Mtu anaweza kufanya isivyo kwa wema tu kwa sababu hakuelezwa mapema.

Dhamiri ya mtu asiye na Kristo inaweza kuwa ni kiongozi mzuri (Yohana 8:9; Warumi 2:15) kama mtu amekwisha fundishwa kiwango cha Mungu cha mema na mabaya. Dhamiri hii inaweza kuwa ***"hatari kama chuma cha moto kiunguzacho"*** (1Timotheo 4:2) Mtu anapomkataa Mungu. Mtu anapokiuka kiwango cha Mungu dhamira yake inasemekana kuwa ni "mbaya" (Tito 1:15), lakini dhamira inaweza kusafishwa (Waebrania 10:22).

Dhamira ya mkristo kupitia njia ya huduma ya Roho Mtakatifu inatakiwa imuongoze kufanya yaliyo mema katika njia mbalimbali za mahusiano ya maisha yake. Inatakiwa imuongoze kuitii serikali yake anamoishi (Warumi 13:5), kutii mwajiri wako (1 Petro 2:19) na kuwa mwangalifu katika kukwaza dhamira ya ndugu yako dhaifu (1 Wakorintho 8:7, 10, 12).

### 6. Akili

Neno la kiyunani kwa ajili ya "akiri" ni "NOUS." Akili ni sehemu ambapo maana zote, hisia na ufahamu huja kwa ajili ya kutathminiwa na kuhitimishwa. Neno hili linahusisha kazi zote za ubongo wa mwanadamu pamoja na nafsi, kwa hiyo ni sehemu ya kukutania kwa vitu vinavyoonekana na visivyoonekana alivyoumbwa navyo mwanadamu. W.E. Vines anasema:

> "Akiri" ni "kiti cha kutahimini dhamiri ikijumuisha na mambo yote yanayoletwa pale ili yapate kueleweka, na hii ni mawazo, maamuzi na tathmini." neno la kiyunani ni "DIANOIA" maana yake ni "kuwaza kwa njia ya," na "ENNOIA" ina maanisha "wazo" au kusudi." Kwa kuwa moyo na akili vinakaribiana lakini vinatofautiana (Waebrania 8:10, 16).[106]

Kusudi la "akiri" limeelezwa katika Agano la Kale, hakuna neno moja la kiebrania. Limeelezwa kwa mfano wa moyo, nafsi na roho. Kwa hiyo tutachukua uelewa wetu wa akili kutoka katika neno la kiyunani lililotumika katika neno hili.

Waliookoka na wasiookoka wana akili (Warumi 14:5). Ni muhimu sana kwa Mungu jinsi mtu anavyofikiri na anavyotumia akili zake Mungu alizompa (Waefeso 4:17-18; Waebrania 4:12 ambapo ENNOIA imetumika na imetafasilia "kusudi"). Bwana ana akili na tunatakiwa tutafuta tuzijue (Warumi 11:34; 1 Wakorintho 2:16). Ametupa akili ili tumpende (Mathayo 22:37; Marko 12:30; Luka 10:27) na kumwelewa (Luka 24:45). Akili za wakristo zimejengwa katika kujua ukweli ulio katika Baba na Mwana (1 Yohana 5:20 ambapo DIANOIA imetafasiria 'kuelewa").

Akiri alizotupa Mungu zinaweza kutoa sababu za maana. Hii ni kweli kwamba zina uwezo wa kukokotoa hesabu na kanuni zake (Ufunuo 13:18) na kuelewa matokeo ya mawazo mazuri (Ufunuo 17:9). Kwa njia ya uwezo huu na uelewa huu tunakuwa na kiongozi mzuri katika nafsi zetu (Warumi 7:23, 25). Maendeleo haya binafsi yanaongoza katika uwezo wa kuwaongoza wengine (1 Wakorintho 14:19) na tunaimarika katika kuujenga mwili wa Kristo (1 Wakorintho 1:10). Akili lazima iwe na uaminifu wa Mungu na wengine (2 Petro 3:1). Akili imekusudiwa kutenda kazi na roho ya mwanadamu katika maeneo yote (1 Wakorintho 14:15).

Kama vile akili inavyoweza kutumiwa katika huduma kwa Mungu (Marko 12:30), yaweza kuchagua kumuasi Mungu au kuacha kuyashika maagizo ya Mungu (Warumi 1:28; 1 Timotheo 6:5; 2 Timotheo 3:8). Yaweza kuwa adui wa Mungu (Wakolosai 1:21). Na akili ina uwezo wa kuasi (Tito 1:15).

Akili za waliookoka zinaweza kuwa si za mazao (1 Wakorintho 14:14) kama zitakuwa zinawaza mambo yake binafsi (Luka 1:51; Waefeso 2:3; Wakolosai 2:18). Inaweza kuyumba kama mafundisho ya uongo yatayafanya kuwa ni ya kweli (2 Wathesalonike 2:2 ambapo NOUS imetafasiliwa kama "kutulia").

Kwa shukrani nyingi tunaona kwamba akili inaweza kuumbwa upya ili ijue mapenzi ya Mungu (Warumi 12:2), inageuka kutoka katika uovu (Waefeso 4:22-24), inaandaliwa kwa matendo (1 Petro 1:13), inaandaliwa kwa mateso yasiyostahili (1 Petro 4:1 ambapo ENNOIA imetafasiliwa kama "kusudi") na kulindwa na amani ya Mungu (Wafilipi 4:7).

### 7. Mwili wa Nyama

Neno "nyama" ni kumbukumbu ya vitu vilivyo hai na labda ni tishu zinazofunika mwili wake (Mwanzo 2:21; Kutoka 12:8; Luka 24:39) au ni vitu vyake (Mwanzo 6:17, 19; 1 Wakorintho 15:39; Waebrania 5:7). Ki Biblia neno "nyama" ni vitu vilivyohusika katika kumuumba mwanadamu apate kukamilika.

Mungu alikuja katika mwili wa nyama kwa njia ya Yesu (Yohana 1:1, 14; 1 Timotheo 3:16) kama mtu wa ukoo wa Daudi (Warumi 1:3; 9:5). Hii ina maana ya kwamba Mungu alikuja kama mwanadamu kabisa. Alikuwa na mwili wa dhambi lakini nyama zake hazikuwa na dhambi (Warumi 8:3). Alikuwa Bwana wa Daudi na pia Mwana wa Daudi kwa wakati mmoja (Mathayo 22:45). Yesu alikuja kuchukua dhambi zetu ili kwamba alete amani kwa mwanadamu na Mungu (Waefeso 2:14-15; Wakolosai 1:22-23) na akaharibu na kuvunja nguvu za shetani (Waebrania 2:14). Neno la Mungu linatuambia kwamba walimu wa uongo watainuka watakaodai kwamba Yesu hakuja katika mwili wa nyama (1 Yohana 4:2; 2 Yohana 1:7).

Agano la Kale limeeleza sababu ya Yesu kuja katika mwili. Pazia la hekalu na hema ilikuwa ni alama ya kwamba mwili wa Yesu utafungua uzima wa milele kwa mwanadamu na Mungu (Waebrania 10:19-20; Mathayo 27:51). “Manna” waliyokula wayahudi katika jangwa kwa muda wa miaka arobaini ilikuwa ni alama ya wokovu kwamba Kristo atakuja katika mwili wa nyama utakaotolewa kwa neema na kupokelewa kwa imani (Kutoka 16:31-35; Yohana 6:51-56). Zaburi ya Daudi inaeleza kwamba mwili wa Masihi hautaoza, habari inayoonesha kufufuka kutoka wafu (Zaburi 16:10; Matendo 2:31) na jibu la Mungu kwa maombi (Waebrania 5:7).

Mateso na kusudi la mwili wa Kristo ulikuwa ni kwamba afanane na wanadamu (1 Petro 4:1-2). Mwili wa mwanadamu unaonekana katika maandiko kuwa ni wadhambi na unavita na Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:16-17). Sehemu ya jukumu la Roho Mtakatifu ni kuonyesha tatizo na madhara yake (Yohana 16:8-11).

Kuna sifa chache za mwili zilizoelezwa katika neno la Mungu. Mwili bila roho huo si hai (Yohana 6:63) mwili huzaa mwili, Roho Mtakatifu huupa mwili roho ili upate kuishi (Yohana 3:6). Tunapenda, furahia, na kuisafisha miili yetu (Waefeso 5:28-29) na mwili unaweza kuwa na Hekima (1 Wakorintho 1:26-29).

Mwili ni dhaifu katika majaribu (Mathayo 26:41) na hata katika wokovu, maovu ya mwili ni maisha ya kila siku ya mwanadamu (Waefeso 2:3). Mwili huharibu njia ya mawazo ambayo akili inafikiri (Wakolosai 2:18). Maovu ya tamaa potofu ya mwili zinaonyesha udhaifu wa mwili Kukubali mamlaka ni vita kwa sababu mwili hautaki kukubali sheria ya Mungu (Warumi 7:5).

Maisha yetu katika mwili huu ndivyo yatakavyohukumiwa na wengine japo sisi hatuwezi kuwahukumu wao katika matendo yao ya mwili (Yohana 8:15). Hatupaswi kuwaheshimu wengine kwa ajiri ya matendo yao ya mwili (2 Wakorintho 5:16), na wala kuwa wajasiri kwa mambo ya mwili, uzoefu, matendo ya haki (Wafilipi 3:2-7). Muda wetu wa kuishi katika mwili unapaswa kuwa katika mapenzi ya Mungu (1 Petro 4:6).

Mwili una madhaifu mengi. Una udhaifu katika kuyakataa maovu (Warumi 6:19) na dunia huupatia mwili mambo mengi ya anasa (1 Yohana 2:16). Mwili unaojiongoza utafanya dhambi nyingi ambazo zitamgharimu mwenye dhambi baraka zake za milele (Wagalatia 5:19-21). Ubinafsi wa mwili huleta kuanguka katika mwili (Wagalatia 6:8). Mwili utaisha (1 Petro 1:24-25). Walimu wa uongo hutenda kwa kuangalia mambo ya mwili na tamaa zake (2 Petro 2:18-19).

Mwili una madhaifu katika mambo ya mapenzi. Ndoa ni kuungana kwa mwanaume na mwanamke katika mwili mmoja na kwa hiyo tamaa za mwili hufuatia, ambazo baadaye huleta uasherati, ukahaba, usagaji (Marko 10:8; Yuda 1:7). Dhambi za hiari zinapelekea katika kuharibu mwili (1 Wakorintho 5:5).

Madhaifu mengine ya mwili ni kwamba uko wazi kupokea mabadiliko yoyote yale (2 Wakorintho 1:17), ambayo yanaweza kuleta mapungufu ya msimamo katika maisha ya waumini. Kama tukuwa ni watu wa kubadili akili zetu kila wakati tutaharibikiwa na kuchanganyikiwa haraka mno.

Mwili pia una mipaka yake. Kinachofanywa katika mwili (mfano kutahiri) haimaanishi kwamba ndiyo kuwa Kiroho (Warumi 2:28). Taratibu haziwezi kumaliza madhaifu ya mwili na mipaka ya mwili (Wakolosai 2:23; 1 Petro 3:21).
Mwili hauwezi kusemwa kwamba una haki kwa kutunza sheria (Warumi 3:19-20) na mwili hauwezi kutenda yaliyo mema (Warumi 7:18). Wala baraka za Mungu zilizopangwa kwa mwili na damu (1 Wakorintho 15:50). Mwili unahitaji nuru ya Mungu (Mathayo 16:17).

Kuna vita ya mwili katika maisha ya waumini na mwili. Mtu apomwamini Yesu anatambua kwamba Yesu alikufa kwa ajiri ya dhambi za mwili wangu (Wagalatia 5:24). Kukubali hii habari kunahitaji ukomavu wa kiroho katika waumini. Muumini asipogundua hii anaweza kujua sasa niko katika mikono ya Mungu (Yohana 10:27-30) na kwamba amewekwa huru na Kristo (Wagalatia 5:1), hivyo anaanza kukosea kwa kufuatisha tamaa za mwili. Hivyo elewa kwamba usalama na uhuru huu haukuwekwa kwa ajiri ya mwili (Galatians 5:13). Hii ni sehemu ya vita bado.

Vita nyingine ya kufahamu ni kwamba mwili una uhuru (Yohana 1:12-13) na tabia za mwili kutenda dhambi hupingana sana na akili (Warumi 7:25) na Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:16). Waumini wanapaswa kuamua kutenda mambo ya mwili au mambo ya Roho Mtakatifu (Warumi 8:3-13). Kwa nguvu ya Roho Mtakatifu tu tunaweza kuzishinda tamaa za mwili (Wagalatia 3:3; 5:16). Elewa vita ya kweli tunayopambana nayo haitoki katika miili ya watu wengine (2 Wakorintho 10:2-3), lakini ni shetani na njama zake (Waefeso 6:12).

Sehemu ya safari yetu ya kiroho ni kutafuta kusafishwa na udhalimu wote wa mambo ya mwili na tuwe watakatifu (2 Wakorintho 7:1). Tunahitaji kutafuta kumweka Yesu katika maisha yetu na tamaa zetu za mwili zitakwisha (Warumi 13:14), ili kwamba Kristo apate kuonekana katika miiili yetu (2 wakorintho 4:11). Hii inaweza kufanyika kwa njia ya maisha ya Imani katika Yesu Kristo (Wagalatia 2:20), ili miili yetu isitahili katika mwili wa Kristo (Wakolosai 1:24).

Hebu tuelewe kwamba Mungu anatupenda na anaweza hata kutupa "enzi katika mwili" ili kwamba tusiharibike (2 Korintho 12:7).

8. **Asili ya Dhambi**
Ukweli wa kwamba dhambi ya Adamu ilimfikia kila mtu imeelezwa na neno "Dhambi ya Asili". Hii ina maanisha kwamba kila mtu (isipokuwa Yesu ambaye hakuwa na baba wa dunia hii) ana dhambi ya asili ya adamu na atahukumiwa (Warumi 5:12-14, 18-19).

"Dhambi ya Asili" ni sehemu ya mwili na inashawishi sana mtu kutenda dhambi katika maisha ya mtu. Tutaisoma dhambi hii ya asili katika sehemu inayofuatia" Mpango wa Mungu"

9. **Mapenzi**
Kuna maneno mawili ya kiyunani yanayoonyesha mapenzi ya mwanadamu. Neno la kwanza, "THELEMA" linaonesha tamaa. Neno la pili, "BOULEMA" linaonyesha mpango. Yote yametumika katika kuonyesha shauku ya Mungu lakini kwa sababu mwanadamu ameumbwa kwa sura ya Mungu (inaonyesha kwamba mwanadamu ana mapenzi) yalitumika kueleza shauku ya mwanadamu au mpango.

Mapenzi ya mwanadamu yana nguvu. kama vile mwanadamu anavyoweza kuchagua Mungu hivyo hivyo anaweza kumkataa (Yoshua 24:15) na ***"pamoja na tamaa ya mwili na akiri"*** (Waefeso 2:3). Mapenzi ya mwanaamu hayana nguvu ya kushinda dhambi ya asili ndani (Warumi 7:15-21). Roho Mtakatifu ndiye atupaye nguvu katika Kristo ya ***"kufanya mambo yote"*** (Wafilipi 4:13).

Haijalishi mtu anaweza kuwa na nguvu gani hiyo haiwezi kumsaidia (Yohana 1:12-13). Ni lazima aikubali zawadi ya Yesu kwa kuliamini jina lake (Yohana 1:12-13; Matendo 4:12). Mtu anapomwamini mwana wa Mungu mtu yule anakuwa na uzima wa milele ambao kamwe haupotei (Yohana 6:39-40).

Mungu anataka mapenzi ya mwanadamu yawe kama yake. Yesu Kristo alitufundisha na aliishi katika ukweli huu (Yohana 5:30; 6:38,39). Sababu ya Daudi kuitwa "Mtu wa moyo wa Mungu" (Matendo13:22) ni kwa sababu alitamani kutenda mapenzi ya Mungu japo wakati mwingine alishindwa.

Shauku ya kutenda mapenzi ya Mungu ni muhimu sana kama tutaelewa (Yohana 7:17). Mungu hataki tusindane bali tuwe na mabadiliko katika maisha yetu. Mtu anaye soma neno la Mungu ili alifahamu na si kuilitenda ni lazima tu ataharibikiwa katika maisha yake.

Katika neno la Mungu tunaona kwamba mwanadamu anaweza kufanya mapenzi yake ili ajilinde (Mathayo 1:19), lakini ni lazima tu atakosea (Mathayo 5:40) atajitahidi kuwaazima na wengine (Mathayo 5:42). Tunaona kwamba mwanadamu anaweza kutamani kumfuata Kristo (Mathayo 16:24-25), awe mkuu (Mathayo 20:26-27), kuishi kama mungu katika Kristo (2 Timotheo 3:12) na kuwatendea wengine vizuri (Mathayo 7:12).

Kama "mapenzi" yatafanyika si kwa tamaa "yatakuwa" ni mpango." Neno la Kiyunani "BOULEMA" linaanisha tamaa imekuwa ni mpango. Neno hii limetafasiriwa katika namna mbalimbali lakini kusudi ni mpango wa kuwa na shauku. Mungu ana mapenzi yaliyopangwa (Warumi 9:19). Mwana naye ana majukumu katika mpango huo (Mathayo 11:27).

Mpango unaweza kuendelezwa katika shauku ili kuwalinda wengine (Matendo 27:43), kuwaumiza (Yohana 11:53; 12:10; Matendo 5:33), au kumwokoa (Matendo 27:39). Kunaweza kukawa na mipango ya safari (Matendo 15:37), kuelewa ukweli (Matendo 23:8), kufanya vita (Luka 14:31) na hata kutenda dhambi (1 Petro 4:3). Mipango inaweza kutoka kwa Mungu au katika miili yetu (2 Wakorintho 1:17).

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 6, Sehemu ya 3

1. **Mwanzo 1:26. Mwanadam ameumbwa kwa sura ya nani?**

2. **Soma Mwanzo 2:7. Mwanadamu alikuwa nini kupitia pumzi ya Mungu?**

3. **Soma Mwanzo 2:18. Kwa nini mwanamke aliumbwa?**

4. **Soma 2 Petro 2:12 na Yuda 1:10. Mwanadamu anaweza kufanya nini tofauti na mnyama ?**

5. **Soma Mwanzo 2:16-17. Adamu alikatazwa nini?**

6. **Soma Mwanzo 2:17. Hkumu ilikuwa ni nini?**

7. **Soma Mwanzo 3:8-19. Maisha ya mwanamke na mwanaume yalikuwaje baada ya kuasi Amri ya Mungu?**

8. **Soma sura zifuatazo na utoe vitu muhimu vya asili ya mwanadamu.**
   a. Mwanzo 2:7
   b. Yakobo 2:26
   c. Warumi 10:9-10
   d. 1 Timotheo 4:2
   e. Warumi 12:2
   f. Mwanzo 2:21
   g. Warumi 5:12–14
   h. Yohana 1:12–13

# Sehemu ya 4
# Migogoro ya Malaika

Ukweli wa kwamba kulikuwa na vita kati ya Mungu umezungumziwa sana katika somo hili. Vita hii inajulikana kama “Migogoro ya Malaika.” Maelezo ya mgogoro huu ni makubwa na yako mbele ya upeo wa somo hili. Lakini mambo muhimu ni ya lazima kwa sababu yanasaidia kujibu swali la muda mrefu la “Kwa nini manadamu yuko hapa?”

Kwa maelezo tu machache kabla ya uumbaji Mungu aliamua kuumba aina nyingine ya uumbaji. Uumbaji huu unajulikana kama “malaika” na kiongozi mkuu wa malaika alikuwa ni Lusifa ambaye alijaribu kufanya mkakati wa kuchukua nafasi ya Mungu (Isaya 14:12-14). Lusifa alitenda dhambi (Ezekieli 28:11-19) na akajulikana kwa jina la Ibilisi au Shetani (Ufunuo 12:9). Shetani alihukumiwa kwenda katika ziwa la Moto ambalo limeandaliwa kwa ajiri yake na malaika zake wanaomfuata (Mathayo 25:41).

Shetani alikana maamuzi ya Mungu kwa sababu sentensi haijatimia. Itatimia baada ya miaka 1,000 ya utawala wa Kristo (Ufunuo 20:14). Mwanadamu yuko katikati na hivyo anayo nafasi ya kuamua katika mgogoro huu kumfuata Mungu au Shetani.

Mtume Paulo ameeleza vizuri kwamba mgogoro huu unaharibu maisha ya Muumini. Alisema katika Waefeso 6:12, ***“kwa maana kushindana kwetu si kwa damu na nyama bali ni juu ya falme na mamlaka juu ya wakuu wa giza hili juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa Roho.”*** Vita ya waumini ni dhidi ya Shetani na malaika zake. Ili kushiriki katika vita hivi tunapaswa ***“tuvae silaha kamili za Mungu ili tuweze kushindana katika siku hizi za uovu, kuyatimiza yote kusimama.”*** (Waefeso 6:13).

Maelezo ya vita na jukumu letu bado hayajajulikana lakini siku moja yataondolewa kwetu (1 Wakorintho 13:12). Kwa sasa tunayoyafahamu yanatosha. tunapaswa kutembea kwa Imani (Waebrania 11:6) na tumpende Mungu na kila mtu (Marko 12:29-31).

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 6, Sehemu ya 4

1. **Soma Isaya 14:12-14.  Nini ilikuwa ni dhambi ya asili ya Shetani?**

2. **Soma Ezekieli 28:11-19.  Nini ilikuwa ni nafasi ya shetani hapo mwanzo kabisa?**

3. **Soma Mathayo 25:41.  Ziwa la moto limeumbwa kwa makusdi gani?**

4. **Soma Ufunuo 20:14.  Shetani na malaika zake watatupwa katika ziwa la moto kipindi gani?**

5. **Soma Yohana 16:11.  Nini kimekwisha tokea tayari kwa shetani?**

6. **Kwa kuwa Shetani amekwisha hukumiwa na mashtaka yake bado hayajatekelezwa je tunapaswa kufanya nini kama hatima?**

7. **Kwa kuwa Shetani alikuwa amekwisha ameangushwa baada ya kuwakosesha Adamu na Hawa je tunapaswa kfanya nini kuhusu kuhusu anguko lake?**

8. **Kwa kuwa mwanadamu yuko kati ya hukumu ya shetani na mashtaka yake sasa tunapaswa kufanya nini katika kuishi kwetu?**

9. **Waefeso 6:10-18.  Wakristo wanapaswa kfanya nini katika kupingana na maazimio ya Shetani?**

## Sura ya 7

# Mafundisho
# ya
# Mipango ya Mungu

# Sehemu ya 1
# Ufunuo: Biblia (Bibliology)

Biblia ni sehemu ya ufunuo wa Mungu mwenyewe uliyoandikwa kwa ajili ya mwanadamu. Na pia Mungu amejifunua katika njia nyingi katika mambo aliyoyafanya. (Warumi 1:20). Neno "ufunuo" kimaandiko lina maana ya "kufunua kitu kilichokuwa kimefunikwa au kufichwa na kukiweka wazi ili kila mtu apate kukiona na kukifahamu." Mungu kapenda kwamba yeye apate kufahamika na kuonekana kwa njia ya neno lake lililoandikwa. Mungu alijidhihirisha katika njia mbalimbali kupitia historia na akawavuvia watu wapate kuandika ufunuo wake. Na hii inajulikana kama "uvuvio"

Mungu ndiye aliyekuwa akiwaelekeza na kuwaongoza kuandika ufunuo na uvuvio huu, uliandikwa bila makosa yoyote katika kitabu cha kwanza. Kwa hiyo kama neno la Mungu Biblia inayo mamlaka yake na kwa jinsi hiyo inatuelekeza na kutuongoza katika maisha na mambo yetu ya kiroho.

Tangu 1450-400 K.K. Mungu aliwavuvia waandishi mbalimbali kuandika vitabu 39 tofauti tofauti ambavyo viliitwa Agano la Kale. Na 46-96 B.K., aliwavuvia watu wengine zaidi kuandika vitabu 27 ambavyo viliitwa Agano Jipya. Muungano wa maandiko huu huitwa maandiko matakatrifu. Ni lazima ieleweke kwamba hasa kwa wanafunzi wapya wa Biblia, Mungu alijifunua kwa waandishi hawa tofauti tofauti na kuwavuvia ili kwamba yeye mwenyewe apate kujifunua kwa mwanadamu ili mwanadamu apate kuwa na mamlaka ya Mungu yaliyoandikwa na akavikusanya vitabu hivi pamoja ambavyo vilifanyika Biblia kama yeye alivyokuwa amekusudua.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 7, Sehemu ya 1

1. **Soma Warumi 1:20. Ni nini kinachoonekana kupitia uumbaji wa Mungu?**
2. **Eleza "Ufunuo."**
3. **Eleza "Uvuvio."**
4. **Pamoja na kuwa Neno la Mungu, Biblia ni nini?**
5. **Nini mwongozo wetu katika mambo ya kiroho?**
6. **Munganiko wa Agano la Kale na Jipya naitwaje?**
7. **Soma yohana 17:17. Neno la Mungu ni nini ?**
8. **Soma zaburi 119 na yatafakali maelezo khusu Neno la Mungu.**

# Sehemu ya 2
# Tatizo: Dhambi (Harmartiology)

**A. Utangulizi**

Kwa ujumla dhambi ina maana ya uvunjaji wa yaliyowekwa ambayo yanafaa. Neno la Mungu linafafanua vizuri kwamba kunatakiwa kuwe na sheria ya juu inayofaa ili kwamba dhambi ipate kuonekana na bila sheria au jambo la muhimu dhambi isingelikuwepo (Warumi 4:15; 5:13). Maneno mazuri yanayoeleza dhambi kwa kiebrania na hata kiyunani ni (CHATA' and HAMARTIA) ikiwa na maana ya kwamba mmoja anakwenda tofauti na kuikosa ile alama. Hii ni sawa na kusema kwamba mtu anapiga mshale kwenye ile alama aliyopangiwa kupiga na halafu anapiga sehemu nyingine ambayo hakuelezwa kupiga; na ikiwa mtu atakuwa amekosea kupiga pale panapotakiwa hata kama ni kigogo tu huyo atakuwa amekosa tu.

**B. Kuna Aina Tatu Tofauti za Dhambi Zilizoainishwa katika Maandiko ya Neno la Mungu**

**1. Dhambi Iliyowekwa**

Katika kuzaliwa kila mwanadamu anakuwa na dhambi iliyowekewa toka kwa Adamu. Neno "kuwekwa" lina maana ya kwamba iliingizwa hata katika watoto wa Adamu (sisi sote) kwa sababu ya dhambi yake ya asili. Warumi 5:12 inasema , ***"kwa hiyo kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni na kwa dhambi hiyo mauti na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi."*** na hata katika Warumi 5:18-19, inasema, ***"tena kama kwa kosa moja*** (hii inamwonesha Adamu alivyotenda kosa) ***watu wote walihukumiwa adhabu kadhalika kwa tendo moja la haki watu walihesabiwa haki yenye uzima, kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi kadhalika kwa kutii kwake mtu mmoja watu wengi wameingizwa katika katika hali ya wenye haki."*** Dhambi ya Adamu na hata matokeo ya hukumu ya dhambi yamerithishwa kwa kila mwanadamu tangu kwa Adamu.

Ni vizuri kuelewa kwamba dhambi hutoka kwa baba wa dunia. Yesu hakuwa na Baba wa duniani ila wa mbinguni hivyo hakurithi dhambi ya Adamu.

**2. Dhambi ya Kurithi**

Matokeo ya "Dhambi ya Kuwekwa" hii ni kwamba kila mwanadamu anakuwa na dhambi ya kurithi ambayo ni ya asili na inamfanya mwanadamu atende dhambi katika maisha yake. Na hii mara nyingi huitwa "Dhambi ya Asili" au "Mtu wa Kale." Japo matokeo ya dhambi ya Adamu ni hukumu lakini hii imekwisha kuondolewa (Warumi 6:6; 8:1), dhambi ya asili hubaki kwa mtu hadi anapokufa kifo cha mwili.

Mtume Paulo anaandika juu ya vita yake mwenyewe na dhambi katika Warumi 7:16-18. anaandika, ***"Lakini kama nikilitenda lile nisilolipenda naikiri ile sheria kuwa ni njema. Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu kwa maana najua kuwa ndani yangu yaani ndani ya mwili wangu halikai neno jema kwa kuwa kutaka nataka bali kutenda lililojema sipati."*** Kulingana na sura hii tunaweza kuhitimisha kwamba japo Paulo alipoteza vita yake na Dhambi ya Asili lakini anatuonyesha kwamba vita hii ilikuwa pia ni ya Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:16-17) na hivyo waumuni wanahitaji ***"kuweka kando tamaa zao"*** (Waefeso 4:20-22).

Elewa kwamba katika haya Yesu hana "dhambi ya kurithi" wala ya "kuwekewa."

**3. Dhambi Binafsi**

Dhambi binafsi ni yale matendo yanayovunja na kuharibu kiwango cha matendo ya Mungu. Japo hatuko katika mila na desturi za Sheria ya Musa lakini maadili na kanuni zilizozungumziwa humo bado zinafanya kazi. Paulo kaandika katika 1 Timotheo 1:8-10, ***"lakini twajua ya kuwa sheria ni njema, kama mtu akiitumia kwa njia iliyo halali; akilifahamu neno hili ya kuwa sheria haimhusu mtu wa haki bali waasi na wasio kuwa wataratibu, na makafiri na wenye dhamb,i na wanajisi, wasiomcha Mungu, na wapigao baba zao, na wapigao mama zao, na wauaji, na wazinifu na wafiraji, na waibao watu, na waongo, nao waapao kwa uongo; na likiwapo neno lolote linginelo lisilopatana na mafundisho yenye uzima; kama vile ilivyonenwa katika Habari Njema ya utukufu wa Mungu ahimidiwaye niliyowekewa amana."*** Dhambi zingine zinaitwa "matendo ya mwili" na yametajwa katika Wagalatia 5:19-21 Inasema, ***"Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi na mambo yanayofanana na hayo; katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu."***

**C. Kuna Makundi Matatu Tofauti ya Dhambi Binafsi**

**1. Dhambi ya Akili**

Kundi hili la dhambi linatokana na jinsi mtu anavyofikiri katika akili zake. Yesu anatueleza katika kitabu cha Mathayo 5:28 kwamba ***"kila mtu amtazamae mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini nae."*** Katika akili zetu na mawazo yetu dhambi yaweza kutokea. Ni dhambi kwa sababu si mawazo matakatifu na tumeamriwa kuwa watakatifu kama Mungu alivyomtakatifu (1 Petro 1:16). Amri ya 10 katika Sheria za Musa inakataa "tusitamani"(kutoka 20:17).

Dhambi ya akili ni kama dhambi zingine binafsi ambazo huvunja sheria ya upendo. Mfano wa dhambi ya akili inaonekana katika Yakobo 2:8-9 Inasema, ***"Lakini mkiitimiza ile sheria ya kifalme kama ilivyoandikwa mpende jirani yako kama nafsi yako mwatenda vema bali mkiwapendelea watu mwafanya dhambi na kuhukumiwa na sheria kuwa wakosaji."*** Mara nyingi dhambi za akili au mawazo hudhihirika katika matendo ambayo huonekana wazi baadaye.

**2. Dhambi ya Ulimi**

Kundi la pili la dhambi binafsi linahusiana na yale mtu anayotamka au kusema. Kitabu cha Yakobo kina mistari mirefu mingi kuhusiana na dhambi chafu ya ulimi (3:1-10). Dhambi ya ulimi imeonyeshwa katika Sheria ya 9 inayosema ***"Usimshuhudie jirani yako uongo"*** (Kutoka 20:16). Shetani (ina maana ya "adui ") ambaye ni mwovu (ina maana "msingiziaji") ni mkuu wa kudhuru na kuwaumiza wengine kwa njia ya maneno. Sifa ya dhambi ya ulimi ni kwamba huwa hauneni mazuri juu ya watu wengine na hata Mungu pia.

**3. Dhambi ya Matendo**

Ya tatu na mwisho ni dhambi inayohusiana na yale ambayo mtu binafsi hutenda. Haya ni matendo ambayo mtu anatenda kila wakati. Mifano mizuri ya dhambi ya kundi hili imeonyeshwa vizuri katika Sheria au Amri ya 6, 7 na 8:

***1) "Usiuwe,"***
***2) "Usizini,"***
***3)*** **Na *"Usiibe."***

Yakobo 4:17 inasema, ***"basi yeye ajuaye kutenda mema wala hayatendi kwake huyo ni dhambi."***

Ni vizuri kuelewa pia kwamba dhambi yaweza kuhusisha makundi yote haya matatu kwa pamoja. Yesu pia alisema uuaji waweza kufanyika katika akili na mawazo na hata katika ulimi halafu ukakamilishwa kwa tendo la kuuwa kabisa. (Mathayo 5:21-23).

Yesu Kristo hakutenda aina yoyote ile ya dhambi. Iwe ni katika kufikiri, kusema wala kutenda kama mwanadamu mwingine (1 Petro 2:22).

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 7, Sehemu ya 2

1. **Soma Warumi 4:15 na 5:13. Kunatakiwa kuwe na nini ili dhambi itokee?**

2. **Soma Warumi 5:12 na 5:18-19. Nini matokeo ya dhambi ya Asili ya Adamu na kwa nini?**

3. **Soma Warumi 7:16-18. Dhmabi ya asili inakaa wapi?**

4. **Soma Wagalatia 5:19-21. Dhambi binafsi zinaitwaje?**

5. **Soma Mathayo 5:28. Ni dhambi gani inayoelezwa hapa?**

6. **Soma Yakobo 3:1-10. Ni aina gani ya dhambi sura hii inaelezea?**

7. **Soma Kutoka 20:13-15. Aina gani ya dhambi mistari hii inazungumzia?**

8. **Kunaaina mbalimbali ya dhambi zimetolewa katika Wagalatia 5:19-21. Zieleze kama niza kukusudia, matendo au dhahiri. Zingine zaweza kuwa zaidi. ] Maelezo ya ziada yametolewaili kuweza kuzioanisha.**
   a. Uzinzi
   b. Uchafu
   c. Mapenzi ya kinyume na maumbile
   d. Sanamu
   e. Uchawi

f. Uadui
g. Mabishano
h. Wivu
i. Kujawa na Hasira
j. Migogoro
k. Kutenga
l. Kutengana kwa sbabu ya mapokeo
m. Upotoshaji
n. Ulevi
o. Sherehe za kilevi

# Sehemu ya 3
# Ufumbuzi / Njia: Wokovu (Soteriology)

**A. Utangulizi**

Kwa kuwa dhambi ni tatizo la kila mwanadamu isipokuwa Yesu Kristo ni lazima mwanadamu aokolewe kutoka katika athali hii. Mungu katika mamlaka zake na kwa ujuzi wake wa kila jambo aliweka mpango ambao utamfanya mwanadamu apate kuokolewa. Mpango ulikuwa na gharama ya kutoa maisha ya Yesu Krito. Yesu Kristo ndiye pekee aliyeweza kukamilisha na kutosheleza haki ya Mungu kwa kulipa gharama ambazo hakuna mwanadamu yeyote angeliweza kuthubutu kulipa. Ilikuwa ni gharama ya ya dhambi. Mwanadamu amepewa neema hii ya wokovu wa Yesu Kristo kwa njia ya imani (2 Wakorintho 8:9).

**B. Injili**

Neno Injili lina maana ya "habari njema." Kwa urahisi tunasema habari njema kuwa ni wokovu kwa njia ya Imani katika Kristo Yesu peke yake. Katika Matendo 16:30, Mlinzi alimuuliza Petro "Nifanye nini ili nipate kuokoka?" Paulo alimjibu, "Mwamini Yesu nawe utaokoka" (16:31). Imani katika Yesu Kristo inaelezeka kuwa ndicho kitu pekee kinachoweza kufanya mtu akaokolewa (Yohana 3:16, 18, 36). Hakuna jina jingine alilopewa mwanadamu limpasalo kumuokoa (Matendo 4:12).

Mungu anataka kila mtu aokolewe (1 Timotheo 2:4; 2 Peter 3:9) na hivyo Yesu Kristo amelipa deni la dhambi la ulimwengu wote (1 Yohana 2:2) ili kwamba awalete watu wote kwake (Yohana 12:32). Roho Mtakatifu huuonesha ulimwengu dhambi yake na pia kuupa njia ya kumwendea Yesu Kristo kama njia ya kumaliza tatizo la dhambi (Yohana 16:7-15).

Na kweli kabisa mwanadamu anatakiwa amkubali Yesu akielewa kwamba ni Mungu aliyefanyika mwanadamu (Yohana 1:1, 14), alikufa ili alipe gharama ya dhambi, akazikwa akionyesha kabisa kwamba alikufa kabisa na kwa ujasiri alifufuka siku ya tatu kutoka wafu (1 Wakorintho 15:3-5).

**C. Neema**

Neema ina maana ya kwamba sisi tulipewa kitu ambacho hatukustahili tukipate. Tunapopata kitu kuokana na kazi fulani inaonekna kama mshahara au posho kwa sababu ya kazi tuliyofanya. Neema tuliyopata katika wokovu ni zawadi ya Mungu. Maandiko yanasema ***"Tumeokolewa kwa neema kwa njia ya imani ambayo haikutokna na juhudi zetu mtu asije akajisifu"*** (Waefeso 2:8-9). Neema ya Mungu imetoa zawadi ya wokovu ambayo tunaipokea kwa njia ya imani. Injili imeelezwa kama Neema ya Mungu (Matendo 20:24). Yesu Kristo alikuwa ni neema kwa Mwanadamu. (Yohana 1:14-17).

**D. Imani**

Imani ni kuamini. Kusitahili hakuko katika mtu aliye na imani bali ni katika kitu cha imani. Wokovu ni tendo la kumkubali Yesu Kristo. Imani si kazi.

Wanadamu, tunatamani kupata wokovu, na wengi wamekosea kwani wanafikiri wokovu hupatikana kwa sababu ya kufanya kazi na matendo mazuri, wokovu hupatikana kwa kuikubali zawadi ya Yesu kwa njia ya neema ya Mungu. Ni kweli kwamba ***"Mungu katuumba ili tuitende kazi iliyo njema"*** (Waefeso 2:10) lakini tunapaswa kutenda yaliyo mema kama matokeo ya wokovu wetu.

Wakati mmoja kipindi cha huduma ya Yesu alikuwa akifundisha juu ya uzima wa milele kama zawadi ambayo angeitoa (Yohana 6:26-27). Watu walimuuliza Yesu ***"Tufanyeje ili tupate kuzitenda kazi za Mungu?"*** (Yohana 6:28). Alijibu akisema, ***"Hii ndiyo kazi ya Mugu,mmwamini yeye aliyetumwa na yeye"*** (Yohana 6:29). Alikuwa akisema kama unaamini unapaswa kufanya kazi ili upate kuokolewa na hii ni wokovu wa kazi. Ikiwa imani yetu ingelikuwa ni "kazi" (japo si hivyo) basi "kazi" hiyo ingelikuwa imewezeshwa na Wokovu wa kazi ya Mungu na hiyo isingelikuwa ni ngumu sana.

Mungu kampa kila mwanadamu uwezo wa kuwa na Imani,na uwezo wa kuamua. Na hii ndiyo sehemu inayosema na kumaanisha kwamba ***"mwanadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu"*** (Mwanzo 1:26-27). Ingawa mwanadamu amepewa uwezo kamili wa kuchagua haina maana kwamba ataamua vizuri kila wakati. Uamuzi wa kuchagua unategemea na mtu mwenyewe . Kwa kuwa kila mwanadamu anao uhuru wa kuchagua na kuamua kwa wale wote waliokana kumchagua Kristo hao tayari wamepingana naye (Mathayo 12:30; Yohana 3:18). Kumchagua Kristo kunakupa wokovu na uzima wa milele mbinguni, bali ukikataa kumchagua kunaleta hukumu na kwenda jehanamu katika ziwa la moto milele (Yohana 3:36).

**E. Kutubu**

Kutubu kunamaana ya “kubadili akili zako na kugeuka.” Ina maana kwamba imani moja inabadilishwa na kuingia imani nyingine. Yesu anatamani kila mtu asiye amini abadili akili zake na kumwendea Yesu peke yake ili wasije kuangamia (2 Petro 3:9; Matendo 20:21). Hii ni pamoja na kutambua kwamba kama mwanadamu hawezi kulipa gharama za dhambi zake bali Yesu Kristo amekwisha lipa gharama hizo kwa ajiri yao (Luka 24:45-47). Hii “kubadili akili” ni msingi wa maisha mapya ya Mkristo. (Waebrania 6:1).

Waumini pia wanapaswa kubadili akili zao pale wanapoona kwamba wameamini au kufanya kitu ambacho si kweli katika maisha yao ya kila siku (2 Timotheo 2:24-25) au wamefanya kitu ambacho hawakutambua kama ni dhambi lakini ni dhambi (2 Wakorintho 7:9-10). Dhambi hizi (na hata zingine) ni lazima ziungamwe mbele za Mungu (1 Yohana 1:9).

**F. Uthibitisho**

Uthibitisho una maana ya kueleza haki ya mtu fulani. Mwanadamu ni mwenye dhambi hana haki au sababu ya kushirikiana na Mungu Mtakatifu (Isaya 64:6; Warumi 3:20). Na hii inashida sana kwa mwanadamu: Je vipi mtu anaweza kuwa na haki ya kuingia katika ufalme wa Mungu? Jibu liko katika mafundisho yake.

Sura muhimu iko katika Warumi 3:19-4:5, inasema: (1) hakuna mtu awezaye kuthibitishwa kwa Sheria (3:20 linganisha Wagalatia 2:16; 3:24), (2) uthibitisho ni zawadi iliyotolewa kwa sababu Yesu alilipa deni la dhambi (alitukomboa) akathibitisha (kustahilisha) hitaji la haki ya Mungu na uhuru (3:24), na (3) uthibitisho ni katika Yesu (3:26). Mwanadamu aliye na imani katika Yesu Kristo kaishapewa haki.

Uthibitisho huu ni neema kwa njia ya imani katika Yesu Kristo. Neema hii hutupatia amani na Mungu wetu (Warumi 5:1) na umetutenga na ghadhabu ya Mungu (Warumi 5:9). Inatuweka huru katika hukumu tuliyokuwa tukistahili kwa sababu ya dhambi yetu ya asili (Warumi 6:7) na inatupa kurithi pamoja na Kristo (Tito 3:4-7).

**G. Utakaso**

Utakaso una maana ya kwamba tumekwisha hesabiwa kama watakatifu. Utakatifu hupimwa kwa haki na kweli ya Mungu. Mtu anapothiibitishwa kwa neema kwa njia ya imani katika Yesu Kristo mtu huyo pia anakuwa amekwisha takaswa na Kristo (Matendo 26:18; Waebrania 2:11), kwa kujitoa kwake wakati wote (Waebrania 10:10-14; 13:12) pia na Roho Mtakatifu (2 Wathesalonike 2:13; 1 Petro 1:2). Tunapokuwa waumini tunashiriki utakaso huu na kila mtu (Waebrania 12:14).

Utakaso huu hauna maana ya kwamba maisha ya mwanadamu au mumini hayatakuwa na dhambi. Kanisa la Korintho lilikosea katika jinsi ya kuishi nab ado liliitwa kuwa kuwa limetakaswa na ni lawatakatifu (1 Wakorintho 1:2, 30; 6:9-12).

Wakristo wanapaswa kumweka Yesu kama kiwango cha utakatifu wao katika maisha yao (1 Wathesalonike 4:3, 4, 7; Waefeso 5:25-26; 1 Petro 3:15). Utakaso hutokea mara wakati mtu anapompokea Yesu. (Warumi 6:19; 1 Wathesalonike 5:23). Hii hukamilishwa na kuamini neno la Mungu (Yohana 17:17-19) na baadaye kupelekwa mbele ya mkuu kwa utakaso ili ifanye kazi vizuri katika Maisha yetu na kazi zetu (2 Timotheo 2:21). Matoleo ya muumini huhalalishwa na kutakaswa mbele za Yesu na Roho Mtakatifu (Warumi 15:15-16). Wale wote wasio na Neema hii Bwana atawaonya (Waebrania 10:29).

**H. Msamaha**

Msamaha maana yake ni “kutupilia mbali.” Ni neno la Kiyunani “APHIEMI” lenye tafasiri ya “acha” (Mathayo 4:20, 22; 5:24). Kama vile mtu mmoja anavyoacha sehemu moja nyuma na kuingia sehemu nyingine hii ni kwamba dhambi zimeachwa nyuma na mwanadamu ameingia sehemu nyingine.si mzigo tena unaoendelea kubebwa (Waebrania 12:2). Katika msalaba dhambi na mambo yake yote “Ilifunikwa” hii inamaana kwamba ilibaki pale lakini hukumu ya dhambi inasubiliwa (Zaburi 32:1 linganisha Warumi 4:7). Neno Toba lina maana ya “funika.” Kwa dhabihu ya Bwana pale msalabani dhambi “ilitupiliwa mbali” (Mathayo 26:27-28). Msamaha ulikuwa ni sehemu muhimu katika ujumbe wa Yohana Mbatizaji (Luka 3:3-4) na Yesu Kristo (Luka 4:18-19; Matendo 5:31). Msamaha waweza kutoka katika kitu tulichokuwa tukidaiwa (Mathayo 6:12-15), dhambi (Mathayo 9:2-6), au fikira za moyo (Matendo 8:22).

Msamaha wa dhambi ni muhimu sana katika wokovu (Luka 1:77). Sadaka ya Kristo, ndiyo iliyolipa deni la dhambi na hii ndiyo ilikuwa ni msamaha wake (Waefeso 1:7; Wakolosai 1:13-14; Waebrania 9:22). Mtu anapompokea Yesu anasamehewa dhambi zake (Matendo 10:43; 26:18). Kwa kuwa Yesu ameisha lipa deni la dhambi hakuna tena dhabihu itakayotolewa ili kufunika dhambi (Waebrania 10:17-18).

Kwa kuwa msamaha ni tendo la neema hebu sasa na tuweke kando dhambi zetu, na Mungu atatenda mambo makubwa hata tusiyoyategemea. Kama tukiweka mambo yetu kando kama vazi ni rahisi kurudia

kuvaa. lakini sote twajua ya kwamba Mungu hakuweka kando dhambi zetu bali alizifuta kabisa na tunaambiwa kwamba , ***"na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu aliwafanya hai pamoja naye akiisha kutusamehe makosa yote akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake iliyokuwa na uadui kwetu akiondoa isiwepo tena akiigongomea msalabani"*** (Wakolosai 2:13-14). Ukweli ni kwamba dhambi zetu hazikuachwa tu bali zilifutwa kabisa ili kwamba sisi tupate kufurahia katika Bwana (Matendo 3:19).

Wakristo ni lazima wawe kama Mungu (Waefeso 5:1) na Kristo (1 Wakorintho 11:1), iliyofundisho kwa hitaji la Roho Mtakatifu wa msamaha (Mathayo 18:21-22). Wakristo ni vema wakawa ni watu wa msamaha kwa kuwa msamaha wa dhambi ni sehemu ya utume mkuu (Luka 24:46-47; Matendo 10:43; 13:38). Ni lazima tuwe tayari kuishi sawa na yale tunayoyafundisha.

Waumini wanapokuwa wamekosa au kufanya dhambi wanaziungama mbele za Mungu ili awasamehe na kuwatakasa (1 Yohana 1:6-10) ili kwamba Mkristo apate kukuwa katika Maisha yake ya Ukristo. Yesu alilipa dhambi zote pale msalabani kwa hiyo tumekwisha kusamehewa. Mkristo anapotubu dhambi atatambua kwamba deni ya dhambi imekwisha lipwa.

**I. Dhambi Isiyo Samehewa (Kumkufuru Roho Mtakatifu)**

Dhambi inayoendelea na haitasamehewa: ni kumkufuru Roho Mtakatifu (Mathayo 12:31-32). Kumkufuru Mungu ni kusema kuwa Mungu ni kitu fulani chochote na wala Mungu hayupo. Mtu anapokuwa ameonja uwepo wa Mungu na anasema kuwa si kweli ni uongo huyo anakufuru. Roho Mtakatifu, Roho wa Kweli (Yohana 14:17) anamwonyesha Yesu ni Masihi (Yohana 14:6; 16:13). Mtu anapomkana Yesu kuwa si masihi huyo anamfanya Mungu kuwa ni Mwongo (1 Yohana 5:10). Hakika, unatakiwa ufahamu kwamba mtu anapokuwa na maisha haya ya duniani hivyo swala la kumkubali Yesu kama mwokozi linabaki palepale. Tunapotaka kujua ukweli huu ni vema kufahamu kwamba kumkufuru Roho Mtakatifu ni kusema kuwa yeye ni mwongo aliposema juu ya Yesu Kristo. Si neno la kihuni lililotumiwa kumweleza Mungu (linganisha Petro alipomkana Yesu katika Mathayo 26:74), lakini hii n dhambi ya wasioamini ambayo huishia katika nyakati za maisha yao. Dhambi hii ni kile kitendo cha kuikataa kazi ya Yesu Kristo kama mwokozi na mwisho wake ni hukumuni.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 7, Sehemu ya 3

1. **Soma Yohana 3:16, 18 na 36. Ni kitu gani cha lazima kwa ajili ya wokovu?**

2. **Soma Yohana 1:1, 14 na 1 Wakorintho 15:3-5. Mtu anapaswa kamini Nini khusu Yesu?**

3. **Soma 1 Timotheo 2:4 na 2 Petro 3:9. Ni nini shauku ya Mungu kuhusu wokov wa mwanadamu?**

4. **Soma Waefeso 2:8-9. Mtu anaokokaje?**

5. **Imani ni nini na faida ni nini?**

6. **Soma 2 Timotheo 2:24-25. Ni kit gani cha lazima kinachoweza kubadili fikra?**

7. **Soma Warumi 3:20 na Wagalatia 2:16 na 3:24. Kitu gani kilichotustahilisha mbele za Mungu na kipi hakijatustahilisha mbele za Mungu?**

8. **Soma 2 Wathesalonike 2:13 na 1 Petro 1:2. Ni nani awatakasae walio katika Kristo?**

9. **Soma Waefeso 1:7 na Wakolosai 1:13-14. Kwa nini Muumini husamehewa?**

10. **Soma Mathayo 12:31-32; Yohana 14:17; Yohana 16:13 na 1 Yohana 5:10. Nini maana ya "kumkufuru Roho Mtakatifu?"**

# Sehemu ya 4
# Usalama: Ahadi ya Mungu

**A. Utangulizi**

Mtu anapookoka kwa imani ya Yesu Kristo maswali mengi yanainuka "twaweza tusiokolewe?" Kama tutatenda dhambi baada ya kuokoka je twaweza kuokolewa tena? Tutaishi maisha gani ya kikrito? Ili kwamba tusipoteze wokovu wetu na upendo wa Mungu? Tutajuaje kwa hakika kwamba tunao uzima wa Miele (1 Yohana 5:13)? Sehemu hii ya masomo yetu itajibu maswali haya ambayo muumini anaweza kujiuliza ili kujibu maswali haya.

**B. Maarifa ya Awali na Matoke Yake**

Maarifa awali ina maana ya kwamba "unajua kabla ya kushika." Yesu alijulikana kabla hata ya misingi ya ulimwengu (1 Petro 1:20). Neno matokeo linatoka katika Lugha ya kiyunani "PROORIDZO" likimaanisha "tia alama kabla ya kushika" ikiwa na maana ya kuweka mipaka.

Imeelezwa katika maneno ya Mungu kwamba maneno yake ya mwanzo ni matokeo ya matukio yake ya baadaye (Warumi 8:29-30; 1 Petro 1:1-2). Ufahamu wa Mungu si kwa maamuzi tu yafanywayo na mwanadamu ila na kwa matukio yanayotokea na hata madhara yake. Ukuu wa Mungu unaonekana katika kuleta mpango ambao alikuwa amempangia mwanadamu na hata malaika uwezo wa maamuzi na hata bado akaleta mpango wake wa kutufanya tufaulu.

Unabii unaoonekana katika neno la Mungu umewekwa ili kudhihirisha maarifa yake (2 Petro 3:17). Twaweza kujua hata kwa upana mambo yanayoweza kutokea; ama ni ya Mungu au hapana.

**C. Agano**

Kanuni ya 8 ya "Mambo Muhimu ya Kutafasiri Maandiko," inaonyesha tofauti tisa ya maagano ambayo Mungu alifanya na Mwanadamu. Mengine yalikuwa ni ya lazima ambayo mwanadamu alipaswa kutii. Na mengie yalikuwa ni ya hiari ambayo Mungu alifanya yeye mwenyewe. Maagano haya yana ahadi za Mungu kwa ajili ya Muumini kwa wakati uliopo na hata milele. Mwanafunzi ni vizuri asome habari zilizotolewa katika maagano haya ili kupata usalama tulionao katika ahadi ya Mungu.

**D. Usalama wa Milele**

Usalama wa milele una maana ya kwamba wokovu haupotei. Tutaendelea kuthibitisha usemi huu kulingana na vile tulivyojifunza. Hebu tukumbuke umuhimu wa sababu zinazopunguza hasa tunapoangalia somo hili. Kama tutaona katika maneno ya Mungu neno la kidunia kwamba hatuwezi kupoteza wokovu ni vizuri kukubaliana na hilo labda Biblia ilete swala jingine. Hii inamaana kwamba kama Biblia itakana swala au neno fulani basi ni lazima kukubaliana nalo kwani Biblia ndiyo chombo pekee kinachoweza kubadili mawazo na maamuzi. Kwa mfano Biblia inaposema, ***"wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu"*** (Warumi 3:23). Wazo pekee lililofanywa hapa ni kwamba Biblia ina maana kwamba ni Yesu tu ndiye tunapaswa kumtegemea ***"yeye hakufanya dhambi"*** (1 Petro 2:22). Sababu hii tunaiita kwamba ni "sababu zilizopunguzwa". Sababu zilizopunguzwa tunatupeleka kwenye hitimisho zuri kama vile, "wote wamefanya dhambi isipokuwa Yesu tu, na hii ni kwamba hata Mimi nina dhambi." Sababu zilizoongezwa kwa upande mwingine, hizi ni sababu zinazotoka upande huu na kwenda upande mzima unaokusudiwa (kwa kuwa mimi ni mwenye, dhambi basi wote wamefanya dhambi). Sababu hizi za kuhusisha wakati mwingine ni kweli lakini kwa Yesu Kristo sababu hii hafanyi kazi. Kosa kubwa laweza kutokea ikiwa sehemu kubwa ya kitu kizima itaachwa.

Uthibitisho wetu wa Usalama wa milele utatumia mambo manne tofauti yaliyo karibu:

1. **Mtazamo wa Kweli wa Kiimani**

   Sasa, hebu tuone mtazamo wa kweli uliokaribu kwenye Usalama wa milele, kwanza, wokovu ni kwa neema kwa njia ya Imani na wala si kwa kazi, kwa hiyo basi wokovu hauwezi kupotea kwa sababu ya kazi, kama vile dhambi (Waefeso 2:8-9). Pili, "kuzaliwa kupya" hutufanya "kwa wana wa Mungu," kwa hiyo kushindwa kwetu hakutamfanya baba yetu abadilike alivyo (Yohana 1:12-13; 2 Timotheo 2:13). Tatu, kwa kuwa Mungu alifanya makubwa japo tulikuwa ni adui zake hivyo hatatufanyia madogo kwani tumekuwa watoto wake (Warumi 5:9-10).

2. **Mtazamo wa Kiroho**

   Ukaribu wa sehemu uko katika kweli kwamba Muumini anasemwa kuwa yuko "ndani" ya Yesu Kristo na kwamba hakuna hukumu kwao walio katika Kristo Yesu (Warumi 8:1). Katika Kristo, upendo wa Baba kwa waumini ni sawa na upendo wa baba kwa mtoto wake hasa kwa sasa kwa kuwa tu watoto wake (Yohana 1:12-13; Warumi 8:38-39; Wagalatia 3:26; Waefeso 1:5-8). Kwa kweli, tayari tunashiriki ufufuo wa Bwana Yesu, ambao una maana ya kwamba hakuna kufa tena (Waefeso 2:6). Wazo jingine

ni kwamba “Kichwa” hakiwezi kuondoa viungo katika mwili na halafu ubaki kuwa ni mwili kamili (1 Korintho 12:13). Sisi ni sehemu yake Kristo.

3. **Mtazamo wa Kulindwa**
   Ukaribu wa kujihami ni kwamba usalama wa milele uko katika Yesu Kristo aliyekaa upande wa kuume wa Mungu Baba ambapo sasa yeye ni mlinzi wetu aliye mshinda Shetani (1 Yohana 2:1-2; Ufunuo 12:10). Alikuwa mpatanishi (“mtu wa katikati”) katikati ya Mungu na mwanadamu aliyepata agano jema (Wagalatia 3:20; 1 Timotheo 2:5; Waebrania 8:6; 9:15; 12:24). Anatuombea ili atukinge na kutuponya (Warumi 8:31-39). Yeyote anayejaribu “kuwapokonya kondoo wake toka mikononi mwake” anakuwa anavamia mamlaka ya Baba na Mwana (Yohana 10:27-29). (Ujumbe wa mwandishi: Huu ni usalama kwangu!)

4. **Mtazamo wa Kiroho**
   Kiroho usalama wa milele uko katika uhisiano wetu na mtu na kazi ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu humchuku mtu ambaye hajaokoka “aliye zaliwa katika mwili wa mbegu iharibikayo” na kumpleleka katika kilele cha imani ili apate kuzaliwa katika “mbegu isiyoharibika.” Kwa hiyo hatutakufa tena (1 Wakorintho 15:42, 52; 1 Petro 1:22-25; Yohana 11:25-26). Kuna zawadi nyingi tulizopewa tu mara baada ya kukoka ambazo ni kamili na hazibadiliki zitokazo kwa Roho Mtakatifu, (Warumi 11:29). Roho Mtakatifu huishi na muumini wakati tu wa wokovu na ufufuo wa mwili wa Mkristo (Warumi 8:9; 1 Yohana 2:27; 2 Wakorintho 1:22). Roho Mtakatifu pia huwabatiza wale waaminio katika umoja na Kristo (Warumi 8:9; 1 Yohana 2:27) na kuwatia mhuri waumini hadi siku ya kuokolea kwao (2 Wakorintho 1:21-22; Waefeso 1:13, 14; 4:30).

E. **Kukubalika**
   Yesu Kristo ni mwana pekee wa Mungu (Yohana 3:16). Tunapoingizwa katika umoja na Kristo kwa njia ya imani tunatazamwa kama “tumekubalika” wana wa Mungu. Kukubalika huku kulifanywa kwa wana wa Israeli wote lakini wengi walimkataa Masihi wao (Warumi 9:3-4).

   Waumini wana nafasi ya kuwa na uhusiano wa karibu na Baba kama walivyo na mwana wake wakijua ya kwamba wao ni Warithi pamoja na Kristo (Warumi 8:15-17; Wagalatia 4:4-7). Siku moja, tutaelewa kwa kina baraka za uhakika huu (Warumi 8:22-23).

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 7, Sehemu ya 4

1. **Soma 1 Yohana 5:13. Mtu anaweza kuwa na hakika wa kwamba ameokoka?**

2. **Soma warmi 8:29-30 na 1 Petro 1:1-2. Ni mambo gani ya Muhimu yanayotonesha tabiri wa matukio ya Mungu kwanza?**

3. **Soma Yohana 10:27-29. Kondoo wa Yesu wameahidiwa nini?**

4. **Soma Waefeso 2:8-9 na Warumi 11:29. Kwa kuwa wokovu ni karama je Mungu anaweza kutnyang’anya tena?**

5. **Soma Yohana 1:12-13 na 2 Timotheo 2:13. Ikiwa muumini ataishiwa Imani je hatakuwa motto wa Mungu tena?**

6. **Soma Warumi 5:9-10 na Luka 6:31-36. Je Mungu alituokoa tungali adui zake? Je kitu gani kilionesha upendo wake mkuu?**

7. **Je ianaleta maana kwamba japo alituokoa tukiwa ni Adui zake akatufanya watoto wake je anaweza kutuacha tena?**
8. **Soma Warumi 8:1. Inahusika na sehemu yetu katika Kristo, je ni kitu gani hakipo tena?**

9. **Soma Warumi 8:35-39. Ni kitu gani chaweza kumtenga Mkristo na upendo wa Kristo?**

10. **Soma 1 Petro 1:22-25. Kwa kuwa uzazi wetu si uharibikao kwa sababu metolewa na Roho mtakatif je twaweza kufa tena?**

11. **Soma warumi 8:15-17. Nini mahusiano ya Muumini kwa Mungu?**

# Sehemu ya 5
# Yajayo: Unabii (Eschatology)

**A. Utangulizi**

Mungu katika neema yake amekwisha weka mpango katika zama zote. Amekwisha tujulisha mambo yote ya kihistoria yatakayotukia. Sehemu zingine ametueleza kwa undani sana. na sehemu zingine kidogo sana. Tunatakiwa tuwe na imani ya kweli kwamba Mungu wetu anayo kesho katika mikono yake.

Unabii ni somo kubwa sana katika neno la Mungu. Kwa kweli, zaidi ya sura 271 kati ya sura 1189 katika Biblia zinahusika na unabii. Na hata kuna mistari ya nyongeza inahusika na unabii na hii ni kama moja ya nne (robo) Biblia. Kuna mistari mingine ya ziada ya unabii imo katika vitabu vingine, kwa hiyo kujifunza juu ya unabii ni muhimu sana.

Tunapojifunza unabii tunachotakiwa kujifunza kwanza ni matukio makubwa yale ambayo bado hayajatokea. Hii itatufanya tuwe na msingi utakaotuongoza katika masomo yetu. Kumbuka tangu Kanuni ya 15 katika somo letu la "Kanuni Muhimu za Kufasiri" katika Sura ya 4, ni kwamba unabii mwingine ulikwisha kamilika lakini mwingine bado.

Katika somo hili tunatakiwa tuelewe majina mbalimbali yaliyotumika kuelezea matukio au mambo yajayo.

**B. Nyakati Mbalimbali katika Historia**

Unabii umeunganishwa na masomo mbalimabli ya kihistoria. Ni vizuri kwa mwanafunzi kupitia tena Kanuni ya 13 ya "Kanuni za Msingi za Kulifafanua Neno la Mungu" inayohusiana na Nyakati mbalimbali katika historia.

Nyakati mbalimbali katika historia ni vipindi vya kihistoria ambapo Mungu aliweka majukumu mbalilmbali kwa watu wake. Kuna mabadiliko ya ukuhani na pia mabadiliko ya sheria ili kuonesha mabadiliko haya (Waebrania 7:12).

Kipindi cha watakatifu kilichoishia kutoka anguko la Adamu hadi kutoka kwa wana wa Israeli katika nchi ya Misri na kimekwisha kamilika. Kipindi cha Waisraeli kilichoanzia pale wana wa Israelli walipotoka Misri (na wakapewa Sheria) hadi Siku ya Pentekosite. Hiki nacho kimekwisha kamilika isipokuwa kile kipindi cha dhiki kuu (Danieli 9:24-27).

Sasa tuko katika kipindi cha kanisa kilichoanzia Siku ya Pentekoste na kitaendelea hadi siku kanisa litakaponyakuliwa.

Miaka elfu kitaanza wakati Yesu atakaporudi mara ya pili na kutawala mika elfu na kitakoma pale atakapomkamata Ibilisi na kumtupa katika ziwa la moto.

**C. Unyakuo**

Neno "Unyakuo" linatokana na Lugha ya kilatini "RAPERE" lililotumika katika kufasiri neno la kiyunani "HARPADZO" lililo katika 1 Wathesalonike 4:17, katika fasiri za Biblia ya kilatini. Na kwa kiingereza ni "kuchukuliwa juu ."

Wakati wa Unyakuo Bwana atawafufua waumini waliolala mauti pamoja na waumini watakaokutwa wakiwa hai na kwenda nao mawinguni pamoja naye (1 Wathesalonike 4:14-17). Uhamisho huu utakuwa ni wa ghafla tu (1 Wakorintho 15:51-52).

Unyakuo utahitimisha Kipindi cha Kanisa na kuanzisha kipindi kingine cha Mateso au muda wa majuma sabini (Daniel 9:24-27).

**D. Mateso**

Neno "Mateso" linatokana na neno la kiyunani (THLIPSIS), likiwa na maana ya "dhiki," kama vile mtu anapokanyaga matunda ya dhabibu kwa miguu yake. Ni kipindi dhiki kuu ya roho na mwili ambacho hakijawahi kutokea duniani, na mhitasari wa mambo yatakayotokea yako katika kitabu cha Ufunuo 6-19.

Mateso haya yatakuwa ni ya miaka saba kwa maana nyingine yanajulikana kama "Majuma Sabini ya Daneli" (Danieli 9:24-27). Nabii Danieli alipewa ufunuo na Mungu wa majuma sabini ya miaka ambayo yalitabiriwa kwa watu wake, Wayahudi. Majuma 69 ya mwanzo yalikamilishwa na Yesu huko Yerusalemu juma kabla ya kwenda msalabani. Na juma la 70 itakuwa ni miaka saba ya mwisho ya kipindi cha waisraeli ambacho kitaisha kati ya Yesu atakapolichukua kanisa na atakaporudi Mara ya Pili.

**E. Kurudi kwa Yesu Mara ya Pili**

Hiki ni kipindi cha haraka sana wakati Yesu atakaporudi Mara ya Pili baada ya miaka saba ya mateso makali (Mathayo 24:29). Ni tofauti na unyakuo kwa sababu hapa Yesu Kristo atakuja na kuweka miguu yake katika dunia hii (Zekaria 14:1-6) lakini katika kunyakua kanisa atakuja mawinguni (Matendo 1:11).

Wakati huu atawashinda adui zake na kuanza kutawala miaka elfu (Ufunuo 19:20–20:6). Kristo ataweka miguu yake katika mlima mizeituni na utapasuka katikati na kuwaokoa Israeli watakokuwa wamebakia (Zekaria 14:1-6). Atazungumza na kumharibu mfalme wa magharibi (2 Wathesalonike 2:8; Ufunuo 19:15). Na halafu, atashusha moto kutoka mbinguni na kumharibu Mfalme wa Kaskazini (Ezekieli 38-39) ambaye tayari amekwisha mharibu Mfalme wa Kusini (Danieli 11:40-44). Halafu ataingia mkono kwa mkono akipigana na Mfalme wa Mashariki (Isaya 63:1-6; Ufunuo 14:20).

**F. Utawala wa Miaka Elfu**

Hii ina maana ya Utawala wa Miaka 1,000 atakayo tawala Yesu Kristo hapa duniani (Ufunuo 20:6). Kuna sura nyingi zinazotupa sifa ya Utawala huu.

Ufalme wa miaka Elfu utakamilisha Agano la Abrahamu, Daudi na Agano Jipya. Pia litaondoa laana ya Edeni (Mwanzo 3:17-19).

Sifa za kimwili zitakazoonekana katika utawala huu ni pamoja na: (1) Hakuta kuwa na vita (Isaya 2:4; Mika 4:3); (2) hakutakuwa na wanyama wa kutisha (Isaya 11:6-9; 35:9; 65:25); (3) hakuna magonjwa wala ulemavu na maisha yatakuwa ni marefu (Isaya 29:17-19); (4) hakuna siasa wala manyanyaso ya kisiasa wala mambo ya kiuchumi (Isaya 14:3-6); (5) ongezeko la watu (Yeremia 30:20); (6) kazi (Yeremia 31:5; Isaya 62:8-9; 65:21, 23); (7) ongezeko la uchumi (Isaya 35:1, 2, 7); na (8) nuru kutoka kwa Bwana (Zekaria 14:6-7). Utawala huu wa miaka elfu wayahudi na watakatifu watakaokutwa wakiwa hai baada ya mateso kama "kondoo" (Mathayo 25:31-46), kutakuwa na wanadamu walio na dhambi ya asili katika utawala huu. Na hivyo watoto watakao wazaa ni lazima waokolewe.

Mambo ya kiroho: (1) hakika (Malaki 4:2; Zaburi 89:14); (2) maarifa kamili ya Bwana (Isaya 11:9); (3) ujazo wa Roho Mtakatifu (Yoeli 2:28-29); (4) Furaha (Isaya 9:3-4); na (5) uhuru, haki na amani (Isaya 9:7; 11:5; 32:16; 42:1-4; 65:25).

Utawala wa Kristo utakuwa ni wa dunia yote (Danieli 7:14; Mika 4:1-2; Zephania 3:9-10; Zaburi 72:8) wenye serikali moja (Ezekieli 37:24-28). Hakuna maasi (Zaburi 72:1-4; Ufunuo 19:15). Na Yerusalemu itakuwa ni kituo cha serikali ya duniani (Isaya 2:2-4; Yeremia 31:6; Mika 4:1; Zephania 2:10-11) na ulilindwa na Uwepo wa Mungu (Isaya 11:9). Itakuwa ni rahisi kutathimini (Isaya 35:8-9) kwa sababu umepanuka (Jeremia 31:38-40; Ezekieli 48:30; Zekaria 14:10). Yerusalemi ndiyo itakayo kuwa kituo cha kuabudia (Yeremia 30:16-21; 31:6, 23; Yoeli 3:17; Zekaria 8:8, 20), ukiwa katikati ya Hekalu la Utawala (Ezekieli 40:1-46:24) na ikiongozwa na Sadoki Kuhani Mkuu (Ezekieli 43:19; 44:15).

**G. Hukumu Kuu ya Kiti cha Enzi Cheupe**

Hukumu ya Kwenye Kiti cha Enzi Cheupe hii itatokea baada ya miaka elfu na ibilisi atakapokuwa ameachiliwa kwa muda mfupi. Atakuwa karuhusiwa kuyadanganya mataifa na kuwaongoza gogu na magogu (Ufunuo 20:7-8). Kwa wale watakao kuwa wakiishi kipindi hiki watakuwa ni mateka wake. Na Bwana atammaliza shetani kwa kushusha moto kutoka mbinguni na kumuunguza shetani na kumweka katika zaiwa la moto pamoja na yule dubu na manabii wake wa uongo (Ufunuo 20:9-10).

Baada ya hayo wasioamini watafufuliwa wapate kupata hukumu yao ya mwisho katika kiti kikuu cha enzi cheupe; watatupwa katika ziwa la moto (Ufunuo 20:11-15).

**H. Haki ya Milele**

Haki ya milele ni "Siku ya Mungu" (2 Petro 3:12). Hii itaanza baada ya hukumu na baada ya kuharibiwa kwa dunia hii na kuletwa dunia na mbingu mpya (Isaya 65:17; 66:22; 2 Petro 3:12-13; Ufunuo 21:1). Dunia Mpya hii itakuwa na Yerusalemu Mpya (Ufunuo 21:2-5) itakayochukua makabila yote kumi na mbili ya Israeli na mitume kumi na mbili. Hakutakuwa na hekalu kwa sababu Yesu Kristo ambaye ni Mwanakondoo wa Mungu atakuwa ni Nuru (Ufunuo 21:22-23). Mto uliojaa maji ya uzima utavujia mito na itatoa aina kumi na mbili tofauti za matunda kila mwezi moja (Ufunuo 22:1-2).

Hakutakuwa na dhambi (Ufunuo 21:24-27). Kwa wale wote ambao hawakumpokea Yesu wala kupata msamaha wa dhambi zao hawatastahili wala kuruhusiwa kuuingia Yerusalemu mpya na mbingu mpya na hata nchi mpya. Watakuwa katika ziwa la moto milele (Ufunuo 21:8). Ni wale tu watakaoshinda ndiyo wale watakaoruhusiwa kuingia katika uzima wa milele pamoja na Mungu Ashukuriwe Mungu ***"imani ni ushindi inayoshinda ulimwengu"*** (1 Yohana 5:4-5).

Tafadhali uelewe kwamba si dhambi zilizoelezwa katika Ufunuo 21:8 zinazomfanya mtu atengwe na Mungu lakini ni zaidi hata ya kushindwa kumwabudu na kumwamini Yesu ili wapate kusamehewa.

## Kwa Masomo Binafsi 7, Sehemu ya 5

1. **Soma Waebrania 7:12. Kinatokea nini mpango wa Mngu unapobadilika?**
2. **Soma 1 Wathesalonike 4:14-17. Wamini watakutana na yesu wapi ipindi cha unyakuo?**
3. **Soma 1 Wakorintho 15:51-52. Je unyakuo wa kanisa tatokea kwa uharaka gani?**
4. **Soma Yohana 14:1-3. Kanisa litakuwa wapi baada ya unyakuo?**
5. **Soma Danieli 9:24-27. Juma la sabini linajumuisha miaka saba ambayo haijakamilishwa. Je kipindi hiki kinaiwaje?**
6. **Soma Ufunuo 19:11-16; Mathayo 24:29-30 na zakaria 14:1-6. Kristo atafanya nini baada ya dhiki kuu?**
7. **Nini tofauti kubwa kati ya unyakuo na kuja mara ya pili ukilinganisha na sehemu zenyewe?**
8. **Soma Ufunuo 19:20; 20:10. Nani amewekwa katika ziwa la moto wakati wa kuja Yesu mara ya pili?**
9. **Soma Ufunuo 20:1-3. Nani atatupwa katika moto huo baada ya kuja yesu mara ya pili?**
10. **Soma Ufunuo 20:4-6. Ni kwa muda gani tawala wa Yesu utaisha hapa duniani?**
11. **Soma ufunuo 20:7-10. Baada ya miaka elfu, shetani ataachiwa kwa mda, aongoze uasi halafu atashindwa na ataishia wapi?**
12. **Soma Ufunuo 20:11-15. Kwa wale ambao majina yao hayataonekana katika kitabu cha uzima baada ya kiti cha Enzi cheupe wataenda wapi?**
13. **Soma 2 Petro 3:10-13 na Ufunuo 21:1. Kitatukia nini baada ya hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi kikubwa?**

Sura ya 8

# Mafundisho ya Makusudi ya Mungu

# Sehemu ya 1
# Maisha Binafsi ya Mkristo (Hodology)

**A. Utangulizi**

Kusudi la Mungu kwa kila mwanadamu ni kwamba awe na sura ya mwana wake, Yesu Kristo (Warumi 8:29). Ameweka sura tatu ili kwamba apate kukamilisha lengo na makusudi yake. Mabadiliko haya atayaita: Sura 1, Sura 2 na Sura ya 3.

Sura ya 1 hutokea pale mtu anapompokea Yesu (Matendo 16:31). Hiki ni kipindi cha wokovu wa milele mtu huyo.

Sura ya 2 hii ni hali inayoendelea ndani ya mtu tangu siku alipompokea Yesu hadi pale anapokufa au atakaponyakuliwa pamoja na kanisa.

Sura ya 3 hii huanzia pale mtu anapokuwa amekufa kifo cha kawaida au siku ya kunyakuliwa na kuishi katika uzima wa milele.

Sura ya Mungu nayohitajika haitaweza kukamilika hadi pale mtu anapofikia ile sura ya 3 ndipo inapokamilika lakini muumini huanza kupata mabadiliko wakati tu wa wokovu (2 Wakorintho 3:18). Sura ya Yesu ni kumbukumbu ya kuwa na mitazamo kama yake yaani unyenyekevu na kujitoa kama dhabihu (Wafilipi 2:5-8). Sehemu hii ya mabadiliko ni sehemu ya jinsi ***"tunavyotembea kama tulivyoitwa na Bwana"*** (Waefeso 4:1-3).

Ukweli wa kwamba kuna sura katika maisha ya mkristo ni muhimu sana kuelewa kwa sababu hutupa kutambua na kutusaidia kuelewa neno la Mungu. Tunapojiuliza swali la "nani" tunatakiwa tuelewe kama Mungu anazungumza na wakristo au wapagani ili kwamba tupate kulitumia na kufasiri vyema neno la Mungu. Hebu weka hii katika akili zako hasa tunapojaribu kuangalia swala zima la Kiroho.

**B. Mambo Kumi na Tatu ya Misha ya Mkristo**

**1. Imani**

Tunasema imani ni kuamini kitu au mtu fulani. Unaamini kwamba kitu hiki au mtu huyu ataweza kutoshereza mahitaji yangu; na makusudi ya Imani ni ile thamani ya imani inayotokea si katika imani tu. Mtu anaweza kufikiri au kuamini kwamba mtu anaweza kuumba mbingu nyingine sawa na hii tunayoishi lakini hakuna kweli nguvu ya kutosha katika mwanadamu ya kumwezesha kufaya uumbaji; na imani hii haina maana wala thamani japo ni Imani.

Imani inapokuwa kwa mtu aliye na maarifa na uwezo wa kukamilisha jambo fulani Imani hiyo inakuwa na thamani. Imani yetu iko kwa Mungu aliye umba mbingu na nchi na huyu ana nguvu, maarifa na hata shauku. Maandiko yanasema, ***"Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yasiyo tarajiwa ni bayana ya mambo yasiyoonekana, maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa kwa imani twafahamu ya kwamba ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyodhahiri"*** (Waebrania 11:1-3).

Imani katika Kristo ni muhimu sana kwani inathibitika (inakuwa na haki) na ni mwongozo wetu katika neema tuliyopewa kama Wakristo (Warumi 5:1-2). Imani ni muhimu sana kwa wasio amini ili wapate kuamini katika Sura ile ya 1. Imani hii huleta uhusiano wetu na Roho Mtakatifu (Wagalatia 3:2-3, 14).

Imani ni muhimu sana katika maisha ya Mkristo (Sura ya 2) kwa sababu ni vigumu kumpendeza Mungu bila Imani (Waebrania 11:6; 2 Wakorintho 5:7). Yeye hufurahi anapoiona Imani ndani yetu (Matayo 8:5-10). Imani ndiyo huushinda ulimwengu na hata mitego ya Ibilisi (1 Yohana 5:4-5). Imani ya mkristo itajaribiwa ili kwamba tupate kukuwa kutoka uchanga hadi tukomae katika Kristo (Yakobo 1:3). Imani yetu hutufanya tukue na kuongezeka katika uhusiano wetu na Roho Mtakatifu (Wagalatia 3:4-5). Imani ni msingi katika maisha ya Mkristo (2 Petro 1:5-9).

Tutakapokua na Kristo milele katika miili yetu iliyofufuliwa hatutakuwa na hitaji la imani kwa sababu tutakua tumemwona yeye kama alivyo (1 Yohana 3:2).

**2. Kiroho**

Kiroho ni neno lililotumika kuonyesha ukina katika uhusiano wetu na Mungu Roho Mtakatifu. Kwa hiyo ni lazima tuwe katika kumtazama Roho Mtakatifu katika maisha yetu. Asiye mkristo hana uhusiano na Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 2:14) na kwa sababu hiyo yeye hana kiwango cha kiroho.

a. **Kutawaliwa**
Kanisa la leo ni tofauti na na kanisa la zamani hasa katika swala zima la jinsi Roho alivyotenda kazi kwa Wakristo. Sasa anatenda kazi na Wakristo kulingana na neno la Yesu (Yohana 14:17). Uwepo kabisa wa Roho Mtakatifu ndani ya muumini ni uthibitisho wa wokovu (Warumi 8:9).

Kutawaliwa na Roho Mtakatifu ni karama au zawadi unayopata wakati wa kumpokea Yesu (Warumi 5:5; Matendo 11:16-17; 1 Wakorintho 2:12) na kama zawadi haiwezi kamwe kukataliwa (Warumi 11:29). Roho Mtakatifu haondoki mtu anapotenda dhambi na hii tunaithibitisha kwamba japo kuwa Wakristo wa mwilini (1 Wakorintho 3:3) wanaotenda dhambi (1 Wakorintho 5:5), *wote* wanae Roho Mtakatifu anayeishi ndani yao (1 Wkorintho 3:16; 6:19).

b. **Kujaza**
Kwa kuwa neno 'Kiroho' linaonyesha kiini cha uhusiano wetu na Roho Mtakatifu "Ujazo wa Roho Mtakatifu" ni mwanzo wa Kiroho. Tunapasa kujazwa na Roho Mtakatifu wakati wote ili kwamba apate kuzaa matunda kupitia sisi (Wagalatia 5:22-23).

Kujazwa kwa Roho Mtakatifu katika Biblia ni kitu kilichooneshwa kama ni kitu muhimu cha kubeba majukumu maalum, kwa kila siku katika maisha ya Mkristo. umuhimu wa kujazwa na Roho Mtakatifu katika maisha na Roho Mtakatifu kwanza kabisa yanaonekana kwa Stephano ambaye alichaguliwa kuwahudumia wajane (Matendo 6:5). Maana hii kubwa tunatakiwa kuiangalia pale kanisa linapokuwa limeanza; huanza kama changa na baadaye linavyoongezeka huwa ni kubwa a lililokomaa (Waefeso 4:11-16).

Na hii kujazwa na Roho Mtakatifu nje ya injili na kitabu cha Matendo ndicho hicho Paulo anaamuru kwamba ***"Msilewe kwa mvinyo bali mjazwe na Roho"*** (Waefeso 5:18). hii inaonesha kwamba kitendo cha kujazwa na Roho Mtakatifu ni muhimu sana kwani wendi kipindi hiki walitumia mvinyo sana. Na hii imeoneshwa katika mafundisho ya Paulo mapema kabisa kwamba "kujazwa" (PLEROO kwa Kiyunani) iliyo katika Waefeso 1:23, 3:19 na 4:10. Amri hii ya Paulo inaonesha kuwa Kujaza na Roho Mtakatifu ni kumfanya mtu atambue na kuelewa swala zima la dhambi na aelewe kwamba Mungu amekwisha samehe dhambi, na umuhimu wa kujazwa humfanya mtu awe wa "Kiroho."

Ukiroho halisi huusisha Neema na Imani; tunaambiwa kwamba ***"kama mlivyompokea Kristo Yesu Bwana enendeni vivyo hivyo katika yeye. Muwe shina na wenye kujengwa katika yeye mmefanywa imara kwa imani kama mlivyofundishwa mkizidi kutoa shukrani"*** (Wakolosai 2:6-7). Tulimpokea kwa neema kwa njia ya imani (Wefeso 2:8-9). Pia tunaelezwa kwamba kujazwa kunakotufanya kuwa wakristo halisi kumejengwa katika kutembea kwa imani (Wagalatia 3:2-3) na bila imani ni vigumu kumpendeza Bwana (Waebrania 11:6).

Kwa kuhitimisha kujazwa kwa Roho Mtakatifu kunamwezesha mkristo awe mkamilifu katika Kristo.

c. **Kuhuzunisha**
Muumini anapotenda dhambi humhuzunisha au huleta masikitiko makali kwa Roho Mtakatifu (Waefeso 4:30). Kadri tunavyotenda dhambi na tunashindwa kuziungama dhambi zetu ndivyo tunavyomhuzunisha Roho Mtakatifu. Neno hili linaeleza kile kinachotokea kwa Mkristo anapokuwa ametenda dhambi.

Mkristo anapokuwa "amemzoea" Roho Mtakatifu hii inatuharibia maisha yetu ya kiroho na hata matunda yetu ya Kiroho na hata tunaharibu na wengine (1 Wathesalonike 5:19). Hatupaswi kujaribu kumuia Roho Mtakatifu ili asitende kzi kwa wengine.

3. **Kuungama Dhambi**
Kwa kuwa tunaelewa kwamba tunapookolewa dhambi zetu husamehewa hivyo tuelewe kwamba kama wakristo bado tutatenda dhambi tu (Warumi 7:14-25). Dhambi si kitu katika wokovu wetu lakini ni mbaya sana katika maisha yetu ya Kikristo. Kwa sababu dhambi huharibu uhusiano wetu na Mungu na hata na wengine pia. Hivyo dhambi huharibu sana ushirika wetu.

Ushirika ni ile hali ya kuwa pamoja; hii yaweza kuwa ni watu, vitu, matukio au hata nyakati hata wasio wakristo waweza kuwa na ushirika kama wataungana kwa ajili ya dhambi fulani. Kama mkristo au asiye mkiristo atavunja ushirika wake basi katikati kunakuwa hakuna furaha tena, kama wakristo ni lazima tuwe na ushirika na Mungu na hata wengine kama watoto wa Mungu. Ushirika ndicho kitu cha pekee alichokiweka Mungu.

Ujumbe wa kurejesha ushirika na Mungu wetu au hata wakristo wenzetu umeelezwa katika 1 Yohana 1:5-10:

Mstari wa 5 unaonesha ushirika. Unasema mstari umuweka vigezo vya usharika. Inasema, ***"nahii ndiyo habari tuliyoisikia kwake na kuihubiri kwenu ya kwamba Mungu ni nuru wala Giza lolote hamna ndani yake."*** Ushirika ni Nuru ya Mungu ambayo ni kweli yake inayoshindana na dhambi.

Mstari wa 6 unaonesha mtihani wa ushirika. Inasema, ***"tukisema ya kwamba twashirikiana naye tena tukienenda gizani twasema uongo wala hatuifanyi iliyo kweli."*** Hii ina maana kwamba Mawazo yetu, maneno na matendo ni lazima yaagaliwe nuruni.

Mstari wa saba 7 hali ya ushirika. Inasema, ***"bali tukienenda nuruni kama yeye alivyo nuruni twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu mwana wake yatusafisha dhambi yote."*** Mawazo yetu, maneno na mienendo yetu iliyo sawa na Kristo huleta ushirika na kila mtu na hutusafisha na dhambi zote.

Mstari wa 8 inaonyesha uongo wa dhambi. Inasema, ***"Tukisema kwamba hatuna dhambi twajidanganya wenyewe na wala kweli haimo ndani yetu."*** Neno Sisi linawawakilisha waumini ka sababu hata Yohana amejiunganisha katika kundi hili. Ikiwa mtu anaamini kwamba yeye hana dhambi na tena ni mkamilifu mtu huyu tayari kaisha jidanganya mwenyewe.

Mstari wa 9 unaonyesha njia ya kumaliza tatizo la dhambi. Inasema ***"kama tutaziungama dhambi zetu yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee na kutusafisha na udhalimu wote."*** Neno la kiyunani limetafasiri "kuungama" (HOMOLOGEO) ina maana ya kushukuru na kukubaliana na Mungu kwamba mawazo, maneno na hata matendo ni dhambi. tafadhali elewa lkwamba hi siyo kanuni ya kwamba Mungu anaweza kusamehe tu hata kama roho haitaki kukiri. Mungu hataki kudhihakiwa (Wagalatia 6:6). Sababu ya kukiri dhambi mtu anatengeneza ushirika wake na anaimani kwamba Mungu anaweza kusamehe. Mstari ni ahadi ya Mungu ambayo wakristo wanapaswa kuifahamu, kuiamini na kuitumia.

Mstai wa 10 unaongelea juu ya wale wasioijua dhambi mana inasema, ***"kama tukisema kwamba hatuna dhambi twamfanya yeye kuwa muongo na wala neno lake halimo ndani yetu."*** Mstari huu unasema kama hatutatambua ya kwamba dhambi inaishi katika maisha yetu tumemfanya Mungu kuwa mwongo na wala neno lake hatulielewe.

Tukiingaalia mistari hii tunaona kwamba ushirika wa kiroho na Mungu wetu (mstari 6) na waumini wengine (mstari wa 7) umeharibiwa na dhambi. Dhambi hizi lazima zitambuliwe mbele za Mungu (mstari 9 – Mungu ni mwaminifu na wa haki ) ili kwamba msamaha utendeke na ushirika wetu udumu.

Tafadhali uelewe kwamba matatizo ya dhambi za nje yamekwisha kusamehewa. lakini Muumini ataendelea kukabiliana na matatizo madogo madogo katika nyakati mabalimbali za maisha yake. Adam na Hawa walisamehewa lakini bado walifukuzwa kutoka katika bustani ya Edeni.

**4. Karama za Kiroho**

Karama za kiroho ni uwezo ambao Mungu hutoa kwa watu wake ili waweze kutenda kazi katika eneo zima la mwili wa Kristo. Neno hili limetoka katika lugha ya kiyunani likiwa na maana ya "umepewa kama matokeo ya neema" (CHARISMA). Ni tofauti sana na kipaji ambacho mtu huzaliwa nacho (Waefeso 4:11) na Roho Mtakatifu hutoa vipawa hivi wakati mtu anapookoka (1 Wakorintho 12:11, 18) katika mwili wa Kristo (Waefeso 2:20). Kila mtu ana kipawa angalau kimoja (1 Petro 4:10), lakini si kila kipaji kinajitegemea (1 Wakorintho 12).

Ni vizuri kuelewa kwamba karama hizi hutenda kazi kwa pamoja na kwa upendo (1 Wakorintho 13) na kwamba vipo ili vipate kusaidiana (1 Petro 4:10). Mtume Paulo ameainisha vizuri katika 1 Wakorintho kwamba hata kama ni karama za kiroho zilizotolewa na Roho Mtakatifu zinaweza kutumika kimwili ili kumfanya mtu awe na Kiburi (1 Wakorintho 12). Karama za kiroho zipo ili kulijenga kanisa na siyo kuleta fujo na migawanyo (1 Wakorintho 14:12, 33).

Kuna sehemu tano katika Agano la Jipya ambapo karama hizi zimetajwa kwa majina. Katika **1 Wakoritho 12:8-10** tunaona kwamba kuna neno la hekima, neno la maarifa, Imani, uponyaji, miujiza, unabii, utambuzi wa roho, lugha na ufasiri wa lugha. Katika **1 Wakorintho 12:28** tunaona mitume, manabii, waalimu, miujiza, karama za kuponya wagonjwa na masaidiano, na maongozi na aina za lugha. Katika **Waefeso 4:11** tunaona mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na walimu. Katika **1 Petro**

**4:11** mawasiliano na huduma yametolewa kama makundi mawili muhimu ya karama za Kiroho. **Warumi 12:6-8** inatupa orodha ya baadhi za karama hizo muhimu.

Tafadali tambua kwamba karam za kiroho zilitolewea katika kanisa lililoanza Siku ya Pentecoste (Matendo 2). Na zingine zilitolewa ili kujenga msingi (Waefeso 2:20) ili kwamba kanisa lipande kuanza, kujengwa na kuimarishwa (1 Wakorintho 14:40). Karama hizi zinaitwa "ishara" na zilitumika katika kuwahubiri wasiowaumini na kuwaimarisha Waumini (1 Wakorintho 14:20-22) mpaka maandiko yalipoandikwa. Ishara hizi zilikuwa ni za muda tu na hazikuhitajika tena baada ya kuwa wamemaliza kazi zao muhimu katika kanisa la kwanza na zilikoma na kupotea kabisa (1 Wakorintho 13:8-10).

Jedwali lifuatalo linaonyesha karama za kiroho za muda ambazo kwa sasa hazitendi kazi katika kanisa:

| **Karama za Kiroho kwa Ajili ya Kanisa Jipya** | |
|---|---|
| **Neno la Hekima**<br>(1 Wakorintho 12:8) | Ni maelekezo katika kanisa la sasa ili kuwajenga na kuwaongoza watu katika kweli |
| **Karama ya Imani**<br>(1 Wakorintho 12:9) | Ni Imani kubwa isiyoonekana katika Bwana ya kuona yote yanawezekana (1 Wakoritnho 13:2 linganisha Matendo 12:1-19) |
| **Neno la Maarifa**<br>(1 Wakorintho 12:8) | Ni ujumbe uliokuwa ukisemwa moja kwa moja katika kanisa ili kuwajenga na kuwaongoza watu hadi pale Agano Jipya lilipokamilika |
| **Uponyaji**<br>(1 Wakorintho 12:9, 28) | Nguvu ya ajabu, ya haraka na uponyaji wa papo kwa papo kwa watu mbalimbali na matatizo yao. |
| **Miujiza**<br>(1 Wakorintho 12:10, 28) | Ni nguvu ya ajabu iliyoharibu kabisa sheria zilizokuwepo na kuziweka kando na hii iliuganishwa na uponyaji, uponywaji wa watu na nguvu za mapepo. (Metendo 19:11-12). |
| **Unabii**<br>(1 Wakorintho 12:10, 28; Warumi 12:6; Waefeso 4:11) | Ni nguvu ya ajabu iliyoeleza mambo yajayo kuhusu kanisa (Matendo 11:27-28) |
| **Karama za Kutambua Roho**<br>(1 Wakorintho 12:10) | Ni nguvu Iiliyohusika katika kuwatofautisha manabii wa kweli na manabii wa uongo (1 Wakoritho 14:32) |
| **Ndimi/Lugha**<br>(1 Wakorintho 12:10, 28) | Ni nguvu iliyowafanya watu wazungumze lugha ambazo hawakuwa wamejifunza wala kuziongea |
| **Ufasiri wa Ndimi/Lugha**<br>(1 Wakorintho 12:10) | Ni nguvu ya ajabu iliyohusika katika kukarimani lugha ambayo watu waliizungumza ilikuwa ngeni na wala hawakujifunza |
| **Mitume**<br>(1 Wakorintho 12:28; Waefeso 4:11) | Karama ya Kiroho iliyokuwa kwa watu kumi na mbili (Ufunuo 21:14) waliochaguliwa na Kristo mwenyewe (Luka 6:13-16; Matendo 9:15; Wagalatia 1:1). |

Tunaambiwa kwamba karama za "Unabii", "Lugha", na "Neno la Maarifa" zitafanyika pale ukamilifu utakapokuwa umefika (1 Wakoritho 13:8-10). Japo kuwa vitu hivyo vitakuwa vimefanyika sasa karama ya kutambua Roho na kutafasiri lugha zitapotea kwa sababu zinafanya kazi kwa pamoja. Elewa kwamba karama zote hizi zinahusika na mawasiliano. Kitabu cha ufunuo kilipoandikwa unabii ulifungwa (Ufunuo 22:18-19). Kwa hiyo ukamilifu lazima ukamilishwe na Mungu alivuvia pumuzi katika neno lake. Hakuna haja ya habari mpya zinazohitajika kwa ajiri ya kanisa. Karama ya ualimu inalenga katika mawasiliano kupitia kile kilichondikwa, neno la Mungu la Agano Jipya.

Ufunuo 21:14 inaonyesha kwamba kulikuwa na mitume kumi na mbili tu. Kuna watu wanaoshikilia kwamba kuna mitume ndiyo lakini hawana karama (Wagalatia 1:19; na ndugu yake Yesu hakuwa mmoja wa wale kumi na mbili). Kwa hiyo uelewe kwamba hii karama ilikuwa ni ya muda.

Karama ya uponyaji na miujiza ilikuwa ni ya muda tu kama ilivyothibitishwa katika Agano Jipya. Mungu bado anaweza na anaponya watu lakini si kwa njia ya karama alizozitoa kwa watu. Bwana bado anajibu maombi (Yakobo 5:16), lakini kazi ya karama ilitegemea maamuzi ya yule aliyekuwa na ile karama. Watu walio na karama ya uponyaji wanapaswa wamwite bwana na uponyaji unatendeka (Matendo 3:6-8; 5:12-16; 9:34). Karama zilitumika katika kanisa la kwanza ili kufafanua injili ya Yesu aliye fufuka (Matendo 8:1-8, 39; 13:4-12; 14:1-4; 19:11-12). Upendo wa wakristo wa kuwapenda na wengine ni njia nzuri ya kuelezea ujumbe wa Bwana Yesu (Yohana 13:34-35).

Tunafahamu kwamba Mtume Paulo alikuwa na karama ya uponyaji (Matendo 20:8-12; 28:8) lakini baadaye katika maisha yake hakuwa na uwezo wa kuponya tena na hata hakumponya rafiki yake

Epafrodito (Wafilipi 2:25-27) au yeye mwenyewe (2 Wakorintho 12:7-9). Kwa kuwa karama hii iliisha kwa Mtume Paulo hata wale wengine ni dhahiri kwamba karama hizi ziliwaisha.

Tunazo karama zilizoletwa kwa ajiri ya kanisa bada ya kuwa limetoka katika uchanga (1 Wakorintho 13:10-13) na hizi ni za moja kwa moja. na karama hizi zinawasilisha neno la Mungu na kuwahudumia wengine (1 Petro 4:10-11).

Jedwali lifuatalo linaonesha Karama za kudumu zinazotenda kazi leo.

| Karama za Kudumu katika Kanisa Jipya | |
|---|---|
| **Kufundisha**<br>(1 Wakorintho 12:28; Warumi 12:7) | Ni nguvu ya ajabu ya kuelezea neno la Mungu ka watu wengine |
| **Misaada**<br>(1 Wakorintho 12:28) | Karama ambayo kwa nguv inasaidia karama za wengine. Inatenda kazi katika maeneo mengi. Mfano ni kuksanya au kuandaa hakula kwa ajili ya watu wengine ili nao wajifunze kuwasaidia wengine (Matendo 6:1-6) |
| **Utawala**<br>(1 Wakorintho 12:28) | Wezo wa kupanga na kusimamia vyanzo ambavyo Mungu amelipatia kanisa |
| **Kutumika**<br>(Warumi 12:7; 1 Petro 4:11) | Karama ya ajabu ya kubeba huduma katika hali ya kivitendo |
| **Kushauri**<br>(Warumi 12:8) | Ni karama ya kutambua na kushauri na kutoshereza mahitaji kwa njia ya kutia moyo katika mwili wa Kristo |
| **Kutoa**<br>(Warumi 12:8) | Ni karama ya kushirika mambo na wengine kwa kiwango kikubwa zaidi ya ilivyokuwa ikitegemewa. Si kwa kiwango kilichopangwa lakini ni kwa hiari, na unakitoa kwa moyo mweupe kabisa |
| **Kuongoza**<br>(Warumi 12:8) | Ni uwezo wa kuelekeza na kusimamia watu kwa usahihi katika huduma ya kanisa |
| **Huruma**<br>(Warumi 12:8) | Ni uwezo wa kutambua na kusaidia wale walio katika mahitaji ya kiroho na kimwili |
| **Uinjilisti**<br>(Waefeso 4:11) | Ni nguvu ya kuwasilisha injili ya Yesu kwa watu au kundi kwa njia ambayo wanaweza kuelewa kwa urahisi |
| **Mchngaji-Mwalimu**<br>(Waefeso 4:11) | Ni karama ya kulichunga kundi la Mungu kwa njia ya mafundisho kwa kutumia neno la Mungu |

5. **Haki**

Mwanzo tuliona kwamba Mungu hutupa haki yake tunapo mwamini mwana wake Yesu Kristo. Hicho kinaitwa Huthibitisho. Waumini hupata changamoto ya kuishi katika mapenzi ya Mungu yaliyo sahihi au vibaya. Haki kwa muumini inahusisha kiwango cha Mungu cha utakatifu wake.

Mam, bo mawili muhimu ya haki za Mungu ni kumpenda Mungu kwa moyo wako wote na kumpenda jirani yako kama unavyojipenda wewe (Marko 12:29-31). haki siyo kutokuwa na dhambi kabisa lakini ni badiliko la fikra na mtazamo zinazokubaliana na Mungu (Wafilipi 2:5-8). Kwa mfano ***"tunapaswa kuwa watu wenye huruma kama baba alivyo mwenye huruma"*** *na tuapaswa kuwapenda hata maadui zetu* (Luka 6:36-40). Tunapaswa kuzaa matunda katika haki hii kwa kuwasaidia maskini (2 Wakorintho 9:8-10). Matedo yaliyo katika sehemu ya Mungu ni sehemu ya haki (Waebrania 11:32-33).

Haki ya Waumini inapaswa kuigwa (1 Timotheo 6:11; 2 Timotheo 2:22-23). Maneno ya Mungu ni muhimu sana katika kuielewa haki yake (2 Timotheo 3:16-17) kwa hiyo n vigumu sana kwa waumini wapya kuelewa (Webrania 5:12-14).

Kuitenda kazi ya Mungu (haki) si swala la matendo ya kuwafurahisha watu (Mathayo 6:1). Mafarisayo walitenda haki zao ili waonwe na watu, na walitenda mambo yao ya desturi zao wakitegemea kuwa wako sawa na maandiko (Marko 7:1- 8).

Roho Mtakatifu humshuhudia kila mtu anapokuwa kienda kinyume na haki (Yohana 16:8-10). Kwa wale wasiomjua Mungu Roho Mtakatifu huwaonyesha kuwa kutokuwa na haki kunawafanya wakose ushirika wao mzuri na Mungu. Kwa imani watu huokolewa wasio wakristo (Waefeso 2:8-9), na kurejesha ushirika wao na Mungu. Muumini hushuhudiwa na Roho Mtakatifu kulingana na dhambi zake walizozifanya katika maisha yake na humuelekeza katika kuziungama ili arejeshe ushirika wake na Mungu humthibitishia haki ili awe na ushirika pamoja naye (1 Yohana 1:6-10). Haki kwa muumini ni

muhimu sana na huletwa na Roho Mtakatifu (Warumi 14:16-17). Haki ni tunda la Nuru ya Yesu Kristo ambaye yeye aliishi kwa utakatifu wa Mungu (Waefeso 5:6-10).

Yesu anasema kama tuna kiu na njaa ya haki tutabarikiwa na kupokea (Mathayo 5:6). Haki ni hamu tunayopaswa kuwa nayo kwa sababu humpa heshima yeye aliyefufuka kutoka wafu (Warumi 6:12-13). Wasio na Kristo kiroho wamekufa mpaka pale watakapompokea Yesu kama mwokozi wao (Warumi 6:23). Tusio na Yesu sisi sote ni wafungwa wa dhambi na hivyo basi kama tukiwa waumini na tuwe wafungwa wa haki (Warumi 6:16-19).

Shetani na majeshi yake hujifanya kama watumishi wa haki ili kuwachanganya waumini na kuwadanganya (2 Wakorintho 11:13-15). Jambo walolifanya ni kuwaudhi wale wanaoishi katika haki (Mathayo 5:10; 1 Petro 3:14). Hakika kuitwa mwenye haki katika maisha yetu kabisa ni vita lakini tutavikwa taji kwa hilo (2 Timotheo 4:6-8). Hebu mwache Bwana atende kazi nawe katika vita hii na ujue kuwa utakuwa na amani katika Roho yako (Waebrania 12:11).

**6. Maombi**

Maombi ni mawasiliano na Mungu. Kujua, kufikiri au kujifunza kuhusu maombi bila kutenda haina maana. Ni muhimu sana mtu anapomwomba Mungu na anasubiri kujibiwa. Maombi ni faida kubwa kwa sababu hutufanya tuingie katika chumba cha enzi cha Mungu (Waebrania 4:16).

Kudumu katika maombi ni faida ya wale wanaotafuta mapenzi ya Mungu katika maisha yao. Na hii ilioneshwa katika kanisa la Kwanza (Matendo 2:42). Wakati wanafunzi wa kwanza wa Yesu alipoomba hitaji la maombi (Luka 11:1), Yesu aliwafundisha sala ya Bwana (Luka 11:2-4). Maombi siyo kuwa makini katika kusema ili Mungu atende mapenzi yako unayotaka bali ni kutegemea mapenzi yake (1 Yohana 5:14). Maombi ni silaha yako katika vita ya malaika (Waefeso 6:18).

Neno la Mungu linatuambia kwamba maombi ni kuwa kwa Baba (Waefeso 5:20; Mathayo 6:9; 1 Petro 1:17), katika nguvu ya Roho Mtakatifu (Waefeso 6:18). Na maombi yetu ni lazima yaishie na Jina la Yesu (Yohana 14:13; 15:16).

Maombi lazima yahusishe mambo matano. Moja ni kuungama dhambi zako (Zaburi 66:18-20; Isaya 59:2; Mathayo 6:14; 1 Yohana 1:9). Ni lazima kuchunguza kama kuna kitu kinachoharibu uhusiano wetu na Mungu. Kitu cha pili ni Kusifu (Mathayo 21:16; Luka 19:37; Warumi 14:11; 15:11; Wafeso 1:6, 12, 14; Webrania 13:15). Sifa ni utambuzi na shukrani za Mungu alivyo. Jambo la tatu ni Shukrani, nahii ni utambuzi na kukubaliana kwa kile Mungu alichokitenda (Waefeso 5:20; 1 Wathesalonike 5:18). Jambo la nne ni Maombezi ikiwa na maana ya kuombea wengine (Waefeso 6:18; webrania 7:25), na jambo la tano ni kuomba ikiwa na maana ya kujiombea (Webrania 4:16).

Waweza kuungama dhambi zako wakati wowote bila kitu chochote. Waweza kumshukuru Mungu au kumsifu na kumpelekea mahitaji yako na ya wengine kwa muda wowote unaohitaji.

**7. Kukua**

Kama tuzaliwavyo katika ulimwengu huu kama watoto tunatakiwa kuzaliwa tena tunapomwamini Mungu (Yohana 3:1-16) na kama tunavyokuwa kutoka utoto hadi utu uzima tunapaswa pia kukua katika maisha ya Kikristo. Tunahimizwa kukomaa kama baba yetu wa Mbinguni (Mathayo 5:48), haitoshi katika maisha haya (Wafilipi 3:12-15).

Swala la kwanza katika ukuaji wetu tutake tusitake tutakwenda mbele zake kama “dhabihu iliyo hai na takatifu” ikiwa na maana ya kwamba kuweka maisha yetu katika huduma kwa ajiri yake (Warumi 12:1-2). Baba yetu hutupa mitihani mingi katika maisha ili tupate kukua (Yakobo 1:2-4). Hii ni mitihani ya kutufanya tumtumaini. Pia alilipa kanisa karama mbalimbali za roho ili zitusaidie katika kukomaa (Waefeso 4:11-14).

Kukomaa maana yake ni ***“kuacha kutenda mambo ya kitoto”*** (1 Wakorintho 13:11). Mtu aliye komaa amekua hata katika kutenda kwake (Mathayo 19:21), maongezi (Yakobo 3:1-2) na hata fikra (1 Wakoritho 14:20). Taweza kutathimini ukomavu wetu kwa kuangalia katika maeneo haya. Haya ni mambo ya upuuzi au ya kitoto ubinafsi, maneno machafu na mawazo mabaya yaliyo mengi. Kama mtu huyu ataishi katika haya halafu yakamwendesha na kumtawala basi mtu huyu hawezi kukomaa.

Kuna sifa nyingi zilizotolewa katika maandiko. Ukomavu si ubinafsi (Mathayo 19:21) ni unyenyekevu (Wafilipi 3:12-15, Wakolosai 1:28). Mtu aliyekomaa huomea na wengine (Wakolosai 4:12) na hutumia uhuru wa kiroho kwa manufaa ya wengi si peke yake tu (Yakobo 1:25; Wagalatia 5:1, 13). Ukomavu huonesha kwamba mtu amekua na yuko katika kiwango kizuri cha haki ya Mungu (Waebrania 5:12-14).

Mtu aliyekomaa anamtegemea Mungu (2 Wakorintho 12:9) akielea kwamba kila kitu kizuri kinatoka kwake (Yakobo 1:17). Kiwango kizuri kabisa cha kuelewa ukomavu hutoka katika ushirika wetu na Mungu ambapo tunakuwa hatuna hofu katika maisha yetu (1 Yohana 4:17-19).

8. **Upendo**

Yesu mwenyewe alisema kwamba upendo ni kitu muhimu katika maisha ya Mkristo. Katika injili ya Marko Yesu alinukuu Kumbukumbu la Torati 6:4-5 akasema amri iliyo kuu. Alisema, ***"Ya kwanza, 'Sikia, O Israeli! Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote kwa roho yako yote kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote'"*** (Marko 12:29-30). Na baadaye Yesu alinukuu Mambo ya Walawi 19:18 ana akasema kwamba ni amri ya pili. Alisema, ***"Na ya pili ni hii, 'Mpende jirani yako kama unavyojipenda, hakuna amri nyingine iliyo kuu zaidi ya hizi"*** (Marko 12:31). Tunapaswa kumpeda Yesu kwa sababu alitupenda kwanza (1 Yohana 4:19). Kama kweli tutampenda yeye basi tutaweza kuwapenda hata na wengine (1 Yohana 4:20-21). Pendo tuliloitiwa si pendo la kawaida kama la mwanadamu ambalo anaweza kuwanalo lakini ni zaidi ya pendo hilo litokalo kwa Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:22). Ni pendo la halisi si la hisia japo hisia inaweza kuhusika.

Upendo umeelezwa na neno la Mungu zaidi ya jinsi sisi tunavyoweza kueleza. Sura zinazoonesha ni 1 Wakorintho 13 inaanza kwa kutufundisha umuhimu wake. Haijarishi ni karama gani za kiroho waweza kuwa nazo au kutenda kwa wema twaweza kutoa au kusaidia lakini kama hatutatenda katika upendo ni kazi bure (1 Wakorintho 13:1-3). Mtume Paulo anatupa maelezo kumi na sita ya upendo (13:4-8). Lakini swali zuri la kujiuliza kuhusu upendo ni kwamba je mimi na kama jibu ni hapana jua upendo umekwish pungua katika maisha yako ya kiroho. faida na matendo mengine ya upendo yameelezwa katika Warumi 12:9-21.

"Dunia" ni adui wa upendo wetu ambao Mungu anataka tuwe nao. "Dunia" ina maanisha vitu vile ambavyo shetani huvitumia kutunasa na kututoa katika mapenzi ya Mungu. Tunapopenda vitu vya duniani kamwe hatutaweza kumpenda Mungu (1 Yohana 2:15).

9. **Mateso**

Mateso maana yake ni maumivu. Yaweza kuwa ni ya mwilini au ni ya akili. Katika Yesu Kristo tunaona mtu aliyekabiliana na mateso anayejulikana na watu malipo ya dhambi zetu juu ya msalaba (1 Petro 2:21-24; 4:1; 5:1). Alikuja kwa kusudi hili (Luka 9:22; 22:15) na akateswa mikononi mwa wasio haki (1 Petro 2:21-24). Kwa hiyo kwa kupitia yeye tunajifunza jinsi ya kukabiliana na mateso ya wasio haki (1 Petro 2:21).

Mapema kabisa tulielezwa juu ya kukomaa katika maisha ya Kikristo. Mateso ni njia sehemu moja wapo ya njia inayoweza kutufanya tukomae (1 Petro 5:10). Mungu katika utukufu wake atatuzawadia taji kwa uvumilivu na ushuhuda wa mateso yetu (1 Petro 2:19-20; 2 Wakorintho 4:17). Ushuhuda wetu uko katika kumtumaini Yesu wakati wa mateso haya (1 Petro 4:19).

Ni baraka kuteseka kwa ajili ya haki, kwa sababu katika kufanya yaliyo mema tukijua ya kwamba Kristo ni Bwana wetu kweli (1 Petro 3:14-17; 4:14). Mateso ya wasio haki ni mateso yatokayo kwa wale walio katika madaraka wanapoanza kuwaudhi waumini kwa sababu yeye ni mfuasi wa Kristo. Ni sehemu ambayo kila mkristo ni lazima apitie kwa nia hii ama ile (Wafilipi 1:27-30).

Mtume Paulo ambaye alipata mateso kwa ajili ya Kristo (1 Petro 5:1) ametueleza tufurahi tunapopata mateso kwa ajili ya Yesu (1 Petro 4:13-16). Anateseka kwa sababu ulimwengu haumtaki Yesu na hata wafuasi wake (Yohana 15:18-20; 1 Petro 4:12). Ni mateso ya Yesu ndiyo yaliyolipa gharama za dhambi lakini ya kwetu hayawezi lakini kwa kushiriki mateso yake inatupa ufahamu wa kujua maumivu aliyoyapata kwa ajili yetu. Tusionee aibu mateso haya (1 Petro 4:16) na elewa kwamba Wakristo wengine wanavumilia mateso (1 Petro 5:9) na watauurithi ufalme wa Mungu (2 Wathesalonike 1:5). Hatupaswi kuogopa mateso (Ufunuo 2:10). Petro anatutahadharisha kwamba tunapoteseka kwa sababu ya dhambi tunampa nafasi ibilisi kitu ambacho hakifai katika maisha ya kikristo (1 Petro 4:15). Dhambi yoyote ni thamani ya mateso (Luka 13:1-5).

10. **Nidhamu**

Neno "nidhamu" (PAIDEUO kwa kiyunani) inaonyesha kuwa ni maamuzi tosha ili kupata kile ulichokikusudia. Kwa mfano katika Luka 23:16-22 inaeleza kumpiga mfungwa (Mfungwa huyo alikuwa ni Yesu ambaye Pilato alitaka kumwadilisha halafu amwachie). Inaingiza pia swala la elimu (Matendo 7:22; 22:3). Bwana Yesu anapolitaka kanisa la sasa kuwafundisha wengine inahtajika ifanyike hii kwa upole (2 Timotheo 2:24-26).

Nidhamu ni sawa na mateso kwa sababu yote yanahusisha maumivu. Unapokuwa unateseka inaleta mawazo ya kwamba unaumia, hata adabu inahusisha maumivu katika kufundisha. Mafunzo yetu yanatakiwa yawe yasiyostahili kwa kusudi la kujenga au yawe yanastahli kwa kusudi la kupata kubadili akili zetu au matendo yetu ya dhambi tunapokuwa tumekwenda tofauti (1 Timotheo 1:18-20).

Uadilishaji wa kimungu ni wa kusudi la kujenga sifa kama baba awezavyo kumfundisha mtoto wake (Waefeso 6:4; Waebrania 12:7). Imekusudiwa ili kujenga matendo ya haki yanayostahili maneno yote ya Mungu yanafaa (2 Timotheo 3:16-17). Siyo furaha wakti huo wa kuadilishwa lakini matokeo yake yanathamani (Waebrania 12:11). Gharama iliyolipa dhambi inatakiwa ituonyeshe umuhimu wa kufundishwa (Tito 2:11-12).

Kama baba wa duniani anavyoadilisha kwa hasira Baba wetu wa mbinguni hutuadilisha kwa upendo (Ufunuo 3:19). Anapotuadilisha ni kwa sababu ya upendo wake alionao kwetu sisi kwa hiyo tusijisikie vibaya anapotusahihisha (Waebrania 12:5). Kusud la Mungu kutuadilisha ni kwamba hapendi tuwe watu wa Dunia hii (1 Wakorintho 11:31-32) na kwa hiyo kama waumini ni lazima tukubali maonyo ya Bwana (Waebrania 12:8).

11. **Kujifunza Biblia**
Umuhimu wa kujifunza neno la Mungu hauwezi kuelezeka. Ni kitabu cha mwongozo ambacho Mungu ametupa ili kituongoze kujua uahusiano wake na wetu (1 Wakoritho 2:16). Kusudi zima la kujifunza neno la Mungu liko katika kujua neno la Mungu. Kwa hiyo hatuwezi kueleza kwa urefu zaidi. Tunapaswa kujifunza neno kila siku.

12. **Kuabudu**
Kuabudu kunatakiwa kuwe ni sherehe ya Yesu. Inahusisha kuwa yeye ni nani na amefanya nini. inaonesha sifa zake na thamani yake. Yesu peke yake ndiye aliyeonekana wa kweli na wathamani (Ufunuo 5:1-7) na mbingu zake zitajulikana kwa njia ya kumwabudu (Ufunuo 4:9-11).

Wasioamini hujaribu kumwabudu na kumtumikia aliyeumbwa na wala si aliyeumba (Warumi 1:25). Shetani naye hupenda kuabudiwa (Luka 4:7), lakini Mungu peke yake ndiye tunapaswa kumwabudu (Luka 4:8). Wengine hata huaabudu malaika kitu ambacho ni uumbaji wa Mungu (Wakolosai 2:18). Kama matokeo ya wanaadamu ni kuabudu vitu vilivyoumbwa wamekuwa hawaabudu amri alizozifanya hata katika neno la Mungu hazimo (Marko 7:7). Hata wamekuwa wanaabudu sehemu au majengo ya kuabudia zaidi ya yeye aliye thamani ya kuabudiwa (Yohana 4:20-22).
Ibada ya kweli hutoka kwa Roho Mtakatifu ambaye anafanya kazi katika maisha yetu akituonesha uthamani wa Yesu Kristo (Yohana 4:23-24; Wafilipi 3:2-3) ili kwamba tupate kumsifu. Inafanyika kwa kuitoa miili yetu kuwa ibada (Warumi 12:1-2) na kulikubali neno lake kwa imani (Webrania 11:21).

Kwa kuwa kuna namna mbalimbali za kuabudu sehemu au matendo anayofanya mtu hayajaelezwa katika maandiko. Kumhukumu mtu jinsi anavyoabudu hiyo si halali.

13. **Kufanya Wanafunzi**
Katika utume mkuu Yesu aliwaambia wanafunzi wake ***"nenda na mkawafanye wanafunzi mataifa yote"*** (Mathayo 28:18). Mfuasi ni mwanafuzi wa neno aliyeamua kumfuata Yesu. Mfuasi si aliyeokolewa tu bali ni zaidi hata ya muumini anayejifunza neno la Mungu ili aishi (Yohana 7:17)

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 8, Sehemu 1

1. **Kuhusiana na mtazamo wa maisha ya Mkristo:**
   a. Soma Matendo 16:30-31. Kuna sura gani htokea katika maisha ya mtu anapompekea Yesu Kristo?
   b. Soma 2 Wakorintho 3:18. Ni sura ganikatika maisha ya mtu ni badiliko la mumini kuwa na sura ya Kristo?
   c. Soma 1 Yohana 3:2. Ni sura ipi katika maisha ya Mtu hutokea tunapomuona Kristo alivyo?

2. **Soma Waebrania 11:6. Mumini anatakiwa kuwa na nini ili kumpendeza Mungu?**

3. **Soma 1 Wakorintho 2:14-15. Ni kit gani cha lazima katika kuelewa vitu vya Kiroho?**
   a. Soma Yohana 14:17. Roho Mtakatifu huishi wapi?
   b. Soma Wagalatia 3:2-3. Mambo gani ya lazima ili kuwa mtu wa Kiroho?
   c. Soma Waefeso 4:30 na 1 Wathessalonike 5:19. Dhambi katika maisha ya Mkristo inaweza kusababisha mambo gani mawili?

4. **Soma 1 Yohana 1:5-10. Je mumini anaweza kutenda dhambi, kama ni ndiyo sasa afanye nini?**

5. **Soma 1 Petro 4:10. Kila Mkristo hpokea nini?**
   a. Soma 1 Wakorintho 13:1-3. Kunatakiwa nini ili kwa mt wa thamani katika kuitenda karama ya Kiroho?
   b. Soma 1 Wakorintho 13:8-11. Inatambia nini kitatokea katika karama zingine?
   c. Soma Yohana 13:34-35 na 1 Petro 4:10. Linganisha swala la kupendana na sababu za kwa nini tlipewa karama za Kiroho.

6. **Soma Warumi 6:16-19. Ni mambo gani yanaweza kutfanya tukawa watumwa?**

7. **Kutokana na mambo matano ya muhimu kuhusu maombi:**
   a. Soma 1 Yohana 1:9. Kuna jambo gani limetolewa hapa?
   b. Soma Warumi 14:11 na 15:11. Kuna jambo gani limetolewa katika sura hizi?
   c. Soma 1 Wathesalonike 5:18. Kuna mambo gani yametolewa hapa?
   d. Soma Waefeso 6:18. Kna jambo gani limetolewa hapa?
   e. Soma Waebrania 4:16. Kuna jambo gani limetolewa hapa?

8. **Soma 1 Petro 2:2 na 2 Petro 3:18. Wakristo wanapaswa kfanya nini baada ya wokovu?**

9. **Soma Marko 12:29-31. Ni nini amri kuu mbili za Mungu?**

10. **Soma 1 Petro 2:19-20 na 1 Petro 5:10. Waumini wanapaswa kuvumilia nini?**

11. **Soma Waebrania 12:6-7. Mungu anatfndisha nini?**

12. **Soma 2 Timotheo 3:16-17. Je kusoma neno la Mungu ni jambo muhimu?**

13. **Soma Yohana 4:23-24 na Wafilipi 3:2-3. Tunatakiwa kumwabdu Mungu kwa namna gani?**

14. **Soma Mathayo 28:18-20. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kfanya nini?**

# Sehemu ya 2
# Maisha ya Kikristo ya Kushirikiana (Ecclesiology)

**A. Kufundisha**

Wakati Yesu alipotoa Utume Mkuu sehemu ya ujumbe wake ilikuwa ni ***"kuwafundisha kuyashika yote"*** (Mathayo 28:20). Yesu alikuwa ni mwalimu (Mathayo 4:23; 5:2; 7:29; 9:35; 11:1; 13:54; 21:23; 22:16; 26:55; 28:15; Matendo 1:1). Wanafunzi wake walifanya kama alivyo waagiza wakaanza kufundisha (Matendo 4:2, 18; 5:21, 25, 28, 42; 11:26; 15:1, 35; 18:11, 25; 20:20; 21:21, 28).

Mafundisho hutupa mwelekeo lakini mahubili hutupa kuchangamka (Wakolosai 1:28; 3:16). Haya yote ni muhimu sana katika kanisa.

Mtume Paulo alipomwelekeza Timotheo alimwambie afundishe wengine ili kwamba wapate nao kuwafundisha wengine (1 Timotheo 4:11; 6:2; 2 Timotheo 2:2). Hivyi ndivyo neno la Mungu linavyosambazwa kutoka kizazi hiki hadi kingine japo wengine wamepewa karama za kufundisha (Warumi 12:7), lakini waumini wote wameitwa ili wapate kufundisha (Waebrania 5:12-14).

**B. Ushirika**

Ushirika ulikuwa ni kitu muhimu sana katika kanisa la kwanza (Matendo 2:42). Ina maana ya kushirikiana na mtu mwingine na si kwa vitu vya kimwili tu (Warumi 15:26; 2 Wakorintho 8:4; 9:13; Waebrania 13:16) bali hata vya kiroho (1 Yohana 1:3, 7). Ushirika unahusisha hata Ibada inyoelezwa katika sehemu ya 1 ya sura hii. Kuabudu kwa pamoja ni kukua kwa Ibada ya watu wote.

Ushirika wa kiroho na waumini wengine (2 Wakorintho 6:14) ni muhimu sana kwa sababu inaonyesha ushirika wetu na Kristo (1 Yohana 1:7) na inasababishwa na ushirika wetu mzuri na Roho Mtakatifu (2 Wakorintho 13:14). Umejengwa katika imani (Philimoni 1:6) na huleta umoja katika mwili wa Kristo (Wafilipi 2:1-2). Tumeitwa katika ushirika huu (1 Wakorintho 1:9) ambao kwa kweli hauwezi kukamilika kama tunaenenda gizani (1 Yohana 1:6).

Msingi wa ushirika wetu wetu uko katika Kristo na mara nyingi huitwa umoja unaotukumbusha utu wake na kazi yake (1 Wakorintho 10:16). Umejengwa katika ushirika kwa njia ya mateso yake (Wafilipi 3:10).

Kama waumini tumekuwa katika ushirika baada ya kutokukubaliana kustahilishwa (Wagalatia 2:9) na halafu tunatenda kazi pamoja katika kuieneza injili (Wafilipi 1:5). Ushirika ni njia ambayo upendo na mahusiano hudumishwa.

Tumeona kwanza kabisa umuhimu wa upendo katika maisha ya Kikristo. Agano Jipya linawapa wafuasi habari nyingi kwa kile kinachotokea katika kumpenda jirani yako ambayo ni kumpenda Mungu (1 Yohana 4:20). Kumpenda mwingine kama unayojipenda wewe hii huitwa "Sheria ya Kifalme" (Yakobo 2:8). Kwa kweli ni kitu kiachohitajika sana kwa waumini kwa sababu tunahitajika hata kuwapenda maadui zetu (Luka 6:35). Tunapaswa kuwatendea watu kama sisi tunavyotaka watutendee (Mathayo 7:12).

Kanuni zifuatazo zinahusika na uhusinao na watu wengine. Zinapaswa zianzie kwenye ndoa, halafu familia, kanisa, na hata kwa wale ambao bado hawajaokoka. Kuna kwa nini nyingi zilizo kwenye Agano Jipya mbazo zitatusaidia kujenga uhusiano wetu. Muumini ambaye hajakomaa ataangalia katika kanuni hizi ili aone kama watu wengine wanazitenda lakini yeye hataziangalia kwa upande wake hata kama wengine hawatakuwa wanazitenda. Muumini aliyekomaa atazitenda kwa sababu ni za muhimu sana na wala hatajaribu kuzitumia kwa matakwa yake binafsi.

**Ngoja tuzitafakari kanuni hizi moja baada ya nyingine:**

- Amri ya **kuwapenda** wengine iko katika sura yingi za Agano Jipya (Yohana 13:34, 35; 15:12, 17; Warumi 13:8; 1 Wathesalonike 3:12; 4:9; 2 Wathesalonike 1:3; 1 Petro 1:22; 1 Yohana 3:11, 23; 4:7, 11, 12; 2 Yohana 1:5). Hii ina maana ya kwamba tunapasa kuishi kulingana na kanuni zilizo katika 1 Wakorintho 13:4-8 na Warumi 12:9-21.
- Tambua kwamba sisi ni **viungo** kwa kila mtu (Warumi 12:5; Waefeso 4:25) ina maana kwamba tayari tuna ushirika kwa sababu sisi ni kiungo katika mwili wa Kristo.
- Tunapaswa **kujitoa** kwa wengine (Warumi 12:10) ikiwa na maana ya kwamba tunapaswa kutenda hata kwa wengine hii ni pamoja na kujitoa kwa wenzetu
- Tunapaswa **kuwaheshimu** wengine ikiwa na maana ya kwamba tunapasa kuwathamini wenzetu (Warumi 12:10).

- Tunapaswa **kufikiri sawa** na wengine hii ina maana ya kwamba kuwatambua na wengine kwamba nao pia wamepokea neema ya Mugu sawa na sisi. (Warumi 12:16; 15:5).
- Tunapaswa **kuwakubalia** na wengine kama Kristo livyotukubali (Warumi 15:7) kama viumbe wanaohitaji neema yake.
- Tunapaswa **kuwatahadharisha** wenzetu tunapoona mambo yao ya kiroho yanaelekea hatarini (Warumi 15:14).
- Tunapaswa **kusalimiana** (Warumi 16:16; 1 Wakorintho 16:20; 2 Wakorintho 13:12; 1 Petro 5:14) kwa "busu takatifu." Hi inamaanisha kushukuru uwepo wa mtu kwa njia ya kumtukuza Mungu kwa uthamani wake.
- Tunapaswa **kutumikiana** (Yohana 13:14; Wagalatia 5:13), ambayo imeonyeshwa kwa njia ya kuosha miguu ya wengine.
- Tunatakiwa **kuwatanguliza wengine** kuliko sisi wenyewe (Wafilipi 2:3).
- Tunapaswa **kuchukuliana mizigo** (Wagalatia 6:2) ikiwa na maana ya kuwasaidia wengie ili waweze kupambana na dhambi katik maisha yao.
- Tunapaswa **kuchukuliana** ikiwa na maana ya kuvumiliana (Waefeso 4:2; Wakolosai 3:13).
- Tunapaswa **kukubaliana** ikiwa na maana ya kutambua mahitaji ya wengine kwanza (Waefeso 5:21).
- Tunapaswa **kutiana moyo** ikiwa na maana ya kuwasaidia wegine wanapokuwa wanaonekana kushuka kiroho (Warumi 1:12; 1 Wathesalonike 4:18; 5:11; Waebrania 3:13; 10:25).
- Tunapaswa **tuwe na amani** na wengine (Marko 9:50). Hi ina maanisha kuwa hatupaswi kuwa karaha katika matendo yetu au mawazo yetu.
- Tunapaswa **kuziungama dhambi zetu** kwa wengine (Yakobo 5:16). Hii inaonyesha kwa wale watu tuliokwazana nao ili kuleta amani na uhusiano amabao umehribika.
- Tunpaswa **kuombeana** (Yakobo 5:16).
- Tunapaswa **kusameheana** kama Bwana alivyotusamehe sisi (Wakolosai 3:13).
- Tunapaswa **kuwa wema ikiwa** na maana ya kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu (1 Wathesalonike 5:15).
- Tunapaswa **kuhamasishana kwa upendo na matendo mema** (Waebrania 10:24). Hii inamaana ya kufikiri kwa jinsi gani wengine waweza kusaidiwa kwa kuwahiniza katika kutenda.
- Tunapaswa **kuwa pamoja** (1 Wakorintho 11:33) hii ina maana ya furaha ya umoja na Wakristo wengine.
- Tunapaswa **kuwa wapole**. Hatupaswi kuwa wakali wenye hasira na wala hamu ya kuwaumiza wengine (Wefeso 4:31-32).
- Tunapaswa **kutazamana** (1 Wakorintho 12:25) ina maana ya kwamba sisi sote tuko katika mwili mmoja wa Kristo.
- Tunapaswa **kutambuana** katika huduma (Luka 7:32). Hatutendi kazi kwa matakwa ya wanadamu lakini kuheshimiana ndani ya familia ya Mungu katika kutambuana kihuduma.
- Tunapaswa **kuwa wakarimu** (1 Petro 4:9). Hii ina maana ya kukaribisha wageni katika makusanyiko yetu.
- Tunapaswa kuwa **wanyenyekevu** kwa wenzetu hii itaonyesha mtazamo wa kila mmoja kwa mwenzake. (1 Petro 5:5).
- Tunapaswa kuwa na **ushirika** na wenzetu. (1 Yohana 1:7).
- Tunapaswa **kujengana** (Warumi 14:19; 1 Wathesalonike 5:11) hii inaonyesha kutiana moyo na kuelekezana.

**C. Uinjilisti**

Unjilisti ni uenezaji wa injili ya Yesu Kristo. Inatangaza habari njema kwamba Yesu Kristo ni Mungu (Yohana 1:1) ambaye alifanyika mwanadamu (Yohana 1:14) ili afe kulipa dhambi ya ulimwengu (1 Yohana 2:1-2) na halafu akafufuka (1 Wakorintho 15:1-3) ili kwamba watako mwamini wawe na uzima wa milele (Yohana 3:16). Si habari njema kwamba sisi sote ni wenye dhambi (Warumi 3:23). Habari njema ni kwamba deni letu limelipwa kwa sababu ya dhambi zetu (Warumi 6:23) zimelipwa (Wagalatia 3:13).

Kanisa, lote linatakiwa litamani kuwaletea watu habari njema. Hatupaswi kuficha taa na kweli tuliyokwisha kupewa (Mathayo 5:14; Warumi 1:16).

Mungu ametupa njia ya uhuru katika kutangaza habari njema. Yaweza kufanyika mtu kwa mtu (Matendo 8) au katika kundi (Matendo 2). Kitu cha mhimu ni kwamba kanisa lazima kusambaza neno la Mungu likitumia mwaliko wake wa kuingia katika uzima wa milele. Na chombo cha muhimu alichopewa mwanadamu kwa ajili ya uinjilisti ni upendo kwa wengine (Yohana 13:34-35).

**D. Huduma**

Huduma ni ile kutambua hali ya Kiroho na kimwili inayohitajika na watu na halafu unatafuta kuwasaidia (Matendo 11:29; 2 Wakorintho 8:3-5). Ni kazi ya kuwa balozi wa Yesu katika kuubeba ujumbe wa Mungu kwa waliopotea na ulimwengu unaoangamia (2 Wakorintho 5:18-21). Kama Mtu atamtambua na kumwelewa Mungu hivyo mtu anaweza kupona kutoka katika ulimwengu huu. Kwa hiyo huduma inabeba ujumbe wa uhuru (1 Timotheo 4:4-6). Sisi tulioamini tumewekwa huru (Wagalatia 5:1) na hivyo tunatumia uhuru huu katika kuwatumikia wengine (Wagalatia 5:13).

Yesu menyewe alitupa mfano ili tuufuate (Mathayo 20:28), kwa hiyo watumishi humfuata kiongozi (Yohana 12:24-26). Wakristo watumishi, na siyo nafasi ya mtu kanisani iwe ndiyo alama ya kuwa mtu wa Kiroho (Mathayo 20:26-28; 23:10-12). Kama waumini hatuna budi ya kukumbuka huruma aliyoionesha Mungu kwetu kwa njia ya wokovu ili tusiwe wajinga au kukata moyo (2 Wakorintho 4:1-2). Mugu ameahidi kwamba hatasahau tendo letu hata moja katika huduma na wengine (Waebrania 6:10-12).

Nafasi za kutumika zimetolewa na Bwana (Matendo 20:24; 1 Wakorintho 12:4-6). Wakristo hawana budi ya kuzikubali nafasi hizi alizotupatia Mungu na karama katika kutumikia wengine. Huduma ni kitu cha muhimu sana katika maisha ya Mkristo (1 Petro 4:10-11) tunapaswa kushiriki sana (Warumi 12:7), unatakiwa kuwa mwaangalifu sana ili usiharibu huduma yako na hata Kristo (2 Wakorintho 6:3).

Huduma lazima zijisifunze kutenda pamoja. Uchaguzi wa kwanza wa mashemasi katika kanisa la kwanza haukufanyika na wao tu bali walihusisha kusanyiko lote lichague watu watakaowaangalia wajane (Matendo 6:1-6). Huduma tofauti zinapofanya kazi pamoja zinasaidia katika kutosheleza mahitaji ya watu.

Bwana ameweka huduma za uongozi ambazo zilikusudiwa kujenga na kuimarisha watu wengine ili wawe watumishi. Mtume Paulo aliandika,

> ***Naye alitoa wengine kuwa Mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu. Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo.*** (Waefeso 4:11-13)

Majukumu ya kiongozi wa kanisa ni kuwaandaa waumini kiroho, kimwili na hata kifikra ili watumike kwa watu wengine ili kwamba na hata wengine waweze kuhubiriwa na wakomae kwa njia ya uhusiano binafsi na Bwana Yesu Kristo. Huduma itendwayo katika upendo inagusa sana kwani ndicho chombo pekee cha uinjilisti kilichopewa kwa kanisa (Yohana 13:1-35).

**E. Umoja**

Makanisa ya watu ni lazima yawe na umoja katika mwili wa Yesu Kristo (Waefeso 4:13). Yesu Kristo, Usiku kabla ya kwenda msalabani aliomba ili wanafunzi wake wawe na umoja. alisema,

> ***Na si hao tu niwaombeao lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lako. Wote wawe a umoja kama wewe baba ulivyo ndani yangu na mimi ndani yako na hao wawe ndani yetu ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao ili wawe na umoja kama sisi tulivyo na umoja, mimi ndani yao nawe ndani yangu ili wawe wamekamilika katika umoja ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi.*** (Yohana 17:20-23)

Kwa kuwa waumini wote wanakuwa na Roho Mtakatifu mara tu anapompokea Yesu, umoja hujengwa kwa ukweli kwamba kuna Roho mmoja tu (Waefeso 4:4) na sisi sote Roho huishi ndani yetu (tazama katika ile sehemu ya kutawaliwa na Roho Mtakatifu). Mtume Paulo alitufundisha umoja huu wa Roho Mtakatifu inahifadhiwa katika kutembea kama tulivyoitwa (Waefeso 4:1-3). Hii ina maana ya kwamba kutembea kwetu kuko katika neema na kumejengewa katika imani (Waefeso 2:8-9). Kwa kuwa sehemu yetu katika Kristo tunaunganishwa kwa njia ya wokovu tunapaswa kutafuta umoja ulio katika upendo ili

kwamba wale wote ambao hawajaokolea wajue ya kwamba sisi ni wanafunzi wa Yesu Kristo (Yohana 13:34-35).

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 8, Sehemu ya 2

1. **Soma 2 Timotheo 2:2. Ni kit gani muhimu katika kanisa?**

2. **Soma 1 Timotheo 6:3. Mafundisho sahihi tayatahmini vipi?**

3. **Soma Waebrania 5:12. Wamini wa mda mrefu wanapaswa kfanya nini?**

4. **Soma 1 Yohana 1:3 na 7. Kitu gani kinachoonekana nanichamuhimu katika kanisa?**

5. **Kna kanni gani za ushirika zimefundishwa katika sura hizi?**
   a. Yohana 13:34-35
   b. Warumi 12:10
   c. Warumi 15:7
   d. Wagalatia 5:13
   e. Wafilipi 2:3
   f. Wagalatia 6:2
   g. Waebrania 3:13 na 10:25
   h. Wakolosai 3:13
   i. Waefeso 4:31-32
   j. 1 Petro 4:9
   k Warumi 14:19

6. **Soma Mathayo 5:14 na Warumi 1:16. Kanisa linapaswa kufanya nini?**

7. **Soma Wagalatia 5:1 na 5:13. Kwa sababu gani tmewekwa huru?**

8. **Soma Waefeso 4:13. Lipi linatakiwa kuwa lengo la kila kanisa?**

9. **Soma Yohana 17:20-23. Ni nini shauku ya Kristo kwa wafuasi wake?**

# Sura ya 9

# Utendaji

# Utangulizi

Sehemu hii itaonesha njia za utendaji katika kuandaa somo kwenye Biblia. Hii imetumika katika kanuni ambazo walimu wengi wamekuwa wakizitumia katika mafundisho yao mazuri ya neno la Mungu. Japo njia hizi zaweza kutofautiana lakini kanuni za kufasiri katika Sura ya 4 ni lazima zifuatwe.

Kwanza fikiri umuhimu wa maadili yanayofaa tunapoandaa somo hili na elewa kwamba maadili yasichukue nafasi huduma ya mafundisho ya Roho Mtakatifu. Nafsi ya Roho Mtakatifu ndiyo inayotuongoza "**katika kweli**" (Yohana 16:13). Njia za wanadamu hazina umuhimu sana na wala zisichukue nafasi.

Tunapaswa kutembea katika Imani na haijalishi ni kwa kiasi gani twaweza kuwa na maarifa katika neno la Mungu (Wakolosai 2:6). Ukomavu wa kiroho hauji kwa matendo ya mwili lakini ni kwa imani (Wagalatia 3:2-5). Shetani anaweza kutulaghai na kuzitumia njia zetu zaidi ya kumtumaini Roho Mtakatifu (Yohana 5:39-47). Maarifa bila upendo wa Kikristo ni bure ambayo ni sifa ya kutokomaa (1 Wakorintho 8:1).

Haijalishi tutatendaje katika maisha yetu ya Kikristo lakini twapaswa kuanza kwa maombi na kuungama dhambi zetu (1 Wakorintho 11:31; Methali 28:13; 1 Yohana 1:9), na tuendelea katika kuomba. Tunapaswa kuomba ili tuzame katika kuelewana, utayari wa kile tunachosoma kabla ya kuanza somo lolote.

# Sehemu ya 1
# Kukielewa Kitabu

**A. Utangulizi**

Baada ya kuwa umechagua kitabu cha kusoma tunapaswa kukisoma mara kwa mara kwa kukirudia kama gazeti au kitabu cha kawaida. Hii inatusaidia kujua yaliyomo katika kitabu hicho na hayajawekwa kujibu maswali ya ndani ya kitheologia.

Kukisoma kitabu chote kwa haraka kinatusaidia kujua mambo muhimu yaliyomo. Tukumbuke kwamba tunapaswa kuyatafasitri yaliyomo kimaandiko kwa kufikiri yaliyo rahisi na ya kawaida kabisa na yale ya ndani kabisa. Kwa kuendelea na kitabu mstari kwa mstari ni njia pekee ya kuelewa mambo ya ndani na ya juu juu katika kitabu hicho.

Pia tunapaswa kuelewa historia na jiografia kwa kuunganisha na vitabu vingine katika Biblia. Somo hili litaangalia kitabu cha 1 Wathesalonike. Kwa kuwasaidia wanafunzi tumetoa historia fupi ya mji wa Thesalonike. Historia hii ni lazima ipatikane kutoka katika vitabu vya ziadi vya Biblia. Vitabu vinavyoitwa kamusi ya Biblia na Utangulizi wa Biblia ni vitabu vya msaada sana.

**B. Jiografia na Historia ya Thesalonike**

Thessalonike ilikuwa ni bandari iliyokuwa sehemu ya juu ya ghuba ya Therma katika upande wa kona ya kaskazini magharibi ya bahari ya Aegean. Ilikuwa jimbo la Rumi ya Makedonia na ilikuwa inajulikana kwa sababu ya mvua zake nyingi na hata eneo la malisho ya kondoo ambapo kondoo wakubwa na makundi makubwa yalikuwa yakichunga. Ilikuwa ni jiji kubwa na la kupendeza nyakati hizo.

Thessalonike iliundwa miaka ya 315 K.K. na Cassander, mwana wa Antipater, muda mfupi baada ya kifo cha Alexander mkuu miaka ya 323 K.K. Baaada ya kifo cha Alexander kulikwa na mpigano makubwa mno. Antipater alikuwa ni mfalme katika jamaa ya mfalme na ndiye aliuita mji huu baada ya mwana wake mke wa Cassander, Mthessalonike, ambaye pia alikuwa ndugu wa karibu wa Alexander mkuu.

Thessalonike ulikuwa ni mji wa kibiashara ulikuwa na wayunani wengi lakini walioathiriwa na jamii ya kiyahudi. Leo hii ni mji wa kiyunani wa Salonika.

**C. Historia ya Kanisa: Matendo 17:1-9**

Kanisa lilianzishwa wakati wa safari ya pili ya kimissionari ya Paulo kama matokea ya maono yake ya Makedonia (Matendo 16:9). Paulo alikuwa akisaidiwa na Sila (ambalo lilikuwa jina lake la kiebrania na, Silvanus lilikuwa jina lake la kirumi), Timotheo, na Luka. Walikuwa wakisafiri katika njia inayounganisha mshariki na magaharibi. Walifika Thessalonicke baada ya kutembelea miji ya Philippi, Amfipoli, na Apolonia (Matendo 17:1).

Paulo alifundisha katika sinagogi kwa muda wa sabato tatu (Matendo 17:2) kwa ujumbe wa kwamba Yesu Kristo amelitimiza Agano la Kale kwa unabii na yeye alikuwa akimzungumzia Masihi (Matendo17:3). Wengi waliookolewa kwa ujumbe huu (Matendo 17:4).

Paulo alikaa huko kwa mda mrefu akiwafundisha waongofu walioamini. Kama matokeo wayahudi wasioamini wakaingiwa na wivu wakakusanyana na wakawaendea (Matendo 17:5). Kundi hili lilienda kwenye nyumba ya Yasoni ili kumleta Paulo ambaye hakuwa pale (Matendo 17:6), kwa hiyo wakamkokota Yasoni wakampeleka mbele ya sheria ya uhamiaji na wakapotosha maneno ya Paulo kuhusu Yesu (Matendo 17:7). Upinzani ukawa mkubwa na Paulo na kundi lake wakaondokoka kuelekea Beroya (Matendo 17:8-10).

**D. Muda na Sababu ya Kuandikwa**

Safari ya pili ya kimisionari ilianza mwaka 49 B.K. baada ya Paulo kuwa amefundisha Antiokia. Baada ya kuondoka Thessalonike Paulo alifundisha Beroya na baadaye Athens kabla ya kwenda Korintho ambako alikaa miezi 18 (Matnedo 18:11). Paulo alimrudisha Timoteo tena huko Thesalonike kwa ajili ya kanisa jipya llokuwa limeanzishwa ili alete taarifa (1 Wathesalonike 3:2). Taarifa yaTimotheo ilikuwa nzuri na matokeo yake ilikuwa ni kitabu hiki. Hii inaonesha kwamba Wathessalonike kiliandiwa miaka ya 50 B.K. kilikuwa ni kitabu cha pili cha kuandikwa na Paulo (cha kwanza ni Wagalatia).

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 9, Sehemu ya 1

**Soma habari zilizotolewa katika Suya ya 3 kuhusu <u>2 Wathessalonike</u>**

## Sehemu ya 2
## Kutengeneza Muhitasari wa Kitabu

Tunapokuwa tayari kuanza kuchukua mtazamo wa karibu wa kitabu, tunatakiwa kuanza kutengeneza muhitasari. Tunachotakiwa kufanya ni kuanza na picha kubwa na halafu unafuatia na ndogo ndogo. Ukweli uko wazi kadri tunavyosoma na kuona picha ndicyo tunavyoelewa. Neno la Mungu liko sawa. Picha kubwa ni Yesu Kristo mwenyewe. Neno lililoandikwa ni ufunuo wa neno hai (Yohana 5:39-47). Kama tutachunguza kwa undani tutaona mambo ya Yesu Kristo ndani.

Tusichanganyikiwe pale tunaposhindwa kuona picha kubwa. Kama tutalazimisha basi tutakuwa tumekosea na lazima tutakwenda tofauti katika kuitafasiri Biblia kwa kile ilichokuwa imekikusudia (Mathayo 23:24).

Unapotengeneza Mhitasari wa kitabu, jambo la kwanza kufikiri ni jinsi gani kitabu kimegawanywa. Vitabu vingi vya Biblia vimepangwa katika mpangilio wa Sura. Na tafasiri za Biblia zinafuata sheria hii ya sura na mistari ya Biblia. Kwa kawaida tafasiri huzingatia mstari wa kwanza katika sura kwa kuukoleza. Soma tafasiri ya watafasiri unayoitumia ili uone ni kwa jinsi gani mtafasiri ameizungumzia sura hiyo. Na kama hautaiona basi endelea hadi pale unapoona kwamba sura imeanza kuleta maana kwako.

Kwa mfano, mgawanyo wa sura ya 1 Wathessalonike ni kama ifuatavyo:

1. 1:1
2. 1:2-10
3. 2:1-12
4. 2:13-16
5. 2:17-20
6. 3:1-10
7. 3:11-13
8. 4:1-8
9. 4:9-12
10. 4: 13-18
11. 5:1-11
12. 5:12-22
13. 5:23-28

Halafu ipe kila sura kichwa cha habari. Utakapokisoma kitabu kwa undani kabisa muhitasari wako utabadilika kadri unavyosoma na kuelewa yaliyomo. Lakini uelewe kwamba hatupaswi kuishi katika vichwa vya habari ulivyovipata. Kusudi letu si kuwa wabunifu wa vitu vingine kwa hiyo uwe rahisi kabisa ili maandiko yakuongoze.

Mhitasari wa 1 Wathessalonke kwa mfano utakuwa hivyi:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | 1:1 | Salaamu |
| 2. | 1:2-10 | Shurani ya mfano wao |
| 3. | 2:1-12 | Nafasi ya Paulo |
| 4. | 2:13-16 | Shukrani ya kwa juhudi zao |
| 5. | 2:17-20 | Shauku ya Paulo ya kuwaona |
| 6. | 3:1-10 | Shauku ya Paulo ya kujifunza juu ya maendeleo yao |
| 7. | 3:11-13 | Tumaini la Paulo kwa mambo yao ya Kiroho Paul's |
| 8. | 4:1-8 | Shauku ya Paulo kwa utakaso wao |
| 9. | 4:9-12 | Maneno ya Paulo juu ya upendo wao |
| 10. | 4:13-18 | Kufa katika Kristo |
| 11. | 5:1-11 | Siku ya Bwana |
| 12. | 5:12-22 | Kusihiana |
| 13. | 5:23-28 | Kuondoka |

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 9, Sehemu ya 2

**Weka maelezo ya kitabu cha 2 Wathesalonike kutokana na migawanyo ya mistari ifuatayo:**

1. **1:1-2**

2. **1:3-12**

**3. 2:1-17**

a. 2:1-12
b. 2:13-15
c. 2:16-17

**4. 3:1-15**

a. 3:1-5
b. 3:6-13
c. 3:14-15

# Sehemu ya 3
# Kupunguza Uelewa Wako katika Kujifunza

Hatua hii inaanza kwa kutambua sura za watu. Kama mfano tutaangalia misitari mbili za sura ya kwanza ya 1 Wathessalonike.

**A. Salamu–1 Wathesalonike 1:1**

1:1 ***Pauol na Silvanus na Timotheo kwa kanisa la Thesalonike kwa Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo: Neema na iwe kwenu na amani.***

Mstari huu unajibu maswali ambayo tungepaswa kujiuliza. Paulo, Silvanus na Timotheo wanahusishwa katika barua hii na kwa hiyo tumekwisha jibu swali la "nani" anaandika na wahusika wa barua hii ni kanisa lililoko Thesalonike kwa hiyo tumekwisha jibu la nani anayeadikiwa.

Na uelewe kwamba Paulo analionesha kanisa kwamba liko kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Na hivyo inaonesha ukaribu uliopo kati ya Mungu na waathirika.

Paulo pia anakuwa na maombi kwa ajili yao. Anasema kwamba neema na amani iwe juu yao.

Ili itusaidie sisi namna ya kuanza elewa kwamba kuna kanuni tatu zilizooneshwa na kufundishwa katika mstari wa 1.

**Kanuni #1:** Watu wakubwa wa Mungu hupenda watu wakue katika ushirika wao na Mungu.
**Kanuni #2:** Watu wakubwa wa Mungu hutamani kushirikiana na wengine ili wapate kuwasaidia kukua.
**Kanuni #3:** Watu wakubwa wa Mungu hushiriki walichonacho na wengine.

Katika kubana upeo wa uelewa wako tutaangalia tena mstari wa pili unaotengeneza aya ya pili.

**B. Shukrani kwa Mfano Wao–1 Wathesalonike 1:2-10**
**1. Kwanza soma aya hii ya pili mara kadha wa kadha:**

1:2 ***Twamshukuru Mungu kwa ajili yenu siku zote, tukiwataja katika maombi yetu;***

1:3 ***wala hatuachi kuikumbuka kazi yenu ya imani na taabu yenu ya upendo na saburi yenu ya tumaini lililoko katika Bwana wetu Yesu Kristo mbele za Mungu Baba yetu,***

1:4 ***ndugu mnaopendwa na Mungu twajua uteule wenu;***

1:5 ***ya kwamba injli yetu haikuwafikia katika maneno tu bali na katika nguvu na katika Roho Mtakatifu na uthibitifu mwingi kama vile mnavyojua jinsi zilivyokuwa tabia zetu kwenu kwa ajili yenu.***

1:6 ***Nanyi mkawa wafuasia wetu na wa Bwana mkiisha kulipokea neno katika dhiki nyingi pamoja na furaha ya Roho Mtakatifu,***

1:7 ***hata mkawa kielezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia na Akaya.***

1:8 ***Maana kutoka kwenu neno la Mungu limevuma si katika Makedonia na Akaya tu bali kila mahali imani yenu mliyonayo kwa Mugu imeenea hata hatuna haja sisi kunena neno lolote.***

1:9 ***Kwa kuwa wao wenyewe wanatangaza habari zenu jinsi tulivyokuwa kuingia kwetu kwenu na jinsi mlivyomgeukia Mungu kuziacha sanamu ili kumtumikia Mungu aliye hai na wa kweli,***

1:10 ***na kumngojea wanae kutoka mbinguni ambaye alimfufua katika wafu nye ni Yesu mwenye kutuokoa na ghadhabu itakayokuja.***

2. **Sasa toa machache kwa kila mstari:**

1:2 = Shukrani katika Maombi
***Twamshukuru Mungu kila siku kwa ajili yenu tukiwataja katika maombi yetu;***

1:3 = Kwa nini Walishukuru - Imani, Tumaini na Upendo
***"Wala hatuachi kuikumbuka kazi yenu ya imani na taabu yenu ya upendo na saburi yenu ya tumaini lililoko katika Bwana wetu Yesu Kristo mbele za Mungu Baba,***

1:4 = Wakiishi katika Wito Wao Walioitiwa na Mungu
***kwa maana ndugu mlioitwa na mliopendwa na Mungu twajua uteule wenu;***

1:5 = Mizizi Yao katika Injili
***ya kwamba injili yetu haikuwafikia katika maneno tu bali na katika nguvu na katika Roho Mtakatifu na uthibitifu mwingi kama vile mnavyojua jinsi zilivyokuwa tabia zetu kwenu kwa ajili yenu.***

1:6 = Tofauti Ambayo Injili Ilifanya
***Nanyi mkawa wafuasia wetu na wa Bwana mkiisha kulipokea neno katika dhiki nyingi pamoja na fuarha ya Roho Mtakatifu,***

1:7 = Matokeo ya Kwanza ya Tofauti ya Injili ni Kuwa Mfano
***hata mkawa kielezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia na Akaya.***

1:8 = Matokeo ya Pili ya Tofauti ya Injili ni Mafanikio
***Maana kutoka kwenu neno la Mungu limevuma si katika Makedonia na Akaya tu na kila mahali imani yenu mliyonayo kwa Mungu imeenea hata hatuna haja sisi kunena neno lolote.***

1:9 = Msingi wa Tofauti Ulikuwa ni Kugeuka na Kuacha Sanamu
***Kwa kuwa wao wenyewe wanatangaza habari zenu jinsi tulivyokuwa kuingia kwetu kwenu na jinsi mloivyomgeukia Mungu mkaziache sanamu lili kumtumikia Mungu aliye hai wa kweli,***

1:10 = Matokeo ya Tofauti Hii ni Maisha ya Mbinguni
***na kumngojea mwanae kutoka mbinguni ambaye alimfufua katika wafu naye ni Yesu mwenye kutuokoa na ghadhabu itakayokuja.***

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 9, Sehemu ya 3

1. **Soma 2 Wathessalonike 1:1-12 mara kadhaa.**

2. **Toa kichwa cha habari kwa kila mstari.**

# <u>Sehemu ya 4</u>
# Kuangalia Mahusiano

**A. Zingatia vielelezo vya somo vinavyojitokeza:**
Tunapoangalia katika kichwa cha habari cha kila mstari katika aya ya pili ya 1 Wathesalonike, tunaanza kuona vielelezo vinavyojitokeza.

1:2 Shukrani katika Maombi

1:3 Kwa Nini Walishukuru - Imani, Tumaini na Upendo

1:4 Wakiishi katika Wito Wao Walioitiwa na Mungu

1:5 Mizizi Yao katika Injili

1:6 Tofauti Ambayo Injili Ilifanya

1:7 Matokeo ya Kwanza ya Tofauti ya Injili Ni Kuwa Mfano

1:8 Matoke ya Pili ya Tofauti ya Injili ni Mafanikio

1:9 Msingi wa Tofauti Ulikuwa ni Kugeuka na Kuacha Sanamu

1:10 Matokeo ya Tofauti Hii ni Maisha ya Mbinguni

Ni rahisi kuona vielelezo vya shukrani na tofauti ambavyo injili ilifanya katika maisha yao.

**B. Tazama kwa ukaribu huku ukichukua unayoyaona katika mistari:**

1:2 = Shukrani katika Maombi
***twamshukuru Mungu kila siku kwa ajili yenu tukiwataja katika maombi yetu;***

Katika msitari huu Paulo anatueleza alichofanya (alitoa shukrani) na aliitoaje (kwa kuomba).

1:3 = Kwa Nini Walishukuru - Imani, Tumaini na Upendo
***wala hatuachi kuikumbuka kazi yenu ya imani na taabu yenu ya upendo na saburi yenu ya tumaini lililoko katika Bwana wetu Yesu Kristo mbele za Mungu Baba,***

Mstari huu unatupa sababu tatu ni kwa nini alitoa shukrani kwa ajili yao:
1. Kazi yao ya Imani,
2. Kazi yao ya Upendo na,
3. Uthabiti wao wa tumaini.

Imani yao tumaini na upendo uko katika vitu vitatu:
1. Uhusiano wao na Yesu Kristo,
2. Ukaribu au undani wao na Baba,
3. Wito wao kutoka kwa Mungu (Mstari wa 4).

1:4 = Wakiishi Katika Wito Wao Walioitiwa na Mungu
***kwa maana ndugu mlioitwa na mliopendwa na Mungu twajua uteule wenu;***

1:5 = Mizizi Yao katika Injili
***ya kwaba injli yetu haikuwafikia katika maneno tu bali na katika nguvu na katika Roho Mtakatifu na uthibitifu mwingi kama vile mnavyojua jinsi zilivyokuwa tabia zetu kwenu kwa ajili yenu.***

Waliikubali injili iliyokuja kwao:
1. katika maneno,
2. katika nguvu,
3. katika Roho Mtakatifu,
4. kwa mwitikio mkubwa na
5. kutoka kwa watu waliofaa.

1:6 = Tofauti Ambayo Injili Ilifanya
***Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana mkiisha kulipokea neno katika dhiki nyingi pamoja na furaha ya Roho Mtakatifu,***

Injili ilileta tofauti. Walioisikia walikomaa na wakawa kama Paulo wafuasi wake na hata Bwana. Waliipokea injili kwa furaha katika kipindi kizito cha mateso.

1:7 = Matokeo ya Kwanza ya Tofauti ya Injili ni Kuwa Mfano
***hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia na Akaya.***

Matokeao ya kwanza injli iliyofanya ilikuwa ni kuwafanya Wathesalonike wawe mfano kwa makanisa jirani.

1:8 = Matoke ya Pili ya Tofauti ya Injili ni Mafanikio
***Maana kutoka kwenu neno la Mungu limevuma si katika Makedonia na Akaya tu, na kila mahali imani yenu mliyonayo kwa Mungu imeenea hata hatuna haja sisi kunena neno lolote.***

Matokeo ya pili yalikuwa kwamba imani yao ilienea hata zaidi ya jirani zao.

1:9 = Msingi wa Tofauti Ulikuwa ni Kugeuka na Kuacha Sanamu

***Kwa kuwa wao wenyewe wanatangaza habari zenu jinsi tulivyokuwa kuingia kwetu kwenu na jinsi mlivyomgeukia Mungu na kuziacha sanamu ili kumtumikia Mungu aliye hai wa kweli,***

Msingi wa kwanza wa tofauti uliofanywa na injili ilikuwa ni kuwafanya waache kuabudu sanamu.

1:10 = Matokeo ya Tofauti Hii ni Maisha ya Mbinguni

***na kumngojea wanae kutoka mbinguni ambaye alimfufua katika wafu naye ni Yesu mwenyewe kutuokoa na ghadhabu itakayokuja.***

Msingi wa pili wa tofauti uliojengwa Wathesalonike walikuwa wakimsubiri Bwana hadi atakaporudi.

Ni Bwana ambaye (1) alifufuka toka wafu (2) atauokoa na ghadhabu inayokuja.

**C. Muhtasari wenyewe utakuwa kama hivi:**

1. **Shukrani - Mstari wa 2**

2. **Kwa nini Shukrani - Mstari Wa 3-4**
   a. Kazi ya Imani na
   b. Kazi ya Upendo na
   c. Uthabiti wa Tumaini
      1) katika Bwana Wetu Yesu Kristo
      2) kwa Uwepo wa Mungu na Baba Yetu
      3) Wito Wao wa Ki-Mungu

3. **Kuikubali Kwao Injili - Mstari Wa 5**
   a. katika Neno
   b. katika Nguvu
   c. katika Roho Mtakatifu
   d. kwa Mwitikio Wote
   e. oka kwa Watu Wanaofaa

4. **Tofauti Mbili Injili Ilizoleta - Mstari Wa 6**
   a. Iliwafananisha na Kundi la Paulo na Bwana.
   b. Ilileta Furaha ya Kiroho Kipindi cha Mateso

5. **Matokeo Mawili ya Tofauti Hizi - Mstari Wa 7-8**
   a. Walifanyika Mfano wa Makanisa Jirani
   b. Walikuwa ni Mfano katika Kuisambaza Imai Yao

6. **Misingi Miwili ya Tofauti Hizi - Mstari 9-10**
   a. Waliacha Kuabudu Mizimu

b. Wakawa na Tumaini la Kumsubiri Bwana
    1) Aliyefufuka toka Wafu
    2) Atakayetuokoa na Ghadhabu Inayokuja

Tunaona kwamba katika sura hii Paulo anatoa mapendekezo makubwa kwa kanisa lililoko Thesalonike. Kwa kweli wanaitwa kuwa ni kanisa “mfano” au “msingi”. Kwa hiyo kama kanisa la leo twaweza kujifunza kutoka katika kanisa hili.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 9, Sehemu ya 4

1. **Angalia katika vichwa vya habari vyako uone uwiano wa jambo la somo lako.**

2. **Angalia kwa makini mistari hiyo huku ukinuku maoni yako.**

3. **Tengeneza maelezo ya moja kwa moja kutoka katika 2 Wathesalonike 1:1-12.**

## Sehemu ya 5
# Kuyatambua Yaliyomo ndani Kabisa

Sasa twaweza kuyatambua mambo ya ndani kwa kulinganisha maandiko kwa maandiko. Njia rahisi ya kutumia ni kwa kuangalia rejea zinazoorodhesha maeneo yote ambayo twaweza kupata neno tunalolihitaji. Kwa njia hii twaweza kufika sehemu katika Biblia yenye maana sawa na neno tunalolitafuta au kufikiri.

Kazi ya rejea tofauti tofauti kwa njia tofauti tofauti. Kuelewa ni kwa jinsi gani hii inafanya kazi hivi ni vizuri sana katika kuelewa kwa undani zaidi. Rejea mbili zinazoeleweka na ni msaada sana ni Englishman's Hebrew na Chaldee. Hizi zinapanga maneno kwa lugha ya kiebrania na kiyunani. Kwa hiyo kwa maneno yote muhimu kama KALOS, "wema," zaweza kuonekana vizuri katika vichwa vya habari tofauti tofauti.

Na rejea ya kawaida kabisa na yenye nguvu kabisa ni ya kiingereza imbayo imepanga kila neno na mfano wake. Kwa mfano, kila neno lililo na kiingereza "wema" limeorodheshwa. Hata hivyo kuna maneno tofauti ya Kiebrania na Kiyunani yaliyotafasiriwa kwa kiingereza kama Wema na kila moja kwa ujumla yanamaanisha kweli ni wema japo mengine yanajaribu kujificha.

Katika kujifunza kwetu Biblia ni vizuri kufahamu ni neno gani linamaanisha "wema" na limetumika. Kwa kusudi hili uimara umesimama sana hasa katika maneno ya Kiyunani na Kiebrania katika Biblia. Kwa mfano kwa kila aya iliyo na neno la kiingereza "wema" ni idadi ya maneno yanayo shabiana na maneno ya Kiyunani na kiebrania yametumika kama mfano (Neno pekee la kiyunani na kiebrania linalowakilisha rejea hizi). Linaonekana kitu kama hiki:

WEMA:
Mathayo 3:10 inayoonyesha matunda mabaya (2570)
Mathayo 5:45 jua kuwaangazia wabaya na wema (18)

Neno "wema" lililotumika katika Mathayo 3:10 (rejea #2570), ne neno la Kiyunani KALOS, linalomanisha "wema wa asili," lkiwa upande mwingine neno wema lililotumika katika Mathayo 5:45 (rejea #18), ni neno la kiyunani AGATHOS, linalomaanisha kwa Wayunani kwamba "inayo kuwa mema".

Maelezo kamili ya maneno ya Kiyunani na Kiebrania yako katika kitabu kiitwacho "Lexicons," ambaho ni kamusi ya maana ya maneno. Utumiaji wa vitabu hivi vitakusaidia sana katika kujifunza Biblia.

Sana tazama neno, "mfano" lililo katika 1 Wathesalonike 1:6. Tafasiri zingine katika kiingereza hutafasiri kama "MIMETES" yaani "mfuasi" (King James Version) badala ya "mfano". Neno la kiyunani lina maana ya kujifananisha au mimi, na limetumika mara sita katika Agano Jipya. linaonekana katika aya zifuatazo:

***1 Wakorintho 4:16 "Basi nawasihi mnifuate mimi."***

***1 Wakointho 11:1 "Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo."***

***Waefeso 5:1 "Hivyo mfuateni Mungu kama watoto wanaopendwa;"***

***1 Wathesalonike 1:6 "Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana mkiisha kulipokea neno katika dhiki nyingi pamoja na furaha ya Roho Mtakatifu,"***

***1 Wathesalonike 2:14 "Maana ninyi ndugu mlikuwa wafuasi wa makanisa ya Mungu yaliyo katika uyahudi katika Kristo Yesu kwa kuwa mlipata, mateso yaleyale kwa watu wa taifa lenu wenyewe waliyoyapata hao kwa Wayahudi,"***

***Waebrania 6:12 "Ili msiwe wavivu bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu."***

Kwa kujifunza sura chache ambazo zina neno "mfano" twaweza sasa kuelewa mambo ya ndani ya somo mfano mambo ya muhimu yatakuwa ni:

- Katika 1 Wakorintho 4:16 tunasoma kwamba Paulo anataka washirika wa kanisa wawe kama yeye. Kwa mtazamo wa kati wa mistari (14-15), tunaona kwamba wanapaswa kuwa kama mtoto anavyomuiga baba yake.

- Katika 1 Wakorintho 11:1, tunagundua kwamba kumuiga Paulo kulikuwa na sifa, maana hatukupaswa kuiga dhmbi na tabia zake (kama utasoma Warumi 7, tunaona kwamba hata Pulo alikuwa na vita na dhambi), lakini Paulo alimfuata Yesu Kristo.

- Katika Waefeso 5:1, tunahimizwa kufanana na Mungu kama mototo afanyavyo kwa baba yake.

- Kanisa la Thesalonike lilimfuata Paulo na Bwana. 1 Wathesalonike 1:6

- Kanisa la Thesalonike lilikuwa kama makanisa ya uyahudi katika uvumilivu na mateso yake (1 Wathesalonike 2:14). Elewa kwamba sura hii iko katika kitabu kimoja, kwa hiyo tunajaribu kuoanisha na kuangalia vifungu kwa mtazamo wa karibu.

- Umuhimu wa kuiga huku ni huduma. Waebrania 6:9-12

Kama tutaweka vifungu hivi pamoja twaweza kuona kwamba tunahimizwa na kutiwa moyo na maandiko kufanya mambo makuu matatu:

1. Tumfuate Mungu, Yesu Kristo na Paulo
2. Tuwafuate kama mtoto anayemfuata baba yake hata kama ni wakati wa mateso
3. Tuwafuate kwa njia ya kuwatumikia wengine

Sasa tunaeza kupambanua na kulipanua neno Kuwa mfano (katika kuhusisha 1 Wathesalonike 1:6) Kwa sababu tumekwisha kuona lengo la Maandiko lina maanisha nini. Tunafahamu kwamba wakati Paulo amewaamuru Wathessalonike wawe kama yeye na kundi lake alikuwa akitazama hili kwa undani kama yeye alivyo na Kristo si kwa madhaifu aliyokuwa nayo kama mwanadamu (linganisha na Warumi 7).

Kwa makusudi haya tunaweza kuona sifa na makusudi ya Baba na mwana kwamba tunatakiwa tuwe kama wao. Kwa mfano, twaweza kuona umuhimu wa kutimiza ahadi au umuhimu wa kuishi katika kweli (Tunapoanza kumzungumzia uwezekano hauna mwisho). Kusudi la kufundisha maneno ya Mungu linatakiwa liwe jambo la kuendelea na maombi. Kama walimu wa Neno la Mungu tunapaswa kuelewa kwamba waumini wapya na ambao hawajakomaa hawawezi wala kuelewa theologia (Waebrania 5:11-14). Tunapaswa tuwe makini katika kukomaa kwetu hasa kwa kuzingatia watu wa namna hii.

Turudi tena kwenye yale tuliyokuwa tukijifunza ili tusipoteze maana halisi ya sura na aya hii. Waumini wa kanisa la Thesalonike walimfuata Paulo na Bwana na wakawa mfano kwa kila mtu.

Kwa kuangalia yaliyomo kwa karibu tu tunaona jinsi kanisa hili lilivyotenda. Na shukrani za Paulo kwa Wathesalonike (mstari wa pili) zilikuwa ni kwa sababu ya vitu vitatu:

1. Kazi yao ya Imani,
2. Kazi yao ya upendo na
3. Uthabithi wao wa matumaini

Agano Jipya lote lina mambo mengi ya kutenda (173), imani (246), kazi (19), upendo (115), uthabiti (32), na matumaini (56) kwamba mtu anaweza kutumia muda, majuma au miezi akifundisha mambo haya. Mambo haya ni muhimu sana katika kuelewa yale kanisa la leo linavyotakiwa kutenda.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 9, Sehemu ya 5

**Sehemu ya 5 na 6 zimeunganishwa. Mwanafunzi anatakiwa vitabu vya rejea kukamilisha somo hili. Tafadhali angalia kila msatri wakilishi n uuhusishe na 2 Wathesalonike 1 weka katika kutafakari.**

# Sehemu ya 6
# Kupanua Uelewa Wako katika Kujifunza

Kuna kitu ambacho mwalimu anapaswa kujifunza kabla hajaanza kufundisha, unategemea uongozi wa Roho Mtakatifu na ukomavu wa kundi analotaka kulifundisha. Hata hivyo masomo ya binafsi humsaidia sana mtu katika kuelewa kina cha maneno ya Mungu. Kama Mkristo aliye na Roho Mtakatifu sasa tunaweza kuelewa haya kwa kuangalia 1 Wakorintho 2:9-10, inayosema:

> ***Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasiki wala hayakuingia katika Moyo wa mwanadamu; mamabo ambayo Mungu aliwaandalia wale awapendao. Lakini Mungu ametuandalia sisi kwa Roho. Maana Roho humchunguza yote hata mafumbo ya Mungu.***

Njia inayofaa ya kuonyesha somo hili ni kwa mifano na kwa hiyo tutaipanua 1 Wathesalonike 1:3 kwa kuunganisha na maneno ya kiyunani. Mstari huu unasema:

> ***Mara kwa mara*** (ADIALEIPO = bila kukoma) ***Kuchukuliana*** (MNEMONEUW = kuchukuliana) ***Yenu*** (wingi) ***Kazi*** (ERGOS = biashara, ajira, ambayo tu anafanya) ***ya Imani*** (PISTIS = mapokeo, kutumaini) ***shughuli*** (KOPOS = kazi) ***ya upendo*** (AGAPE = kutenda kilichochema hata kama haupendi kutenda) ***na kustahimili*** (HUPOMONE = uvumilivu katika shida) ***ya matumaini*** (ELPIS = mategemeo) ***katika Bwana wetu Yesu Kristo kweye uwepo*** (EMPROSTHEN = katika sura ya) ***ya Mungu na Baba,***

**Kanuni za Maandiko: Waeleze watu ni kwa nini tunamshukuru Mungu kwa ajili yao (linganisha mstari wa 2).**

**Pointi Muhimu: Kwa kujua hili ndilo kanisa linalofaa na limetathiminiwa kwa imani yake, matumaini na upendo.**

**A. Mambo Mengine Ya Kuangalia:**

1. **Moja au zaidi ya mambo haya yanaonekana kuwa ni muhimu kwa kila nyaraka ya Agano Jipya na haijalishi nani ni mwandishi wake.**

2. **Elewa kwamba "kutenda kazi" na kazi ya upendo yote yametazamwa.**

3. **Kwa hiyo haya matatu ni muhimu sana.**

4. **Sifa zote hizi tatu zaweza kukua.**
    a. Imani (2 Wathesalonike 1:3)
    b. Tumaini (Warumi 15:13)
    c. Upendo (2 Wathesalonike 1:3)

5. **Ni sifa zilizopangwa na Mungu zipate kutendwa ili zionekane katika maisha yetu.**
    a. Imani (Waebrania 11:1)
    b. Tumaini (Warumi 8:24)
    c. Upendo (Waefeso 3:16-19)

6. **Ikiwa mtu atapoa kiroho maendeleo atakayokuwa ameyafanya lazima yataharibika. (Ufunuo 3:14-20)**

7. **Paulo alituambia upendo kilikuwa ni kitu kikubwa sana na kama hutakuwa na upendo hakuna faida (1 Wakorintho 13:1-3, 13)**

8. **Kama mtu hatakuwa hata na kimoja wapo ya vitu hivi matokeo yake ni uasi kama wagalatia au Wakorintho.**

**B. Waweza kupanua kujifunza kwako kwa kufanya hizi kanuni tatu:**

1. **Kazi ya Imani**
    a. Kazi ya imani ina maanisha kwamba imani imekuwa ni kazi yako na maisha yako yanategemea hapo.
    b. Kiyunani inasema, "kazi ya imani," inayoonyesha kwamba unaendelea katika kumwamini Yesu Kristo.
    c. Mitazamo mingine "kazi ya imani" kuwa msambazaji wa injili ya Yesu Kristo.

d. Neno, “Imani,” limetumika katika maandiko kuonesha mwili wa kweli ulio katika neno lililoandikwa. Lakini kwa kuwa hiki ni kitabu cha tatu cha Agano Jipya baada ya Yakobo na Wagalatia kilichoandiwa, inakuwa na mashaka kidogo Paulo anapozungumzia.
e. “Kazi ya imani” haithibitishi kwamba inaokoa. (Warumi 3:27-28; Wagalatia 2:16)
f. Imani, na si kazi, inathibitisha kutochanganya na miungu. (Warumi 4:5)
g. Mtu anayefanya kazi ili kupata wokovu huyo anacheza tu mbele za Bwana. (Warumi 9:32)
h. Viongozi wakubwa wanajitazama kama watenda kazi na si watawala. (2 Wakorintho 1:24)
i. Mtu anapokuwa ameokolewa, amethibitishwa kwa imani, imani inayoendelea katika Yesu Kristo ni lazima izae kazi ya neema. (2 Wakorintho 8:7)
j. Muumini hampokei Roho Mtakatifu kwa sababu ya kazi lakini kazi ni matokeo ya kukua kiroho. (Wagalatia 3:2-5)
k. Imani hutenda kwa njia ya upendo wa Kiroho kwa sababu ya tumaini. (Wagalatia 5:5-6)
l. lakini ibilisi anataka imani isomeshwe na atumie hila kama vile uasi kuijaribu. (Wagalatia 5:7, 13)
m. Imani yetu si kuwa kwetu tu bali katika Mungu anatenda kazi ndani yetu. (Wakolosai 2:12; Wafilipi 2:12-16)
n. Tuombe ili hata waumini wengine wawe na kazi yenye nguvu katika imani. (2 Wathesalonike 1:11; Yakobo 2:14-26)

**Kanuni: Kanisa hili lilikuwa na imani ambayo ilionekana kwa kumruhusu mungu atende kazi ndani yao.**

2. **Kazi ya Upendo**
a. Hii ni sehemu pekee katika Agano Jipya ambayo maneno mawili (kazi na upendo) yanatumika kwa ukaribu pamoja.
b. Zawadi mojawapo ya maishani ni kwamba kazi yako inaweza kukufanya ufurahie maisha yako na mkeo umpendaye. (Muhubiri 9:9)
c. Neno hili pekee la kazi linaonesha kazi itakayojitoshereza katika furaha yake.
d. Hii ni kazi ambayo inafaida hata kwa wengine. (Yohana 4:37-38)
e. Kazi hii ni ushirika katika biashara za Mungu ya upendo. (1 Wakorintho 3:6-9)
f. Kazi inategemea kazi ya Bwana na si katika bure. (1 Waorintho 15:58)
g. Hakuna atakayekuja kudai juu ya kazi ya mwingine. (2 Wakorintho 10:14-18)
h. Watenda kazi wasio waaminifu watawajibika juu ya kazi zao. (2 Wakorintho 11:23-27)
i. Watenda kazi wa Mungu wanatakiwa kutenda hadi kwenye kimo cha furaha kama itawezekana ili kutowalemea waumini wapya. (1 Wathesalonike 2:9; 2 Wathesalonike 3:8)
j. Hakuna anayetaka aione kazi yake kuwa si ya faida. (1 Wathesalonike 3:5)
k. Kazi bila upendo inaharibu kanisa. (Ufunuo 2:2-7)
l. Upendo huu ni AGAPE (Kiyunani) upendo wa kutenda kilicho sahihi na kweli hata kama haujisikii kutenda.
m. Kwa, “kazi ya upendo” ni kazi iliyo kwenye kimo cha kuchosha inayotenda kazi ya haki na kweli kwa wengine hata kama haujisikii.
n. Ni kazi isiyokuwa na sababu wala makusudi ya aina yoyote ile.
o. Ina fanya mwili wako kuwa hekalu na dhabihu takatifu (Warumi 12:1), ikiwafikiria wengine kuwa ni bora kuliko wewe (Wafilipi 2:3), ikikamilisha amri mbili (Marko 12:29-31).

**Kanuni: Kanisa hili lilikuwa katika kimo cha kutenda hata zaidi ya upendo wa mungu na wengine.**
**Kanuni: Elewa kwamba hii ni sifa ya mwili wa kanisa na si mchungaji.**

3. **Ustahimili (Uvumilivu) wa Matumaini**
a. “Ustahimilivu katika Matumaini” ni uvumilivu katika mapito unaosababishwa na matumaini.
b. Neno la kiyunani ELPIS linalotafasiriwa kama “tumaini” lina maana ya kutegemea yajayo.
c. Tumaini huwa kwa mtu wa Yesu Kristo. (1 Timotheo 1:1)
d. Kadri Kristo anavyoumbika ndani yako, ndivyo utakavyozidi kumuelewa kwa wingi na utukufu wake. (Wakolosai 1:27)
e. Imani, matumaini na upendo yote haya yamewekwa tangu ufufuko wa Yesu Kristo. (1 Petro 1:20-22)
f. Tumaini lililo katika Yesu hutakasa. (1 Yohana 3:1-3)
g. Kwa wale wanaovumilia huzaa matunda. (Luka 8:15)
h. Kwa wale wanaovumilia katika kutenda mema watapata uzima wa milele. (Warumi 2:5-11)
i. Uvumillivu ni kitu muhimu sana katika kujenga tumaini. (Warumi 5:1-5)
j. Tumaini si kitu kinachoonekana lakini kwa uvumilivu tunatumaini. (Warumi 8:23-26)
k. Uvumilivu na kutiwa moyo kutoka katika neno la Mungu ni vitu viwili vinavvydumisha matumaini. (Warumi 15:4)
l. Uvumilivu na kutiwa moyo huku kunatoka kwa Mungu ambaye hutegemea kwamba ,maisha yetu yatabadilka na kuleta mahusiano na wengine. (Warumi 15:5-7)

m. Uvumilivu na kazi ni sifa za kuwa mtumishi wa Mungu. (2 Wakorintho 6:1-12)
n. Ufahamu wa Mungu hutolewa ili tuwe wavumilivu. (Wakolosai 1:9-14)
o. Kanisa linapoonyesha uvumilivu hata wengine katika mwili wa Kristo ataguswa. (2 Wathesalonike 1:4; 2 Wathesalonike 3:5)
p. Uvumilivu ni utendaji wa mtu wa Mungu. (1 Timotheo 6:11-12)
q. tunahitaji kuwa wavumilivu. (2 Timotheo 3:10-13)
r. Watu wazima wanapaswa kuwa mfano wa uvumulivu. (Tito 2:2)
s. Uvumilivu ulio katika imani ni muhimu katika kupokea baraka za Mungu (Waebrania 10:36-39)
t. Uvumilivu ni mbio tunazoshindana. (Waebrania 12:1-3)
u. Uvumilivu ni jambo linaloonyesa ukomavu wa muumini. (Yakobo 1:2-4)
v. Uvumilivu ni kitu kinachokamilisha hizi amri kuu mbili. (2 Petro 1:5-7)
w. Kanisa lililo katika uvumilivu lakini halina upendo, liko katika hatari. (Ufunuo 2:2-4)
x. Kanisa lililo na upendo, imani huduma na uvumilivu, lakini linavumilia maovu nalo pia liko katika hatari. (Ufunuo 2:19-20)
y. Uvumilivu wa Yesu msalabani ni ukombozi wa waumini kuwatoa katika dhiki. (Ufunuo 3:10-11)

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 9, Sehemu ya 6

**Sehemu hii imenganishwa na Sehemu ya 5.**

# Sehemu ya 7

# Kufanya Michanganuo

Kama mwalimu wa Neno la Mungu, unatakiwa uwe na mambo mengi kuliko darasa lako unayoweza kuyaelewa na kuyakumbuka. Ndiyo unataka wengine waelewe ujumbe na waukumbuke, hivyo hakikisha uwe na ukweli na unaoeleweka ili usiwachanganye watu. Ni vizuri kufanya somo lako kuwa rahisi na la kivitendo.

Fanya mchanganuo. Na njia mojawapo ya kufanya hili ni kwa kutumia vielelezo. Kwa mfano, kama tutaangalia pointi ya msumari uliogongelewa katika ubao kila nyundo inayo gonga ule msumari itaufanya uingie hadi pale kile kilichokusudiwa kikamilike. Hivyo, kila kielelezo ni lazima kifanane na kile kilichokusudiwa katika mchanganuo huo.

Rejea njia tulizojifunza katika kusoma neno la Mungu. Tumesema ni lazima tutazame picha iliyo kubwa kwanza na baadaye maelezo yaliyomo ndani na halafu uoainishe maelezo na picha uliyoipata.

Katika 1 Wathessalonike 1:2, tunamuona Paulo anawashukuru wengine waliokuwa wakikuwa katika imani. Ujumbe mmoja waweza kuwa ***“Kushukuru kwa kila jambo.”*** Ujumbe kama huu ni mzuri kwa sababu Mkristo mchanga hujitazama mwenyewe yapi yanapungua kwake zaidi ya kushukuru kwa yale anayopata.

Mara Yesu alipochukua mikate mitano na samaki wawili na alimshukuru Mungu. Japo hakikuwa cha kutosha alishukuru kwa kile alichokuwa nacho si kwa kuomba chakula zaidi na muujiza ukatokea.

Tunasoma tukio hilo lote katika injili zote nne (Mathayo 14:15-21; Marko 6:37-44; Luka 9:13-17; Yohana 6:5-13). Bwana hakumwomba Baba akizidishe chakula. Badala yake katika injli zote nne Yesu alimshukuru Mungu. Tunaweza kuwapa changamoto wanaotusikiliza kwa kuwauliza maswali, Je unautumia muda wako katika kumshukuru Mungu au katika kumlaumu?” Tunaweza kutumia mifano ya watu ambao wana vitu na wanamshukuru Mungu. Watu wanaokusikiliza hakikisha wanaelewa umuhimu wa kumshukuru Mungu. Neno la kiyunani linaloonyesha kushukuru ni EUCHARISTIA. Limetokana na maneno mawili ya kiyunani: “EU” na “CHARIS.” “EU” lina maana ya “wema.” CHARIS ina maana ya, “neema.” Kwa hiyo shukrani ni utambuzi wa mema na neema ya Mungu. Kwa wale wasioshukuru yamkini hawaelewi wala kuikubali neema.

Vielelezo ni msaada sana katika kuyaeleza maandiko. Vielelezo vizuri havitoki katika vitabu bali hutoka katika maisa yetu. Mwasilishaji ni lazima awe makini na mwangalifu sana kwa yale Mungu anayomtendea katika maisha yake.

## Kwa Masomo Binafsi: Sura ya 9, Sehemu ya 7

**Andaa Mahubiri yanayohusu kumtkuza Bwana Yesu Kristo kutoka katika kitabu cha cha 2 Wathesalonike 1.**

# Barua ya Mwisho

Tunapenda tukutie moyo katika kutembea na kutenda kwako na Bwana wetu Yesu Krito. Kitabu cha Misingi (*FOUNDATIONS*) kimekuwa ni msaada sana katika elimu yako ya Biblia na tunafahamu kwamba utaendelea kukua katika neema na ufahamu wa Bwana wetu Yesu Kristo (2 Petro 3:18). Tunaomba tukutie moyo kwa kile ulichojifunza katika kitabu hiki na uanze kuyatenda katika maisha yako na huduma yako. Ukaribu wako na Yesu Kristo utakufanya uelewe kwa ufasaha neno la Mungu na kulifanya neno lililoandikwa litende kazi katika maisha yako.

Misingi *(FOUNDATIONS)* ni kitabu ambacho ni silaha unayohitaji ili uwe mwanafunzi mzuri na mfasiri mzuri wa neno la Mungu. Tunataka tukutie moyo uyachukue yale uliyoyapata katika kujifunza kwako na uanze kuwafundisha na kuwaimarisha Wakristo wengine. Ni vizuri kuelewa kwamba unapotenda ukweli utapelekwa kwa walimu wengi wa uongo ambao kazi yao ni kuharibu ile kweli iliyo katika maandiko kwa mafundisho na tafasiri zao zisizo sahihi (Wafilipi 3:2). Kwa kujilinda, tenda kama Waberoya walivyotenda (Matendo 17:11) na vitafakari vitu unavyovisoma na kuvisikia na usiwe mwepesi wa kukubali vitu kuwa ni vya kweli mpaka vitafakari katika maandiko na kuona Biblia inasema nini.

Ni maombi yetu kwamba utaendelea katika safari yako ya imani na huduma. Tunaishi katika ulimwengu mkubwa japokuwa nguvu yetu yaweza kuwa ni ndogo na isiyotosheleza, lakini kwa yeye Mungu mtawala kwa kila kitu tukifanyacho, yeye atalijenga kanisa lake. Kama washirika wa mwili wa Kristo na tukiwa kundi katika huduma moja tunaelewa kwamba ni majukumu yetu kufanya wanafunzi na kushirikisha ujumbe wa Imani ambao Yesu ametukabidhi. Sisi sote tutakapofika mbinguni tutafurahia kwa jinsi Bwana alivyotutumia kwa utukufu wake. Mungu awabariki katika yote unayofanya na uendelee kujifunza kujionesha kuwa mtenda kazi wa Mungu asiye na sababu ya kutahayari (2 Timotheo 2:15).

VILLAGE MINISTRIES INTERNATIONAL

# MAJIBU

# Sura ya 1

## Sehem ya 1
## Maandalizi Binafsi

### Sura ya 1, Sehemu ya 1

1. Inahusika na mtu kabla hajaokoka (1 Wakorintho 15:44, 46). Inaeleza mtu ambaye anawivu, anaubinafsi, anakiburi na muongo (Yakobo 3:14-15). Inatumika kueleza walimu wa uongo wakati wa siku za mwisho (Yuda 1:18-19).
2. Lafaa kwa (1) mafundisho; (2) kuonya; (3) kuongoza; and (4) kuadibisha katika haki. Lengo ni kuwa ***"atende kila tendo jema."***
3. Mungu atampa kila aombaye.
4. Kujionesha kwa Mungu watendakazi tusio na sababu ya kutahayari. Lengo ni ***"tukilishika neno la kweli kwa usahihi."***
5. Kusamehe na kusafisha
6. Lazima mtu akubali kuishi katika hilo.
7. Tunatakiwa kutembea katika neema kwa njia ya Imani. Hii inamana ya kwamba tunashkru neema iliyotolewa kwa ajili yetu kwa wokovu na ina neema kwa wengine. Pia tunapomtmaini Mungu kwa ajili ya wokovu (imani) tnamtumaini yeye atupatie mahitaji ya maisha yetu.
8. Lengo ni kukutwa katika amani, hanta waa wala hatuna malalamiko. Tnapaswa kukua katika (1) neema na (2)ufahamu wa Bwana wetu Yes Kristo.
9. (1) Tembea katika Nuru na (2) Kuungama dhambi zetu
10. Shetani na jeshi lake ni adui. Tunapaswa kupigana hali tumevaa silaha zote za Mungu.
11. (1) Kufikia moja wa Imani lio katika fahamu wa kweli wa mwana wa Mungu, (2) ukomav wa Mkristo na (3) kipimo cha kimo kilicho katika ukamilifu wa Kristo

## Sehemu ya 2
## Biblia

### Sura ya 1, Sehemu 2

1. Kamili kwa wale wanaotoa dhabihu (mstari wa 1) na kutusafisha dhambi (mstari wa. 3)
2. Kuonesha nafsi ya Kristo
3. (1) Kufundisha, (2) Kuonya, (3) Kuwaongoza na (4) Kuwaadibisha katika Haki
4. (1)Kuwaongoza waumini katika kukomaa na (2) Kuwaimalisha katika kazi njema
5. Ufahamu wa kweli wa Maandiko utamuongoza mtu katika nafsi ya Kristo.
6. Msaada umekwisha tolewa kutoka mtu mmoja hadi mwingine na msaada huo umekbaliwa. Msaada huo umejaa Ahadi zinazolinda mahusiano.
7. (1) Heria, (2) Historia, (3) Mashairi, (4) Manabii Wakubwa na (5) Manabii Wadogo
8. Ndiyo. Mfmo niwakibinadamu.
9. (1) Historia, (2) Nyaraka na (3) Unabii

## Sehem ya 3
## Mtazamo wa Kihistoria

### Sura ya 1, Sehemu ya 3

1. Uumbaji wa mbingu na nchi zilizopo, uangamizwaji wake na uumbaji wa mbingu na nchi mpya.
2. Dhambi zake za kwanza zilikuwa kujitwalia utukufu na sehemu yake ni katika Ziwa la moto.
3. Nitaumbwa tena kikamilifu.
4. Mtu wa kwanza alitenda dhambi lakini Yesu hakutenda dhambi.
5. Shetani na majeshi yake ni adui. Tnamshinda kwa kvaa silaha kamili za Mungu.
6. Wanadamu wote wamesulubiwa.
7. Uasi wa dini ni wa kwanza na uchumi unafatia.
8. Katika Mbingu na Nchi Mpya

9. Katika kuja kwa Yesu kwa mara ya kwanza Kristo aliteseka na akafa. Lakini kwa ujio wake wa mara ya pili Yesu atawashinda adui zake. Elewa kwamba atafufuliwa kutoka wafu bili kwamba kuja kwake kwa mara ya pili kutimie.
10. Yesu Kristo alikuja kuwatmikia watu wote. Mpinga Kristo atajitumikia yeye mwenyewe.
11. Kufanya mataifa kwa wanafunzi.

## Sehemu ya 4
## Mtazamo wa Kikalenda
### Sura ya 1, Sehemu ya 4

1. Anguko la Adamu
   Gharika la Nuhu
   Ahadi ya Abrahamu
   Kutoka kwa Wana wa Israeli
   Mwaka wa Nne wa Sulemani
   Kuangka kwa Falme wa Kaskazini
   Kuangka kwa Falme wa Kusini
   Kuzaliwa kwa Yesu
   Kifo, Kuzikwa na Kufufuka kwa Yesu Kristo
   Kitab cha Mwisho cha Biblia
2. Mwanzo na Ayubu
3. Kutoka–Mambo ya Walawi–Hesabu–Kumbukumbu la Torati–Yoshua–Waamzi–Ruthu–1 Samuel–2 Samuel–1 Wafalme1-5–Zaburi–1 Mambo ya Nyakati
4. 1 Wafalme 6-22–2 Wafalme–2 Mambo ya Nyakati–Methali–Methali–Wimbo wa Sulemani–Obadia–Yoeli–Yona–Amosi–Hosea–Mika–Isaya–Nahumu–Zephania–Habakuki
5. Yeremia–Maombolezo–Ezekieli–Danieli–Ezra–Nehemia–Zekaria–Hagai–Malaki
6. Mathayo–Luka–Marko–Yohana–Matendo
7. Yakobo–Wagalatia–1 Wathesalonike–2 Wathesalonike–1 Wakorintho–2 Wakorintho–Warumi–Filemon–Waefeso–Wakolosai–Wafilipi–1 Timotheo–Tito–2 Timotheo–Waebrania–1 Petro–2 Petro–Yuda–1 Yohana–2 Yohana–3 Yohana–Ufunuo

## Sehemu ya 5
## Maandalizi ya Kujifunza Biblia

### Sura ya 1, Sehemu ya 5

1. Nani = Sedekia, Nebukadneza na jeshi lake
   Nini = Nebukadnezza aliiznguka Yerusalemu na kuuvunja ukuta wa mji.
   Lini = Mwaka wa tisa na mwezi wa kumi wa tawala wa Sedekia
   Wapi = Yerusalemu
   Kwa nini = haijajibiwa katika mistari hii lakini imejibiwa sehemu nyingine (Tazama 40:2-3)
   Kwa jinsi gani = Nebukadneza aliuzungka mji
2. Mioyo yetu yote, roho, akili na nguvu
3. Imani na Upendo kwa kila mmoja

# Sra ya 2 na 3

**Hakuna majibu yaliyotolewa kwa Sura ya 2–3 kwa sababu kuna namna nyingi za kujibu.**

# Sura ya 4

## Sehemu ya 1
## Sheria ya Kwanza

### Sura ya 4, Sehemu ya 1A

1. Tili ni kwa ajilki ya wanafunzi kufanya.

2. Katika msatri wa 4 na 5 neno “Bwana” linaonesha mamlaka yake linaloonesha Enzi yake. Na ukweli kwamba yuko katika kiti cha Enzi katika msatri wa 4 ni udhihirisho wa ngv yake. Katika msatri wa 7 kuna maelezo ya moja kwa moja kwamba Bwana ni mwenye haki Ktika msatri wa 6 anawahukumu waovu inamaanisha kwamba yeye ni mwaminifu. Katika msatri wa 1 ni kwamba yeye ni kimbilio na inaonesha upendo. Katika msatri wa 4 inaonesha mbinguni ikiwa na maana ya kwamba uzima wa milele. Katika mstari wa 6 anasema analeta mvua inamaana yeye ana nguvu zote. Katika msatri wa 4 kweli kwamba anasifa ya kuwa sehemu zote mbinguni na duniani ni kwasababu yeye yuko sehemu zote. Katika msatri wa nne na tano kwamba macho yake yanawatazama wanadamu na kwamba anaweza kuwajaribu wenye haki na waovu inaonesha ufahamu wake wa ndani kabisa kama mtu na hivyo inatuleta katika sifa ya kwamba yeye anajua yote. Katika msatri wa 7 maelezo ya kwamba “Bwana ni mwenye haki” inaonesha ubora wake usiobadilika na hivyo inatupa sifa ya kwamba yeye habadiliki. Katika msatari wa 1 wanazabri wansema wanaweza kukimbilia kwa Bwana hii inaonesha tumaini lake na kutuleta katika sifa yake ya kwamba yeye ni Kweli.

## Sura ya 4, Sehemu ya 1B

1. Yesu Kristo ni Mungu aliye vaa mwili wa wanadamu.
2. Damu ya ng’ombe na mbuzi ilitolewa kama Dhabihu ya tambiko na sadaka za kuteketezwa katika Sheria ya Musa nah ii haikumaliza tatizo la mwanadamu ni dhabih ya Yesu tu ndiyo inaweza kufanya hivyo. Sadaka hizo zilikuwa ni kivli cha kitu halisi Yesu Kristo.
3. Yona alitumwa na Mungu kupeleka Injili kwa mataifa. Ninawi ulikuwa ni mji wa waashuru ambao ulikuwa ni wa watu wa mataifa (Yona 1:2) na hivyo Yesu hakuwa injili ya wayahudi tu bali hata watu wa mataifa mengine Yona akajitoa mwenyewe kuwaokoa watu wake (Yona 1:12) kama Kristo alivyofanya. Yona akakaa siku tatu katika tumbo la samaki (Yona 1:17) na vivyo hivyo Yesu alikaa siku tatu usiku na mchana katika kaburi, Yona ni picha ya huduma, kifo na maziko na ufufuo wa Yesu Kristo.
4. Yesu alikuwa ni Mungu aliye vaa mwili wa mwanadamu hapo Bethelehemu. (Tunaambiwa kwamba Mtawala wa waisraeli ajae ni yule ambaye amekuwepo tangu zamamni za kale, milele yote ambayo sifa hiyo anayo Mungu; Mika 5:2.) Yesu alisema kwamba yeye ni mkte ulioshuka kutoka mbinguni letao uzima (Yohana 6). Mkate lizaliwa katika nyumba ya mikate.
5. Meza iliyokuwa ikitumika katika ushirika ilimwakilisha Yesu kama mleta uzima wa kiroho na ile stendi ya Taa inamwakilisha Yesu kama “Nuru ya Ulimwengu.”
6. Yesu alikuwa ni “Mwanakondoo wa Mungu” aliyejitoa mara moja kwa ajili ya wanadamu.
7. Hii ni kazi yako mwanafunzi.

# Sehemu ya 2
# Sheria ya Pili

## Sura ya 4, Sehemu ya 2A

1. a. Uzao wa mwanamke–Mwanzo 3:15 na Mathayo 1:23
   b. Uzao wa Ibrahimu–Mwanzo 12:3 na Mathayo 1:1
   c. Uzao wa Isaka–Mwanzo 21:12 na Mathayo 1:2
   d. Uzao wa Yakobo–Mwanzo 35:10-12 na Mathayo 1:2
   e. Kabila la Yuda–Mwanzo 49:8-11 na Mathayo 1:2
   f. Ukoo wa Yese–Isaya 11:1 na Mathayo 1:5-6
   g. Nyumba ya Daudi–2 Samweli 7:12-16 na Mathayo 1:6
   h. Atazaliwa Bethelehemu–Mika 5:2 na Mathayo 2:1
   i. Mungu na mwanadamu–Zaburi 110:1 na Yohana 1:1, 14
   j. Ataitwa Emanueli–Isaya 7:14 na Mathayo 1:23
   k. Nabii–Kumbukumb la Torati 18:18 na Yohana 7:40
   l. Kuhani–Zaburi 110: 4 na Waebrania 5:9-10
   m. Hakimu–Isaya 33:22 na Yohana 5:22
   n. Mfalme–Yeremia 23:5 na Ufunuo 19:16
   o. Mpakwa mafuta maalumu na Roho Mtakatifu–Isaya 11:2 na Mathayo 3:16
   p. Shauku ya nyumba ya Bwana–Zaburi 69:9 na Yohana 2:17
2. Kwamba Yesu alitimiliza unabii kuhusu Masihi

## Sura ya 4, Sehemu ya 2B

1. a. Warumi 8:35-39 Hakuna kitu kinachoweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.
   b. Yohana 3:16 Wale wote wanaomwamini Mwana wa Mungu wanao uzima wa milele.
   c. Yohana 3:18 Kwa wale wasio mwamini Mwana pekee wa Mungu wamwekwisha kuhukumiwa.

d. Yohana 3:36 Kila anayemwamini Mwana anao uzima wa milele bali asiyeamini ghadhabu ya Mungu iko juu yao.
e. Waefeso 2:8-10 Wokovu ni neema kwa njia ya imani ili kwamba mumini atende kazi zilizo njema.
f. 1 Yohana 2:1-2 Kama Mkristo atafanya dhambi Yesu ni mwanasheria mlinzi aliyelipa deni la dhambi kwa ajili ya ulimwengu wote.
g. Tito 3:5 Hatuokolewi kwa matendo mema.
2. Tazama ndani

## Sura ya 4, Sehemu ya 2C

1. a. Abram aliahidiwa taifa, kuheshimiwa na watu na baraka kwa ajili ya kuwabariki wengine.
   b. Mungu ameahidi kuwabariki wale wanaombariki Abram.
   c. Mungu ameahidi kuzibariki familia zote duniani.
2. a. Ondoka iache nchi yako na uende katika nchi atakayokuonesha Mungu
   b. Acha ndugu zako
   c. Acha nyumba ya baba yako
3. Kwa sababu Baba yake Abrahamu alikuwa ni mtii kwa Bwana
4. Kwa sababu alimwamini ( alikuwa na Imani)
5. Hapana
6. Hapana
7. Ndiyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo (Wagalatia 3:26)

## Sura ya 4, Sehemu ya 2D

1. a. 15:1-11 Ufufuo wa Kristo ni kitovu cha Injili ya wokovu
   b. 15:12-19 Kufufuka kwa Kristo ni muhimu kwa wokovu wetu
   c. 15:20-28 Ufufuo wa Waumini takuja katika hatua
   d. 15:29-34 Ufufuo si leseni ya kufanya mambo yetu
   e. 15:35-49 Ufufuko nafndishwa kwa asili
   f. 15:50-58 Ufufuko tatukia gafla
2. Kuamini kwamba (1) Yesu alikufa ili ktimiza maandiko, (2) Kwamba alizikwa, (3) Kwamba alifufuka siku ya tatu kutoka wafu na (4) Kwamba aliwaonekania wanafunzi wake

## Sura ya 4, Sehemu ya 2E

1. Imani katika Mwana
2. Kuamini katika Mwana
3. Ndiyo
4. Walikuwa na uwezo wa kuamua, ikimaanisha walikuwa na uhuru.
5. Mwanadamu anauhuru wa kukubali au kukataa kubeba amri, na kwa hiyo huu ni uhuru.

## Sura ya 4, Sehemu ya 2F

1. a. Agano la Edeni
   b. Agano la Musa
   c. Agano la Palestina
2. a. Agano la Adamu
   b. Agano la Nuhu
   c. Agano la Abrahamu
d. Agano la Daudi
   e. Agano jipya kwa Waisraeli
   f. Agano jipya kwa kanisa
3. Waweza kuamua kutoa maelezo tofauti tofauti.

# <u>Sehemu ya 3</u>
# Sheria ya Tatu

## Sura ya 4, Sehemu ya 3A

1. Neema yake
2. Imani
3. Kani njema
4. Hapana
5. Ndiyo, kama ilivyoshuhudiwa na Yohana alipotumia “sisi” inayomwingiza na yeye

6. Kuungama
7. Mungu
8. (1) Sifa kwa Mungu na (2) ushirika
9. (1) Kuweka Roho ya huruma, (2) wema, (3) unyenyekevu, (4) upole, (5) uvumilivu, (6) kuchukuliana, (7) kusameheana, (8) kuweka upendo, (9) neno la Kristo likae ndani yako, (10) mfundishane, (11) muonyane, (12) muimbe kwa shukrani na(13) mfanye yote kwa jina la Bwana
10. Malipo

## Sura ya 4, Sehemu ya 3B

1. Msimame imara na msiwe katika utumwa tena.
2. Kutumikiana
3. Kwa kufanya mambo yote kwa ajili ya tukufu wa Mungu.
4. Uhuru
5. Sheria ya uhuru
6. Kama mtu atakayehukumiwa kwa sheria ya uhuru
7. Kama mtumishi wa Mungu
8. Wameahidi uhuru lakini wao ni watumwa wa rushwa.
9. Huru unatakiwa utumike katika kutumikiana (Wagalatia 5:13; 1 Petro 2:16) na fanyeni mambo yote kwa utukufu wa Mungu (1 Wakorintho 10:28-31). Huru nawezeshwa na Roho Mtakatifu (2 Kor 3:17). Ni sheria (Yakobo 1:25) kwa hilo tutahukumiwa (Yakobo 2:12). Walimu wa uongo wataiahidi lakini ni uongo (2 Petro 2:1, 17-19)

## Sura ya 4, Sehemu ya 3C

1. Kwa imani katika Yesu Kristo
2. Kwa neema kwa njia ya imani
3. Kazi njema
4. Haifai (2:20) na imekfa (2:26)
5. Hapana
6. Ndiyo
7. Wat “wanaoweza” kusimama kwa ajili ya mtu yeyote
8. Hapana
9. Imani katika Kristo Yesu “inaokoa” na “inathibitisha” mbele za Mungu. Kazi njema ilitolewa kama matokeo ya Imani katika Kristo yanayoonekana na watu wengine kwa hiyo mtu anaokolewa kutoka katika ushahidi usiofaa na kuthibitidhwa katika macho ya mtu aliye ni shuhuda mzuri.

## Sura ya 4, Sehemu ya 3D

1. Ndiyo
2. Haupotei
3. Kwa wanaotenda dhambi hawataurithi uzima wa milele.
4. Ndiyo
5. Wokovu wa wamini umetunzwa katika kilele cha imani ya Yesu Kristo. Kuna aina mbali mbali ya thawab kwa ajili ya waumini wanaotenda mambo mema. Ikiwa muumini atatenda mambo mabaya ya dhambi na akaacha kutenda mema kwa hiyo hatarithi ufalme wa Mungu.
6. Utunze hata kama ni kwa mateso kwa sababu ya upendo kwa ajili ya Bwana.
7. Mchungaji wa shauku, mwaminifu, mnyenyekevu na kama mfano kwa wale waliowekwa katika mamlaka yako.
8. Upendo wa Kristo unaoonekana (inahusisha maisha yake na kurudi kwake)

## Sura ya 4, Sehemu ya 3E

1. Sheria
2. Kiongozi wa familia
3. Ambayo imeandikwa katika mioyo yao
4. Haruni na wanawe ambao walikuwa ni kabila la Walawi
5. Sheria aliyopewa Musa na Mungu
6. Kwa wale walio Waumini (“waliochagliwa klingana na ufahamu wa Mungu Baba kwa kazi ya takaso wa Roho Mtakatifu kwamba mtamtii Roho Mtakatifuna kuunganishwa na damu yake”)
7. Sheria ya upendo
8. Wana wa sadoki wa kabila la Walawi
9. Sheria iliyowekwa na Bwana
10. Ni tofauti katika hali na njia ya dhabihu.

## Sura ya 4, Sehemu ya 3F

1. Ni kawaida kabisa.
2. Si jambo la tafasiri binafsi.
3. Roho Mtakatifu aliwagusa watu.
4. Maandiko (Isaya) yalitimia–Masihi alikuja (1) kuhubiri injili kwa maskini, (2) kutangaza kufunglia kwa waliofungwa, (3)kuwafungua macho vipofu, (4) na kuwaweka huru waliosetwa (5) na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.
5. Ndiyo
6. Ndiyo
7. Hapana
8. Hapana
9. Hapana
10. Sura katika 1 Wathesalonike inahusika na unyakuo ambapo kanisa litachkuliwa na Kristo katika mawinguni. Na sra katika Zakaria zinahusika na kipindi Yesu atakapokuja mara ya pili kkanyaga ardhi hii. Ni matukio mawili tofati.
11. (1) Simba wa Kabila la Yuda, (2) Ukoo wa Daudi (3) Mwanakondoo

# <u>Sehem ya 4</u>
# Sheria ya Nne

## Sura ya 4, Sehemu ya 4A

1. (1) Mtazamo wa ju, (2) mme wa mke mmoja, (3) kiasi, (4) mwangalifu, (5) anayejiheshimu, (6) mkarimu, (7) anayeweza kufundisha, (8) asiyezoelea ulevi, (9) asiyemgomvi, (10) mpole, (11) asiyemwoga, (12) asiyependa fedha, (13) anayetunza nyumba yake, (14) anajua kulea watoto wake, (15) asiyealiyeongoka karibuni na (16) mwney heshima nzuri nje na kanisa lake
2. Kwa uhalisi, majibu haya yatatofautiana kila mtu.

## Sura ya 4, Sehemu ya 4B

1. Hekima
2. Anayependa kusoma Neno
3. Wangalizi anapaswa kuwa ni mwenye mtazamo wa juu
4. Ndiyo
5. Majibu yote yatategeme na kila mwanafunzi.
6. Majibu yote yatategeme na kila mwanafunzi.
7. Majibu yote yatategeme na kila mwanafunzi.

## Sura ya 4, Sehemu ya 4C

1. Wivu na magomvi
2. Matendo ya mwili
3. Mtu anaweza kutumia hata sra kujaribu kuhakikisa jibu lake badala ya kutafuta ukweli kutoka kwa Mungu.
4. Uelewa wetu, kwa sababu ufahamu peke yake namfanya mtu awe na kiburi
5. Ndiyo
6. Hapana, kwa sabab inahusisha upendeleo.
7. Kudumu
8. Kujitathmini na kungama dhambi
9. Hekima
10. Kukumbuka yaliyo katika sura katika kutafakari
11. Yote yaliyo katika Biblia ni neno la Mungu
12. Mawazo ya Mungu yako juu ya mawazo ya mwanadamu.
13. Wivu, ubinafsi na kiburi

# Sura ya 5

## Sehemu ya 1
## Utatu

### Sura ya 5, Sehemu ya 1
1. Mmoja
2. Baba, Mwana na Roho Mtakatifu
3. Anapanga
4. Hufanya kazi za Baba
5. Humfunua Mwana
6. Inaonekana Ktoka katika maandiko kwamba kila nafsi inamiliki sifa sawa
7. Ndiyo
8. Ndiyo
9. Ndiyo
10. Ndiyo
11. Ndiyo
12. Ndiyo
13. Ndiyo
14. Ndiyo
15. Ndiyo
16. Ndiyo

## Sehemu ya 2
## Majina ya Mungu

### Sura ya 5, Sehemu ya 2
1. a. Mungu = ELOHIM (3)
   b. Mungu Mweza = EL SHADDAI (5)
   c. Mungu Aliye Juu = EL ELYON (8)
   d. Mungu wa Milele = EL OLAM (7)
   e. BWANA = YAHWEH (9)
   f. BWANA Atatoa = YAHWEH JIREH (10)
   g. BWANA ni Bendera yangu = YAHWEH NISSI (2)
   h. BWANA ni Amani = YAHWEH SHALOM (6)
   i. BWANA wa Wote = YAHWEH SABBAOTH (1)
   j. BWANA, MKUU NA MMILIKI = ADONAI (4)
2. a. MNGU = THEOS (3)
   b. BWANA = KURIOS (1)
   c. MKUU = DESPOTES (2)

## Sehemu ya 3
## Mungu Baba (Paterology)

### Sura ya 5, Sehemu ya 3
1. Binafsi
2. Ushirika
3. a. Mamlaka: “Baba wa utukufu”– “Mngu aliye juu”– “Mungu wa utukufu”–“Mungu wa miungu”– “Mungu wa amani“–“Mung wa juu”–“Mungu mkuu ”– “Mfalme mkuu juu ya vyote”– “Mfalme wa utukufu ”– “Bwana Mungu Mwenyezi”–“Amani”– “BWANA aliye juu”– “Bwana Mungu wetu”– “Mungu wa Majeshi”– “ Majeshi ya mbinguni, aliye juu”– “Wa Majeshi ”– “Aliye juu Sana ” – “Wimbo wangu”– “Mungu wa Kweli”
   b. Haki: “Mtakatifu”– “Mungu wa wivu na Kisasi ”
   c. Mwaminifu: “Mungu wa Imani...asiye na upendeleo”–“Yeye wa kuogopwa”
   d. Upendo: “Mungu mwaminifu”–“Baba wa rehema”–“Wivu” “Upendo”–“Wa Upendo”

e. Uzima wa Milele: "Mzee wa siku"– "Mungu wa Milele"–"Mngu wa walio hai"–A "Mungu aliye hai na wakweli"
f. Omnipotence: "Mwenye mamlaka"– "Mungu mkuu na mweza"– "Bwana Mungu mweza"
g. Omnipresence: Yuko mahali pote
h. Omniscience: "Mungu wa hekima"
i. Habadiliki: "Mungu wa pekee"–"Mkamilifu"
j. Mkweli: "Mungu wa kweli"

4. a. Mamlaka: "Mfalme wa Milele"–"Mngu ju ya falme zote duniani"– "Mungu asiye wa majanga"– "Mfalme wa mbingu"–"Bwana"–"Bwana wan nchi yote "– "Bwana wa mbingu na nchi"– "Bwana wa wafalme "–"Mwanasheria wetu"– "Mmiliki wa mbingu na nchi "
   b. Muumbaji: The "Msanifu"– "Mjenzi"– "Mungu na Baba wa Bwana wetu Yes Kristo"–"Mungu mumbaji wangu"– "Mungu wa wenye mwili wote"–"Anayefariji mioyo ya wote"– "Bwana muumbaji wetu"– "Muumbaji wako"– "Muumbaji wa vyote"– "Mfinyanzi"
   c. Mlinzi: "Mlinzi wa wasio na msaada "–"Baba wa wasion na Baba"– "Mungu wa malipo"–Mungu alipaye kisasi kwa ajili yangu"–"Hakimu wa wajane"– "Bwana mlizi wetu"–"Wakili wangu"–"Maficho yangu"–"Kimbilio langu wakati wa shida"–"Kimbilio na nguvu yetu"– "Kimbilio la watu wake"– "Kimbilio katika dhoruba"– "Ibada"– "Ulinzi uokoao"–"Nguzo ya waliokandamizwa"–"Nguzo nyakati za shida"– "Msaada uliopo wakati wa shida"
   d. Mfano: "Baba Mtakatifu"–A "Mkuu mbinguni"–"Baba wa haki"
   e. Mtoaji: "Baba wa Nuru"– "Baba wa Roho"–"Chemchemi za maji ya uzima"–"Mungu wa Abraham, Isaka, na Yakobo"– "Mng wa faraja zote"– "Mungu wa wokovu wangu"–"Mungu nguvu yetu"– "Mungu anayetia moyo "–"Aliye mfufua Yesu kutoka wafu"– "Mungu anayesafisha majeruhi yako"– "Mwokozi wetu"– "Nguvu ya moyo wangu"
   f. Hakimu: "Hakimu wa dunia yote"–"Bwana mtuliza dhoruba"–"Hakimu wetu"–"Hakimu wa haki"
   g. Kiongozi: "Nuru yangu"–"Mwalimu"
   h. Upendo: "Mme wako"–"Baba aliye hai"–"Mwokozi wako"– "Anayesikia maombi"– "Mungu atonzaye maagano na upendo"– "Mungu na Neema na huruma"
   i. Mtoaji: "Mkulimar"–"Atoaye kwa wingi hata zaidi ya jinsi tnavyoomba na kufikiri"– "Baba wa Rehema"– "Mungu wa Msamaha"– "Mungu wa nguvu yangu"–"Mungu Baba yetu"–"Mungu Baba"– "Mungu amwambiaye mwanadamu mawazo yake"– "Bwana atoaye"– "Bwana akutakasaye"– "Nguvu"
   j. Nguvu yetu: "Utukufu wa Isareli"–"Mungu mwamba wetu"–"Mungu wa tumaini"– "Mungu wa upendo na amani"–"Mungu war oho wa mwenye mwili wote"–"Mungu aonaye"–"Msaada wa yatima"–"Akufarijiaye"–"Mtakatifu"–"Bwana bendera yangu"–"Bwana mwamba wangu"–"Bwana akuponyae"–"Ujasiri wangu"–"Msaada wangu"–"Tumaini langu"–"Msaada wangu"–"Makao yetu"– "Mwamba wa kujificha"– "Mwamba nguvu yangu"–"Mwamba wa wokovu wangu"– "Nguvu ya wokovu wangu"–"Mfariji wangu"

# <u>Sehemu ya 4</u>
# Mungu Mwana (Christology)

## Sura ya 5, Sehemu ya 4

1. Amekuwepo kabla ya kuvaa mwili.
2. Masihi ni Mungu na mwanadamu.
3. Hakutenda dhambi.
4. Masihi ni Mungu (9:6) alizaliwa na bikira (7:14) kutoka ukoo wa Yese (11:1) mwili wake ambao hakuuthamini.
5. a. Akawa laana yetu (mpatanishi)
   b. Alituokoa (alilipa deni la dhambi)
   c. Mpatanishi wet kwa Mungu
   d. Alistahili haki ya Baba na uaminifu.
6. a. Alikufa kabisa na wala hakuzimia, akazikwa na walinzi wakawekwa kabisa katika mlango wa kaburi na wayahudi.
   b. Sanda zilibaki pale na mwili ukaondolewa.
   c. Kulikuwa na mashahidi wengi walioona ufufuko wa Kristo.
   d. Ufufuo wa Yesu ni wa muhimu katika Injili.
7. Amekaa katika mkono wa kuume wa Baba.
8. a. Anatuombea
   b. Ni wakili wetu
   c. Mpatanishi
   d. Kuhani wetu mkuu

9. Kiongozi
10. Mwema (Yohana 10:11), Mkuu (Waebrania 13:20) ni mkuu (1 Peter 5:4)
11. a. Wa milele: "Alpha na Omega"–"Mtunzi na mkamishaji wa Imani yetu"–"Mwanzilishi wa wokovu"–"Mwanzo na mwisho"–"Mbarikiwa na mwenye nguvu"–"Baba wa milele"–"Uzima wa milele"–"Wa kwanza na wa mwisho"–"Mzaliwa wa kwanza katika umbaji"–"muumbaji wako
    b. Mungu mwanadamu: "Mwanzo wa umbaji wa Mungu"–"Tawi la Bwana"–"Kristo wa Mungu"–"Mwakilishi wa asili ya Mungu"–"Sura ya Mngu asiyeonekana"–"Immanuel"–"Mwanadamu kutoka mbinguni"–"Mungu mweza"–"Mmoja na Baba"–"Mungu mwokozi wetu"–"Mungu na mwokozi wetu"–"Nuru ya utukufu wake"–"Mwana wa Mungu aliye hai"–"Mwana wa Mungu aliye juu"
    c. Ukamilifu wake: "Amen"– "Mtakatifu na mwenye haki"–"Mtakatifu wa Mungu"–"Karama isiyoelezeka"–"Bwana wa utukufu"–"Mkuu"–"Bwana wa utukufu wetu"–"Hakimu wa haki"–"Mwenye Haki"–"Mwana wa Mungu"–"Mkate wa Kweli"–"Nuru ya kweli"–"Mzabib wa kweli"–"Kweli"–"Aliyekuja kwetu kwa haki, utakaso na ukombozi"–"Neno la Mungu"
    d. Kuzaliwa kwake na maisha yake: "Mkate wa uzima"–"Jiwe lililochaguliwa, Jiwe la pembeni"–"Mwaminifu na kweli"–"Shahidi wa kweli na mwaminifu"–"Utkufu wa wat wake Isareli"–"Mwana wake wa Pekee"–"Mtumishi mtakatifu"–"Yesu wa Nazareth"–"Adamu wa mwisho"–"Aliye hai"–"mwanadamu aliyethibitishwa na Mungu"–"Mtu wa hzuni"–"MNAZARETI"–"Mwana wa Daudi"–"Wa pekee kutoka kwa Baba"–"Shina la Daudi"–"Shhuda uliozaliwa kwa wakati maalumu"
    e. Kifo chake: "manukato"–"Aliyetupenda na kutuweka huru kutoka katika dhambi"–"Sauti ya wokovu"–"Mwanakondoo wa Mungu"–"Pasaka Yetu"– "Sadaka ya wote"
    f. Kufufuka kwake: "Shahidi mwaminifu"–"Aliyezaliwa kwanza"–"tunda la kwanza la walio lala"–"Ufufuko na uzima"
    g. Kupaa kwake na kukaa kwa Baba: "Wakili wetu"–"Mung wa dnia yote"–"Mungu juu ya yote"–Mchngaji mwema"–"Khani mkuu"–"Mshindi wa vyote"
    h. Huduma yake: "Mpakwa mafuta"–"Mtume"–"Mkate wa Mungu"–"Bwana harusi"–"Nyota njema ya asubuhi"–"Mchngaji mkuu"–"Yesu Kristo Bwan wangu"–"Yesu Kristo Bwana wetu"–"Komandoowa watu wote"–"Faraja ya Isareli"–"Agano la watu"– "Mlango"–"Mwamba wa milele"–"Rafiki wa watoza ushuru na wenye dhambi"–"Nuru kuu"–"Mchungaji mwema"–"Kipimo cha agano jema"–"Mlinzi war roho yako"–"Kiongozi"–"Aliyekuja kutawala mataifa"–"Anayetakasa"–"Anayechnguza akili na mioyo"–"Kichwa cha mwili"–"Kichwa cha kanisa"–"Kiongozi juu ya mamlaka na sheria zote"–"Kuhani mkuu"–"Tumaini la Isareli"–"Hakimu wa walio hai na wafu"–"MFALME WA WAFALME"–"Mfalme wa mataifa"–"Uzima"–"Roho iletayo uzima"–"Nuru ya ufunuo wa mataifa"–"Nuru ya Uzima"–"Nuru ya watu"–"Jiwe lililo hai"–"Bwana"–"Bwana na mwokozi Yesu Kristo"–"BWANA WA MABWANA"–"Bwana wa amani"–"Bwana wa mavuno"–"Bwana wa Sabato"–"BWANA haki yetu"–"Mpatanishi wa Agano jipya"–"Kuhani mwaminifu na warehema"–"Mtumishi wa agano"–"Masihi"–"Nyota ya asbuhi"–"Uzima wetu"–"Bwana wetu"–"Bwana na Mkuu wetu"–"Amani yetu"–"Mwokozi"–"Tabibu"–"Mfalme na mwokozi"–"Mfalme wa Uzima"–"Mfalme wa Uzima"–"Mfalme wa wafalme"–"Nabii"–"Achukuae dhambi zetu"–"Mtakasaji"–"Mtawala wa wafalme hawa"–"Mwokozi wa limwengu"-"Mchungaji"–"Mlinzi war oho yako"–"Ni msaada wa watu"–"Chanzo cha wokovu wa milele"–"Ni nguzo ya nyakati zako"–"Jiwe"–"Jiwe lililokataliwa na wajenzi"–"Mwalimu"–"Jiwe lililo jaribiwa"–"Njia"–"utajiri wa wokovu"–"Hekima"–"Aliyekuja kwetu hekima ya Mungu"–"Ushuhuda kwa watu"–"Msahuri wa ajabu"–"Neno"–"Neno la uzima"–"Mme wako"–"Mwokozi wako"–"Wokovu wako"

# Sehemu ya 5
# Roho Mtakatifu (Pneumatology)

## Sura ya 5, Sehemu ya 5

1. Busara, mawazo na hiari
    a. Anaakili.
    b. Anamawazo/anafikiri.
    c. Anamaamuzi/hiari.
2. a. Anamajukumu katika uumbaji wa mwanadamu.
    b. Anajukumu katika funuo wa mwanadamu.
    c. Anajukumu katika uelewa wetu.
    d. Anajukumu katika uvuvio wa maandiko.
    e. Anajukumu katika miujiza.
    f. Anajukumu katika kuzaliwa kwa yesu na bikira.
    g. Anauonesha ulimwengu dhambi zake.
    h. Anajizalisha pale mtu anapookoka.
    i. Huwabatiza waumini.
    j. Anatufunga.

k. Anaishi kwa waumini .
l. Atawajaza waumini.
m. Ni wamuhimu katika maombi.
n. Anatuhakiki.
o. Anatuombea.
p. Hutupa karama.
q. Hutufundisha.
r. Huzaa matunda kupitia sisi.
s. Hutupa furaha.
t. Huleta upendo na matumaini kwa waumini.
u. Huleta haki, amani na fraha kwetu.
v. Hutupa nguvu ili tuwe na matumaini.
w. Hutakasa huduma.
x. Hudumisha ushirika kati ya waumini.

3. a. Kazi zake: "Msaidizi mwingine"–"Karama"–"Msaidizi"–"Dhamana"–"Aliyeahidiwa"–"Roho ya kurithi"–"Roho ya Kristo"–"Roho ya ushauri na nguvu"–"Roho ya Imani"–"Roho ya neema and kukirimia"–"Roho ya mwana wake"–"Roho ya Hukumu"–"Roho ya uaminifu"–"Roho ya maarifa na hofu kwa Bwana"–"Roho ya uzima"–"Roho ya Bwana"–"Roho ya kweli"–"Roho ya hekima na uelewa"–"Roho ya hekima na ufunuo"–"Sauti ya mwenyezi Mungu"–"Sauti ya Bwana"
   b. Nafsi yake: "Oumzi ya Mungu"–"Roho ya hukumu na shauku"–"Roho ya utukufu"–"Roho ya Mungu"–"Roho ya kiungut"–"Roho ya utakatifu"–"Roho ya mungu wetu"–"Roho ya Mungu aliye hai"– "Roho wa BWANA Mungu"

# Sura ya 6

## Sehemu ya 1
## Uumbaji (Cosmology)

### Sura ya 6, Sehemu ya 1

1. Mungu
2. Alisema na akaumba vitu vitu kutoka vitu visivyoonekana.
3. Nuru na Giza–Mistari ya 3-5
   Eneo la maji–Mistari ya 6-8
   Nchi kavu na bahari–Mistari ya 9-10
   Miti na majani–Mistari ya 11-13
   Jua, mwezi, nyota–Mistari 14-18
   Viumbe vya baharini, Ndege–Mistari 19-23
   Viumbe vya ardhini, Mwanadamu–Mistari ya 24-31
4. Mbingu mpya na nchi nchi mpya

## Sehemu ya 2
## Malaika (Angelology)

### Sura ya 6, Sehemu ya 2

1. a.. Akili
   b. Kufikiri
   c. Uwezo wa kuchagua
2. Ndiyo
3. Chini
4. Bwana
5. Hapana
6. Ndiyo
7. Mikaeli
8. Makerubi
9. Kutumika kwa waumini
10. Kiongozi wa malaika aliyepingana na Mungu
11. Ziwa la moto

12. Ubinafsi uliochagua kuasi na kumpa Mungu changamoto
13. Mpinzani
14. Msingiziaji
15. Aliyembwa na mwongo
16. Aliyejigeuza
17. Kuwapofusha watu wasio waumini ( watu wasio na Imani)
18. Mashetani na Roho chafu
19. Ujumbe ulioletwa kwa ajili ya Yesu Kristo
20. Dhidi ya jeshi la shetani

## Sehemu ya 3
## Mwanadamu (Anthropology)

### Sura ya 6, Sehemu ya 3
1. Mungu
2. Roho iliyo hai
3. Haikuwa vyema mwanaume akae peke yake.
4. Sababu
5. Asile mti wa "kujua mema na mabaya."
6. Kifo
7. Wakajificha mbele za Mungu badala ya kuktana naye (3:8, 10). Waliona aibu kwa ajili ya utupu wa (3:10). Wakawalaumu wengine kwa sababu ya maamuzi yao (3:12-13). Uhasama ukainuka (3:14-15). Kutakwa na uchungu kwa mwanamke kipindi cha kujifungua (3:16). Kanzi nzito ikahitajika kwa ajili ya mwanadamu kujipatia riziki (3:17-19).
8. a. Mwili na roho
   b. Roho ya mtu
   c. Moyo
   d. Hisia
   e. Akili
   f. Mwili
   g. Asili ya Dhambi kutoka kwa Adamu
   h. Hiari

## Sehemu ya 4
## Migogoro ya Malaika

### Sura ya 6, Sehemu ya 4
1. Maamuzi binafsi
2. Alikuwa ni mlinzi wa enzi ya Mungu.
3. Kwa ajili ya shetani na malaika zake
4. Baada ya miaka 1000 ya utawala wa Kristo
5. Amekwisha hukumiwa.
6. Amekwisha kubali mashtaka.
7. Ilitokea kabla ya Adamu na Eva
8. Tunajambo la kufanya kuhusu rufaa ya shetani.
9. Kuvaa silaha kamili za Mungu.

# Sura ya 7

## Sehemu ya 1
## Ufunuo: Biblia (Bibliology)

### Sura ya 7, Sehemu ya 1
1. Mitazamo yake isiyoonekana
2. Kukifanya kitu kijulikane

3. Mngu alitumia watu kuandika ujumbe wake kwa niaba yake
4. Mamlaka yetu
5. Muongozo wetu
6. Biblia
7. Kweli
8. Hakuna jibu sahihi hapa

# Sehemu ya 2
# Tatizo: Dhambi (Harmartiology)

## Sura ya 7, Sehemu ya 2

1. Kuvunja sheria ya Mungu
2. Hukumu kwa watu wote kwa sababu dhambi yake iliwafikia watoto wake wote
3. Katika mwili wetu
4. Matendo ya mwili
5. Dhambi ya Kuwaza
6. Dhambi ya Ulimi
7. Dhambi ya Wazi
8. a. Uasherati–Kuwaza na Kufanya
    b. Uchafu–Kutenda Wazi
    c. Uzinzi–Kuwaza na Kutenda
    d. Sanamu–Kuwaza na Kutenda
    e. Miungu–Kuwaza na Kutenda
    f. Chuki–Kuwaza
    g. Magomvi–Kutenda
    h. Wivu–Kuwaza
    i. Kulipuka Kwa Hasira–Kuwaza na Kutenda
    j. Hasira–Hasira
    k. Mafarakano–Kuwaza, Tendo, ni Dhahiri
    l. Kujitenga–Mawazo
    m. Husuda–Kwaza
    n. Levi–Dhambi ya Wazi
    o. Karamu za Ulevi–Dhambi ya Wazi

# Sehemu ya 3
# Ufumbuzi: Wokovu (Soteriology)

## Sura ya 7, Sehemu ya 3

1. Kumwamini Yesu Kristo
2. Ni Mungu aliyefanyika mwanadamu, akafa kwa ajili ya dhambi zetu, akazikwa na kufufuka siku ya tatu
3. Kuokoka na kuifahamu kweli, kutubu na si kuangamia
4. Kwa neema kwa njia ya Imani (katika Yesu Kristo)
5. Imani ni kuamini na faida katika kitu hicho ulichokiamini.
6. Badiliko la akili amablo linaitwa kuungama
7. Imani katika Kristo imetuthibitisha na siyo kazi za sheria.
8. Roho Mtakatifu
9. Kwa saba dhambi zetu zimelipwa na hivyo tumeokolewa
10. Kukataa ujumbe wa Roho Mtakatifu kwamba Yesu ni masihi. Kwa kuwa mwanadamu anaweza kungama dhambi zake wakati wote kabla hajafa na dhambi ni kile kitendo cha kufa ukiwa umemkataa Yesu Kristo kama Mwokozi.

# Sehemu ya 4
# Usalama: Ahadi za Mungu

## Sura ya 7, Sehemu ya 4

1. Ndiyo
2. Ufahamu wake wa awali

3. Hakuna mtu wa kumpokonya kutoka kwake au kwa Baba
4. Hapana
5. Hapana
6. Ndiyo, alituokoa tungali adui zake tendo ambalo ni kuwa aliloonesha upendo wake
7. Hapana
8. Hukumu
9. Hakuna kitu
10. Hapana
11. Mwana aliyetwaliwa

## Sehemu ya 5
## Mambo Yajayo: Unabii (Eschatology)

### Sura ya 7, Sehemu ya 5

1. Ukuhani na badiliko la sheria
2. Mawinguni
3. Machoni
4. Pamoja na Kristo katika nyumba ya Baba
5. Dhiki kuu
6. Atarudi na kukanya miguu yake katika mlima mizeituni.
7. Katika unyakuo, Kristo hatakanya migu yake kaika dunia hii bali tutakutana naye mawingni. Atakapokuja mara ya Pili atakanyaga ardhi hii kwa miguu yake.
8. Dub na Manabii wa Uongo
9. Shetani
10. Miaka 1,000
11. Katika Ziwa la Moto
12. Katika Ziwa la Moto
13. Mungu ataumba mbingu mpya na nchi mpya

# Sura ya 8

## Sehemu ya 1
## Maisha Binafsi ya Mkristo (Hodology)

### Sura ya 8, Sehemu ya 1

1. a. Sura ya Kwanza–wokovu
   b. Sura ya Pili– hatua za kukomaa
   c. Sura ya Tatu–milele
2. Imani
3. Kiroho
   a. Ndani ya Mumini
   b. Imani
   c. Roho Mtakatifu anaweza kuhuzunishwa au kuzimishwa
4. Ndiyo. Waumini wanapasw kuungama dhambi zao.
5. Karama ya Kiroho
   a. Upendo
   b. Watalaani
   c. Kupendana knamwonesha Kristo katika ulimweng sioamini. Karama za Kiroho zinatakiwa kutumika kutumikiana. Kumbuka kwamba karaza zile za muda zilitumika kumwonesha Kristo katika ulimwengu usio amini na kanisa lilijifunza kupendana.
6. Haki
7. a. Ungama dhambi
   b. Sifa
   c. Shukurani
   d. Sifa kwa watakatifu wote ambayo ni maombezi
   e. Maombi binafsi amabyo ni sifa
8. Kuwa, katika Neema na ufahamu wa Yesu Kristo.

9. Mpende Mungu na na mpendane.
10. Mateso ya wasio haki
11. Kwa ajia ya maonyo
12. Ndiyo
13. Katika roho na kweli
14. Enendeni mkawafanye mataifa kuwa wanafunzi mkiwabatiza na kuwafundsiha.

## Sehemu ya 2
## Maisha ya Kikristo ya Kushirikiana (Ecclesiology)

### Sura ya 8, Sehemu ya 2

1. Kuwafundisha wengine waweze kuwafundisha wengine
2. Kwa kiwango cha neno la Yesu Kristo
3. Fundisha
4. Ushirika na Mungu na kila mtu
5. a. Mpendane
   b. Kujitoa na kuheshimiana
   c. Kukubaliana
   d. Kutumikiana
   e. Kuwahesabu wengine kuwa ni bora kuliko wewe
   f. Kuchukuliana mizigo
   g. Kutiana moyo
   h. Kusameheana
   i. Kuwa wema kwa kila mmoja
   j. Kuonesha ukarimu kwa kila mmoja
   k. Kujengana
6. Kusambaza nuru, injili ya Yesu Kristo kwa watu wote.
7. Kutumika kwa wengine
8. Umoja wa imani
9. Kwamba wawe na umoja

# Sura ya 9

## Sehemu ya 1-7

Majibu katika sehemu hii yanatofatiana. Kwa hiyo unaombwa kuyajibu na wewe.

# Orodha ya Vitabu

Orodha ya vitabu vifuatavyo haijaribu kuingiza vichwa vyote vya habari vinavyotumika katika msomo yetu kwani hii itakuwa kama tumechuka kitabu chote. Bali inawakilishi mamlaka na kazi yote iliyotumika katika kuandika kitabu hiki.


Archer, Gleason L., Jr., *A Survey of Old Testament Introduction,* Moody Press, 1964.

Archer, Gleason L., Jr., *Survey of the Old Testament,* Moody Press, Chicago, 1978.

Chafer, Lewis Sperry, *Systematic Theology*, Vol. I-VIII, Dallas Seminary Press, 1947.

Dunnett, Walter M., *New Testament Survey,* Evangelical Teacher Training Association, Wheaton, 1967.

Gaebelein, Frank E., General Editor, *The Expositor's Bible Commentary, New Testament,* Zondervan, Grand Rapids, 1976-1992.

Geisler, Norman L., *A Popular Survey of the Old Testament,* Baker Book House, Grand Rapids, 1977.

Harris, R. Laird, Gleason L. Archer, Jr. and Bruce K. Waltke, *Theological Word Book of the Old Testament,* Moody Press, Chicago, 1980.

Harrison, Roland Kenneth, *Introduction to the Old Testament,* William B. Eerdmans Publishing Co., 1969.

Hartill, J. Edwin, *Principles of Biblical Hermeneutics,* Zondervan Publishing House, 1947.

Hiebert, D. Edmond, *An Introduction to the New Testament*, Vol. I-III, Moody Press, 1975.

Hoehner, Harold W., *Chronological Aspects of the Life of Christ,* Zondervan Publishing House, 1977.

Jensen, Irving L., *2 Kings with Chronicles, A Self-Study Guide,* Moody Press.

Machen, J. Greshem, *The New Testament, An Introduction to Its Literature and History*, edited by W. John Cook, The Banner of Truth Trust, Edinburgh, 1976.

Ramm, Bernard, *Protestant Biblical Interpretation,* Baker Book House, 1970.

Ryrie, Charles C., *Basic Theology,* Victor Books, 1986.

Tenney, Merrill C., *New Testament Survey,* William B. Eerdmans Publishing Co., 1961.

Tenney, Merrill C., *New Testament Times,* William B. Eerdmans Publishing Co., 1965.

Tenney, Merrill C., General Editor, *The Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible*, Vol. I-V, Zondervan Publishing House, 1978.

Thayer, Joseph Henry, *Thayer's Greek-English Lexicon of the New Testament,* Associated Publishers and Authors.

Thiele, Edwin R., *A Chronology of the Hebrew Kings,* Zondervan Publishing House, 1977.

Thiessen, Henry Clarence, *Introduction to the New Testament,* Eerdmans, Grand Rapids, 1943.

Unger, Merrill F., *Introductory Guide to the Old Testament,* Zondervan Publishing House, 1951.

Vine, W.E., Merrill F. Unger & William White, Editors, *An Expository Dictionary of Biblical Words,* Thomas Nelson, Inc., 1985.

Walvoord John F., Roy B. Zuck, Editors, *The Bible Knowledge Commentary,* Victor Books, Wheaton, 1983,1985, electronic media.

Wilkinson, Bruce and Kenneth Boa, *Talk Thru the Old Testament*, Vol. I, Thomas Nelson Publishers.

## Ujumbe wa Mwish

[1] Adapted from J. Edwin Hartill, *Principles of Biblical Hermeneutics,* p. 9

[2] Bruce Wilkinson and Kenneth Boa, *Talk Thru the Old Testament*, Vol. I, Thomas Nelson Publishers, 1983, p. 39

[3] Some of the ideas for this chart were drawn from *A Popular Survey of the Old Testament*, by Norman L. Geisler, Baker Book House, Grand Rapids, 1977, p. 83 and *Talk Thru The Bible* by Bruce Wilkinson and Kenneth Boa, Thomas Nelson Publishers, Nashville, 1983, p. 47-49

[4] Wilkinson and Boa, p. 59

[5] Notes from the *NIV Study Bible*, Zondervan, 1985, electronic version

[6] Wilkinson and Boa, p. 72

[7] Charles Caldwell Ryrie, *Ryrie Study Bible, Expanded Edition*, Moody, Electronic Media

[8] John F. Walvoord, Roy B. Zuck, Editors, *The Bible Knowledge Commentary*, Victor Books, Wheaton, 1983,1985, Electronic Media

[9] Wilkinson and Boa, p. 84

[10] Irving L. *Jensen, 2 Kings with Chronicles, A Self-Study Guide*, Moody, p. 20

[11] Charles Caldwell Ryrie, *Ryrie Study Bible, Expanded Edition*, Moody, Electronic Media

[12] Ibid

[13] Wilkinson and Boa, p. 100

[14] Ibid., p. 101

[15] Ibid., p. 110

[16] Ibid., p. 117

[17] Walvoord/Zuck, Electronic Media

[18] Wilkinson and Boa, p. 125

[19] Walvoord/Zuck, Electronic Media

[20] Norman L. Geisler, *A Popular Survey of the Old Testament*, Baker, Grand Rapids, 1977, p. 180

[21] Ibid., p. 181

[22] Ryrie, p. 777

[23] Archer, Electronic Edition

[24] Ryrie, P. 831

[25] Archer, Electronic Edition

[26] Adapted from Archer's *Survey of the Old Testament*, Electronic Media

[27] Charles L. Feinberg, *Class Notes*, Dallas Theological Seminary, p. 3,  1960's

[28] Geisler, p. 195-196

[29] Wilkinson and Boa, p. 164

[30] Geisler, p. 214

[31] Ryrie, p. 1032

[32] R. Laird Harris, Gleason L. Archer, Jr., Bruce K. Waltke, *Theological Word Book of the Old Testament*, Vol. 2, p. 544

[33] Carl Laney, *Bibliotheca Sacra*, Oct.-Dec. 1981, p. 315-316

[34] Charles C. Ryrie, *The Ryrie Study Bible, Expanded Edition,* Moody Press, 1995, p. 1151

[35] Norman L. Geisler, *A Popular Survey of the Old Testament*, Baker, Grand Rapids, 1977, p. 227-228

[36] Ibid., p. 228

[37] Archer, Electronic Media

[38] Wilkinson and Boa, p. 200

[39] Adapted from Wilkinson and Boa, p. 209

[40] Hebrew class at Dallas Theological Seminary taught by Dr. Robert Chisholm, Spring 1993

[41] John F. Walvoord, Roy B. Zuck, Editors, *The Bible Knowledge Commentary*, Victor Books, Wheaton, 1983, 1985, electronic media

[42] Wilkinson and Boa, p. 252

[43] Ibid., p. 263

[44] Gleason Archer, Electronic Media

[45] Ibid

[46] Ibid

[47] Wilkinson and Boa, p. 296

[48] Charles C. Ryrie, *Ryrie Study Bible, Expanded Edition*, Moody, p. 1498

[49] J. Greshem Machen, *The New Testament, An Introduction to Its Literature and History*, edited by W. John Cook, The Banner of Truth Trust, Edinburgh, 1976, p. 16

[50] Merrill C. Tenney, *New Testament Times*, Eerdmans, Grand Rapids, 1965, p. 107-108

[51] Charles C. Ryrie, *Ryrie Study Bible, Expanded Edition*, by, Moody, p. 1500

[52] Ibid., p. 1498

[53] Ibid., p. 1499

[54] Bruce Wilkinson and Kenneth Boa, *Talk Thru The Bible*, Thomas Nelson, Nashville, 1983, p. 305

[55] Charles C. Ryrie, *Ryrie Study Bible, Expanded Edition*, Moody, p. 1509

[56] John F. Walvoord, Roy B. Zuck, editors, *The Bible Knowledge Commentary*, Victor Books, Wheaton, 1983,1985, Electronic Media

[57] Walter M. Dunnett, *New Testament Survey*, Evangelical Teacher Training Association, Wheaton, 1967, p. 17

[58] Ryrie, p. 1574

[59] Wilkinson/Boa, p. 321

[60] Ibid., p. 327

[61] Ryrie, p. 1614

[62] Ibid., p. 1614

[63] Wilkinson/Boa, p. 328

[64] Ibid., p. 328

[65] Walvoord/Zuck, Electronic Media

[66] Ibid

[67] Wilkinson/Boa, p. 338

[68] Walvoord/Zuck, Electronic Media

[69] Ibid

[70] Wilkinson/Boa, p. 353

[71] Walter M. Dunnett, *New Testament Survey*, Evangelical Teacher Training Association, Wheaton, 1967, p. 40

[72] J. Sidlow Baxter, *Explore the Book*, p. 63-64

[73] Ryrie, p. 1786

[74] Wilkinson/Boa, p. 374

[75] Henry Clarence Thiessen, *Introduction to the New Testament*, Eerdmans, Grand Rapids, 1943, pp. 202-03

[76] Gaebelein, Electronic Media

[77] Walvoord/Zuck, Electronic Media

[78] Frank E. Gaebelein, General Editor, *The Expositor's Bible Commentary, New Testament*, Zondervan, Grand Rapids, 1976-1992, electronic media

[79] Ryrie, p. 1886-1887

[80] A.T. Robertson, *Paul and the Intellectuals*, Revelation. and ed. W. C. Strickland (Nashville: Broadman, 1959), p. 12

[81] Wilkinson/Boa, p. 413

[82] Dr. S. Lewis Johnson in *Bibliotheca Sacra*, *Studies in the Epistle to the  Colossians*, beginning Vol. 118, # 471

[83] Walvoord/Zuck, Electronic Media

[84] Ryrie, p. 1939

[85] Wilkinson/Boa, p. 444

[86] Thiessen, p. 271

[87] Wilkinson/Boa, p. 450

[88] Walvoord/Zuck, Electronic Media

[89] Ryrie, p. 1966

[90] Wilkinson/Boa, p. 465

[91] Ryrie, p. 1966

[92] Ron Blue, *The Bible Knowledge Commentary*

[93] The *NET Bible*, The Biblical Studies Press

[94] Walvoord/Zuck, Electronic Media

[95] *NIV Study Bible*, Electronic Library

[96] *NET Bible*, Electronic Media

[97] Ryrie, p. 2005

[98] Adapted from R.T. Ketcham, D.D.; found in J. Edwin Hartill's *Principles of Biblical Hermeneutics*

[99] Charles C. Ryrie, *Basic Theology*, Victor Books, 1986, p. 295

[100] Ibid., p. 343

[101] W.E. Vine, *Vine's Expository Dictionary of Biblical Words*, Thomas Nelson Publishers 1985

[102] Harris, Archer, Waltke, *Theological Wordbook of the Old Testament*, 1980, Moody Bible Institute, p. 127

[103] W.E. Vine, *Vine's Expository Dictionary of Biblical Words*, 1985, Thomas Nelson Publishers, p. 51

[104] Merrill C. Tenney, General Editor, *Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible*, Zondervan Publishing House, Grand Rapids, Michigan, 1978, Vol. I p. 505

[105] W.E. Vine, *Vine's Expository Dictionary of Biblical Words,* Thomas Nelson Publishers, 1985, p. 685

[106] Ibid